*UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA*

# ISAYA:

## SHAHIDI DHAHIRI ZAIDI WA AGANO LA KALE JUU YA MPANGO WA MILELE, WA KIULIMWENGU NA WA UKOMBOZI WA YHWH:

## NABII NA SIKU ZIJAZO

## SURA YA 40-66

BOB UTLEY,
PROFESA WA KANUNI ZA UFASIRI
(UFASIRI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO
AGANO LA KALE, VOL.11B

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS
2010

# Uboreshaji wa Toleo la The New American Standard Bible — 1995

## Limerahishwa kwa ajili ya usomaji:

◙ Fungu lenye maneno ya Kiingereza cha kale "thee's" and "thou's" n.k. yamekwisha boreshwa kwenye Kiingereza cha kisasa.
◙ Maneno na vifungu ambavyo visingaliweza kueleweka kutokana na mabadiliko kwenye maana yake kipindi cha miaka 20 iliyopita vimekwisha kuboreshwa kwenye Kiingereza cha kisasa.

◙ Sentensi yenye kuanza na neno "Na" mara nyingi imekwisha kutafasiliwa kwa ajili ya kuwa katika Kiingereza kizuri, katika namna ya kuutambua huu utofauti kati ya lugha za kale na Kiingereza cha kisasa. Kiyunani na Kiebrania cha mwanzo hakina uwekaji wa vituo vya uandishi kama yale yanayopatikana katika Kiingereza, kwa namna mbalimbali utengaji wa maneno katika Kiingereza cha kisasa unasaidia kama mbadala wa neno "na" kwenye asili yake. Kwa namna nyingine, kiunganishi "na" kimetafasiriwa katika maneno tofauti kama vile "kisha" au "lakini" kama litumikavyo kwenye muktadha, pindi neno katika lugha ya mwanzo inavyoruhusu tafasiri hiyo.

## Lenye usahihi zaidi kuliko lilivyowahi kuwa:

◙ Watafiti wa leo juu ya maandishi bora ya Kiyunani nay ale ya kale ya Agano Jipya yamekwisha kupitiwa upya, na baadhi ya sura zingine zimekwisha kuboreshwa hata kwa ajili ya uaminifu mkubwa kwenye maandishi ya mwanzo.
◙ Vifungu vyenye kufanana vimekwisha kulinganishwa na kupitiwa upya.

◙ Vitenzi vyenye kuwa na maana kubwa vimekwisha kutafasiliwa upya katika baadhi ya vifungu ili kuleta habari nzuri kwa ajili ya matumizi ya muktadha.

## Na bado toleo la NASB linaendelea:

◙ Uboreshaji wa toleo la NASB sio badiliko kwa ajili ya manufaa ya badiliko la utafasiri. Toleo la mwanzo la NASB linabaki kuwa jaribio la muda, na badiliko limewekwa kwa kiwango cha chini katika kutambua kiwango kilichowekwa na toleo la Biblia ya New American Standard Bible.

◙ Uboreshaji wa toleo la NASB unaendeleza utamaduni wa toleo la NASB wa tafasiri ya wazi ya asili ya Kiyunani na Kiebrania pasipo ushirikiano. Mabadiliko katika andiko yamekwishatunzwa ndani ya vigezo vikali vilivyowekwa na Lockman Foundation's Fourfold Aim.

◙ Watafasili na washauri waliochangia katika uboreshaji wa toleo la NASB ni wale wanazuoni wasiopenda ubadilishaji wa Biblia ambao wamehitimu katika lugha za kibiblia, thiolojia, au degree zingine za juu. Wanawakilisha aina tofauti ya historia ya nyuma ya kimadhehebu.

## Kuendeleza utamaduni:

Toleo la asili la NASB limepata mrejesho mzuri wa kuwa ndio lenye tafasiri ya Biblia iliyo sahihi. Tafasiri zingine katika miaka ya hivi karibuni nayo kwa kiasi fulani yamedai kuwa sahihi na mepesi ya kusoma, lakini msomaji yeyote mwenye macho ya kudadisi kwa undani hatimaye atagundua kuwa hayana mwendelezo ulio sahihi. Wakati kipindi fulani kwa uwazi, mara kwa mara huchagua kufasiri lile la mwanzo, mara nyingi kukiwa na usomaji mdogo na wakijitoa zaidi kwenye utiifu. Kiasili ufasiri sio kitu kibaya; kinawezekana na lazima uelezee maana ya kifungu kama mtafasiri alivyokielewa na kukitafasiri. Na hatimaye, hatahivyo kuweka muhtasari ni kama fasiri juu ya Biblia kama ilivyo katika Kutafsiri. Uboreshaji wa toleo la NASB unaendeleza utamaduni wa kuwa fasiri ya kweli ya Biblia, ikifunua kile ambacho maandiko ya asili kwa hakika yanakisema – sio tu kila ambacho mfasiri anaamini ndicho kinachomaanishwa.

—The Lockman Foundation

# ORODHA YA YALIYOMO


Maelezo sahihi ya Vyanzo vya kiufundi vilizotumika katika fasili hii ..... i

Maelezo sahihi ya muundo wa maneno ya Kiebrania yanayogonganisha fasili ya maandiko ..... iii

Vifupisho Vilivyotumika Katika Fasihi Hii ..... ix

Neno Toka kwa Mwandishi:Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ..... x

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika ..... xii

Fasihi

Utangulizi wa Kitabu cha Isaya ..... 01

Isaya 40 ..... 10

Isaya 41 ..... 39

Isaya 42 ..... 54

Isaya 43 ..... 69

Isaya 44 ..... 78

Isaya 45 ..... 88

Isaya 46 ..... 111

Isaya 47 ..... 116

Isaya 48 ..... 124

Isaya 49 ..... 133

Isaya 50 ..... 143

Isaya 51 ..... 147

Isaya 52 ..... 156

Isaya 53 ..... 164

Isaya 54 ..... 175

Isaya 55 ..... 181

Isaya 56 ..... 188

Isaya 57 ..... 193

Isaya 58 ..... 202

Isaya 59 ..... 208

Isaya 60 ..... 214

Isaya 61 ..... 220

Isaya 62 ..... 226

Isaya 63 ..... 232

Isaya 64 ..... 245

Isaya 65 .......... 251
Isaya 66 .......... 262
Kiambatisho cha Kwanza: Utangulizi wa Ushairi wa Kiebrania .......... 272
Kiambatisho cha Pili: Utangulizi wa Unabii wa Agano la Kale .......... 275
Kiambatisho cha Tatu: Mapitio Mafupi ya Kihistoria .......... 279
Kiambatisho cha Nne: Majedwali
1. Kipindi cha Matukio Muhimu katika Agano la Kale .......... 286
2. Wafalme na Matukio ya Wababeli, Washamu, na Utawala wa Kinasaba wa Kiyunani .......... 288
3. Wafalme wa Tawala Zilizogawanyika .......... 292
Kiambatisho cha Tano: Kauli ya Kimafundisho .......... 295

# MADA MAALUM: ORODHA YA YALIYOMO


Agano, 40:1 ..... 12

Mkono, 40:2 ..... 14

Majina ya Uungu, 40:3 ..... 15

Wema, 40:6 ..... 19

"Roho" katika Biblia, 40:7 ..... 20

Kwanini matukio ya siku za mwisho yana mkanganyiko?, 40:9 ..... 22

Masihi, 40:10 ..... 28

Utatu, 40:13 ..... 30

Hakimu, Haki, hukumu katika Isaya, 40:14 ..... 31

Imani kwa Mungu mmoja, 40:14 ..... 31

Upendeleo wa Kiijlisti wa Bob, 40:15 ..... 33

Mungu anaelezewa kama mwanadamu (Lugha ya kibinadamu), 41:2 ..... 42

Fidia/ukombozi, 41:14 ..... 47

Utakaso, 41:14 ..... 49

Chukizo, 41:24 ..... 51

Utu wa Roho, 42:1 ..... 57

Amini, Tumaini, Imani na uaminifu katika Agano la Kale, 42:3 ..... 58

Mbingu, 42:5 ..... 62

Utukufu, 42:8 ..... 63

Maneno kwa ajili ya msamaha, 43:25 ..... 76

Uchaguzi/Kuamriwa kabla na Hitaji la uwiano wa Kithiolojia, 44:18 ..... 82

Toba katika Agano la Kale, 44:22 ..... 84

Wako wapi Wafu?, 44:23 ..... 85

Kujua, 45:5 ..... 93

Malaika na Mapepo, 45:12 ..... 96

Milele (O'lam), 45:17 ..... 99

Kifungu Muhimu cha Utangulizi katika Ufunuo (mvutano 1-4), 45:23 ..... 103

Mabaki (Namna Tatu), 46:3 ..... 112

Ibada kwa Walio na Huzuni, 47:1 ..... 118

Kuabudu Mwezi, 47:7 ..... 119

Moto, 47:14 ..... 122

Haki, 48:1 ..... 127

Tabia za Mungu wa Israeli, 49:7……137
Edeni, 51:3……149
Mwana wa Adamu, 51:12……153
"Jina" la YHWH, 52:6……159
Siku Hiyo, 52:7……160
Amani (*Shalom*), 52:7……161
Yesu Mnazareti, 53:2……167
Je Uponyaji ni Mpango wa Mungu kwa kila Kizazi?, 53:3……169
Bwana wa Majeshi, 54:5……177
Dhamana ya Mkristo, 55:11……186
Ibada ya ustawi wa Mashariki ya Karibu ya Kale, 57:5-6……196
*Molech*, 57:5-6……197
Pembe zitumiwazo na Israeli, 58:1……203
Sabato, 58:13……207
Elfu (*eleph*), 60:22……219
Kupakwa mafuta katika Biblia, 61:1……221
Wokovu (Neno la Agano la Kale), 62:1……227
Edomu na Israeli, 63:1……234
Utatu, 63:9……237
Ubaba wa Mungu, 63:16……239
Maamuzi ya kabla dhidi ya Utashi huru wa Mwanadamu, 63:17……241
Mbingu, 64:1……246
Mambo ya ajabu, 64:3……247
Jina la Bwana, 65:2……253
Vitabu viwili vya Mungu, 65:6……255
Mtazamo wa Kibiblia Juu ya Pombe na Ulevi, 65:8……256
Amina, 65:16……259
Wanawake katika Biblia, 66:12……267

## MAELEZO MAFUPI YA VYANZO VYA KIUFUNDI VILIVYOTUMIKAKWENYE MFULULIZO WA FASIHI HII

I. Maneno/misamiati

Kuna maneno mengi mazuri mbali mbali yanayopatikana katika lugha ya Kiebrania cha kale.

A. *Hebrew and English Lexicon of the Old Testament* kilichoandikwa naFrancis Brown, S. R. Driver, na Charles A. Briggs. Yanaegemea juu ya misamiati ya Kijerumani ya William Gesenius. Yanajulikana kwa vifupisho vya BDB.

B. *The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na Ludwig Koehler na Walter Baumgartner, yaliyotafasiliwa na, M. E. J. Richardson. Yanajulikana kwa vifupisho vya KB.

C. *A Concise Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na William L. Holladay na inaegemea juu ya maneno ya Kijerumani (#A).

D. Idadi tano mpya za usomaji wa neno la kithiolojia lililoandikwa*The New International Dictionary ofOld Testament Theology and Exegesis*, kilichohaririwa na Willem A. Van Gemeren. Yanajulikana kwa vifuapisho vya NIDOTTE.

Ambapo kuna aina ya maneno muhimu, nimeonyesha tafasiri mbali mbali za Kiingereza (NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB) toka kwenye tafasiri za "neno-kwa-neno" na "mlinganyo wa nguvu" (kama vile Gordon Fee & Douglas Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 28-44).

II. Visarufi

Utambulisho wa kisarufi mara nyingi huzingatia juu ya John Joseph Owens' *Analytical Key to the Old Testament* katika juzuu ya nne.Hili limehakikiwa na Benjamin Davidson's *Analytical Hebrew and Chaldee Lexicon of the Old Testament.*Vitu vingine vya kusaidia kwa ajili ya visarufi na sintaksi ambazo zinatumika sana katika vipengere vya juzuu za agano la kale za mtiririko wa "kuelewa Biblia" ni "ule msaada wa mfuatano wa watafasiri" toka kwa United Bible Societies. Kimeandikwa "kitabu kidogo cha mkononi ."

III. Kimaandiko

Mimi nimejikita kwenye uvuvio wa konsonanti za maneno ya Kiebrania(sio katika hoja za voweli za Kimosoreti na maoni.kama ilivyo katika maandiko yote yaliyonukuliwa kwa mkono,kwenye maandiko ya kale, kuna baadhi ya sura zenye maswali. Hili huwa hivyo mara nyingi kwa sababu ifuatayo:

1. *hapax legomenon* (maneno yaliyotumika mara moja tu katika Agano la Kale la Kiebrania)
2. Maneno ya kinahau (maneno na vifungu ambavyo maana yake iliyo wazi imekwisha potea)
3. Kutojulikana kihistoria (kukosekana kwa habari kuhusu ulimwengu wa kale)
4. Wingi wa elimu-maana ya Kisemitiki wa misamiati finyu ya Kiebrania
5. Matatizo yanayohusianishwa na uandishi wa maaandishi ya Kiebrania ya kale ya waandishi wa mwanzo kwa kutumia mkono.
6. Waandishi wa Kiebrania waliosomea huko Misri waliojisikia kuwa huru kuyahariri maandiko waliyoyanakili kwa ajili ya kuyafanya kuwa kamili na ya kueleweka wakati wa siku zao (NIDOTTE kur. 52-54).

Kuna vyanzo mbali mbali vya maneno na maandiko ya Kiebrania nje ya tamaduni ya kimaandiko ya Kimasoreti.

1. Torati ya Kisamaria
2. Magombo ya Bahari ya Chumvi
3. Baadhi ya sarafu, herufi na vigae vya vyungu vilivypatikana baadaye (vipande vya vigae vya vyungu vilivyotumika kuandikiapo maandiko), lakini kwa maeneo mengine,hakuna uhusiano wa

kimachapisho katika Agano la Kale kama yale yaliyoko katika machapisho ya Agano Jipya la Kiyunani. kwa ajili ya ufasaha wa makala mazuri juu ya uendelevu wa kimaandiko ya andiko la Kimasoreti (miaka ya 900 B.K) angalia "Uendelevu wa andiko la Agano la Kale" na Bruce K. Waltke katika toleo la NIDOTTE, juzuu. 1, kur. 51-67.

Andiko la Kiebrania lililotumika ni *Biblia Hebraica Stuttgartensia* toka German Bible Society, 1997, ambayo inaegemea juu ya Leningrad Codex ( 1009 B.K). Mara chache, matoleo ya kale (maandiko ya kale ya Kiyunani, Kiarama Targums, Syriac Peshitta, na Latin Vulgate) yanazungumzika kama Kiebrania ni kigumu au kinatatiza kwa wazi.

# MAELEZO SAHIHI YA MUUNDO WA KIVITENZI VYA KIEBRANIA AMBAVYO VINAGONGANA NA FASIRI YA MAANDIKO

I. Maendeleo mafupi ya kihistoria ya Kiebrania

Waebrania ni sehemu ya kifamilia ya lugha ya Shemu kusini mwa Asia. Jina (lililotolewa na wasomi wa sasa) limetokana na Mwana wa Nuhu, Shemu (kama vile Mwa. 5:32; 6:10). Kizazi cha Shemu kimeorodheshwa katika Mwa. 10:21-31 kama Waarabu, Washamu, Waarameni, na Waashuru.

Kiukweli, baaadhi ya lugha za Kisemiti zinatumia na mataifa yaliyoorodheshwa katika ukoo wa Hamu (kama vile Mwa. 10:6-14), Wakaanani, Wafoeniki, na Waethiopia.

Waebrania ni sehemu ya kikundi cha kaskazini Magharibi mwa lugha hizi za Kisemiti. Wasomi wa leo wana mifano ya kikundi cha lugha ya kale toka :

A. Waamori (*Mari Tablets* tokea karne ya 18 K.K.  huko Akadi
B. Wakaanani (*Ras Shamra Tablets* tokea karne ya 15 Ugariti
C. Wakaanani (*Amarna Letters*  tokea karne ya 14 wakaanani wa huko Akadi)
D. Wafoeniki (Waebrania walitumia alfabeti za Wafoeniki)
E. Wamoabu (Mawe ya mfalme Mesha, 840 K.K)
F. Waaramaiki (lugha rasmi ya Himaya ya Uajemi iliyotumika katika Mwa. 31:47; Yer. 10:11; Dan. 2:4b-6; 7:28; Ezr. 4:8-6:18; 7:12-26 na iliongewa na Wayahudi katika karne ya kwanza huko Palestina

Lugha ya Kiebrania iliitwa "lugha ya Kaanani." Mara ya kwanza iliitwa "Kiebrania" katika utangulizi Mhubiri (Hekima ya Yoshua Bin Sira) kuhusu 180 K.K. na baadhi ya maeneo mengine ya awali, kama vile *Anchor Bible Dictionary*, juzuu 4, kur. 205na kuendelea) sana sana yanakaribiana kufanana na Wamoabu na kabila lililotumika huko Ugariti. Mifano ya ya Waebrania wa kale wanaopatikana nje ya Biblia ni

1. Kalenda ya Gaza, 925 K.K. (andiko la kijana wa shule)
2. Andiko /ujumbe wa Siloam, 705 K.K (maandiko yaliyopatikana katika njia za chini)
3. Vigae vya waebrania, 770 K.K (kodi inanakiriwa kwenye vigae vya chungu)
4. Herufi zilizoandikwa kwenye vigae, 587 K.K (mawasiliano kwenye vita)
5. Mihuri na sarafu za watu wa Makabi
6. Baadhi ya maandiko yaliyopatikana katika magombo ya Bahari ya Chumvi
7. Maandiko mbali mbali (kama vile "lugha[Kiebrania], " ABD 4:203 nakuendelea)

Kama ilivyo lugha zingine za Kisemiti, inaainishwa na maneno yaliyoundwa na konsonanti tatu (mizizi mitatu ya kikonsonanti). Ni lugha thabiti isiyopindika. Mizizi mitatu ya konsonanti inabeba msingi wa maana ya neno, wakati kiambishi awali, kiambishi tamati, au maneno ya nyongeza yanaonyesha utendaji wa kisarufi (voweli zinaongezeka baadae, kama vile Sue Green, *Linguistic Analysis of Biblicla Hebrew*, uk 46-49).

Misamiati ya Kiebrania inaonyesha tofauti kati ya lugha ya mjazo na ushairi. Maana ya neno imehusianishwa na asili ya ngano/hadithi (sio usanifu wa lugha). Mchezo wa neno na mchezo wa sauti ni vitu vya kawaida (*paronomasia*)

II. Dhana ya utabiri

A. VITENZI

Neno la kawaida linalotarajiwa ni KITENZI, KIWAKILISHI, KIIMA (likiwa na vivumishi vyake), KISHAMIRISHO (kikiwa na vivumishi chake). KITENZI cha msingi kisicho pungua ni *Qal,* chenye muundo wa UMOJA, JINSI YA KIKE, na TIMILIFU. Ni namna misamiati ya Kiebrania na Kiaramaiki inavyopangwa. VITENZI vinanyumbulishwa majina kuonyesha

1. Namba-umoja, wingi, umiliki wa vitu viwili
2. Jinsi-jinsi ya kiume na jinsi ya kike (isio na jinsi)
3. Dhamira-elekezi, tegemezi, shurutishi (kwa kulinganisha lugha za Magharibi ya leo, uhusiano wa kitendo kuelekea ukweli halisi)
4. Njeo-(dhana)

WAKATI TIMILIFU, inayomaanisha kutimiliza, kwa maana ya kuanza, kuendelea, na kuhitimisha kitendo. Mara zote muundo huu ulitumika kwa ajili ya kitendo kilichopita,

a. tukio linatokea. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema "muundo mzima ulioelezewa kwa wakati timilifu pia umezingatiwa kuwa wenye uhakika. Wakati usiotimilifu unaweza kuonyesha hali ya kuwezekana au shauku au yenye kutarajiwa, lakini wakati timilifu unaliona hili kama lenye uhakiki, halisi na kweli" (uk. 36).S. R. Driver, *A Treatise on the Use of the Tenses in Hebrew*, inaielezea kama: wakati timilifu unaofanya kazi kuonyesha vitendo vyenye kutimilizwa ambavyo hakika vinasimama wakati ujao, lakini vinachukulia kama vyenye kujitegemea juu ya kusudi lisilobadilika la nia thabiti ambalo laweza kuongewa kama kitu halisi kilichochukua nafasi: kwa hiyo suluhisho, ahadi,au tamko, hasa lile la ki-Ungu mara nyingi linatamkwa katika njeo ya wakati timilifu"(uk. 17 mf., utimilifu wa kinabii). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anauelezea muundo wa kimaneno kwa namna hii:
"….inaiangalia hali kutokea nje, kwa ukamili wake. Kwa namna hiyo kinaelezea ukweli mrahisi, ingawa kinawezakuwa ni kitendo au hali (ukijumuisha hali ya kuwa au fikra). Kinapotumika katika vitendo, mara nyingi inakitazama kitendo kama kilicho kamili toka kwenye hoja ya mzungumzaji mwenye ustadi au msimuliaji (ikiwa ni kamili au sio kamili kwa maana ya uhalisia au ukweli na sio hoja). Utimilifu unaweza kuhusika katika kitendo /hali ya wakati uliopita, uliopo ao ujao. Kama ilivyoelezewa hapo juu, muda, ambao unashawishi namna gani mtu anaweza kutafasiri utimilifu kwenda kwenye njeo ya lugha iliyobobea kama Kiingereza, lazima ipimwe toka kwenye muktadha"(uk.86)
b. WAKATI USIOTIMILIFU, unaoelezea kitendo kilichoko katika mchakato (kisichotimilifu, chenye kujirudia, chenye kuendelea, au chenye udharura), mara nyingi huenenda kuelekea lengo. Mara nyingi muundo huu ulitumika kwa kitendo cha wakati uliopo na ujao.J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema "NYAKATI ZOTE ZISIZOTIMILIFU zinawakilisha hali yakutokukamilika. Zinaweza kuwa ni zenye kujirudia au kuendelea au za dharura. Kwa maneno mengine, au kwa sehemu Fulani inaanza au kiasi Fulani inahakikiwa. Kwa namna zozote katika baadhi ya maana haijamalizika, yaani., haijakamilika" (uk. 55). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anasema "ni vigumu kupunguza kiini cha kutokutimia kwenda dhana moja, kwa vile inajumuisha vyote dhima na dhamira. Muda mwingine wakati usiotimilifu hutumika kwa namna ya kuarifu na kutengeneza maelezo pingamizi. Wakati mwingine inakitazama kitendo zaidi kitegemezi, kama kinadharia, dharura, chenye kuwezekana na nakadharika" (uk. 89)
c. Neno lililoongezewa *waw,* linalounganisha KITENZI kwenye kitendo cha KITENZI kilichopita
d. Dhana SHURUTISHI, inayosimamia juu ya uhiari wa mnenaji na kitendo muhimu cha wasikilizaji
e. Katika Uyahudi ya kale muktadha mpana uliweza kuamua mwelekeo wa muda wa uandishi uliokusudiwa.

B. Miundo mikuu saba iliyobadilishwa na maana zake. Kiuhalisia miundo hii inatenda pamoja na nyenzake katika muktadha na haipaswi kutengwa

1. *Qal* (*Kal*), ni muundo wa kawaida na wa msingi katika miundo yote. Unadokeza kitendo rahisi au hali ya nafsi. Hakuna kisababishi au ulazima uliotumika.
2. *Niphal*, ni muundo wa pili ulio wa kawaida sana. Mara nyingi huwa katika hali ya KUTENDWA, lakini muundo huu pia hutenda kama wenye kubadilishana na kujirejea. Pia hauna kisababishi au ulazima uliotumika.
3. *Piel*, muundo huu ni muundo tendaji na huelezea kuhusu kukifanya kitendo kuwa katika hali ya nafsi. Maana ya msingi ya shina la neno *Qal* inajitokeza au kuendelea kwenye hali ya nafsi.
4. *Pual*, ni neno mfanano TENDWA wa neno *Piel*. Mara nyingi huelezewa kwa KIAMBATA
5. *Hithpael*, ambalo ni shina la kujirejea au kubadilishana. Linaelezea usisitiaji wa kitendo au hali ya kudumu ya kitendo kulinganisha na shina la neno *Piel* . Muundo adimu TENDWA unaitwa *Hothpael*.
6. *Hiphil*, ni muundo tendaji wa usababishaji shina tofauti na neno *Piel*. Unawezakuwa na dhana ya ruksa, lakini mara nyingi unarejelea kwenye sababu ya tukio. Ernst Jenni, Mjerumani mwenye asili ya kiebrania mwana sarufi, anaamini kuwa neno *Piel* linadokeza kitu fulani kuja kwa hali ya nafsi, wakati *Hiphil* inaonyesha jinsi inavyotokea.
7. *Hophal,* ni neno mlingano TENDWA kulinganisha na neno *Hiphil*. Haya mashina ya mwisho mawili ndiyo madogo yaliyotumika kati ya yale mashina saba.

Wingi wa habari hii unapatikana toka *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, cha Bruce K. Waltke na M. O'Connor, kur. 343-452

Chati ya kundi na kisababishi chake. Namna moja katika uelewa wa muundo wa KITENZI cha Kiebrania ni kukiangalia chenyewe katika kipengere cha mahusiano ya IRABU. Baadhi ya mashina ya maneno yanatofautiana na mashina ya maneno mengine (yaani*Qal - Niphal; Piel - Hiphil)*, chati iliyoonyeshwa hapa chini inajaribu kuangazia kwenye utendaji wa msingi wa mashina ya KITENZI na visababishi vyake.

| **IRABU au KIIMA** | **HAKUNA KUNDI LINALOFUATA** | **KUNDI TENDAJI LINALOFUATA** | **KUNDI TENDEWA LINALOFUATA** |
|---|---|---|---|
| TENDAJI | *Qal* | *Hiphil* | *Piel* |
| YA KATI TENDWA | *Niphal* | *Hophal* | *Pual* |
| KUJIREJEA/KUTENDEANA | *Niphal* | *Hiphil* | *Hithpael* |

Chati hii imechukuliwa toka katika majadiliano mazuri ya muundo wa kivitenzi katika uelewa wa utafiti wa lugha ya Akkadia (kama vile Bruce K. Waltke, M. O'Conner, *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, ukurasa wa 354-359)

R. H. Kennett, *A Short Account of the Hebrew Tenses*, ametoa onyo lenye kufikirika kuwa muhimu. "mara nyingi nimeweza kuanzisha katika mafundisho, kuwa kiongozi cha wanafunzi kilicho kigumu katika vitenzi vya Kiebrania ni kupata maana iliyoelezewa katika fikra za Waebrania wenyewe; kuwa ndiyo kusema, kuna tabia ya kutoa kwa mwelekeo wa kufanana kwa kila njeo za Kiebrania kama namba fulani ya muundo wa Kilatini au Kiingereza ambapo njeo hiyo mahsusi kwa kawaida yaweza kutafasiriwa. Matokeo ni kushindwa kutofautisha wingi wa hivi vivuri venye maana, ambavyo vinatoa uhai aina hiyo na nguvu kwenye lugha ya Agano la Kale. Ugumu katika matumizi ya vitenzi vya Kiebrania uko tu katika hoja ya mtizamo, kwa hiyo moja kwa moja yanatofautiana na ya kwetu, kutokana na kile Waebrania wanaangalia kitendo; muda wa mambo, ambao pamoja nasi ni upendeleo wa kwanza, kama neno lenyewe, "njeo" linavyoonyesha, kwao kuwa ni chaguo la pili. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa mwanafunzi kwa uwazi aweze kuchukua, sio kwa wingi miundo ya Kilatini au Kiingereza ambayo inaweza kutumika kutafasiri kila njeo za Kiebrania, bali kiasi Fulani dhana ya kila kitendo, kama kilivyowasilishwa katika fikra za Waebrania. Jina la 'njeo" kama lilivyotumika katika vitenzi vya Kiebrania vinapotosha. Kile kinachoitwa 'njeo' za Kiebrania hakielezei muda lakini kwa kidogo hali ya kitendo. Hakika hakikuwekwa kwa ajili ya kuleta mkanganyiko ambao ungaliweza kutokea kupitia matumizi ya neno 'kauli' kwa namna zote mbili ya nomino na vitenzi, 'kauli' zingalikuwa nzuri zaidi kwenye usanifu kuliko 'njeo.' Mara nyingi ni lazima kitu kiwekwe akilini kuwa haiwezekani kutafasiri kitenzi cha Kiebrania kwenda kwenye Kiingereza bila kutumia udhibiti ambao haupo kabisa katika Kiebrania. Waebrania wa mwanzo kamwe hawakufikiria kitendo chaweza kuwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao, lakini walifikilia tu kwenye *utimilifu* yaani., kitendo kilichokwisha tendeka, au *kisicho timilifu,* yaani., kama katika njia ya kusonga mbele. Tunaposema kuwa njeo Fulani ya Kiebrania wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao katika Kiingereza, hatumaanishi kuwa mawazo ya Kiebrania ya hicho kama wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao, lakini tu kuwa lazima itafasiliwe katika Kiingereza.

Wakati wa kitendo Waebrania hawakujaribu kuelezea kwa namna yeyote ya muundo wa kuongea kwa maneno (utangulizi na uk.1). kwa angalizo la pili, Sue Groom, *Linguistic Analysis of Biblical Hebrew*, anatukumbusha sisi, "hakuna namna ya kuweza kujua ikiwa muundo wa wasomi wa sasa wa elimu-maana na uhusiano wa maana katika lugha zilizokufa au kupotea ni taswira ya fikra zao, au lugha zao mama, au maeneo hayo yalikuwepo katika Waebrania wenye hadhi" (uk. 28).

C. Dhamira (ambazo ni mifanano ilichukuliwa toka kwenye lugha za kimagharibi ya sasa)
   1. Imetokea, inaendelea kutokea (NI KAULI ELEKEZI), mara nyingi inatumia njeo WAKATI TIMILIFU au WAKATI UNAOENDELEA ( KAULI ZOTE ENDELEVU ziko katika KAULI ELEKEZI).
   2. Itatokea, ingalia tokea (KAULI TEGEMEZI)
      a. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU ya wazi
         1) Zenye KUFUNGAMANA (likiongezewa herufi h), nafsi ya kwanza KAULI ISIOTIMILIFU ambayo mara nyingi huelezea kutakia heri, hitaji, au kutia moyo (yaani., matendo ya hiari ya mzungumzaji)
         2) ASILI NA UFAFANUZI ZAIDI WA NENO (badiliko la ndani), mtu wa tatu KAULI ISIOTIMILIFU (inawezakuwa mtu wa pili katika sentensi kanushi) ambayo mara nyingi inaelezea ombi, ruhusa, maonyo, au ushauri
      b. Hutumia njeo ya WAKATI TIMILIFU ikiwa na *lu* au *lule.* Miundo hii inafanana na sentensi YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI katika lugha ya Koine ya huko Uyunani. Maelezo yasiyo sahihi (Kishazi chenye kuelezea tamko ndani ya sentensi yenye masharti) yenye kuleta hitimisho lisilo sahihi (Kishazi kikuu ndani ya sentensi yenye masharti).
      c. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU na muktadha wa *lu,* vile vile maelekezo wa wakati ujao, kuangalia matumizi ya KAULI TEGEMEZI. Baadhi ya mifano inapatikana kwa J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew OldTestament ni* Mwa.13:16; Kumb. 1:12; I Fal. 13:8; Zab. 24:3; Isa. 1:18 (kama vile kur. 76-77).

D. *Waw* – Kinyume chake/yenye matokeo yaliyofuatana/rejeshi. Huu muonekano wa kipekee wa isimu zenye kushughulikia kupanga maneno ya kisarufi ya Kiebrania imeleta mkanganyiko mkubwa kwa miaka mingi. Imetumika kwa namna nyingi mara nyingi ikizingatia juu ya uwasilishaji. Sababu ya mkanganiyiko ni wale wasomi wa mwanzo walikuwa watu wa Ulaya na wakajaribu kutafasiri katika ulelewa wa lugha zao za asili. Na hili lililopoonekana kuwa gumu wakaanza kulaumu lugha ya Kiebrania kuwa ni ya zamani, lugha ya kikale. Lugha za Ulaya ni NJEO (za muda) zinazoegemea kwenye VITENZI. Baadhi ya namna na madokezo ya visarufi yaliainishwa na herufi WAW ambayo iliongezwa kwenye shina la KITENZI TIMILIFU au KITENZI ISIOTIMILIFU. Hii inabadilisha namna ya kitendo kilivyo tazamwa.
   1. Katika simulizi za kihistoria VITENZI vinaunganishwa pamoja katika mfuatano vikiwa na mwongozo wa kawaida
   2. Kiambishi awali cha *waw* kinaonyesha uhusiano maalum kikiwa na KITENZI kilichopita.
   3. Muktadha mpana mara nyingi ni kiini cha uelewa wa mfuatano wa KITENZI. VITENZI vya Kisemiti haviwezi kutathimini utengano. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anaeleza utofauti wa Waebrania katika matumizi ya neno *waw*kabla ya KAULI TIMILIFU na KAULI ISIOTIMILIFU (kur. 52-53). Kama wazo la msingi la KAULI TIMILIFU ni muda uliopita, kuongezeka kwa neno *waw* mara zote linatenda kwa dhana ya wakati ujao. Hili pia ni kweli kwa KAULI ISIOTIMILIFU ambayo wazo lake la msingi ni la wakati uliopo au wakati ujao; kuongezeka kwa neno *waw* lililowekwa katika wakati uliopita. Hili ni badiliko la muda lisilo la kawaida ambalo linaelezea kungezeka kwa neno *waw,* sio kwenye badiliko la maana yake ya msingi ya njeo yenyewe. KAULI TIMILIFU ya neno *waw* inatenda kazi vizuri kwenye unabii, wakati KAULI ISIOTIMILIFU ya neno *waw* inatenda vizuri kwenye simulizi (kur. 54,68). Watts anaendeleza ufafanuzi wake, " kwa ajili ya kuonyesha tofauti iliyopo ya msingi kati ya neno *waw* kiunganishi na neno *waw* linalojirudia, utafasiri ufuatao unatolewa:
      1) Neno *waw* ambalo ni kiunganishi hutokea mara nyingi kuonyesha ufanano.
      2) Neno *waw* kwa mfululizo linatokea mara zote kuonyesha mwendelezo. Ni muundo pekee wa neno *waw* unaotumika ukiwa na mfululizo wa kauli isiotimilifu. Uhusiano kati ya kauli zisizotimilifu zilizounganishwa nayo yaweza kuwa ni mfuatano wa muda, matokeo ya kimantiki, sababu za kimantiki, au tofauti za kimantiki. Kwa namna yeyote ile kunamfuatano"(uk.103)

E. KITENZIJINA-Kuna aina mbili ya vitenzijina

1. KITENZIJINA CHA MOJA KWA MOJA, chenye "nguvu, kinachojitegemea, kinachoshambulia maelezo yaliyotumika kwa ajili ya matokeo ya kuvutia…..kama kiima, mara nyingi hakina kitenzi kilichoandikwa, kitenzi 'kuwa" kikiwa kinaeleweka, hakika, neno linabaki kusimama lenyewe wazi,"(J. Wash Watts, *ASurvey of Syntax in the Hebrew Old Testament,*" uk. 92).
2. KITENZIJINA KINACHOJENGA, ambacho "kinahusiana kisarufi kwenye sentensi na vihusishi, viwakilishi milikishi, na uhusiano uliojengeka" (uk.91). J. Weingreen, *A Practical Grammar for Classical Hebrew*, anaelezea hali ya muundo:

   > "ikiwa maneno mawili (au zaidi) yanaunganikana kwa karibu ambapo kwa pamoja yanatengeneza wazo moja ambatani, neno lenye kujitegemea (au maneno) yanasemekana kuwa katika hali ya muundo." (uk. 44).

F. VIWAKILISHI VYA KUULIZA
1. Mara zote huonekana kwanza kwenye sentensi.
2. Umuhimu wa kufasiri
   a. *ha*- haitarajia mwitikio
   b. *halo'*- mwandishi anategemea jibu la "ndiyo"

KAULI HASI
1. Mara nyingi hujitokeza kabla ya maneno yenyewe yanayo kanushwa.
2. Neno mojawapo kanushi ni *lo'.*
3. Neno *al* lina kidokezo dharura na hutumika likiwa na asili na ufafanuzi zaidi wa neno.
4. Neno *lebhilti*, linamaanisha "ili kwamba……sio" linatumika likiwa na VITENZIJINA.
5. Neno *'en* linatumika likiwa KAULI ENDELEVU.

G. SENTENSI ZENYE MASHARTI
1. Kuna aina nne ya sentensi zenye masharti ambazo kimsingi zinafanana katika lugha ya Koine ya huko Ugiriki.
   a. Kitu Fulani kinaonekana kuwa kikitokea au mawazo kama yalivyotimilizwa (DARAJA LA KWANZA katika Kiyunani)
   b. Kitu Fulani kinyume na ukweli ambacho utimilisho wake hauwezekani (DARAJA LA PILI)
   c. Kitu fulani ambacho kinawezekana au hata kuonekana kutokea(DARAJA LA TATU)
   d. Kitu fulani ambacho ni yumkini kutokea, kwa hiyo utimilisho ni agharabu(DARAJA LA NNE)
2. ALAMA ZA VISARUFI
   a. Vinafikiliwa kuwa kweli au hali iliyopo inatumia KAULI TIMILIFU ELEKEZI au KAULI ENDELEVU na mara zote kishazi kidogo kinatambulishwa kwa
      1) *'im*
      2) *Ki*
      3) *hin* au *hinneh*
   b. muundu ulio kinyume na ukweli mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU kikiwa na utangulizi wa KIAMBATA *lu* au *lule*
   c. zaidi muundo wenye uyumkini mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU katika kishazi kidogo, mara zote *'im* au *ki* vinatumika kama kauli ya mwanzo ENDELEVU
   d. Yumkini muundo mdogo hutumia KAULI TEGEMEZI ISIOTIMILIFU katika kishazi kidogo na mara zote *'im ni* utambulisho wa KAULI ENDELEVU.

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

AB Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman
ABD Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman
AKOT Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens
ANET Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard
BDB A Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs
IDB The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick
ISBE International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr
JB Jerusalem Bible
JPSOA The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America)
KB The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner
LAM The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa
LXX Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
MOF A New Translation of the Bible by James Moffatt
MT Masoretic Hebrew Text
NAB New American Bible Text
NASB New American Standard Bible
NEB New English Bible
NET NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition
NRSV New Revised Standard Bible
NIDOTTE New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren
NIV New International Version
NJB New Jerusalem Bible
OTPG Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith
REB Revised English Bible
RSV Revised Standard Version
SEPT The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
TEV Today's English Version from United Bible Societies
YLT Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young
ZPBE Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS[4]). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.
2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya

zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.

3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today's English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya $UBS^4$ na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
Juni 27, 1996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:


## DHANIO

1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe


Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.

## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.




Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

### 1. Mzunguko wa kwanza wa usomaji

a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
   1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
   2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
   3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
   1) Agano la kale
      a) Simulizi za waebrania

        b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
        c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
        d) Alama za siri za ki-sheria
    2) Agano jipya
        a) Simulizi (Injili, matendo)
        b) Hadithi za mafumbo (Injili)
        c) Barua/nyaraka
        d) Fasihi za mafunuo

2. **Mzunguko pili wa usomaji**
    a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
    b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
    c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

3. **Mzunguko wa tatu wa usomaji**.
    a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
    b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
        1) Mwandishi
        2) Tarehe
        3) Wapokeaji
        4) Kusudu mahsusi la uandishi
        5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
        6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
    c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
    d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

4. **Mzunguko wa nne wa usomaji**
    a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
        1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
        2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
        3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
    b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
        1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
        2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
        3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
    c. Taja vipengele vifuatavyo:-
        1) Istilahi muhimu
        2) Istahili zisizo za kawaida
        3) Muundo muhimu wa kisarufi
        4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
    d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
        1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
            a) Vitabu vya thiolojia
            b) Biblia za marejeo
            c) Itifaki
        2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.

3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
   1) Soma biblia
   2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
   3) Tangulizi za biblia
   4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18
   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi

wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."

2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm,*Protestant Biblical Interpretation(tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi
   b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
   c. Habari za kisarufi
   d. Usomaji wa neno

    e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
    a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
    b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
    c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
    d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
    a. Tofauti za mswada
    b. Maana ya maneno mbadala
    c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
    d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# UTANGULIZI WA ISAYA

I. **MAELEZO YA UFUNGUZI**

A. Isaya ananukuliwa mara kwa mara zaidi katika Agano Jipya kuliko manabii wengine (zaidi ya mara 411). Ujumbe wake ulikuwa mojawapo hali ya uungu mmoja ya ujumla isiyoshikiliwa kimsimamo na mpango wa ukombozi kwa uumbaji wote.
   1. Mungu mmoja
   2. ulimwengu mmoja
   3. imani moja

B. Isaya ni kitabu cha kupendeza sana cha kimasihi.
   1. wana maalum wa Zama Mpya, sura za 7-14
   2. Wimbo wa Mtumishi, 41:1-4; 42:1-9; 49:1-7; 50:4-11; 52:13-53:12 (yawezekana 61:1-3)
   3. Ufalme wa kimasihi ujao (Zama mpya), sura za 56-66. Kuanguka kwa Mwanzo 3 sio neno la mwisho!

C. E. J. Young, katika *An Introduction to the OT*, anaeleza kwamba:
   1. “Kitabu cha Isaya kinachukluliwa kuwa kitabu cha unabii mkuu katika Agano la Kale,” ukurasa wa 168.
   2. “Katika manabii wote wa Isaraeli, Isaya alielewa kwa ukamilifu zaidi ufahamu wa Mungu na mpango wake kwa ajili ya vizazi,” ukurasa wa 171.
   3. “Katika utambuzi wa kiroho hapitwi na chochote katika Agano la Kale lote,” ukurasa wa 172.

II. JINA LA KITABU

   A. Kitabu kinaitwa jina kwa jina la msemaji wake wa kinabii.
   B. Jina Lake Linamaanisha “wokovu wa YHWH” au “YHWH anaokoa.” Jina la Kiebrania linaloishia na herufi “iah” yanakuwa ni vifupisho vya maneno kwa ajili ya YHWH, kama ilivyo kwa majina mengi ya kingereza ambayo yanaanza na “j” na irabu, mfano Joshua (Yoshua) na Joel (Yoeli).

III. UTAKATIFUZAJI (CANONIZATION)

   A. Hili ni gombo la kwanza kati ya nne za manabii wa mwisho.
      1. Isaya
      2. Yeremia
      3. Ezekieli
      4. Kumi na mbili (manabii wadogo wadogo)
   B. Ilikubalika mapema na kuwekwa kwenye ukamilifu katika maandiko matakatifu ya Israeli.

IV. AINA YA FASIHI

   A. Ufanisi wa kifasihi wa Isaya unapita manabii wote wa Agano la Kale. Uwezo wake wa kucheza na lugha na ushairi ni wa kushangaza na kuvutia. Kitabu zaidi ni ushairi (angalia Kiambatisho cha kwanza).
   B. Ni ngumu sana kukaa chini na kusoma Isaya yote kwa wakati mmoja. Ni ngumu kuainisha kitabu. Hii ni kwasababu Isaya alikuwa muhubiri, sio tu mwandishi au mhariri. Kitabu chake kinawandikia jumbe zake za kuzungumzwa kwa kipindi kirefu sana cha muda. Hizi zimeunganishwa kwa pamoja wakati mwingine
      1. kwa maudhui
      2. kwa mfuatano wa matukio
      3. kwa matukio yanayoathiri Israeli
      4. kwa taratibu za kimila za Mashariki ya Karibu ya kale ambazo ni tofauti na za kwetu
      5. zaidi zsana kwa maneno ya msingi na matumizi ya maneno

V. UANDISHI

A. Mitazamo ya Wayahudi juu ya uandishi
   1. The Talmud's *Baba Bathra* 15 ilisema kuwa Hezekia na watu wake waliandika (yaani walihariri au kukusanya/kutunga) Isaya, Mithali, Muhubiri, na Wimbo Uliobora.
   2. Ben Sirah, katika *Ecclesiasticus* 49:17-25, kilichoandikwa mnamo mwaka wa 185 k.k., alisema, "Isaya, mwana wa Amozi," alikiandika kitabu (1:1; 12:1; 13:1).
   3. II Nyakati 32:32 inathibitisha maono ya Isaya, kama inavyofanya sambamba katika Wafalme (II Wafalme. 18:19-20:19 anatwambia kuhusu mtu).
      a. Alitokea katika familia yenye heshima ya kifalme katika Yerusalemu, yawezekana hata mpwa kwa Mfalme Uzzia.
         (1) baadhi ya ushahidi kwamba "iah" (kama jina linavyoishia), ambalo ni kifupisho cha YHWH, ilifanyika karibia kati ya ufalme
         (2) Uwezekano wa Isaya kumfikia Mfalme Uzia pia unatusaidia kufahamu muunganiko wa familia yake
         (3) Angalia Talmud, "Meg." 10b
      b. Alioa nabii mke (8:3).
         (1) mwana wa kwanza, "Shear-Jashub," ambayo inamaanisha "mabaki yatakayorudi"
         (2) mwana wa pili, "Maher-shalal-hash-baz" (8:3), ambayo inamaanisha "kuharakisha mateka,kuharakisha mali"
      c. Isaya alikuwa na huduma ya kinabii ndefu zaidi kati ya manabii wengine wote wa Agano la Kale. Alikuwa msemaji wa Mungu katika Yuda tokea kipindi cha Yotham (742-735 k.k.) mpaka kile kipindi cha Hezekia (715-687 k.k.) kukiwa na uwezekano wa hata kufikia katika utawala wa Manasse (687-642 k.k.); Manasse yawezekana alikuwa mshauri mwenza kutokea mnamo mwaka 696 k.k.
      d. Ikiwa II Nyakati 26:22 inamaanisha kwa Isaya, hivyo alikuwa mwandishi rasmi na mtunzaji wa nyaraka za kifalme za wafalme.
      e. Desturi inasema alichanwa ka msumeno ndani alipopachikwa kwenye gogo (kama vile *Assumption of Isaiah*) wakati wa utawala wa Manase (kama vile Waebrania 11:37).
   4. Moses ben Samuel Ibn Gekatilla, mnamo mwaka wa 110 b.k, anasema kwamba sura za 1-39 ni za Isaya, lakini sura za 40-66 ziliandikwa wakati wa kipindi cha Hekalu la Pili (Kipindi cha Uajemi, 538-430 k.k.).
   5. Ibn Ezra (mnamo mwaka 1092-1167 b.k) ikifuatiwa na uongozi wa Gekatilla's na kukataliwa, au angalau akiulizwa, sura za 40-66 kwa karne ya 8 ya Isaya.

B. Maoni ya Kizuoni ya kisasa juu ya uandishi
   1. Muhtasari mzuri wa kihistoria unapatikana katika R. K. Harrison's *Introduction to the OT*, Eerdmans, 1969.
   2. Mjadala mzuri wa sababu za kiufundi kwa kuelezea waandishi wawili unaweza kupatikana katika S. R. Drivers' *Introduction to the Literature of the OT*, kuchapishwa tena mwaka 1972.
   3. Hakuna Maandiko ya kiebrania au kiyunani (LXX) yaliyowahi kupatikana ambayo yanaonesha mgawanyiko katika sura za 1-39 na 40-66.
      a. Kuna nafasi ya mstari mwishoni mwa sura ya 33 katika mabaki ya magombo ya bahari ya chumvi. Hii inamaanisha mgawanyiko katika kipengele hiki na sio sura 39. 3
      b. Kunaonekana kuwa na muundo wa usambamba kati ya 1-33 na 34-66. Huu muundo wa pande mbili umejikita katika siku za mwandishi mwenyewe na alafu siku za usoni,ilikuwa kawaida katika manabii wa kiebrania (kama vile Ezekieli, Danieli, na Zekaria).

4. Uanazuoni wa kisasa hauna umoja wa ukubaliano juu ya waandishi wangapi au wapi kugawa kitabu.

C. Baadhi ya sababu kwa ajili ya umoja wa Isaya
   1. Misamiati ishirini na tano inapatikana katika vipengele vyote viwili vya Isaya ambavyo havipatikani mahali pengine katika Agano la Kale (NIV, utangulizi kwa Isaya, ukurasa wa 1014).
   2. Jina/Cheo "Mtakatifu Pekee wa Israeli" inatokea mara 13 katika sura za 1-39 na mara 14 katika sura za 40-66 na mara sita tu katika vitabu vyote vingine vya Agano la Kale.
   3. Yesu, katika Yohana 12:38,40, ananukuu katika Isa. 53:1 na 6:10 na hivyo kuchukua sifa za wote Isaya.
   4. Vifungu vya habari kutoka Isaya 40-66 vinapewa sifa kwa Isaya katika Mt. 3:3; 8:17; 12:17; Luka 3:4; 4:17; Yohana 1:23; Mdo. 8:28; na Rum. 10:16-20.
   5. Hakuna ushahidi wa kimaandiko kwa mgawanyiko wa kitabu katika sura ya 39 (MT, DSS, au LXX).
   6. Hakuna historia ya nabii mkuu anayetajwa (Deutro-Isaiah) katika karne ya R. K. Harrison, katika *Introduction to the OT*, anatoa maoni yake juu ya somo, "Hoja kutoka katika mtindo wa kifasihi zilikuwa tupu kabisa mwishoni mwa karne ya kumi na nane, lakini katika ufahamu wa maarifa mapana ya lugha za Mashariki ya Karibu ya kale sasa wamedhania nafasi ya juu kidogo kwa umuhimu. Somo kabisa la uangalifu wa mtindo ilikuwa na hali ya kupendeza sana kwa waumini wa nadharia ya uchambuzi wa kifasihi ya Graf-Wellhausen, ambaye hakuona kusitasita katika kila mambo yaliyokuwa yakipitiwa yanayohusiana na mwandishi wa kibiblia, na hata kukataa sehemu ya kiwango chake hicho chake kwasababu ya muundo wa kifasihi na misamiati ya kila sura haikutokea kufa na ufanano. Inavyoonekana haikutokea kwa wale wachunguzi wa mwanzo kwamba ilikuwa inawezekana tu kugeuza baadhi ya dhana za mtindo wa m mwandishi wa kale na matokeo yake usomaji wa makini wa nyaraka ukapewa yeye na kwamba kule kutanguliwa na kukataliwa kwa sehemu au yote ya hicho kiasi ingethibitishwa tu kwa kigezo cha baadhi ya udhibiti mkali wa nje" (ukurasa wa 776).

D. Baadhi ya sababu kwa uandishi wa mara mbili wa Isaya.
   1. Katika sura za 40-66 jina la "Isaya" halitajwi.
   2. Sura za 40-66 haishabihiani na mazingira ya kihistoria ya Isaya.
   3. Kunaonekana kuwepo kwa kuchanganya kwa rejea za Isaya kwa:
      a. kuvamiwa kwa Ashuru, uhamishoni, na hukumu
      b. kuvamiwa kwa Babeli, uhamishoni, na hukumu
   4. Kuna baadhi za sababu kwa kuwa na baadhi ya nadharia kadhaa za uandishi.
      a. kubadilika kwa mazingira ya kihistoria
         (1) kabla ya kuvamiwa kwa Yuda, 1-39
         (2) uhamishoni, 40-55
         (3) Baada ya uhamisho wa Yuda, 56-66
         (4) katika Isaya 1-39 Hekalu halitawahi kuanguka 40-66 inavyoonekana limekwisha anguka. Mwandishi anaonekana kuwa uhamishoni.
      b. kubadilika kwa masharti kuwafunua wateule wa Mungu
         (1) mtoto wa kimasihi
         (2) Mtumishi anayeteseka
         (3) Israeli kama
            (a) mke, 50:1
            (b) mtumishi wa YHWH, 54:17

5. Wanazuoni wa kisasa wenye msimamo mkali
    a. Kauli ya E. J. Young kuhusu sura za 56-66 ni za msaada, “uwezekano mwingine ni ule wa kuongozwa na Roho, nabii zilizokusanywa na mhariri kutoka kwa manabii tofauti tofauti wa shule la Isaya katika maudhui ya msingi ya kipengele hiki,” (ukurasa wa 188).
    b. Kauli ya R. K. Harrison, “Waandishi wa sasa wanashikilia msimamo kwamba Isaya kama ilivyo wingi wa maandiko ya kinabii yaishiyo hata leo, yanawakilisha makusanyo ya kauli zilizotolewa nyakati tofauti tofauti na kama vile kazi hizo hazitoi faida ya kuteda kwao kutoka katika ile iliyoruhusiwa na nabii zingine kubwa za Agano la Kale. Katika muunganiko huu ni muhimu kutambua kwamba hoja zimejikita juu ya tofauti za mtindo na uelezeo wa kifasihi ni kwa ghafla inaathiriwa na mtindo huu, kwakuwa makusanyo yanaweza kuchukuliwa kwa namna ya kuwakilisha mtindo mzima wa mwandishi juu ya vipindi vingine tofauti vya shughuli za ubunifu. Kuhesabiwa haki kwa ajili ya kuelezea kazi kama makusanyo katika namna bora ya neno hilo linapewa uzuri kwa mstari wa ufunguzi wa unabii ambao unaundwa kutiwa kichwa kwa kazi, na kuzungumza kibayana juu yam abo mya kiufunuo kwa Isaya Mwana wa Amozi alipokea katika maono juu ya Yuda na Yerusalemu katika siku za Uzia, Yotham, Ahazi, na Hezekia. Kama ilivyo kwa makusanyo yote ni ushaidi wa wazi kwamba kitabu kilichojaa uchaguzi tu wa nabii takatifu na mahubiri yanayopatikana, na kuna uwezekana mkubwa kwamba Isaya alitoa nyaraka zaidi kuliko kuliko zilizobaki katika kitabu chake. Asili ya unabii kama makusanyo yanaoneshwa zaidi kwa uwepo wa maelezo ya ziada katika Isa. 2:1 na 13:1, ambayo yanaeza kuwa yamewakilishwa, au kuelekeza kwenye uwepo wa, makusanyo ya mwanzo ya kauli za kinabii,” (ukurasa wa 780).
6. Mtindo wa Kifasihi sura za 40-66 ni tofauti na zile za 1-39.

E. Maelezo ya kuhitimisha juu ya uandishi
1. Wanazuoni wa ki-Mungu wanaendelea kukataa kuhusu namna gani kitabu chetu cha Isaya cha Agano la Kale kilikuja kuwa katika muundo wa sasa (kama vile DSS na MT). Msisitizo mkuu lazima uwekwe katika uvuvio wake na uaminifu katika kufunua tabia na makusudi ya YHWH.
2. Lazima tukatae madhanio yoyote ambayo yanakataa ufunuo wa uaminifu kupitia Isaya. Hii pia inajumuisha kukataliwa kwa kabla wa kukataliwa kwa unabii unaotabiriwa na kushushwa kwa Agano la Kale kwa kutojumuishwa kwa hadithi za wakati wa sasa za wanadamu wakati wa sasa.

VI. TAREHE

A. Isaya ni sehemu ya manabii wa karne ya 8.
1. Yona, Amosi, na Hosea katika Ufalme wa Kaskazini (Israeli), wakati wa Utawala wa Yeroboamu II (786-640 k.k.)
2. Isaya na Mika katika ufalme wa Kusini (Yuda)

B. Alizaliwa mnamo mwaka 760 k.k na aliitwa rasmi katika huduma ya kinabii mnamo mwaka 742 k.k. katika mwaka ambao Uzia alikufa (6:1). Uzia pia anaitwa Azaria (783-742 k.k.).

C. Isaya alikuwa na huduma kutoka siku za mwishoni mwa Uzia (783-742 k.k.) kupitia Yotham (742-735 k.k.), Ahazi (735-715 k.k.), Hezekia (715-687 k.k.), na katika utawala wa Manase (687-642 k.k.) kwasababu Isaya anatabiri/anaandika kifo cha Sanakarebu katika 37:38 (yaani 681 k.k.) D. R. K Harrison anasema kwamba kitabu ni makusanyo ya maandiko ya manabii na mahubiri ya miaka

mingi kupitia. Mwishowe ilikusanywa na kuhaririwa baada ya kifo cha nabii mnamo mwaka wa 630 k.k.

VII. MAZINGIRA YA KIHISTORIA YA MANABII WA KARNE YA NANE

A. Nyaraka za kibiblia zinapatikana katika

1. II Wafalme 14:3-17:6
2. II Nyakati 25-28
3. Amosi
4. Yona
5. Hosea
6. Isaya
7. Mika

B. Muhtasari rahisi kabisa wa hali ya ibada za sanamu kati ya watu wa Mungu inaweza kuonekana katika Hosea.

1. 2:16, “Hawataniita Mimi tena Baali”
2. 4:12-14, “ . . . binti wanafanya ukahaba . . .”
3. 4:17, “Efraimu amejiunga na sanamu; mwacheni”
4. 13:2 “wanadamu wanabusu ndama!” (ibada)

C. Mazingira ya Kijamii

1. Ulikuwa ni muda wa kufanikiwa kiuchumi na kupanuka kijeshi kwa wote Israeli na Yuda. Hatahivyo mafanikio haya yalikuwa yenye faida tu kwa tabaka la matajiri. Maskini walikuwa wamenyonywa na kudharauliwa. Ilikuwa inaonekama kama “maisha duni na kuuwawa” yalifanyika sanamu!
2. Ustahimilivu wa kijamii na mali za wote Israeli na Yuda inahusiana na visababishi kadhaa.
    a. Utawala mrefu na wenye mafanikio wa Yeroboamu II (786-746 k.k.) katika Kaskazini na Uzia (783-742 k.k.) huko kusini
    b. Kushindwa kwa Ashuru wa Shamu Adad-Nirari III katika 802 k.k.
    c. Kukosekana kwa mgogoro kati ya Israeli na Yuda
    d. Utozwaji kodi na unyonyaji wa njia za kibiashara kutokea kaskazini mpaka kusini kupitia daraja la nchi kavu la Palestina kulisababisha ukuaji wa ghafla wa kiuchumi, hata starehe kwa matajiri
3. Ile “Ostraca ya Samaria,” ambayo inawekwa katika tarehe wakati wa kipindi cha Yeroboamu II, inaonekana kuashiria mpangilio wa kiutawala na utaratibu wa kitaasisi kama wa Suleimani. Hii inathibitisha kupanuka kwa uwazi kati ya “walio nacho” na “wasionacho.”
4. Kukosekana kwa ukweli wa matajiri ni wazi unachukuliwa kaika Amosi ambaye anaitwa “nabii wa haki ya jamii.” Rushwa ya kimahakama na kufanywa uongo kwa uzito wa kibiashara ni mifano mizuri miwili ya kutendwa vibaya kwa kle kilichozoeleka inavyoonekana katika wote Israeli na Yuda. D. mazingira ya kidini
    1. Ulikuwa ni muda wa shughuli nyingi za kidini za nje lakini imani ya kweli kidogo sana. Ibada ya Uzao wa Kanaani ilikuwa imeunganishwa katika dini ya Israeli. Watu walikuwa waabudu sanamu lakini waliita dini ya YHWH. Mwenendo wa watu wa Mungu kuelekea muunganiko wa kisiasa ulikuwa umewajumuisha katika ibada ya kipagani na shughuli.
    2. Ibada ya Sanamu ya Israeli inatajwa katika II Wafalme 17:7-18.
        a. Katika mstari wa 8 walifuatisha namna ya ibada ya Wakanaani.
            (1) Ibada ya ustawi (kama vile Mambo ya Walawi 18:22-23)
                (a) sehemu za juu, mistari 9, 10, 11

(b) nguzo takatifu (Baali), mistari ya 10, 16

(c) Asherim, mstari wa 16, hivi vilikuwa viwakilishi vya mbao za Masuria wa kike wa Baali. Zilikuwa aidha nyama zilivofanywa kwa ndama au miti iliyo hai.(2) ulozi, mstari wa 17. Hii ilishutumiwa katika Mambo ya Walawi 19-20 na Kumbu kumbu la Torati 18.

b. Katika mstari wa 16 waliendelea kuabudu ndama wa dhahabu wawili, wakiashiria YHWH, waliowekwa katika Dani na Betheli kwa Yeroboamu I (I Wafalme 12:28-29).

c. Mstari wa 16 waliabudu miungu ya anga ya Babeli:jua, mwezi, nyota na mkusanyiko wa sayari na vitu vya anga.

d. Mstai wa18 waliabudu mungu moto wa ustawi wa-Foinike, *Molech*, kwa kuwatoa sadaka watoto (kama vile Mambo ya Walawi 18:21; 20:2-5). Tendo hili linaitwa *molech*; halikuwa jina la mungu.

3. Ibada ya Baali (kama vile W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, ukurasa wa 82 na kuendelea)

a. Chanzo bora kabisa cha ki-akiolojia ni "Ba'al Epic kutoka Ugarit ." (Hadithi ya Baali kutoka Ugarit)

(1) Inamuelezea Baali kama mungu wa majira anayekufa na kuinuka. Alishindwa na Mot na kufungiwa kuzimu. Maisha na uhai wote ulikwisha. Lakini akisaidiwa na mungu mke (*Anat*), anainuka na kumshinda *Mot* kila majira ya kipupwe. Alikuwa mungu wa ustawi aliyekuwa akiabudiwa kwa miujiza ya kuiga iga.

(2) Alikuwa akijulikana pia kama Hadad.

b. *El* alikuwa ni mungu mkuu wa miungu ya Wakanaani, lakini umaarufu wa Baali uliteka nafasi yake.

c. Israeli alikuwa amehamasishwa zaidi na hali ya kuabudu Baali kupitia Yezebeli ambaye ambaye alikuwa Mfalme wa binti wa Tiro. Alichaguliwa na Omri kwa ajili ya kijana wake, Ahabu.

d. Katika Israeli alikuwa akiabudiwa katika maeneo ya sehemu za nyumbani. Alikuwa akiwakilishwa na jiwe lililoinuliwa. Suria wake, Ashera, anawakilishwa na nguzo za kuchonga ikiwakilisha mti wa uzima

4. Vyanzo kadhaa na aina za ibada za sanamu vinatajwa.

a. nguzo ya dhahabu huko Betheli na Dan waliokuwa wamepangwa na Yeroboamu I kumwabudu YHWH.

b. Kuabudu mungu wa ustawi wa Tiro na mungu wa kike katika eneo la maeneo ya juu

c. Kuabudu miungu kwa umuhimu kulihusishwa katika muungano wa kisiasa wa siku hiyo

D. Muhtasari mfupi wa kuvamiwa kwa Ashuru na Babeli wakati wa karne ya nane ambayo iliathiri Palestina.

1. Manabii wane wa karne ya nane walikuwa wakijihusisha wakati wa kuinuka kwa ufalme wa Hedekeli-Frati wa Ashuru. Mungu angetumia taifa hili katili kuhukumu watu wake, na hasa Israeli.

a. Tukio la kibayana lilikuwa mageuzi ya muungano wa kisiasa na kijeshi kwa muungano wa Yordani ulio julikana kama "Syro-Ephramatic League" (735 k.k.). Shamu na Israeli walijaribu kulazimisha Yuda kuungana nao dhidi ya Ashuru. Badala yake Ahazi alituma barua kwa Ashuru kwa ajili ya msaada. Mfalme wa kwanza mwenye nguvu wa Ashuru, Tiglath-Pileser III (745-727 k.k.), aliitikia changamoto ya kijeshi na kuvamia Shamu.

b. Baadaye mfalme wa Ashuru aliyepandikizwa Hoshea (732-722 k.k.), katika Israeli pia aliasi, akikata shauri kwa Misri. Shalmaneser V (727-722 k.k.) alivamia Misri tena. Alikufa kabla ya Israeli haijakaliwa na kutiishwa lakini aliyemfuatia kimadaraka, Sargon II (722-705 k.k.), aliutwaa mji mkuu Samaria mnamo mwaka 722 k.k. Ashuru ilisafirisha zaidi za wana wa Israeli 27,000 katika tukio hili kama Tiglath-Pileser alivyo peleka uhamishoni maelfu hapo kabla mnamo mwaka 732 k.k.

2. Baada ya kifo cha Ahazi (735-715 k.k.) muungano mwingine wa kijeshi ulitengenezwa nan chi za ukanda wa Yordani na Misri dhidi ya Ashuru (714-711 k.k.). Ulikuwa ukijulikana kama "Uasi wa Ashdodi." Miji mingi ya Kiyudea iliharibiwa wakati Ashuru alipovamia tena. Mwanzoni Hezekia alisaidia muungano huu lakini baadaye aliondoa msaada wake.

3. Hatahivyo, muungano mwingine tena ulijaribu kuchukua fursa ya kifo cha mfalme mwenye nguvu wa Ashuru Sargon II, mnamo mwaka 705 k.k., pamoja na uasi mwingi mwingine uliotokea ambao ulitokea katika ufalme wote wa kiashuru.
   a. Hezekia alishiriki kikamilifu uasi huu. Katika ufahamu wa changamoto hii Senakarebu (705-681 k.k.) alivamia (701 k.k.) Palestina na akafanya hema karibu na jiji la Yerusalemu (II Wafalme 18-19; Isaya 36-39), lakini jeshi lake kimiujiza liliharibiwa na Mungu.
   b. Kumekuwapo na maswali kati ya wanazuoni kama ni kwa kiasi gani na mara ngapi Senakeribu alivamia (mfano John Bright ana uvamizi mmoja mnamo 701 k.k. na nyingine yawezekana mnamo 688 k.k., kama vile *The History of Israel*, ukurasa wa 270).
   c. Hezekia aliachwa kama mabaki ya Kiashuru lakini kwasababu ya udhihirishwaji wa kiburi chake (39:1-8). Yerusalemu aliangukia kwa Nebukadneza mnamo mwaka 587-586 k.k.

4. Isaya kibayana alitabiri urejesho wa watu wa Mungu chini ya Koreshi II, mtawala wa Uajemi Kati (41:2-4; 44:28; 45:1; 56:11). Ninawi (mji mkuu wa Ashuru) ulianguka mnamo mwaka wa 612 k.k. kwa Babeli, lakini mji wa Babeli ulianguka mnamo mwaka wa 539 k.k. kwa Jeshi la Koreshi. Mnamo mwaka 538 k.k. Koreshi alitoa tamko kwamba watu wote waliopelekwa uhamishoni ikijumuisha Wayahudi wangerudishwa nyumbani. Hata alitoa fedha kutoka katika hazina yake kwa ajili ya kujenga upya mahekalu ya kitaifa. Alikuwa mtu anayehusudu uchawi na aliyetaka miungu yote kumpa kibali yeye.

VIII. VIPENGELE VYA KIFASIHI

A. Ainisho Fupi
   1. Sura za 1-39, nabii na siku zake
   2. Sura za 40-66 (au yawezekana 40-55 na 56-66), zama mpya

B. Sura za 1-39, mazingira ya kihistoria za siku za Isaya (kabla ya uhamisho)
   1. Sura za 1-6, chini ya mfalme Uzia na Yotham
   2. Sura za 7-14, chini ya mfalme Ahazi
   3. Sura za 15-39, chini ya mfalme Hezekia (Sura za 36-39 ni sambamba na II Wafalme 18:13-20:19)

C. Sura za 40-66, wakati wa uhamisho na kipindi kabla ya uhamisho, ni aina za ufalme wa baadaye
   1. Kama sura za 1-39 zianaaksi mahubiri ya Isaya na ni dhahiri uwasilishaji wa kinywa, sura za 40-55 zinaaksi mazingira mapya. Hukumu ya Mungu imekuja na sasa marejesho ni maudhui makubwa. Kuna pia mguso wa kimuundo kwamba sura hizi hazihusiano sana na uwasilishwaji wa kinywa kama uwasilishwaji wa uandishi.
   2. Sura za 1-39 kidhahiri zinahusu tishio la kiashuru na tishio na kibabeli katika aina, kibayana katika sura za 13-14, 21 na 39. Sura za 40-55 zinahusiana na kipindi cha kiajemi na urejeshwaji wa watu wa Mungu kwenye nchi ya Ahadi.

3. Sura za baadaye za Isaya, 56-66, ni za matukio ya siku za mwisho zikitumia sitiari za kihistoria kutoka Mashariki ya Karibu ya kale kuonesha matukio ya mbele ya ibada za kiujumla kwa imani moja kwa YHWH.

D. Ugumu wa uaninishaji wa Isaya

1. Wanazuoni wengi wa kisasa wanagawa kitabu katika angalau sehemu mbili: sura za 1-39 na 40- 66. R. K. Harrison: sura za 1-33 na 34-66 kwa sababu ya uwazi katika maandiko ya DSS. Huu mgawanyo wa wazi wa DSS kati ya sura za 33 na 34 imetuinulia maoni kwamba Isaya alizalishwa na wafuasi wake katika juzuu hizi mbili. W. H. Brownlee amependekeza kwamba juzuu mbili ziakisiane katika muundo.

| | **Juzuu 1** | **Juzuu 2** |
|---|---|---|
| Sura za1-5 | kuharibiwa na kurejeshwa | sura za 34-35 |
| sura za 6-8 | Historia za kimaisha | sura za 36-40 |
| sura za 9-12 | wakala wa Baraka za kimungu na hukumu | sura za 41-45 |
| Sura za 13-23 | ibada dhidi ya nguvu ya kigeni | sura za 46-48 |
| Sura za 24-27 | ukomboziwa kiujumla na kukombolewa kwa Israeli | sura za 49-55 |
| sura za 28-31 | mahubiri ya kimaadili | sura za 56-59 |
| sura za 32-33 | kurejeshwa kwa taifa | sura za 60-66 |

2. Baadhi ya shabaha ya maainisho ktika mazingira ya kihistoria, wakati wengine wakiweka shabaha katika maudhui ya kimasihi

| | **NIV** | **Leupold** |
|---|---|---|
| sura za 7-12 | "Unabii ulioanzishwa na Waarmu ana tishio la Wana wa Israeli dhidi ya Yuda" | "Kitabu cha Immanuel" |
| sura za 28-33 | "Ole Sita: Tano za kukoswa uaminifu wa Israeli na moja juu ya Ashuru" | "Kitabu cha Sayuni" (Jiwe Kuu la Pembeni) |

3. Baadhi ya mifano ya kutoeleweka kwa vipengele vya kifasihi (sura za 1-12)
   a. Muainisho wa sura za 1-12 na E. Y. Young, kurasa za 211-214
      (1) 1:1-12:6 Muainisho juu ya Unabii wa Yuda na Yerusalemu
         (a) 1:1-31 mashitaka makuu
         (b) 2:1-4:6 utawala wa Masihi na hukumu juu ya watu
         (c) 5:1-30 kushamiri kwa uovu wa Yuda
         (d) 6:1-13 maono ya Isaya juu ya Bwana
         (e) 7:1-12:6 Unabii unaozungumzwa wakati wa utawala wa Ahazi
   b. Muainisho wa sura za 1-12 na R. K. Harrison, kurasa wa 764
      (1) unabii juu ya kuharibiwa na kurejeshwa kwa Yuda, sura ya 1-5
      (2) Kuitwa kwa Isaya; vitu vya kihistoria, sura za. 6-8
      (3) ufalme wa kiulimwengu wa kisasa na kazi zake, sura za 9-12
   c. Muainisho wa sura 1-12 na Toleo la NIV Study Bible, kurasa wa 1016
      (1) Sura za 1-6
         (a) Utangulizi: mashitaka dhidi ya Yuda kwa kuvunja agano, sura 1
         (b) Nidhamu ya baadaye na utukufu wa Yuda na Yerusalemu, sura za 2-4
            i. Baraka za babadaye za Yerusalemu (2:1-5)

ii. Nidhamu ya Bwana kwa Yuda (2:6-4:1)
iii. Kurejeshwa kwa Sayuni (4:2-6)

(c) hukumu ya taifa na uhamisho (sura ya 5)
(d) agizo la pekee la Isaya (sura ya 6)

(2) Sura za 7-12

(a) Ahazi anaonywa asiogope Waaramu na muungano wa Wana wa Israeli (sura ya 7)
(b) mwana wa Isaya na mwana wa Daudi (8:1-9:7)
(c) Hukumu dhidi ya Israeli (9:8-10:4)
(d) Ufalme wa kiashuru na ufalme wa kidaudi (10:5-12:6)

i. kuharibiwa kwa kiashuru (10:5-34)
ii. kuanzishwa kwa ufalme wa kiadaudi (sura za 11)
iii. wimbo wa furaha kwa ajili ya ukombozi (sura ya 12)

IX. KWELI KUU

A. Isaya alishikilia Yuda katika uaminifu kwenye agano la ki-Daudi (II Samueli 7), Lakini pia alirejerea kwenye kusudi la asili la agano la ki-Ibrahimu (Mwanzo 12:1-3), ambalo lilikuwa ni Mungu kuchagua Israeli ili kuchagua ulimwengu (yaani Kutoka 19:5-6). Ni kwa kushangaza kiasi gani huku kutawala kwa ujumla kwa YHWH namna kulivyo. Mungu sio tu kwamba atarejesha Israeli, bali atapanua mpango wake wa ukombozi kwa ulimwengu mzima!

B. Isaya kibayana alitabiri uamsho wa matukio ya kiulimwengu katika siku zake yeye mwenyewe na katika siku za baadaye (hivyo hivyo Mika). Ufalme huu ni mtakatifu nani wa ulimwengu wote (vile vile kwa Mika). Hivi vyote ni vipengele vya uungu mmoja vitakatifu vya kiukombozi.

C. Isaya kwa uwazi anaonesha utupu na ujinga wa watu wa Mungu katika kutumaini katika nguvu za kibinadamu, ulimwengu ulioanguka. Ukombozi utakuja kutokea kwa YHWH tu!

D. Isaya anafunua tabia tatu zenye nguvu sana za mpango wa Mungu za ukombozi.

1. Masihi ajaye
2. Masihi kama mtumishi mwenye kuteseka
3. Utawala wa kiulimwengu wa Masihi

# ISAYA 40

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA* (Mabano yanaonyesha Ushairi) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ukuu wa Mungu | Watu wa Mungu Wanafarijika | Nabii anaitwa kutangaza ujio wa Mungu | Maneno yenye matumaini | Utabiri wa ukombozi |
| 40:1-2<br>(1-2) | 40:1-2<br>(1-2) | 40:1-2<br>(1-2) | 40:1-2<br>(1-2) | 40:1-2<br>(1-2) |
| 40:3-8<br>(3-8) | 40:3-5<br>(3-5) | 40:3-5<br>(3-5) | 40:3-5<br>(3-5) | 40:3-5<br>(3-5) |
| | 40:6-8<br>(6-8) | 40:6-11<br>(6-11) | 40:6-8<br>(6-8) | 40:6-8<br>(6-8) |
| 40:9-11<br>(9-11) | 40:9-11<br>(9-11) | | 40:9<br>(9) | 40:9<br>(9) |
| | | | 40:10-11<br>(10-11) | 40:10-11<br>(10-11) |
| | | Muumbaji wa ulimwengu | Mungu wa Israeli asiyelinganishwa | Ukuu wa Mungu |
| 40:12-17<br>(12-17) | 40:12-17<br>(12-14) | 40:12-17<br>(12-17) | 40:12-14<br>(12-14) | 40:12<br>(12) |
| | | | | 40:13-18<br>(13-18) |
| | (15-17) | | 40:15-17<br>(15-17) | |
| 40:18-20<br>(18-20) | 40:18-20<br>(18-20) | 40:18-20<br>(18-20) | 40:18-20<br>(18-20) | |
| | | | | 40:19-24<br>(19-24) |
| 40:21-26<br>(21-26) | 40:21-24<br>(21-23) | 40:21-23<br>(21-23) | 40:21-22<br>(21-22) | |
| | | | 40:23-26<br>(23-26) | |
| | (24) | 40:24<br>(24) | | |
| | 40:25-26<br>(25-26) | 40:25-26<br>(25-26) | | 40:25-31<br>(25-31) |
| 40:27-31<br>(27-31) | 40:27-31<br>(27-31) | 40:27-31<br>(25-31) | 40:27-31<br>(27-31) | |

*Ingawa hazikuvuviwa, mgawanyo wa aya ni ufunguo wa uelewa na ukifuata kusudio la mwandishi wa awali. Kila tafasiri ya kisasa imegawanyika na kuifupisha aya. Kila aya ina mada kuu, ukweli kuu, au wazo kuu. Kila toleo linafupisha mada hiyo katika njia yake tofauti. Jinsi unavyosoma andiko, jiulize mwenyewe ni tafasiri ipi inafaa kwenye uelewa wako juu ya somo na mgawanyo wa aya.

Katika kila sura lazima tusome biblia kwanza na kujaribu kutambua somo lake (aya), kwa hiyo linganisha uelewa wetu na matoleo ya kisasa. Mara tu unapoelewa kusudi la mwandishi wa awali kwa kufuata mantiki na uwasilishaji wake tunaweza kuielewa biblia. Mwandishi tu wa awali ndiye aliyevuviwa-wasomaji hawana mamlaka ya kubadiri au kuufanyia marekebisho ujumbe. Wasomaji wa biblia wana majukumu ya kutumia ukweli uliovuviwa katika siku zao na maisha yao. Angalia kuwa maandiko yote ya kiufundi na vifupisho vimeelezea kwa upana katika Kiambatisho cha Kwanza, cha Pili na cha Tatu.

**Kumbuka kuwa maneno yote ya kiufundi na vifupisho vyake yameelezewa kikamilifu katika kiambatisho cha kwanza, mbili, na tatu**

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozokwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Isaya aliishi katika karne ya 8 K.K, lakini bado Isaya 40-66 inafaa kwenye muundo wa kihistoria wa kurudi kwake toka uhamishoni Babeli chini ya Zerubabeli na Yoshua katika Ezra 1-6, kufuatia tamko la Koreshi II katika mwaka wa 538 K.K. (karne ya 6 K.K)
B. Kitabu cha Isaya ni cha maafikiano (angalia utangulizi). Mungu akaudhihirisha mpango wake wa mbeleni kwa mjumbe mwaminifu. Napinga nadharia ya waandishi wawili au watatu. Naamini kuwa kitabu kilihaririwa au kutungwa.
C. Mungu hajawahi kusahau ahadi zake za maagano, lakini ameanzisha agano jipya kwa namna ya mateka (kama vile Yer. 31:31-34). Hili agano jipya hatimaye linaelezewa katika maisha, huduma, kifo, na ufufuko wa Yesu.
D. Tukirudi kihistoria toka Babeli hakudhoofisha unabii, hatima ya mtizamo wa sura ya 40-66 ni kuja kwa mara ya kwanza na pili ya Masihi. Sura ya 40 inatengeneza utangulizi wa sura pekee za kimasihi zijulikanazo kama “nyimbo za Mtumishi” (kama vile 42:1-9; 49:1-7; 50:4-11; 52:14-53:13).
E. Kama Isaya 1-39 inavyoshughulika na mateka wa Ashuru na Babeli, sura ya 40-66 inazungumzia juu ya wale wanaorudi Yuda na Yerusalemu. Mazingira ya hadhira yalibadilika!
F. Aya za 1-11 zinatoa utangulizi na muhtasari wa kipengere kizima. Siku mpya imewadia!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:1-2**
**1 Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo,**
**watu wangu, asema Mungu wenu.**
**2 Semeni na moyo wa Yerusalemu,**
**kauambieni kwa sauti kuu ya kwamba vita vyake vimekwisha,**
**uovu wake umeachiliwa;**
**kwa kuwa amepokea kwa mkono wa Bwana adhabu maradufu kwa dhambi zake zote.**

**40:1 "Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo"** Neno hili (BDB 636, KB 688, *Piel* KAULI SHURUTISHI, WINGI) linatumka katika sura ya 1-39 mara tatu tu, lakini katika sura ya 40-66 mara kumi na nne (hasa katika neno *Piel*). Laweza kuwa ni cheo kwa ajili ya hiki kipengere cha Isaya. Kinaonyesha huruma ya uangalizi na uwajibikaji wa YHWH (kama vile 12:1). Neno lenyewe linaonekana ni kutokana na kule kuhema kwa nguvu kwa farasi. YHWH anaonekana kuhuzunika kwamba anapaswa kuwaadhibu watu wake. Adhabu imekwisha. Haijulikani kama hii ni kwa sababu ya kwamba

1. Wamekwisha tubu (yaani., Ezekiel 18)
2. YHWH kuchagua kutenda kwa niaba yao hata kama hawatubu ipasavyo (kama vile Ezek. 36:22-38).

Siku mpya (yaani., agano jipya, kama vile Yer. 31:31-34) imechwea! Inasimamia juu ya tabia ya YHWH, na sio utendaji wa watu wake (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3); uwezo wake, na sio wao; mpango wake wa milele ambao wao ni sehemu yake. Hoja moja zaidi juu ya aya ya ufunguzi. KITENZI kiko katika WINGI. Kwa hiyo YHWH anamuelezea nani kama msemaji wao?

1. Manabii mbalimbali (kama vile 52:8)
   a. Manabii binafsi
   b. "shule" (yaani., wafuasi) wa Isaya
2. Malaika wa baraza la mbinguni (yaani., "Sisi" wa Isaya 6:8 na 41:22-23)
3. Toleo la LXX linaongezea neno, "zungumzeni, enyi makuhani, na moyo wa Yerusalemu"

Tambua uhusiano uliopo kati ya UMOJA ("irabu" ya mistari ya 3 na 6, na VITENZI VYA WINGI). Kuna KAULI SHURUTISHI kumi na mbili katika mistari ya 1-11. Aya za 1-11 zinaainishwa na KAULI SHURUTISHI, wakati mistari ya 12-17 inaainishwa na mtiririko wa maswali yenye kutegemea jibu la "hapana". Kuwepo mara mbili kwa KAULI SHURUTISHI kunatoa msisitizo kwenye kitendo. Hii ilikuwa ni mbinu ya kawaida ya fasihi katika kipengere hiki cha Isaya (kama vile 51:9,17; 52:1,11; 57:14; 62:10).

◙**"watu wangu. . .Mungu wenu"** Haya ni maneno ya kimaagano (kama vile Mwanzo 12, 15, n.k.). kipindi cha Wayudi kukimbilia uhamishoni huko Babeli walipatwa na mshangao ikiwa YHWH alikuwa bado ni Mungu wao wa agano. Jina la Uungu hapa ni *Elohim* (angalia Mada Maalum katika 40:3) na mara zote linatumika kwa ajili ya Mungu kama muumbaji, mtoaji, na mwezeshaji wa maisha yote juu ya sayari hii. YHWH (kama vile mst. 2a) ni jina ambalo kwa kawaida linahusiana na Mungu kama alama ya agano (angalia Mada Maalum katika 52:6), mwokozi, na mkombozi.

### MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji.

Agano ni namna ambayo Mungu mmoja wa kweli anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadmu kwa wazi unaonekana katika dhana ya agano. Baadhi ya maagano

yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. wito wa Abramu(kama vile Mwanzo 12)
3. agano pamoja na Abramu (kama vile Mwanzo 15)
4. utunzaji wake na ahadi kwa Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. kwa imani Musa anawatoa wana wa Israeli toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Kumbukumbu la Torati 27-29)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika “agano jipya”. Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Eze. 18 na Eze. 36:27-38.). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na lile Jipya. Malengo ya haya yote ni sawa:

1. urejesho wa ushirika uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uanzishwaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu.

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubalifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu,watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo, Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, bali ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani, Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekena kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika kitabu cha Waebrania.

◙**“asema”** Kuna VITENZI mbalimbali (yaani., wanenaji mbalimbali tofauti) vilivyotumika katika sura hii vyenye kuhusiana na kuutangaza ujumbe mpya wa Mungu.

1. Semeni – BDB 180, *Piel* KAULI SHURUTISHI, mst. 2
2. kauambieni kwa sauti – BDB 894, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mistari ya 2,6
3. Sauti ya mtu aliaye – BDB 894, *Qal* KAULI TENDAJI SHURUTISHI
4. Paza sauti yako – BDB 926, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, mst. 9
5. Iambiye – BDB 55, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mst. 9

Hili linatenda kazi kama wito wa pili wa Isaya (kama vile sura ya 6). Kifungu cha maneno “hawatasikia. . .” sasa kimebadilishwa na kuwa “waambieni.”

**40:2 “kwa upole”** Hili ni nenoלבבב, “neno la upendo” toka kwenye asili ya neno “moyo” ("לב, BDB 523, KB 516, kama vile Mwa. 34:3; 50:21; Amu. 19:3; Ruth 2:13; Hos. 2:14). Biblia inatumia uhusiano wa karibu wa mwanadamu kuuelezea upendo wa Mungu na uhusiano wake na mwanadamu. Huu ni muundo wa sehemu ya lugha ya mwanadamu.

◙

**NASB, NKJV** **“vita”**
**NRSV** **“ameukomboa muda wake”**

**TEV** **"ameteseka vya kutosha"**
**NJB** **"kipindi cha huduma"**
**JPSOA** **"wakati wa huduma"**
**REB** **"wakati wa mateso umekwisha"**

Nomino (BDB 838, hapa JINSI YA KIKE lakini mara nyingi hutumika kama JINSI YA KIUME) yaweza kumaanisha

1. Vita
2. Vita (Dan. 10:1)
3. Utumishi wa Walawi (yaani Hes. 4:3,23,30,35,39,43)
4. Adhabu (kama vile Ayu. 7:1; 14:14; Isa. 40:2)

Israeli ilipaswa kuwa "ufalme wa kikuhani" (kama vile Kut. 19:5-6), lakini uasi wao ukabadilika kuwa "utumishi" wa Mungu ndani ya "adhabu" ya kuivumilia hukumu ya Mungu (mateka wa Ashuru na Babeli).

◙**"uovu umekwisha ondolewa"** Hii inamaanisha "adhabu ya uovu imekwisha kuondolewa (BDB 953, *Niphal* KAULI TIMILIFU, kama vile Law. 1:4; NASB ujumbe mdogo wa kukumbuka; TEV).

◙**"kwa mkono wa Bwana"** YHWH aliwapa Israeli hukumu kamili. Uvamizi na kukimbilia uhamishoni haikuwa nguvu ya Ashuru (yaani., 8:7; 10:5) wala Babeli bali ni kutoka kwa YHWH. Mtazamo wa dunia ya Mashariki ya Kale ulikuwa kwamba pindi nchi zinapokwenda kwenye vita, miungu yao hupigana na Yule mwenye nguvu ndiye hushinda, lakini huu sio ukweli wenyewe. Israeli ilishindwa na kukimbilia uhamishoni kwa sababu ya dhambi zake dhidi ya YHWH. Akaileta hukumu.
Neno "mkono" ni lahaja ya Kisemiti kwa ajili ya uwakala.

## MADA MAALUM: MKONO (KAMA ILIVYOELEZEWA TOKA EZEKIELI)

Neno "mkono" (BDB 388, KB 386) lina matumizi na madokezo mbalimbali.

1. kwa maana iliyo wazi (yaani., mkono wa binadamu)
   a. alama ya mtu kamili, Ezek. 3:18; 18:8,17; 33:6,8
   b. alama ya udhaifu wa mwanadamu, Ezek.7:17,27; 21:7; 22:14
   c. alama ya maadui wa kigeni, Ezek. 7:21; 11:9; 16:39; 21:31; 23:9,28; 28:10; 30:12; 34:27; 38:12; 39:23
   d. kwa maana iliyo wazi mkono, Ezek. 8:11; 12:7; 16:11; 37:17,19,20
   e. alama ya mamlaka ya kiongozi mbovu, Ezek. 13:21,22,23; 34:10
   f. alama ya taifa, Ezek. 23:31,37,42,45; 25:14; 27:15; 28:9; 30:10,22,24,25; 31:11; 39:3
2. lugha ya kibinadamu kumwelezea Mungu
   a. namna ya utoaji maono wa YHWH, Ezek. 1:3; 3:14,22; 8:1; 33:22; 37:1; 40:1 (2:9 ni taswira nyingine ya ufunuo – gombo lililoshikiliwa mkononi)
   b. mamlaka ya YHWH katika hukumu, Ezek. 6:14; 13:9; 14:9,13; 16:27; 20:33; 25:7,13,16; 35:3; 39:21
   c. YHWH Mwenyewe (uwepo wake binafsi), Ezek. 20:22
   d. mamlaka ya YHWH ya kuokoa, 20:34 (yumkini matumizi muhimu toka Kutoka, kama vile 3:20; 4:17; 6:1; 7:19; 13:3)
3. lugha ya kibinadamu kuelezea *Makerubi*, Ezek. 1:8; 8:3; 10:7,8,12,21
4. lugha ya kibinadamu kuelezea malaika wa maangamizi, Ezek. 9:1-2; 21:11
5. alama ya ahadi au kiapo, Ezek. 17:18; 20:5 (mara mbili), 6,15,23,28; 36:7; 44:12; 47:14
6. alama ya furaha, Ezek. 25:6
7. lugha ya kibinadamu kumwelezea malaika, Ezek. 40:3,5; 47:3

◙**"amepokea maradufu kwa dhambi zake zote"** Hili si la kimahesabu bali ni la kiushairi kwa ajili ya habari nzima (kama vile Yer. 16:18; Ufu. 18:6; kwa maana iliyo chanya angalia Isa. 61:7; Zak. 9:12). Rehema huja baada ya hukumu (yaani., Law. 26:40-45).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:3-8**
**3 Sikiliza, ni sauti ya mtu aliaye,**
**Itengenezeni nyikani njia ya Bwana;**
**Nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu.**
**4 Kila bonde litainuliwa,**
**Na kila mlima na kilima kitashushwa;**
**Palipopotoka patakuwa pamenyoka,**
**Na palipoparuza patasawazishwa;**
**5 Na utukufu wa Bwana utafunuliwa,**
**Na wote wenye mwili watauona pamoja;**
**Kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya.**
**6 Sikiliza, ni sauti ya mtu asemaye, Lia!**
**Nikasema, Nilie nini?**
**Wote wenye mwili ni majani,**
**Na wema wake wote ni kama ua la kondeni;**
**7 Majani yakauka, ua lanyauka;**
**Kwa sababu pumzi ya Bwana yapita juu yake.**
**Yakini watu hawa ni majani.**
**8 Majani yakauka, ua lanyauka;**
**Bali neno la Mungu wetu litasimama milele.**

**40:3 "Itengenezeni njia ya Bwana"** KITENZI hiki (BDB 815, *Piel* KAULI SHURUTISHI) kimsingi kinamaanisha "geukeni," lakini hapa kinatumika kwa maana maalumu ya "kutengeneza njia ya vitu" (kama vile 40:3; 42:16; 49:11; 57:14; 62:10; Mal. 3:1).
Dhana ya "njia ya utakatifu" juu ya watu wa Mungu (waliorudi toka utumwani) wakimrudia Yeye (yaani., kwenye hekalu lake) ni yenye kujirudia katika Isaya (kama vile 11:16; 26:7; 35:8; 42:13).
Katika muktadha huu ni YHWH Mwenyewe anayewarudia watu wake. Wanapaswa kuiandaa njia, ikimaanisha maandalizi ya kiroho/kimwili.
Aya hii ni usanifishaji binafsi wa Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 3:3; Marko 1:3; Luka 3:4-6). Kipenegere hiki kimedhihirishwa katika Zak. 14:10, ambapo uwekaji sawa wa mandhari ya nchi kuelekea Yerusalemu unatumika kama stiari kwa ajili ya njia ya kumfikia Mungu (kama vile Mal. 3:1; 4:5,6). Yaweza kuainishwa kama "itengenezeni njia" (kumbuka mistari yenye kufanana).

◙**"Bwana"** Hili ni rejeo kwa YHWH. Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

A. *El*(BDB 42, KB 48)
   1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, "kuwa shupavu" au "kuwa mwenye nguvu" (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).
   2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra),akaitwa "baba wa miungu" na "bwana wa mbinguni"
   3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
      a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sanaBDB 42 & 751 II), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
      b. *El-Roi* ("Mungu aonaye" au "Mungu ajifunuaye Mwenyewe" BDB 42 & 909), Mwanzo 16:13
      c. *El-Shaddai* ("Mungu Mkuu" au "Mungu mwenye huruma zote" au "Mungu wa mlima"), BDB 42 & 994) Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
      d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu

kwa Daudi, II Sam. 7:13,16

   e. *El-Berit* (Mungu wa Agano"), BDB 42 & 136), Waamuzi 9:46

4. *El* inalinganishwa na
   a. YHWH katika Zaburi. 16:1-2; 85:8; Isa. 42:5, Hes. 23:8
   b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, "Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
   c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
   d. "wivu" katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
   e. "rehema" katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31
   f. "mkuu na mzuri" katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
   g. "maarifa" katika I Sam. 2:3
   h. "kimbilio langu" katika II Sam. 22:33
   i. "mlipa kisasi wangu" katika II Sam. 22:48
   j. "mtakatifu" katika Isa. 5:16
   k. "muweza" katika Isa. 10:21
   l. "wokovu wangu" katika Isa. 12:2
   m. "mkuu na mwenye nguvu" katika Yer. 32:18
   n. "anayepatiliza: katika Yer. 51:56
5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH,* kurudiwa)

B. *Elyon*(BDB 751, KB 832)
1. Maana yake ya msingi ni "juu," "aliyetukuzwa," au "kuinuliwa" (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme.
   18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
   a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
   b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
   c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
   d. *El* - Hes. 24:16
   e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya "Mungu aliye Juu") katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
   a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
   b. Balaamu, Hes. 24:15
   c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
   d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)

C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
3. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
4. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7.
5. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104).

Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*Elohim* KUR. 1,2,5; YHWH, kur. 2,6; hata *Adoni*, uk. 4) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.

6. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa

Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.

7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
   a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa "wingi wa ukuu," mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
   b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7.
   c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH (BDB 217, KB 394)

1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na*Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo
   a. Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili, Zaburi 104)
   b. Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu (Zaburi 103).

Mwanzo 2:4-3:24 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.

2. Katika Mwanzo 4:26 inasema"*wanadamu* wakaanza kuliiitia jina la BWANA" (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
   a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
   b. kutoka katika mzizi wa kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
   c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) "kuzungumza"
   d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha "Yeye anayetosheleza," au "yeye anaye anzisha"
   e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "Yeye ambaye yupo," au "Yeye aliyepo sasa" (katika namna ya wakati ujao, "Yeye atakayekuwako")
   f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* "yeye asababishaye kuwa"
   g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwanzo. 3:20), maana "Mungu mmoja tu aishiye milele"
   h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, "nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
      (1) *Yah* (mfano Hallelu – yah, BDB 219, kama vile Kut. 15:2; 17:16; Zab. 89:8; 104:35)
      (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
      (3) *Yo* (majina mfano Joeli)

3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania

"mmiliki," "Mkuu," "mume," "bwana"—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka "bwana." Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.

4. Kama ilivyo kwa*El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
   a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa ), Mwanzo. 22:14
   b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), BDB 217 & 950, *Qal* HALI YA KUENDELEA),Kutoka. 15:26
   c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), BDB 217 & 651,Kutoka. 17:15
   d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye, BDB 217 & 872, *Piel* HALI YA KUENDELEA),Kut. 31:13
   e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 & 1022)*,* Waamuzi. 6:24
   f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi ,BDB 217 & 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
   g. *YHWH - Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu,BDB 217 & 944, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Zab. 23:1
   h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 & 841), Yer. 23:6
   i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa**,**BDB 217 & 1027), Eze. 48:35

◙**"nyikani"** Ezekieli aliuona utukufu wa Mungu ukiondoka hekaluni huko Yerusalemu na kuelekea mashariki (kama vile Ezek. 10:18-19; 11:22-23; 43:1-3). Mungu aliondoka na mateka na aya hii inarejerea kurudi kwake Yuda na Yerusalemu.

**40:4** Muktadha huu unarejerea kwenye maandalizi ya watu wa Mungu kwa ajili ya kurudi kwake Yerusalemu. Utaambana na kurudi kwa mateka. Atawalinda, kuwalisha, na kuwatunza (kama vile mistari ya 9-11). Huu ni mwendelezo na maelezo ya kuitengeneza njia nyikani. Ni stiari kwa ajili ya watu kumwendea Mungu pasipo gharama. Mungu ameishatoa njia mpya (yaani., agano jipya, kama vile Yer. 31:31-34). Hii njia mpya imechukuliwa kama namna mpya ya kuondoka

1. Hapa kutoka katika utumwa wa kimwili
2. Kiistiari ni kwa ajili ya siku ya mwisho

**40:5 "utukufu wa Bwana"** Utukufu wa Bwana ni uhusiano mwingine kwa Isaya 6 (yaani., mst. 3). Sura ya 40 inatenda kazi kama wito wa pili wa Isaya. Angalia Mada Maalum katika mst. 25.
Hili ni dokezo la "wingu la utukufu" ambalo lilionekana kipindi cha wana wa Israeli wakitoka Misri na kipindi cha kutangatanga nyikani kama alama ya uwepo binafsi wa Mungu. Walimu wa Kiyahudi waliliita *Shekinah*, kutokana na neno la Kiebrania "kuishi." Wayahudi waliorudi walihitaji kuhakikishiwa upya mwendelezo wa uwepo binafsi wa Mungu (kama vile Kut.13:21-22; 14:19). Safari mpya imewadia!
Kwa ajili ya "utukufu" angalia Mada Maalum katika 42:8.

◙**"na wote wenye mwili watauone pamoja"** "Mwili" (BDB 142) inamaanisha wanadamu (kama vile mst. 7). Hii ni sehemu ya ulimwengu (yaani., 49:6; 51:4-5; 52:10) ambayo inaainishwa na Isaya.

◙**"kwa kuwa kinywa cha Bwana kimenena haya"** Hii ni lahaja ya Kiebrania kwa ajili ya nguvu ya neno lililonenwa na YHWH (kama vile mst. 8; Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,26 na Isa. 55:11).

**40:6 "Lia"** Angalia kumbukumbu katika 40:1.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"akajibu"** |
| **NKJV** | **"akasema"** |
| **NRSV, NJB** | **"nimesema"** |

**TEV** **"nauliza"**
**REB, LXX,**
**DSS** **"nimeuliza"**

Tambua kuwa irabu mbili zinahusika hapa. Kufuatia toleo la DSS, kwenye tolea la LXX linaonekana kumaanisha ni malaika/roho akiongea na Isaya.

◙**"wenye mwili ni majani"** Hii stiari yenye kujirudia inarejerea kwenye udhaifu na kuishi kwa muda kwa mwanadamu ukilinganisha na umilele wa Mungu (kama vile Mwa. 6:3; Ayubu 10:4; 14:1-2; Zab. 78:39; 90:5-6; 103:15-18; I Pet. 4:24-25).
Ni nani anayeongelewa?
1. Wanadamu wote
2. Mataifa yenye nguvu

Inavyoonekana ni ujumbe wa Mungu kwa ajili ya serikali ya Mwanadamu. Yawezakuwa ni nguvu ya muda, lakini kwa wakati wake na kwa ukweli (yaani., katika nuru ya nguvu za Mungu) siyo!!

◙**"wema wake"** Hili limetafasiriwa toka neno la Kiebrania*hesed* (kama vile BDB 338, I, #4). Hili neno linatumika kama agano la Mungu la upendo na uaminifu.

## MADA MAALUMU: WEMA (*HESED)*

Neno hili (BDB 338 I, KB 336 II) lina maeneo mapana ya maana.

A. Lilitumika katika kuwaunganisha wanadamu
   1. Wema kwa wenzetu (mf. 1 Sam. 20:14; 2 Sam. 16:17; 2 Nya. 24:22; Ayubu 6:14; Zab. 141:5; Mit. 19:22; 20:6)
   2. wema kwa maskini na wahitaji (mf. Mika 6:8)
   3. upendo wa Israeli kumuelekea HWH (kama vile Yer. 2:2; Hos. 6:4,6)
   4. uzuri wa maua ya kondeni (kama vile Isa. 40:6)
B. Lilitumika katika uungaishaji na Mungu
   1. uaminifu wa agano na upendo
      a. " ukombozi kutoka katika maadui na taabu" (mf. Mwa. 19:19; 39:21; Kut. 15:13; Zab. 31:16; 32:10; 33:18,22; 36:7,10; 42:8; 44:26; 66:20; 85:7; 90:14; 94:18; 107:8,15,21,31; 109:21-22; 143:8,12; Yer. 31:3; Ezr. 7:28; 9:9)
      b. "katika ulinzi wa maisha kutokka katika kifo" (mf. Ayubu 10:12; Zab. 6:4-5; 86:13)
      c. "katika wepesi wa maisha ya kiroho" (mf. Zab. 119:41,76,88,124,149,159)
      d. "katika ukombozi wa kutoka dhambini" (kama vile Zab. 25:7; 51:1; 130:7-8)
      e. "katika kutunza maagano" (mf. Kum. 7:9,12; 2 Nya. 6:14; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4; Mik. 7:20)
   2. kuzielezea sifa za Mungu (mf. Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoel 2:13; Yona 4:2; Mika 7:20)
   3. wema wa Mungu
      a. "utele" (mf. Hes.14:18; Neh. 9:17; Zab. 86:5; 103:8; 145:8; Yoeli 2:13; Yer. 4:2)
      b. "ukuu katika kiwango chake" (mf. Kut. 20:6; Kum. 5:10; 7:9)
      c. "umilele" (mf. 1 Nya. 16:34,41; 2 Nya. 5:13; 7:3,6; 20:21; Ezra 3:11; Zab. 100:5; 106:1; 107:1; 118:1,2,3,4,29; 136:1-26; 138:8; Yer. 33:11)
      d. nguvu zilizo sawa (mf. Zab. 59:17)
      e. ilihusiana na nguvu za Mungu (mf. Zab. 62:11c-12a)
   4. matendo ya wema (mf. 2 Nya. 6:42; Zab. 89:2; Isa. 55:3; 63:7; Omb. 3:22)

Neno hili linatafsiriwa kwa njia mbalimbali katika tafsiri za Kiingereza. Nafikiri maelezo bora yaliyo katiaka ufupisho yangelikuwa "hakuna kamba iliyounganisha utii wa agano la Kimungu" neno hili ni sambamba na neno la Agano Jipya "upendo" (agapaō). Munguni mwaminifu na mwenye upendo kwa sababu ya Yeye

**40:7-8** VITENZI vyote ni KAULI TIMILIFU (yaani., kitendo kamili) isipokuwa maelezezo ya kuhitimisha, "neno la Mungu wetu litadumu milele" (KAULI ISIOTIMILIFU).
Huu ulikuwa ni ukweli kwamba kurudi kwa mateka kulihitajika. Inaonekana kuwa neno la Mungu kwa ajili ya uangalizi na ulinzi umekwisha shindwa! Hata hivyo, tatizo halikuwa neno la Mungu, bali ni watu wa mungu waliotenda dhambi!

**40:7 "pumzi"** Hili neno la Kiebrania*ruah* (BDB 924) laweza kumaanisha "upepo," "pumzi," au "roho."

## MADA MAALUM: ROHO KATIKA BIBLIA

I. Agano la Kale (*ruah*, BDB 924, KB 1197; angalia Mada Maalum: Uhai, Upepo, Roho [Agano la Kale])
   A. matendo ya wenye kuamini Mungu mmoja (yaani., Roho, ikitumika mara 90 katika Agano la Kale)
      1. kwa maana chanya, Mwanzo 1:2
      2. kwa maana hasi, 1 Sam. 16:14-16,23; 1 Fal. 22:21-22; Isa. 29:10
   B. nguvu ya Mungu atoaye uhai kwa mwanadamu (yaani., uhai wa Mungu, kama vile Mwa. 2:7)
   C. tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yanalitafasiri neno *ruah* kama *pneuma* (likitumika mara 100 katika toleo la LXX)
   D. baadaye maandiko ya dini ya Kiyahudi, maandiko kuhusu matukio ya siku ya mwisho na magombo ya Bahari ya Chumvi, yakishawishiwa na wafuasi wa Zoroastria, *pneuma* linatumika kuhusu malaika na mapepo

II. maneno ya Kiyunani
   A. *pneō*, kuvuma
   B. *pnoē*, upepo, uhai
   C. *pneuma*, roho, upepo
   D. *pneumatikos*, kufungamana katika roho
   E. *pneumatikōs*, kiroho

III. Historia ya nyuma ya falsafa ya Kiyunani (*pneuma)*
   A. Aristotle walilitumia neno kama nguvu ya maisha inayojengeka tokea kuzaliwa mpaka pale unapojitambua.
   B. Jamii ya wanafilosofia wa kale walilitumia neno hili kama kisawe cha neno *psuchē,* (nafsi) hata *nous* (fikra) katika maana ya milango mitano ya fahamu na ufahamu wa mwanadamu.
   C. katika mawazo ya Wayunani neno likajakuwa lenye kuendana na tendo la Kiungu (yaani., utabiri, miujiza, ushirikina, unabii, n.k.).

IV. Agano Jipya (*pneuma*; angalia Mada Maalum: Roho katika Agano Jipya)
   A. Uwepo maalum wa Mungu, mamlaka, na uwezesho
   B. Roho anahusiana na kazi ya Mungu katika kanisa (zaidi katika Yohana)
      1. Unabii
      2. Miujiza
      3. ujasiri wa kuitangaza injili
      4. hekima (yaani., injili)
      5. furaha
      6. kuwaleta katika enzi mpya
      7. mabadiliko (yaani., kuomboleza na kuishi ndani yetu)
      8. Kufanana na Kristo
      9. karama maalum za huduma
      10. maombi ya waamini

Roho huamsha shauku ya mwanadamu kwa ajili ya ushirika pamoja na Mungu, kwa namna walivyoumbwa. Huu ushirika unawezekana kwa sababu ya kazi na hali ya ubinadamu wa Yesu, Masihi wa Mungu (angalia Mada Maalum: Masihi). Uamusho mpya wa kiroho hutuongoza katika maisha yanayomfanana Yesu, uhudumiaji, na kuamini.

   C. kwa uzuri yaweza kufahamika kama mwendelezo wa kiroho pamoja na Roho Mtakatifu kwa

upande mwingine, na mwanadamu kama kiumbe mwenye mwili wa sayari hii, lakini pia kiumbe cha kiroho katika taswira ya Mungu, kwa upande mwingine.

D. Paulo ni mwandishi wa Agano Jipya ambaye alianzisha thiolojia ya Roho/roho.
   1. Paulo hutumia Roho kutofautisha mwili (yaani., asili ya dhambi)
   2. Paulo hutumia roho kuutofautisha mwili
   3. Paulo hutumia Roho/roho kutofautisha fikra za mwanadamu, ufahamu, ubinadamu

E. baadhi ya mifano toka 1 Wakorintho
   1. Roho Mtakatifu, 1 Kor. 12:3
   2. Nguvu na hekima ya Mungu huelezewa kupitia Roho Mtakatifu, 1 Kor. 2:4-5
   3. Matendo ya Mungu kupitia waumini
      a. mawazo mapya, 1 Kor. 2:12; 14:14,32
      b. hekalu jipya, 1 Kor. 3:16; 6:19-20
      c. maisha mapya (yaani., uadilifu), 1 Kor. 6:9-11
      d. maisha mapya yanayoonyeshwa katika ubatizo, 1 Kor. 12:13
      e. kuwa pamoja na Mungu (yaani., kubadilishwa), 1 Kor. 6:17
      f. hekima ya Mungu, na sio hekima ya kidunia, 1 Kor. 2:12-15; 14:14,32,37
      g. kukirimiwa karama za kiroho kwa kila mwamini kwa ajili ya huduma, 1 Wakorintho 12 na 14
   4. utofauti wa kiroho na kimwili, 1 Kor. 9:11; 10:3; 15:44
   5. tofauti ya ulimwengu wa kiroho na ulimwengu wa kimwili, 1 Kor. 2:11; 5:5; 7:34; 15:45; 16:18
   6. namna ya kurejerea maisha ya ndani/ukiroho wa mwanadamu kama utofautianavyo toka mwili wa mtu, 1 Kor. 7:34

F. Mwanadamu huishi katika aina mbili za ulimwengu kutokana na uumbaji (yaani., ulimwengu wa kimwili na wa kiroho). Mwanadamu akashindwa kuwa na ushirika wa karibu na Mungu (Mwanzo 3). Kupitia maisha ya Kristo, kifo, ufufuo, na ahadi ya kurudi tena, Roho humwombolezea mwanadamu aliyeanguka kutumia imani katika injili (yaani., Yohana 6:44,65), kwa namna fulani wamerejeshwa kwenye ushirika pamoja na Mungu. Roho ni sehemu mojawapo ya Utatu ambao huainisha enzi mpya ya haki. Roho ni mwakilishi wa Mungu na Mwana ni mtetezi katika "zama" hizi (angalia Mada Maalum: Yesu na Roho). Tatizo linaendelea kuwepo kwa vile zama mpya imejitokeza kwa wakati muafaka, wakati zama za kale za dhambi za uasi bado zipo zinaendelea kuwepo. Roho hubadilisha zama za kale kuwampya, ingawa zote bado zingali zikiishi.

**40:8 "neno la Mungu litadumu milele"** Ahadi za Mungu ni za uhakika, hata katikati ya nidhamu ya Kiungu (kama vile Zab. 103:17-18; Isa. 55:8-11; 59:21; Yer. 29:10; Mt. 5:17-20; 24:35). Haya maelezo ni imani thabiti ya tumaini/uhakika wa kila mwamini.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:9-11**
**9 Wewe uuhubiriye Sayuni habari njema,**
**Panda juu ya mlima mrefu;**
**Wewe uuhubiriye Yerusalemu habari njema,**
**Paza sauti kwa nguvu;**
**Paza sauti yako, usiogope;**
**Iambie miji ya Yuda, Tazameni, Mungu wenu.**
**10 Tazameni, Bwana Mungu atakuja kama shujaa,**
**Na mkono wake ndio utakaomtawalia;**
**Tazameni, thawabu yake i pamoja naye,**
**Na ijara yake i mbele zake.**
**11 Atalilisha kundi lake kama mchungaji,**
**Atawakusanya wana-kondoo mikononi mwake;**
**Na kuwachukua kifuani mwake,**
**Nao wanyonyeshao atawaongoza polepole.**

**40:9 "Wewe Sayuni. . .wewe Yerusalemu"** Maneno haya yote yanairejerea Yerusalemu. Hekalu lilijengwa juu ya Mlima Moria lakini neno"Sayuni" (kilima kingine ndani ya mji ambapo Daudi aliweka makazi yake) ni lahaja kwa ajili ya mji wote.

Uwainishaji huu unamrejerea nani?

1. Manabii wa Mungu
2. Walimu wa Kilawi
3. Wajumbe wa zama mpya (yaani., Yohana Mbatizaji)

Je? Hili linarejerea kwa

1. Waliorudi toka uhamishoni Babeli (yaani., 52:7-9; 62:10-12)
2. Ushindi wa wamakabayo
3. Kuja kwa Yesu mara ya kwanza (Isa. 62:11 lililorejerewa katika Mt. 21:50
4. Kuja kwa Yesu mara ya pili (Isa. 40:10; 62:11, kulikodokezwa katika kitabu cha ufunuo 22:12)

Kuna sintofahamu kati ya (1) ahadi ya Mungu ya kuirejesha Israeli na (2) zama mpya katika Kristo. Hapa ni pale simulizi kubwa lazima ijumuishe agano Jipya. Yesu alilitimiliza hili tumaini, lakini ujio mara mbili wa Yesu (Mwokozi, baadaye mfalme) kulisababisha utimilifu wa mara ya pili. Nabii hizi za matukio ya siku za mwisho bado ni za mbeleni. Pasi na shaka halikutimilizwa katika ujio wa Zurubabeli na Yoshua mwaka wa 539 K.K. na tena sio katika kipindi cha maisha ya Yesu wa Nazareti.

Wazo moja jingine, kwenye aya, mistari ya 9-11, ni tangazo "mlinzi" kwenye mji unaokabiliwa na kikundi cha watu/jeshi. Hata hivyo, tambua Yule mwenye nguvu (yaaani., Mungu) anakuja, na sio kama mvamizi lakini kama mchungaji mwenye huruma. Anakuja kuokoa, kulinda na kama mpaji. Wachungaji wa Isaeli (Zaburi 23) wakairudia nchi/watu wao waliowaacha katika Ezekieli 8-10!

## MADA MAALUM: UTABIRI WA AGANO LA KALE JUU YA WAKATI UJAO DHIDI YA UTABIRI WA AGANO JIPYA ("UTANGULIZI WA MUHIMU" KWA UFUNUO)

Wakati wote wa kujifunza kwangu matukio ya siku za mwisho nimejifunza kwamba Wakristo wengi hawana mfuatano wa matukio ya siku za mwisho au hawataki kuukuza. Kuna baadhi ya wakristo ambao wanaweka shabaha zao au wanaamua kujikita kwenye eneo la Ukristo kwa sababu za kithiolojia, kisaikolojia au kidini. Wakristo hawa wanaonekana kuchanganyikiwa na kwa namna gani itamalizika na kwa namna fulani kukosa umaana wa injili! Waaminio hawawezi kuathiri ajenda ya Mungu ya siku za mwisho, lakini wanaweza kushiriki katika upelekaji wa injili (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Waaminio wengi wanathibitisha kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na kupelekea kwa siku za mwisho kwa ahadi za Mungu. Matatizo ya kiufasiri yanaibuka kutoka kwa namna gani kilele hiki cha muda kitakuja kutoka katika mitazamo kadhaa ya kibiblia (Angalia Mada Maalum:Ukinzani katika Maandiko)

1. mvutano katika ya nadharia za kinabii za agano la kale na nadharia za kitume za Agano Jipya
2. mvutano kati ya hali ya kuabudu Mungu mmoja (Mungu mmoja kwa ajili ya wote) na kuchaguliwa kwa Israeli (watu maalum)
3. mvutano katika ya hali ya kipengele chenye masharti cha maagano ya kibiblia na ahadi ("ikiwa. . .ndipo") na hali isiyo na masharti ya uaminifu wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka
4. mvutano kati ya aina za fasihi za Mashariki ya Karibu na nadharia za magharibi za kifasihi
5. mvutano kati ya ufalme wa Mungu kwa sasa na ule wa baadaye.
6. mvutano kati ya imani katika kurudi punde kwa Kristo na imani kwamba baadhi ya matukio lazima yatokee kwanza.

Ebu kwanza tujadili mivutano hii moja baada ya nyingine

**MVUTANO WA KWANZA** (vipengele vya kijiografia, kitaifa na kikabila vya Agano la Kale dhidi ya waaminio wote katika ulimwengu)

Manabii wa Agano la Kale walitabiri kurejeshwa kwa ufalme wa Kiyahudi katika Palestina ukiwekwa kitovu

Yerusalemu ambapo mataifa yote ya nchi yatakusanyika kusifu na kutumikia mtawala wa Ki-Daudi, lakini Yesu au Mitume wa Agano Jipya hawajikiti katika agenda hii. Je kwani Agano la Kale halijavuviwa (kama vile Mt. 5:17-19)? Je waandishi wa Agano jipya wameondoa sehemu muhimu za matukio ya siku za mwisho?
Kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu:

1. manabii wa Agano la Kale (Isaya, Mika, Malaki)
2. waandishi wa siku za mwisho (kama vile Ezek. 37-39; Dan. 7-12; Zek.)
3. Kipindi kati ya kuandikwa kwa Agano la Kale na Agano Jipya, waandishi wa siku za mwisho wa kiyahudi wasio wakanoni (kama I Enoch, ambaye anaelezewa katika Yuda)
4. Yesu mwenyewe (kama vile Mt. 24; Marko 13; Luka 21)
5. maandiko ya Paulo (kama vile I Kor. 15; II Kor. 5; I The. 4-5; II The. 2)
6. maandiko ya Yohana (I Yohana na Ufunuo).

Je haya yote kwa ufasaha yanafundisha ajenda ya siku za mwisho (matukio, mpangilio wa matukio, watu)? Ikiwa sio, kwanini? Je si kwamba wote wamevuviwa (isipokuwa maandiko ya kiyahudi ya kati ya kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya)?
Roho alifunua kweli kwa waandishi wa Agano la Kale kwa namna na vipengle ambavyo wangeweza kuelewa. Hatahivyo kupitia ufunuo endelevu Roho amepanua dhana hizi za matukio ya siku za mwisho kwa mtazamo wa kijumla ("siri za Kristo," kama vile Efe. 2:11-3:13. Angalia Mada Maalum katika 10:7). Hii hapa ni baadhi ya mifano inayoelekeana kwa umuhimu:

1. Jiji la Yerusalemu katika Agano la Kale linatumika kama sitiari ya watu wa Mungu (Sayuni), lakini inakadiriwa katika Agano Jipya kama neno linaloelezea ukubalifu wa Mungu wa watubuo wote na wanadamu waaminio (Yerusalemu mpya ya Ufunuo 21- 22). Upanuzi wa kithiolojia wa jiji la kibayana la kimwili katika watu wapya wa Mungu (Wayahudi na Mataifa waaminio) inaakisiwa kwa kuoneshwa mbele katika ahadi za Mungu kukomboa mwanadamu aliyeanguka katika Mwanzo 3:15, kabla hata haijakuwako Myahudi yeyote au mji mkuu wa kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (kama vile Mwanzo 12:1-3) ilijumuisha Mataifa (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5).
2. Katika Agano la Kale adui za watu wa Mungu ni mataifa yazungukayo mataifa ya Mashariki ya Karibu ya Kale, lakini katika Agano Jipya wamepanua kwa watu wasio amini, walio kinyume na Mungu na waliovuviwa kishetani. Vita vimehamisha kutoka kijiografia, kimgogoro wa kikanda kwenda ulimwenguni kote, mgogoro wa kiulimwengu (kamavile Wakolosai).
3. Ahadi ya nchi ya ambalo ni jambo kuu sana katika Aano la Kale (Ahadi kwa mababa wa imani katika Mwanzo, kama vile Mwanzo 12:7; 13:15; 15:7,15; 17:8) sasa imekuwa kwa dunia yote. Yerusalemu mpya inashuka chini kwa dunia iliyotengenezwa upya, sio Mashariki ya Karibu tu au kutojumuisha (kama vile Ufunuo 21-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ni dhana za kinabii za Agano la Kale zilizopanuliwa ni
   a. uzao wa daudi saa umetahiriwa kiroho(kama vile Rum. 2:28-29)
   b. watu wa agano sasa wanajumuisha Mataifa (kama vile Hos. 1:10; 2:23, akinukuu katika Warumi 9:24-26; pia Mambo ya Walawi 26:12; Kutoka 29:45, ikinukuliwa katika II Kor. 6:16-18 na Kutoka 19:5; Kumb. 14:2, ikinukuliwa katika Tito 2:14)
   c. hekalu sasa ni Yesu (kama vile Mt. 26:61; 27:40; Yohana 2:19-21) na kupitia kanisa la mahali pamoja (kama vile I Kor. 3:16) au mwamini mmoja mmoja (kama vile I Kor. 6:19)
   d. Hata Israeli na tungo zinazofunua tabia za Agano la Kale sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu (yaani "Israeli," kama vile Rum. 9:6; Gal. 6:16, yaani "ufalme wa makuhani," kama vile I Pet. 2:5, 9-10; Ufunuo 1:6)

Nadharia ya kinabii imetimilizwa, imepanuliwa na sasa imekuwa jumuishi. Yesu na waandishi wa kitume hawawasilishi nyakati za mwisho kwa namna ile ile ya Manabii wa Agano la Kale (kama vile Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecyand Fulfillment*). Wafasiri wa kisasa wanaojaribu kulifanya nadharia ya Agano la Kale kuwa ya maana ya wazi au ya tabia ya kawaida kugeuza ufunuo katika kitabu cha kiyahudi kabisa na kulazimisha maana! Waandishi wa Agano Jipya hawawakatai manabii wa Agano la Kale lakini wanaonesha ufanyaji wao kazi wa kilele wa kiulimwengu. Hakuna mpangilio au mfumo wa kimantiki kwa matukio ya siku za mwisho ya Yesu au Paulo. Makusudi yao kimsingi ni ukombozi na sio uchungaji.

Hatahivyo, hata ndani ya Agano Jipya kuna mvutano. Hakuna mfumo wa wazi wa matukio ya siku za mwisho. Katika njia nyingi Ufunuo kwa kushangaza unatumia Maelezo ya Agano la Kale katika kuelezea mwisho badala yamafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko 13)! Inafuata aina ya fasihi iliyoanzisha na Ezekieli, Daniel na Zekaria lakini ilikuzwa wakati wa kipindi kati ya uandishi wa Agano la Kale na Agano Jipya (fasihi ya kiyahudi ya siku za mwisho). Hii inaweza kuwa ilikuwa nji ya Yohana kuunganisha Maaagano ya Kale na Jipya. Inaonesha utaratibu wa zama-kuu ya uasi wa kibinadamu na kujizatiti kwa Mungu katika ukombozi! Lakini lazima itambuliwe kwamba ingawa Ufunuo unatumia lugha, watu na matukio ya Agano la Kale, inafasiri kwa ufahamu na namna ya karne ya kwanza ya Rumi (kama vile Ufunuo 1:7).

**MVUTANO WA PILI** (hali ya kuabudu Mungu mmoja dhidi ya wateule wa Mungu)

Msisitizo wa kibiblia upo juu ya Mungu binafsi, kiroho, muumbaji-mkombozi (kama vile 8:10; Isa. 44:24; 45:5-7,14,18,21- 22; 46:9; Yer. 10:6-7). Upekee wa Agano la Kale katika siku zake ilikuwa hali ya kuabudu Mungu mmoja (angalia Mada Maalum: Ibada kwa Mungu mmoja).Mataifa yote yanayozunguka yalikuwa ni waabudu miungu wengi. Kuwepo kwa Mungu mmoja ni moyo wa ufunuo wa Agano la Kale (kama vile Kumb. 6:4). Uumbaji ni jukwaa kwa kusudi la ushirika kati ya Mungu na mwanadamu, waliofanywa kwa sura yake na mfano (kama vile Mwanzo1:26-27). Hatahivyo, mwanadamu aliasi, akitenda dhambi dhidi ya upendo wa Mungu, uongozi na kusudi (kama vile Mwanzo 3). Upendo wa Mungu na kusudi lilikuwa kubwa na lenye nguvu sasa na hakika alihaidi kukomboa mwanadamu aliyeanguka (kama vile Mwanzo 3:15)!

Mvutano unainuka pale ambapo Mungu anachagua kumtumia mwanadamu mmoja, familia moja, taifa moja kufikia wanadamu waliobakia. Wateule wa Mungu wa Ibrahimu na Wayahudi kama ukuhani wa kikuhani (kama vile Kutoka 19:4-6) kulisababisha kiburi badala ya huduma, kutengwa badala ya kujumuishwa. Wito wa Mungu kwa Ibrahimu ulijumuishwa Baraka za kimakusudi kwa wanadamu wote (kama vile Mwanzo 12:3). Lazima ikumbukwe na kusisitizwa kwamba uchaguzi wa Agano la Kale ulikuwa kwa ajili ya huduma, sio wokovu. Israeli yote haijawahi kuwa sawa na Mungu, haijawahi kukombolewa kimilele kwa msingi tu wa haki yake (kama vile Yohana 8:31-59; Mt. 3:9), lakini kwa imani binafsi na utii (kama vile Mwanzo 15:6, ikinukuliwa kutoka Warumi 4). Israeli ilipoteza lengo lake (kanisa sasa ni ufalme wa kikuhani, kama vile 1:6; II Pet.2:5,9), twakibadilisha majukumu kuwa upendeleo, huduma kuwa msimamo maalum! Mungu anachagua mmoja ili achague wote.

**MVUTANO WA TATU** (maagano yenye masharti dhidi ya maagano yasiyo na masharti)

Kuna mvutano wa kithiolojia au fumbo kati ya maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti. Ni hakika kweli kwamba kusudi/mpango wa Mungu na ukombozi sio wa kimasharti (kama vile Mwanzo 15:12-21). Hatahivyo, mwitikio wa kimajukumu wa kibiadamu siku zote huwa ni wa kimasharti!

Ile "ikiwa. . .basi" ya utaratibu huu unatokea kote katika Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu ni mwaminifu; mwanadamu si mwaminifu. Mvutano huu umesababisha mkanganyiko mkubwa. Wafasiri wamejifanya kuweka shabaha juu ya moja tu "pembe ya mkanganyiko," Uaminifu wa Mungu au juhudi za mwanadamu, utawala wa Mungu au utashi huru wa mwanadamu. Vyote ni vya kibiblia na ni vya muhimu (Angalia Mada Maalumaaaa;Uchaguzi/Kuamriwa kabla na Hitaji la uwiano wa Kithiolojia)

Hii inahusiana na matukio ya siku za mwisho, kwa ahadi za Mungu za Agano la Kale kwa Israeli; Hadhi yake inajumuishwa (kama vile Ezek. 36:22-38). Maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti yanakutana katika Kristo (kama vile Isa. 53), sio Israeli! Kilele cha uaminifu wa Mungu kinategemea ukombozi wa wote watakaotubu na kuamini, sio nani alikuwa baba yako/mama yako, sio Israeli, ni msingi wa maagano yote ya Mungu na ahadi. Ikiwa kuna maelezo ya kithiolojia katika Biblia, sio kanisa bali Israeli (kama vile Mdo. 7 na Gal. 3).

Kusudio la ulimwengu la kutangaza injili limepita kwa kanisa (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Bado ni agano la kimasharti! Hii sio kumaanisha kwamba Mungu amekataa kabisa Wayahudi (kama vile Rum. 9-11). Kuna weza kuwa kuna mahali na kusudi la siku za mwisho, kuamini Israeli (kama vile Zek 12:10).

**MVUTANO WA NNE** (nadharia ya kifasihi ya Mashariki ya Karibu dhidi ya nadharia za kimagharibi).

Aina za fasihi ni kipengele muhimu katika usahihi wa kufasiri Biblia. Kanisa limeendelea katika mazingira ya kidesturi ya kimagharibi (kiyunani). Fasihi ya mashariki zaidi ni ya kimafumbo, ya kisitiari na kiishara kuliko kuwa ya kisasa,nadharia za desturi za kifasihi za kimagharibi (angalia Mada Maalum: Fasihi ya Mashariki (ukinzani wa kibiblia)). Imejikita kwa watu, matukio na mazingira kuliko kweli ziazopendekezwa. Wakristo wamekuwa na hatia ya kutumia historia na nadharia za kifasihi kufasiri nabii za Kibiblia (zote Agano la Kale na Agano Jipya). Kila kizazi na jambo la kijiografia limetumia desturi yake, historia na ubayana wake kufasiri Ufunuo. Kila mmoja wao amekuwa na makosa! Ni kiburi kufikiria kwamba desturi za kisasa za kimagharibi ni shabaha ya unabii wa kibiblia!

Aina ya fasihi ambayo kutoka kwake mwandishi wa asili na aliyevuviwa anachagua kuandika ni mkataba wa kifasihi na mwandishi. Kitabu cha Ufunuo sio masimulizi ya kihistoria. Ni muunganiko wa barua (sura za 1-3), unabii na zaidi fasihi ya nyakati za mwisho. Ni mbaya kuifanya Biblia kusema zaidi ya kilichokusudiwa na mwandishi wa asili kama ilivyo kuifanya iseme kidogo kuliko ilivyokusudiwa! Kiburi cha wafasiri na mafundisho hata zaidi isivyokuwa sawa katika kitabu kama ufunuo.

Kanisa halijawahi kukubaliana katika fasiri sahihi ya ufunuo. Shida yangu ni kusikia na kushughulikia Biblia nzima, sio baadhi ya sehemu zilizochaguliwa. Mtazamo wa mashariki wa Biblia inawasilisha ukweli katika jozi zilizojaa mvutano. Mwenendo wetu wa magharibi kuelekea ukweli unaopendekezwa usiokatalika lakini usio na uwiano! Nafikiri inawezekana kuondoa angalau baadhi ya vizuizi katika kufasiri Ufunuo kwa kutambua makusudi yake yanayobadilika kuelekea vizazi vinavyofuata vya waaminio. Ni dhahiri kwa wafasiri wengi kwamba Ufunuo lazima ufasiriwe katika ufahamu wa siku zake wenyewe na aina yake ya fasiri. Mkabiliano wa kihistoria kwa Ufunuo lazima ushughulikiwe na wasomaji wa kwanza wangefanya na wangeelewa. Kwa namna nyingi wafasiri wa kisasa wamepoteza maana za viwakilishi vya kitabu. Msukumo mkubwa wa kwanza wa Ufunuo. Ulikuwa ni kutia moyo waamini watesekao. Ilionesha namna Mungu anavyoshughulikia historia (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale); Ilikiri kwamba historia inaenda kuelekea mwisho wa uteuzi, hukumu au baraka (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale). Ilikiri katika muktadha wa upendo wa Mungu, uwepo, nguvu na utawala wa siku za mwisho wa kiyahudi wa karne ya kwanza!

Inafanya kazi katika njia hizihizi za kithiolojia kwa kila kizazi cha waaminio. Inachukua mahangaiko ya kiulimwengu ya jumla ya mazuri na mabaya. Maelezo ya karne ya kwanza yanaweza yakawa yamepotea kwetu lakini yasiyo na nguvu wala ukweli wa kufariji. Wakati wafasiri wanajaribu kulazimisha maelezo ya ufunuo kwenye historia ya sasa, utaratibu wa fasiri za uongo!

Inawezekana kwamba maelezo ya kitabu yanaweza kufanyika fasihi isiyo ya kawaida tena (kama ilivyokuwa katika Agano la Kale kuhusiana na kuzaliwa, kuishi na kufa kwa Kristo) kwa kizazi cha mwisho cha Waaminio kama walivyokabiliana na kuchinjwa na kiongozi mpinga-Mungu (kama vile II The.2) na desturi. Hakuna mtu anayeweza kujua kutimilizwa huku kwa kibayana kwa Ufunuo mpaka maneno ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko13; na Luka 21) na Paulo (kama vile I Kor. 15; I The. 4-5; na II The. 2) pia inafanyika dhahiri kihistoria. Kudhania, kufikiria na mafundisho vyote hivi sio sahihi. Fasihi ya matukio ya siku za mwisho yanaruhusu mabadiliko. Mshukuru Mungu kwa taswira na viwakilishi ambavyo vinapita masimulizi ya kihistoria! Mungu anawawala na kushughulikia mabo yake; Anatawala; Anakuja!

Fasiri nyingi za kisasa zinakosa suala la uchaguzi wa aina ya fasihi ya uwasilishaji! Wafasiri wa kisasa wa Magharibi mara kwa mara wanatafuta mfumo sahihi uliowazi wenye mantiki wa kithiolojia kuliko kuchukuliana na aina ya fasihi yenye utata, wakilishi ya kitamthilia ya matukio ya siku za mwisho. Kweli hii inaelezewa vizuri na Ralph P. Martin katika makala yake,"Approaches to New Testament Exegesis," katika kitabu *New Testament Interpretation*, kilichohaririwa na I. Howard Marshall:

"Mpaka tutakapotambua ubora wa kitamthilia wa maandiko haya na kukumbuka njia ambayo lugha inatumika kama chombo cha kuelezea ukweli wa kidini, tutakuwa tumefanya kosa kubwa sana katika uelewa wetu wa matukio ya siku za mwisho na kimakosa kujaribu kufasiri maono yake kana kwamba ni kitabu cha riwaya ya kawaida na kinachojihusisha kuelezea matukio ya kihalisia na historia inayoandikika. Kujaribu njia ya pili ni kukimbia katika kila mtindo wa matatizo ya fasiri. Zaidi sana inapelekea kwenye uharibifu wa maana ya msingi katika lugha za hadithi za kufikirika za Mungu mtawala katika Kristo na fumbo la utawala wake ambao unaunganisha uweza na upendo (kama vile 5:5,6; Simba ndiye mwana kondoo)" (ukurasa wa 235).

W. Randolph Tate katika kitabu chake *Biblical Interpretations* alisema:
"Hakuna fasihi ingine ya Biblia ambayo imesomwa kwa dhati na shauku kubwa na kwa matokeo yenye kukatisha tama kama vitabu vya matukio ya siku za mwisho. Aina hii ya fasihi ilipata shida kutokana na historia ya kimajanga ya kufasiriwa vibaya kwasababu ya kukosekana kwa uelewa wa msingi wa muundo wake wa fasihi, mpangilio na kusudi. Kwasababu ya madai yake sana ya kufunua kile ambacho karibia kinatokea, vitabu vya mwisho wa ulimwengi vimekuwa vinatazamwa kama mwongozo kuelekea katika kuyajua jua mambo yajayo. Kosa kubwa zaidi katika mtazamo huu ni dhana kwamba muuundo wa vitabu vya rejea ni umri wa msomaji wa sasa kuliko kuwa wa mwandishi. Huu mkabiliano usio kuwa na mwongozo wa matukukio ya siku za mwisho (hasa Ufunuo) unaifanya kazi kama vile ni namba za siri ambazo matukio ya kisasa yanaweza kutumika kutafsiria viwakilishi vya andiko. . .Kwanza, mfasiri lazima atambue kwamba vitabu vya siku za mwisho vinazungumzia jumbe zake kupitia uwakilishi wa kiishara. Kufasiri ishara kibayana wakati inapokuwa kisitiari ni kupotosha fasiri. Tatizo sio kama matukio katika za mwisho ni ni ya kihistoria. Matukio yanaweza yakawa sio ya kihistoria; yanaweza kuwa kweli yalitokea, au yatatokea lakini mwandishi anayawasilisha na kuzungumza maana zake kupitia taswira na nadharia" (ukurasa wa 137).
Kutoka katika *Dictionary of Biblical Imagery*, iliyohaririwa na Ryken, Wilhost na Longman III:
"Wasomaji wa leo mara kwa mara wanashangazwa na kuchanganywa na aina hii ya fasihi. Taswira isiyotegemewa na ya nje ya uzoefu wa ulimwengu huu. Kuichukilia Fasihi hii kwa inavyoonekana inawaacha wasomaji wengi wakikwaruza kwaruza wakiwa wamejizatiti 'nini kitatokea wakati,' hivyo kukosa kusudio la ujumbe wa maandiko ya siku za mwisho" (ukurasa wa 35).

**MVUTANO WA TANO** (ufalme wa mungu uliopo sasa lakini wa baadaye)

Ufalme wa Mungu ni wa sasa na ni wa baadaye. Hili fumbo la kithiolojia linafanyika shabaha katika hatua ya matukio ya siku ya mwisho. Ikiwa mtu atategemea kutimilizwa kwa kibayana kwa nabii zote za Agano la Kale kwa Israeli hivyo ufalme wa Mungu zaidi unafanyika urejesho wa Israeli kwenye eneo lao la kijiografia na utawala wa kabla wa kithiolojia! Hii ingepelekea kwamba Kanisa kwa siri linanyakuliwa katika sura ya 5 na sura zilizosalia zinahusiana na Israeli (lakini angalia dokezo katika Ufunuo 22:16).
Hatahivyo ikiwa shabaha ipo katika ufalme kuanzishwa na Masihi anayetabiriwa katika Agano la Kale, alafu lipo na kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo na alafu inaweka shabaha kwenye kufanyika mwili, maisha, mafundisho, kifo na kufufuka kwa Kristo. Msisitizo wa kithiolojia upo katika wokovu wa sasa.
Ufalme umekuja, Agano la Kale limetimilizwa katika kujitoa kwa wokovu kwa Kristo kwa wote na sio utawala wake wa Milenia na baadhi! Ni kwa kweli na hakika kwamba Biblia inazungumza juu ya ujio wote wa Kristo, lakini wapi ambapo msisitizo unawekwa? Inaonekana kwangu kwamba nabii nyingi za Agano la Kale zinalenga juu ya ujio wa kwanza, uanzishwaji wa ufalme wa Kimasihi (kama vile Danieli 2). Katika namna nyingi huu utawala wa Mungu unafananishwa na utawala wa milele wa Mungu (kama vile Danieli 7). Katika Agano la Kale shabaha ipo katika utawala wa Mungu wa milele, japo namna ya udhihirisho wa utawala huo ni huduma ya Masihi (kama vile I Kor. 15:26-27). Sio swali la nini ni kweli; vyote ni kweli lakini msisitizo upo wapi? Lazima isemwe kwamba baadhi ya wafasiri wanafanya kulenga kwenye utawala wa milenia wa Masihi (kama vile Ufunuo 20) kwamba wamekosa shabaha ya kibiblia juu ya utawala wa milele wa baba. Utawala wa Kristo ni tukio la kuanzia kama kiashiria. Kama kuja kwa mara mbili huku kwa Kristo hakukuwa dhahiri katika Agano la Kale, wala haitakuwa pia kutawala kwa muda kwa Masihi!
Msingi wa mahubiri na mafundisho ya Yesu ni ufalme wa Mungu. Ni vyote sasa (katika wokovu na huduma), na baadaye (katika utawala mkuu wa ulimwengu na nguvu). Ufunuo, ikiwa utalenga kwenye utawala wa kimasihi wa kimelenia (kama vile Ufunuo 20), itakuwa mwanzo tu na sio kilele (kama vile Ufunuo 21-22). Sio dhahiri kutoka katika Agano la Kale kwamba utawala wa muda ni mughimu; ukweli ni kwamba utawala wa Kimasihi wa Danieli 7, ni wa milele na wala sio wa ki-milenia.

**MVUTANO WA SITA** (kurudi kwa hakika kwa Kristo dhidi ya kuchelewa *Parousia*)

Waamini wengi wamefundishwa kwamba Yesu anakuja hivi karibuni, ghafla na bila taarifa (kama vile Mt.

10:23; 24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30; Ufunuo 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; angalia Mada Maalum:Kurudi Punde). Lakini katika kila kizazi kitarajiacho cha waamini hata hivyo kimekosea! Ukaribu (uharaka) wa kurudi kwa Yesu ni tumaini lenye nguvu lililohaidiwa kwa kila kizazi, lakini ukweli kwa mmoja tu (na yule aliyeteseka na huyo tu). Waaminio lazima waishi kama vile anarudi kesho, lakini apange na kufanyia kazi Agizo Kuu (kama vile Mt. 28:19-20) ikiwa atakawia.

Baadhi ya vifungu katika Injili na I na II Wathesalonike wamejikita katika kukawia katika Kuja kwa Mara ya Pili (*Parousia*). Kuna baadhi ya matukio ya kihistoria ambayo lazima yatokee kwanza:

1. kuhubiriwa kwa injili ulimwenguni kote (kama vile Mt. 24:14; Marko 13:10)
2. ufunuo "mwanadamu mdhambi" (kama vile Mt. 24:15; II The. 2; Ufunuo 13)
3. mateso makuu (kama vile Mt. 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata wa kimakusudi (kama vile Mt. 24:42-51; Marko 13:32-36)! Ishi kila siku kama vile ni siku yako ya mwisho lakini panga na jifunze kwa ajili ya huduma yako ya baadaye!

**MWENDELEZO NA UWIANO**

Lazima isemwe kwamba shule tofauti tofauti za fasiri za siku za mwisho zote zinajumuisha ukweli nusu. Wanaelezea na kufasiri vizuri baadhi ya maandiko. Tatizo linatokana na mwendelezo na uwiano. Mara kwa mara kuna mpangilio wa kauli za kupendekeza ambazo zinatumia maandiko ya kibiblia kujaza mafuvu yaliyowekwa kabla ya kithiolojia. Biblia haifunui mantiki, mtitiriko wa matukio na mfumo wa siku za mwisho. Iko kama albamu ya familia. Picha ni za kweli lakini siku zote hazipo katika mpangilio, katika muktadha katika mfuatano wa kimantiki. Baadhi ya picha zimeanguka kutoka kwenye albamu na vizazi vya baadaye vya ndugu wa familia hawajui hakika namna ya kuzirudisha. Msingi wa fasiri sahihi wa Ufunuo ni kusudio la mwandishi wa asili kama inavyofunuliwa katika uchaguzi wake wa ina ya fasihi anayoitumia. Wafasiri wengi wanajaribu kubeba vifaa vyao vya kutendea kazi na taratibu kutoka katika aina zingine za fasihi za Agano Jipya kwenda kwenye fasiri zao za Ufunuo. Wanaweka shabaha kwenye Agano la Kale badala ya kuruhusu mafundisho ya Yesu na Paulo kupangilia muundo wa kithiolojia na kuruhusu Ufunuo kufanya kazi kama kielelezo.

Lazima nikiri kwamba naikabili fasiri hii juu ya Ufunuo nikiwa na baadhi ya uoga na wasiwasi si kwasababu ya laana ya Ufunuo 22:18-19, lakini ni kwasababu ya kiwango cha mkanganyiko ulioletwa na ufasiri wa kitabu hiki na kuendelea kusababisha kati ya watu wa Mungu. Napenda Ufunuo wa Mungu. Ni kweli wakati wanadamu wote wanakuwa waongo (kama vile Rum. 3:4)! Tafadhali tumia fasiri hii kama jaribio la kuamsha mawazo na sio kutoa maana ya mwisho kama kielekezi na sio mwongozo, kama "vipi ikiwa," na sio "hivyo Bwana asema." Nimekuja kugundua usio kwa uso mapungufu yangu mwenyewe, ubaguzi na ajenda ya kithiolojia. Lakini pia nimeona yale ya wafasiri wengine. Inakaribia kuonekana kwamba watu wanatafta Ufunuo kile wanachotegemea kukipata. Aina ya fasihi inajipelekea yenyewe katika matumizi mabaya!

Hata hivyo ipo katika Biblia kwa makusudi. Imewekwa katika kama hitimisho "neno" sio kwa ajali au bahati mbaya. Ina ujumbe kutoka kwa Mungu kwa watoto wake wa kila kizazi. Mungu anataka tuelewe! Tumuunge mkono, sio kutengeneza magenge; Ebu tukiri kile kilicho wazi na kilicho cha msingi na kikuu, sio yote yanaweza, yataweza au yangeweza kuwa kweli. Mungu atusaidie sisi sote!

◙**"habari njema"** Hiki ni KITENZI cha neno בשׂר (BDB 142, *Piel* HALI YA KUENDELEA) chenye kumaanisha "kutoa habari zenye kufurahisha." Hapa linaonyesha ujumbe wa huruma wa ukombozi na ukubalifu wa YHWH (kama vile 40:9 [mara mbili]; 41:27; 52:7 [mara mbili]; Nahum 1:15). Paulo anafanya rejeo la Isa. 52:7 katika Rum. 10:15 na kuyahusianisha kwa Kristo (Rum. 10:16 inafanya rejeo kwa Isa. 53:1). Injili ya Yesu Kristo inaainishwa kama "habari njema" katika Agano la Kale.

◙**"usihofu"** KITENZI hiki (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI SHURUTISHI) ni AMRISHI katika kuleta maana, kikirejerea Yerusalemu (yaani., watu wa Mungu). Dhambi huleta hofu! Ni mara ngapi Mungu analisema hili kwa watu wake! (kama vile 41:10,13.14; 43:1,5; 44:2,8 [maneno tofauti]; 51:7,12; 54:4,14).

◙**"Iambieni miji ya Yuda"** Wale wangojeao baaadaye, waandishi wa kipindi kile baada ya Waisraeli kutoka Misri badala ya Isaya wamepata shida kulielezea rejeo hili kwa sababu miji yote iliangamizwa na Nebukadneza II mnamo mwaka wa 586 K.K.

◙**"Tazameni Mungu wenu"** Mungu angali na watu wake! Usubilishaji umefikia kikomo (kama vile 25:9; 26:8; 33:2; 40:31; 49:23; 51:5; 60:9)!

**40:10 "Bwana Mungu"** Kwa maana iliyo wazi hili neno ni "*Adonai* YHWH," ambalo kiuhalisia linatafasiliwa "Bwana, BWANA" kama vile Zab. 110:1). "Bwana" ni neno la Kiebrania *adon*, lenye kumaanisha bwana, mmiliki, mme, bwana.

◙**"Na mkono wake ndio utakaomtawalia"** Hii ni lahaja ya lugha ya Kisemiti ya namna ya kumwelezea Mungu (angalia Mada Maalum katika 41:2) kwa tendo na nguvu za Kiungu. Kutoka Isa. 9:6-7; 11:1-5; na Mika 5:2-5a, tunafahamu hili linarejerea kwenye suala la Masihi (kama vile Zaburi 110).

## MADA MAALUM: MASIHI

Ugumu katika kutafasiri neno hili ni kwa sababu ya matumizi tofauti kuhusiana na neno lenyewe "Masihi" au "aliyetiwa mafuta" (BDB 603, KB 645). Neno lilitumika katika kumwekea mtu mafuta maalumu kuonyesha wito wa Mungu na kumkabidhi majukumu ya uongozi.

1. Lilitumika kwa wafalme wa Kiyahudi (mf. 1 Sam. 2:10; 12:3; 24:6, 10;2 Sam. 19:21; 23;1; Zab. 89:51; 132:10, 17; Wim. 4:20; Hab. 3:13; "Malkia mtiwa mafuta" katika Dan. 9:25)
2. Lilitumika kwa makuhani wa Kiyahudi (yaani, "makuhani walitiwa mafuta," Kut. 29:7; mf. Law. 4:3, 5, 16; 6:15; 7:36; 8:12; bila shaka Zab. 84:9-10; na 133:2)
3. Lilitumika kwa makasisi, na Manabii (kama vile. Mwa. 26:7; 1 Nya. 16:22; Zab. 105:15, iliyomaanisha watu wa Agano kwa pamoja; yumkini Hab. 3:13)
4. Lilitumika kwa manabii (kama vile. 1 Fal. 19:16; yumkini 1 Nya. 29:22)
5. Lilitumika juu ya Koreshi (kama vile. Isa. 45 :1)
6. # 1 na # 2 umeunganishwa katika Zab. 110 na Zekaria 4.
7. Lilitumika kwa ujio maalumu wa Mungu, Ufalme wa Daudi kuleta enzi mpya ya haki
   a. uzao wa Yuda (kama vile. Gen. 49:10)
   b. nyumba ya Yesse (kama vile.2 Sam 7)
   c. utawala wa ulimwengu (kama vile. Zaburi 2; Isa. 9:6; 11:1-5; Mik. 5:1- 4 na kuendelea)
   d. Huduma kwa wahitaji (kama vile Isa. 61:1-3)

Mimi binafsi nimevutiwa na utambulisho wa neno "aliyetiwa mafuta" na Yesu wa Nazareti (kama vile.Yn. 1:41; 4:25) kwa sababu

1. kutambulishwa kwa ufalme wa milele katika Danieli 2 kipindi cha utawala wa nne
2. kutambulishwa kwa "mwana Adamu" katika Dan. 7:13 akipewa ufalme wa milele
3. maneno ya ukombozi wa Dan. 9:24, ambayo yanaashiria mwisho wa historia ya ulimwengu ulioanguka
4. matumizi ya Yesu ya kitabu cha Danieli katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14)

Lazima kukiri kuwa hii ni mada nadra katika Agano la Kale, bila shaka Dan. 9:25. Lazima pia ifahamike kuwa Yesu haingii sana katika maelezo ya jumla kuhusu Masihi katika Agano la Kale

1. hakuwa kiongozi katika Israeli
2. hakutiwa mafuta rasmi na kuhani
3. sio kama mwokozi wa Israeli
4. sio tu "mwana wa Adamu" lakini kwa mshangao "Mwana wa Mungu"

◙**"thawabu yake i pamoja naye,**
**na ijara yake i mbele zake"** Hiki kifungu kilicho kamili pia kinapatikana katika Isa. 62:11 na kikadokezwa katika Ufu. 22:12.

Aya ya 10 inazungumza juu ya uwepo binafsi wa Kiungu (41:10a). Immanueli amekwisha kuja (kama vile 7:14)!

**40:11 "kama Mchungaji"** YHWH, mwenye uweza (kama vile mst. 10), pia ni Mchungaji (kama vile Zaburi 23; 80:1; Yer.31:10; Ezek. 34:11-16). Tambua kuwa pia katika Ezek. 34:23, YHWH amemuweka Masihi wake kumwakilisha Yeye! Yesu ni "Mchungaji mzuri" (kama vile Yohana 10). Ni Mchungaji "aliyejeruhiwa" wa Zakaria 11-12 na Isa. 52:13-53:12.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40: 12-17**
**12 Ni nani aliyeyapima maji kwa konzi ya mkono wake,**
**na kuzikadiri mbingu kwa shubiri,**
**na kuyashika mavumbi ya dunia katika pishi,**
**na kuipima milima kwa uzani,**
**na vilima kama kwa mizani?**
**13 Ni nani aliyemwongoza roho ya Bwana,**
**na kumfundisha kwa kuwa mshauri wake?**
**14 Alifanya shauri na nani,**
**ni nani aliyemwelimisha na kumfunza njia ya hukumu,**
**na kumfunza maarifa, na kumwonyesha njia ya fahamu?**
**15 Tazama, mataifa ni kama tone la maji katika ndoo,**
**huhesabiwa kuwa kama mavumbi membamba katika mizani;**
**tazama, yeye huvinyanyua visiwa kama ni kitu kidogo sana.**
**16 Lebanoni nayo hautoshi kwa kuni,**
**wala wanyama wake hawatoshi kwa kafara.**
**17 Mataifa yote huwa kama si kitu mbele zake;**
**huhesabiwa kwake kuwa duni ya si kitu, na ubatili.**

**40:12-17** Kama aya za 9-11 zinavyoueleza ujumbe wa YHWH kuhusu uwepo binafsi kama mwokozi, aya za 12-17 zinamwelezea Yeye kama Muumbaji.

1. Aliyeyapima maji (yaani., mdhibiti na msimamizi wa machafuko ya maji ya asili), mst. 12
2. Aliyesanifisha mbingu ya hii dunia, mst. 12
3. Akaiamuru nchi kavu ("huyakadiria mavumbi" na "kuipima milima. . .na vilima" [nadharia ya ufanano wa Kiebrania]"), mst. 12
4. Akamwongoza Roho kama mshauri, pasipo baraza, mistari ya 13-14
5. Katika kuilinganisha akili na uwezo wa ubunifu wa Mungu, mwanadamu si kitu chochote (kama vile mistari ya 6-8, hili linafanana na lile la 38-41), mistari ya 15-17

**40:12 "aliyeyapima maji"** VITENZI vyote vilivyoko mstari wa 12 ni KAULI TIMILIFU (yaani., kitendo kilichokwisha kutimia). Huu ni mlolongo wa maswali yanayotarajia jibu la "hapana."vinafanana na kitabu cha Ayubu 38-41, ambapo Mungu alilijibu swali la Ayubu kwa kutetea Enzi yake na mamlaka. Aya ya 12 inafanana na ile ya 41:26. Tambua uwepo wa ufanano kwenye.

1. aliyeyapima – BDB 551, KB 547]
2. kuzikadiria – BDB 1067, KB 1733
3. kuyashika– BDB 465, KB 463
4. kuipima – BDB 1053, KB 1642

Haya ni matendo ya kiistiari ya Muumba. Habari za uumbaji za Mwanzo 1 pia ni taswira ya udhibiti wa Mungu wa kuutunza ulimwengu. Kitabu kipya kizuri ni cha John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*.

**40:13-14** "yeye" azungumuziwaye katika aya hizi aweza kuhusianishwa huko nyuma kwenye WINGI wa mistari ya 1-3. Kama ndivyo ilivyo, inahusiana na baraza la mbinguni. Hawa watumishi wa kimalaika waweza kuonekana katika

1. Aya zenye neno "Sisi" katika Mwanzo 1 na 6

2. I Fal. 22:19-23
3. Ayu. 1:6-12; 2:1-6,7
4. Danieli 7:10,26

**40:13 "Nani aliye,mwongoza Roho wa Bwana"** Mistari ya 13 na 14 zinafanana. Hii sio aya ya ki-Utatu bali ni aya ya Agano la Kale, zaidi kama Mwanzo 1:2, ambayo inazungumzia juu ya "Roho" kama uwepo wa Mungu (angalia Mada Maalum katika mst. 7).

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

A. Injili
  1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
  2. Yohana 14:26

B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39

C. Paulo
  1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
  2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
  3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
  4. Gal. 4:4-6
  5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
  6. 1 The. 1:2-5
  7. 2 The. 2:13
  8. Tit. 3:4-6

D. Petro – 1 Pet. 1:2

E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
  1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
  2. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7

A. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
  1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
  2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
  3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  4. Zakaria 3:1-2

B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14

C. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12

D. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10

E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na

baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)

2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho

**40:14 "nani aliyemwelisha na kumfunza njia ya haki"** Tambua nadharia ya ufanano. "njia" ni mazingira ya nyuma ya Agano la Kale kuelekea dhana ya agano Jipya ya neno "mapito," ambalo lilitumiwa na kanisa la mwanzo katika matendo. Hili linaongelea juu ya imani ya kibiblia kama stadi ya maisha ya kuwa na ushirika na Mungu. kwa ajili ya neno"haki" angalia Mada Maalum hapa chini. Aya hii kwa asili inatetea imani ya Mungu mmoja.

## MADA MAALUM: HAKIMU, HUKUMU, NA HAKI (שפט) KATIKA ISAYA

Hili ni neno lililotumika kwa upana sana (BDB 1047, KB 1622) katika Agano la Kale. Toleo la NIDOTTE, juzuu ya 4, uk. 214, limeainisha mgawanyo wake na umuhimu wake.
Torati, 13%, waamuzi wa kibinadamu
Vitabu vya kihistoria, 34%, viongozi wa kibinadamu
Vitabu vya hekima, 22%, kazi za kiungu
manabii, 31%, hasa kazi za kiungu
kumbuka jedwali lifuatalo kutoka kitabu cha Isaya:

| YHWH kama mwamuzi | Masihi kama mwamuzi | Waamuzi bora wa Israeli | Wamuzi bora wa Kiisraeli |
|---|---|---|---|
| 2:4 | 9:7 | 1:17 | 1:23 |
| 3:14 | 11:3, 4 | 26:8 | 3:2 |
| 4:4 | 16:5 | 56:1 | 5:7 |
| 5:16 | 32:1 | 58:2, 8 | 10:2 |
| 28:6, 17, 26 | 40:14 | | 59:4, 9, 11, 14, 15 |
| 30:18 | 42:1, 3, 4 | | |
| 33:5, 22 | 51:4, 5 | | |
| 61:8 | 53:8 | | |
| 66:16 | | | |

Israeli ilipaswa kuaksi tabia ya YHWH kwa mataifa. Ilishindwa, kwa hiyo YHWH akainua Mwisraeli mmoja "bora" kutimiliza ufunuo binafsi ulimwenguni (yaani., Masihi, Yesu wa Nazareti, Kristo Yesu, kama vile Isa. 52:11-53:12)!

◙ Aya hii ni kiini cha kutetea imani ya Mungu mmoja. Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: IMANI YA MUNGU MMOJA

Mwanadamu amehisi kuwa kuna ukweli zaidi kuliko ule wa kimaumbile (yaani, yanayoathiriwa na mambo yaliyo nje ya uwezo, kama vimbunga, mfumo wa kupatwa kwa jua au mwezi, kimondo, hali ya hewa,matukio, vifo, n.k.). Wataalamu wa Elimu ya Mwanadamu wanatwambia kuwa walivikuta vitu ndani ya makaburi ya kale ya hominoids ambavyo vilikuwa kwa ajili ya maisha ya baadaye, ambavyo vilionekana kama nyongeza ya maisha haya. Utamaduni wa kwanza ulioandikwa ulikuwa Sumer (Tigri ya kusini, Mto wa Eufrate), ulianza mnamo 10,000 - 8,000 K.K. Hawa waliandika mashairi kuyaeleza maoni yao ya miungu na ushirika wao. Kisha, zaidi ya hayo kama wanadamu na udhaifu wao. Mila zao zilianza kuwepo katika mtindo wa masimulizi marefu kabla ya wao kuandika.

Kulikuwa na kukua kwa theolojia kutokana na

1. imani juu ya vitu vyote ni hai
2. miungu wengi wa
3. mungu mkuu (au wa uwili)

Dhana ya "Mungu mmoja" (aliye mmoja na nafsi ya kwanza, Mungu wa maadili asiye na mahusiano ya mke), si "mungu mkuu" miungu wengi au mungu mzuri wa uwili w ki-Irani (Wafuasi wa Zoroaster, ni wa pekee kwa Israeli (Abrahamu na Ayubu, 2000 K K.). Ni mmoja pekee huko Misri (Amenhotep IV, pia anajulikana kama Akhenaten, 1367-1350 au 1386-1361 K.K. AMBAYE ALIABUDU Atemi, mungu jua, kama mungu pekee). Tazama J. Assmann, *The Mind of Egypt*, kr. 216-217.

Dhana hii inaelezwa katika vifungu kadhaa ndani ya Agano la Kale.

1. "hakuna aliye kama HWH Elohim,wetu" Kut. 8:10; 9:14; Kumb. 33:26; 1 Fal. 8:23
2. "hapana mwingine zaidi Yake," Kumb. 4:35,39; 32:39; 1 Sam. 2:2; 2 Sam. 22:32; Isa. 45:21; 44:6,8; 45:6,21
3. "YHWH ni mmoja" Kumb. 6:4; Rum. 3:30; 1 Kor. 8:4,6; 1 Tim. 2:5; Yakobo 2:19
4. "hakuna aliye kama Wewe," 2 Sam. 7:22; Yer. 10:6
5. "Wewe ni Mungu wa pekee," Zab. 86:10; Isa. 37:16
6. "kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwepo mwingine," Isa. 43:10
7. "hapana mwingine; zaidi ya mimi. . .hapana mwingine," Isa. 45:5,6,22
8. " Yeye ni chanzo cha vitu vyote," Isa. 45:7 (kama vile. Amosi 3:6)
9. "hapana mwingine, hapana Mungu tena," Isa. 45:14,18
10. "hapana mwingine zaidi ya mimi," Isa. 45:21
11. "hapana mwingine;. . .hakuna aliye kama mimi," Isa. 46:9

Lazima ikubalike kwamba haya mafundisho ya muhimu yamefunuliwa katika njia endelevu. Semi za kale zingeweza kueleweka kama "mungu mmoja" au Mungu mmoja wa matendo (kuna miungu wengine, yaani, Yoshua. 24:15; 1 Fal. 18:21), lakini Mungu mmoja kwetu (kama vile Kut. 15:11; 20:2-5; Kumb. 5:7; 6:4,14; 10:17; 32:12; 1 Fal. 8:23; Zab. 83:18; 86:8; 136:1-9).

Maandiko ya kwanza ambayo yalianza kudokeza juu ya umoja (Mungu mmoja wa kifalsafa) ni ya kale (kama vile Kut. 8:10; 9:14; 20:2-3; Kumb. 4:35,39; 33:26). Madai kamili na yenye mashindano yanapatikana katika Isaya 43-46 (kama vile 43:10-11; 44:6,8; 45:7,14,18,22; 46:5,9).

Kitabu cha Agano la Kale kinaishusha thamani ya miungu ya mataifa kama

1. uumbaji wa mwanadamu – Kumb. 4:28; 2 Fal. 19:18; Zab. 115:4-8; 135:15-18; Isa. 2:8; 17:8; 37:19; 40:19; 41:7,24,29; 44:10,12; 46:6-7; Jer. 10:3-5; Ufu. 9:10
2. pepo wabaya– Kumb. 32:17; Zab. 106:37; Isa. 8:19; 19:3c; 1 Kor. 10:20; Ufu. 9:20
3. majivuno, tupu – Kumb. 32:21; 2 Fal. 17:15; Zab. 31:6; Isa. 2:18; 41:29; Yer. 2:5; 10:8; 14:22; Yer. 2:5; 8:19
4. kisicho mungu – Kumb. 32:21; 2 Nya. 13:9; Isa. 37:19; Yer. 2:11; 5:7; 1 Kor. 8:4-5; 10:20; Ufu. 9:20

Kitabu cha Agano Jipya kinadokeza juu ya Kut. 6:4 katika Rum. 3:30; 1 Kor. 8:4,6; Efe. 4:6; 1 Tim. 2:5; na Yakobo 2:19. Yesu analinukuu hili kama amri ya katika Mt. 22:36-37; Marko 12:29-30; Luka 10:27. Kitabu cha Agano la Kale, pamoja na Agano Jipya, kinadai kwamba ukweli wa viumbe vingine vya kiroho (pepp wabaya, malaika), lakini muumbaji mmoja wa pekee/ Mungu mwokozi (YHWH, Mwa. 1:1).

Mungu mmoja wa Kibiblia anabainishwa na

1. Mungu ni mmoja na wa pekee (asili ya uhai wake ni dhahania, haidhihirishwi)

2. Mungu ni nafsi (kama vile Mwa. 1:26-27; 3:8)
3. Mungu ni wa maadili (kama vile Kut. 34:6; Neh. 9:17; Zab. 103:8-10)

Mungu aliwaumba wanadamu kwa sura na mfano wake (Mwa. 1:26-27) kwa ushirika (yaani., #2). Yeye ni Mungu mwenye wivu (kama vile Kut. 20:5-6)

Kutoka kitabu cha Agano Jipya

Mungu ana umilele wa aina tatu, uthihirisho wa nafsi (tazama Mada Maalum: Utatu)

1. Mungu amefuliwa kwa ukamilifu na utimilifu katika Yesu (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15-19; Ebr. 1:2-3)

Mpango wa Mungu wa milele kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka ni kujitoa dhabihu kwa Mwana Wake wa pekee (Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; FlP. 2:6-11; Webrania)

**40:15-17 "mataifa ni kama tone la maji katika ndoo…… huhesabiwa kuwa kama mavumbi membamba katika mizani. . . Mataifa yote huwa kama si kitu mbele zake"** Huu ni msisitizo juu ya nguvu za Mungu (kama vile Yer. 10:10), sio juu ya ukosefu wake wa uangalizi au huruma juu ya mataifa. YHWH alimtuma Yesu kwa ajili ya ukombozi wa kizazi chote cha mwanadamu. Hata hivyo, mataifa yaliyoasi yatahukumiwa (kama vile 17:13; 29:5,7).

## MADA MAALUM: UPENDELEO WA KIINJILISTI WA BOB

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Jer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31),wale wote walioumbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israel, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.

Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anaoanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israeli. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihirisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Ibrahimu, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, "kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu"). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakilisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)

6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
    a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
    b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
    c. Mika 4:1-3
    d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipya" (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimarisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihirishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya limejikita shabaha yake juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israeli ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumaini utaendelea kuchukua muda kusoma Mada Maalum:Kwanini Ahadi za kiagano za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti sana na Ahadi za kiagano za Agano Jipya. Unaweza ukaipata mtandaoni katika wavuti www.freebiblecommentary.org.

**40:16** Hoja ya hii aya ni kuwa hata katika eneo (yaani., Lebanoni) ambalo limejaa msitu mkubwa na kujaa wanyama wa mwitu asingaliweza kutoa dhabihu ya kutosha kwa ukubwa wa agano la Mungu wa Israeli. Kwa ajili ya jaribio la ubadhirifu wenye kufanana na utoaji dhabihu ya kutosha angalia muhtasari katika I Fal. 8:63.

**40:17**
**NASB** "isio maana"
**NKJV** "isio thamani"
**NRSV, NJB** "tupu"

Neno hili, תהו; (BDB 1062), limetumika kuelezea pindi dunia ikiwa tupu katika Mwa. 1:2 (kama vile Isa. 34:11; 45:18; Yer.4:23). Pia limetumika juu ya sanamu za kuchonga (I Sam. 12:21; Isa. 41:29; 44:9).

Isaya huzitumia katika sura ile ile kwa ajili ya utupu wa watawala wa kibinadamu (yaani., Misri, Ashuru, Babeli, Uajemi, na maadui wote wa watu wa Mungu). Muungano wa mwanadamu na nguvu havilinganishi na mipango na nguvu za YHWH.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA)40: 18-20**
**18 Basi, mtamlinganisha Mungu na nani?**
**Au mtamfananisha na mfano wa namna gani?**
**19 Sanamu fundi mmoja huiyeyusha,**
**na mfua dhahabu huifunika dhahabu,**
**huifulia mikufu ya fedha.**
**20 Yeye aliye maskini sana hata hawezi kutoa sadaka ya namna hii,**
**huchagua mti usiooza,**
**hujitafutia fundi mstadi wa kusimamisha sanamu ya kuchonga isiyoweza kutikisika.**

**40:18-20** Kipengele hiki kinashughulika na ujinga wa ibada ya sanamu katika Isa. 44:9-20 na 46:1-7.

◙**"mtamlinganisha Mungu na nani"** Haya ni maelezo (kama vile mst. 25; 46:5; Kut. 8:10; 15:11; I Sam. 2:2; Mika. 7:18) ya uthibitisho mkubwa wa kithiolojia wa Wayahudi ambao tunauita imani ya Mungu mmoja (kama vile Kumb.6:4-5). Angalia Mada Maalum katika mst. 14.

**40:19**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kuunda"** |
| **NKJV, NRSV** | |
| **NJB** | **"kuyeyusha"** |
| **TEV** | **"tengeneza"** |
| **REB** | **"kuunda"** |
| **JPSOA** | **"kufua"** |

KITENZI hiki (BDB 864,, KB 1057) kimetumika mara mbili na kinarejerea juu ya uyeyushaji wa chuma katika umbo maalum (kama vile 41:7; 46:6). Toleo la NIDOTTE, juzuu ya 2, uk. 1000 inapendelea neno "ufuaji" kuliko tafasiri iliyozoeleka "uyeyushaji," kwa sababu ya nadharia ya ufanano wa visawe vya Kiebrania (angalia kiambatisho cha kwanza: Utangulizi wa Ushairi wa Kiebrania).

**40:20 "mti"** Neno hili (BDB 781) limetumika kwa aina ya mti unaotengenezwa kinyago (kama vile 44:19; 45:20; Hos. 4:12). Wawezakuwa hasa ni mti mgumu lakini baadaye ukaoza

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:21-26**
**21 Je! Hamkujua? Hamkusikia?**
**Hamkuambiwa tokea mwanzo?**
**Hamkufahamu tangu kuwekwa misingi ya dunia?**
**22 Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia,**
**na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi;**
**yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na kuzikunjua kama hema ya kukaliwa;**
**23 ndiye awatanguaye wakuu,**
**na kuwabatilisha waamuzi wa dunia.**
**24 Naam, hawakupandwa;**
**hawakutiwa katika ardhi kama mbegu;**
**naam, shina lao halikutia mizizi katika ardhi;**
**tena awapuzia tu, wakanyauka,**
**upepo wa kisulisuli wawaondoa kama mabua makavu.**
**25 Mtanifananisha na nani, basi,**
**nipate kuwa sawa naye? Asema yeye aliye Mtakatifu.**
**26 Inueni macho yenu juu, mkaone;**
**ni nani aliyeziumba hizi;**
**aletaye nje jeshi lao kwa hesabu;**
**aziita zote kwa majina;**
**kwa ukuu wa uweza wake, na kwa kuwa yeye ni hodari kwa nguvu zake;**
**hapana moja isiyokuwapo mahali pake.**

**40:21-26** Ubeti huu kithiolojia unahusiana na mistari ya 12-17. Yote inaelezea Mungu kama muumbaji, yote pia ni midogo na muhimu katika kuilinganisha. Yeye ndiye ukweli, kweli mtupu, mwenye kuishi milele! Sanamu haziwezi ishi na wanadamu wanaishi kwa mapenzi yake! Lakini kwa mshangao mkubwa anapenda kutujua sisi, kutusamehe, na kuwa na ushirika nasi! Ni Mungu wa aina gani, nani kama Yeye?

**40:21 "je? Hamkujua"** Huu mlolongo wa maswali, kama ulivyo mst. 28, unamaanisha kuwakumbusha Wayahudi juu ya Mungu wa mafunuo ya kabla.

◙**"toka misingi ya dunia"** Katika muktadha hili ni dokezo lingine kwenye uumbaji. Chakushangaza, kifungu kile kile kimerudiwa mara tano katika Agano Jipya kikirejerea matendo ya YHWH kabla ya uumbaji.

1. Mt. 25:34 – "kurithi ufalme ulioandaliwa kwa ajili yako tokea misingi ya dunia kuwepo"
2. Yohana 17:24 – "kwa maana ulinipenda kabla ya kuweka msingi wa dunia"
3. Efe. 1:4 – "alituchagua Yeye hata kabla ya misingi ya dunia kuwepo"
4. I Pet. 1:19-20 – alifahamika hata kabla ya misingi ya dunia kuwepo"
5. Ufu. 13:8 (uwezekano wa kuwepo na kitu)
    a. "kwa kila mtu ambaye jina lake halikuandikwa tokea misingi ya dunia kuwepo"
    b. "mwanakondoo aliyechinjwa kabla ya msingi wa dunia"

Mungu alikuwa mtendaji kabla, kabla na baada ya uumbaji. Alikuwa akitenda ndani ya Adamu, Nuhu, Abramu, Yakobo, Israeli na Kristo kwa ajili ya ukombozi wa wanadamu wote (angalia Mada Maalum katika 40:15)!

**40:22 "Yeye ndiye aketie juu ya duara ya dunia. . .pazia. . .hema"** Hii ni dhana ya kawaida Mashariki ya Kati ya Kale (kama vile 42:5; Ayu. 9:8; kama vile. 104:2; Yer. 10:12; 51:15; Zak. 12:1). Katika kitabu cha Wamisri kiitwacho *Book of the Dead*, mbingu imeelezewa kama "ngozi." Na Rig Veda ameielezea mbingu kama "kitu kilichonyooshwa kama cha kuzikwa." Kwa kawaida hii ni njia ya kiistiari inayozungumzia juu ya anga la mbinguni (yaani., mazingira ya hii sayari) juu ya dunia. Ni lugha ya stiari.
Neno "pazia" (BDB 201) limetumika katika maana hii hapa tu. Neno linamaanisha "kugandamiza" (kama vile 40:15, "vumbi"). Inavyoonekana laweza pia kumaanisha kitu fulani "chembamba" (KB 229, yaani., utando unaoifunika dunia). Kumbuka wafasiri wanaangalia

1. muktadha
2. Asili ya Kisemiti
3. Lugha zinazofanana

lakini #1 unapewa kipaumbele!

**40:25 "Yeye aliye Mtakatifu"** Angalia maelezo kamili katika 6:3 (vol. 11A). Cheo ni uhusiano mwingine wa kimakusudi kati ya wito wa kwanza wa Isaya, alipoambiwa kuwa Israeli haitasikia mpaka itakapoangamizwa (kama vile 6:9-11) na wito wa pili, ambapo aliambiwa "kuzungumza kwa upole" juu ya Israeli. Itasikia sasa!

**40:26 "yainue macho yako. . .uone"** Hizi zote ni*Qal* KAULI SHURUTISHI. Tambua mistari inayofanana ya mst. 26 a,b.

◙**"na utazame ni nani aliyeziumba hizi nyota. . .Huwaita kwa majina yenu. . .na hakuna hata mmoja atakayepotea"** Ni muhimu machoni pa Wababeli waabuduo nyota kuwa Mungu amechaguliwa kama muumbaji pekee, mwezeshaji, na mmiliki wa miili ya mbinguni (kama vile Mwa. 1:16; Zab. 8:3; Yer. 31:35).
Neno "akaumba" katika mst. 26 ni neno la Kiebrania *Bara*. Limetumika katika kitabu cha Mwanzo 1 juu ya uumbaji wa Mungu. Halikuwahi kutumika kwa kitu chochote au mtu yeyote isipokuwa kwenye uumbaji wa Mungu. Linajitokeza mara 20 katika kitabu cha Isaya 40-66 (kama vile 40:26,28; 41:20; 42:5; 43:1,7,15; 45:7[mara mbili],8,12,18[mara mbili]; 48:7; 54:16[mara mbili]; 57:19; 65:17,18[mara mbili]).

◙**"hakuna atakayepotea hata mmoja"** Hii ni nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha "hakuna hata mmoja atakayeshindwa kujiwasilisha kwa Bwana wake" Mungu anadhibiti nyota na sayari. Zenyewe si miungu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 40:27-31**
**27 Mbona unasema, Ee Yakobo, mbona unanena, Ee Israeli,**
**Njia yangu imefichwa, Bwana asiione,**
**na hukumu yangu imempita Mungu wangu asiiangalie?**
**28 Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana,**
**Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki;**
**akili zake hazichunguziki.**
**29 Huwapa nguvu wazimiao,**

humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo.
30 Hata vijana watazimia na kuchoka,
na wanaume vijana wataanguka;
31 bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya;
watapanda juu kwa mbawa kama tai;
watapiga mbio, wala hawatachoka;
watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia.

**40:27 "Njia yangu imefichwa, Bwana asiione,**
**na hukumu yangu imempita Mungu wangu asiiangalie**" Wayahudi (yaani., "Ee Yakobo. . .Ee Israeli") walifikiri kuwa YHWH amekwisha waacha (kama vile 49:14). YHWH amekwisha uficha uso wake toka kwao kwa muda sasa (kama vile 1:15; 8:17; 54:8; Warumi 9-11).

**40:28** Tambua nyadhifa kwa ajili ya Mungu.

1. Mungu aishie milele – Mwa. 21:33 na kumbuka Kut. 15:18; Kumb. 32:40; Zab. 90:2; Yer. 10:10
2. Bwana – YHWH (angalia Mada Maalum katika 40:3)
3. Muumbaji – (hii ndiyo imekuwa nguvu ya sura ya 40)
4. Pia anaitwa "aliye Mtakatifu" katika mst. 25

Mungu wa ahadi sasa amekuwa ni Mungu wa matukio!

◙**"hazimii wala hachoki"** Hii ni nahau ya Kiebrania yenye kumaanisha "Yeye huvumilia."
Kuna mchezo wa maneno unaohusiana na neno "kuchoka," "kuzimia" katika mistari ya 28-31.

1. mst. 28 – hazimii, BDB 419, KB 421
   hachoki, BDB 388, KB 386
2. mst. 30 – hazimii, BDB 419, KB 421
   hachoki, BDB 388, KB 386
3. mst. 30 – kujikwaa, KITENZIJINA na KITENZI CHA WAKATI USIOTIMILIFU BDB 505, KB 502)
4. mst. 31 – hachoki, BDB 388, KB 386hazimii, BDB 419, KB 421

YHWH huleta nguvu na uimalifu kwa wale wote wanaosubiri na kuamini! Nguvu ya YHWH imeelekezwa kwa watu wake (kama vile mistari ya 29-31). Wana nguvu kwa vile Yeye anazo nguvu!

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"hazieleweki"** |
| **NKJV** | **"ngumu kuchunguzika"** |
| **NRSV** | **"lisilochunguzika"** |
| **NJB** | **"zaidi ya ufahamu"** |

Neno la Kiebrania (BDB 350) kimsingi linamaanisha kuchunguza. Hapa linakanushwa (kama vile Ayubu 5:9; 9:10; 36:26; Zab. 145:3). Paulo anaelezea ukweli ule ule katika Rum. 11:33 na anarejea Isa. 40:13-14. Mungu yupo katika udhibiti! Njia zake ni kweli na mawazo yake yadumu. Hapana mshangao, wala makosa! Anatupenda, yu pamoja nasi, yupo kwa ajili yetu (kama vile mistari ya 29-31)!

**40:29 "huwapa nguvu wazimiao"** YHWH huwafariji wale anaowahukumu (kama vile 41:10; . 107:9; Yer. 31:25). Haya yanafanana na maelezo ya Yesu, "njooni kwangu, wote msumbukao na kuelemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" katika Mt. 11:28-30.

**40:30 "vijana watazimia na kuchoka"** Hii inarejerea kwa vijana walichaguliwa kujiunga na mafunzo ya kijeshi.

◙**"wanaume vijana wataanguka"** Hiki ni*Qal* KITENZIJINA HALISI na *Niphal*KAULI ISIOTIMILIFU cha asili ile ile (BDB 505, KB 502), ambacho kinachopanua wazo.

**40:31 “wamngojeao”** Hili ni neno la Kiebrania (BDB 875, KB 1082) ambalo linazungumzia matarajio ya hali ya juu. Linatumiwa na wakulima kwa ajili ya kusubilia mazao (kama vile Isa. 5:4,7). Linatumiwa na wanyang’anyi walioko kwenye mawindo (kama vile Zab. 56:6;119:95). Watu wa Mungu humngojea Yeye (kama vile 8:17; 25:9; 30:18; 33:2).

◙**“watapata nguvu mpya”** KITENZI hiki (BDB 322, KB 321, *Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFU) inamaanisha

1. hatamgeuza – Law. 27:10
2. hatambadili – Mwa. 31:7,41; 35:2
3. Hatasababisha wafanikiwe – Isa. 40:31

◙**“kama tai”** The Jewish Study Bible (ukurasa wa 864) inasema palikuwepo na imani iliyozoeleka kuwa tai hujinyonyoa manyoya ili kupata nguvu mpya (kama vile Zab. 103:5).

# ISAYA 41

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Israeli Anatiwa moyo | Israeli anahakikishiwa Msaada wa Mungu | Majaribu kwa Mataifa (41:1-42:4) | Hakikisho la Mungu juu ya Israeli | Koreshi, Chombo cha Yahweh |
| 41:1-4 (1-4) | 41:1 (1) | 41:4 (1) | 41:1 (1) | 41:1-7 (1-7) |
| | 41:2-4 (2-4) | 41:2-10 (2-10) | 41:2-4 (2-4) | |
| 41:5-16 (5-16) | 41:5-7 (5-7) | | 41:5-7 (5-7) | Israeli, Iliyochaguliwa na Kulindwa na Yahweh |
| | 41:8-10 (8-10) | | 41:8-10 (8-10) | 41:8-20 (8-20) |
| | 41:11-13 (11-13) | 41:11-13 (11-13) | 41:11-13 (11-13) | |
| | 41:14-16 (14-16) | 41:14-16 14-16) | 41:14-16 (14-16) | |
| 41:17-20 (17-20) | 41:17-20 (17-20) | 41:17-20 (17-20) | 41:17-20 (17-20) | |
| | Kutofaa kwa miungu | | BWANA anaipinga miungu ya Uongo | Kutofaa kwa miungu |
| 41:21-24 (21-24) | 41:21-24 (21-24) | 41:21-24 (21-24) | 41:21-24 (21-24) | 41:21-29 (21-29) |
| 41:25-29 (25-29) | 41:25-29 (25-29) | 41:25-29 (25-29) | 41:25-29 (25-29) | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili

3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Katika sura hii YHWH anaonyesha uweza na ukuu wake kwa kumuita Koreshi II (Uajemi, kama vile mist. ya 2, 25) kuitawala Irani toka Babeli. Badililiko hili la utawala litaonyesha.
   1. Mpango wa YHWH wa kuwakomboa watu wake (yaani, kurudi kutoka uhamishoni)
   2. Hukumu ya YHWH juu ya watu wanaoabudu sanamu ambazo haziwezi kusikia, au kutenda jambo lo lote.

B. Sura ya 41 idadi pana za maagizo yaliyotumika kama mbinu ya kifasihi yenye maswali yaliyo na majibu yenye kufahamika kwa muulizaji.
   1. Inaelekezwa kwa "enyi visiwa," mst. wa 1
      a. nisikilizeni" – BDB 361, KB 357, *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI
      b. "mataifa wajipatie nguvu mpya"– BDB 322, KB 321, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU katika maana AMRISHI
      c. "na waje karibu" – BDB 620, KB 670, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI
      d. "wakanene"– BDB 180, KB 210, *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KAULI AMARISHI
      e. "na tukaribiane pamoja kwa hukumu" – BDB 897, KB 1132, *Qal* ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
   3. Kifungu hiki kilikusudiwa "atokaye mashariki" (yaani, Koreshi II), mst. wa 2 – BDB 921, KB 1190, *Hiphil* ya KAULI AMRISHI kila kisiwa kinanena, "iweni wenye nguvu" – BDB 304, KB 302, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI
   4. YHWH anawaambia watu wake
      a. "usiogope" – BDB 431, KB 432, *Qa*l ya KAULI ISIYO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI (Pia tambua mist. ya 13, 14)
      b. "Usiogope; mimi nitakusaidia" – BDB 1043, KB 1609, *Hithpael* ya KAULI AMRISHI
   5. YHWH (na baraza la mbinguni) ya kuwa ninyi ni miungu (mist. ya 21-24)
      a. "toeni hoja zenu zenye nguvu" – BDB 897, KB 1132, *Piel* ya KAULI ISIO TIMILIFU
      b. "Wayatangaze na kutujulisha yatakayokuwa" – BDB 620, KB 670, *Hiphil* ya KAULI ISIYO TIMILIFU
      c. "watuonyeshe mambo ya zamani" – BDB 620, KB 670, *Hipil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI
      d. "wamdhihirishie yatakayotokea" – BDB 616, KB 665, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI
      e. "tukapate kuyatia moyoni, tukajue mwisho wake" – BDB 616, KB 665, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
      f. "tukapate kuyatia moyoni" – BDB 962, KB 1321, *Qal* ya KAULI YA KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
      g. "wamdhihirishie yatakayotokea baadaye" – BDB 393, KB 390, *Qal ya* KAULI YA KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
      h. "Tujulisheni yatakayokuwa baadaye" – BDB 1033, KB 1570, *Hiphil* ya KITENZI CHA KAULI SHURUTISHI
      i. "Wayatangaze na kutujulisha yatakayokuwa" – BDB 616, KB 665, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
      j. "nasi tutakiri ya kuwa ninyi ni miungu" – BDB 393, KB 390, *Qal* ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
      k. "tendeni mema" – BDB 405, KB 408, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI NUSIO TIMILIFU inayotumika kataika maana ya KAULI AMRISHI

l. “tendeni mabaya” – BDB 949, KB 1269, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI NUSIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI
m. “watatahayarika na kufadhaika” – BDB 1043, KB 1609, *Hithpael ya* KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
n. “tukaone pamoja” – BDB 431, KB 432 (or BDB 906, KB 1157, *Qal* ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO), Qal ya KAULI AMRISHI

6. YHWH naye atawajilia maliwali kama akanyagaye matope, na kama mfinyanzi afinyangaye udongo. katika mist. ya 25-2
   a. “aliyeihubiri habari ” – BDB 393, KB 390, *Qal* ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
   b. “tupate kusema, Yeye ni mwenye haki’?” – BDB 55, KB 65, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, iliyo katika maana ya KITENZI CHENYE KUTIA MOYO
   c. “hapana hata mmoja” – BDB 906, KB 1157, *Qal* ya KAULI AMRISHI

C. Kuna majaribio ya kistiari ambapo mataifa yanaitwa kwa ajili ya kutoa hesabu (mist. ya 1,21) kwa kuwa badala ya toba mbele za uwepo wa YHWH, kwa nguvu na utabiri, walitengeneza sanamu mpya.
D. Tambua idadi ya nyakati zailizotumika “Ni” inatumika. YHWH alichagua kulitenda hili. Hili linafanana na Eze.36:27-38.
E. Kipindi kipya cha kutoka kinachotokana na uhamisho kinafafanuliwa katika maneno ya kilimo kama ilivyokuwa katika Isaya 35. Ahadi za Kumbukumbu la Torati 27-29 sasa zinatambulishwa.
F. Israeli imerejeshwa katika hadhi ya agano kwa human a uweza wa YHWH

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:1-4**
[1] **Nyamazeni mbele zangu, enyi visiwa,**
**na mataifa wajipatie nguvu mpya; na waje karibu wakanene;**
**na tukaribiane pamoja kwa hukumu.**
[2] **Ni nani aliyemwinua mmoja atokaye mashariki,**
**ambaye katika haki amemwita mguuni pake?**
**Ampa mataifa mbele yake,**
**na kumtawaza juu ya wafalme;**
**awatoa wawe kama mavumbi kwa upanga wake,**
**kama makapi yaliyopeperushwa kwa upinde wake.**
[3] **Awafuatia, apita salama hata kwa njia asiyoikanyaga kamwe kwa miguu yake.**
[4] **Ni nani aliyetenda na kufanya jambo hilo,**
**aviitaye vizazi tangu mwanzo?**
**Mimi, Bwana, wa kwanza na wa mwisho, mimi ndiye.**

**41:1** Mstari wa1 ni mbinu ya kifasihi inayotumika katika agano la Kale mara kwa mara (yaani, kipengele cha kimahakama, kama vile 1:18-20; 43:26; 50:8;Hosea 4; Mika 6; angalia Kiambatisho cha Pili). YHWH anayaleta mataifa, na katika mst. 21, sanamu zao mbele ya kiti chake cha hukumu.

◙
**NASB, NKJV,**
**NRSV** **“visiwa vya pembezoni”**
**TEV** **“nchi za mbali”**
**NJB, REB** **“pembezoni na visiwani”**

Hili neno (BDB 15) linamaanisha “pwani” au “jimbo.” Mara nyingi Isaya analitumia neno hili kuayarejelea Mataifa yaliyomo katika maeneo ya Shamu (kama vile 11:11; 24:15; 40:1,5; 41:1; 42:4,10,12; 49:1; 51:5; 59:18; 60:9; 66:19).

Hili linafanana na neno "watu" (BDB 522, kama vile 49:1). Inaonekana kwamba taifa la Edomu linatumika kama ishara ya "mataifa yote yaliyoasi" (yaani, 34:5-17; 63:1-6; Yer. 49:7-22; Omb. 4:21-22; Eze. 25:12-14; 35:1-15; Obadia, Mal. 1:2-4). Katika Isaya neno hili mara nyingi linasimama badala ya Mataifa ya Wapagani, kama Filistia na Fonesia (kama vile 23:2-6).

◙**"Nyamazeni"** Hili neno lingine linalohusiana na kipengele cha kimahakama (kama vile. Hab. 2:20; Zek. 2:13). Hakuna lingine liwezalo kusemwa katika nuru ya uwepo na nguvu ya YHWH.

◙**"wajipatie nguvu mpya"** Inashangaza kwamba KITENZI kile kile (BDB 322, KB 321, *Hiphil* cha KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU kinachotumika katika maana ya KAULI AMRISHI) kinatumika kwa watu wa Mungu katika 40:31 na sasa kinatumika kwa neno "watu" (yaani, Mataifa).

◙**"waje karibu"** Hiki KITENZI "kuvutia" (BDB 620, KB 670, *Qal* CHA KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU kinachotutumika katika maana ya KAULI AMRISHI) kinaweza kumaanisha makuhani wenye kumsogelea YHWH katika dhabihu na ibada, lakini hapa huku ni kuikaribia hukumu kwa maan ya ulinzi (kama vile 34:1; 48:16).

**41:2"mashariki "** Kifungu hiki kinamrejelea Koreshi II (kama vile "mtu toka kaskazini," mst. wa 25). Huyu anatajwa kwa jina hasa katika Isa. 44:28; 45:1. Koreshi II

1. alikuwa Mfalme wa Anshani mnamo mwaka 558 K .K.
2. aliupokea uatawala wa Media mnamo mwaka 550 K.K.
3. aliitawala Lidia mnamo mwaka 546 K.K.
4. aliitawala Babeli mnamo 539 K.K.
5. alitoa maagaizo mnamo mwaka 538 K.K. kwamba makundi kuwasili kwa makundi ya watu yaliyohamishwa Ashuru na Babeli lazima yarejee nyumbani, wakiwemo Wayahudi

◙**"ambaye katika haki "** Toleo la JPSOA linakitafsiri kifungu hiki kwa kuunganisha mawazo ya mstari wa 1 na 2, "aliyemwinua mmoja atokaye mashariki "

Toleo la Jewish Study Bible (864) linataja kwamba toleo la Targums linakitafsiri kifungu hiki ili kumrejelea Ibrahimu ambaye YHWH alimwita kutoka Uri ya Wakaldayo. Sehemu ya kijeshi ya mst. wa 2 ingeirejelea Mwanzo 14, Ibrahimu kuwashinda wafalme.

◙**"mguuni pake"** Lazima ikumbukwe kwamba Sanduku la Agano lilitazamwa kama mahali pa YHWH kuweka miguu na, ambapo, ndipo palipo na uwepo wake. Hiki ni kifungu kinachomweleza Mungu kama mwanadamu.

## MADA MAALUM : MUNGU ANAELEZWA KAMA MWANADAMU

I. Aina hii ya lugha (yaani, Uungu unaelezwa katika maneno ya kibinadamu) ni wa kawaida katika Agano la Kale (baadhi ya mifano)
   A. Viungo vya mwili
      1. macho - Mwa. 1:4,31; 6:8; Kut. 33:17; Hes. 14:14; Kumb. 11:12; Zek. 4:10
      2. mikono – Kut. 15:17; Hes. 11:23; Kumb. 2:15
      3. viganja – Kut. 6:6; 15:16; Kumb. 4:34; 5:15;26:8
      4. masikio – Hes. 11:18; 1 Sam. 8:21; II Fal. 19:16; Zab. 5:1; 10:17; 18:6
      5. uso – Kut. 33:11; Law. 20:3,5,6; Hes. 6:25; 12:8; Kumb. 31:17; 32:20; 34:10
      6. vidole – Kut. 8:19; 31:18; Kumb. 9:10; Zab. 8:3
      7. sauti – Mwa. 3:9,11,13; Kut. 15:26; 19:19; Kumb. 26:17; 27:10
      8. miguu – Kut. 24:10; Ezek. 43:7
      9. umbo la mtu – Kut. 24:9-11; Zaburi 47; Isa. 6:1; Ezek. 1:26
      10. malaika wa Bwana – Mwa. 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16; Kut. 3:4,13-21; 14:19; Amu. 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   B. Matendo ya mwili (angalia mifano)

1. kuongea kama moja ya mfumo wa uumbaji- Mwa. 1:3,6,9,11,14,20,24,26
2. kutembea (yaani sauti ya) - Mwa. 3:8; Law.26:12; Kumb. 23:14; Hab. 23:14
3. kufunga mlango wa safina ya Nuhu – Mwa. 7:16
4. kunukia dhabihu – Mwa. 8:21; Law. 26:31; Amo. 5:21
5. kurudi chini – Mwa. 11:5; 18:21; Kut. 3:8; 19:11,18,20
6. maziko ya Musa – Kumb. 34:6

C. Mihemuko ya kibinadamu (baadhi ya mifano)
   1. majuto/toba- Mwa. 6:6,7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:29,35; Amo. 7:3,6
   2. hasira- Kut. 4:14; 15:7; Hes. 11:10; 12:9; 22:22; 25:3,4; 32:10,13,14; Kumb. 6:15; 7:4; 29:20
   3. wivu - Kut. 20:5; 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15; 32:16,21; Yosh. 24:19
   4. karaha/chuki- Law. 20:23; 26:30; Kumb. 32:19

D. Maneno ya kifamilia (baadhi ya mifano)
   1. Baba
      a. wa Israeli- Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 31:9; Hos. 11:1
      b. wa Wafalme- 2 Sam. 7:11-16; Zab. 2:7
      c. sitiari za vitendo vya kibaba- Kumb. 1:31; 8:5; 32:6-14; Zab. 27:10; Mith. 3:12; Yer. 3:4,22; 31:20; Hosea 11:1-4; Mal. 3:17
   2. Mzazi – Hosea 11:1-4
   3. Mama- Isa. 49:15; 66:9-13 (mshabihiano wa unyonyeshaji wa mama)
   4. Kijana mpendwa mwaminifu-Hosea 1-3

II. Sababu za kutumia aina hii ya lugha

A. Ni muhimu kwa Mungu kujidhihirisha Mwenyewe kwa viumbe vya kibinadamu. Hakuna msamiati mwingine kuliko ule wa kuanguka, manaeno ya kidunia. Dhana iliyosambaa ya Mungu kuwa wa jinsia ya kiume ni mfano mmoja wa lugha ya kumwelezea binadamu kwa sababu Mungu ni roho!

B. Mungu anachukulia dhana ya maana halisi ya maisha ya mwanadamu na kuwatumia ili kujidhihilisha Mwenyewe kwa mwanadamu aliyeanguka (baba, mama, mzazi, mpendwa)

C. Ingawa ni muhimu, Mungu hahitaji kuwekewa pingamizi kwa aina yeyote juu ya umbo la kibinadamu (kama vile Kutoka 20; Kumbukumbu 5)

D. Hatima ya Mungu kuelezewa kama mtu ni kubadilika kwa Yesu katika umbo la kibinadamu! Mungu akawa mtu, mwenye kugusika (kama vile Yohana 1:1-3). Ujumbe wa Mungu ukafanyika Neno la Mungu (kama vile Yohana 1:1-8).

IIII. Kwa majadala wa kimhutasari, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, sura ya 10, "Anthropomorphism," in *The International Standard Bible Encyclopaedia*, kr. 152-154

◙**"Yeye"** tambua mambo yote ambayo YHWH aliyamfanyia Koreshi II.

1. alimwinua kutoka mashariki
2. alimwita katika haki
3. aliyaleta mataifa mbele zake
4. alimtawaza juu ya wafalme
   a. kama mavumbi
   b. kama makapi Mstari wa 3 inaeleza juu ya harakisho la ushindi wake . Mstari wa 4 unamfafanua Bwana ambaye anakamilisha ushindi kwa ajili ya makusudi yake ya ukombozi na urejesho kwa watu wake.

◙

**NASB** **"kumtawaza juu ya wafalme"**
**NKJV** **"kuwatawala "**
**NRSV, JPSOA** **"kuwakanyaga"**
**TEV** **"ushindi"**
**NJB** **"mambo"**

**REB "kuwaondosha"**

Tatizo ni hiki KITENZI hadimu (BDB 921, KB 1190, *Hiphil* ya KAULI AMRISHI). Hiki kinaonekana kutoendana na muktadha, kina uchaguzi mwingi sana. Hiki KITENZI lazima kimrejelee Koreshi.

**41:3**
**NASB "kupita na miguu yake**
**NKJV "alikuwa amepita na miguu yake"**
**NRSV, NJB "bila hata kuigusa njia na miguu yake"**
**REB "kwa upole na haraka zaidi ya msafiri mwingine wa miguu"**
**JPSOA "hakuna minyororo iliyofungwa katika miguu yake"**
Kiebrania ni tata. Matoleo ya kale hayakukielewa

1. LXX – "njia ya miguu yake itadumu katika amani"
2. Peshitta – "hataipita njia hiyo kwa mguu"
3. DSS – "hawaitengi njia yake kwa miguu"

Tafsiri nyingi za lugha ya Kiingereza zinakiona kifungu hiki kama stiari ya mwendo kasi. Hata hivyo, toleo la JPSOA linalitafsiri neno hili "njia" kama "pingu" kutoka asili ya Kiaramu cha Kale. Hili linaweza kurejelea himaya mpya (Biblia ya NET ).

**41:4"aviitaye vizazi tangu mwanzo"** Hii ni nahau inayouzungumzia utawala wa YHWH wakati na historia (kama vile 40:21; 41:26; 44:7; 45:21). YHWH anaelekeza uumbaji, wito wa Ibrahimu, na uzao wake kwa makusudi yake. Unabii wa Agano la Kale uliotabiriwa unajikita katika nguvu za kiuthibitisho za Bibia iliyovuviwa!

**◙"'Mimi, Bwana, wa kwanza na wa mwisho, mimi ndiye'"** Kuna mfuatano wa maneno ya Kiebrania na miundo iliyotumika hapa kumfafanua Mungu.

1. "Bwana linatokana na KITENZI "kitenzi kisaidizi" (kama vile Kut. 3:14, angalia Mada Maalum katika 40:3)
2. "kwanza na mwisho" (kama vile Isa. 44:6)
3. "Mimi ndiye" huakisi neno "YHWH" (kama vile Isa. 43:10; 46:4; Yohana 8:57-58; 13:9)

Kwa pamoja, maneno haya yanaonekana kuakisi kwamba Mungu ndiye aishiye pekee, Mungu aishiye daima (angalia Mada Maalum: Imani ya Mungu Mmoja katika 40:14). Haya yanatumika kumzungumzia Yesu , Masihi wa YHWH katika Ufu. 1:8,17; 22:13.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:5-17**

**5 Visiwa vimeona, vikaogopa;**
**ncha za dunia zilitetemeka; walikaribia, walikuja.**
**6 Wakasaidiana, kila mtu na mwenzake,**
**kila mtu akamwambia ndugu yake;**
**Uwe na moyo mkuu.**
**7 Seremala akamtia moyo mfua dhahabu,**
**na yeye alainishaye kwa nyundo akamhimiza yule apigaye fuawe,**
**akiisifu kazi ya kuunga, akisema, Ni kazi njema; naye akaikaza kwa misumari isitikisike.**
**8 Nawe, Israeli, mtumishi wangu;**
**Yakobo, niliyekuchagua; mzao wa Ibrahimu, rafiki yangu;**
**9 wewe niliyekushika toka miisho ya dunia,**
**na kukuita toka pembe zake, nikikuambia, Wewe u mtumishi wangu;**
**nimekuchagua wala sikukutupa;**
**10 usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe;**
**usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako;**
**nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam,**
**nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.**
**11 Tazama, wote walioona hasira juu yako watatahayarika na kufadhaika;**

**watu washindanao nawe watakuwa si kitu, na kuangamia.**
**12Utawatafuta wala hutawaona wale wapiganao nawe;**
**watakuwa si kitu; watakuwa kama kitu kisichokuwa, wale waliofanya vita juu yako.**
**13Kwa maana mimi, Bwana, Mungu wako, nitakushika mkono wako wa kuume, nikikuambia,**
**Usiogope; mimi nitakusaidia.**
**14Usiogope, Yakobo uliye mdudu, nanyi watu wa Israeli;**
**mimi nitakusaidia, asema Bwana, na mkombozi wako ni Mtakatifu wa Israeli.**
**15Tazama, nitakufanya kuwa chombo kikali kipya cha kupuria, chenye meno;**
**utaifikicha milima, na kuisaga; nawe utafanya vilima kuwa kama makapi.**
**16Utawapepeta, na upepo utawapeperusha;**
**upepo wa kisulisuli utawatawanya;**
**nawe utamfurahia Bwana, utajitukuza katika Mtakatifu wa Israeli.**
**17Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana;**
**ndimi zao zimekauka kwa kiu; mimi, Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha.**

**41:5"ncha za dunia"** Huu mstari wa pili unafanana na kifungu "nchi za pembezoni," angalia maelezo katika mst. wa 1. Vyote vinarejelea Mediterania na ulimwengu wote Mashariki "unao julikana".

**41:6-7**KITENZI cha Kiebrania "kuwa na moyo mkuu" (BDB 304, KB 302) kianatumika mara tatu katika mistari hii.

1. *Qal ya* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU – uwe na moyo mkuu, mst. wa 6
2. *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU - kutia moyo, mst. wa 7
3. *Piel ya* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU – akaikaza, mst. wa 7

Mataifa yaliitazamia miungu yao kwa ajili ya kuhitaji msaaada, katika hali isiyokuwa ya matumaini, miungu yao isingeona, kusikia, au kutenda!

**41:8"Nawe, Israeli, mtumishi wangu"** Kumekuwa na mjadala mwingi kuhusu neno"Mtumishi wangu." Hili linaonekana kutumika katika namna tatu tofauti ndani ya kitabu cha Agano la Kale.

1. mkwa mtu binafsi kama mfalme au nabii (kama vile Hes. 12:7)
2. kwa taifa la Israel i(kama vile Isa. 42:19; 44:21)
3. hatimaye kwa wazo la mwisraeli, Masihi (kama vile Isa. 52:13-53:13)

Katika kitabu cha Isaya uchaguzi wa pili na wa tatu mata nyingi unachanganywa.

◙**"niliyekuchagua"** Hiki KITENZI (BDB 103, KB 119, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ni mkazo juu ya uchaguzi wa Mungu (kama vile mst. wa 9; 43:10; 44:1,2; 49:7; Kumb. 7:6;14:2). Katika Agano la Kale uchaguzi ulikuwa kwa ajili ya utumishi (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6), ambapo katika uchaguzi wa Agano Jipya ni kwa ajili ya wokovu ambao unaelekea katika utumishi.

◙**"mzao wa Ibrahimurafiki yangu"** Tambuawito na ahadi ya YHWH katika Mwanzo 12,15,22. Hii ahadi ya Kimsingi ya Mababa wa Kiroho inasisitizwa na Paulo katika Warumi 4 naWagalatia 3. Ibrahimu pia anaitwa rafiki wa YHWH katika II Nya. 20:7; Yakobo 2:23. Walizungumza ana kwa ana katika Mwanzo 18.

**41:9"wewe niliyekushika toka. . kukuita"** VITENZI vyote ni vya KAULI YA WAKATI TIMILIFU (yaani, tendo lililokamilika).

1. niliye kushika – BDB 304, KB 302, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU
2. kukuita – BDB 894, KB 1128, *Qal ya* KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Pia tambua ufanano wa visawe kati ya

1. kutoka miisho ya dunia
2. toka pembe zake

Katika muktadha kifungu hiki kinawarejelea ambayo Ashuru iliweka makazi yake (yaani, walipohamishiwa) Waisraeli (722 K. K..) na Babeli walipoweka makazi kwa Wayudea (605, 597, 586, 582 K.K. .).

◙**"nimekuchagua wala sikukutupa"** Yuda alihisi kwamba Mungu amewakataa kwa sababu ya uhamisho nan a maangamizi ya Yerusalemu na Hekalu. Hiki KITENZI "kukutupa" (BDB 549, KB 540, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, ILIYOKANUSHWA) kinatumika katika Law. 26:44, ambapo YHWH alihaidi kuwaondosha watu wake moja kwa moja kwa sababu ya dhambi na agano lao kuvunjwa. Swali linakuja, Je! Ni kwa namna gani ahadi hii iliathiriwa na Agano Jipya? Inaonekana kwangu kuwa kuna uchaguzi wa aina kuu mbili.

1. Kizingiti cha Israeli kinayo nafasi katika nyakati za mwisho (yaani, Warumi 9-11).
2. Watu wa Mungu wamekuwa wale wanao mtumaini na kushi katika Yeye. Katika Agano la Kale hili lilirejelea uzao wa Ibrahimu, lakini pia Melkizedeki (Mwanzo 14); Ayubu (Ayubu 1); Yethro (Kutoka); Kalebu (Yoshua); Uria (II Samweli 11); na wengine hawakuwa Waisraeli. Katika Agano Jpya kinapewa mapana kwa Mataifa yote yanayoamini (yaani, Rum. 2:28-29; Wagalatia 3).

**41:10 "usiogope"** Hili ni neno la kawaida sana kutoka kwa YHWH hadi kwa watu wake (kama vile mist. ya 13,14; 43:1,5; 44:2,8; 51:7,12; 55:4,14). Elewa ni kwa nini hatupaswi kuogapa.

1. YHWH yuko nao kibinafsi
2. YHWH ni Mungu wao wa agano
3. Atawahimarisha
4. Atawasaidia (mist. ya 10,14)
5. Atawashikilia (mist. ya 10.13)
6. Wale wote walio kinyume nao wata
   a. aibishwa
   b. wataangamizwa
   c. hawatakuwa kitu (mist. ya 11-12)
   d. watapotea

◙**"kwa maana mimi ni pamoja nawe"** Katika kifungu hiki hakuna KITENZI kilichoelezwa (angalia NKJV). Kuna neno la kimzaha lililokusudiwa kwa udhairi wake (kama vile mst.wa 13) kati ya maana ya KITENZI kinachohitajika (mimi) na jina la Mungu , YHWH (Mimi ni Niki ambaye niko, kama vile Kut. 3:14). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 40:3. Hakuna ahadi kuu katika Biblia yote (kama vile Mt. 28:20; Matendo ya Mitume 18:20).

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"usifadhaike"** |
| **NKJV, Peshitta** | **"usikate tamaa"** |
| **NRSV, REB** | **"usiogope"** |
| **TEV** | **"pasiwepo na jambo la kukutisha"** |
| **NJB** | **"usiwe na shaka"** |
| **LXX** | **"usishangae"** |

KITENZI cha Kiebrania (BDB 1043, KB 1609) katika neno *Hithpael*, kinamaanisha "usiangaze macho (katika mfadhaiko)."

Inawezekana kwamba KITENZI kinatokana na asili nyingine (שתע), ambayo inapatikana katika Ugaritiki, maana yake "ogopa" (Biblia ya NET, uk. 1250, #21).

**41:11** "**wote walioona . . . washindanao**" Kumbuka kwamba Mungu amehaidi kuwabariki wale wanawabariki watu wake na kuwalaani wale wanao walaani (kama vile Mwa. 12:3). Lazima ikumbukwe kwamba nguvu za Israeli, imani, na tumainie lilikuwa katika YHWH, si katika wao wenyewe. Tambua namna ya kurudi kwa wapinzani wa Waisraeli kunavyobainishwa.

1. walioona hasira juu yako, mst. wa 11
2. washindanao nawe, mst. 11
3. wale wapiganao nawe, mst. wa 12
4. wale waliofanya vita juu yako, msv. wa12

Pia tambua maangamizi yatakayowapata.

1. watatahayarika, mst. wa 11
2. kufadhaika, mst. wa 11
3. watakuwa si kitu, mst. wa 11
4. kuangamia , mst. wa 11
5. hutawaona, mst. wa 12
6. watakuwa si kitu, mst. wa 12
7. kitu kisichokuwa, mst. wa 12

**41:14"Yakobo uliye mdudu, nanyi watu wa Israelil"** Hii rejeayenye kumrejelea Yakobo kama mdudu si neno la kuaibisha , bali linaonekana kuwa stiari ya msaada wake (kama vile Ayubu 25:6;Zab. 22:6) pasipokuwa na tamko la Mungu, hii ni sawa na taswira ya Eze. 16:6.

◙**"mkombozi wako"** Hili jina (jina la KAULI ENDELEVU, kama vile 43:14) linaakisi neno la Kiebrania *Go'el* (BDB 145, KB169). Hili neno la Kiebrania linarejelea "mkombozi wa jamaa wa karibu" au "mlipa kisasi." Hili linatumika kwa mtu yule anaye mnunua jamaa yake wa karibu kutoka utumwani au mateka wa vita (kama vile mfano wa Boazi katika in Ruthu 4:1 na kuendelea)

## MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

. AGANO LA KALE

A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
   1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
   2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
      a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
      b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
      c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)
B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
   1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
      a. Kimaumbile
      b. Kijamii
      c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
   2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
      a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
      b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
   3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., *go'el*, BDB 145).
   4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
      a. Baba
      b. Mme
      c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

. AGANO JIPYA

A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
   1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisis ni wa Kristo.
   2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laanae" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
   3. *Luō,* "kuweka huru"
      a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
      b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
         1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
         2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
         3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
      c. *Lutrōsis,* "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
         1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
         2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
         3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
   4. *Apolytrōsis*
      a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
         1) Luka 21:28
         2) Warumi 8:23
         3) Waefeso 1:14; 4:30
         4) Waebrania 9:15
      b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
         1) Warumi 3:24
         2) 1 Wakorintho 1:30
         3) Waefeso 1:7
         4) Wakolosai 1:14
   5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).

B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.

   1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
   2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
   3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
   4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).

5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!
6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu(tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

◙**"Mtakatifu wa Israeli "** Hili ni jiana la Uungu linalopendwa sana katika Isaya (kama vile 1:4; 5:19; 10:17,20; 12:6;17:7; 29:19,23; 30:11,12,15; 31:1; 37:23; pia katika sehemu ya pili ya Isaya, 40:25; 41:14,16,20; 43:3,14,15; 45:11; 47:4; 48:17; 49:7; 54:5; 55:5; 60:9,14). Kwa kuwa yeye ni "mtakatifu" yawapasa watu wake kuwa watakatifu (kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; I Pet. 1:16).

Hili jina, katika maana hii, mvutano wa dhambi usiowezekana, watu walioanguka kukubalika katika kiwango cha utakatifu. Agano la Musa halikuwa na uwezekano wa kutunzwa (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3; Waebrania). Agano la kale ilikuwa njia ya kuonyesha kutokuwepo uwezekano wa wanadamu kukifikia kiwango cha Mungu, bado aliendelea kuwa amoja naye, kwao, akiwaandaa kwa ajili ya kutoa majibu ya hali ya kuanguka kwao. Yeye si mpenzi wa kiwango chake, bali anautoa upendo wake kupitia Msia. Agano Jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38) ni agano la imani na toba, tendo la kibinadamu, ingawa jambo hili linawekwa katika Ufananano na Kristo(kama vile Yakobo 2:14-26). Mungu huwataka watu wenye kuiakisi tabia yake kwa mataifa (kama vile Mt. 5:48).

## MADA MAALUM: UTAKASO

Kitabu cha Agano jipya kinadai kwamba wenye dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kumtoa mtu hatiani).

Lakini Agano Jipya pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, ni utakaso.

**<u>Mwitikio wa Awali Uendelevu wa Ufanano na Kristo</u>**

| | |
|---|---|
| Matendo 20:23:26:18 | Warumi 6:19 |
| Warumi 15:16 | 2 Kor. 7:1 |
| I Wakorintho1:2-3; 6:11 | 1 Wathesalonike. 3:13; 4:3-4,7; 5:2 |
| 2 Wathesalonike 2:13 | 1 Timotheo 2:15 |
| Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12 | 2 Timotheo 2:21 |
| 2 Petro 1:2 | 1 Petro 1:15-16 |
| | Waebrania 12:14 |

**41:15-16** Maadui wa wanaelezwa kama "milima" (BDB 249) na "vilima" (BDB 148) ambavyo "utaifikicha," ambapo hili ni neno la kilimo linalohusu mavuno (kama vile Mika 4:13; Hab. 3:12). Huu ni ushairi wa Kiebrania, iweni makini na tafsiri za maneno!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:17-20**
**17 Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana;**
**ndimi zao zimekauka kwa kiu; mimi, Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha.**
**18 Nitafunua vijito vya maji juu ya vilima,**
**na chemchemi katikati ya mabonde;**
**nitageuza jangwa kuwa ziwa la maji,**
**na mahali pakavu kuwa vijito vya maji.**
**19 Nitapanda katika jangwa mwerezi,**
**mshita, mhadasi, na mbono;**
**nitatia katika nyika mberoshi, mtidhari, na mteashuri pamoja;**
**20 ili waone, na kujua, wakafikiri, na kufahamu pamoja,**
**ya kuwa mkono wa Bwana ndio uliofanya jambo hilo.**
**Mtakatifu wa Israeli ndiye aliyeliumba.**

**41:17-20** Hii mistari inauakisi uwepo wa Mungu na zile baraka ambazo katika asili yake zinaleta mazidisho(kama vile Kumbukumbu la Torati 7).

**41:19** Kwa chanzo kizuri cha kuitambua mimea na wanyama wa kale angalia toleo la UBS *Fauna and Flora of theBible.*

**ANDIKO LA NASB (LILIOBORESHWA) 41:21-24**
**21 Haya, leteni maneno yenu, asema Bwana;**
**toeni hoja zenu zenye nguvu, asema mfalme wa Yakobo.**
**22 Wayatangaze na kutujulisha yatakayokuwa;**
**watuonyeshe mambo ya zamani, ni mambo gani,**
**tukapate kuyatia moyoni, tukajue mwisho wake;**
**au wamdhihirishie yatakayotokea baadaye.**
**23 Tujulisheni yatakayokuwa baadaye, nasi tutakiri ya kuwa ninyi ni miungu;**
**naam, tendeni mema au tendeni mabaya, ili tujipime, tukaone pamoja.**
**24 Tazameni, ninyi si kitu, tena kazi yenu si kitu; awachaguaye ninyi ni chukizo.**

**41:21** Hiki ni kipengele cha kimahakama (kama vile mst. wa 1).

◙**"asema mfalme wa Yakobo"** kifungu hiki kinajitokeza hapa pekee. YHWH ndiye aliyekuwa mfalme mkuu wa watu wa Agano (kama vile 44:6; I Sam. 8:7). Jina la Yakobo (yaani, Israeli) linawawakilisha watu wote wa Agano, makabila yote kumi na matatu (kama vile 45:4).

**41:22-24** Kifungu hiki kinairejelea miungu ya taifa.Mungu anawaita kutenda ama kutabiri ama kufanya jambo lo lote, lakini haiwezi kwa kuwa inayo majivuno ama haina kitu chochote (mist. ya 24,28-29).

**41:23** Mstari huu ni moja ya sehemu miongoni mwa hizo ambapo walinganishaji wa toleo laMT walitambua utofauti wa Kiebrania na kupendekeza mabadiliko.
Toleo la MT lina neno "ona," 23c (*qere*, ובאה, BDB 906, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, NKJV, Leupold), lakini wanapendekeza neno "ogopa" (*ketiv*,ובריא, BDB 431, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, NASB). Toleo la UBS Text Project linalipa neno "ona" daraja B (mashaka fulani).

**41:24** "chukizo" Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM : CHUKIZO (AGANO LA KALE)

Maana ya msingi ni "kuchukiza" au "yenye ubaya."  Hili ni tendo la kukiuka mipaka.
Neno "Cchukizo" (BDB 1072, KB 1702) lianweza kurejelea mambo kadhaa:

1. Mambo yaliyohusiana na Wamisri:
    a. hawa walichukizwa kwa tendo la kula na Waebrania, Mwa. 43:32
    b. walichukizwa kwa tendo la kuchangamana na wachungaji, Mwa. 46:34
    c. walichukizwa nkwa tendo la Waebrania kutoa dhabihu, Kut. 8:26

2. mambo yaliyohusiana na fikra za YHWH kuyahusu matendo ya Israeli:
    a. chakula kisicho safi, Kumb. 14:3-20
    b. miungu, Kumb. 7:25; 27:15
    c. roho za kiapagani,Kumb. 18:9,12
    d. kutoa dhabihu (kuteketeza) ya watoto kwa Moleki, Law. 18:21; 20:2-5; Kumb. 12:31; 18:9,12; 2 Fal. 16:3; 17:17-18; 21:6; Yer. 32:35
    e. miungu ya Mkanaani, Kumb. 13:14; 17:4; 20:17-18; 32:16; Isa. 44:19; Yer. 16:18; Eze. 5:11; 6:9; 11:18,21; 14:6; 16:50; 18:12
    f. kuwatoa dhabihu wanyama wenye makufuru, Kut. 17:1 (kama vile Kumb. 15:19-23; Mal. 1:12-13)
    g. kutoa dhabihu kwa miungu, yer. 44:4-5
    h. kujitwalia mwanamke aliyetarakishwa, Kumb. 24:1-4
    i. wanawake kuvaa mavazi ya wanaume (huenda ni idada za ki- Kanaani), Kumb. 22:5
    j. Usilete ujira wa kahaba (ibada za ki-Kanaani), Kumb. 23:18
    k. miungu ya Israeli, Yer. 2:7
    l. Kujamiina kwa jinsia (huenda ni ibada za ki-Kikanaa), Law. 18:22; 20:13
    m. kutumia vipimo visivyo sahihi, Kumb. 25:15-16; Mit. 11:1; 20:23
    n. sheria za vyakula ziilikiukwa (huenda ni ibada za ki-Kanaani), Kumb. 14:3

3. Mifano iliyo katika Fasihi ya Vitabu vya Hekima:
    a. Ayubu 30:10 – Ayubu juu ya jamii yake
    b. Zaburi 88:8 – wanazaburi katika umoja wao
    c. Mithali
        1) Mit. 3:32 – mtu mkaidi
        2) Mit. 6:16-19
            a) macho ya kiburi, Mit. 6:17a
            b) ulimi wa uongo, Mit. 6:17a
            c) mauaji, Mit. 6:17b
            d) mshauri mbaya, Mit. 6:18a; 15:26
            e) wepesi wa kukimbilia uovu,Mit. 6:18b
            f) shahidi wa uongo, Mit. 6:19a
            g) Naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu, Mit. 6:19b
        3) Mit. 11:1; 20:10,23 – vipimo visivyo sawa
        4) Mit. 11:20 – moyo wenye uhalifu
        5) Mit. 12:22 –midomo ya uongo
        6) Mit. 15:8; 21:27 – sadaka za mtu mbaya
        7) Mit. 15:9 – njia za mtu mbaya
        8) Mit. 16:5 – moyo wa majivuno
        9) Mit. 17:15
            a) asemaye kwamba asiye haki ana haki
            b) asemaye kwamba mwenye haki

(10) Mit. 28:9 – aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria

4. Kuna kifungu cha matukio ya siku ya mwisho, "chukizo la huzuni," ambacho kinatumika katika Danieli (kama vile Dan. 9:27; 11:31; 12:11). Hiki kinaonekana kuayarejelea matukio matatu tofauti tofauti (utimilifu mwingi wa unabii):
   a. Antiochus IV Epiphanes wa kipindi Wamakayo cha uwazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya (kama vile 1 Mak. 1:54,59; 2 Mak. 6:1-2)
   b. Jemedari wa Kirumi (Mfalme wa aliyefuatia), Titus, aliyeitawanya Yerusalemu na kuliharibu hekalu mnamo 70 B.K (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14; Luka 21:20)
   c. Kiongozi wa ulimwengu wa nyakati za mwisho aliyeitwa "mtu wa sheria" (kama vile 2 The. 2:3-4) au "Mpinga Kristo" (kama vile 1 Yohana 2:18; 4:3; Ufunuo 13)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 41:25-29**
**25Nimemwinua mtu toka kaskazini, naye amekuja;**
**toka maawio ya jua amekuja anitajaye jina langu;**
**naye atawajilia maliwali kama akanyagaye matope,**
**na kama mfinyanzi afinyangaye udongo.**
**26Ni nani aliyeihubiri habari tokea mwanzo, tupate kuijua?**
**Na tokea zamani, tupate kusema, Yeye ni mwenye haki?**
**Naam, hapana hata mmoja aliyetujulisha;**
**naam, hapana hata mmoja aliyetuonyesha;**
**naam, hapana hata mmoja aliyesikia maneno yenu.**
**27Mimi kwanza nitauambia Sayuni, Tazama;**
**hawa ndio; nami nitampa Yerusalemu mletaji wa habari njema.**
**28Na nitazamapo, hapana mtu,**
**hata katika watu hao hapana mshauri mmoja,**
**ambaye, nikimwuliza, aweza kunijibu neno.**
**29Tazama, hao wote ni ubatili;**
**kazi zao si kitu; sanamu zao ni upepo na fujo.**

**41:25"Nimemwinua mtu toka kaskazini"** Kwa mara nyingine kifungu hili kinamrejeleaKoreshi II (kama vile mst. wa. 2; 44:28; 45:1). Uelekeo wa pekee ambao ungemwongoza mtu kuingia ndani ya Palestine kutoka Mataifa yanayokaribia na Irani ulikuiwa ule wa kaskazini kwa sababu jangwa lilikuwa limefunika mashariki moja kwa moja (yaani., "kutoka miwio ya jua").

◙**"anitajaye jina langu"** Kipengele hiki kinaweza kuirejelea II Nya. 36:22-23 au Ezra 1:1-2.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"atawajilia maliwali"** |
| **NKJV** | **"atakuja dhidi ya watawala"** |
| **NRSV, TEV,** | |
| **NJB** | **"atembea juu ya watawala"** |
| **REB** | **"analinda juu ya watawala"** |
| **JPSOA** | **"atawaangusha watawala"** |

Toleo la MT lina KITENZI cha kawaida "kuja" (BDB 97, KB 112, *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ambacho, kinawasababisha watafsiri watoe madhaanio kutokana na muktadha, kinamaanisha "kwenda mbele." Toleo la UBS Textual Project liapenekeza uwezekano wa kuwepo asili nyingine.

1. ויבא–atawajilia/endelea mbele
2. ויבם– atawasogelea

Hata hivyo, toleo hili linaweka #1 katika anddiko lakini linalipa neno hili daraja “C” (mashaka yenye kudhaaniwa). Toleo la NET Bible linapendelea uchaguzi #2 (uk. 1251 #18).

**41:26** YHWH anauonyesha uwepo na nguvu zake kwa matendo yake yaliyotabiriwa ndani ya historia (kama vile 43:9; 45:21).

**41:27“hawa ndio”** Kipengele hiki kinaonekana kuwarejelea manabii wa kweli, kama vile mist. ya 28 na 29 inawarejele manabii wa kweli na huzuni ya watu kwa sanamu isio na msaada.

# ISAYA 42

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ahadi ya Mungu juu Ya Mtumishi wake | Mtumishi wa Bwana | Wimbo wa kwanza wa Mtumishi | Mtumishi wa BWANA | wimbo wa kwanza wa Mtumishi |
| 42:1-4<br>(1-4) | 42:1-4<br>(1-4) | 42:1-4<br>(1-4) | 42:1-4<br>(1-4) | 42:1-9<br>(1-9) |
| | | Ushindi wa Utukufu Wa Mungu | | |
| 42:5-9<br>(5-9) | 42:5-9<br>(5-9) | 42:5-9<br>(5-9) | 42:5-7<br>(5-7) | |
| | BWANA asifiwe | | 42:8-9<br>(8-9) | |
| | | | Wimbo wa Sifa | wimbo wa Ushindi |
| 42:10-13<br>(10-13) | 42:10-13<br>(10-13) | 42:10-13<br>(10-13) | 42:10-13<br>(10-13) | 42:10-17<br>(10-17) |
| Upofu wa watu | Ahadi ya msaada wa BWANA | | Mungu anahaidi kusaidia watu wake | |
| 42:14-17<br>(14-17) | 42:14-17<br>(14-17) | 42:14-17<br>(14-17) | 42:14-15<br>(14-15) | |
| | | Israeli, kipofu na Mtumishi Kiziwi<br>42:18-43:7 | 42:16-17<br>(16-17) | |
| 42:18-22<br>(18-22) | 42:18-20<br>(18-20) | 42:18-25<br>(18-25) | 42:18-20<br>(18-20) | 42:18-25<br>(18-25) |
| | Uasi wa Israeli<br>42:21-22<br>(21-22) | | 42:21-22<br>(21-22) | |
| 42:23-25<br>(23-25) | 42:23-25<br>(23-25) | | 42:23-25<br>(23-25) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi na kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Hii ni ya kwanza kati ya ushairi maalumikikusudiwa kwa au juu ya Mtumishi wa YHWH.

1. 42:1-4 au 42:1-7 au 42:1-9
2. 49:1-6 au49:1-7 au 49:1-13
3. 50:4-9 au 50:4-11
4. 52:13-53:12

Hakika  zile tatu za kwanza zinapoishia bado ni mjadala.

B. Mtumishi ana mwelekeo wa aina zote mbili wa jumla (yaani Israel) na ule wa mmoja mmoja (yaani Masihi). Ni muktadha tu au maelezo ya matendo ya Mtumishi yanayoweza kutofautisha kati ya mielekeo hii miwili. Kwa namna ya kithiolojia Masihi ni "Muisraeli halisia" au "Kuhani" wa ufalme wa makuhani (angalia Agano Jipya kitabu cha Waebrania).

C. Fasiri za Kiaramu na utafasili uitwaoTargums unaelezea kwamba Mtumishi ni Masihi.Atakuwa mwisraeli mmoja anayeyatimiliza mapenzi ya YHWH kwa ajili ya taifa na ulimwengu. Kama Koreshi II alikuwa chombo katika mkono wa YHWH kwa ajili ya safari ya ukombozi/wokovu (yaani kurudi kutoka uhamishoni), hivyo pia Masihi ataleta ukombozi wa kiroho au atarejesha kutoka katika kutengwa kutokako na anguko (Mwanzo 3). Atarejesha taswira ya Mungu iliyoharibiwa kwa mwanadamu na kuruhusu ushirika wa karibu wa Edeni kurejeshwa!

Koreshi alikuwa upanga kwa ulimwengu (kama vile 41:6) lakini Masihi atakuwa nuru (kama vile 42:6). Nuru ni sitiari kwa ajili ya ukombozi wa kiroho (kama vile 49:6).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:1-4**
**1 Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye;**
**mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye;**
**nimetia roho yangu juu yake;**
**naye atawatolea mataifa hukumu.**
**2 Hatalia, wala hatapaza sauti yake,**
**wala kuifanya isikiwe katika njia kuu.**
**3 Mwanzi uliopondeka hatauvunja,**
**wala utambi utokao moshi hatauzima;**
**atatokeza hukumu kwa kweli.**
**4 Hatazimia, wala hatakata tamaa,**
**hata atakapoweka hukumu duniani;**
**na visiwa vitaingojea sheria yake.**

**42:1 "tazama"** Hizi "tazama" mbili (BDB 243, kama vile 41:29 na 42:1) zinaleta ulinganifu wa sanamu zisizo kuwa na uhai za mataifa na shughuli za YHWH , uchaguzi wa Mungu dhidi ya uchaguzi wa taifa (kama vile 41:29). Kama ilivyo katika sura ya 40, swali linaulizwa "YHWH anazungumza na nani?" Inaweza kuwa
1. nabii
2. baraza la mbinguni
3. mbinu tu ya kifasihi kwa ajili ya YHWH kuelezea mawazo yake kwa watu wake wa Agano

◙**"Mtumishi wangu"** Hii ilikuwa ni hadhi ya heshima na kuitwa (BDB 713).
1. ilitumika katika namna ya ujumla
    a. mababa wa imani kama kundi – Kumb. 9:27
    b. manabii – II Wafalme. 9:7; 17:13; Ezra 9:11; Yer. 7:25; 26:5; 29:19; 35:15; 44:4

c. Israeli – Zab. 105:6; 136:22; Isa. 41:8-9; 42:18-19; 44:1,2,21; 45:4; 48:20; 49:3; Yer. 30:10; 46:27,28
d. Tafsiri la Agano la Kale la Kiebrania linaongeza tungo kwa mstari wa 1, ambalo inafanya irejeree taifa la Israeli ("Yakobo ni mtumishi wangu, nitamsaidia; Israeli ni mteule wangu")

2. ilitumika kwa namna ya mmmoja mmoja
   a. Ibrahimu – Mwanzo. 26:24; Zab. 105:6
   b. Ayubu – Ayubu1:8; 2:3; 42:7,8
   c. Isaka – Mwanzo. 24:14
   d. Yakobo – I Nyak. 16:13; Zab 105:6; Ezek. 28:25
   e. Musa – Kutoka. 14:31; Hes. 12:7-8; Kumb . 34:5; Yosh. 1:1-2,7,13,15
   f. Yoshua – Yosh. 24:29; Waamuzi. 2:8
   g. Kalebu – Hes 14:24
   h. Daudi – Ezek. 37:25
   i. Zerubbabeli – Hag. 2:23
   j. Suleimani – I Wafalme. 3:8
   k. Isaya – Isa. 20:3; 44:26
   l. Yesu – Mt. 12:15-21 nukuu Isa. 42:1-4

◙**"ambaye. . .Mimi"** Tazama mambo ambayo YHWH ameyafanya na atayafanya kwa Mtumishi wake maalum.
1. ambaye nampenda, mstari wa1
2. ambaye moyo wangu wamfurahia, mstari wa 1
3. nimeweka Roho yangu ndani Yake, mstari wa 1

◙**"Ata . ."** Tazama vitu mtumishi atakavyovifanya(mfululizo wa VITENZI VYA WAKATI USIOTIMILIFU).
1. ataleta haki kwa mataifa (yaani maana ya kiulimwengu, kama vile mistari ya 1; 4b,c)
2. atalia sana, mstari wa 2
3. hataiinua sauti Yake, v. mstari wa 2
4. hatofanya sauti yake isikike katika maeneo, v.mstari wa 2
5. hatovunja funjo lililochubuliwa, mstari wa 3
6. hatozima mwale uwakao, mstari wa 3
7. kwa uaminifu ataleta, mstari wa 3
8. hatovunjwa moyo, mstari wa 4
9. hatokatiliwa mbali, mstari wa 4
10. hataileta haki katika nchi, mstari wa 4

◙**"Mteule wangu"** Neno hili (BDB 103, KB 119) huashiria uchaguzi wa watu juu ya YHWH maeneo, vikundi kumtumikia Yeye.
1. maamuzi jumuishi
   a. uzao wa mababa wa imani – kumb. 4:37; 10:15
   b. Israeli – Kumbu.7:7; Zaburi. 135:4; Isa. 44:1; Ezek. 20:5
   c. watu – I Wafalme. 3:8
   d. kabila la Yuda – I Nyakati.28:4; Zab.78:68
   e. Walawi – I Nyakati.15:2; II Nyakati.29:11
2. mtu mmoja mmoja
   a. Ibrahimu – Neh. 9:7
   b. Yakobo – Zab.135:4

c. Haruni – Hes.16:5; 17:5; Zab. 105:26
d. Daudi – I Sam. 10:24; 16:8,9,10; Zab. 78:70
e. Suleimani – I Nyakati.29:1
f. Zerubabbeli – Hag. 2:23

3. maeneo (yaani hekalu) – Kumb. 12:5,11,14,18,21,26; 14:23,24,25

◙**"nafsi yangu inapendezwa"** Hii ni sawa na cheo kinachotumiwa na Baba kwa ajili ya Yesu, "Mpendwa wangu" (kama vile Mt.3:17; 17:5).

◙ **"Nimeweka Roho yangu juu Yake"** Hii inarejerea kwa Mtumishi alitiwa mafuta na kuwezeshwa kwa ajili ya jukumu (kama vile 11:2; 59:21; 61:1). Angalia Mada Maalum: "Roho" (*pneuma*) katika Biblia katika 40:7.

## MADA MAALUMU: UTU WA ROHO

Kwenye Agano la Kale "Roho wa Mungu" (yaani *ruach*) ilikuwa nguvu iliyotimiza kusudi la YHWH, lakini kuna kidokezo kwamba alikuwa mtu binafsi (yaani Mungu mmoja, tazama Mada Maalumu: U-Mungu mmoja). Hata hivyo kwenye Agano Jipya ukamilifu wa nafsi ya ubinadamu na utu wa Roho umefunuliwa:

1. Anaweza kufanyiwa kufuru (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Hufundisha (kama vile. Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Hushuhudia (kama vile Yohana 15:26)
4. Ana hukumu, anaongoza (kama vile Yohana 16:7-15)
5. Anaitwa "ambaye" (yaani, *hos*, kama vile Efe 1:14)
6. Anaweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anaweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)
8. Anaweza kupingwa (kama vile Matendo 7:51)
9. Anawatetea waaminio (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)
10. Humtukuza Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya utatu (hapa yapo matatu mioongoni mwa mengi, tazama Mada Maalumu: Utatu) pia anazungumza juu ya watu watatu.

1. Mt. 28:19
2. 2 Kor. 13:14
3. 1 Pet. 1:2

Ingawa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni sio na jinsi wakati linapohusika Roho, Agano Jipya kila mara hutumia KIVUMISHI KIONYESHI CHA JINSIA YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho anahusishwa na shughuli za binadamu.

1. Matendo 15:28
2. Rum. 8:26
3. 1 Kor. 12:11
4. Efe. 4:30

Mwanzoni kabisa mwa matendo, jukumu la roho lina sisitizwa (kama katika injili ya Yohana). Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali, sura mpya. Yesu kila wakati alikuwa na Roho. Ubatizo wake haukuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali mwanzo wa sura mpya. Roho ndio njia yenye nguvu ya makusudi ya Baba kwa sura yake (tazama Mada Maalumu:Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)!

◙**"Ataleta haki"** Angalia Mada Maalum katika 40:14.

◙**"kwa mataifa"** Tazama maana ya kiulimwengu ya tungo hii na mistari ya. 4b na c, 6c na d, 10-12! Katika manabii wa Israeli, ni Isaya ambaye aliona kwa udhahiri ujumuishwaji wa Mataifa katika ufalme wa YHWH wa siku zijazo!

**42:2 "Hatolia au kuinua sauti Yake"** Hii aidha

1. inaunganishwa na 53:7, inayorejerea hukumu ya Yesu
2. maelezo ya staili yake ya huduma ya upole
3. rejea ya maombi ya msaada ambayo Mtumishi hayaitaji (kama vile 65:14)

Chimbuko la neno hili linapendelea zaidi #3.

**42:3 "Mwanzi uliopondeka..**
**wala utambi utokao moshi"** Hii inaelezea huduma ya huruma, uelewa na uvumilivu kwa wale ambao kwa namna fulani wamejeruiwa na kupewa msongo wa mawazo (kama vile 57:15).

◙
**NASB, NRSV,**
**NJB** **"kwa uaminifu"**
**NKJV, LXX** **"kweli"**
**JPSOA** **"namna ya kweli"**

Mzizi wa kiebrania ni לאמת (BDB 52) na inatokea hapa tu. Andiko laUSB linatoa alama ya "A" kwa "kweli" na sio "kwa mataifa" (kama vile NEB). Zote "kweli" na "aminifu" ziko katika kipimo cha kimaana wa maana ya mzizi.

## MADA MAALUMU: Kusadiki, Amini, Imani na Uaminifu katika Agano la Kale

I. Maelezo ya awali

Inahitajika kuanza kwamba utumiaji wa dhana ya kithiolojia, ni wa muhimu katika Agano Jipya, hauko wazi kama ulivyoelezewa katika Agano la Kale. Hakika upo, lakini umethibitishwa katika aya na watu muhimu waliochaguliwa.

Vitu ambavyo havikupatana katika Agano la Kale

A. Watu binafsi na jamii
B. Ukabiliano binafsi na utii wa agano

Imani kwa ujumla ni ukabiliano binafsi na stadi ya maisha ya kila siku! Ni rahisi kuelezea katika maisha ya mfuasi mwaminifu kuliko katika muundo wa kinahau (yaani., usomaji wa neno). Dhana hii binafsi imeelezewa vizuri katika

A. Ibrahimu na uzao wake
B. Daudi na Israel

Watu hawa walikutana/kukabiliana na Mungu na maisha yao yalibadilika jumla (sio maisha kamilifu kihivyo, lakini ni kuendelea katika imani). Majaribu yalifichua udhaifu na nguvu ya imani yao ya kukabiliana na Mungu, lakini hatima, uhusiano wa kuamini umeendelea muda wote! Imani ilijaribiwa na kusafishwa, lakini ikaendelea kama ushuhuda kwa moyo wao wa ibada na stadi ya maisha.

II. Asili kuu iliyotumika
   A. ןמא (BDB 52, KB 63)
      1. KITENZI
      a. Shina la neno *Qal* -kutegemeza, kustawisha (yaani 2 Fal. 10:1,5; Esta. 2:7, matumizi yasio ya kithiolojia)
      b. Shina la neno ni *phal*-kuhakikisha au fanya imara, kuanzisha, kuhakiki, kuwa mwaminifu
         1) Kwa watu, Isa. 8:2; 53:1; Yer. 40:14
         2) Kwa vitu, Isa. 22:23
         3) Kwa Mungu, Kumb. 7:9; Isa. 49:7; Yer. 42:5
      c. Shina la neno *Hiphil* –kusimama imara, kusadiki, kuamini
         1) Ibrahimu alimwamini Mungu, Mwa. 15:6
         2) Waisrael katika Misri waliamini, Kut. 4:31; 14:31 (ilikanushwa katika Kumb. 1:32)

3) Waisrael wakamwamini YHWH alipoongea kupitia Musa, Kut. 19:9; Zab. 106:12,24
4) Ahazi hakuamini katika Mungu, Isa. 7:9
5) Yeyote aliyeamini katika Yeye, Isa. 28:16
6) Ukweli wa kuamini kuhusu Mungu, Isa. 43:10-12

2. NOMINO (JINSI YA KIUME) –kubaki kuwa mwaminifu (yaani., Kumb. 32:20; Isa. 25:1; 26:2)
3. KIELEZI-kweli kabisa, kweli, nakubali, iwe hivyo (kama vile. Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Isa. 65:16; Yer. 11:5; 28:6). Hii ni namna ya liturujia ya neno “amina” katika agano la kale na agano jipya.

B. תמא (BDB 54, KB 68) nomino jinsi ya kike, uimarifu, kuwa mwaminifu, kweli
1. Kwa watu, Isa. 10:20; 42:3; 48:1
2. Kwa Mungu, Kut. 34:6; Zab. 117:2; Isa. 38:18,19; 61:8
3. Kwenye ukweli, Kumb. 32:4; 1 Fal. 22:16; Zab. 33:4; 98:3; 100:5; 119:30; Yer. 9:5; Zak. 8:16

C. הנומא (BDB 53, KB 62), uimara, kusimama imara, uaminifu
1. Katika mikono, Kut. 17:12
2. Katika muda, Isa. 33:6
3. Katika watu, Yer. 5:3; 7:28; 9:2
4. Kwa Mungu, Zab. 40:11; 88:11; 89:1,2,5,8; 119:138

III. Matumizi ya Paulo juu ya dhana ya Agano la Kale

A. Paulo anaegemea uelewa wake mpya kuhusu YHWH na Agano la Kale juu ya ukabiliano wake na Yesu akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-19; 22:3-16; 26:9-18).

B. Alipatwa kuungwa mkono na Agano la Kale kwa uelewa wake mpya katika aya mbili muhimu za Agano la Kale ambazo zilitumia asili ya neno (ןמא).
1. Mwa. 15:6- ukabiliano binafsi wa Abrahamu ulioanzishwa na Mungu (Mwanzo 12) ukasababisha maisha matiifu ya imani (Mwanzo 12-22). Paulo analidokeza hili katika Rumi 4 na Wagalatia 3.
2. Isa.28:16- wale walioamini ndani yake (yaani., kujaribiwa kwa Mungu na uwekaji wa jiwe kuu la pembeni kwa uthabiti) kamwe hautakuwa
   a) Rum. 9:33 “aibisha” au “katisha tamaa”
   b) Rum.10:11, kama ilivyo hapo juu
3. Hab. 2:4-wale wote wanaomfahamu Mungu Yule aliye mwaminifu lazima waishi maisha ya uaminifu (kama vile Yer. 7:28). Paulo analitumia neno hili katika Rum. 1:17 na Gal 3:11 (pia angalia Hab. 10:38)

IV. Matumizi ya Petro ya dhana ya Agano la Kale

A. Petro anaunganisha
1. Isa. 8:14 – 1 Pet. 2:8 (jiwe la kujikwaa)
2. Isa. 28:16 – 1 Pet. 2:6 (jiwe kuu la pembeni)
3. Zab. 118:22 – 1 Petr. 2:7 (jiwe lililokatariwa)

B. Alibadilisha lugha ya kipekee ambayo iliielezea Israel kama “jamii iliyochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa teule, watu waliomilikiwa ya Mungu mwenyewe” toka
1. Kumb. 10:15; Isa. 43:21
2. Isa. 61:6; 66:21
3. Kut. 19:6; Kumb. 7:6

Na sasa anatumia kwa minajili ya imani ya kanisa katika Kristo (kama vile 1 Petr. 2:5,9)

1. Matumizi ya Yohana kwenye dhana hii

A. Utumiaji wake kwenye Agano Jpya

Neno “aaminiye" linatokana na neno la Kiyunani pisteuō ambalo pia laweza kutafasiliwa “ kuamini,” “sadiki,” au “imani.” Kwa mfano, nomino haionekani kwenye injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna mashaka kama kwenye uhalisia wa kundi kujitoa kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha wao. Mifano mingine wa utumiaji wa kubabiababia wa neno hili “kuamini” unapatikana katika Yohana

8:31-39 na Mdo. 8:31; 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi kuliko ukubalifu wa awali. Lazima uambatane na mchakato wa uanafunzi (Mt. 13:20-22,31-32).

B. Utumiaji wake ukiwa na vivumishi
   1. eis inamaanisha “ndani ya” muundo huu wa kipekee unasisitiza waumini kuweka imani yao kwa Yesu
      a. ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
      b. ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45 48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Flp. 1:29; 1 Petr. 1:8)
      c. ndani yake (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
      d. ndani ya mwana (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
      e. ndani ya Yesu(Yohana 12:11; Mdo 19:4; Gal. 2:16)
      f. ndani ya nuru (Yohana 12:36)
      g. ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
   2. *ev* inamaanisha “katika” kama ilivyo katika Yohana 3:15; Marko 1:15; Mdo 5:14
   3. *epi* ikimaanisha “katika” au “juu ya” kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
   4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
   5. *hoti*, likimaanisha “kuamini kwamba,” inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
      a. Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
      b. Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
      c. Yesu ndani ya Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
      d. Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
      e. Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
      f. Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
      g. Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
      h. Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30)
      i. Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye “Mimi ndiye” (Yohana 8:24; 13:19)
      j. Tutaishi naye (Rum. 6:8)
      k. Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

V. Hitimisho

A. Imani ya Kibiblia ni ukubarifu wa mwanadamu katika neno/agano la Kiungu. Mungu siku zote huanzisha (yaani., angalia Mada Maalumu: Agano)
   1. Toba (angalia Mada Maalumu: Toba)
   2. Sadiki/amini (angalia Mada maalumu)
   3. Utii
   4. Usitahimilivu (angalia Mada maalumu: Usitahimilivu)

B. Imani ya Kibiblia ni
   1. Uhusiano binafsi (imani ya awali)
   2. Uthibitisho wa kweli wa Kibiblia (imani katika ufunuo wa Mungu, yaani., andiko)
   3. Kuwajibika katika utii sahihi (uaminifu wa kila siku)

Imani ya Kibiblia sio tiketi ya kwenda mbinguni au utaratibu wa bima. Ni mahusiano binafsi. Na hili ndio kusudi la uumbaji, mwanadamu aliumbwa katika sura na mfanano (kama vile Mwa. 1:26-27) wa Mungu. Suala hapa ni kwamba “urafiki wa karibu.” Mungu anapendelea ushirika, sio msimamo fulani wa kithiolojia! Lakini ni ushirika na Mungu aliye mtakatifu anataka kuwa wana waonyeshe tabia za “kifamilia” (yaani., utakatifu, kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Petr. 1:15-16). Anguko (kama vile Mwanzo) liliathiri uwezo wetu kuwajibika kwa usahihi. Kwa hiyo, Mungu akatenda kwa niaba yetu (kama vile Ezek. 36:27-38), akitupatia “moyo mpya” na “roho mpya” inayotuwezesha kupitia imani na toba ili kuwa na ushirika na Yeye na kumtii Yeye!

Yote haya matatu ni muhimu. Yote haya matatu yanapaswa kudumishwa. Kusudi ni kumjua Mungu (wote kwa maana ya Wayunani na Waebrania)

C. Uaminifu wa mwanadamu ni matokea (Agano la Jipya), na sio msingi (Agano la Kale) wa uhusiano na Mungu: imani ya mwanadamu katika uaminifu wake; kusadiki kwa mwanadamu katika kuamini kwake. Moyo wa Agano Jipya katika mtazamo wa wokovu ni kwamba mwanadamu lazima mwanzoni kabisa awajibike na aendelea kuwajibika kwenye neema na rehema ya Mungu, iliyoonyeshwa katika Kristo. Alipenda, alitumwa, alitoa, lazima tuwajibike katika imani na kuamini (kama vile Efe. 2:8-9 na 10)

Mungu aliye mwaminifu anawahitaji watu waaminifu kujidhihilisha kwao kwa ajili ya ulimwengu usio na imani na kuwaleta wote kwenye imani binafsi katika Yeye.

**42:4 ". . .mpaka . ."** Hii inaelekea kumaanisha kwamba "kukanyagwa" (yaani, 52:13-53:12) kutatokea lakini kwa muda ulioamriwa.

◙**"katika nchi. . .nchi za pwani"** Hizi ziko katikauhusiano wa ki-mrandano na hiyo kuwa visawe.
Hii tena ni rejea kwa mataifa ya kipagani. Angalia dokezo katika 41:4.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:5-9**
**5Mungu Bwana anena, yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitanda;**
**yeye aliyeitandaza nchi na mazao yake;**
**yeye awapaye pumzi watu walio juu yake;**
**yeye awapaye roho wao waendao ndani yake.**
**6Mimi, Bwana, nimekuita katika haki,**
**nami nitakushika mkono,**
**na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu,**
**na nuru ya mataifa;**
**7 kuyafunua macho ya vipofu,**
**kuwatoa gerezani waliofungwa,**
**kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa**
**7kuyafunua macho ya vipofu,**
**kuwatoa gerezani waliofungwa,**
**kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa.**
**8Mimi ni Bwana; ndilo jina langu;**
**na utukufu wangu sitampa mwingine,**
**wala sitawapa sanamu sifa zangu.**
**9Tazama, mambo ya kwanza yamekuwa,**
**nami nayahubiri mambo mapya; kabla hayajatokea nawapasheni habari zake.**

**42:5-9** Kipengele hiki ni sawasawa na 40:12-17, ambayo inaweka msisitizo kwa YHWH kama muumbaji na mtawala wa uumbaji unaoonekana.

**42:5 "Mungu Bwana"** Kuna majina mawili ya uungu (angalia mada maalum katika 40:3).

1. *El* – Jina la jumla la Mungu katika Mashariki ya Karibu ya kale (BDB 42). Hapa pana KIBAINISHI CHA WAZI
2. YHWH – Jina la agano kwa ajili ya Mungu kutoka katika KITENZI "kitenzi kisaidizi" (BDB 217)

◙**"aliyeziumba"** Hiki KITENZI (BDB 135, KB 153, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU) inatumika kipekee kwa ajili ya Mungu kuumba (kama vile Mwanzo. 1:1).

◙**"mbingu"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: MBINGU (AGANO LA KALE)

Neno la Kiebrania (BDB 1029, KB 1559, lililotafasiriwa "mbingu," "anga," "mbingu," "hewa") laweza kurejea kwenye vitu vingi (yaani.,mfuatano wa kuba au tufe la uumbaji wa mwanzo):

1. katika Mwa. 1:8-20 linarejerea anga lililoko juu ya dunia sehemu ambayo mawingu hutanda na ndege huruka.
2. Kuba (kama vile. 1:6,20; Isa. 40:22; 42:5) juu ya dunia ni mahali ambapo Mungu hutuma mvua kunyesha (yaani., "madirisha ya mbingu," kama vile Zab. 78:23-29; Mal. 3:10 au "mabirika ya mbinguni," kama vile Ayubu 38:37).
3. Hili kuba ndipo nyota hukaa nasayari hutembea juu yake. Laweza kurejerea ulimwengu wote (mamilioni na mamilioni ya kundi la nyota).
4. Juu ya hili kuba ndipo kuna makazi ya Mungu (yaani., mbingu ya tatu au ya saba; angalia Mada Maalum: Mbingu na Mbingu ya Tatu). Ni mbingu iliyoko juu sana (mf., Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27,30,32; Zab. 2:4; 148:4; Isa. 66:1).
5. misisitizo ya kithiolojia
   a. Mungu ni muumbaji wa vitu vyote.
   b. Yeye hudhibiti uumbaji (yaani., nuru na giza, mvua na ukame).
   c. Huumba na kuweka mianga ya usiku (jua, mwezi, nyota, sayari, vimondo).
   d. Kuna matufe au ulimwengu wa kweli:
      1) Dunia
      2) juu ya dunia
      3) visivyoonekana /kimalaika (kama vile Kol. 1:16)
      4) Uwepo wa Mungu na makazi
   e. vyote vinahusiana na kudhibitiwa kwa mapenzi yake

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"uzao"** |
| **NKJV, NRSV** | **"vyote vitokavyo huko"** |
| **TEV** | **"vyote viishivyo huko"** |
| **NJB** | **"vile vitokavyo kwake"** |
| **JPSOA** | **"kile kiletwacho"** |

Neno (KB 993) linaweka mwelekeo wa aina mbili.

1. Mimea – Ayubu 31:8; Isa. 34:1; 42:5
2. wanadamu (sitiari kwa ajili ya uzao) – Ayubu 5:25; 21:8; 27:14; Isa. 22:24; 44:3; 48:19; 61:9;65:23

Tazama mfuatano wa"Yeye"

1. aliumba mbingu
2. Akazikunjua
3. akaitandaza nchi
4. akatandaza uzao wake
5. anatoa "uhai" (*nephesh*, BDB 675) kwa watu waishio juu yake
6. hutoa"roho" (*ruah*, BDB 924) kwa wale watembeao ndani yake

Ikiwa wanataka kutengeneza mnyororo kama wa Mwanzo 1, basi mimea haswa ndiyo itakuwa maana inayofaa. Ikiwa ni aina ya mrandano wa visawe basi watu watakuwa ndiyo shabaha. Uhai, sio maada ndiyo hutoka kwa YHWH. Yeye ni Mungu aishiye milele, Mungu pekee anayeishi!

**42:6-7** Mistari hii inaelezea kile ambacho YHWH anakifanya kwa watu Wake. Anawachagua kwa ajili ya Kusudi (Angalia Mada maalum katika 40:15).

1. aliwaita (BDB 894, KB 1128, *Qal*KAULI YA WAKATI TIMILIFU) katika haki
2. akawashika kwa mkono (BDB 304, KB 302, *Hiphil* HALI YA KUSIHI)
3. Anawalinda (BDB 665, KB 718, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
4. aliwateuwa kama watu wake wa agano (BDB 678, KB 733, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
    a. kama nuru kwa mataifa
    b. kuwafungua macho vipofu
    c. kuwafungua waliofungwa

uzao wa Ibrahimu ilikuwa vyote
1. Ufalme wa makuhani
2. Mfalme/Kuhani (Masihi, kama vile Zaburi 110)

aliyekuja kuukomboa ulimwengu kutoka katika giza na gereza la dhambi (Mwanzo 3).
Kuna baadhi ya mashaka kuhusu mzizi wa Kiebrania wa #3
1. kulinda (נצר) – NASB, NKJV, NRSV
2. kutengeneza (יצר) – NJB, JPSOA, REB

Tazama kile ambacho Masihi/Mtumishi atakitimiliza.
1. utawala wa haki (kama vile 9:6-7; 11:3-4)
2. utawala wa kiulimwengu wote (kama vile 45:22; 49:6; 52:10; Mika 5:4)
3. kuwafungua macho vipofu (kama vile 29:18; 32:3; 35:5)
4. kuwafungua wafungwa (kama vile 61:1)

**42:8 "Mimi ni BWANA,hilo ndilo Jina Langu"** Hili ni jina la agano la Mungu. Angalia Mada maalum katika 40:3.

◙**"Utukufu wangu"** Hili ni neno gumu (BDB 458) kulitolea maana. katika 6:3 linajaza nchi yote. Katika 40:5 Itafunuliwa kwa nchi yote. Katika namna inaonekana inawakilisha uwepo binafsi wa YHWH.
Katika Agano Jipya, utukufu wa YHWH unafunuliwa kikamilifu katika nafsi ya Masihi, Yesu (kama vile Yohana 1:14; 11:4,40; 17:4).

## MADA MAALUMU: UTUKUFU (AGANO LA KALE)

I. Maana yake ya kimsingi

Kuna maneno yapatayo ishirini yaliyo litafasiri neno "utukufu" (*doxa)* Tafsiri ya maandiko ya kale la Kiyunani, lakini neno la Kiebrania lililo muhimu sana ni *kabod* (BDB 458-459, 455-458). Maana yake ya msingi ni ile ambayo ni nzito. Lilikuwa ni neno la kibiashara lililotumika kwenye ununuzi wa miamala (yaani vipimo). likaja kuwa na elimu-maana kubwa ambapo dhana ya uzito ikajitokeza katika kilo, watu wenye nazo, mahali na vitu.

II. Ilitumiwa na YHWH

A. ikajakuwa ndo njia ya kuelezea uwepo binafsi wa kumfunua YHWH. Ilijumuisha nguvu zake, uweza wa kifalme (yaani, uliopita mipaka) akiwa na u-mtu wake na uwepo katika umbo la kihalisia.
B. Ilidokeza YHWH katika uumbaji, kama vile Zab. 19:1; 29:3,9; 104:31
C. Lilitumika katika udhihilisho wa wazi wa Mungu kwa mwanadamu likijiungamanisha na utengenezaji wa agano la watu wake. Yeye ni "utukufu wa Israeli", kama vile 1Sam. 15:29
    1) Safari yao ya kutoka Misri kama vile Hes. 14:22 (ilitabiliwa katika Mwa. 15:12-21)
    2) Katika wingu la utukufu lililowafunika na kuwaongoza kama vile Kut. 16:7,10
    3) Utoaji wa sheria zake katika mlima Sinai

4) Matendo yake ya utoaji na hukumu wakati wa kutangatanga nyikani
   a. Uwasi wa awali uliohusiana na taarifa ya wapelelezi kumi na mbili, cf. Hes. 14:9-10
   b. Uingiliaji kati wa Musa kwa niaba yao kama vile Hes. 14:20-21
   c. Uasi wa Kola kama vile Hes. 16:19
   d. Mgogoro wa maji, kama vile Hes. 26:6

D. Ombi la Musa kutaka kumwona Mungu, kama vile Kut. 33:18-23

E. Lilitumika na YHWH mwenyewe (yaani umuhimu wake)
   1) 1Nya. 29:11
   2) Zab 106:20; Yer. 2:11; Hos. 4:7; Rum. 1:23
   3) Isa. 42:8; 45:7; 48:11; 58:8; 60:1-2,19 (Ufunuo 21:23; 22:5)
   4) Zek. 2:5,10

F. Lilitumika katika muunganikano wa uwepo wa YHWH na/ katika
   1) Hema takatifu, kama vile Kut. 16:7,10; 29:43; 40:34-35; Law. 9:6,23
   2) Hekalu, kama vile 1 Fal. 811; 2 Nyakati 5:14; 7:1-3; Isa. 6:3; Hag. 2:3,9
   3) Sanduku la agano, kama vile 1 Sam. 4:22; Zab. 63:2; 78:61

G. Lilitumika katika ufalme wa YHWH, kama vile 1 Nyakati 29:12-13; Zab. 24:7-10; 45:3

H. Lilitumika na YHWH katika hali ya kuadilisha (yaani, haki), kama vile Zab. 29:3; 97:6; Isa. 42:8; 48:11; 58:8; Hab. 2:14

III. Lilitumika kwa wanadamu na mataifa

A. Binadamu
   1. Likiendana na "nafsi" (yaani, *nephesh)* kama vile Mwa. 49:6; Zab. 16:9; 108:1
   2. Mali, kama vile Mwa. 31:1; Zab. 49:16,17; Isa. 10:3; 61:6; 66:11-12
   3. Heshima, kama vile Mwa. 45:13; Zab. 8:6; Hag. 2:7
   4. Sifa njema, kama vile Ayubu 19:9; 29:20; Zab. 4:2; 49:17
   5. Uzuri, kama vile 1 Nyakati 29:12,28; 2 Nyakati 17:5; 18:13; 32:27

B. Mataifa
   1) Misri,
   2) Efraimu, kama vile Hos. 9:11
   3) Samaria, kama vile Hos. 10:5

C. Wafalme
   1) Ahausuero, kama vile Esta 1:4
   2) Israeli, kama vile Zab 21:6
   3) Antiochus IV, kama vile Dan. 11:39

D. Majeshi ya mataifa
   1) shamu, kama vile Isa. 8:7
   2) Israeli, kama vile Isa. 17:4
   3) Kedari, kama vile Isa. 21:16

IV. Lilitumika kwenye maelezo ya siku za mwisho

A. YEHOVA atarudi kwenye hekalu lake jipya, kama vile Ezek. 43:2,4,5; 44:4

B. YHWH atauvuta ulimwengu wote kwake, kama vile Isa. 40:5; 59:19; 60:1-3; 66:18-19

C. YHWH ataishusha Yerusalemu "mpya" kama vile Isa. 66:10; Zek. 12:7

V. Kusudi la uumbaji ni kumtukuza YHWH

A. Aliumba kwa ajili ya utukufu wake, kama vile Isa. 43:7

B. Utukufu ni juu yake, kama vile 1 Nya. 16:29

C. Imba/sifu utukufu wake, kama vile Zab. 66:2; 96:8; 115:1

D. Yote tuyatendayo twayatenda katika yeye, kwa ajili ya utukufu wake, kama vile 1 Kor. 10:31; 2 Kor. 4:15; Efe. 5:22; 6:5; 1 Petro 2:12

E. Maelezo ya kwanza ya Katekismu

◙**"Sigawani Utukufu wangu na mwingine"** Angalia Isa. 40:18-26, inayozungumza juu ya uhalisia wa YHWH na kutokuwepo kwa uhalisia wa sanamu.

**42:9 "mambo mapya. . .wimbo mpya"** Neno "mpya" (BDB 294) ni maudhui inayojitokeza tokeza katika Isa. 43:19; 48:6; 62:2; 65:17; 66:33 na pia katika Kitabu cha Agano Jipya cha Ufunuo.

◙**" kabla hayajatokea nawapasheni habari zake"** Hii inarejerea 40:18-26, where ambapo anaiambia sanamu zitabiri kuonesha uhalisia wake na inashindikana, lakini YHWH yeye anaweza!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:10-13**
**10Mwimbieni Bwana wimbo mpya,**
**Na sifa zake tokea mwisho wa dunia;**
**Ninyi mshukao baharini, na vyote vilivyomo,**
**Na visiwa, nao wakaao humo.**
**11 Jangwa na miji yake na ipaze sauti zao,**
**Vijiji vinavyokaliwa na Kedari;**
**Na waimbe wenyeji wa Sela,**
**Wapige kelele toka vilele vya milima.**
**12Na wamtukuze Bwana,**
**Na kutangaza sifa zake visiwani.**
**13 Bwana atatokea kama shujaa;**
**Ataamsha wivu kama mtu wa vita;**
**Atalia, naam, atapiga kelele;**
**Atawatenda adui zake mambo makuu.**

**42:10-13** Mistari hii ina mrandano na msisitizo wa kiulimwengu wa "miji ya pwani" ya 41:1. Mataifa kwa shauku yanasubiria nuru (yaani 2:2-4; 40:4,5,6; 49:6).
Kwa wale watafutao nuru, YHWH ni kimbilio na msaada (mistari ya 6-7), lakini kwa wale waendeleao kushikilia sanamu Yeye ni mpiganaji (mstari wa 13)!

◙Kuna amri kadhaa katika mistari hii.

1. "imba" – BDB 1010, KB 1479, *Qal*KAULI SHURUTISHI, mstari wa 10
2. "inua *sauti zao*" – BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKTI USIO TIMILIFU ikitumika katika HALI YA KUSIHI, mstari wa 11
3. "imba kwa sauti" – BDB 943, KB 1247, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika namna ya HALI YA KUSIHI, mstari wa 11
4. "imba kwa kelele" – BDB 846, KB 1011, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika katika HALI YA KUSIHI, mstari wa 11
5. "toa utukufu" – BDB 962, KB 1321, *Qal*KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika katika HALI YA KUSIHI, mstari wa 12
6. "tangaza" – BDB 619, KB 665, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikitumika KATIKA HALI YA KUSIHI, mstari wa 12

**42:10** Mistari miwili ya mwisho ya mstari wa 10 inarejerea katika kikundi kilekile kama a"nchi za pwani" ya 41:1 (kama vile 42:12b).

1. enyi mwendao chini ya bahari
2. enyi visiwa

**42:11 "Kedari"** Hii (BDB 871) yawezekana inarejere mataifa ya Kiarabu. Mzizi wa Kiebrania unaweza ukarejerea kwa

1. makabila ya Kiarabu ya wafugaji – Isa. 21:16; 42:11; 60:7; Yer. 2:10; 49:28; Ezek. 27:2
2. Uzao wa Ishmaeli – Mwanzo. 25:13; I Nyakati.1:29

◙**"Sela"** Hii inamaanisha "Mwamba" (BDB 709). Hii yawezekana inarejerea Petra, mji mkuu wa Edomu (BDB 701,kama vile 16:1).

◙**"imba kwa sauti. . .paza sauti kwa furaha"** Wanafurahia juu ya nini? Utukufu wa YHWH umewaijilia wao (mstari wa 12a). Nuru imekuja kwa mataifa (mstari wa 6d). Nuru hiyo ni watu wa agano na maarifa yao ya YHWH!

**42:13** Hii inaelezea kwa maneno ya kijeshi uvamizi wa Bwana dhidi ya mataifa yaabuduyo ssanamu ambayo hupinga mapenzi yake na kurudi kwa watu wake.
1. atakwenda mbele kama mpiganaji
2. ataamsha ari kama mtu wa vita
3. atapiga kelele
4. atainua kilio cha vita
5. atashinda juu ya adui zake (yaani waabuduo sanamu, kama vile mstari wa 17)

Neno "shauku" (BDB 888) pia linatumika katika 9:7; 26:11; 37:32; 59:17 kuonesha matendo ya kimakusudi ya YHWH yanayohakikishia ushindi!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:14-17**
[14]**Siku nyingi nimenyamaza kimya;**
**nimenyamaza, nikajizuia;**
**sasa nitapiga kelele kama mwanamke aliye katika kuzaa;**
**nitaugua na kutweta pamoja.**
[15] **Nitaharibu milima na vilima, nitavikausha vyote vimeavyo;**
**nitaifanya mito ya maji kuwa visiwa, na kuyakausha maziwa ya maji.**
[16]**Nitawaleta vipofu kwa njia wasiyoijua;**
**katika mapito wasiyoyajua nitawaongoza;**
**nitafanya giza kuwa nuru mbele yao;**
**na mahali palipopotoka kuwa pamenyoka.**
**Haya nitayatenda, wala sitawaacha.**
[17] **Watarudishwa nyuma, wataaibishwa sana,**
**hao wanaotumainia sanamu za mawe,**
**na kuziambia sanamu za madini, Ninyi ndinyi miungu yetu.**

**42:14** Hii yawezekana inarejerea kipindi cha uhamishoni. YHWH alivumilia uhamisho wa watu Wake wa agano kwa hisia kali
1. nimekaa kimya kwa muda mrefu
2. nimekaa kimya na kujizuia Mwenyewe
3. nimesubiri kwa maumivu kama mwanamke atakaye kujifungua
    a. kwa huzuni (BDB 821, KB 949)
    b. kwa kuomboleza (BDB 983, KB 1375)
    c. kwa kukema (BDB 675, KB 730)

**42:15-16** YHWH anafunua msaada wake kwa watu wa agano wanaorudi.
1. Mstari wa 15 ni sitiari ya kuandaa njia laini na nzuri kwa ajili ya kurudi (pia mstari wa. 16d)
2. Mstari wa 16a-c unaelezea kujali kwake kwa wale wanaorudi
3. Mstari wa 16e-f unaelezea kujitoa na kujizatiti kwa YHWH katika kutenda (*Qal*KAULI TIMILIFU mbili)

**42:17** Huu ni mwendelezo wa YHWH kukataa na kuhukumu ibada ya sanamu (yaani, 1:28-31; 44:9-11; 45:16)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:18-22**
**[18] Sikilizeni, enyi viziwi; tazameni, enyi vipofu, mpate kuona.**
**[19] Ni nani aliye kipofu, ila mtumishi wangu?**
**Au aliye kiziwi, kama mjumbe wangu nimtumaye?**
**Ni nani aliye kipofu, kama yeye aliye na amani?**
**Naam, kipofu kama mtumishi wa Bwana?**
**[20]Unaona mambo mengi, lakini huyatii moyoni;**
**masikio yake ya wazi, lakini hasikii.**
**[21]Bwana akapendezwa, kwa ajili ya haki yake,**
**kuitukuza sheria, na kuiadhimisha.**
**[22]Lakini watu hawa ni watu walioibiwa na kutekwa;**
**wote wamenaswa katika mashimo,**
**wamefichwa katika magereza; wamekuwa mawindo,**
**wala hapana aokoaye;**
**wamekuwa mateka, wala hapana asemaye, Rudisha.**

**42:18-22** Huu ubeti unaelezea watu wa agano. Cha kushangaza ni kwamba wao pia walikuwa wamefanyika waabudu sanamu! Lakini bado walikuwa wanawajibika hata zaidi kwa ajili ya hali zao za kiroho kwasababu walikuwa na

1. mababa wa imani
2. maagano
3. ahadi (kama vile Rum. 9:4-5)

Wale ambao walitakiwa kuleta nuru kwa mataifa yaliyo gizani wenye wamefanyika giza! Walichukuliwa na laana ya Isa. 6:9-10, lakini kulikuwa na tumaini katika Isa. 35:5!

**42:18** Tazama KAULI SHURUTISHI mbili

1. sikia – BDB 1033, KB 1570, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. angalia– BDB 613, KB 661, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

◙**" enyi viziwi.......enyi vipofu"** Maneno haya yanatokea mara kadhaa katika muktadha huu na ni maelezo kwa Isa. 6:9-10.

**42:19** Tazama mrandano katika ya majina (1) "Mtumishi wangu," mstari wa 1; (2) "Mjumbe wangu," mstari wa 2; na (3) "mtumishi wa Bwana" katika mstari wa 4. Pia tambua marudio ya mara tatu ya "vipofu" (BDB 734). Kinyume ni kwamba "kipofu" ni yule anayeelezewa kama aliye

| | |
|---|---|
| NASB | "yeye aliye na amani na mimi" |
| NKJV | "yeye aliye mkamilifu |
| NRSV | "yeye aliyejitoa" |
| JPSOA | "mteule" |
| REB | yeye atumainiye" |

Neno la Kiebrania משלם (BDB 1023) halina uhakika. Kumekuwako nadhania kadhaa. Inaonekana

1. kufanana majina mengine ya Israeli (angalia juu)
2. jina ambalo lilionesha umbali kiasi gani Israeli ilikuwa kutoka katika wito wake na kujitambua

**42:20** Kuna mafanano wa dhahiri kati ya sehemu mbili za mstari wa 1 (zikihusiana na uono) na mstari wa 2 (zikihusiana na kusikia).

Jozi ya kwanza ni ile ambayo Waandishi wa toleo la MT walilitambua kama kuwa na utofauti

1. toleo la MT lilikuwa na "kuona," *Qal* KITENZI JINA HALISI (*qere*)
2. wanazuoni wa kiyahudi walipendekeza "mmekwisha kuona," *Qal* KAULI TIMILIFU (*ketiv,* pia katika gombo la Bahari ya Chumvi)

**42:21** Tatizo la Israeli halikuwa sheria ya Mungu bali kukosekana kwa uwezo wao wa kuitendea kazi (kama vile mstari wa 22; yaani Ezek. 36:22-38). IDhambi ya Israeli ilikuwa na matokeo! Agano Jipya la Yer. 31:31- 34 lilikusudiwa kujibu kukosekana huku kwa uwezo kwa wanadamu (kama vile mistari ya 23-25)

◙

**NASB, NJB "mapangoni"**
**NKJV, NRSV,**
**JPSOA "shimoni"**

Toleo la MT lina "vijana" (BDB 104), lakini muktadha unamaanisha muunda uleule "katika matundu/mashimo" (BDB 359).

1. בחורים–vijana
2. בהורים – katika mashimo

Muktadha, muktadha, muktadha ni muhimul! Mrandano wa Kiebrania katika ushairi ni muhimu katika fasiri!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 42:23-25**
**23Ni nani miongoni mwenu atakayetega sikio lake kuyasikia hayo?**
**Atakayesikiliza na kusikia kwa wakati ujao?**
**24 Ni nani aliyemtoa Yakobo awe mateka,**
**aliyemtia Israeli katika mikono ya wanyang'anyi?**
**Si yeye, Bwana? Yeye tuliyemkosa,**
**ambaye hawakutaka kwenda katika njia zake,**
**wala hawakuitii sheria yake.**
**25Kwa sababu hiyo alimwaga ukali wa hasira yake juu yake, na nguvu za vita;**
**ukawasha moto wa kumzunguka pande zote, wala hakujua;**
**ukamteketeza, wala hakuyatia hayo moyoni mwake.**

**42:24 "kwenda"** Hii imetumika katika Biblia kuonesha imani ya kibiblia kuwa ni kujitoa na kujizatiti, sio thiolojia tu. Hii yawezekana ni chanzo cha majina ya mwanzo ya Ukristo katika Matendo ya Mitume, "Njia" (kama vile 9:2; 19:9,23; 22:4; 24:14,22; na Yohana 14:6)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Israeli waliuihitaji ujumbe huu sana? (kama vile 40:27)
2. Kwanini nguvu ya Mungu inasisitizwa?
3. Je Jina la "Mtumishi wangu" linarejere kwa Wayahudi au kwa Masihi?
4. Kwanini ujumuishiwa Mataifa katika rejea kadhaa muhimu sana katika kifungu hiki cha habari?
5. Kwanini Mungu alichagua Wayahudi?

# ISAYA 43

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Israeli yakombolewa | Mkombozi wa Israel | Israeli,kipofu na mfu | Ahadi ya Mungu ya Kuwaokoa watu wake | Mungu, mlinzi na mwokozi wa Israeli |
| 43:1-7 (1-7) | 43:1-7 (1-7) | 43:1-7 (1-7) | 43:1-5a (1-5a) | 43:1-7 (1-7) |
| | | | 43:5b-7 (5b-7) | |
| Israeli ni shahidi wa Mungu | | Mtumishi Israeli ni shahidi wa BWANA | Israeli ni shahidi wa BWANA | Yahweh pekee ni Mungu |
| 43:8-13 (8-13) | 43:8-13 (8-13) | 43:8-13 (8-13) | 43:8-9 (8-9) | 43:8-12a (8-12a) |
| | | | 43:10 (10) | |
| | | | 43:11-13 (11-13) | |
| | | | | 43:12b-13 (12b-13) |
| Babeli itaangamizwa | | Ukombozi na urejesho Wa Israeli | Kuokoka kutoka Babeli | Dhidi ya Babeli |
| 43:14-21 (14-21) | 43:14-15 (14-15) | 43:14-21 (14-21) | 43:14-15 (14-15) | 43:14-15 (14-15) |
| | | | | Miujiza ya safari mpya |
| | 43:16-21 (16-21) | | 43:16-17 (16-17) | 43:16-21 (16-21) |
| | | | 43:18-21 (18-21) | |
| Kushindwa kwa Israeli | Kumtetea Israeli asiye mwaminifu | | Uovu wa Israeli | Kutokushukuru kwa Israeli |
| 43:22-24 (22-24) | 43:22-24 (22-24) | 43:22-24 (22-24) | 43:22-25 (22-25) | 43:22-28 (22-28) |
| 43:25-28 (25-28) | 43:25-28 (25-28) | 43:25-28 (25-28) | | |
| | | | 43:26-28 (26-28) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

A. Israeli wana sehemu pekee kama watu wa maagano ya YHWH wamefunuliwa wazi katika mist. wa. 1-7.
   1. Aliwaumba, mist. 1,7
   2. Aliwakomboa, mst. 1
   3. Aliwaita kwa jina lake, mist . 1,7
   4. Aliwalinda ,mst. 2
   5. Yeye ni Mungu wa maagano yao, mst. 3
   6. Ni wa thamani mbele za macho yake, mst. 4
   7. Aliwaheshimu, mst. 4
   8. Aliwapenda, mst. 4
   9. Yuko pamoja nao, mst. 5

B. YHWH alitaka kuwatumia wao kujifunua mwenyewe kwa mataifa, mist. 8-10 (hasa mstari wa. 10c).

C. Aya ya 10d-f - 13 ni uthibitisho wa kipekee wa kithiolojia wa YHWH. Tazama mada maalum: Imani ya Mungu mmoja katika 40:14.

D. YHWH atawarudisha watu wake kutoka utumwani (mist. 5-6,14,16,19-20)
   1. Kupitia kwa Koreshi II
   2. Na mwishoni kupitia kwa Masihi

E. YHWH atawakomboa Israeli hata kama hawakustahili (kama vile. mist. 22-24).

F. YHWH kama mkombozi wa Israeli anasisitiza katika Sura hii (kama vile. mist. 1,3,11,14,25-26). Matendo YHWH kwa sababu yake na kwa ajiri ya makusudi yake. Israeli ni chombo cha thamani kwenye mkono wa Mungu kwa ajiri ya ukombozi wa ulimwengu.

G. Majina kwa ajiri ya Mungu yametumika katika Sura ya 43 (tazama mada maalum: Majina kwa ajiri ya Uungu katika 40:3)
   1. **"BWANA"** (mist. 1,3,11,14) YHWH – Jina la Agano kwa ajili ya Mungu (kama vile Kut. 3:14), "mimi," linatokana na KITENZI cha Kiebrania "kitenzi kisaidizi."
   2. **"Mungu"** (mst. 3; *"El* katika mst. 13) *Elohim* – hili ni neno la WINGI. Waalimu wa sheria ya Kiyahudi wanasema YHWH ni jina la Mungu kwa ajiri ya Rehema, ambapo *Elohim* linahusika na ulimwengu kwa ujumla (yaani., muumbaji,

Mmiliki ). Majina haya mawili kwa ajiri ya Mungu kwa sehemu kubwa katika Agano jipya ni ya kawaida.

3. **"Mtakatifu wa Israeli"** (mist. 3,15) – Cheo hiki kinaelezea utakatifu wa Mungu na usio kuwa na mipaka (tazama utambulisho, V, C na muhtasari katika 40:25).
4. **"Mwokozi"** (mist. 3,11,12) *Yasha* – hili linatokana na asili moja kama vile Yoshua na Yesu. Msingi wake unamaanisha "kuwa mkubwa" au "enye nafasi kubwa" (kama vile 19:20; 45:15,21; 49:26; 60:16; 63:8).
5. **"Mkombozi"** (mst. 14) – hili linatokana na asili moja kama *Go'el*, mkombozi mwenye uhusiano wa Damu au mlipa kisasi (kama vile. Ruth 4:4,6). Neno hili linamwelezea Mungu kama mkombozi wetu wa karibu wenye uhusiano wa Damu (kama vile 41:14; 44:6,24;47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16). Ni mfano mwingine wa uhusiano binafsi wa Mungu pamoja nasi. Mifano mingine ni Mungu kama Mzazi au Mme.
6. **"Muumbaji"** (mst. 15) – YHWH muumbaji (kama vile. 40:28) pia ni Agano maalum la Mungu wa Israeli. Hiki (KITENZI *bara*, kama vile. mst. 1)ni Dhamira ya kawaida (kama vile. Isaya 40-66).
7. **"Mfalme"** (mst. 15) –Mungu ni mfalme wa kweli wa Israeli. Inawezekana ni mfalme pekee kwa uwakilishi ulimwenguni (kama vile 1 Samweli 8).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:1-7**
**1 Lakini sasa, Bwana aliyekuhuluku, Ee Yakobo,**
**yeye aliyekuumba, Ee Israeli,**
**asema hivi, Usiogope, maana nimekukomboa;**
**nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu.**
**2 Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe;**
**na katika mito, haitakugharikisha;**
**uendapo katika moto, hutateketea;**
**wala mwali wa moto hautakuunguza.**
**3 Maana mimi ni Bwana, Mungu wako;**
**Mtakatifu wa Israeli, mwokozi wako,**
**nimetoa Misri kuwa ukombozi wako;**
**nimetoa Kushi na Seba kwa ajili yako.**
**4 Kwa kuwa ulikuwa wa thamani machoni pangu,**
**na mwenye kuheshimiwa, nami nimekupenda;**
**kwa sababu hiyo nitatoa watu kwa ajili yako; na kabila za watu kwa ajili ya maisha yako.**
**5 Usiogope; maana mimi ni pamoja nawe;**
**nitaleta wazao wako toka mashariki,**
**nitakukusanya toka magharibi;**
**6 nitaiambia kaskazi, Toa;**
**nayo kusi, Usizuie;**
**waleteni wana wangu kutoka mbali,**
**na binti zangu kutoka miisho ya dunia.**
**7 Kila mmoja aliyeitwa kwa jina langu,**
**niliyemwumba kwa ajili ya utukufu wangu;**
**mimi nimemwumba, naam, mimi nimemfanya.**

**43:1 "BWANA"** Hili ni kutoka katika neno YHWH. Katika Kut. 3:14 linatafsiriwa kama "Mimi." Muundo huu ni kutoka katika KITENZI cha Kiebrania "kitenzi kisaidizi." Tazama mada maalum katika 40:1.

◙**"aliyekuumba"** Hii ni *Qal* KAULI ENDELEVU (BDB 135, KB 153). Hii ni dhamira ya kawaida kupitia nyimbo za mtumishi. Hapa inarejelea kuimarika kwa taifa (yaani Mwa 12,15,22).

Mstari wa pili wa Sura ya 43 unafanana KITENZI "aliyekuumba" (BDB 427, KB 428, *Qal* KAULI ENDELEVU, kama vile. mstr. 21; 44:2,21,24). YHWH sio tu kwamba ni muumbaji wa ufalme unaoonekana lakini pia na watu wa maagano (kama vile. Mwa 12,15,18,22)

◙**"Ee Yakobo. . .Ee Israeli"** Hizi KAULI ZA MSEMAJI mbili zote zinarejelea kundi la watu wa maagano, uzao wa Ibrahimu.

◙**"usiogope"** Hii ni Amri (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika maana ya KITENZI AMRISHI). Hivyo basi mara kwa mara hili ni neno la Mungu kwa watu wake, hasa baada ya uhamisho na kuharibiwa kwa Yerusalemu na Hekalu (kama vile 40:9; 41:10,13,14; 44:2; 54:4).

◙**"nimekukomboa"** Tazama Mada Maalum katika 41:14.

◙**nimekuitakwajinalako"** Hii (zote "nimekukomboa" na "nimekuita" ni *Qal* KAULI ZA WAKATI TIMILIFU) inarejelea chaguo la Mungu kwa Israeli (kama vile. 7; 45:3-4). Huu ni wito maalumu kupitia kwa Ibrahim (kama vile. Mwa 12,15,18,22).

◙**"wewe u wangu"** Tazama mstr. 21 na Kut. 19:5-6. Israeli ni watu wa pekee wa YHWH.

**43:2 "maji. . .moto. . .mwali wa moto"** Hili ni Andiko la Ajabu sana! Hii imetumika kama sitiari ya matatizo ,hofu, na maadui!

◙**"nitakuwa pamoja nawe"** Hii ni ahadi kubwa sana ya Mungu (yaani., uwepo wake binafsi, kama vile. mstr, 5; Kumbt. 31:6,18;Zab. 23:4; Mt. 28:20).

◙**"wala mwali wa moto hautakuunguza "** kwa mfano mmojawapo,tazama Daniel 3.

**43:3 "Mwokozi"** maana ya msingi huu wa asili unaweza kutafsiriwa "Maana ya msingi ya mzizi huu inaweza kutafsiriwa kama "kuwa mkubwa" (BDB 446, KB 448). Majina ya Yoshua na Yesu msingi wake uko katika asili hii.

◙**ukombozi"** Hii inaongelea gharama kubwa ya kukombolewa (tazama mada maalum katika 41:14). Jambo linaloonekana katika aya ni ushindi wa Koreshi II.

**43:4** kunamfanano wa wazi kati ya

1. mstr. 3 – kukomboa kunakohusisha Misri,KushI, na Seba badala ya Israeli
2. mstr. 4 – kukomboa kunakohusisha
    a. Baadhi ya watu
    b. Baadhi ya kabila za watu

Toleo la UBS Text Project (uk. 111) linatupatia chaguo lingine (yaani., Ashuru. . .Edomu),ambalo linapatikana katika toleo la REB. Mabadiliko haya yanawezekana bila kubadilisha Konsonanti.hata hivyo, toleo la UBS linatathimini chaguo Namba1 kama A (mwelekeo wa juu zaidi).

Aya ya 3 na 4 ni Fasihi inayoonyesha njia ya YHWH kwa upendo mkubwa juu ya Israeli na mapenzi yake kwa ajiri ya ushindi wa majeshi ya Koreshi kuwahakikishia Irsaeli kurudi Palestina.

**43:5-7** Hii inaakisi kurejea kutoka Uhamishoni Babeli chini ya amri ya Koreshi II.

**43:7 "aliyeitwa. . .niliyemwumba. . .nimemwumba. . .nimemfanya"** Mungu ana makusudi kwa ajiri ya Israeli (kama vile. mstr. 10; Mwa. 12:1-3; Kut.19:5-6). Tazama mada maalum katika 40:15.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:8-13**
**8 Walete vipofu walio na macho, na viziwi walio na masikio.**

**[9]Na wakusanyike mataifa yote,**
**kabila zote wakutanike;**
**ni nani miongoni mwao awezaye kuhubiri neno hili,**
**na kutuonyesha mambo ya zamani?**
**Na walete mashahidi wao, wapate kuhesabiwa kuwa na haki;**
**au na wasikie, wakaseme, Ni kweli.**
**[10]Ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana,**
**na mtumishi niliyemchagua;**
**mpate kujua, na kuniamini, na kufahamu ya kuwa mimi ndiye;**
**kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote,**
**wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine.**
**[11]Mimi, naam, mimi, ni Bwana,**
**zaidi yangu mimi hapana mwokozi.**
**[12]Nimetangaza habari, nimeokoa, nimeonyesha,**
**na hapakuwa mungu wa kigeni kati yenu;**
**kwa sababu hiyo ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana,**
**nami ni Mungu.**
**[13]Naam, tangu siku ya leo, mimi ndiye;**
**wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu;**
**mimi nitatenda kazi, naye ni nani awezaye kuizuia?**

**43:8 "vipofu"** Hii ni kwa sababu ya kuendelea kutokuamini na kutokutii maagano (kama vile. 6:9-10 na 42:18-22).

**43:9** Kuna mfuatano wa *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU imetumika kama VITENZI AMRISHI (kama vile. Toleo la NRSV na NJB, "na. . .").

1. Na walete mashahidi wao (BDB 678, KB 733)
2. Na wapate kuhesabiwa haki (BDB 842, KB 1003)
3. Na wasikie (BDB 1033, KB 1570)
4. Na wakaseme (BDB 55, KB 65)

Mataifa, kama sanamu katika Sura ya 40, hawajui yajayo. Ni YHWH pekee ameshikilia Nyakati na historia katika mkono wake. Atatumia Israeli kujifunua mwenyewe na mwishoni atamtumia Masihi, mtumishi wake mwaminifu.

**43:10-13** Tambua njia nyingi za kipekee za YHWH, nguvu, na umilele umeelezwa .

1. Anawataka wanadamu, aliyewaumba kwa Sura yake, ili
   a. waelewe (BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
   b. waamini (BDB 52, KB 63, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
   c. wafahamu (BDB 106, KB 122, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)
2. Yeye ni Mungu pekee
   a. Mimi ndiye, mistr. 10,11,12,13
   b. Kabla yangu hakumbwa Mungu awaye yote mstr. 10
   c. Baada yangu mimi hatakuwepo mwingine, mst. 10
   d. Zaidi yangu mimi hapana mwokozi, mst. 11
3. Matendo yake (yote *Hiphil* KAULI TIMILIFU)
   a. Ameongea (BDB 616, KB 665)
   b. Anaokoa (BDB 446, KB 448)
   c. ametangaza (BDB 1033, KB 1570)
4. anatoka katika umilele, mst. 13a
5. nguvu zake , mst. 13b,c

Hizi ni kweli ambazo mataifa wanahitaji kuzijua na kuzithibitisha, mst . 9.

**43:10 "ninyi ni mashaidi wangu"** Hii ni sitiari kwa ajiri ya mandhari ya mahakama (kama vile mstr. 12; :18; 41:21; 44:8; Rum.8:31-38), amababapo mataifa yote yatakusanyika (kama vile mstr. 9).

◙**"kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote"** Hii inarejelea imani ya Mungu mmoja (kama vile mistr. 10-13, tazama mada maalum katika 40:14). Hii inaakisi katika Kut. 20:5.

**43:13 "milele"** Hii inafuata tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania . Toleo la MT lina "tangu siku."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:14-21**
**14Bwana, Mkombozi wenu, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi;**
**Kwa ajili yenu nimetuma ujumbe Babeli**
**nami nitawashusha wote mfano wa wakimbizi,**
**naam, Wakaldayo, katika merikebu zao walizozifurahia.**
**15Mimi ni Bwana, Mtakatifu wenu,**
**Muumba wa Israeli, mfalme wenu.**
**16Bwana asema hivi,**
**yeye afanyaye njia katika bahari;**
**na mahali pa kupita katika maji yenye nguvu;**
**17atoaye gari na farasi,**
**jeshi la askari na uwezo;**
**wamelala, hawataondoka;**
**wametoweka, wamezimwa mfano wa utambi.**
**18Msiyakumbuke mambo ya kwanza,**
**wala msiyatafakari mambo ya zamani.**
**19 Tazama, nitatenda neno jipya;**
**sasa litachipuka;**
**je! Hamtalijua sasa?**
**Nitafanya njia hata jangwani,**
**na mito ya maji nyikani.**
**20Wanyama wa kondeni wataniheshimu,**
**mbweha pia na mbuni;**
**kwa sababu nimewapa maji jangwani,**
**na mito nyikani,**
**ili kuwanywesha watu wangu, wateule wangu;**
**21watu wale niliojiumbia nafsi yangu,**
**ili wazitangaze sifa zangu.**

**43:14 "nami nitawashusha wote mfano wa wakimbizi"** Hii inarejelea kuanguka kwa Babeli chini ya Koreshi II. Sio nguvu za Koreshi ndizo zitakazo ipiga Babeli mpya lakini ni nguvu na makusudi ya YHWH (yaani, "kwa ajili yenu").

Inawezekana kuna batilisho la konsonanti ya Kiebrania.

1. "wakimbizi" (NASB, NKJV, NET Bible)
2. "mawakili" (JPSOA, NRSV, NJB, TEV)

◙**"Wakaldayo"** Herodotusi (450 k.k.), *Hist.* I,anatumia neno hili kurejelea kundi la kabila fulani (kama vile. 2 Fal. 24:1-4; Dan. 5:30) kama vile tabaka la kikuhani (kama vile Dan. 2:2; 3:8; 4:7; 5:7,11) ambao walitumika Enzi ya Koreshi II. Hata kabla ya wakati huo nyakati za Ashuru kumbukumbu zilitumia neno (BDB 505) katika maana ya kabila (kama vile R. K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, ukr. 1113). Pia soma mjadala bora wa uwezekano wa maneno mawili yanayofanana yanayochanganya (yaani., *Kal-du* dhidiya. *Kasdu*) katika *The Expositors BibleCommentary*,juzuu. 7,ukrs . 14-15 au Robert Dick Wilson, *Studies in the Book of Daniel*,mfuatano

wa 1.

Kwa sababu katika Mwa. 11:28 inaeleza kwamba Uru wa Wakaldayo ilikuwa ni makazi ya Tera na familia yake, labda Wakaldayo walikuwa ni kabila la kisemiti (yaani kikundi cha jamii moja kama Waebrania).

◙ Inawezekana kuna batilisho lingine la konsonanti ya Kiebrania.

1. Katika merikebu (NASB, NKJV)
2. Katika maombolezo (JPSOA, NRSV, NJB, TEV, REB, NET Bible)
3. Toleo la LXX lina "merikebu walizozifurahia"

Inawezekana kwamba mstr. 14 unaweza kuchukuliwa kama watu wa Babeli walifikilia wanaweza kuokoka dhidi ya jeshi la Uajemi kwa kutumia mto (yaani, Frati) kwa merikebu zao.

**43:15 "mfalme wenu"** Hii inawezekana ina muunganiko na 2 Samweli 7.

**43:16** Hii imetumika (1) Safari ya kutoka Misri (kama vile Mstr. 17; Kut 14-15) kama mfano kwa ajili kurudi kutoka Babeli au (2) YHWH anatawala dhoruba ya maji.

**43:19 "Nitafanya njia hata jangwani,"** Hii ni dhamira ya kawaida Kibiblia (kama vile. 40:1-4).

◙**"mito"** Hati ya kukunjwa kutoka katika Bahari ya Chumvi ina "njia" (REB).

**43:20** Badala ya laana (kama vile. Kumb 27-29) wanyama wa kondeni watakuwa sio wakali. Maua ya asili yatatoa nuru ya uwepo na Baraka za YHWH.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:22-24**
**22 Lakini hukuniita, Ee Yakobo,**
**bali umechoka nami, Ee Israeli.**
**23 Hukuniletea wana-kondoo kuwa kafara zako,**
**wala hukuniheshimu kwa dhabihu zako.**
**Sikukutumikisha kwa matoleo,**
**wala sikukuchosha kwa ubani.**
**24 Hukuninunulia manukato kwa fedha,**
**wala hukunishibisha kwa mafuta ya sadaka zako;**
**bali umenitumikisha kwa dhambi zako,**
**umenichosha kwa maovu yako.**

**43:22-24** Hii kwa ujumla sio shutuma za dhabihu lakini ni juu ya msukumo mwovu (kama vile. Yeremia 7). VITENZI vyote ni KAULI ZA WAKATI TIMILIFU ambavyo vinaonyesha mtazamo wa makazi ya Uasi.

**43:24 "manukato"** Hii inarejelea mafuta matakatifu (kama vile. Kut. 30:23; Yer. 6:20).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 43:25-28**
**25 Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe,**
**wala sitazikumbuka dhambi zako.**
**26 Unikumbushe, na tuhojiane;**
**eleza mambo yako, upate kupewa haki yako.**
**27 Baba yako wa kwanza alifanya dhambi,**
**na wakalimani wako wameniasi.**
**28 Kwa hiyo nitawatia unajisi wakuu wa patakatifu,**
**nami nitamfanya Yakobo kuwalaani, na Israeli kuwa tukano**

**43:25 "Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe" Msamaha** wa Mungu ni tendo la dhahiri, sio matendo mema (kama vile. 37:35; 48:9,11; Ezek. 36:22-38).

◙**"wala sitazikumbuka dhambi zako"** Munguanaposamehe, Mungu anasahau (kama vile. 1:18; 38:17; 44:22; Zab.103:12; Mika 7:19). Haja ya ukweli katika haki ya shetani ni kuendeleza shutuma! Ohoo Neema na Rehema za Mungu!

## MADA MAALUM: MANENO YA MSAMAHA

Hapa pana maneno mengi ya Kiebrania au nahau ambazo zinaelezea msamaha wa Kiungu wa dhambi na uasi wa mwanadamu.

1. "samehe," "samehe," (סלח– BDB 699, KB 757, yaani, Kut. 34:9; Law. 4:20, 26, 31, 35; 5:10,13, 16, 18; 6:7; 19:22; Hes. 14:20; 15:25-28; 30:5,8,12; I Fal. 8:30, 34, 36, 39, 50; Zab. 25:11;103:3; Isa. 55:7; Dan. 9:19; Amosi 7:2 (neno hili mara zote linatumika kumhusu Mungu, na kamwe si wanadamu)
2. "nifute," "ondoa," נשׂא(ni KITENZI kilichozoeleka kikiwa na maana nyingi) – BDB 669, KB 724,yaani., Kut. 23:21; 32:32; 34:7; Hes. 14:18; Yosh. 24:19; Zab. 25:18; 32:1,5; 85:2; 99:8; Mika7:18
3. "funika," "lipia kosa," כפר, – BDB 497, KB 493, yaani., ni cha kawaida katika kitabu cha Walawi; Zab. 65:3; 78:38;79:9; Isa. 6:7; 22:14; Yer. 18:23; Ezek. 16:63; Dan. 9:24
4. "ondoa," "futa,"מחה– BDB 562, KB 567, yaani, Neh. 4:5; Zab. 51:1,9; Isa. 43:25; 44:22; Yer. 18:23
5. "ponya," רפא– BDB 950, KB 1272, yaani., II Nya. 7:14; Zab. 41:4; 103:3; Isa. 6:10; 57:18; Yer.3:22; 17:14; 30:17; Hosea 5:13; 14:4
6. "kutokuwapita kamwe," עבר– BDB 716, KB 778, yaani., Mith. 19:11; Amosi 7:8; 8:2; Mika 7:18
7. "osha," כבס, – BDB 460, KB 459, yaani, Zab. 51:2,7; Yer. 2:22; 4:14
8. "jitakase," טהר– BDB 372, KB 369, yaani., Law. 16:30; Zab. 51:7; Mith. 20:9; Ezek. 24:13; 36:25
9. "umezitupa dhambi zote nyuma yako," שׁלד– BDB 1020, KB 1527, yaani., Isa. 38:17; Mika 7:19
10. "unisafishe," חטא– BDB 306, KB 305, yaani., Zab. 51:7 (kidokezo hiki cha kujisafisha Kiungu cha KITENZI kilichozoeleka, kinapatikana hapa tu)
11. "sitiri uso wako," סתר– BDB 711, KB 771, yaani., Zab. 51:9
12. "kumbuka" (kinyume), זכר,' – BDB 269, KB 269, yaani., Isa. 43:25

"kuyakanyaga" (kifasihi "jizuie"), כבשׁ, – BDB 461, KB 460, yaani., Mika 7:19

**43:26 "Tuhojiane"** Hii inaakisi sitiari halali ya chumba cha mahakama (kama vile. 1:18; 41:21; Rum. 8:31-38). Aya hii ina mfuatano wa amri za hakimu.

1. unikumbushe – BDB 269, KB 269, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. tuhojiane – BDB 1047, KB 1627, *Niphal* HALI YA KUSIHI
3. eleza mambo yako – BDB 707, KB 765, *Piel* KAULI SHURUTISHI

**43:27 "Baba yako wa kwanza alifanya dhambi"** kiuhalisia ni "Baba."inaweza kurejelea kwa Adamu au Yakobo au Myahudi yeyote yule wa kale. Inaonyesha kwamba upendo wa Mungu unastahimili. Agano la kale halikukaa kwenye dhambi ya asili, lakini katika ufahamu wake wa uwepo na kusambaa pote. Baadhi ya waalimu wa sheria ya Kiyahudi, kama vile Paulo, anatilia mkazo Mwa 3, lakini wengine wanatilia mkazo Mwa 6.

◙**"wakalimani"** Hii labda inarejelea

1. manabii
2. makuhani
3. wanasiasa

**43:28 "Kwa hiyo nitawatia unajisi wakuu wa patakatifu,"** KITENZI hiki "unajisi" (BDB 320 III, KB 319, *Piel* KAULI WA WAKATI USIO TIMILIFU) ni sawa na "kupenya" (BDB 318, kama vile 2 Fal. 25:18-27). Toleo la NEB na

REB kidogo inabadili konsonanti ya Kiebrania kwenda “wakuu wako wemekufuru patakatifu pangu”, inayofuata toleo la LXX.
VITENZI viwili kwa vyovyote vinatia shaka katika mst. 28 vinarejelea wakati wa uliopita au wakati ujao. Andiko la Kiebrania lina muunganiko na Aya ya 27 na 28. Aya ya 28 ni dhahili inarejelea wakati uliopita. Kwa ujumla Sura ya 43 inahusika na ukombozi wa sasa wa YHWH kwa Israeli kutoka uhamishoni. NJEO ya Kiebrania hatupatii muda , bali matendo; muda ni lazima uhakikishwe kutoka kwenye muktadha.

◙**“kuwalaani”** Hii ni kutoka katika neno *herem* (BDB 356). Kitu kama “patakatifu,” hivyo lisilowezekana kwa anguko la binadamu,hivyo basi, ni lazima iangamizwe. Na mfano utakuwa ni Yeriko ( kama vile. Yoshua 6).

# ISAYA 44:1-23

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Baraka za Israeli | Baraka za Mungu wa Israeli | Yeshuruni | Bwana ndiye Mungu pekee | Baraka zilizohifadhiwa kwa ajili ya Israeli |
| 44:1-5<br>(2-5) | 44:1-5<br>(2-5) | 44:1-5<br>(1-5) | 44:1-5<br>(1-5) | 44:1-5<br>(1-5) |
| | Hapana Mungu Mwingine | Upekee wa Mungu | | Yupo Mungu mmoja tu |
| 44:9-17 | 44:9-11<br>(9-11) | 44:9-11 | 44:9-11 | 44:9-11 |
| | 44:12<br>(12) | 44:12-17 | 44:12 | 44:12 |
| | 44:13-14<br>(13-14) | | 44:13-17 | 44:13-17 |
| | 44:15-17<br>(15-17) | | | |
| 44:18-20 | 44:18-20<br>(18-20) | 44:18-20 | 44:18-19 | 44:18-19 |
| | | | 44:20 | 44:20 |
| Mungu husamehe Na kuokoa | Israeli haijasahaulika | Israeli imesamehewa na kukombolewa | Bwana, Muumbaji, na Mwokozi | Utii kwa YHWH |
| 44:21-23<br>(21-23) | 44:21-22<br>(21-22) | 44:21-22<br>(21-22) | 44:21-22<br>(21-22) | 44:21-23<br>(21-13) |
| | 44:23<br>(23) | 44:23<br>(23) | 44:23<br>(23) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni<u>mwongozo</u>kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:1-5**
**1 Lakini sikia sasa, Ee Yakobo, mtumishi wangu;**
**na Israeli, niliyekuchagua;**
**2 Bwana, aliyekufanya,**
**na kukuumba toka tumboni,**
**yeye atakayekusaidia, asema hivi;**
**Usiogope, Ee Yakobo, mtumishi wangu;**
**na wewe, Yeshuruni, niliyekuchagua.**
**3 Kwa maana nitamimina maji juu yake aliye na kiu,**
**na vijito vya maji juu ya mahali pakavu;**
**nitamwaga roho yangu juu ya wazao wako,**
**na baraka yangu juu yao utakaowazaa;**
**4 nao watatokea katika manyasi,**
**kama mierebi karibu na mifereji ya maji.**
**5 Mmoja atasema, Mimi ni wa Bwana;**
**na mwingine atajiita kwa jina la Yakobo;**
**na mwingine ataandika juu ya mkono wake,**
**Kwa Bwana, na kujiita kwa jina la Israeli.**

**44:1 "sikia sasa"** Hii ni KAULI SHURUTISHI (BDB 1033, KB 1570) inayoainisha mafunuo mengi katika kitabu cha Isaya (kama vile 1:2,10; 6:8,9,10; 7:13; 28:14; 32:9; 33:13; 34:1; 36:13; 39:5; 42:18; 46:3,12; 47:8; 48:1,12,14, 16; 51:1,7,21; 55:2,3; 59:1; 66:5).
Neno linamaanisha "kusikia kwa ajili ya kutenda." Likajakuwa jina ( *Shema*) la maombi maarufu ya Kiyahudi katika Kumb. 6:4-5.

◙**"Ee Yakobo, Mtumishi wangu"** Tambua ufanano uliopo kati ya mstari wa 1 na 2. YHWH alikuwa akiielezea Israeli yenye ushirikiano.

◙**"niliyekuchagua"** YHWH
1. Ameichagua Israeli, mistari ya 1,2
2. ameifanya Israeli, mst. 2
3. Kuiumba Israeli, mst. 2
4. kuisaidia Israeli, mst. 2

**44:2** Tambua ufanano uliopo kati ya mstari wa 1 na 2.
1. "nimekufanya" – BDB 793, KB 889, *Qal* KAULI ENDELEVU, mstari wa 1
2. "amekuumba" – BDB 427, KB 428, *Qal* KAULI ENDELEVU, mstari wa 2

Kuna maneno mbalimbali ya Kiebrania yaliyotumika kuyaelezea matendo ya kiubunifu ya YHWH.

◙**"Usiogope"** Kifungu hiki (BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU iliyotumika kwa maana ya KUAMRISHA) mara nyingi inatumika katika sura hizi 40-66 (kama vile 40:9; 41:10,13,14; 43:1,5; 44:2; 51:7; 54:4,14; 57:11).
Hawakustahili kuogopa kwa sababu
1. Walikuwa watu wa Mungu
2. Alikuwa nao
3. Adhabu yao ilishakwisha
4. Angaliwapatia vyote walivyohitaji

◙**"Yeshuruni"** Hili (BDB 449) lilikuwa ni jina adimu kwa ajili ya Waisraeli likimaanisha "yeye aliyemwaminifu"

(kama vile Kumb. 32:15; 33:5,26). Linafanana na lile "Ee Yakobo Mtumishi wangu."

◙**"nitamimina"** KITENZI hiki (BDB 427, KB 428, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU) mara nyingi hutumika kuhusiana na utiwaji mafuta au utoaji dhabihu. Katika aya hii kimejirudia mara mbili.

1. mara moja kwa ajili ya miujiza ya kuwepo maji
2. mara moja kwa ajili ya Roho (kama vile. [1] 32:15, neno tofauti [BDB 788]; [2] Yoeli 2:28, neno tofauti [BDB 1049])

YHWH ni chanzo cha baraka na kwa ajili ya watu wa jangwani maji yalikuwa alama ya uhai na utosherevu (kama vile mst. 4).

◙**"juu ya wazao wako"** Baraka, kama ilivyo laana, ilitembea ndani ya familia (kama vile Kumb. 5:9-10; 7:9). Hivi vizazi vijavyo vitajijua vyenyewe ni nani ndani ya YHWH na kufurahia ndani yake (mst. 5).

**44:5** Swali la kimuktadha ni kwa nani hii aya inamrejerea.

1. Kizazi cha Ibrahimu chenye kujivuna
2. Wageni waliodai na kumsifu Mungu wa Israeli (kama vile 56:3-6)

KITENZI "kuita" (BDB 894, KB 1128, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU) kinatafasiriwa

1. KAULI YA KUTENDWA katika lugha ya Kiaramu Targums, "ataitwa"
2. KAULI YENYE KUJIREJEA (*Niphal*) katika toleo la LXX na Peshitta, "atajiita"
3. KAULI TENDAJI katika Kiebrania, "utaitwa" (yaani., tendo la kuabudu)

Inanionyesha mimi toka kwenye muktadha wa dhana ya ufanano wa mistari ya 2 na 3 kuwa inazungumzia juu ya wageni. Kama ndivyo basi, hivyo haya ni moja ya yale maandiko ambayo yanawahakikishia wasio Wayahudi kumfikia Mungu mmoja wa kweli! Sio tu mtumishi ambaye ni nuru ya mataifa, bali mwokozi wa mataifa! Andiko la Mwanzo 3:15 linatimilika, vile vile pia 12:3!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:6-8**
**6 Bwana, Mfalme wa Israeli, Mkombozi wako, Bwana wa majeshi, asema hivi;**
**Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho;**
**zaidi yangu mimi hapana Mungu.**
**7 Naye ni nani kama mimi atakayeita,**
**na kuyahubiri haya, na kunitengenezea, tangu nilipowaweka watu wa kale?**
**Na mambo yanayokuja na yatakayotokea, wayatangaze.**
**8 Msiogope wala msifanye hofu;**
**je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha?**
**Na ninyi ni mashahidi wangu. Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi?**
**Hakika hapana Mwamba;**
**mimi sijui mwingine.**

**44:6** Tambua majina yalitotumika kwa ajili ya Mungu katika muktadha huu (yaliyo sawa na yale ya 43:3,15).

1. Bwana (YHWH)
2. Mfalme wa Isareli
3. Mwokozi (BDB 145 I, kama vile 41:14)
4. Bwana wa Majeshi
5. Mimi ni wa kwanza na wa mwisho (kama vile 41:4; 43:10; 48:12; Ufu. 1:8,17; 22:13)
6. Mungu (*Elohim*)
7. Mwamba, mst. 8 (kama vile 17:10; 26:4; 30:29; Zab. 18:2)

Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 40:3.

Majina haya yanasisitiza upekee, umilele, uaminifu, na nguvu ya Mungu wa Israeli.

◙**"hakuna Mungu mwingine zaidi yangu"** Huu ni uthibitisho wa kipekee na imani ya Mungu mmoja. Angalia Mada Maalum katika 40:14. Hii ni dhana inayojirudia katika Isaya.

**44:7 "mambo yanayokuja na yanayotokea, wayatangaze"** Hili tena ni dokezo kwenye mandhari ya baraza. YHWH anapingana na sanamu kuthibitisha uwepo na nguvu zao lakini hazitaweza (kama vile Isa. 41:21-24; 43:8-9). Haziwezi kutabiri mambo yajayo.
Tambua idadi ya matamko yaliyotolewa kwa miungu ya uongo (sanamu za mataifa).

1. tangaza – BDB 894, KB 1128, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI
2. tamka – BDB 616, KB 615, *Hiphil* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI
3. hesabu – BDB 789, KB 884, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI
4. tamka – ni kama mstari wa #2

**44:8** Kwa namna ya udhaifu wa miungu ya uongo ya mataifa, Israeli haihitaji

1. kutetemeka – BDB 808, KB 922, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI
2. kuogopa – BDB 923 (רהה), KB 437 (ירה), *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI (ikiwa na asili tofauti toka mst. 2)

◙**"ninyi ni mashahidi wangu"** YHWH alikuwa na kusudi maalumu la kimafunuo kwa ajili ya watumishi /mtumishi wake.

◙**"mimi sijui mwingine"** YHWH anajijibu maswali yake Mwenyewe. KITENZI ni *Qal* KAULI TIMILIFU; hapana miungu mingine ila Mimi tu (angalia Mada Maalum katika 40:14).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:9-11**
**9 Wachongao sanamu, wote ni ubatili; wala mambo yao yawapendezayo hayatafaa kitu; wala mashahidi wao wenyewe hawaoni, wala hawajui; ili watahayarike. 10 Ni nani aliyejichongea mungu mmoja, au aliyesubu sanamu isiyofaa kitu? 11 Tazama, wenziwe wote watatahayari; na mafundi, hao ni wanadamu; na wakusanyike pamoja, wakasimame; wataogopa na kutahayari pamoja.**

**44:9-20** Hiki ni kipengele cha lugha ya mjazo kinachoshughulika na ujinga wa kuiabudu sanamu (kama vile Yer. 10:2-16).

**44:9**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ubatili"** |
| **NKJV** | **"isiofaa"** |
| **NRSV** | **"si kitu"** |
| **TEV** | **"isio na thamni"** |
| **NJB** | **"isio na maana"** |

Hili ni neno la Kiebrania (BDB 1062) linalotafasiliwa kama "utupu" katika Mwa. 1:2; "ukiwa" katika Isa. 34:11; na "utupu" katika 41:29. Hapa linaonesha utupu.

**44:11** Kuna mlolongo wa KAULI ZISIZO TIMILIFU zikitumika kama AMRISHI zikielezea alama za miungu ya sanamu na wamwabuduo.

1. wakakusanyike pamoja – BDB 867, KB 1062, *Hithpael* KAULI ISIO TIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI
2. wakasimame – BDB 763, KB 840, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI
3. wataogopa – BDB 808, KB 922, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI
4. watahayari pamoja – BDB 101, KB 116, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU ikitumika kwa maana ya KAULI AMRISHI

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:12-17**
**[12] Mfua chuma hufanza shoka, hufanya kazi kwa makaa, huitengeneza sanamu kwa nyundo, huifanyiza kwa nguvu za mkono wake; naam, huona njaa, nguvu zake zikampungukia; asipokunywa maji huzimia. [13] Seremala hunyosha uzi; huiandika kwa kalamu ya mate; huitengeneza kwa randa, huiandika kwa bikari, huifanza kwa mfano wa mwanadamu, sawasawa na uzuri wa mwanadamu, ili ikae nyumbani. [14] Yeye hujikatia mierezi, hutwaa mtiriza, na mwaloni, hujichagulia mti mmoja katika miti ya msituni; hupanda mvinje, mvua ikausitawisha. [15] Kisha utamfaa mwanadamu kwa kuni; hutwaa kipande, akaota moto; naam, huuwasha moto, akaoka mkate; naam, huufanya mungu, akauabudu; huifanya sanamu ya kuchonga, akaisujudia. [16] Sehemu moja huiteketeza; kwa sehemu nyingine hula nyama; huoka chakula kiokwacho, akashiba; naam, huota moto, akasema, Aha, nimeota moto, nimeona moto; [17] na kwa sehemu iliyobakia hufanya mungu, yaani, sanamu yake ya kuchonga; husujudu mbele yake akaiabudu, akaiomba, akasema, Uniokoe; maana wewe u mungu wangu.**

**44:14-20** Hii inaonyesha ujinga wa ibada ya sanamu (kama vile Yer. 10:2-16).
1. Hupanda mvinje
2. Hujikatia kwa ajili ya
   a. kuota moto
   b. kupikia chakula
   c. kuchongea vinyago
3. Husujudu mbele yake akaiabudu, sehemu ya mti uliobaki. Akaiomba, akasema uniokoe!
4. Mtengenezaji husahau maandalizi yote kwa sababu amejidanganya mwenyewe (mst. 20)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):44:18-20**
**[18] Hawajui wala hawafikiri; maana amewafumba macho, wasione, na mioyo yao, wasiweze kufahamu. [19] Wala hapana atiaye moyoni, wala hapana maarifa, wala fahamu kusema, Nimeteketeza sehemu motoni, naam, pia nimeoka mkate juu ya makaa yake; nimeoka nyama nikaila; nami, je! Kilichobaki nikifanye kuwa chukizo? Je! Nisujudie shina la mti? [20] Hula majivu; moyo uliodanganyika umempotosha, asiweze kuiokoa nafsi yake, wala kusema, Je! Sio uongo mkononi mwangu?**

**44:18** Kutokuamini na ushirikina ni matokeo ya
1. Anguko
2. Mkono wa YHWH?

Agano la Kale linahusianisha visababishi vyote na Mungu (yaani., Farao, pia kumbuka 6:9-10; 29:10), lakini bado mwanadamu anahusika kwa ajili ya matendo yao. Hili ni fumbo la Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu (yaani., umuhimu wa matendo ya mwanadamu kwa ajili ya msamha wa Mungu, kama vile 55:7). Huenda Zaburi 81:12 ikahitimisha vizuri (kama vile Rum.1:24,26,28)

## MADA MAALUM: UCHAGUZI/MAAMUZI YA KABLA NA HITAJI LA USAWA WA KITHIOLOJIA

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hivyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile.Warumi10:11,13).

Umuhimu wa huu muvatano wa kitheolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya

mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milelel!
Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu
2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. udhihilisho na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhumu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kitheolojiaya “agano” inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu(k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maanddishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maneneo na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa thiolojia!

**44:19 “ni chukizo”** Angalia Mada Maalum: Chukizo katika 41:24.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:21-23**
**21 Kumbuka haya, Ee Yakobo;**
**nawe Israeli, maana wewe u mtumishi wangu;**
**nimekuumba; u mtumishi wangu;**
**Ee Israeli, hutasahauliwa na mimi.**
**22 Nimeyafuta makosa yako kama wingu zito,**
**na dhambi zako kama wingu; unirudie;**
**maana nimekukomboa.**
**23 Imbeni, enyi mbingu, maana Bwana ametenda hayo;**
**Pigeni kelele, enyi mabonde ya nchi;**
**Pazeni nyimbo, enyi milima;**
**Nawe, msitu, na kila mti ndani yake.**
**Maana Bwana amemkomboa Yakobo,**
**Naye atajitukuza katika Israeli.**

**44:21-23** Kwa namna ya mashahidi wa uongo waiabuduyo sanamu, ushahidi wa kweli wa watu wa YHWH ni wa muhimu! Wanalazimishwa

1. kukumbuka, mst. 21 – BDB 269, KB 269, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. kurudi, mst. 22 – BDB 996, KB 1427, *Qal* KAULI SHURUTISHI

Uumbaji wa YHWH pia unatakiwa kushuhudia

1. Imbeni kwa furaha, enyi mbingu, mst. 23 – BDB 943, KB 1247, *Qal* KAULI SHURUTISHI
2. Pigeni kelele enyi mabonde ya nchi, mst. 23 – BDB 929, KB 1206, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
3. Pazeni nyimbo enyi milima na misitu, mst. 23 – BDB 822 KB 953, *Qal* KAULI SHURUTISHI

Ni jambo la kinyume kuwa watengeza sanamu huchoma na kutengeneza sanamu, lakini miti hufurahia ukombozi wa YHWH na ushuhuda wa Israeli kwa utukufu wake.

**44:21**
**NASB, NKJV,**
**NRSV** **“hautasahauliwa na Mimi”**
**REB, LXX,**
**Peshitta,**
**JPSOA** **“kamwe sintakusahau”**
Tofauti iko kwenye kauli ya mnenaji tu. Toleo la UBS linatoa uchaguzi wa #1 (NASB) alama “C” (pasipo mashaka).

**44:22** Hii ni ahadi nyingine kubwa ya ajabu ya msamaha kamili. KITENZI “niyafutaye” (BDB 562, KB 567, *Qal* KAULI TIMILIFU) pia kimetumika katika 43:25; Zab. 51:3,11. Mungu akisamehe, husahau (kama vile 1:18; 38:17; 43:25; 44:22; Mika 7:19).
Misingi kamili ya uondoaji wa makosa yetu ni
1. Ukombozi waYHWH
2. Toba ya muumini

## MADA MAALUM: TOBA (AGANO LA KALE)

Dhana hii ni ya muhimu sana lakini ni vigumu kuitolea ufafanuzi. Wengi wetu tunao ufafanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufafanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) amabayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekea" ufafanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.
1. *nacham* ( BDB 636, KB 688)
2. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.
a. "kupunzika" au "kufariji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
b. "kuhuzuka" (m.f. Mwa. 6:6,7)
c. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Num. 23:19; Ayubu 42:5-6)
d. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa
1. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4

2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hiii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kupitia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipya inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inaweza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nacham* linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi's sin with Bathsheba (kama vile 2 Samuel 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahiajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejesha ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

**44:23**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"mabonde ya nchi"** |
| **NRSV, JPSOA** | **"vina vya nchi"** |
| **TEV** | **"sehemu zilizoko chini ya nchi"** |
| **NJB** | **"mabonde ya nchi"** |
| **LXX, Peshitta** | **"misingi ya nchi"** |

Inavyoonekana hii inarejerea *Sheol* (BDB 982).

## MADA MAALUMU: WALIOKUFA, WAKO WAPI? *(SHEOL/HADES, GEHENNA, TARTARUS*

I. Agano la Kale
   A. Watu wote wanakwenda shimoni (*sheol)* (hakuna mizizi yenye chanzo kimoja cha neno na asili ya neno lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)
   B. Tabia za shimoni (*sheol*)
      1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), kumb.32:22

2. Gereza lenye vizuizi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
7. panahusiana na *utelekezaj*i (maangamizo; angalia Mada Maalumu: *Kutelekezwa*. . .*Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
8. panahusiana na “shimo lefu” (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
9. waovu hushuka ndani ya shimo la *sheol*,Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5
11. kule watu huitwa *Repha'im* (yaani., "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11

II. Agano Jipya

A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usioonekana)

B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheo*l)

1. inarejerea mauti, Mt. 16:18
2. imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14
3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (Gehenna), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Luk 10:15; 16:23-24
4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Luk 16:23

C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)

1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Luk 23:43
2. Sehemu ya waovu iitwayo “kwenye vifungo vya giza”,iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa “shimoni” Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3

*D. Gehenna*

1. inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, “bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalem). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YWHW (Kama vile Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.
3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza,kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna
   a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk 9:43
   b. Mahali pa milele, Mk 9:48 (Mt. 25:46)
   c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28
   d. panafanana na *Sheol,* Mt. 5:29-30; 18:9
   e. Panaainisha waovu kama “wana wa Jehanamu” Mt. 23:15
   f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
   g. Dhana ya Gehenna inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8).Yawezekana ziwa la moto pakawa

ndo mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimoni, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimoni, kama vile Luk 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).

h. ilikuwa haikusanifiwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41

E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimoni (*sheol),* kuzimu(*hades)* na Jehanamu(*Gehenna*) kuwa

1. kiasili watu wote walikwenda shimoni/kuzimu
2. uzoefu wao wa (mema/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezewa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawezi kutengeneza andiko juu ya mfano.

III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

A. Agano jipya halifundishi juu ya "zinaa ya nafsi," ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa

1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili
3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla

B. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo

1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
2. Ibrahamu angeweza tayari kuwa na mwili, Mk 12:26-27; Luk 16:23
3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mipya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
6. Paulo anadai kuwa waumini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

IV. Mbinguni

A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.

1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Heb. 4:14; 7:26
3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Heb. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)

B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).

C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msemo (mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafahamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia

A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*

B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

# ISAYA 44:24-45:25

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| | Yuda itarejeshwa | Kuagizwa kwa Koreshi (44:24-45:13) | | Mungu, muumba wa Ulimwengu na BWANA wa Historia |
| 44:24-28 (21-28) | 44:24-28 (24-28) | 44:24-28 (24-28) | 44:24-28 (24-28) | 44:24-28 (24-28) |
| Mungu anamtumia Koreshi | Koreshi,Chombo cha Mungu | Kuagizwa kwa Koreshi (44:24-45:13) | BWANA anamteua Koreshi | Koreshi, chombo cha Mungu |
| 45:1-7 (1-7) | 45:1-7 (1-7) | 45:1-4 (1-4) | 45:1-4 (1-4) | 45:1-7 (1-7) |
| Mamlaka ya mwisho Ya Mungu (5-7) | (5-8) | 45:5-7 | 45:5-8 | Maombi |
| 45:8 (8) | 45:8 (8) | 45:8 (8) | | 45:8 (8) |
| | | | BWANA wa Uuumbaji Na Historia | Nguvu ya Juu ya Yahweh |
| 45:9-10 (9-10) | 45:9-10 (9-10) | 45:9-13 | 45:9-13 (9-13) | 45:9-13 (9-13) |
| 45:11-13 (11-13) | 45:11-13 (11-13) | | | |
| | BWANA,mwokozi pekee | Kuongoka kwa mataifa | | Kuongolewa kwa Mataifa |
| 45:14-17 (14-17) | 45:14 (14) | 45:14-17 (14-17) | 45:14-17 (14-17) | 45:14-19 (14-19) |
| | 45:15-17 (15-17) | | | |
| 45:18-19 (19) | 45:18-19 (18-19) | 45:18-19 (18-19) | 45:18-19 (18-19) | |
| | | | BWANA wa Ulimwengu Na sanamu za Babeli | Mungu, BWANA wa ulimwengu wote |
| 45:20-25 | 45:20-21 | 45:20-21 | 45:20-21 | 45:20-25 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (20-25) | (20-21) | (20-21) | (20-21) | (20-25) |
| 45:22-25 | 45:22-23 | 45:22-23 | | |
| | (22-25) | (22-23) | (22-23) | |
| 45:24-25 | | 45:24-25 | | |
| | | (24-25) | (24-25) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia ukr. wa xvi na kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu.
Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA ISAYA 44:24-45:25

A. Huu ni unabii bayana sana. Koreshi II, pia akijulikana kama Koreshi Mkuu, anatajwa kwa jina katika 44:28 na 45:1. Kwa wale wanaokataa uwezekano wa unabii juu ya mambo yanayoweza kutokea baadaye ni ushahidi mkuu katika 41:22-23; 44:7,26), Huu ni msukumo mkubwa kwa nadharia ya uandishi wa waytu kadhaa wa Isaya. Ninaamini kwamba Isaya kimeandikwa na mwandishi mmoja tu na kwamba Mungu si tu kwamba alifunua mambo ya siku zijazo za ufalme wa Ashuru bali pia na wa Wababeli na Waajemi kupitia nabii huyu wa karne hii ya 8 K.K .
B. Hii rejea haswa kwa Koreshi inahusika na tangazo la mnamo 538 K.K. ambalo liliruhusu watu wote wa uhamishoni kurudi katika maeneo yao ya asili na kujenga mahekalu yao ya kitaifa kwa msaada wa hazina ya Uajemi. Kwa ajili ya rejea dhahiri juu ya kurudi kwa Wayahudi angalia Ezra 1:2-4; 6:3-5. Kisababishi cha msingi kwa ajili ya hili ilikuwa kwa ajili ya kila taifa kuomba kwa mungu wao kwa niaba yake na mtawala ayakayekuja nyuma yake (kama vile Ezra 6:10; 7:23).
C. Nafikiri kwamba Isaya 45:6 ni muhimu kupitiliza. Inaonesha tena si tu kwamba kusudi la Mungu kuchagua Israeli lakini pia Mungu kumchagua Koreshi. Mungu alimchagua Ibrahimu ili kuchagua ulimwengu na alichagua Koreshi kwa ajili ya kusudi hilo hilo.
D. Tazama ni mara ngapi maneno tofauti kwa ajili ya kuumba yametumika.
    1. BDB 427, KB 428 – kutengeneza, kuumba, 44:24; 45:7,9 (mara mbili), 18 (mara mbili)
    2. BDB 793, KB 889 – kufanya, kufanya, 44:24; 45:7,9,11,18
    3. BDB 135, KB 153 – kuumba, 45:7 (mara mbili), 8,12,18 (mara mbili)

Msisitizo wa kithiolojia wa hiki kipengele cha “zama mpya” ni

a. YHWH pekee ndiye aliyeumba kila kitu
b. YHWH aliumba Israeli
c. YHWH ndiye pekee na wa aina yake (imani kwa Mungu mmoja)
d. YHWH anathibitisha uwepo wake kwa
    i. utabiri wake wa mambo yajayo
    ii. uwepo wa Israeli

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

| ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 44:24-28 |
|---|
| **24Bwana, mkombozi wako, yeye aliyekuumba tumboni, asema hivi;<br>Mimi ni Bwana, nifanyaye vitu vyote;<br>nizitandaye mbingu peke yangu;<br>niienezaye nchi; ni nani aliye pamoja nami?<br>25Nizitanguaye ishara za waongo,<br>na kuwatia waganga wazimu;<br>niwarudishaye nyuma wenye hekima,<br>na kuyageuza maarifa yao kuwa ujinga;<br>26 nilithibitishaye neno la mtumishi wangu,<br>na kuyafikiliza mashauri ya wajumbe wangu;<br>niuambiaye Yerusalemu, Utakaliwa na watu,<br>nayo miji ya Yuda, Itajengwa,<br>nami nitapainua mahali pake palipobomoka;<br>27niviambiaye vilindi, Kauka, nami nitaikausha mito yako;<br>28nimwambiaye Koreshi, Mchungaji wangu,<br>naye atayatenda mapenzi yangu;<br>hata ataunena Yerusalemu, Utajengwa;<br>na hilo hekalu, Msingi wako utawekwa.** |

**44:24-28** Hii ni sentensi moja kwa Kiebrania. Ni mfuatano wa tungo rejeshi ambazo zinafasiriwa kwa NIV kama "ambaye. . ." Ni muhimu kwamba kipengele hiki cha muundo huu ni kwasababu ya kilele kinachopatikana katika kutajwa kwa jina la Koreshi kwa jina katika mstari wa 28. Kimsingi ni kipengele cha kushughulikia "Mungu awezaye" dhidi ya sanamu zisizoweza. YHWH anatangaza kabla kitu gani kitatokea kuthibitisha uwepo wake na nguvu (kama vile 41:22-23; 44:7,26).

Tazama orodha ya "ambaye. . ." katika NIV (yaani, *Qal* KAULI ENDELEVU).

1. aliyekuumba katika tumbo, mstari wa 24
2. aliyevifanya vitu vyote, mstari wa 24
3. yeye pekee aliyezitandaza mbingu, mstari wa 24
4. ambaye aliyeitandaza nchi yeye Mwenyewe, mstari 24
5. yeye avurugaye miujiza ya manabii wa uongo, mstari 25
6. yeye apinduaye elimu ya wenye hekima., mstari wa 25
7. yeye apelekaye maneno ya watumishi wake, mstari wa 25
8. yeye auambiaye Yerusalemu, "itakaliwa" mstari wa. 25
9. yeye auambiaye maji ya kina, "kauka" mstari wa 27
10. yeye amwambiaye Koreshi, "yeye ni mchungaji wangu" mstari wa 28

**44:24 "Mkombozi"** Hili neno Go'el, ambalo lina maana ile ile kama "fidia" ikiwa na nyongeza la wazo la ndugu wa karibu kama wakala. Mara kwa mara ni jina kwa ajili ya Mungu. Angalia Mada maalum katika 41:14 na dokezo katika 43:14.

◙**"yeye aliyekuumba tumboni"** Hii kimsingi inarejerea kutengenezwa kwa taifa la Israeli (kama vile mstari wa 2). Inatumika kipekee juu ya yale yaliyoshuhudiwa katika kutoka Misri. Hii nadharia ya kuzaa pia inajitengenezea yenyewe kwenda katika dhana ya watu wa Mungu kama wana wa Mungu.

◙**"Mimi ni Bwana. . ."** Hii tungo kibayana ni, "Mimi ni YHWH," ambayo ni tungo ya ufunguzi katika Agano la Kale. Ni mbinu ya kifasihi juu ya jina la kiagano la Mungu, kutoka katika KITENZI "kitenzi kisaidizi" (kama vile Kutoka. 3:14). Maana yake ya msingi ni "Mimi niishiye milele, Mungu pekee niishiye." Angalia Mada Maalumu katika 40:3.

◙**"nifanyaye vitu vyote"** Huu ni msisitizo wa Mungu kama vyote Muumbaji na Mwokozi (kama vile 45:12,18).

◙**"nizitandaye mbingu peke yangu"** Hapa tena ni Mungu kama Muumbaji. Hii ni tungo inayotumika katika Isa. 40:22; 42:5; 45:12,18; 51:13.

◙**"niienezaye nchi"** Kiingereza "vyote" (*qere*, NEB) kibayana ni swali lisilo hitaji jibu, "Mimi ni nani?" (*ketiv*, DSS, LXX, NRSV). Huu ni msisitizo kama tungo hapo juu, "Kwa uweza wangu mwenyewe," ya nafasi ya kipekee ya Mungu. Yeye ni mmoja na Mungu Muumbaji pekee (kama vile Ayubu 38:4 na kuendelea). Angalia Mada Maalum: Imani katika Mungu mmoja katika 40:14.

◙**"waongo....waganga.......wenye hekima"** Mstari huu ni ufunuaji wa shughuli za kichawi zifanywazo na mataifa yaliyozunguka. Mungu anaweka ukomo wa kujadili manabii wake wa kweli katika mstari wa 26. Kibiblia, njia ya kubaini nabii wa kweli inapatikana katika Kumb.13:1-3; 18:22. Manabii wa ungo na manabii wa kweli wanakwenda kulinganishwa ili kuweza kufunua kwamba Mungu ni Mungu pekee. Inawezekana kwamba neno la Kiebrania "wenye majivuno" linaweza kumaanisha

1. waongo, wazushi (BDB 95 III)
2. wasema uzushi, kutoka katika mzizi wa ki-Akkadian (AB, vol. 20, ukurasa wa 72), ambalo lingefanya kuwe na mfanano na "waganga" (mstari wa 2). Tazama kwa namna gani maneno haya ya kiebrania yanavyofanana. #1 בדים kwenda #2 ברים

Makuhani wa Barim wa Babeli walikuwa wakijulikana kwa utabiri wao (Leupold, ukurasa wa 133).

**44:26 "nilithibitishaye neno la mtumishi wangu"** Mungu anashughulikia historia. Uweza wake wa kuyasema matukio ya siku za baadaye ni njia moja wapo ya kuwathibitishia wanadamu wote kwamba Mungu ni Muumbaji Pekee, Mungu Mkombozi (kama vile 41:22-23; 45:7,26). Katika vipengele hivi vya unabii wa Isaya unatumika kama namna ya Mungu kuonesha uweza wake dhidi ya shughuli za uchawi kutokuwa na nguvu ya kujua matukio ya siku zijazo.

Maneno "mtumishi" (BDB 712) na "mjumbe" (BDB 521) anafanana. Ya kwanza ni UMOJA na ya pili ni WINGI. Je hii ilikusudiwa kurejerea

1. mtumishi
2. manabii

Au wote waeleweke kama nabii? Hivyo, "mtumishi" ingekuwa njia ya kuwapa sifa manabii wote.

Mstari huu unawezakuwa maelezo kwa Isa. 2:2-4 au Mika 4:1-4.

◙**"niuambiaye Yerusalemu, Utakaliwa na watu"** Huu ni unabii wa dhahiri wa sio tu urejesho wa Yerusalemu lakini pia miji ya Yuda (kama vile. 2:2-4; Mika 4:1-3).

**44:27** Kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya maana ya mstari huu. Hizi ni nadharia:

1. YHWH anashughulikia mawimbi ya machafuko (kama vile Mwanzo 1; Zab. 74:12-17; Isa. 51:10).
2. Ni rejea kwa Mungu kugawanya Bahari ya Shamu na Mto Yordani na hivyo ni rejea kwa Safari ya Kutoka Misri kuelekea Kanaani.
3. Mungu anaweza akathibiti kizuizi chochote na inatumika katika namna ya Mungu kukausha au kuushinda Mto Frati (yaani dokezo katika Isa. 11:15-16) ili kwamba Koreshi aweze kuishinda Babeli.
4. Hii inatumika kwa baadhi ya namna kwamba Mungu ni mdhibiti wa umande inayothibitisha kwamba yeye ni Mungu wa Ustawi na sio Baali.

**44:28 “nimwambiaye Koreshi”** Koreshi anatajwa kwa jina kwa mara ya kwanza katika muktadha huu. Yeye pia anatajwa katika 45:1. Josephus, katika kitabu chake, *Antiquities of the Jews*, 11.5, inasema kwamba desturi za Kiyahudi zinaamini kwamba nabii zilioneshwa kwa Koreshi na kwamba aliwaruhusu Wayahudi kurejea Yuda. Pia tunajifunza kwamba Koreshi alifurahishwa na nabii hizi katika II Nyakati 36:22-23.

◙**“Mchungaji wangu”** Neno hili kimsingi linazungumzia kiongozi au mtawala. Kuna maneno yenye nguvu ya kifalme yatumikayo hapa, “mchungaji” (BDB 944 I) katika 44:28 na “aliyetiwa mafuta” (BDB 603) katika 45:1. Maneno yote mawili yanaonesha kwamba Mungu atamtumia Koreshi kutimiliza makusudi yake. Hii haimanishi kwamba Koreshi alifanyika mwamini (kama vile mstari wa 5c), lakini kwamba Mungu anatumia mwanadamu kama chombo cha kukamilishia makusudi yake (yaani Kutoka 3:7-10).

◙**“Msingi wako utawekwa”** Kutimilizwa kwa unabii huu, kunakohusiana na jiji la Yerusalemu na hekalu, inapatikana katika vitabu vya Ezra, Nehemia, na Haggai.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:1-7**
**1 Haya ndiyo Bwana amwambiayo Koreshi,**
**masihi wake,ambaye nimemshika mkono wake wa kuume,**
**ili kutiisha mataifa mbele yake,name nitalegeza viuno vya wafalme;**
**ili kufungua milango mbele yake,hata malango hayatafungwa.**
**2 Nitakwenda mbele yako, na kupasawazisha mahali palipoparuza;**
**nitavunja vipande vipande milango ya shaba,**
**na kukata-kata mapingo ya chuma;**
**3 nami nitakupa hazina za gizani,**
**na mali zilizofichwa za mahali pa siri,**
**upate kujua ya kuwa mimi ni Bwana,**
**nikuitaye kwa jina lako, naam, Mungu wa Israeli.**
**4 Kwa ajili ya Yakobo, mtumishi wangu, na Israeli, mteule wangu,**
**nimekuita kwa jina lako; nimekupa jina la sifa; ijapokuwa hukunijua.**
**5 Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu;**
**nitakufunga mshipi ijapokuwa hukunijua;**
**6 ili wapate kujua toka maawio ya jua, na toka magharibi,**
**ya kuwa hapana mwingine zaidi ya mimi;**
**Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine.**
**7 Mimi naiumba nuru, na kulihuluku giza;**
**mimi nafanya suluhu, na kuhuluku ubaya;**
**Mimi ni Bwana, niyatendaye hayo yote.**

**45:1 “aliyepakwa mafuta”** Hili ni jina katika agano la Kale linalotumika kwa watu wa aina kadhaa ya watu.
1. kwa Mfalme Sauli, I Sam. 12:3; 24:6
2. kwa watu wa Mungu, Hab. 3:13
3. kwa mababa wa Imani, Zab. 105:15
4. kwa makuhani, Law. 4:3,5,16
5. kwa “yule ajaye,” Dan. 9:25; Zab. 2:2

Imetumika kama jina la kimasihi lililokuzwa wakati wa kipindi cha kati cha Biblia. Neno “Masihi” (angalia Mada maalum katika 40:14) inatoka katika neno la Kiebrania “Aliyepakwa Mafuta.” Koreshi akiitwa kwa neno hili kuonesha kwamba Uchaguzi katika Agano la Kale kimsingi ilikuwa kwa ajili ya huduma na sio wokovu.

◙**“kwa mkono wa kuume”** Angalia Mada maalum katika 40:2.

◙**"nitalegeza viuno vya wafalme"** Hii inarejerea kulegezwa mshipi ambayo inaweza ikawa inamaanisha mavazi ya mwanaume yalikuwa yakivaliwa kwa kuacha huru jambo lililofanya iwe ngumu kutembea au mshipi inaweza kuwa ulikuwa ukibeba silaha na wao waliwalikuwa wakiachia chini ardhini (kama vile mstari wa 5).

**45:2**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kunyoosha sehemu zilizoparuza"** |
| **NKJV** | **"kunyoosha maeneo yaliyopinda"** |
| **NRSV, TEV** | **"kunyoosha milima"** |
| **NJB** | **"kufungua malango"** |

Toleo la NRSV ni dhahiri (kama vile 49:11). Pia inapatikana katika matoleo ya DSS na LXX. Milima yawezekana ikawa sitiari ya matatizo au hofu (kama vile 40:4; 41:15; 42:15).

◙**"nitavunja vipande vipande milango ya shaba, na kukata-kata mapingo ya chuma;"** Hizi zote ni sitiari kuonesha kwamba Mungu atasababisha Koreshi kufanikiwa katika mapambano yake juu ya miji yenye ngome za ukuta ya Mesopotamia na Palestina. Inafurahisha kwamba mwanahistoria, Herodotus, 1:179, anataja kwamba mji wa Babeli ulikuwa na zaidi ya malango ya shaba 100.

**45:3 "nami nitakupa hazina za gizani"** Huu ni utajiri uliofichwa katika falme za Mesopotamia na Mashariki ya karibu.

**45:4 "Kwa ajili ya Yakobo, mtumishi wangu,**
**na Israeli, mteule wangu"** Hapa tuna sababu za kwanza mbili kwa nini Mungu alimtumia Koreshi: (1) urejesho wa wateule Wake na (2) Alitaka watu wa Israeli kuwa nuru kwa ulimwengu, mstari wa 6. Israeli haikuwa nuru hivyo Mungu alimtumia Koreshi (kama vile Ezek. 36:22-38).

◙**"ijapokuwa hukunijua"** Mungu anamtumia Koreshi japokuwa hakumjua Yeye. Kuna mbinu ya kimchezo juu ya neno "kujua" katika mistari ya 4,5,6. Katika Kiebrania neno "kujua" linazungumzia uhusiano wa ukaribu wa kibinafsi (kama vile Mwanzo 4:1), sio tu ufahamu wa kiakili. Hakuna sifa alizonazo Koreshi kwamba Mungu anatakiwa amchague yeye lakini Mungu anamtumia kwa ajili ya makusudi ya kiungu (Angalia Mada maalum katika 40:15).

## MADA MAALUM: AKAMJUA (kama ilivyoelezewa toka Kumbukumbu la Torati)

Neno la Kiebrania "kujua"(BDB 393) lina maana kadhaa (mazingira ya kimaana) katika shina la neno *Qal*.

1. Kuelewa mema na mabaya - Mwa. 3:22; Kumb. 1:39; Isa. 7:14-15; Yohana 4:11
2. Kujua kwa kuelewa - Kumb. 9:2,3,6; 18:21
3. Kujua kupitia mazoea - Kumb. 3:19; 4:35; 8:2,3,5; 11:2; 20:20; 31:13; Yos. 23:14
4. kufikiri - Kumb. 4:39; 11:2; 29:16
5. kujua kibinafsi
    a. mtu - Mwa. 29:5; Kut. 1:8; Kumb. 22:2; 33:9, Yer. 1:5
    b. mungu -Kumb. 11:28; 13:2,6,13; 28:64; 29:26; 32:17
    c. YHWH - Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
    d. kizinaa - Mwa. 4:1,17,25; 24:16; 38:26
6. ujuzi wa kujifunza - Isa. 29:11,12; Amosi 5:16
7. kuwa mwenye hekima - Kumb. 29:4; Mit. 1:2; 4:1; Isa. 29:24
8. maarifa ya Mungu
    a. kwa Musa - Kumb. 34:10
    b. kwa Israeli- Kumb. 31:21

Kithiolojia #5 ni wa muhimu. Imani ya kibiblia ni ushirika wa ndani, wa kila siku, unaokua pamoja na Mungu(angalia Mada Maalum: *Koinōnia*). Sio sheria pekee au maisha ya kiadilifu pekee. Ni imani binafsi ya kiushirika. Hii ndio sababu Paulo alitumia nyumba ya mshirika katika Efe.5:22-6:9 kuelezea upendo wa Kristo kwa ajili ya kanisa.

**45:5 "Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine;"** Huu ni uthibitisho wa imani juu ya Mungu mmoja (kama vile 44:24; 45:6-7,14,18,21,22, angalia mada maalum katika 40:14).

◙**"zaidi yangu mimi hapana Mungu"** Hakuna njia nyingine ya kurejerea kwa imani juu ya Mungu mmoja (kama vile 44:6,8; 43:11).

◙**"nitakufunga mshipi"** Hii inamaansha "kuvikwa uweza." Silaha silivaliwa katika viuno (kama vile mstari wa 1). Hii ni kinyume cha 1d.

**45:6 "ili wapate kujua toka maawio ya jua, na toka magharibi**
**"hapana mwingine zaidi ya mimi"** Hapa tena ni unabii ushangazao kwamba Mungu anachagua Koreshi kwa ajili ya kusudi lile lile ambalo aliichagua Israeli ambali ilikuwa ni kujifunua mwenyewe kwa ulimwengu wote ili kwamba ulimwengu uweze kuja kumjua yeye.

**45:7** Mstari huu ulisababisha hofu kuu kati wa wafasiri kwasababu inaonekana kumfanya Mungu Muumbaji awe mwovu. Kimsingi, kile kinachoonekana hapa ni kukataliwa kwa kuwepo kwa u-pili katika ulimwengu. Hii inaweza ikaaksi ushawishi wa Uajemi juu ya imani ya Zoroastra, japo hatuna uhakika juu ya uhusiano wa Koreshi kwa u-pili huu uliokuzwa. Mstari huu kimsingi unasema kwamba kuna kisababishi kimoja tu katika ulimwengu (kama vile Muhubiri 7:14; Amosi 3:6b). Mungu anahusika na mambo yote. Anatumia uovu kwa ajili ya makusudi Yake! Hii ni njia nyingine ya kuthibitisha na kukiri Imani juu ya Mungu mmoja.

Mstari wa 7 is a series ofni mfululizo wa *Qal* KAULI ENDELEVU zinazohusiana na shughuli za uumbaji za Mungu zikiwekwa katika jozi za ulinganifu.

1. kutengeneza – BDB 427, KB 428
2. kuumba – BDB 135, KB 153
3. kusababisha – BDB 793, KB 889
4. kuumba – BDB 135, KB 153
5. kufanya – BDB 793, KB 889

Kuwa makini na kuchukua mstari mmoja mje ya muktadha wa ushairi na kuutumia kama msingi wa kauli ya kimafundisho. Aina ya ushairi na muktadha ni muhimu katika ufasiri sahihi!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:8**
**8 Dondokeni, enyi mbingu, toka juu,**
**Mawingu na yamwage haki; Nchi na ifunuke,**
**ili kutoa wokovu, Nayo itoe haki ikamee pamoja;**
**Mimi, Bwana, nimeiumba.**

**45:8** Nabii anatumia mgogoro wa siku zake mwenyewe kubashiri ufalme wa Mungu wa siku za mbeleni. Katika muktadha, mstari huu unachagizwa na mstari wa 6, ambayo inamaanisha kwamba hizi ni siku za mbele

zitarajiwazo kwa kutamaniwa wakati wanadamu wote watakapo jua na kumwabudu Mungu, ambalo lilikuwa kusudi la asili la uumbuji wa Mwanzo (kama vile Mwanzo 3:8).

◙Mstari wa 8 ni mfuatano wa amri (yaani maombi) yakielekezwa kwa utaratibu wa kiumbaji wa Mungu.

1. Tiririka chini – BDB 950, KB 1271, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. mimina – BDB 633, KB 683, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU ikitumika katika HALI YA KUSIHI
3. fungua – BDB 834, KB 986, *Qal* KAULI YA ISIO TIMILIFU itumikayo katika HALI YA KUSIHI
4. zaa matunda – BDB 826, KB 963, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU itumikayo katika HALI YA KUSIHI
5. chomoza – BDB 855, KB 1033, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU itumikayo katika HALI YA KUSIHI

YHWH anamaliza na aya/mstari pamoja na kauli ya muhtasari wa nguvu ya uumbaji Wake (BDB 135, KB 153, *Qal* KAULI ILIYO TIMILIFU)! Msisitizo huu juu ya Mungu kama Muumbaji inatambulisha sehemu zilizobakia za sura (haswa mstari wa 18). Kama alivyoumba nchi, ndio vyo hivyo pia Israeli. Uuumbaji una makusudi ya kimahusiano.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:9-10**
**9 Ole wake ashindanaye na Muumba wake!**
**Kigae kimoja katika vigae vya dunia!**
**Je! Udongo umwambie yeye aufinyangaye; Unafanya nini?**
**Au kazi yako, Hana mikono?**
**10 Ole wake amwambiaye baba yake, Wazaa nini?**
**Au mwanamke, Una utungu wa nini?**

**45:9 "Ole wake ashindanaye na Muumba wake! —"** Tumeona maelezo kadhaa kwa maeneo ya mfano wa kifasihi wa kimahakama katika Isaya 40-45. Sasa "ole" linatambulisha mfano mwingine wa kifasihi wa kinabii, "wimbo wa maombolezo." Ilikuwa onyo "kimauti" kwa wale (Wayahudi na Mataifa) wanaomdhihaki YHWH. Katika muktadha, ubeti huu ungemaanisha mshangao unaohisiwa na Wayahudi katika ujumuishi wa Mataifa!
Hii inaonesha uwepo wa baadhi ya Wayahudi walioitikia hasi kwa nji ya Mungu ya kushughulikia ukombozi (kama vile mstari wa 11). Walichukizwa kwamba Mungu angetumia mtawala asiyeamini kama Koreshi (kama vile 13). Hii ni sawasawa na nabii Habakuki mawazo ya mashaka kuhusu Mungu kuutumia Babeli.

◙**"Je! Udongo umwambie yeye aufinyangaye;"** Hii dhana ya binadamu kama udongo wa mfinyanzi na Mungu kama mfinyanzi ni ya kawaida katika Biblia, yawezekana kwasababu

1. wanadamu wamefanywa kutokana na mavumbi au mfinyanzi na atarudi mavumbini (kama vile Isa. 39:16; Yer. 18:1 na kuendelea; Rum. 9:20-21)
2. Inadokeza uhuru wa YHWH kutenda kazi na uumbaji Wake pale anapotaka na kwa ajili ya makusudi yake

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV,** | **"Yeye hana mikono"** |
| **NRSV, JPSOA** | **"kazi yako haina mikono"** |
| **REV, REB** | **"huna ufundi"** |
| **NJB** | **"kazi yako haina mikono"** |
| **Peshitta** | **"je Mimi si kazi ya mikono yako"** |
| **NAB** | **"ufanyacho hakina mikono"** |

Hii inaweza kumaanisha

1. sanamu hazina mikono
2. mafundi hawana ufundi
3. chombo hakina mikono

Ni bora tu kutambua utata na kutazama katika mistari mingine ya 9 na mstari wa 10 kwa ajili ya maana ya ujumla ya kimuktadha. Hicho kiumbwacho hakiwezi kohoji muumbaji Wake!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:11-13**
**11 Bwana, Mtakatifu wa Israeli,**
**na Muumba wake, asema hivi;**
**Niulize habari za mambo yatakayokuja;**
**mambo ya wana wangu,**
**na habari ya kazi ya mikono yangu; haya! Niagizeni.**
**12 Mimi nimeiumba dunia,**
**nimemhuluku mwanadamu juu yake;**
**Mimi, naam, mikono yangu mimi,**
**imezitanda mbingu, na jeshi lake lote nimeliamuru.**
**13 Mimi nimemwinua katika haki,**
**nami nitazinyosha njia zake zote;**
**ataujenga mji wangu,**
**naye atawaacha huru watu wangu waliohamishwa,**
**si kwa kulipwa fedha, wala kwa kupewa zawadi, asema Bwana wa majeshi.**

**45:11** Mstari huu unaanza na majina kadhaa kwa ajili ya Mungu.
1. YHWH
2. Mtakataifu wa Israeli
3. Mtengenezaji wa Israeli (BDB 427, KB 428, *Qal* KAULI ENDELEVU)

Alafu inaendelea msisitizo juu ya YHWH kama mtabiri wa matukio (yaani utawala wa Koreshi).
Toleo la UBS Text Project (ukurasa wa 125) unapendekeza, "niulizeni juu ya mambo yajayo, (lakini) juu ya wanangu na kazi ya mikono yangu, nami nitajibu!"

**45:12 "na jeshi lake lote nimeliamuru"** Hapa tena YHWH anakuza sehemu Yake ya kipekee kama Muumbaji wa mbingu na nchi. Wababeli waliabudu nyota na sayari. Hii ni kauli kali sana kwamba YHWH aliamuru (BDB 845, KB 1010, *Piel* KAULI ILIYO TIMILIFU) majeshi yake yote (kama vile 40:26). Msisitizo huu wa YHWH kama muumbaji na mdhibiti wa viumbe vyote vya mbinguni (yaani jua, mwezi, nyota na sayari) hufanya kazi kama Mwanzo 1 katika kuonesha ujinga na makosa ya kuabudu vitu vya anga.
Katika Isa. 24:21-22 neno "majeshi" linatumika kwa ajili ya nguvu za kimalaika nyuma ya mataifa (kama vile LXX ya Kumb. 32:8 na Danieli 10). Ikiwa ni ya kimalaika au ya kisayari, YHWH mdhibiti wa miungu wadogowadogo wa ulimwengu waitwao *elohim*. Hakuna Mungu mwingine bali YHWH, lakini zipo nguvu zingine za kiroho.

# MADA MAALUM: MALAIKA NA MAPEPO

A. Watu wa Kale walikuwa waabudu wanyama. Walichukua vitu vya asili na wanyama wakavipa tabia za kibinadamu. Maisha yalielezwa kupitia kujamiiana kwa vitu hivi vya kiroho pamoja na wanadamu.

B. Kuvipa sifa za kibinadamu kwenye vitu visivyo na ubinadamu kwa muda kulikuwa ni ibada ya sanamu (miungu wengi). Siku zote mapepo (*genii*) yalikuwa miungu midogo au miungu isiyoeleweka (mwema au muovu) kwamba kuliathiri maisha ya kibinadamu binafsi.
   1. Mesopotamia, machafuko na migogoro
   2. Misri, mpangilio na kazi
   3. Kanaani, angalia W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel*, Fifth Edition, ukurasa 67-92

C. Agano la Kale halijikiti au kukuza somo la mungu mdogo, malaika, au mapepo, yawezekana kwasababu ya uungu mmoja kunakotiliwa mkazo (angalia Mada Maalum hali ya uungu mmoja, kama vile Kutoka 8:10; 9:14; 15:11; Kumbukumbu la Torati 4:35,39; 6:4; 33:26; Zaburi 35:10; 71:19; 86:8; Isaya 46:9; Yeremia 10:6-7; Mika 7:18). Haitaji miungu ya uongo ya mataifa ya kipagani (*Shedim,* BDB 993, kama vile Kumbukumbu la Torati 32:17; Zaburi 106:37) na inawataja au kuwapa sifa za kibinadamu baadhi yao.

1. *Se'im* (miungu yenye tama za ngono au mapepo yenye manyoya, BDB 972 III, KB 1341 III, kama vile Mambo ya Walawi 17:7; 2 Mambo ya Nyakati 11:15; Isaya 13:21; 34:14)
2. *Lilith* (la kike, pepo linalotongoza usiku, BDB 539, KB 528, kama vile Isa. 34:14)
3. *Mavet* (Neno la kiebrania kwa ajili ya mauti lilitumika kwa ajili ya mungu wa wakanaani aishiye chini ya nchi, *Mot*, BDB 560, KB560, kama vile Isaya 28:15,18; Yeremia 9:21; na yawezekana Kumbukumbu la Torati 28:22)
4. *Resheph* (tauni, moto, au mvua ya mawe, BDB 958, KB 958, kama vile Kama vile 32:24; Zaburi 78:48; Habakuki 3:5)
5. *Dever* (magonjwa, BDB 184, kama vile Zaburi 91:5-6; Habakuki 3:5)
6. *Az'azel* (jina halijulikani vizuri, lakini yawezekana ni pepo la jangwani au jina la sehemu, BDB 736, KB 736, kama vile Walawi 16:8,10,26)

(Mifano hii imechukuliwa kutoka katika *Encyclopaedia Judaica*, vol. 5, ukurasa 1523.)Hatahivyo, hakuna kuabudu kwa upili au kujitegemea kimalaika YHWH katika Agano la Kale. Shetani ni mtumishi wa YHWH (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3), isiyo ya kujitegemea, adui anayejiongoza mwenyewe (kama vile A. B. Davidson, *A Theology of the Old Testament,* kurasa 300-306).

D. Waumini wa kiyahudi wakati wa uhamishoni mwa Babeli (586-538 K.K.). Lilishawishiwa kithiolojia na waashuru waliopewa sifa za kibinadamu za upili wa (Zoroastrianism) dini ya wafuasi wa Zarathustra walioamini katika mungu mmoja kabla ya kuja kwa uislamu katika karne ya 6 K.K, mungu mkuu mwema *Mazda* au *Ormazd* na mpinzani muovu aitwaye *Ahriman*. Hii iliruhusu ndani ya baada ya uhamisho wa uyahudi ya upili uliopewa sifa za kibinadamu kati ya YHWH na Malaika zake na Shetani au mapepo.

Thiolojia ya dini ya Kiyahudi ya uovu uliopewa sifa za kibinadamu inaelezeka na kuandikwa vizuri katika kitabu cha Alfred Edersheim's *The Life and Times of Jesus the Messiah*, Toleo la 2, appendix XIII (kurasa za 749-863) na XVI (kurasa 770-776). Dini ya kiyahudi iliwapa sifa za kibinadamu za uovu katika njia tatu.

1. Shetani au *Sammael*
2. nia za uovu (*yetzer hara*) ndani ya mwanadamu
3. malaika wa mauti

Edersheim anatoa tabia hizi

1. mshitaki
2. mjaribu
3. anaye adhibu (toleo la 2, ukurasa 756)

Kuna utofauti wa alama ya kithiolojia kati ya baada ya uhamisho wa kiyahudi na uwasilishaji wa Agano Jipya na maelezo ya uovu.

E. Agano Jipya, hasa Injili, zinaelezea uwepo na upinzani wa viumbe waovu kwa mwanadamu na kuelekea kwa YHWH (katika uyahudi, Shetani alikuwa adui kwa mwanadamu lakini sio kwa Mungu). Wanapinga mapenzi ya Mungu, utawala, na ufalme

Yesu alikabiliana na kuwaondoa viumbe wa kipepo (1) roho chafu (kama vile Luka 4:36; 6:18) au (2) roho za uovu (kama vile Luka 7:21; 8:2), kutoka katika viumbe vya kibinadamu. Yesu kwa dhahiri alitengeneza utofauti katika ya ugonjwa (wa mwili na akili) na ya kipepo. alidhihirisha nguvu zake na maarifa yake ya kiroho kwa kutambua na kufanyia kazi roho hizi za uovu. Mara Nyingi walimtambua Yeye na kujaribu kumwambia, lakini Yesu alikataa ushuhuda wao, alitaka ukimya wao, na kuwaondoa. Kupunga pepo ni ishara ya kushindwa kwa ufalme wa shetani

Kuna kukosekana kwa taarifa kwa kushangazwa katika barua za kitume za Agano Jipya kwa somo hili. Kupunga pepo hakujawahi kamwe kutajwa kama karama ya kiroho wala mbinu au taratibu kwa kutolewa kwa vizazi vijavyo vya wahudumu au waaminio.

F. Uovu ni halisi; uovu ni nafsi; uovu upo. Si asili yake au kusudio lake ndilo linalofunuliwa. Biblia inaeleza kwamba kweli yake na kwa nguvu inapinga ushawishi wake. Hakuna kuwepo kwake katika upili katika kilele kiuhalisia. Mungu anahusika na kushughulikia kila kitu; uovu umeshindwa na kuhukumiwa na utaondolewa kutoka katika uumbaji.

G. Watu wa Mungu lazima wapinge uovu (kama vile Yakobo 4:7). Hawatakiwi kutawaliwa nao (kama vile 1 Yohana 5:18), lakini wanaweza kushawishiwa na mashuhuda wao na kushawishi kuharibika (kama vile Efe. 6:10-18). Uovu unafunuliwa kama sehemu ya mtazamo wa ukristo. Wakristo wa kisasa hawana haki ya kutoa maana upya ya uovu (hali ya tafsiri mpya ya Rudolf Baltmann); kupunguza nguvu ya uovu (miundo ya kijamii ya Paul Tillich), hakujaribu kuelezea hili kwa ukamilifu katika maneno ya kisaikolojia (Sigmund Freud). Ushawishi wake umeenea lakini umeshindwa. Waamini wanahitaji kutembea katika ushindi wa Kristo!

**45:13 "Mimi nimemwinua katika haki"** Toleo la NIV linafasiri "yeye" kama Koreshi. YHWH anamchochea Koreshi ili ayafanye mapenzi yake. Hii inarejerea kwa (1) kuvamia kwa ghafla na kwa ukamilifu kwa Koreshi (2) matamko ya Koreshi yaliyoruhusu makundi yote ya uhamishoni kwenda nyumbani na kuyajenga mahekalu yao ya kitaifa. Tamko hili lilitolewa mnamo mwaka 538 k.k, mwaka mmoja baada ya kuanguka kwa Babeli.

◙**"si kwa kulipwa fedha, wala kwa kupewa zawadi"** YHWH atampatia Koreshi II ushindi na pia atawaachia Israeli kurudi Yuda bila rushwa wala malipo (TEV).
Toleo la Jewish Study Bible (ukurasa wa 876) unasema kwamba mstari wa 14 unarejerea zawadi ya YHWH kwa Koreshi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:14-17**
***14*Bwana asema hivi, Kazi ya Misri, na bidhaa ya Kushi,**
**na Waseba, watu walio warefu, watakujilia, nao watakuwa wako;**
**watakufuata; watakuja katika minyororo;**
**wataanguka chini mbele yako, watakuomba, wakisema,**
**Hakika Mungu yu ndani yako;**
**wala hapana mwingine, hapana Mungu tena.**
***15* Hakika wewe u Mungu ujifichaye nafsi yako,**
**Ee Mungu wa Israeli, Mwokozi.**
***16*Watatahayarika, naam, watafadhaika,**
**wote pia; wale wafanyao sanamu wataingia fadhaa pamoja.**
***17* Bali Israeli wataokolewa na Bwana kwa wokovu wa milele; ninyi**

**45:14** Haijajulikana ikiwa mistari ya 14-17 inajumuisha vipengele vya kifasihi. Ni dhahiri kwamba mistari ya 15-17 inarejerea Israeli. Inawezekana kwamba mstariwa 14 unaweza ukawa unarejerea kwa Uajemi (kama vile 43:3) na sio Yuda. Hatahivyo mataifa haya haya yanatolewa kama fidia kwa watu wa Mungu 43:3. Ulimwengu wote ulikusudiwa kuja kwa Mungu 45:20-22. Hatahivyo, Yuda angekuwa chini ya mstari wa 14. Hii inafanana na unabii kwamba mataifa yote yatakusanywa ili kurejeshwa Sayuni (kama vile 2:2-4; 60:1 na kuendelea; Zab. 72:8-11).
Muhtasari wa mstari wa 14, "Hakuna Mungu mwingine," inatupeleka mpaka mstari wa 16 (yaani "wao"). Vyote sanamu na wanaoziabudu

1. wataaibishwa – BDB 101, KB 116, *Qal* KAULI TIMILIFU
2. watafedheheshwa – BDB 487, KB 480, *Niphal* KAULI TIMILIFU

Lakini Israeli haitafanya hivyo (kama vile mstari wa 17)!

**45:15** Tazama majina ya Mungu

1. Mungu (*El,* BDB 42)
2. Mungu (*Elh*, BDB 43) wa Israeli
3. Mwokozi (BDB 446)

Mwokozi wa Israeli alijificha Mwenyewe mbali na watu Wake kwa kipindi cha muda kwasababu ya dhambi zao na uasi (kama vile 1:15; 8:17; 54:8; 57:17; Zaburi 44:24; 88:14, pia dokezo katika Ayubu 13:24). Japo kipindi hicho cha hukumu kimepita (kama vile 40:2) na sasa kurudi na kurejeshwa kumeanza kupitia Koreshi. Toleo la AB, vol. 20, ukurasa wa 82, linapendekeza huku kufichwa kwasababu Israeli lilikuwa taifa dogo na lisilothaminika kwa muda huu.

**45:16** Angalia dokezo katika mstari wa 14. Mstari wa 16 kithiolojia unafanana na 44:11.

**45:17** Hii ni ahadi nzuri sana japo wasomaji wanahitaji kukumbuka ni la kimasharti juu ya agano la utii wa kiagano wa Israeli. Kwa kusoma hii tu na kusahau kwamba Israeli tena ilitawaliwa na kuharibiwa na wote Uyunani na Rumi kunaonesha ukomo wa uhakiki wa kimaandiko.

Tatizo halikuwa upendo wa YHWH na ahadi, lakini kukosekana kwa uwezo wa Israeli wa kutotii amri Zake.

Maneno ya Kiebrania "isiyo na mwisho" (BDB 761) na "milele" (BDB 761) Yanatoka katika mzizi wa Kiebrania ambao una upana mkubwa wa kimaana (uwanja wa maana). Angalia Mada maalum hapa chini.

## MADA MAALUMU: MILELE (*'olam*)

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, םלוע (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzuu. 3, uk. 345). Yametumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na maudhui). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

1. vitu vya kale
   a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
   b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
   c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
   d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
   e. mda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. mda/ wakati ujao
   a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
   b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
   c. uwepo endelevu
      1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
      2) mbinguni, Zab. 148:5
   d. uwepo wa Mungu
      1) Mwa. 21:33
      2) Kut. 15:18
      3) Kumb. 32:40
      4) Zab. 93:2
      5) Isa. 40:28
      6) Yer. 10:10
      7) Dan. 12:7
   e. Agano
      1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
      2) Kut. 31:16

    3) Ufu. 24:8
    4) Hes. 18:19
    5) 2 Sam. 23:5
    6) Zab. 105:10
    7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
    8) Yer. 32:40; 50:5

f. Agano maalumu na Daudi
    1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
    2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
    3) 2 Nya. 13:5
    4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
    5) Isa. 9:7; 55:3

g. Masihi wa Mungu
    1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
    2) Isa. 9:6

h. Sheria za Mungu
    1) Kut. 29:28; 30:21
    2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
    3) Hes. 18:8,11,19
    4) Zab. 119:89,160

i. Ahadi za Mungu
    1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51
    2) 1 Fal. 9:5
    3) Zab. 18:50
    4) Isa. 40:8

j. Uzao wa Abrahamu na nchi ya ahadi
    1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
    2) Kut. 32:13
    3) 1 Nya. 16:17

k. Sikukuu za ahadi
    1) Kut. 12:14,17,24
    2) Ufu. 23:14,21,41
    3) Hes. 10:8

l. umilele, kudumu milele
    1) 1 Fal. 8:13
    2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
    3) Isa. 26:4; 45:17
    4) Dan. 9:24

m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
    1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
    2) kudumu katika uwepo Wake, Zab. 41:12; 61:4,7
    3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
    4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
    5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
    6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
    7) tukuza jina lake,Zab. 86:12; 145:2
    8) baliki jina lake, Zab. 145:1

n. linatumiwa na Isaya kueleza enzi mpya
    1) agano la milele, Isa. 24:5; 55:3; 61:8
    2) YHWH kama mwamba wa milele, Isa. 26:4

3) furaha ya milele,Isa. 35:10; 51:11; 61:7
4) Mungu wa Milele, Isa. 40:28
5) Wokovu wa milele, Isa. 45:17
6) Wema wa milele, Isa. 54:8
7) Ishara ya milele, Isa. 55:13
8) Jina la milele, Isa. 56:5; 63:12,16
9) Nuru ya milele, Isa. 60:19,20

Matumizi yenye hali ya ukanushi kuhusiana na adhabu ya milele kwa waharifu inapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya kila wakati anatumia "moto" kuelezea hasira ya Mungu (kama vile. Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini katika Isa. 33:14 "ndipo anasema wa milele"

3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
   a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
   b. Zab. 90:2 (Mungu pekee)
   c. Zab. 103:17 (huruma zake)

Kumbuka, muktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani, Yeremia 7, tazama Mada Maalumu: Agano). Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la thiolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka pia, Agano Jipya linajumuisha ahadi zote za Agano la kale (tazama Mada Maalumu: utabiri wa mambo yajayo ya Agano la Kale dhidi ya utabiri wa mambo yajayo ya Agano Jipya.).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:18-19**
**18Maana Bwana, aliyeziumba mbingu, asema hivi;**
**Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya;**
**ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu;**
**Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine.**
**19Sikusema kwa siri, katika mahali pa nchi ya giza;**
**sikuwaambia wazao wa Yakobo; Nitafuteni bure;**
**Mimi, Bwana, nasema haki; nanena mambo ya adili.**

**45:18 "ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa"** Haya ni maelezo ya Mwanzo 1:2. Yanaweza kufasiriwa kama "bia umbo" (BDB 1062). Mungu siku zote alikuwa na kusudi kwa ajili ya uumbaji. Kusudi hilo ni kwamba ilitakiwa ikaliwe. Kulikuwa na ukuaji wa uumbaji wa Mungu. Hii haithibitishi baadhi ya uharibifu kati ya Mwanzo 1:1 na 1:2 (yaani Nadharia ya Ombwe).

◙**"aliiumba ili ikaliwe na watu)"** Hii inatumika na walimu wa Kiyahudi kuweka mkazo kwamba kila mmoja anatakiwa aoe na kuolewa (kama vile Mwanzo 1:28; 9:1, 7).

**45:19** YHWH ameelezea tena na tena katika kipengele hiki kwamba Yeye ni Mungu asikiaye na atendaye; Ajuaye siku za baadaye na kuamua uelekeo wake! Maelezo ya kithiolojia ni ushahidi wa kimsingi wa Uwepo Wake! Ushahidi mwingine ni uwepo wa Israeli na kurudi kwake katika Nchi ya Ahadi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 45:20-25**
**20Jikusanyeni mje; na kukaribia pamoja, ninyi wa mataifa mliookoka;**
**hawana maarifa wale wachukuao mti wa sanamu yao ya kuchonga;**
**wamwombao mungu asiyeweza kuokoa.**
**21Hubirini, toeni habari; naam, na wafanye mashauri pamoja;**
**ni nani aliyeonyesha haya tangu zamani za kale?**
**Ni nani aliyeyahubiri hapo zamani? Si mimi, Bwana?**

**Wala hapana Mungu zaidi ya mimi;**
**Mungu mwenye haki, mwokozi; hapana mwingine zaidi ya mimi.**
**22 Niangalieni mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia;**
**maana mimi ni Mungu; hapana mwingine.**
**23 Kwa nafsi yangu nimeapa, neno hili limetoka kinywani mwangu katika haki,**
**wala halitarudi, ya kwamba mbele zangu kila goti litapigwa, kila ulimi utaapa.**
**24 Mmoja ataniambia, Kwa Bwana, peke yake, iko haki na nguvu;**
**naam, watu watamwendea yeye, na wote waliomkasirikia watatahayarika.**
**25 Katika Bwana wazao wote wa Israeli watapewa haki, na kutukuka.**

**45:20 "Jikusanyeni mje; na kukaribia pamoja,**
**ninyi wa mataifa mliookoka;**
**hawana maarifa"**
Baadhi husema hii inarejerea kutawanyika, waisraeli walioko uhamishoni (yaani "enyi wakimbizi ya mataifa," pia dokezo katika mstari wa 25), wakati wengine pia wakiamini ni mwaliko mwingine kwa mataifa ya kipagani, kama ilivyo katika mistari ya 6,22,23 (kama vile Rum. 14:11; Flp. 2:10). Vyote vinawezekana katika muktadha huu.
Kuna mfuatano wa amri katika mistari ya 20-22 inayohusiana na namna gani wanadamu wanatakiwa kumwendea YHWH na kuitikia msaada wake wa upatikanaji wake.

1. jikusanyeni wenyewe – BDB 867, KB 1062, *Niphal* KAULI SHURUTISHI, mstari wa 20
2. njoo – BDB 97, KB 112, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mstari wa 20
3. nikaribiaeni – BDB 620, KB 670, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, mstari wa 20
4. nigeukieni – BDB 815, KB 937, *Qal* KAULI SHURUTISHI, mstari wa 22
5. mkaokolewe – BDB 446, KB 448, *Niphal* KAULI SHURUTISHI, mstari wa 22

Agano Jipya linatumia mstari wa 23 katika nukuu mbili ambazo zinarejerea kwa wanadamu wote (yaani Rum. 14:1 na haswa Flp. 2:10)! Ni mwaliko mzuri wa nmna gani na kutimilizwa kwake kwa Mwanzo 3:15 na 12:3 (angalia Mada Maalum katika 40:15).

◙**"wachukuao mti wa sanamu yao ya kuchonga"** Hii inatoa wito kwa mataifa kukataa sanamu ambazo haziwezi kutenda kazi na kuja kwa Mungu wa Israeli anayeweza kfanya kazi na ambaye atawaokoa.

**45:21** Hii ni taswira ya tukio la kimahakama. Inatabiri (1) Koreshi na mafanikio yake na (2) kurudi kwa Israeli kama chombo cha kiinjili ili kuuleta ulimwengu kwa Mungu. Hapa Mungu anaitwa "Mwokozi" na katika muktadha huu inamaanisha sio tu kwa Wayahudi pekee lakini kwa ulimwengu wote (kama vile mstari wa 22). Maana dhahiri ya Imani juu ya Mungu mmoja (angalia Mada mlum katika 40:14) ni kwamba Mungu mmoja anawapenda wanadamu wote aliowaumba kwa sura yake (kama vile Mwanzo 1:26-27).

**45:22 "Niangalieni mimi"** Hili ni neno la Kiebrania ambalo linatumika kwa ajili ya kuabudu (BDB 815, KB 937). Kama ambavyo watu wanamgeukia Mungu na kuacha ibada za sanamu na dhambi (kama vile 55:7).
Wanadamu wana uchaguzi. Wanaweza kumgeukia YHWH na kuokolewa au kuwageukia sanamu (kama vile Law. 19:4,31; 20:6; Kumb. 31:18,20) na hawana tumaini!

◙**"mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia"** Hii ni rejea kwa wokovu wa ulimwengu wote unaotolewa kwa wanadamu na tumaini kwa YHWH kwasababu hakuna Mungu mwingine (kama vile Mstari wa 21). Kutolewa kwa ajili ya ulimwengu mzima kunawekwa wazi sana katika Isaya. Hii inaweza kufasiriwa "wajiokoe wao wenyewe" (*Niphal* KAULI SHURUTISHI), ambayo ingekuwa kebehi kwa Mwanzo 12:3.

**45:23 "Kwa nafsi yangu nimeapa"** Hakuna kiapo kingine kikubwa zaidi ya hiki!

◙**“neno hili limetoka kinywani mwangu katika haki,
wala halitarudi,”**
Hii ni imani ya kale juu ya nguvu ya neno lizungumzwalo (kama vile 24:3; 25:8; 40:8; 55:10-11). Mungu alilisema; anataka ulimwengu uokolewe (yaani Yohana 3:16)!

◙**“ya kwamba mbele zangu kila goti litapigwa, kila ulimi utaapa”** Hii inatumika kwa muktadha wa YHWH. Hatahivyo katika Wafilipi 2:10 inatumika kama uumbaji makini wote kumkiri Yesu Kristo kama Bwana. Muktadha tena unaonesha kwamba Mungu anataka ulimwengu wote kumwendea Yeye na baadaye ufunuo utaonesha kuwa ni kupitia Masihi wake, Yesu Kristo, kwamba kujitoakwake kiulimwengu kungeweza kutimilizwa (kama vile Marko 10:45; II Kor. 5:21).
Suala la Kithiolojia liko wazi sana. Ikiwa Agano Jipya ni ufunuo, hivyo ahadi za Agano la Kale kwa taifa la Israeli yamekwisha kupanuliwa.

## MADA MAALUM: UTABIRI WA AGANO LA KALE JUU YA WAKATI UJAO DHIDI YA UTABIRI WA AGANO JIPYA (“UTANGULIZI WA MUHIMU” KWA UFUNUO)

Wakati wote wa kujifunza kwangu matukio ya siku za mwisho nimejifunza kwamba Wakristo wengi hawana mfuatano wa matukio ya siku za mwisho au hawataki kuukuza. Kuna baadhi ya wakristo ambao wanaweka shabaha zao au wanaamua kujikita kwenye eneo la Ukristo kwa sababu za kithiolojia, kisaikolojia au kidini. Wakristo hawa wanaonekana kuchanganyikiwa na kwa namna gani itamalizika na kwa namna fulani kukosa umaana wa injili! Waaminio hawawezi kuathiri ajenda ya Mungu ya siku za mwisho, lakini wanaweza kushiriki katika upelekaji wa injili (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Waaminio wengi wanathibitisha kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na kupelekea kwa siku za mwisho kwa ahadi za Mungu. Matatizo ya kiufasiri yanaibuka kutoka kwa namna gani kilele hiki cha muda kitakuja kutoka katika mitazamo kadhaa ya kibiblia (Angalia Mada Maalum:Ukinzani katika Maandiko)

1. mvutano katika ya nadharia za kinabii za agano la kale na nadharia za kitume za Agano Jipya
2. mvutano kati ya hali ya kuabudu Mungu mmoja (Mungu mmoja kwa ajili ya wote) na kuchaguliwa kwa Israeli (watu maalum)
3. mvutano katika ya hali ya kipengele chenye masharti cha maagano ya kibiblia na ahadi (“ikiwa. . .ndipo”) na hali isiyo na masharti ya uaminifu wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka
4. mvutano kati ya aina za fasihi za Mashariki ya Karibu na nadharia za magharibi za kifasihi
5. mvutano kati ya ufalme wa Mungu kwa sasa na ule wa baadaye.
6. mvutano kati ya imani katika kurudi punde kwa Kristo na imani kwamba baadhi ya matukio lazima yatokee kwanza.

Ebu kwanza tujadili mivutano hii moja baada ya nyingine

**MVUTANO WA KWANZA** (vipengele vya kijiografia, kitaifa na kikabila vya Agano la Kale dhidi ya waaminio wote katika ulimwengu)

Manabii wa Agano la Kale walitabiri kurejeshwa kwa ufalme wa Kiyahudi katika Palestina ukiwekwa kitovu Yerusalemu ambapo mataifa yote ya nchi yatakusanyika kusifu na kutumikia mtawala wa Ki-Daudi, lakini Yesu au Mitume wa Agano Jipya hawajikiti katika agenda hii. Je kwani Agano la Kale halijavuviwa (kama vile Mt.

5:17-19)? Je waandishi wa Agano jipya wameondoa sehemu muhimu za matukio ya siku za mwisho?

Kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu:

1. manabii wa Agano la Kale (Isaya, Mika, Malaki)
2. waandishi wa siku za mwisho (kama vile Ezek. 37-39; Dan. 7-12; Zek.)
3. Kipindi kati ya kuandikwa kwa Agano la Kale na Agano Jipya, waandishi wa siku za mwisho wa kiyahudi wasio wakanoni (kama I Enoch, ambaye anaelezewa katika Yuda)
4. Yesu mwenyewe (kama vile Mt. 24; Marko 13; Luka 21)
5. maandiko ya Paulo (kama vile I Kor. 15; II Kor. 5; I The. 4-5; II The. 2)
6. maandiko ya Yohana (I Yohana na Ufunuo).

Je haya yote kwa ufasaha yanafundisha ajenda ya siku za mwisho (matukio, mpangilio wa matukio, watu)? Ikiwa sio, kwanini? Je si kwamba wote wamevuviwa (isipokuwa maandiko ya kiyahudi ya kati ya kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya)?

Roho alifunua kweli kwa waandishi wa Agano la Kale kwa namna na vipengle ambavyo wangeweza kuelewa. Hatahivyo kupitia ufunuo endelevu Roho amepanua dhana hizi za matukio ya siku za mwisho kwa mtazamo wa kijumla ("siri za Kristo," kama vile Efe. 2:11-3:13. Angalia Mada Maalum katika 10:7). Hii hapa ni baadhi ya mifano inayoelekeana kwa umuhimu:

1. Jiji la Yerusalemu katika Agano la Kale linatumika kama sitiari ya watu wa Mungu (Sayuni), lakini inakadiriwa katika Agano Jipya kama neno linaloelezea ukubalifu wa Mungu wa watubuo wote na wanadamu waaminio (Yerusalemu mpya ya Ufunuo 21- 22). Upanuzi wa kithiolojia wa jiji la kibayana la kimwili katika watu wapya wa Mungu (Wayahudi na Mataifa waaminio) inaakisiwa kwa kuoneshwa mbele katika ahadi za Mungu kukomboa mwanadamu aliyeanguka katika Mwanzo 3:15, kabla hata haijakuwako Myahudi yeyote au mji mkuu wa kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (kama vile Mwanzo 12:1-3) ilijumuisha Mataifa (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5).
2. Katika Agano la Kale adui za watu wa Mungu ni mataifa yazungukayo mataifa ya Mashariki ya Karibu ya Kale, lakini katika Agano Jipya wamepanua kwa watu wasio amini, walio kinyume na Mungu na waliovuviwa kishetani. Vita vimehamisha kutoka kijiografia, kimgogoro wa kikanda kwenda ulimwenguni kote, mgogoro wa kiulimwengu (kamavile Wakolosai).
3. Ahadi ya nchi ya ambalo ni jambo kuu sana katika Aano la Kale (Ahadi kwa mababa wa imani katika Mwanzo, kama vile Mwanzo 12:7; 13:15; 15:7,15; 17:8) sasa imekuwa kwa dunia yote. Yerusalemu mpya inashuka chini kwa dunia iliyotengenezwa upya, sio Mashariki ya Karibu tu au kutojumuisha (kama vile Ufunuo 21-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ni dhana za kinabii za Agano la Kale zilizopanuliwa ni
   a. uzao wa daudi saa umetahiriwa kiroho(kama vile Rum. 2:28-29)
   b. watu wa agano sasa wanajumuisha Mataifa (kama vile Hos. 1:10; 2:23, akinukuu katika Warumi 9:24-26; pia Mambo ya Walawi 26:12; Kutoka 29:45, ikinukuliwa katika II Kor. 6:16-18 na Kutoka 19:5; Kumb. 14:2, ikinukuliwa katika Tito 2:14)
   c. hekalu sasa ni Yesu (kama vile Mt. 26:61; 27:40; Yohana 2:19-21) na kupitia kanisa la mahali pamoja (kama vile I Kor. 3:16) au mwamini mmoja mmoja (kama vile I Kor. 6:19)
   d. Hata Israeli na tungo zinazofunua tabia za Agano la Kale sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu (yaani "Israeli," kama vile Rum. 9:6; Gal. 6:16, yaani "ufalme wa makuhani," kama vile I Pet. 2:5, 9-

10; Ufunuo 1:6)

Nadharia ya kinabii imetimilizwa, imepanuliwa na sasa imekuwa jumuishi. Yesu na waandishi wa kitume hawawasilishi nyakati za mwisho kwa namna ile ile ya Manabii wa Agano la Kale (kama vile Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecyand Fulfillment*). Wafasiri wa kisasa wanaojaribu kulifanya nadharia ya Agano la Kale kuwa ya maana ya wazi au ya tabia ya kawaida kugeuza ufunuo katika kitabu cha kiyahudi kabisa na kulazimisha maana! Waandishi wa Agano Jipya hawawakatai manabii wa Agano la Kale lakini wanaonesha ufanyaji wao kazi wa kilele wa kiulimwengu. Hakuna mpangilio au mfumo wa kimantiki kwa matukio ya siku za mwisho ya Yesu au Paulo. Makusudi yao kimsingi ni ukombozi na sio uchungaji.

Hatahivyo, hata ndani ya Agano Jipya kuna mvutano. Hakuna mfumo wa wazi wa matukio ya siku za mwisho. Katika njia nyingi Ufunuo kwa kushangaza unatumia Maelezo ya Agano la Kale katika kuelezea mwisho badala yamafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko 13)! Inafuata aina ya fasihi iliyoanzisha na Ezekieli, Daniel na Zekaria lakini ilikuzwa wakati wa kipindi kati ya uandishi wa Agano la Kale na Agano Jipya (fasihi ya kiyahudi ya siku za mwisho). Hii inaweza kuwa ilikuwa nji ya Yohana kuunganisha Maaagano ya Kale na Jipya. Inaonesha utaratibu wa zama-kuu ya uasi wa kibinadamu na kujizatiti kwa Mungu katika ukombozi! Lakini lazima itambuliwe kwamba ingawa Ufunuo unatumia lugha, watu na matukio ya Agano la Kale, inafasiri kwa ufahamu na namna ya karne ya kwanza ya Rumi (kama vile Ufunuo 1:7).

**MVUTANO WA PILI** (hali ya kuabudu Mungu mmoja dhidi ya wateule wa Mungu)

Msisitizo wa kibiblia upo juu ya Mungu binafsi, kiroho, muumbaji-mkombozi (kama vile 8:10; Isa. 44:24; 45:5-7,14,18,21- 22; 46:9; Yer. 10:6-7). Upekee wa Agano la Kale katika siku zake ilikuwa hali ya kuabudu Mungu mmoja (angalia Mada Maalum: Ibada kwa Mungu mmoja).Mataifa yote yanayozunguka yalikuwa ni waabudu miungu wengi. Kuwepo kwa Mungu mmoja ni moyo wa ufunuo wa Agano la Kale (kama vile Kumb. 6:4). Uumbaji ni jukwaa kwa kusudi la ushirika kati ya Mungu na mwanadamu, waliofanywa kwa sura yake na mfano (kama vile Mwanzo1:26-27). Hatahivyo, mwanadamu aliasi, akitenda dhambi dhidi ya upendo wa Mungu, uongozi na kusudi (kama vile Mwanzo 3). Upendo wa Mungu na kusudi lilikuwa kubwa na lenye nguvu sasa na hakika alihaidi kukomboa mwanadamu aliyeanguka (kama vile Mwanzo 3:15)!

Mvutano unainuka pale ambapo Mungu anachagua kumtumia mwanadamu mmoja, familia moja, taifa moja kufikia wanadamu waliobakia. Wateule wa Mungu wa Ibrahimu na Wayahudi kama ukuhani wa kikuhani (kama vile Kutoka 19:4-6) kulisababisha kiburi badala ya huduma, kutengwa badala ya kujumuishwa. Wito wa Mungu kwa Ibrahimu ulijumuishwa Baraka za kimakusudi kwa wanadamu wote (kama vile Mwanzo 12:3). Lazima ikumbukwe na kusisitizwa kwamba uchaguzi wa Agano la Kale ulikuwa kwa ajili ya huduma, sio wokovu. Israeli yote haijawahi kuwa sawa na Mungu, haijawahi kukombolewa kimilele kwa msingi tu wa haki yake (kama vile Yohana 8:31-59; Mt. 3:9), lakini kwa imani binafsi na utii (kama vile Mwanzo 15:6, ikinukuliwa kutoka Warumi 4). Israeli ilipoteza lengo lake (kanisa sasa ni ufalme wa kikuhani, kama vile 1:6; II Pet.2:5,9), twakibadilisha majukumu kuwa upendeleo, huduma kuwa msimamo maalum! Mungu anachagua mmoja ili achague wote.

**MVUTANO WA TATU** (maagano yenye masharti dhidi ya maagano yasiyo na masharti)

Kuna mvutano wa kithiolojia au fumbo kati ya maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti. Ni hakika kweli kwamba kusudi/mpango wa Mungu na ukombozi sio wa kimasharti (kama vile Mwanzo 15:12-21).

Hatahivyo, mwitikio wa kimajukumu wa kibiadamu siku zote huwa ni wa kimasharti!

Ile "ikiwa. . .basi" ya utaratibu huu unatokea kote katika Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu ni mwaminifu; mwanadamu si mwaminifu. Mvutano huu umesababisha mkanganyiko mkubwa. Wafasiri wamejifanya kuweka shabaha juu ya moja tu "pembe ya mkanganyiko," Uaminifu wa Mungu au juhudi za mwanadamu, utawala wa Mungu au utashi huru wa mwanadamu. Vyote ni vya kibiblia na ni vya muhimu (Angalia Mada Maalumaaaa;Uchaguzi/Kuamriwa kabla na Hitaji la uwiano wa Kithiolojia)

Hii inahusiana na matukio ya siku za mwisho, kwa ahadi za Mungu za Agano la Kale kwa Israeli; Hadhi yake inajumuishwa (kama vile Ezek. 36:22-38). Maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti yanakutana katika Kristo (kama vile Isa. 53), sio Israeli! Kilele cha uaminifu wa Mungu kinategemea ukombozi wa wote watakaotubu na kuamini, sio nani alikuwa baba yako/mama yako, sio Israeli, ni msingi wa maagano yote ya Mungu na ahadi. Ikiwa kuna maelezo ya kithiolojia katika Biblia, sio kanisa bali Israeli (kama vile Mdo. 7 na Gal. 3).

Kusudio la ulimwengu la kutangaza injili limepita kwa kanisa (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Bado ni agano la kimasharti! Hii sio kumaanisha kwamba Mungu amekataa kabisa Wayahudi (kama vile Rum. 9-11). Kuna weza kuwa kuna mahali na kusudi la siku za mwisho, kuamini Israeli (kama vile Zek 12:10).

**MVUTANO WA NNE** (nadharia ya kifasihi ya Mashariki ya Karibu dhidi ya nadharia za kimagharibi).

Aina za fasihi ni kipengele muhimu katika usahihi wa kufasiri Biblia. Kanisa limeendelea katika mazingira ya kidesturi ya kimagharibi (kiyunani). Fasihi ya mashariki zaidi ni ya kimafumbo, ya kisitiari na kiishara kuliko kuwa ya kisasa,nadharia za desturi za kifasihi za kimagharibi (angalia Mada Maalum: Fasihi ya Mashariki (ukinzani wa kibiblia)). Imejikita kwa watu, matukio na mazingira kuliko kweli ziazopendekezwa. Wakristo wamekuwa na hatia ya kutumia historia na nadharia za kifasihi kufasiri nabii za Kibiblia (zote Agano la Kale na Agano Jipya). Kila kizazi na jambo la kijiografia limetumia desturi yake, historia na ubayana wake kufasiri Ufunuo. Kila mmoja wao amekuwa na makosa! Ni kiburi kufikiria kwamba desturi za kisasa za kimagharibi ni shabaha ya unabii wa kibiblia!

Aina ya fasihi ambayo kutoka kwake mwandishi wa asili na aliyevuviwa anachagua kuandika ni mkataba wa kifasihi na mwandishi. Kitabu cha Ufunuo sio masimulizi ya kihistoria. Ni muunganiko wa barua (sura za 1-3), unabii na zaidi fasihi ya nyakati za mwisho. Ni mbaya kuifanya Biblia kusema zaidi ya kilichokusudiwa na mwandishi wa asili kama ilivyo kuifanya iseme kidogo kuliko ilivyokusudiwa! Kiburi cha wafasiri na mafundisho hata zaidi isivyokuwa sawa katika kitabu kama ufunuo.

Kanisa halijawahi kukubaliana katika fasiri sahihi ya ufunuo. Shida yangu ni kusikia na kushughulikia Biblia nzima, sio baadhi ya sehemu zilizochaguliwa. Mtazamo wa mashariki wa Biblia inawasilisha ukweli katika jozi zilizojaa mvutano. Mwenendo wetu wa magharibi kuelekea ukweli unaopendekezwa usiokatalika lakini usio na uwiano! Nafikiri inawezekana kuondoa angalau baadhi ya vizuizi katika kufasiri Ufunuo kwa kutambua makusudi yake yanayobadilika kuelekea vizazi vinavyofuata vya waaminio. Ni dhahiri kwa wafasiri wengi kwamba Ufunuo lazima ufasiriwe katika ufahamu wa siku zake wenyewe na aina yake ya fasiri. Mkabiliano wa kihistoria kwa Ufunuo lazima ushughulikiwe na wasomaji wa kwanza wangefanya na wangeelewa. Kwa namna nyingi wafasiri wa kisasa wamepoteza maana za viwakilishi vya kitabu. Msukumo mkubwa wa kwanza wa Ufunuo. Ulikuwa ni kutia moyo waamini watesekao. Ilionesha namna Mungu anavyoshughulikia historia (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale); Ilikiri kwamba historia inaenda kuelekea mwisho wa uteuzi,

hukumu au baraka (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale). Ilikiri katika muktadha wa upendo wa Mungu, uwepo, nguvu na utawala wa siku za mwisho wa kiyahudi wa karne ya kwanza!

Inafanya kazi katika njia hizihizi za kithiolojia kwa kila kizazi cha waaminio. Inachukua mahangaiko ya kiulimwengu ya jumla ya mazuri na mabaya. Maelezo ya karne ya kwanza yanaweza yakawa yamepotea kwetu lakini yasiyo na nguvu wala ukweli wa kufariji. Wakati wafasiri wanajaribu kulazimisha maelezo ya ufunuo kwenye historia ya sasa, utaratibu wa fasiri za uongo!

Inawezekana kwamba maelezo ya kitabu yanaweza kufanyika fasihi isiyo ya kawaida tena (kama ilivyokuwa katika Agano la Kale kuhusiana na kuzaliwa, kuishi na kufa kwa Kristo) kwa kizazi cha mwisho cha Waaminio kama walivyokabiliana na kuchinjwa na kiongozi mpinga-Mungu (kama vile II The.2) na desturi. Hakuna mtu anayeweza kujua kutimilizwa huku kwa kibayana kwa Ufunuo mpaka maneno ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko13; na Luka 21) na Paulo (kama vile I Kor. 15; I The. 4-5; na II The. 2) pia inafanyika dhahiri kihistoria. Kudhania, kufikiria na mafundisho vyote hivi sio sahihi. Fasihi ya matukio ya siku za mwisho yanaruhusu mabadiliko. Mshukuru Mungu kwa taswira na viwakilishi ambavyo vinapita masimulizi ya kihistoria! Mungu anawawala na kushughulikia mabo yake; Anatawala; Anakuja!

Fasiri nyingi za kisasa zinakosa suala la uchaguzi wa aina ya fasihi ya uwasilishaji! Wafasiri wa kisasa wa Magharibi mara kwa mara wanatafuta mfumo sahihi uliowazi wenye mantiki wa kithiolojia kuliko kuchukuliana na aina ya fasihi yenye utata, wakilishi ya kitamthilia ya matukio ya siku za mwisho. Kweli hii inaelezewa vizuri na Ralph P. Martin katika makala yake,"Approaches to New Testament Exegesis," katika kitabu *New Testament Interpretation*, kilichohaririwa na I. Howard Marshall:

"Mpaka tutakapotambua ubora wa kitamthilia wa maandiko haya na kukumbuka njia ambayo lugha inatumika kama chombo cha kuelezea ukweli wa kidini, tutakuwa tumefanya kosa kubwa sana katika uelewa wetu wa matukio ya siku za mwisho na kimakosa kujaribu kufasiri maono yake kana kwamba ni kitabu cha riwaya ya kawaida na kinachojihusisha kuelezea matukio ya kihalisia na historia inayoandikika. Kujaribu njia ya pili ni kukimbia katika kila mtindo wa matatizo ya fasiri. Zaidi sana inapelekea kwenye uharibifu wa maana ya msingi katika lugha za hadithi za kufikirika za Mungu mtawala katika Kristo na fumbo la utawala wake ambao unaunganisha uweza na upendo (kama vile 5:5,6; Simba ndiye mwana kondoo)" (ukurasa wa 235).

W. Randolph Tate katika kitabu chake *Biblical Interpretations* alisema:

"Hakuna fasihi ingine ya Biblia ambayo imesomwa kwa dhati na shauku kubwa na kwa matokeo yenye kukatisha tama kama vitabu vya matukio ya siku za mwisho. Aina hii ya fasihi ilipata shida kutokana na historia ya kimajanga ya kufasiriwa vibaya kwasababu ya kukosekana kwa uelewa wa msingi wa muundo wake wa fasihi, mpangilio na kusudi. Kwasababu ya madai yake sana ya kufunua kile ambacho karibia kinatokea, vitabu vya mwisho wa ulimwengi vimekuwa vinatazamwa kama mwongozo kuelekea katika kuyajua jua mambo yajayo. Kosa kubwa zaidi katika mtazamo huu ni dhana kwamba muuundo wa vitabu vya rejea ni umri wa msomaji wa sasa kuliko kuwa wa mwandishi. Huu mkabiliano usio kuwa na mwongozo wa matukukio ya siku za mwisho (hasa Ufunuo) unaifanya kazi kama vile ni namba za siri ambazo matukio ya kisasa yanaweza kutumika kutafsiria viwakilishi vya andiko. . .Kwanza, mfasiri lazima atambue kwamba vitabu vya siku za mwisho vinazungumzia jumbe zake kupitia uwakilishi wa kiishara. Kufasiri ishara kibayana wakati inapokuwa kisitiari ni kupotosha fasiri. Tatizo sio kama matukio katika za mwisho ni ni ya kihistoria. Matukio yanaweza yakawa sio ya kihistoria; yanaweza kuwa kweli yalitokea, au yatatokea lakini mwandishi anayawasilisha na

kuzungumza maana zake kupitia taswira na nadharia” (ukurasa wa 137).

Kutoka katika *Dictionary of Biblical Imagery*, iliyohaririwa na Ryken, Wilhost na Longman III:

“Wasomaji wa leo mara kwa mara wanashangazwa na kuchanganywa na aina hii ya fasihi. Taswira isiyotegemewa na ya nje ya uzoefu wa ulimwengu huu. Kuichukilia Fasihi hii kwa inavyoonekana inawaacha wasomaji wengi wakikwaruza kwaruza wakiwa wamejizatiti ‘nini kitatokea wakati,’ hivyo kukosa kusudio la ujumbe wa maandiko ya siku za mwisho” (ukurasa wa 35).

**MVUTANO WA TANO** (ufalme wa mungu uliopo sasa lakini wa baadaye)

Ufalme wa Mungu ni wa sasa na ni wa baadaye. Hili fumbo la kithiolojia linafanyika shabaha katika hatua ya matukio ya siku ya mwisho. Ikiwa mtu atategemea kutimilizwa kwa kibayana kwa nabii zote za Agano la Kale kwa Israeli hivyo ufalme wa Mungu zaidi unafanyika urejesho wa Israeli kwenye eneo lao la kijiografia na utawala wa kabla wa kithiolojia! Hii ingepelekea kwamba Kanisa kwa siri linanyakuliwa katika sura ya 5 na sura zilizosalia zinahusiana na Israeli (lakini angalia dokezo katika Ufunuo 22:16).

Hatahivyo ikiwa shabaha ipo katika ufalme kuanzishwa na Masihi anayetabiriwa katika Agano la Kale, alafu lipo na kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo na alafu inaweka shabaha kwenye kufanyika mwili, maisha, mafundisho, kifo na kufufuka kwa Kristo. Msisitizo wa kithiolojia upo katika wokovu wa sasa.

Ufalme umekuja, Agano la Kale limetimilizwa katika kujitoa kwa wokovu kwa Kristo kwa wote na sio utawala wake wa Milenia na baadhi! Ni kwa kweli na hakika kwamba Biblia inazungumza juu ya ujio wote wa Kristo, lakini wapi ambapo msisitizo unawekwa? Inaonekana kwangu kwamba nabii nyingi za Agano la Kale zinalenga juu ya ujio wa kwanza, uanzishwaji wa ufalme wa Kimasihi (kama vile Danieli 2). Katika namna nyingi huu utawala wa Mungu unafananishwa na utawala wa milele wa Mungu (kama vile Danieli 7). Katika Agano la Kale shabaha ipo katika utawala wa Mungu wa milele, japo namna ya udhihirisho wa utawala huo ni huduma ya Masihi (kama vile I Kor. 15:26-27). Sio swali la nini ni kweli; vyote ni kweli lakini msisitizo upo wapi? Lazima isemwe kwamba baadhi ya wafasiri wanafanya kulenga kwenye utawala wa milenia wa Masihi (kama vile Ufunuo 20) kwamba wamekosa shabaha ya kibiblia juu ya utawala wa milele wa baba. Utawala wa Kristo ni tukio la kuanzia kama kiashiria. Kama kuja kwa mara mbili huku kwa Kristo hakukuwa dhahiri katika Agano la Kale, wala haitakuwa pia kutawala kwa muda kwa Masihi!

Msingi wa mahubiri na mafundisho ya Yesu ni ufalme wa Mungu. Ni vyote sasa (katika wokovu na huduma), na baadaye (katika utawala mkuu wa ulimwengu na nguvu). Ufunuo, ikiwa utalenga kwenye utawala wa kimasihi wa kimelenia (kama vile Ufunuo 20), itakuwa mwanzo tu na sio kilele (kama vile Ufunuo 21-22). Sio dhahiri kutoka katika Agano la Kale kwamba utawala wa muda ni mughimu; ukweli ni kwamba utawala wa Kimasihi wa Danieli 7, ni wa milele na wala sio wa ki-milenia.

**MVUTANO WA SITA** (kurudi kwa hakika kwa Kristo dhidi ya kuchelewa *Parousia*)

Waamini wengi wamefundishwa kwamba Yesu anakuja hivi karibuni, ghafla na bila taarifa (kama vile Mt. 10:23; 24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30; Ufunuo 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; angalia Mada Maalum:Kurudi Punde). Lakini katika kila kizazi kitarajiacho cha waamini hata hivyo kimekosea! Ukaribu (uharaka) wa kurudi kwa Yesu ni tumaini lenye nguvu lililohaidiwa kwa kila kizazi, lakini ukweli kwa mmoja tu (na yule aliyeteseka na huyo tu). Waaminio lazima waishi kama vile anarudi kesho, lakini apange na kufanyia kazi Agizo Kuu (kama

vile Mt. 28:19-20) ikiwa atakawia.

Baadhi ya vifungu katika Injili na I na II Wathesalonike wamejikita katika kukawia katika Kuja kwa Mara ya Pili (*Parousia*). Kuna baadhi ya matukio ya kihistoria ambayo lazima yatokee kwanza:

4. kuhubiriwa kwa injili ulimwenguni kote (kama vile Mt. 24:14; Marko 13:10)
5. ufunuo "mwanadamu mdhambi" (kama vile Mt. 24:15; II The. 2; Ufunuo 13)
6. mateso makuu (kama vile Mt. 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata wa kimakusudi (kama vile Mt. 24:42-51; Marko 13:32-36)! Ishi kila siku kama vile ni siku yako ya mwisho lakini panga na jifunze kwa ajili ya huduma yako ya baadaye!

**MWENDELEZO NA UWIANO**

Lazima isemwe kwamba shule tofauti tofauti za fasiri za siku za mwisho zote zinajumuisha ukweli nusu. Wanaelezea na kufasiri vizuri baadhi ya maandiko. Tatizo linatokana na mwendelezo na uwiano. Mara kwa mara kuna mpangilio wa kauli za kupendekeza ambazo zinatumia maandiko ya kibiblia kujaza mafuvu yaliyowekwa kabla ya kithiolojia. Biblia haifunui mantiki, mtitiriko wa matukio na mfumo wa siku za mwisho. Iko kama albamu ya familia. Picha ni za kweli lakini siku zote hazipo katika mpangilio, katika muktadha katika mfuatano wa kimantiki. Baadhi ya picha zimeanguka kutoka kwenye albamu na vizazi vya baadaye vya ndugu wa familia hawajui hakika namna ya kuzirudisha. Msingi wa fasiri sahihi wa Ufunuo ni kusudio la mwandishi wa asili kama inavyofunuliwa katika uchaguzi wake wa ina ya fasihi anayoitumia. Wafasiri wengi wanajaribu kubeba vifaa vyao vya kutendea kazi na taratibu kutoka katika aina zingine za fasihi za Agano Jipya kwenda kwenye fasiri zao za Ufunuo. Wanaweka shabaha kwenye Agano la Kale badala ya kuruhusu mafundisho ya Yesu na Paulo kupangilia muundo wa kithiolojia na kuruhusu Ufunuo kufanya kazi kama kielelezo.

Lazima nikiri kwamba naikabili fasiri hii juu ya Ufunuo nikiwa na baadhi ya uoga na wasiwasi si kwasababu ya laana ya Ufunuo 22:18-19, lakini ni kwasababu ya kiwango cha mkanganyiko ulioletwa na ufasiri wa kitabu hiki na kuendelea kusababisha kati ya watu wa Mungu. Napenda Ufunuo wa Mungu. Ni kweli wakati wanadamu wote wanakuwa waongo (kama vile Rum. 3:4)! Tafadhali tumia fasiri hii kama jaribio la kuamsha mawazo na sio kutoa maana ya mwisho kama kielekezi na sio mwongozo, kama "vipi ikiwa," na sio "hivyo Bwana asema." Nimekuja kugundua usio kwa uso mapungufu yangu mwenyewe, ubaguzi na ajenda ya kithiolojia. Lakini pia nimeona yale ya wafasiri wengine. Inakaribia kuonekana kwamba watu wanatafta Ufunuo kile wanachotegemea kukipata. Aina ya fasihi inajipelekea yenyewe katika matumizi mabaya!

Hata hivyo ipo katika Biblia kwa makusudi. Imewekwa katika kama hitimisho "neno" sio kwa ajali au bahati mbaya. Ina ujumbe kutoka kwa Mungu kwa watoto wake wa kila kizazi. Mungu anataka tuelewe! Tumuunge mkono, sio kutengeneza magenge; Ebu tukiri kile kilicho wazi na kilicho cha msingi na kikuu, sio yote yanaweza, yataweza au yangeweza kuwa kweli. Mungu atusaidie sisi sote!

**45:24 "na wote waliomkasirikia watatahayarika"** Hii hainoneshi kwamba siku moja watu wote ikiwa wanaamini kwa YWHW au hapana watamtambua Yeye kama Bwana (kama vile Wafilipi 2). Baadhi watakuwa tayari washamkiri Yeye na kuokolewa lakini wengine watamkubali muda mfupi tu kabla ya hukumu na kutengwa (kama vile Mt. 25:31-46; Ufunuo 20:11-15).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha tabia za Mungu zinazotajwa katika Isaya 45:24-28. (kuna vishazi rejeshi tisa)
2. Kwanini Mungu alimchagua Koreshi?
3. Nini umuhimu wa neno la Kiebrania "kujua" (kama vile 45:4-6)?
4. Kwanini Isa. 45:6 ni muhimu sana?
5. Orodhesha mara na namna mafundisho ya imani ya Mungu mmoja inatajwa katika kifungu hiki.
6. Je Isa. 45:8 inarejerea kurudi kutoka uhamishoni au Ufalme wa Kimasihi? Kwanini?
7. Nini umuhimu wa Isa. 45:22?
8. Kwa namna gani Isa. 45:23 inatumika katika Agano Jipya na ina umuhimu gani kwa kifungu hiki

# ISAYA 46

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Sanamu za Babeli na Mungu wa kweli | Sanamu za kuchonga na Mungu aishiye | Bwana anaiunga mkono Israeli | Bwana wa ulimwengu na sanamu za Babeli | Anguko la Babeli |
| 46:1-2<br>(1-2) | 46:1-2<br>(1-2) | 46:1-2<br>(1-2) | 46:1-2<br>(1-2) | 46:1-13<br>(1-13) |
| 46:3-4<br>(3-4) | 46:3-4<br>(3-4) | 46:3-4<br>(3-4) | 46:3-4<br>(3-4) | |
| 46:5-7<br>(5-7) | 46:5-7<br>(5-7) | 46:5-7<br>(5-7) | 46:5-7<br>(5-7) | |
| 46:8-11<br>(8-11) | 46:8-11<br>(8-11) | 46:8-11<br>(8-11) | 46:8-11<br>(8-11) | |
| 46:12-13<br>(12-13) | 46:12-13<br>(12-13) | 46:12-13<br>(12-13) | 46:12-13<br>(12-13) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozowa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Leupold, katika fasihi yake juu ya Isaya, uk. 147, ananikumbusha kwamba
    1. katika Isaya 14 ufalme wa Babeli unahukumiwa
    2. katika Isaya 46 miungu ya Babeli inahukumiwa
    3. Katika Isaya 47 taifa, linaloainishwa kama malkia, linahukumiwa

B. Babeli, katika Biblia, ni sitiari kwa ajili ya jamii nzima ya mwanadamu iliyojikusanya pamoja na kutenda mbali na Mungu. Ni jaribio la mwanadamu kuyafikia mahitaji yake kwa rasilimali yake mwenyewe. Babeli inaainishwa kama nyangumi mkubwa katika kitabu cha Ufunuo 18.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:1-2**
[1] **Beli anaanguka chini, Nebo anainama;**

**sanamu zao ziko juu ya wanyama, na juu ya ng'ombe;**
**vitu vile mlivyokuwa mkivichukua huku na huku vimekuwa mzigo,**
**mzigo wa kumlemea mnyama aliyechoka.**
**2 Wanajiinamisha, wanainama pamoja;**
**hawakuweza kuutua mzigo,**
**bali wao wenyewe wamekwenda kufungwa.**

**46:1 "Beli"** *Bel* (BDB128, KB 132, lugha ya Akadia kwa maana ya "bwana") linafanana na jina la Kikanaani *Ba'al*. Hili ni rejea ya mungu mkuu wa hekalu la miungu yote ya huko Akadia (*Enlil*, ambaye alikuwa akiitwa "bwana"). Baada ya Babeli kuingia madarakani jina kuu la uungu lilibadilika na kuwa *Marduk* (BDB 597, kama vile Yer. 50:2).

◙**"Nebo"** Huyu alikuwa ni mwana wa*Marduk* (ametajwa hapa tu katika Agano la Kale) na alikuwa ni mungu wa kujifunza na kuandika (BDB 612). Beli na Nebo wanaweza kuonekana kwa wingi katika majina ya Wababeli wa kipindi cha (Nebukadneza [Dan. 1:1]; Nebushazban [Jer. 39:13]; Nebuzaradan [Jer. 39:9]; Nabopolasa [mfalme wa kwanza wa Babeli mpya, na babake Nebukadneza]; Nabonidus [babake Beshaza, mfalme wa mwisho wa Babeli mpya]; Belteshaza [Dan. 1:7]; Belshaza [Dan. 5:1]). Hawa walikuwa ni miungu wakuu wa hekalu la miungu wengi wa Babeli.

◙**"anasimama. . .juu ya"** Kuna mchezo juu ya dhana ya neno "akainama" (BDB 505, KB 499). Linahusiana na 45:23, miungu ya Wababeli kuinama mbele ya YHWH muumbaji.

◙**"mlivyokuwa mkivichukua. . .vimekuwa mzigo. . .mzigo wa kumwelemea"** Kuna mchezo kwenye neno "mkivichukua" katika mistari ya 1-2 na 3-4. Kwanza kabisa miungu ya Babeli lazima ibebwe juu ya wanyama wenye kubeba mizigo kujaribu kukwepa Waajemi au misafara ya matambiko iliyokuwa ikifanyika kwenye miji mikubwa yote. Mungu huwachukua wanawe, kiistiari katika tumbo la mama na baadaye, muda wote wa maisha yao (kama vile mst. 1). Ni kutokuweza kwa miungu ya Babeli kusikia, kutenda dhidi ya utunzaji, kutoa na matendo ya neema ya Mungu wa Israeli, ambaye wanakinzana katika mistari ya 1-4.

**46:2 "Bali wao wenyewe wamekwenda kufungwa"** Hapa hawa miungu ya Wababeli wanaainishwa kama wenye kwenda kufungwa na watu wao.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:3-4**
**3 Nisikilizeni, enyi wa nyumba ya Yakobo,**
**ninyi mlio mabaki ya nyumba ya Israeli,**
**mliochukuliwa nami tangu tumboni, mlioinuliwa tangu mimbani;**
**4 na hata uzee wenu mimi ndiye,**
**na hata wakati wenu wa mvi nitawachukueni;**
**nimefanya, nami nitachukua; naam, nitachukua na kuokoa.**

**46:3 "Sikilizeni"** Huu, kama ulivyo mst. 12, ni *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 1033, KB 1570). Angalia kumbukumbu katika 44:1.

◙**"mabaki"** Angalia Mada Maalum hapo chini

## MADA MAALUM: MABAKI, (BDB 984, KB 1375), MAANA TATU

Dhana ya Agano la Kale ya kifungu cha "mabaki matakatifu" ni kigezo cha sasa cha Manabii (hasa manabii wa karne ya nane na Yeremia). Neno hili linatumika katika maana tatu:

1. wale waliomudu kuishi ndani ya uhamisho (yaani Ezra 9:8,14-15; Neh. 1:2-3; Isa. 10:20-23; 17:4-6; 37:4,31-32; 46:3; Yer. 23:3; 31:7-8; 42:15,19; 44:12,14,28; Mika 2:12; 5:7-8; 7:18; Hag. 1:12-14; 2:2; Zek.

8:6,11-12)
2. wale waliobaki kuwa waaminifu kwa YHWH (yaani, Isa. 4:1-5; 11:11,16; 28:5; Yoeli 2:32; Amosi 5:14-15)
3. wale walio sehemu ya matengenezo mapya ya siku za mwisho na uumbaji mpya (yaani, Amosi 9:11-15; Zek. 8:6)

Ule mfano wa udongo katika Marko 4:1-20 na Mt. 13:1-23, ambao unanukuu Isa. 6:9-10, ni mfano mzuri wa namna Agano Jipya linavyolielewa neno hili (pia nukuu Rum. 9:6 katika kuirejelea Israeli ya siku za Paulo).

Haya "mabaki" ya Agano Jipya yameundwa na Wayahudi waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:27-29) na Mataifa waliomwamini Kristo (kama vile Rum. 9:24-26). Makundi yote yanazungumziwa katika Rum. 9:30-35; 11:11-24,25-32. Kuamini juu ya Israeli si suala la rangi (yaani, Rum. 9:6; 2:18-19), bali kuliamini kundi la wafuasi waaminifu wa mambo mapya wa Mungu, ufunuo kamili katika Yesu. Kulizungumza hili kunaonekana kuwa ni kuyakataa maandiko ya Agano la Kale (yaani, Yer. 31:7-9; Mika 5:7-8) kuhusu taifa la Israeli kuwa mabaki. Tafadhari tazama katika Mada Maalumu yangu: Kwa nini Ahadi za Agano la Agano la Kale Zinaonekana kuwa Tofauti Sana na Ahadi za Agano Jipya? Injili hubadilisha kila kitu!

◙**"mliochukuliwa name tangu tumboni"** Hili kimsingi ni rejeo kwa Mungu kama mzazi na Israeli kama mwana. Hata hivyo, pia inarejea kwenye uumbaji wa taifa la Israeli ikianzia safari ya kutoka Misri (kama vile Kumb. 1:31; Isa. 63:9).

**46:4 "Hata wakati wa uzee wenu"** Mungu sio tu kwamba aliiumba Israeli bali pia ataiwezesha (yaani., "kuwabeba" au "kuwachukua", kama vile Kut. 19:4; Kumb. 1:31; 32:11).

◙**"Mimi ndiye"** Hii (kifasihi Mimi ndiye, kama vile NKJV) ni dhana kuwa Mungu habadiliki (kama vile NJB, kama vile. Mal. 3:6). Hata kama Israeli wamekuwa si waaminifu kwenye agano, lakini bado Mungu anabaki kuwa mwaminifu. Yeye ni Mungu mwaminifu wa Agano. Yeye ni Yule Yule, jana leo, na hata milele!

◙**"name nitawachukua na kuwaokoa"** Hili ni rejeo kwa taifa la Israeli, lakini limebainishwa kwa kila mwamini (VITENZI VYA UMOJA). Angalia VITENZI katika mst. 4.

1. Mungu kaiumba Israeli (*Qal* KAULI TIMILIFU, BDB 793, KB 889)
2. Mungu ataendelea kutoa na kulinda
   a. kuwachukua – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 687, KB 741 (mara mbili)
   b. kuwabebeni – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 669, KB 724 (mara mbili)
   c. kuwaokoeni – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 572, KB 589

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:5-7**
**5 Mtanifananisha na nani, na kunisawazisha naye, na kunilinganisha naye, ili tuwe sawasawa? 6 Watu wamwagao dhahabu kutoka mfukoni, na kupima fedha katika mizani, huajiri mfua dhahabu, akaifanya mungu; huanguka, naam, huabudu. 7 Humchukua begani, humchukua, wakamsimamisha mahali pake, akasimama; hataondoka katika mahali pake, naam, mmoja atamwita, lakini hawezi kujibu, wala kumwokoa na taabu yake.**

**46:5 "Mtanifananisha na nani"** Huu ni msisitizo kuwa hakuna mtu wa kulinganishwa na YHWH (kama vile 43:11; 44:6,8; 45:6). Huu ni ulinganifu kati ya YHWH na miungu ya mataifa (kama vile Isa. 40:18-20; 44:9-20).

Tambua dhana ya ufanano iliopo.

1. Mtanifananisha na nani Mie – *Piel* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 197, KB 225)
2. na kunisawazisha naye – *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 1000, KB 1436)
3. Na kunilinganisha naye – *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 605, KB 647)
4. ili tuwe sawasawae – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 197, KB 225)

YHWH ni wa kipekee. Hajawahi kuwepo, Mungu mmoja wa kweli (angalia Mada ,Maalum: Imani ya Mungu Mmoja katika 40:14). Pia kumbuka dhana ya kithiolojia ya Utatu kwenye Mada Maalum katika 40:13.

**46:6-7** Hizi aya mbili zinaleta tofauti kati ya Mungu mmoja wa kweli katika mst wa 5 na miungu ya mataifa.

1. Watu hutoa pesa kutengeneza miungu na baadaye kuiinamia na kuiabudu (mst. 6)
2. Baadaye huchukua huku na kule na hataondoka mahali pake; na haiwezi kumuokoa (mst. 7)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:8-11**
**8 Kumbukeni haya, mkajionyeshe kuwa waume;**
**jifahamisheni haya, ninyi mkosao;**
**9 kumbukeni mambo ya zamani za kale;**
**maana mimi ni Mungu, wala hapana mwingine;**
**mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi;**
**10 nitangazaye mwisho tangu mwanzo,**
**na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado;**
**nikisema, Shauri langu litasimama,**
**nami nitatenda mapenzi yangu yote.**
**11 Nikiita ndege mkali kutoka mashariki,**
**mtu wa shauri langu toka nchi iliyo mbali;**
**naam, nimenena, nami nitatekeleza;**
**nimekusudia, nami nitafanya.**

**46:8 "Kumbuka"** Aya hii na mstari wa kwanza aya ya 9 ina mlolongo wa KAULI SHURUTISHI.

1. kumbukeni, mst. 8 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 269, KB 269)
2. mkajionyeshe, mst. 8 – *Hithpoel* KAULI SHURUTISHI (BDB 84, KB 100)
3. jifahamisheni, mst. 8 – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI (BDB 996, KB 1427)
4. kumbukeni, mst. 9 – ni kama ule #1

Namba 2 ni wa kipekee. Toleo la Aramaic Targums linatafasiri kama "iweni wajasiri," yumkini linatokana na asili ya Kiarama (kama vile Leupold, uk. 145).

◙**"ninyi mkosao"** Hii inaonyesha kuwa baadhi huko Israeli bado wana mashaka kuhusu namna Mungu alivyokuwa akitenda kazi yake ya ukombozi (kama vile 45:9-11, kitabu cha Habakuki). Kundi lile lile linarejerewa katika mst. 12 kama "lenye mambo ya kutaabisha" kwa jamaa ya Wayahudi.

**46:9 "mambo ya zamani ya kale"** Hili lingalirejerea kwa

1. Agano la YHWH na Ibrahamu ( 43:18; 65:17; Yer. 16:14; 23:7)
2. Matendo ya YHWH ya kuwa nao unasaba (yaani., safari ya Waisraeli kutoka Misri)
3. Ahadi ya kale kwa Israel kuwa taifa teule na kushikamana kwenye agano (kama vile Kumb. 32:7)
4. Ushahidi wa YHWH wa uwepo wake kwa kuyatabiri yajayo (kama vile mistari. 10,11; 42:9)

◙**"maana Mimi ni Mungu"** Angalia kumbukumbu katika mst.5.

**46:10-11** Tena, Mungu anatumia mfano wa utabiri wa unabii kuonyesha kuwa yupo katika uthibiti wa historia. Msisitizo wa kusudi lake, unataja mara nyingi katika mistari ya 10-11, inaonyesha kuwa historia haipo kwa bahati mbaya lakini ina makusudi ya Kiungu (yaani., imani ya viumbe vyote kuumbwa na Mungu; kama vile Isa. 14:24,26; 25:1).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 46:12-13**
**12 Nisikilizeni, ninyi mlio na moyo mshupavu, mlio mbali na haki;**

[13] **Mimi ninaleta karibu haki yangu, haitakuwa mbali,**
**na wokovu wangu hautakawia; nami nitaweka wokovu katika Sayuni**
**kwa ajili ya Israeli, utukufu wangu.**

**46:12-13** Hii ni aya ya muhimu sana na inayoonyesha kuwa Mungu atawaonea huruma hata juu ya Waisraeli wasio amini. Hii inaonyesha kuwa Wayahudi hawakustahili pendo la Mungu na rehema. Wengi wao walikuwa bado wakorofi na wenye shingo ngumu (kama vile 48:4), lakini Mungu akauleta wokovu kwao kwa sababu Yeye alivyo na si kwa sababu ya wao walivyo (kama vile Ezek. 36:22-38). Hili ni muundo wa agano jipya (kama vile Yer. 31:31-34).

Hii kwa maana iliyo wazi ni

1. Maongeo yangu (BDB 420) yataendelea kuwepo – BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU
2. Makusudio yangu yote (BDB 481 TUNGO 343), nitayatimiliza – BDB 793 I, KB 889, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU

Huu uhakika wa YHWH kuutimiliza mpango wake wa Kiungu pia umeonekana katika 14:24; 25:1; 40:8; 55:11 (angalia Millard Erickson, *Christian Theology*, toleo la 2., kurasa za 371-390).

Kifungu kilichopo mstari wa 10a kithiolojia kinafanana na kile cha 41:4; 44:6; 48:12. YHWH Yeye yupo tokea mwanzo na ataendelea kuwepo hadi mwisho (yaani., mwanzo na mwisho)!

◙

**NASB, NKJV,**
**LXX, Peshitta "haki"**
**NRSV "ukombozi"**
**TEV, JPSOA,**
**REB "ushindi"**
**NJB "nitaleta haki…….haki"**

Neno la Kiebrania lililotumika mara mbili ni "haki" (BDB842). Toleo la BDB linasema limetumika juu ya wokovu wa Mungu (#6a), Isa. 45:8; 46:13; 51:6. Neno la Kiebrania "wokovu" (BDB 448) linafanana na lile lililoko katika mst. 13b.

◙**"mlio mbali"** Haya maelezo ya watu wa agano la Mungu yanapingana na ukaribu ("ambao hauko mbali," mst. 13b) wa ukombozi wa YHWH

1. Kupitia Koreshi II (utaratibu wa upangaji wa matukio)
2. kupitia Masihi (matukio ya siku ya mwisho)

# ISAYA 47

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maombolezo kwa Ajiri ya Babeli | Aibu ya Babeli | Maombolezo juu ya Babeli | Hukumu ya Babeli | Maombolezo kwa ajili ya Babeli |
| 47:1-7 (1-7) | 47:1-3 (1-3) | 47:1-4 (1-4) | 47:1-3 (1-3) | 47:1-3 (1-3) |
| | 47:4 (4) | | 47:4 (4) | 47:4-7 (4-7) |
| | 47:5-7 (5-7) | 47:5-7 (5-7) | 47:5-7 (5-7) | |
| 47:8-11 (8-11) | 47:8-9 (8-9) | 47:8-9 (8-9) | 47:8-9 (8-9) | 47:8-15 (8-15) |
| | 47:10-11 (10-11) | 47:10-13 (10-13) | 47:10-13 (10-13) | |
| 47:12-15 (12-15) | 47:12-15 912-15) | | | |
| | | 47:14-15 (14-15) | 47:14-15 (14-15) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya ya tatu
8. Nk

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kama Sura ya 46 inatilia mkazo kuangamizwa kwa sanamu za Babeli , hivyo Sura ya 47 inaelezea kuangamizwa kwa utawala huo (yaani mji wa Babeli) sambamba na imani ya manabii na makuhani wake.

B. Aya ya 1-7 ina mfuatano wa KAULI SHURUTISHI zilizoelekezwa Babeli , inaonyeshwa kwa picha ya Kahaba/malkia.

1. Shuka, mst. 1 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 432, KB 434)
2. Keti mavumbini, mst. 1 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 442, KB 444)
3. Keti chini, mst. 1 – inafanana na namba 2 (tambua muda wa namba ambao neno hili limetumika kwetu katika mst. 1 [mara mbili],5, 8 [mara mbili])
4. twaa, mst. 2 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 542, KB 534)
5. usage, mst. 2 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 377, KB 374)
6. vua utaji wako, mst. 2 – *Piel* KAULI SHURUTISHI (BDB 162, KB 191)
7. ondoa mavazi yako, mst. 2 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 362, KB 359)
8. funua mguu wako, mst. 2 – *Piel* KAULI SHURUTISHI (BDB 162, KB 191)
9. pita katika mto, mst. 2 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 716, KB 778)
10. uchi wako utafunuliwa, mst. 3 – *Niphal* KITENZI AMRISHI (BDB 162, KB 191)
11. kaa kimya, mst. 5 – sawa sawa na#3,4
12. ingia gizani, mst. 5 – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 97, KB 112)

C. Muundo wa fasihi ya kinabii ya Sura hii “wimbo wa maombolezo”. Unatambulika kwa mdundo /mita wa kipekee kwa Kiebrania (3, 2 mdundo, kama mashairi ya maombolezo). Ni wimbo wa maombolezo lakini katika maana ya dhihaka (wimbo wa dhihaki).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:1-7**
**1 Haya, shuka, keti mavumbini,**
**Ewe bikira, binti Babeli;**
**Keti chini pasipo kiti cha enzi,**
**Ewe binti wa Wakaldayo;**
**Maana hutaitwa tena mwororo, mpenda anasa.**
**2 Twaa mawe ya kusagia, usage unga;**
**Vua utaji wako, ondoa mavazi yako,**
**Funua mguu wako, pita katika mito ya maji.**
**3 Uchi wako utafunuliwa,**
**Naam, aibu yako itaonekana.**
**Nitalipa kisasi; simkubali mtu ye yote.**
**4 Mkombozi wetu, Bwana wa majeshi ndilo jina lake,**
**Mtakatifu wa Israeli.**
**5 Kaa kimya, ingia gizani,**
**Ee binti wa Wakaldayo;**
**Maana hutaitwa tena Malkia wa falme.**
**6 Nalikuwa nimekasirika na watu wangu,**
**naliutia unajisi urithi wangu,**
**nikawatia mkononi mwako;**
**wewe hukuwatendea rehema;**
**uliwatia wazee nira yako, nayo nzito sana.**
**7 Ukasema, Mimi nitakuwa bibi milele;**
**hata hukuyatia hayo moyoni mwako,**
**wala hukukumbuka mwisho wa mambo hayo.**

**47:1 “Haya shuka”** Hii ni moja ya aina tatu za fasihi zilizotumiwa na manabii wa Kiebrania kupitishia ujumbe wao wa kiroho.

1. wimbo wa maombolezo
2. Uwanja wa baraza
3. Ahadi ya ufunuo

◙**"Ewe bikira binti Babeli"** Hii ni lahaja ya semiti ya ulinzi na ufasaha uliokithiri katika sitiari ya familia. Yeye (himaya ya Babeli mpya) aliyekuwa thabiti na kulindwa, sasa amekuwa sio salama na asiye lindwa.

◙**"keti mavumbini. . .keti chini pasipo kiti cha enzi"** hili ni neno kwa neno "keti" (kama vile. mist. 2[mara mbili],5,8 [mara mbili]). Ni moja ya ishara ya maombolezo ya uhalisia.

## MADA MAALUMU: IBADA KWA WALIO KATIKA HUZUNI

Waisraeli walieleza huzuni kwa mpendwa wao aliyefariki na toba binafsi, pamoja na makosa ya jinai yaliyofanyika kwa ujumla kwa njia kadhaa:

1. Kurarua mavazi, Mwa. 37:29,34; 44:13; Waamuzi. 11:35; 2 Sam. 1:11; 3:31; 1 Fal. 21:27; Ayubu 1:20
2. Kuvaa gunia, Mwa. 37:34; 2 Sam. 3:31; 1 Fal. 21:27; Yer. 48:37
3. Kuvua viatu, 2 Sam. 15:30; Isa. 20:3
4. Kuweka mikono kichwani, 2 Sam. 13:19;Yer. 2:37
5. Kuweka vumbi kichwani, Yos. 7:6; 1 Sam. 4:12; Neh. 9:1
6. Kuketi sakafuni, Omb. 2:10; Ezek. 26:16 (kulala chini, 2 Sam. 12:16); Isa. 47:1
7. Kupiga kifua, 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26; Nah. 2:7
8. Omboleza , 1 Sam. 25:1; 2 Sam. 11:26
9. Kata mwili, Kumb. 14:1; Yer. 16:6; 48:37
10. Kufunga, 2 Sam. 1:12; 12:16,21; 1 Fal. 21:27; 1 Nya. 10:12; Neh. 1:4
11. Kuimba na kusifu katika maombolezo, 2 Sam. 1:17; 3:31; 2 Nya. 35:25
12. Upara (nywele zilikatwa), Yer. 48:37
13. Kunyoa ndevu, Yer. 48:37
14. funika kichwa au uso, 2 Sam. 15:30; 19:4

Hizi zilikuwa ishara za nje kutokana na hisia za ndani

◙**"Wakaldayo"** Hii inafanana na "Babeli," tazama muhtasari katika 43:14.

◙**"Maana hutaitwa tena mwororo, mpenda anasa"** Maneno haya mawili (BDB 940 and 772) yametumika kwenye Kut. 28:56 kwa ajiri ya anasa, maisha ya ubadhirifu. Hii ni kinyume na mist wa . 2-3, ambapo sasa ni

1. mtumwa
2. kahaba

**47:2-3** Huu ni mfuatano wa tungo uliotumika kumwelezea yeye mmoja aliyekuwa malkia wa mataifa (mist. 5,7) na sasa ni mtumwa.

1. Alisaga unga, mst. 1
2. Alivua utaji wake, mst. 2
3. Aliandaa mavazi yake kwa ajiri ya kazi ngumu, mst. 2
4. Alipita katika mito ya maji mwenyewe bila kuvushwa (inawezekana huko uhamishoni), mst. 2
5. Uchi wake ulifunuliwa, mst. 3
   a. kama hukumu kwa ajiri ya dhambi (kama vile. 20:4)
   b. vazi baya lililopambwa kwa manukato mazuri na ukahaba

**47:3**
**NASB** **"na sitamkubalia mtu"**
**NKJV** **"sitapatanishwa na mtu"**
**NRSV** **"sitamhurumia mtu"**

**TEV** **"hakuna atakaye nizuia"**
**NJB** **"hakuna atakayesimama kwenye njia yangu"**
**JPSOA** **"hakuna mtu atakaye tetea"**
**REB** **"usionyeshe huruma kwa yeyote"**

Hii kwa kiasi fulani ni utata lakini neno (BDB 803) lina mahusiano na maelezo ya asili na historia ya neno kwa maombi ya kuombea (kama vile. 53:12; 59:16; Yer. 36:25).inaonekana ina maana kwamba hakuna hata mmoja anaeweza kuomba kwa ajiri ya Babeli au kwamba hakuna mwanadamu wenye maombi yenye nguvu ya kutosha kuzuia mpango alioamua YHWH kwa ajiri ya hukumu yake.

**47:4** Hili ni neno kutoka kwa mwandishi ambalo linaonyesha mshangao wake katika mtiririko wa shairi. Matatu kati ya majina mazuri ya Mungu yameonekana hapa kama ambavyo nabii anamsifu Mungu kuwa yeye ni nani . majina hayo ni

1. mkombozi – anatilia mkazo kwa Mungu kama mwokozi; ndiye yeye ambae anawanunua watu kutoka utumwani
2. Bwana wa Majeshi – cheo cha Uajemi kinacholenga moja ya maeneo mawili
    a. baraza takatifu, Isa. 24:21-22
    b. nyota ya uungu wa Babeli, Isa. 40:26
3. Mtakatifu wa Israeli – jina kwa ajiri ya Mungu ambae anapita kwa niaba ya watu wake.

**47:5 "Kaa kimya, ingia gizani"** Hii nguvu kuu ya ulimwengu sasa imekuwa mkulima. Aya hii inatuambia yeye anaangalia giza na kuwa kimya (KAULI SHURUTISHI mbili).

◙**"malkia wa falme"** Hii ni Nahau ya mtazamo wa Babeli mpya na nguvu zake. (kama vile. mst. 7). Malkia alikuja kuwa mtumwa wa ngono (kama vile. mist. 2-3,8a). kile alichokifanya uhamishoni sasa kitatokea kwake (yaani.,utabiri unasababishwa na msingi wa nyuma).

Na sasa inawezekana kwamba hii Nahau inasimulia kwa Nabonidus akiiongoza Babeli mpya kutoka kwa *Marduk* kwenda kumwabudu mungu mwezi aliyeitwa "malkia wa mbingu". Aliitwa *Sin* (Akkadian or *Nanna* (Summerian)

## MADA MAALUM: KUUABUDU MWEZI

Kuabudu mwezi kulikuwa ni simulizi iliyosambaa Mashariki Karibu ya kale ikianzia na Sumeri (ustaarabu wa kwanza unaojulikana). Kulikuwa na namna ya wote mwanamke na mwanaume kwenye simulizi. Kiasili mungu mwezi alikuja kutokana na ubakaji wa mungu mke wa ngano, *Ninlil* by *Enlil*, mungu wa anga. *Enlil* alifukuzwa nje ya miungu na kuhukumiwa chini ya ulimwengu kwa matendo yake, lakini wakati*Ninlil* alipojua kwamba alikuwa na mtoto alijiunga naye. Mtoto, *dhambi*(au*Zin*), alikubaliwa kupanda katika anga kila usiku.

Kuabudu mwezi kulikusudiwa katika vipindi/hatua tofauti tofauti:

1. Mwezi mpya – *Asimbabbar*
2. Mwezi mmeguko – *Sin*
3. Mwezi wote – *Nana*(ki-Sumeria "kuangaziwa" kutoka*En-su*, "bwana wa hekima")

Majina haya kimsingi yanamaanisha "bwana mwenye hekima" (yaani *Suen*) au "kumulikia" (*Nanaa*), waliabudu katika Uru ya Wakaldayo. Jiji lenyewe mara kwa mara liliitwa Nannar. Jozi zenye rutuba ziliabudiwa katika ziggurats (piramidi kubwa zilizo tambarare juu) zilizokuwa katika mji. Yule Mungu jua (*Shamash*) alikuwa mzaliwa wa kwanza kwa wenzi na baadaye *Ereshkigal* (malkia wa ulimwengu wa chini) na*Inanna* (Malkia ya anga/mbingu).

Ibada/ dini ilisambaa maeneo yote ya Kusini Mashariki ya Mashariki ya Karibu ya kale, lakini maeneo makubwa na vituo vikubwa vilikuwa ni

1. Uru
2. Harani

3. Tema
4. Kanaani
5. Makka

Kimsingi hadithi hii imeunganisha na mkazo wa ustawi pamoja na kuabudu vitu vya anga.

**47:6 "Nalikuwa nimekasirika na watu wangu"** Hii inafafanua ni kwa nini Wayahudi wlipelekwa uhamishoni. Katika ulimwengu wa kale uungu wa taifa uliwalinda. Jambo la kweli ni kwamba wote Israeli na Yuda walichukuliwa mateka ilionekana na ulimwengu kama miungu ya mwezi mpevu ina nguvu sana kuliko Mungu wa Israeli, lakini hili sio tatizo. Mungu hutumia nguvu za miungu ya mwezi mpezu kuwahukumu watu wake kwa dhambi zao (kama vile.42:24).

◙**"wewe hukuwatendea rehema;"** Ingawa Mungu aliwapa Ashuru na Babeli watu wake ili kuwaadhibu, waliwaadhibu kwa ukali zaidi na sasa watahukumiwa kwa kutokuwa na rehema juu yao.

**47:7 "hata hukuyatia hayo moyoni mwako,**
**wala hukukumbuka mwisho wa mambo hayo."**

VITENZI hivi viwili ni *Qal* KAULI ZA WAKATI TIMILIFU, ambavyo vinadokeza mtizamo wa makazi.

1. Hakufikilia , kifasihi. "hukuyatia moyoni mwako"
2. Wala hukukumbuka mwisho wao

tambua kwa jinsi gani mst. 8 unaendeleza fikra.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:8-11**

**8 Sasa, basi, sikia haya, wewe upendaye anasa,**
**ukaaye na kujiona salama,**
**wewe usemaye moyoni mwako,**
**Mimi ndiye, wala hapana mwingine zaidi yangu mimi;**
**sitaketi mfano wa mjane,**
**wala sitajua kufiwa na watoto;**
**9 lakini mambo haya mawili yatakupata katika dakika moja siku moja,**
**kufiwa na watoto, na ujane;**
**yatakupata kiasi kitimilifu,**
**uchawi wako ujapokuwa mwingi,**
**na uganga wako mwingi mno.**
**10 Maana umeutumainia ubaya wako; umesema,**
**Hapana anionaye;**
**hekima yako, na maarifa yako yamekupotosha,**
**nawe umesema moyoni mwako,**
**Mimi ndiye, wala hapana mwingine zaidi yangu mimi.**
**11 Kwa sababu hiyo ubaya utakupata;**
**wala hutajua kutopoa kwake;**
**na msiba utakuangukia;**
**hutaweza kuuondoa;**
**na ukiwa utakupata kwa ghafula,**
**usioujua.**

**47:8-9 "ukaaye na kuijiona salama. . . lakini mambo haya mawili yatakupata katika dakika moja siku moja "** inaonekana kutoka Danieli 5 na kutoka kwa Herodotus kwamba watu wa Babeli walicheka lilipokuwa likijitokeza jeshi la Uajemi. Hata hivyo, jeshi la Uajemi waliugeuza mkondo wa maji wa mto Eufrate, na kupita chini ya kuta za mji huu muhimu uliotukuka, na siku moja mji uliangamizwa (kama vile. Daniel 5). Watu wa Babeli waliona Uajemi

kama wakombozi kwa sababu ya Belshazzar na Baba yake, Nabonidus, walianza kumwabudu miungu migeni aliyeitwa *Sin* (*Nanna*, tazama mada maalum katika 47:5) na Cyrus aliwaruhusu kurudi katika Uungu wa asili—*Bel*, *Marduk*, na *Nebo*.

**47:8 "Mimi ndiye, wala hapana mwingine zaidi yangu mimi;"** Hii ni changamoto ya wazi kwa YHWH (kama vile. mst. 10). Nani aliyewakomboa watu wake? Nani aliye wa kweli?, Mungu wa pekee"

**47:9 "kufiwa na watoto"** muhtasri Isa. 13:16,18. Kile alichokifanya kwa wengine kinatokea kwake!

◙**"uchawi wako ujapokuwa mwingi. . .uganga wako mwingi mno"** mkazo wa mazoea ya imani ya Kibabeli, yanafanya kuwa bayana hapa katika mst. 9, na inaendelea katika mist. 11-13. Mazoea haya yalishutumiwa katika Kumb. 18:9nakuendelea. Uchawi wote wa Babeli haukuweza kumlinda , ambao ulionyesha matendo maovu na kuathiriwa kwa mazoea ya imani (yaani., udhaifu wa miungu yake).

**47:10 "umetumainia ubaya wako"** Hati ya kukunjwa ya bahali ya Shamu "ubaya" kwa kubadilisha "d" kwenda "r," ambalo lina maana "ufahamu." Huenda haya maneno yakafaa muktadha.

◙**"hapana anionaye"** Hii inadokeza kwamba walifahamu ni nini walichokuwa wanatenda ni machukizo na kujaribu kujificha wao wenyewe (kama vile. Isa. 29:15).

**47:11 "kutopoa"** Hii ina maana "toa hongo." Kutopoa uchawi hauwezi kumshawishi YHWH (kama vile. mst. 3c).

◙**"kuuondoa"** Hili ni neno la Kiebrania "kufunika" na limetumika katika Agano la kale kama dhana ya upatanisho kwa namna ya kiti cha rehema kufunikwa na damu (kama vile. Law 16).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 47:12-15**
**12 Simama sasa na uganga wako,**
**na wingi wa uchawi wako,**
**uliojitaabisha nao tangu ujana wako;**
**labda utaweza kupata faida,**
**labda utaweza kushinda.**
**13 Umechoka kwa wingi wa mashauri yako;**
**basi, na wasimame hao wajuao falaki,**
**wazitazamao nyota,**
**watabirio kila mwezi mambo ya mwezi huo,**
**wakakuokoe na mambo yatakayokupata.**
**14 Tazama, watakuwa kama mabua makavu;**
**moto utawateketeza;**
**hawatajiokoa na nguvu za mwali wa moto;**
**hautakuwa kaa la kukota moto,**
**wala moto wa kukaa karibu nao.**
**15 Ndivyo yatakavyokuwa mambo hayo uliyojitaabisha nayo;**
**wale waliofanya biashara nawe tangu ujana wako**
**watatanga-tanga mbali nawe, kila mtu akienda zake;**
**hapatakuwa na mtu wa kukuokoa.**

**47:12 "labda utaweza kushinda"** Leupold anaongeza neno "mimi" kuonyesha uwezekano kwamba Mungu anawaambia waone kama uganga wao unaweza kumtisha yeye au kumsababisha yeye atikisike. Hii inaonekana ndio maana ya kifungu hiki. labda, hata hivyo, inarejelea jeshi la Uajemi (NJB).

**47:13** Sio tu miungu ya Kibabeli haina msaada na yenye kutia aibu, (kama vile. mist. 1-3,5), lakini pia hata manabii na washauri/wachawi wake (kama vile. mst. 14).

◙

**NASB, NKJV,**
**LXX "ushauri"**
**NRSV, NJB "washauri"**
**TEV "shauri"**

Hili ni neno mojawapo la Kiebrania (BDB 420) kwamba limetafsiriwa "kusudi" katika 46:10,11. Hii labda ni taswira kati ya mipango ya YHWH/makusudi yake yatapita na makosa, udhaifu, mipango iliyoharibika/makusudi ya viongozi wa kidini wa Babeli!

hakuna wa "kumshauri" YHWH (kama vile. 40:13).daima anaitimiza mipango yake (kama vile. 44:26; 46:10.11).

◙

**NASB, NKJV,**
**TEV, NJB,**
**LXX "watazama nyota"**
**NRSV "wanaojifunza mbinguni"**
**JPSOA "wasoma mbingu"**
**Peshitta "wakaldayo"**
**Emphasized Bible "wagawa mbingu"**

Toleo la MT lina *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFUya BDB 211, KB 237 (*ketiv*), ambalo linaonekana lina maana "kugawa" kutoka kwenye asili ya Kiarabu. Wanazuoni wa Kimasoreti wanashauri kwamba *Qal* KAULI ENDELEVU ya asili moja ya kuchunguza (*qere*). Kama ndio ukweli basi unafanana na "wale wachunguza nyota" (yaani ,wanajimu).

**47:14 "tazama hawatakuwa kaa la kukota moto,**
**wala moto wa kukaa karibu nao."**
Moto hapa umetumika kama hukumu juu ya imani ya mazoea ya Babeli. Moto hutumika majumbani kwa makusudi ya kupikia chakula na kutupatia joto, lakini moto huu utakuwa moto wa hukumu.

# MADA MAALUM: MOTO (BDB 77, KB 92)

Moto unavyo vidokezo chanya na hasi katika maandiko.

A. Chanya
   1. Husisimua (kama vile Isaya 44:15; Yohana 18:18)
   2. Huwasha nuru (kama vile Isaya 50:11; Mt. 25:1-13)
   3. Hupikia (kama vile Kut. 12:8; Isay 44:15:16; Yohana 21:9)
   4. Husafisha (kama vile Hes. 31:22-23; Mit. 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer. 6:29; Malaki 3:2-3)
   5. Utakatifu wa Mungu (kama vile Mwa 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Eze. 1:27; Waebrania 12:29)
   6. Uongozi wa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes. 14:14; Wafalme 118:24)
   7. Uwezeshaji wa Mungu (kama vile. Matendo 2:3)
   8. Ulinzi wa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)
B. Hasi
   1. Huunguza (kama vile Yos. 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7
   2. Huangamiza (kama vile Mwa. 19:24; Walawi 10:1-2)
   3. Hasira (kama vile Hes 21:28; Isay 10:16; Zek 123:6)

4. Adhabu (kama vile Mwa. 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17
5. Ishara ya mbaya ya siku ya mwisho (kama vile.Ufunuo 13:13)

C. Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi mara nyingi hudhihirishwa kwa tanuru ya moto.
   1. Hasira yake huunguza (Kama vile Hos. 8:5; Sefania 3:8)
   2. Humimina moto (kama vile Nah. 1:6)
   3. Moto wa milele (kama vile Yer. 15:14; 17:4; Mt 25:41; Yuda aya ya 7)
   4. Hukumu ya siku ya mwisho (kama vile Mt. 3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; The. 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu. 8:7; 16:8; 20:14-15)

D. Moto mara nyingi huonekana katika tanuru
   1. Mwa.15:17
   2. Kutoka 3:2
   3. Kutoka 19:18
   4. Zaburi 18:7-15; 29:7
   5. Eze. 1:4, 27; 10:2
   6. Ebr. 1:7; 12:29

E. Kama sitiari yingi katika Biblia (yaani, chachu, simba) moto unaweza kuwa Baraka au kufuatana na mazingira au muktadha.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri. Hii inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Kuna uhusiano gani kati ya Isa. 45:23 na 46:1-2?
2. Kuna mchezo gani wa maneno kati ya Isa. 46:1-2 na 46:3-4?
3. Taja njia ambazo zimetiliwa mkazo na waamini wa Mungu mmoja katika Isaya 46 na 47.
4. Ni kwa namna gani 46:8 ina vitu vya kufanana na Isa. 46:12?
5. Ni kwa namna gani mmoja anaweza kupatanishwa na utawala wa Mungu katika historia na utawala wa mwanadamu?
6. Kwa nini katika Isa. 46:12-13 ni muhimu kwa dhana yetu ya haki kwa imani?
7. Taja njia ambazo Babeli iliangamizwa kutoka kwenye anasa hadi kwenye utumwa.
8. Taja aina ya mzoea ya imani yanayopatikana katika Isa. 47:9-13.

# ISAYA 48

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ukaidiwa Israeli Kusikia na Kuona kila Kitu | Israeli Anauona Utukufu wa Mungu | Kusikia na Kuona | Mungu ni Bwana wa nyakati zijazo | Yahweh Ametabiri kila kitu |
| 48:1-11 (1-11) | 48:1-2 (1-2) | 48:1-2 (1-2) | 48:1-2 (1-2) | 48:1-11 (1-11) |
| | 48:3-5 (3-5) | 48:3-5 (3-5) | 48:3-5 (3-5) | |
| | 48:6-8 (6-8) | 48:6-8 (6-8) | 48:6-8 (6-8) | |
| | 48:9-11 (9-11) | 48:9-11 (9-11) | 48:9-11 (9-11) | |
| Ukombozi Uliohaidiwa | Mpango wa Kale wa Mungu Wa Kuikomboa Israeli | | Koreshi, Mtwala aliyechaguliwa na Bwana | Yahweh Amemchagua Koreshi |
| 48:12-16 (12-16) | 48:12-13 (12-13) | 48:12-13 (12-13) | 48:12-13 (12-13) | 48:12-15 (12-15) |
| | 48:14-16 (14-16) | 48:14-16 (14-16) | 48:14-15 (14-15) | Hatima ya Israeli |
| 48:16 (16a) | | | | |
| Bwana, Anao Mpango Kwa watu wake | | | | |
| 48:17-19 (17-19) | 48:17-19 (17-19) | 48:17-19 (17-19) | 48:17 (17) | |
| 48:18-19 (18-19) | Mwisho wa Uhamisho | | | |
| 48:20-22 (20-22) | 48:20-21 (20-21) 48:22 (22) | 48:20-22 (20-22) | 48:20-22 (20-22) | 48:20-22 (20-22) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA.

A. Kama YHWH anavyoiasa Babeli katika sura ya 46 na 47, na sasa anawaasa watu wake, waliorejea, mabaki yake ya uaminifu.
B. Tambua namna tofauti ambazo zinairejelea Israeli.
   1. nyumba ya Yakobo, mst. wa 1
   2. mnaoitwa kwa jina la Israeli, mst. wa 1
   3. mliotoka katika maji ya Yuda, mst. wa 1
   4. mnaoapa kwa jina la Bwana, mst. wa 1
   5. na kumtaja Mungu wa Israeli, mst. wa 1
   6. wewe u mkaidi, mst. wa 4
   7. na shingo yako ni shingo ya chuma, mst. wa 8
   8. Ee Yakobo, mist. ya 12,20
C. Angalia majina tofautitofauti na vianishi vya YHWH
   1. jina la Bwana**,** mst. wa 1
   2. Mungu wa Israeli, mist. ya 1,2
   3. mimi ndiye, mst. wa 12
   4. Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho pia, mst. wa 12
   5. Bwana (YHWH), mist. ya 14,17,20,22
   6. Bwana MUNGU(*Adon* YHWH), 16
   7. Mkombozi, mst. wa 17
   8. mtakatifu, mst. wa17
   9. Bwana Mungu wako, mst. wa 17
D. Kuna mistari yenye maana kadhaa na yenye umuhimu kithiolojia katika kipengele cha Isaya ambayo itafafanuliwa katika Agano Jipya.
   1. 45:23
   2. 46:8-11
   3. 48:8-11
   4. 48:16
E. Leupold anaiita surah ii kwa jina la "A Sharp Rebuke and a Gracious Challenge" (uk. 158). Hii kazi iliyo kati ya hukumu na huruma inainisha fasihi ya kinabii na inatokea kwa uchache au pasipo mabadiliko.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 48:1-11** |
|---|

**[1]Sikieni haya, enyi watu wa nyumba ya Yakobo, mnaoitwa kwa jina la Israeli,**
**mliotoka katika maji ya Yuda;**
**mnaoapa kwa jina la Bwana,**
**na kumtaja Mungu wa Israeli,**
**lakini si kwa kweli, wala si kwa haki.**
**[2] Maana hujiita wenyeji wa mji mtakatifu,**
**hujitegemeza juu ya Mungu wa Israeli; Bwana wa majeshi ni jina lake.**
**[3] Mimi nimehubiri mambo ya kale tangu zamani;**
**naam, yalitoka katika kinywa changu, nikayadhihirisha;**
**naliyatenda kwa ghafula, yakatokea.**
**[4]Kwa sababu nalijua ya kuwa wewe u mkaidi,**
**na shingo yako ni shingo ya chuma,**
**na kipaji cha uso wako ni shaba;**
**[5]basi nimekuonyesha tangu zamani;**
**kabla hayajatukia nalikuonyesha; usije ukasema,**
**Sanamu yangu imetenda haya;**
**sanamu yangu ya kuchonga, na sanamu yangu ya kuyeyusha, imeyaamuru.**
**[6]Umesikia haya; tazama haya yote;**
**nanyi, je! Hamtayahubiri? Nimekuonyesha mambo mapya tangu wakati huu,**
**naam, mambo yaliyofichwa, usiyoyajua.**
**[7]Yameumbwa sasa, wala si tokea zamani;**
**na kabla ya siku hii ya leo hukusikia habari yake;**
**usije ukasema, Tazama, naliyajua.**
**[8]Naam, hukusikia; naam, hukujua;**
**naam, tokea zamani sikio lako halikuzibuka;**
**maana nalijua ya kuwa wewe watenda kwa hila nyingi,**
**nawe umeitwa mkosaji tangu kuzaliwa kwako;**
**[9]kwa ajili ya jina langu nitaahirisha hasira yangu,**
**na kwa ajili yako nitajizuia, ili nisifiwe, wala nisikukatilie mbali.**
**[10]Tazama, nimekusafisha, lakini si kama fedha;**
**nimekuchagua katika tanuru ya mateso.**
**[11]Kwa ajili ya nafsi yangu, kwa ajili ya nafsi yangu, nitatenda haya;**
**je! Litiwe unajisi jina langu?**
**Wala sitampa mwingine utukufu wangu.**

**48:1 "sikieni"** Hii ni KAULI SHURUTISHI ya kawaida (BDB 1033, KB 1570) kwa Isaya, pamoja na Kumbukumbu la Torati, Wafalme, Ayubu, Zaburi, na Amosi, kuanza katika kipengele kipya (kama vile 1:2,10; 7:13;28:22; 36:13; 37:17; 47:18;46:3,12; 47:8; 48:1,2,14,16; 49:1; 51:1,7; 55:2; 66:5). YHWH anahitaji ujumbe wake "usikike" na "kuishi kwa huo." Ufunuo unahitaji utii! Ukweli si wa kifikratu bali ni wa maisha!

**NASB, NRSV** **"enyi watu wa Yuda"**
**NKJV** **"enyi chemchemi za Yuda"**
**TEV** **"enyi mnaotokana na uzao wa Yuda"**
**NJB** **"wenye asili ya maji ya Yuda"**

Kuna maneno matatu ya Kiebrania ambayo yanajaribu kutoa ufafanuzi wa andiko hili

1. "maji," וממי (toleo la UBS Text Project linalipa neno hili daraja "B" )
2. "watu," וממעי (NASB, NRSV, AB)
3. "uzao," ומזרע

Haya maneno yote ya Kiebrania ni ya kistiarai kwa maana ya asili ya vizazi vya kundi fulani, kabila, familia. Tambua kwamba vizazi vyote vinasawiriwa kwa majina ya

1. Yakobo
2. Israeli
3. Yuda

Kipengele hiki kinamaanisha kwamba walioreka (hasa makabila matatu kutoka kusini yanayoitwa Yuda) kutoka uhamishoni. Sasa Israeli inaurejelea uzao wotw wa Ibrahimu, kama ilivyofanyika kabla ya Umoja wa falme uliokuwepo kabla ya kugawanyika mnamo mwaka 922 K.K.

◙**"mnaoapa. . . kumtaja"** Hivi VITENZI vyote vinayarejeea matendo ya ibada.

1. Mnaoapa kwa jina (kama vile 19:18; 65:16)
2. mtaja (kif. "sababisha kukumbuka," *Hiphil* , kama vile 12:4; 26:13; 62:6)

◙

**NASB, NKJV,**
**LXX "lakini si kwa kweli, wala si kwa haki"**
**NRSV "lakini si katika kweli au haki"**
**TEV "lakini hamlimaanisha neno mnalolisema"**
**NJB "ijapokuwa si katika imani njema au kwa unyoofu"**
**JPSOA "ingawa si katika kweli na utiifu"**
**REB "lakini pasipo uaminifu na utiifu"**

Ole, ni lalamiko la namna gani la tathmini ya ibada za Israeli! Hili neno "kweli" ni אמת(BDB 54) na linamaanisha "uaminifu." Angalia Mada Maalum katika 42:3.

Kwa maelezo ya neno la pili, דקה׳ (BDB 842) angalia Mada Malum hapa chini.

## MADA MAALUM : HAKI

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenyewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsi ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsi ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae . Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko,hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

A. <u>kutangaza</u> haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
B. <u>kwa kutoa haki</u> huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)
C. <u>kumtoa</u> Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
D. <u>kurejesha</u> ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi

5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

A. toba
B. imani
C. utii kwenye stadi ya maisha
D. ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, uliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo.Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano(tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana).Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [ utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

A. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
    1. Warumi 3:26
    2. 2 Wathesalonike 1:5-6
    3. 2 Timotheo 4:8
    4. Ufunuo 16:5
B. Yesu ni haki
    1. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
    2. Mathayo 27:19
    3. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
C. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki.
    1. Mambo ya Walawi 19:2
    2. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
D. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
    1. Warumi 3:21-31
    2. Warumi 4

3. Warumi 5:6-11
4. Wagalatia 3:6-14
5. Iliyotolewa na Mungu
    a. Warumi 3:24; 6:23
    b. 1 Wakorintho 1:30
    c. Waefeso 2:8-9
6. Iliyopokelewa kwa imani
    a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
    b. 2 Wakorintho 5:7,21
7. kupitia matendo ya Mwana
    a. Warumi 5:21
    b. 2 Wakorintho 5:21
    c. Wafilipi 2:6-11

E. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
1. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
2. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
3. Waefeso 1:4; 2:10
4. 1 Timotheo 6:11
5. 2 Timotheo 2:22; 3:16
6. 1 Yohana3:7
7. 1 Petro 2:24

F. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
1. Matendo 17:31
2. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

A. agizo la Mungu
B. zawadi ya Mungu
C. tendo la Kristo

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasisitiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

A. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
B. injili ni ukweli (msisitizo wa Augustine na Luther)
C. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

**48:2** Hii mistari miwili ya kwanza inanikumbusha juu ya Mahubiri ya Yemia “ndani ya Hekalu” katika Yeremia 7, ambapo Waisraeli waliliamini hekalu lakini si YHWH.

1. walijikusanya baada ya mji mtakatifu (BDB 894, KB 1128, *Niphal ya* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile mst. wa 1)

2. walikuwa wakijifunza (BDB 701, KB 759, *Niphal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU)

Ibada zao zionekana kuwa na misingi ya imani na za mwenendo mwema lakini zilikuwa za uongo na zilikuwa na uelekeo wa kuwa na chimbuko baya.

**48:3** Kwa mara nyingineYHWH anauzungumzia (tambua idadi ya "Mimi'") juu ya utawala na historia yake. Anatumia utabiri wa unabii ili kuwaonyesha watu wake uwepo na uweza wake.

**48:4** YHWH anawafafanua watu wake kama
1. wakaidi (kama vile Eze. 2:4; 3:7)
2. wenye shingo kali kama chuma
3. vipaji vya nyuso zao ni vya shaba

◙**"nalijua"** Hili neno (BDB 393, KB 390) limetumika mara kadhaa katika sura hii (kama vile 48:4,6,7,8 [mara mbili]), ambapo neno hili liamaanisha "maarifa yahusuyo," lakini lazima limaanishe "ushirika wa karibu na "

**48:6** Kuna baadhi ya maswali kuhusu namna VITENZI vya mistari miwili ya kwanza vinavyopaswa kutafsiriwa. Nalipenda toleo la NJB,"Mmesikia na kuyaona haya yote, kwa nini hamkuyakiri?" Hili neno"yakiri" linaurejelea utabiri wa YHWH (kama vile mst. wa 5). YHWH anautoa uwepo wake kupitia maarifa yake na utawala wa matukio yajayo yanaiyagusa mataifa yote si Israeli/Yuda pekee.

**48:8"watenda kwa hila nyingi"** Huu muundo wa kisarufi wenye uchochezi ni *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU na *Qal* ya KITENZI JINA HALISI cha asili ile ile (BDB 93, KB 108).

◙**"nawe umeitwa mkosaji tangu kuzaliwa kwako"** Angalia Kumb. 9:7. Katika wakati wa kuondoka Misri, Israeli bado ilikuwa ikiabudu sanamu (yaani, Eze. 20:8,13; Amosi 5:25-26).

**48:9** Huu ni muhtasari mzuri wa tatizo naYHWH na uzao wa Ibrahimu. Yeye alitaka kuwatumia ili waweze kumjua na kuja kwake (kama vile Mwa. 12:3, angalia Mada Maalum katika 40:15). Lakini hawakuwa waaminifu. Yeye anadai kuwa, "kila nafsi itendayo dhambi itakufa" yaani, Mwa. 2:16,17; Eze. 18:4,20). Na sasa neno la Mungu na kusudi la Mungu linageuka kuwa mvutano. Yeye atachagaua kutenda kwa ajili ya mema yaliyo makuu (yaani, wokovu wa wanadamu wote, kama vile I Sam. 12:22; Zab. 106:8; Yer. 14:7; Eze. 20:8-9,14,17). Andiko ambalo linatoa ubainishaji mzuri kuhusiana na kipengele hiki ni Eze. 36:22-38! YHWH anatenda juu ya Israeli kwa ajili ya kusudi lake lililo kuu! Je! Hiki si kile ambacho Isa. 48:11 inakikiri? Huu ni ujumbe wa ajabu wa Isaya. Angalia Mada Maalum katika 40:15.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 48: 12-16**

**12 Nisikilize mimi, Ee Yakobo; na Israeli, niliyekuita;**
**mimi ndiye. Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho pia.**
**13 Naam, mkono wangu umeuweka msingi wa dunia,**
**na mkono wangu wa kuume umezitanda mbingu;**
**niziitapo husimama pamoja.**
**14 Kusanyikeni, ninyi nyote, mkasikie; ni nani miongoni mwao aliyehubiri haya?**
**Bwana amempenda; atatimiza mapenzi yake juu ya Babeli,**
**na mkono wake utakuwa juu ya Wakaldayo.**
**15 Mimi, naam, mimi, nimenena; naam, nimemwita;**
**nimemleta, naye ataifanikisha njia yake.**
**16 Nikaribieni, sikieni haya; tokea mwanzo sikunena kwa siri;**
**tangu yalipokuwapo, mimi nipo;**
**na sasa Bwana MUNGU amenituma, na roho yake.**

**48:12"Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho pia"** Hii ni nahau inayotumika mara kwa mara katikaIsaya (kama vile 41:4; 44:6) na inakuwa kielelezo cha kawaida kwa Kristo katika Ufu. 1:8,17; 22:13! Hii inadaokeza juu ya Mungu wa uumbaji (mst. wa 13) na umilele wake. Umilele uliokuwepo, umilele utakao kuwepo. Mungu wa pekee ndiye YHWH (angalia Mada Maalum: Imani ya Mungu Mmoja katika 40:14).

**48:14** Hizi KAULI SHURUTISHImbilizamstari wazinarudiwa katika mst. wa 16, mshororo wa 1.

Pia tambua ufanano uliopo kati ya kifungu cha "Bwana amempenda" na "Mkono wake ." Koreshi ni chombo cha Mungu dhidi ya Babeli badala ya Israeli.

**48:15** Kifungu cha kwanza ("Mimi, naam, mimi, nimenena," BDB 180, KB 210, *Piel*ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ni njia ya kuikubali nguvu ya neno lililozungumzwa na YHWH (kama vile 55:11). Kusudi lake haliwezi kupingwa kupingwa!

**48:16**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"na sasa Bwana MUNGU amenituma, na roho yake"** |
| **NKJV** | **"na sasa Bwana MUNGU na roho yake wamenituma"** |
| **NRSV** | **"na sasa Bwana MUNGUamenituma na roho yake"** |
| **TEV** | **"Na sasa BWANA aliye Mkuu ameniwezesha na kunituma"** |
| **NJB** | **"na sasa Bwana Mwenyezi amenituma kwa roho yake"** |
| **JPSOA** | **"na sasa Bwana MUNGU amenituma, aliyetukuzwa kwa roho yake"** |
| **LXX** | **"na sasa BWANA ameanituma na roho yake"** |

La haulaa! Ni nafsi ngapi na ni nani ambao wamekuwa wakitajwa? Nani anenaye ? Ni dhahiri kuwa mmoja wao ni YHWH. Huenda roho wake ni sawa na yule anayezungumzwa katika Mwa 1:2; Isa. 11:2; 42:1; 61:1. Lakini "ndiye" ni nani?

1. "Mimi" wa mshororo wa 3
2. nabii Isaya
3. Masihi (au Mtumishi)
4. Koreshi II (kama anavyozungumza) Wakristo wanaweza kuuona Utatu ndani ya andiko hili (angalia Mada Maalum katika 40:13). Hizi nafasi tatu zinazofanana zinatajwa kwa mara nyingine katika 61:1. Angalia Mada Maalum: Utu wa Roho katika 42:1.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 48: 17-19**
**17Bwana, mkombozi wako, mtakatifu wa Israeli, asema hivi;**
**Mimi ni Bwana, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida,**
**nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata.**
**18 Laiti ungalisikiliza amri zangu!**
**Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji,**
**na haki yako kama mawimbi ya bahari;**
**19Tena wazao wako wangalikuwa kama mchanga,**
**na hao waliotoka katika tumbo lako kama chembe zake;**
**jina lake lisingalikatika, wala kufutwa mbele zangu.**

**48:17 "Bwana, mkombozi wako,mtakatifu wa Israeli"** Hili ni jina la mara kwa mara katika kipengele hiki chaIsaya (kama vile 41:14; 43:14; 49:7,26; 54:5,8). Jina hili linaelezwa katika utofauti wa namna fulani lakini namna ya ufanano katika 49:26,

◙**"Bwana, mkombozi wako, mtakatifu wa Israeli."** Angalia Mada Maalum : Majina ya Uungu katika 40:3.

◙**"nikufundishaye ili upate faida"**Hili neno "faida" (BDB 418 I, *Hiphil* ya TUNGO YA KITENZI JINA HALISI) katika maana ya manufaa (kama vile Ayubu 21:15; 35:3; Yer. 12:13; Isa. 47:12). Mara nyingi neno hili linatumika katika

kuainisha kuwa sanamu haziwezi kufanya lo lote kwa yule aziabuduo (kama vile 44:9,10; 57:12; I Sam. 12:21; Yer. 2:8; 7:8,11; 23:32; Hab. 2:18).

◙**"nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata"** Hii ni nahau ya Kisemiti yenye kuzungumzia maisha ya haki kama "njia njema" (kama vile Zab. 32:8; 119:105). Hapa huenda kifungu hiki kinaurejelea uwepo wa YHWH na yeye kuifanya njia ya kutoka uhamishoni (kama vile mst. wa 20; 49:9-10).

**48:18-19** Hili ni andiko la " ngali. . ." ambalo linalirejelea agano la Baraka na laana za Mambo ya Walawi 26 na Kumbukumbu la Torati 27-29. Israeli ilitenda dhambi na ilirudia kusababisha matokeo mabaya zaidi. Huyu aliumbwa kwa haki na ufunuo, lakini kutotii kwake na kuabudu sanamu kulileta matokeo ya kuwepo giza na mkanganyiko.

| |
|---|
| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 48: 20-22**<br>**20 Haya, tokeni katika Babeli, Kimbieni kutoka kwa Wakaldayo;**<br>**Hubirini kwa sauti ya kuimba, tangazeni haya,**<br>**Yatamkeni mpaka mwisho wa dunia,**<br>**semeni, Bwana amemkomboa mtumishi wake, Yakobo.**<br>**21 Wala hawakuona kiu alipowaongoza jangwani;**<br>**Alitoa maji katika mwamba kwa ajili yao;**<br>**Pia akaupasua mwamba, maji yakatoka kwa nguvu.**<br>**22 Hapana amani kwa wabaya, asema Bwana.** |

**8:20** Huu ni mtiriko wa maagizo ya kurudi kwa Wayahudi waliokuwa uhamishoni.
1. tokeni katika Babeli – *Qal* yaKAULI SHURUTISHI (BDB 422, KB 425)
2. Kimbieni kutoka kwa Wakaldayo – *Qal* ya KAULI SHURUTISHI (BDB 137, KB 156)
3. Hubirini kwa sauti ya kuimba – *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI (BDB 616, KB 665)
4. tangazeni haya – *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI (BDB 1033, KB 1570)
5. Yatamkeni mpaka mwisho wa dunia – *Hiphil* ya KAULI SHURUTISHI (BDB 422, KB 425)
6. semeni . . . – *Qal* ya KAULI SHURUTISHI (BDB 55, KB 65)

YHWH anawaasa watu wake kuondoka uhamishoni na kurudi nyumbani. Yeye analitangaza kusudi lake kwa ulimwengu (kama vile 62:11; Yer. 31:10; 50:2) na ya kwamba amelitimiza! Anawataka watu wote wamjue ili yeye (kama vile 2:2-4; 42:6; 45:22-23; 51:4-5; 60:1,3; Matendo 13:46-49)!

**48:21** Safari ya kurudi kutoka uhamishoni Ashuru na Babeli ilionekana kama safari na kutangatanga nyikani. YHWH atawapa kila hitaji yao. Yeye atakuwa pamoja nao kama alivyokuwa pamoja na Waisraeli katika kipindi cha safari.

**48:22** Huu ni usemi ulio katika muhtasari ambao unahusiana na wale wasioamini, waabudu sanamu (kama vile 57:21; 59:8). Pito lo lote lisilokuwa naYHWH ni pito la uharibifu na uozo. Tendo la kufanua uamuzi huu, katika Agano la Kale linajulikana kama "njia mbili" (kama vile Kumb. 30:15; Mit. 4:10-19; Yer. 21:8; Mt. 7:13-14).

# ISAYA 49

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Wokovu unafika Miisho ya Dunia | Mtumishi,nuru ya mataifa | Wimbo wa pili wa mtumishi | Israeli,nuru ya mataifa | Wimbo wa pili wa mataifa |
| 49:1-4<br>(1-4) | 49:1-2<br>(1-2) | 49:1-4<br>(1-4) | 49:1-3<br>(1-3) | 49:1-7<br>(1-7) |
| | 49:3-4<br>(3-4) | | | |
| | | | 49:4-5<br>(4-5) | |
| 49:5-7<br>(5-7) | 49:5-6<br>(5-6) | 49:5-6<br>(5-6) | | |
| | | Kurudi na urejesho | 49:6<br>(6) | |
| | 49:7<br>(7) | 49:7<br>(7) | 49:7a<br>(7a) | |
| | | | 49:7b<br>(7b) | |
| | | | Urejesho wa Yerusalem | Shangwe ya kurudi nyumbani |
| 49:8-13<br>(8-13) | 49:8-9a<br>(8-9a) | 49:8-12<br>(8-12) | 49:8-10<br>(8-10) | 48:8-12<br>(8-12) |
| | 49:9b-12<br>(9b-12) | | | |
| | | | 49:11-16<br>(11-16) | |
| | 49:13<br>(13) | 49:13<br>(13) | | 49:13-17<br>(13-17) |
| Ahadi juu ya Sayuni | Mungu atamkumbuka Sayuni | | | |
| 49:14-21<br>(14-21) | 49:14-18<br>(14-18) | 49:14-18<br>(14-18) | | |
| | | | 49:17-18<br>(17-18) | |
| | | | | 49:18-22<br>(18-22) |
| | 49:19-21<br>(19-21) | 49:19-21<br>(19-21) | 49:19-21<br>(19-21) | |
| 49:22-23<br>(22-23) | 49:22-23<br>(22-23) | 49:22-23<br>(22-23) | 49:22-23<br>(22-23) | |
| | | | | 49:23-26<br>(23-26) |
| 49:24-26<br>(24-26) | 49:24<br>(24) | 49:24-26<br>(24-26) | 49:24<br>(24) | |
| | 49:25-26<br>(25-26) | | 49:25-26<br>(25-26) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

A. Kipengele cha fasihi katika Isaya 40-66 kinalenga urejesho wa Mungu kwa watu wake kupitia kazi ya "mtumishi wake" (kama vile. Sura 49-57).

B. Kifungu hiki kinafahamika kama wimbo wa pili wa mtumishi. Tazama orodha kamili ya nyimbo/mashairi katika utangulizi wa Sura ya 42, A.

C. Sura hii ina ukweli muhimu kadhaa. 1. Mungu aliandaa mwokozi/mtumishi maalum 2. Huyu mtumishi maalumu atawaleta watu wote kwa Mungu 3. Mungu hawezi kulisahau taifa lake, Israeli

D. Muhtasari wa dhana zinazofanana na taswira kati ya Sura ya 40 na 49

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:1-4**
**1Nisikilizeni, enyi visiwa;**
**tegeni masikio yenu, enyi kabila za watu mlio mbali sana;**
**Bwana ameniita tangu tumboni;**
**toka tumbo la mama yangu amenitaja jina langu.**
**2Naye anifanya kinywa changu kuwa kama upanga mkali;**
**katika kivuli cha mkono wake amenisitiri;**
**naye amenifanya kuwa mshale uliosuguliwa;**
**katika podo lake amenificha;**
**3akaniambia; Wewe u mtumishi wangu, Israeli,**
**ambaye katika wewe nitatukuzwa.**
**4Lakini nikasema, Nimejitaabisha bure,**
**nimetumia nguvu zangu bure bila faida;**
**lakini hakika hukumu yangu ina Bwana,**
**na thawabu yangu ina Mungu wangu**.

**49:1 "Nisikilizeni"** tazama muhtasri kamili katika utangulizi KAULI SHURUTISHI katika 48:1.

Kuna KAULI SHURUTISHI mbili zinazotambulisha kipengele hiki kipya cha fasihi.

1. nisikilizeni – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 1033, KB 1570)
2. Tegeni masikio – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI (BDB 904, KB 1151)

Ufunuo wa Mungu na makusudi yake alimaanisha kusikilizwa, kufahamika, na kuitikia matendo yake!

◙**"Enyi visiwa . . .kabila za watu mlio mbali sana" T**ungo hizi zinzofanana zinaonyesha jukumu la "watumishi" linalodokezwa ulimwenguni (kama vile. 42:7). Upendo wa Mungu

1. Anakumbuka Agano lake na uzao wa Ibrahimu (kama vile. mist. 5-6b)
2. Anakumbuka ahadi kwa wanadamu wote, Mwa. 3:15; 12:3 (kama vile. mst. 6c)

Kuna vipengele viwili vya ujumbe wa YHWH

1. Kuwatoa uhamishoni Wayahudi chini ya Koreshi
2. Kuwarudisha mataifa chini ya mtumishi/Masihi

Wakati wote katika Isaya anatizama kwa kipindi hiki (Ashuru);ijayo karibu (Babeli, Uajemi), na umbali wa wakati ujao (kipindi cha injili). Upendo wa YHWH ni kwa ajiri ya Israeli

1. Wenye haki
2. Ufunuo kwa ajiri ya mataifa haujatimilizwa bado.

Mamlaka ya Kiinjili (tazama mada maalum katika 40:15) yamebadilishwa kwenda kwa watu wa Mungu wa Agano jipya (kama vile. Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo 1:8).

◙**"BWANA aliniita tangu tumboni"** toleo la NASB lina VIWAKILISHI vilivyoandikwa kwa herufi kubwa ili kuonyesha kwamba vinamrejelea Masihi, mtumishi mmoja mmoja. Upekee wa Mungu kuitwa unaelezewa kama mtumishi aliyeitwa kabla hajazaliwa (kama Yeremia, kama vile. Yer. 1:5). Kuna hofu ya wazi katika ujumbe wa "mtumishi"kati ya mmoja mmoja na kipengele cha ushirika wa mtumishi. Iko wazi kutoka 41:8-9; 42:19; 43:10; 49:3 kwamba jina linahusiana na Israeli. Hata hivyo, mmoja mmoja analenga kwenye VIWAKILISHI VYA UMOJA kwenye Sura ya 49 na kazi ya binafsi katika 52:13-53:12 inaonyesha kwamba vifungu hivi vina malengo mawili. Malengo haya mawili pia yanaonekana katika Sura ya 42. Aya ya 1-4 inasimulia Masihi, ambapo mist. 19-21 ni wazi unahusika na Israeli. Israeli imeitwa iwe ufalme wa kikuhani ili kuwaleta watu kwa Mungu , Mwa. 12:1-3; Kut. 19:4-6. Alishindwa kwa sababu hakuweza kulitunza agano. Mungu alitimiza makusudi yake ya ukombozi kwa ulimwengu kupitia Mwisraeli mmoja mwaminifu—Yesu! Hofu hii ni sawa kati ya mmoja mmoja na uhusiano unaoweza kuonekana kwamba 49:6 ina dondoo katika Luka 2:32 inarejelea huduma ya Yesu na katika Mdo 13:46-49 inarejelea huduma ya Paulo na Barnaba.

◙**"toka tumbo la mama yangu"** neno hili "tumbo" ni dhahili "sehemu za ndani" (BDB 588). Hii inaongelea Uumbaji na maendeleo ya mtoto (kama vile. Zab. 139:13). Hili ni sawa na neno lililotumika kwenye 48:19 kwa ajiri ya "watoto" (tazama muhtasri Mwa. 15:4).

◙**"amenitaja jina langu"** mtumishi aliitwa na kupewa jina kabla hajazaliwa na YHWH. Yeye ni uwakilishi wake wa pekee . mfanano huu ni nini kile YHWH amefanya kwa ajiri ya taifa la Israeli katika 43:1. Kuna ukweli usio kuwa shaka unaoendelea kati uhusiano na taswira ya mmoja mmoja inayomsimulia mtumishi!

**49:2 "Naye anifanya kinywa changu kuwa kama upanga mkali "** hii ni sitiari ya kuelezea mnenaji mwenye ushawishi mkubwa, na hapa katika Efe. 6:17;Ebr. 4:12 inaongelea ufunuo. Imetumika kuelezea utukufu wa Kristo kama hakimu katika Isa. 11:4; Ufu. 1:16; 2:12-16; 19:15,21.

◙**"katika kivuli cha mkono wake"** Aya hii ina sitiari mbili ya ulinzi na maficho (kama vile. 51:16) mpaka wakati muafaka. Kazi ya mtumishi ni maalumu na isiyo kuwa na mashaka. Mawazo haya yanakamatwa na tungo kutoka Agano jipya la kisasa "hata ulipowadia utimilifu wa wakati" (kama vile. Marko 1:15; Gal. 4:4; Efe. 1:10; 1 Tim. 2:6; Tito 1:3).

**49:3-4** Aya hii inalenga kwamba mtumishi anahusisna na Israeli, lakini mtumishi huyu anashindwa wajibu wake! Israeli ni chombo cha Mungu kilichochaguliwa kwa ajiri ya ukombozi wa ulimwengu,mst. 6c,d, lakini sasa lazima na yeye aokolewe (kama vile. mist. 5-6a,b; 53:8d).

**49:4** kuna maswali ya kimuktadha kama aya hizi zinasimulia kushindwa kwa Israeli au mateso ya Masihi. VITENZI vyote ni KAULI YA WAKATI TIMILIFU. Labda makusudi yana utata!

Mistari miwili ya mwisho mst. 4 inaelezea uaminifu katika haki ya Mungu na thawabu (kama vile . mst. 5c).

◙**"thawabu yangu ina Mungu wangu."** Nafikilia hii ina muunganiko na 53:10-11. Thawabu itatolewa kwa ukombozi wa ulimwengu mzima.!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:5-7**
**5 Na sasa Bwana asema hivi, yeye aliyeniumba tangu tumboni niwe mtumishi wake,**
**ili nimletee Yakobo tena, na Israeli wakusanyike mbele zake tena;**
**(maana mimi nimepata heshima mbele ya macho ya Bwana,**
**na Mungu wangu amekuwa nguvu zangu);**
**6 naam, asema hivi, Ni neno dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu**
**ili kuziinua kabila za Yakobo, na kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa;**
**zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa,**
**upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia.**
**7 Bwana, mkombozi wa Israeli, Mtakatifu wake,**
**amwambia hivi yeye anayedharauliwa na wanadamu;**
**yeye anayechukiwa na taifa hili;**
**yeye aliye mtumishi wao watawalao;**
**Wafalme wataona, watasimama;**
**wakuu nao watasujudu;**
**kwa sababu ya Bwana aliye mwaminifu, Mtakatifu wa Israeli aliyekuchagua.**

**49:5 "ili nimletee Yakobo tena "** Aya hii na mst. 6b inaonyesha kwamba mtumishi lazima airejeshe Israeli, hivyo, mtumishi hawezi kuwa Israeli.

◙**"(maana mimi nimepata heshima mbele ya macho ya Bwana,
na Mungu wangu amekuwa nguvu zangu);** Haya ni maoni kutoka kwa mtumishi. Labda ni njia ya kumtia nguvu mtumishi katikati ya masikitiko na upinzani atakabiliwa wakati wa huduma yake (kama vile. 53:1-12).

**49:6 "kuwarejeza watu wa Israeli waliohifadhiwa"** tungo hii inarejelea mabaki ya waaminifu (tazama mada maalumu katika 46:3) wa watu waliochaguliwa, chombo kilichochaguliwa cha ufunuo. Matumaini ya urejesho, Israeli anaeamini inaonekana katika Zek. 12:10 na Rum. 9-11 (tazama fasiri huru juu ya vitabu hivi katika www.freebiblecommentary.org).

◙**"zaidi ya hayo nitakutoa uwe nuru ya mataifa,
upate kuwa wokovu wangu hata miisho ya dunia."** Tambua mtumishi/Masihi ana makusudi mawili. Kama mst. 5 unaakisi huduma iliyolengwa na Israeli ya Injili, ambapo mst. 6 unawakilisha kuenea kwa kanisa la awali la ulimwengu . kuenea huku kwa injili katika ulimwengu ni wazo lililorudiwa katika Isaya (kama vile. 2:2-4; 42:6; 45:22-23; 51:4; 60:1,3; Mdo 13:46-49).

**49:7 "Bwana, mkombozi wa Israeli, Mtakatifu wake "** Huu mfuatano wa majina (tazama muhtasari katika 48:17) unatuonyesha hofu kati ya

1. Miujiza na Mungu wa asili
2. Mungu kama Mwokozi na Mungu kama hakimu
3. Mungu kama rafiki na Mungu kama msimamizi

Ni lazima tushikilie kwa pamoja haki na utakatifu. Litaunda kusudi moja! YHWH anawataka watu watakao onyesha tabia yake.

◙**"amwambia hivi yeye anayedharauliwa na wanadamu;**
**yeye anayechukiwa na taifa hili; yeye aliye mtumishi wao watawalao;"** Hii inadokeza mtumishi aliye mnyenyekevu , hata kukataliwa kwa mtumishi (kama vile. 50:4-11; 52:14-53:6; Zab. 22). Lakini mwisho kabisa mamlaka ya Dunia nzima itamtambua yeye (kama vile Flp. 2:6-11, ambayo inagusiwa katika Isa. 45:22-23). Sio kejeli kwamba mmoja amedharauliwa na kuchukiwa na mataifa (kama vile. Zab. 2) ndiye yeye atakayeleta wokovu kwa mataifa!

◙**"kwa sababu ya Bwana aliye mwaminifu, Mtakatifu wa Israeli aliyekuchagua"** Huu hapa ni ufunguo wa matumaini yetu, uaminifu wa YHWH'.matumaini yetu ni tabia yake yeye anaetuita, anaetuahidi, na mkombozi!

## MADA MAALUM: TABIA ZA MUNGU WA ISRAELI (AGANO LA KALE)

1. Mwenye huruma (BDB 933, KB 1216) – Kut. 34:6; Kumb. 4:31; 2 Nya. 30:9; Zab. 86:15; 103:8; 111:4; Neh. 9:17,31; Yoel 2:13; Yona. 4:2
2. Mwingi wa fadhili (BDB 337, KB 333) – Kut. 34:6; 2 Nya. 30:9; Zab. 86:15; 103:8; 111:4; Neh. 9:17,31; Yoel 2:13; Yona. 4:2
3. Si mwepesi wa hasira (BDB74 MUUNDO WA MANENO BDB 60) – Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoel 2:13; Yona. 4:2
4. Amejaa huruma (BDB 912 I MUUNDO WA MANENO BDB 338) – Kut. 34:6-7; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoel 2:13; Yona. 4:2
5. Mwaminifu (au "kweli," BDB 54, angalia Mada Maalum: Kusadiki, Amini, Imani, na Uaminifu katika Agano la Kale) – Kut. 34:6; Kumb. 7:9; Zab. 86:15; Isa. 49:7; Yer. 42:5
6. Mwenye kujaa msamaha (BDB 699, KB 757) – Neh. 9:17
7. Hatawasahau ninyi (BDB 736 I, KB 806) – Neh. 9:17,31
8. Hughairi mabaya (BDB 636, KB 688, *Niphal* KAULI ENDELEVU + BDB 948) – Yoel 2:13; Yona. 4:2
9. Mungu Mkuu (BDB 42, 152) – Neh. 1:5; 9:32
10. Mungu Mkuu na mwenye kuogofya (BDB 152, 431) – Neh. 1:5; 4:14; 9:32
11. Atunzaye maagano (BDB 1036, 136) – Neh. 1:5; 9:32
12. Mwenye rehema kwa wampendao (BDB 338) – Neh. 1:5; 9:32 (angalia Mada Maalum: Wema (*hesed*)

Haya yote yanaelezea hisia za Mungu dhidi ya watu wake, Israeli. Tabia yake haibadiliki (kama vile Mal. 3:6), kwa hiyo, haya pia yanatumika pia kwa wale wafuasi wake waaminifu (yaani., 2 Kor. 1:3).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:8-13**
**[8]Bwana asema hivi,**
**Wakati uliokubalika nimekujibu,**
**na siku ya wokovu nimekusaidia;**
**nami nitakuhifadhi, nitakutoa uwe agano la watu hawa,**
**ili kuiinua nchi hii, na kuwarithisha urithi uliokuwa ukiwa;**
**[9]kuwaambia waliofungwa, Haya, tokeni;**
**na hao walio katika giza, Jionyesheni.**
**Watajilisha katika njia,**
**na juu ya majabali watapata malisho.**
**[10]Hawataona njaa, wala hawataona kiu;**
**hari haitawapiga, wala jua;**
**kwa maana yeye aliyewarehemu atawatangulia,**
**naam, karibu na chemchemi za maji atawaongoza.**
**[11]Nami nitafanya milima yangu yote kuwa njia,**
**na njia kuu zangu zitatukuzwa zote.**
**[12]Tazama, hawa watakuja kutoka mbali;**
**na tazama, hawa kutoka kaskazini, na kutoka magharibi,**
**na hawa kutoka nchi ya Sinimu.**

| |
|---|
| [13]**Imbeni, enyi mbingu; ufurahi, Ee nchi;**<br>**Pazeni sauti ya kuimba, enyi milima;**<br>**Kwa kuwa Bwana amewafariji watu wake,**<br>**Naye atawahurumia watu wake walioteswa.** |

**49:8** Tambua kwamba "wakati uliokubalika" na "siku ya wokovu" ni sawasawa. Andiko hili linagusiwa katika 2 Kor. 6:2. Limetumika katika Zab. 69:13-15 kwa ajiri ya siku ya ukombozi. Linaweza kudokeza ukombozi/wokovu wa kimwili au kiroho. Mwaka wa Jubilee (Law. 25:10) msingi wake ni ishara ya kusamehewa madeni. Katika muktadha huu wanaongelea juu ya kurudi Palestina, ambao ulianza kwa amri ya Koreshi mwaka wa 538 K.K. na ulikamilishwa kwa ushawishi kadhaa.

1. Sheshbaza – Ezra 1
2. Zerubabeli na Yoshua – Ezra 2
3. Nehemia – Nehemia 1
4. Ezra – Nehemia 8

Tambua VITENZI vinavyopatikana katika mst. 8 kwamba vinaelezea matendo ya YHWH.

1. nimekujibu wewe – *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (BDB 772, KB 851)
2. nimekusaidia wewe – *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (BDB 740, KB 810)
3. nitakuhifadhi wewe – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 665, KB 718)
4. Nitakupatia wewe – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 678, KB 733)
   a. kuiinua nchi – *Hiphil* TUNGO YA KITENZI JINA HALISI (BDB 877, KB 1086)
   b. kuwarithisha urithi – *Hiphil* TUNGO YA KITENZI JINA HALISI (BDB635, KB 686)

◙**". . . nitakutoa uwe agano la watu hawa"** Tungo hii ilitumika mapema kwenye 42:6 ambapo katika dhamira ya 49:6,8 kufanana. Maagano ya YHWH na Ibrahimu na uzao wake ni ya kudumu zaidi kuliko Israeli sasa (kama vile. Mwa. 12:3; tazama mada maalumu katika 40:15). Na hii pia ni kwa ajiri ya ulimwengu mzima (yaani.,mataifa). Hii ni mantiki na teolojia inayodokeza kuamini katika Mungu mmoja-Mungu mmoja pekee (tazama mada maalumu katika 40:14), wanadamu wote wameumbwa kwa Sura ya Mungu (kama vile. Mwa. 1:26-27), na kuahidi kuwaokoa wanadamu wote katika Mwa. 3:15, zamani kabla halijakuwepo taifa la Israeli.

**49:8d-12** Aya hizi ni sitiari ya kuwalisha kondoo katika malisho yenye utele. Wanaakisi Baraka za maagano ya Kumb. 27-28. Watu wa Mungu watarejeshwa katika nchi ya ahadi! Paulo analitumia andiko hili kwa ajiri ya Enzi mpya kwenye 2 Kor. 6:2. Aya ya 10 pia imetumika kwenye Ufu. 7:16, ambayo inaonyesha mataifa wamehusishwa.

**49:9** waisraeli wanaelezewa kama wako kifungoni (yaani .,wafungwa, BDB 63, kama vile. 42:7; 61:1).

1. Wale waliofungwa
2. Hao walio katika giza

wanaambiwa

1. tokeni – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 422, KB 425)
2. jionyesheni – *Niphal* KAULI SHURUTISHI (Kifasihi. "jionyeshe," BDB162, KB 191)

**49:10 "kwa maana yeye aliyewarehemu atawatangulia,"** Hii inaelezea majina kwa ajiri ya YHWH.

1. Yeye aliyewarehemu – *Piel* KAULI ENDELEVU (BDB 933, KB 1216)
2. Yeye atawatangulia – *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 624, KB 675)
3. Yeye atakaewaongoza – *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 624, KB 675)

◙ Sitiari ya kilimo ya vyakula kutoka mst. 9 inaendelea .

1. Hawataona njaa
2. Hawatona kiu
3. Hari haitawapiga

Kurudi nyumbani itakuwa rahisi sana , watalindwa na wingi wa chakula tele. Taswira hii ni sawa na ile iliyotumika kwenye Ufu. 7:16 nyakati za Masihi. Masihi aliye YHWH ni mchungaji wao (kama vile. Zab. 121:5-6).

**49:11** njia ya kufikia Yerusalemu ni sitiari ya uhakika kwa kuondoa vizuizi vyote na kufanyiwa matengenezo, hata kupainua, barabara kuu (kama vile. 11:16; 19:23; 62:10).

Kutakuwa na jamii yabubujiko- huru kati ya mataifa kwa ajiri ya kusudi la kumwabudu YHWH.
mataifa yanakuja!

Inatia shauku ni kwa jinsi gani Isaya alitumia mara nyingi njia kuu kama taswira.

1. Njia kuu kwa ajiri ya wayahudi kutoka uhamishoni, 11:16; 57:14
2. Njia kuu kwa ajiri ya mataifa kuja kuabudu, 19:23
3. Njia kuu ya utakatifu, 26:7; 35:8; 43:19; 49:11; 51:10
4. Njia kuu ya Masihi, 40:3; 42:16

**49:12 ". . . na hawa kutoka nchi ya Sinimu"** sehemu sahihi kwa ajiri ya nchi hii ina mashaka. Msukumo wa andiko hili ni kwamba Mungu atawarudisha watu wake nyumbani, hata kutoka katika nchi za mbali.

1. NASB, NKJV, Peshitta – "Sinimu"
2. NRSV, REB – "Syene"
3. TEV, NIV, NJB – "Aswani"
4. DSS – "Syenians"

Hii yote ni aina mbalimbali ya mji wa kale wa kubahatisha kusini mwa Misri ambao ulikuwa na idadi kubwa ya Wayahudi (kama vile. Ezek. 30:6)

**49:13 "Enyi mbingu. . .Enyi nchi. . . Enyi milima"** hii imetumika kama mashahidi wa hukumu ya Mungu dhidi ya watu wake (yaani., 44:23). Na sasa wametumika kama mashahidi wenye furaha ya uaminifu wa Mungu (kama vile. 48:1nakuendelea)!

tambua mfuatano wa KAULI SHURUTISHI.

1. imbeni – *Qal* KAULI SHURUTISHI(BDB 943, KB 1247)
2. ufurahi – *Qal* KAULI SHURUTISHI(BDB 162, KB 189)
3. Pazeni – *Qal* KAULI SHURUTISHI(BDB 822, KB 953)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:14-21**

**14 Bali Sayuni alisema, YEHOVA ameniacha,**
**Bwana amenisahau.**
**15 Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye,**
**hata asimhurumie mwana wa tumbo lake?**
**Naam, hawa waweza kusahau,**
**lakini mimi sitakusahau wewe.**
**16 Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu;**
**kuta zako ziko mbele zangu daima.**
**17 Watoto wako wafanya haraka,**
**hao wakuharibuo, nao waliokufanya ukiwa,**
**watatoka kwako.**
**18 Inua macho yako, ukatazame pande zote;**
**hao wote wanajikusanya na kukujia.**
**Kama niishivyo, asema Bwana,**
**hakika utajivika na hao wote, kama kwa uzuri, nawe utajifungia hao, kama bibi arusi.**
***19* Maana katika habari za mahali pako palipokuwa ukiwa,**
**pasipokaliwa na watu,**
**na nchi yako iliyoharibika hakika sasa utakuwa mwembamba usiwatoshe wenyeji wako, nao waliokumeza watakuwa mbali.**
***20* Watoto ulionyang'anywa watasema masikioni mwako,**

**Mahali hapa ni pembamba,**
**hapanitoshi; nipe nafasi nipate kukaa.**
21**Ndipo utasema moyoni mwako,**
**Ni nani aliyenizalia watoto hawa,**
**na mimi nimefiwa na watoto wangu,**
**nami ni peke yangu,**
**nimehamishwa, ninatanga-tanga huko na huku?**
**Tena ni nani aliyewalea hawa?**
**Tazama, naliachwa peke yangu; hawa je! Walikuwa wapi?**

**49:14-21** Aya hizi ni maneno ya Mungu ya kumtia moyo Yerusalem aliyekataliwa na aliye tasa (yaani , Sayuni).tambua idadi ya neno "kusahau" (BDB 1013, KB 1489) ilivyotumika.

1. "bwana amenisahau mimi" – *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU
2. "mwanamke aweza kumsahau mtoto wake" – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
3. "hawa waweza kusahau" – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
4. "mimi sitakusahau wewe" – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

Mungu anatumia lugha ya elimu ya binadamu kuelezea upendo wake na ulinzi wa uaminifu kwa waliorudi kwa maana ya sitiari ya njaa (sikiliza mahubiri katika mtandao www.freebiblecommentary.orgchini ya "maandiko magumu yenye mkanganyiko," namba 111, "Jinsi ke ya Mungu"

**49:15** Hii ni sitiari ya nguvu ya Agano la upendo la Mungu (kama vile. 66:9-13). YHWH anaelezewa katika neno hili kama mwanamke anyonyeshaye. Tazama mada maalum katika 41:2.

**49:16-17** Hii ni sitiari nyingine ya nguvu imara ya maagano yanayokumbukwa na Mungu baina ya uzao wa Ibrahimu. Hata kama Yerusalem iko kwenye maangamizi, watu wa Mungu wataona siku mpya ya urejesho!

**49:17**
**NASB** **"mjenzi wako ana haraka"**
**NKJV** **"watoto wako wanafanya haraka"**
**NJB** **"wajenzi wako wana haraka"**
**JPSOA** **"haraka mtoto wako anakuja"**

Toleo la UBS (uk. 134-135) linaonyesha chaguzi mbili.

1. Mtoto wako , בָּנַיִךְ– MT, DSS
2. wajengaji wako, בּוֹנַיִךְ– ambapo toleo la UBS huita "kauli ya mnenaji wa Babeli"

toleo la UBS linatupatia chaguo namba 2 yenye alama C (enye mashaka makubwa).
mstari wa pili pia una swali.

1. REV – "wajenzi wako wamewashinda waharibifu wako"
2. NEB – "wale wote waliokujenga wamefanya bora zaidi na kwa haraka kuliko wale waliokungusha chini"

Utofauti huu unahusika pekee kwenye unenaji wa konsonanti za Kiebrania (UBS Text Project, uk. 135).

**49:18** Yerusalemu imeangamizwa! Taswira yake ni kama asiyekuwa na mtoto (kama vile. Mist. 20-21). Mme wake , YHWH, sasa anamrejesha na kupatia watoto wengi kama taji ya uzee wake!
YHWH anawapa waliorudi wito wa

1. Inua macho yako – *Qal* KAULI SHURUTISHI(BDB 669, KB 724)
2. Ukatazame pande zote – *Qal* KAULI SHURUTISHI(BDB 906, KB 1157)

**49:21-22** Wale wote waliorudi Yerusalem,ambayo ni ishara ya kumwabudu YHWH (yaani , hekalu),watakuwa wengi kiasi kwamba mji hauwezi kuwatosheleza wote!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:22-23**
[22]**Bwana MUNGU asema hivi,**
**Tazama, nitawainulia mataifa mkono wangu,**
**na kuwatwekea kabila za watu bendera yangu;**
**nao wataleta wana wako vifuani mwao,**
**na binti zako watachukuliwa mabegani mwao.**
[23]**Na wafalme watakuwa baba zako za kulea,**
**na malkia zao mama zako za kulea;**
**watainama mbele yako kifudifudi,**
**na kuramba mavumbi ya miguu yako;**
**nawe utajua ya kuwa mimi ni Bwana,**
**tena waningojeao hawatatahayarika.**

**49:22-23** Katika mstr. 7 viongozi wa mataifa wamemkataa na kufanya uasi dhidi ya Masihi wa Mungu (kama vile. Zab 2). Na sasa wamekuja kutubu Yerusalem na kuwareta watu wa maagano na Mungu, Wayahudi, pamoja nao. Aya hii haina maana ya kulikuza Agano la kale , lakini maagano aliyoyafanya Mungu! Watu wa mataifa unyenyekevu kwa ajiri YHWH itaonekana hashima yao kwa watu wake (kama vile. 45:14).

**49:22 "kuwatwekea kabila za watu bendera yangu; "** hii inafanana na "nitawainulia mataifa mkono wangu." Mtumishi atakuwa ishara/bendera kwa ajiri ya mataifa (yaani, mataifa) kuungana (kama vile. 11:10,12). Mwisho kabisa wa urejesho wa watu wa maagano ni urejesho wa wanadamu wote! Tazama mada maalum katika 45:23.

**49:23 "nawe utajua ya kuwa mimi ni Bwana "** Israeli wana maana wawe mashahidi kwa mataifa. Na sasa mataifa watakuwa mashahidi kwa Israeli. Kama watu wa mataifa watamwamini YHWH na kubadilika kuwa kundi kubwa, hii ni ishara kwamba Mungu yuko pamoja nao lakini ni lazima wawe na imani (kama vile. Rumi 9-11).

◙**"tena waningojeao hawatatahayarika "** dhana ya "kungojea" inapatikana mara nyingi katika Isaya: 25:9; 26:8; 40:31 (Zab. 37:9). Hii ni hali zinazofanana kwa wote wale "wamtumainio" mtumishi!

Tungo "hawatatahayari" ni dhana nyingine ya Agano la kale (kama vile. 45:17; Zab. 25:3; Yoeli 2:27). Wale wote watakamsubiria/kumwamini hawatatahayarika/ kuvunjwa matumaini!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 49:24-26**
[24]**Je! Aliye hodari aweza kunyang'anywa mateka yake,**
**au jeshi lao waliofungwa halali wataokoka?**
[25]**Naam, Bwana asema hivi,**
**Hata jeshi la wafungwa wake aliye hodari watapokonywa mikononi mwake,**
**na mateka yake aliye jabari wataokoka;**
**kwa maana nitateta na yeye atetaye nawe,**
**nami nitawaletea wana wako wokovu.**
[26]**Na hao wanaokuonea nitawalisha nyama yao wenyewe,**
**nao watalewa kwa kuinywa damu yao wenyewe, kama kwa mvinyo mpya;**
**na wote wenye mwili watajua ya kuwa mimi, Bwana, ni mwokozi wako,**
**na Mkombozi wako ni Mwenye enzi wa Yakobo.**

**49:24-26** Aya hizi ni sitiari ya tukio la safari ya pili . Mungu anawakomboa watu wake tena kutoka kwa mataifa yenye nguvu duniani . ina maana kwamba makusudi ya Mungu katika ukombozi huu, kama ukombozi wake wa kwanza, sio tu kwamba watu wake wa maagano waachiwe huru lakini mataifa yote yamjue yeye (kama vile. mst. 26c; 45:6; Mal. 1:11).

**49:24b**
**NASB, NRSV,**
**NJB “uonevu”**
**NKJV “mwenye haki”**
**REB “pasipo huruma”**
**JPSOA “mshindi”**

tafsiri inayofuatiwa na toleo la NKJV inapatikana katika toleo la MT, lakinia matoleo mengine kutoka DSS, Syriac, na Vulgate.

1. haki – צדיק
2. uonevu – ערי٢

**49:25 “kwa maana nitateta ”** hili ni “baraza la mahakama” kitaswira. Inawezekana imetumika katika Yer. 50:34 na inatoa mwanga kwenye aya hii.

YHWH/mtumishi anabadilika kutoka mwendesha mashitaka na kuwa wakili!

**49:26d** Tambua tena ukuu wa majina kwa ajili ya Uungu wa Israeli (kama vile. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17;49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16)

# ISAYA 50

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mungu anamsaidia Mtumishi wake | Mtumishi, Tumaini la Israeli | Agano, Uaminifu na Hukumu | | Adhabu ya Israeli |
| 50:1-3 (1-3) | 50:1-3 (1-3) | 50:1-3 (1-3) | 50:1 (1) | 50:1-3 (1-3) |
| | | | 50:2-3 (2-3) | |
| | | | Utii wa Mtumishi wa BWANA | Wimbo wa tatu wa Mtumishi |
| 50:4-11 (4-11) | 50:4-6 (4-6) | 50:4-6 (4-6) | 50:4-6 (4-6) | 50:4-11 (4-11) |
| | 50:7-9 (7-9) | 50:7-9 (7-9) | 50:7-9 (7-9) | |
| | 50:10-11 (10-11) | 50:10-11 (10-11) | 50:10-11 (10-11) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. wa xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Huuu ni wimbo wa tatu wa Mtumishi (50:4-9).
B. Katika 49:25d taswira ya baraza inatumika pamoja na Mtumishi kama mlinzi mtetezi. Hapa taswira ya baraza natumika kuamaanisha YHWH kama mwenye kuwatarakisha watu wa agano lake kwa ajili ya mtumishi kwa ajili ya ukosefu wao wa uaminifu.
C. Katika kutofautisha uaminifu wa watu wa agano , uaminifu wa Mtumishi, ukamilifu wa Mwisraeli, ni tofauti ya kutisha. Yeye atatimiza kile ambacho Israeli haikuweza kukitimiza!

D. Tambua kwamba tafsiri nyingi za lugha ya Kiingereza zinavitazamisha vifungu katika mist. ya 4-11, ambayao ingeweza kudokeza kweli kuu tatu.

1. mist. ya 4-6
2. mist. ya 7-9
3. mist. ya 10-11

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 50:1-3**
[1]**Bwana asema hivi, Iko wapi hati ya talaka ya mama yenu,**
**ambayo kwa hiyo naliachana naye?**
**Au nimewauza ninyi kwa nani katika watu wanaoniwia?**
**Ninyi mliuzwa kwa sababu ya maovu yenu;**
**tena mama yenu ameachwa kwa sababu ya makosa yenu.**
[2]**Basi, nilipokuja, mbona hapakuwa na mtu?**
**Nilipoita, mbona hapakuwa na mtu aliyenijibu? Je!**
**Mkono wangu ni mfupi, hata nisiweze kukomboa?**
**Au je! Mimi sina nguvu za kuponya?**
**Tazama, kwa kukemea kwangu naikausha bahari,**
**mito ya maji naifanya kuwa jangwa;**
**samaki wao wanuka kwa sababu hapana maji, nao wafa kwa kiu.**
[3]**Mimi nazivika mbingu weusi,**
**nami nafanya nguo ya magunia kuwa kifuniko chao**.

**50:1** Kuna vipengele viwili vya sheria ya lale vilivyotumika kusistiza msimamo wa sheria za Israeli.
1. talaka kwa mwanamke asiye mwaminifu (kama vile 54:6-7; Yer. 3:1,8; Hos. 2:4)
2. kumuuza mtu utumwani kwa ajili ya deni (kama vile Kumbu. 32:30; II Fal. 4:1; Neh. 5:5)

Kwa sababu ya “maovu”na “makosa” ya Israeli, Israeli alihukumiwa na kupelekwa uhamishoni. Huu haukuwa udhaifu wa YHWH, bali uasi wa watu wake (kama vile 59:2).

**50:2** Mstari huu unaanza na mfululizo wa maswali manne yenye mubalagha, kama ulivyo mst. wa 1 ulivyokuwa na maswali mawili. Swali la kwanza linajikita kwa YHWH, akishangazwa kwa sababu ya ukosefu wa upatanisho na utii wa imani. Anauliza kama Israeli amepoteza tumaini katika uwezo wake wa kuokoa!

◙**“Mkono wangu ni mfupi”** Hii ni *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU na *Qal* ya KITENZI JINA HALISI cha asili ile ile (BDB894, KB 1126), ambayo inachochea dhana, hapa kuna swali.

◙**“kukomboa”** Anagalia Mada Maalum katika 41:4. Neno hili lina ufanano na neno “kuokoa.”

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 50:4-11**
[4]**Bwana MUNGU amenipa ulimi wa hao wafundishwao,**
**nipate kujua jinsi ya kumtegemeza kwa maneno yeye aliyechoka,**
**huniamsha asubuhi baada ya asubuhi;**
**huniamsha, sikio langu lipate kusikia kama watu wafundishwao.**
[5]**Bwana MUNGU amenizibua sikio langu,**
**wala sikuwa mkaidi, wala sikurudi nyuma.**
[6]**Naliwatolea wapigao mgongo wangu,**
**na wang'oao ndevu mashavu yangu;**
**sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate.**

**[7]Maana Bwana MUNGU atanisaidia;**
**kwa sababu hiyo sikutahayari, kwa sababu hiyo nimekaza uso wangu kama gumegume,**
**nami najua ya kuwa sitaona haya.**
**[8] Yeye anipatiaye haki yangu yu karibu;**
**ni nani atakayeshindana nami?**
**Na tusimame pamoja; ni nani aliye hasimu yangu?**
**Na anikaribie basi.**
**[9] Tazama, Bwana MUNGU atanisaidia;**
**ni nani atakayenihukumu kuwa mkosa?**
**Tazama hao wote watachakaa kama vazi;**
**nondo atawala.**
**[10]Ni nani miongoni mwenu amchaye Bwana,**
**aitiiye sauti ya mtumishi wake?**
**Yeye aendaye katika giza, wala hana nuru,**
**naye alitumainia jina la Bwana, na kumtegemea Mungu wake.**
**[11]Tazama, ninyi nyote mwashao moto,**
**mjifungiao hiyo mienge;**
**endeni ninyi katika mwali wa moto wenu,**
**na katikati ya mienge mliyoiwasha.**
**Mtayapata haya kwa mkono wangu;**
**mtalala kwa huzuni.**

**50:4-6** Mistari hii inaeleza kipengele cha huduma ya Mtumishi (katika maneno yake mwenyewe).

1. alipewa karama ya kusikia
2. alipewa karama ya kumtegemeza , mst. wa 4a
3. huniamsha, sikio langu lipate kusikia
   a. ameiridhisha kila roho (kama vile Yer. 31:25), mst. 4b
   b. YHWH, mist. 4c,d,5a
4. Hakuwa mkaidi, mst. wa 5b
5. Hakurudi nyuma, mst. wa 5c
6. Alijitoa kwa ajili ya kufedheheshwa (kama vile Mt. 26:67; 27:30; Marko 15:9)
   a. mgongo wake ulipigwa
   b. kichwa chake kilipigwapigwa kwa mwanzi
   c. walimtemea mate

Maarifa ya matendo ya Mtumishi yatapelekea kukataliwa kwa ujumbe na watu wake kwa wale waliokataa kusikiliza (kama vile mst. wa 11).

**50:4**a "**wafundishwao**" Hili ni neno adimu (BDB 541), linajitokeza hapa tu (mara mbili) na 8:16 katika maana hii. Mara nyingi neno hili linatafsiriwa kama "kufundishwa" (54:13).

**50:4b**
**NASB, NRSV "kumtegemeza"**
**NKJV "kulinena neno katika majira ya yule anayemtegemeza"**
**TEV "kumuhimarisha yule ategemezwaye"**
**NJB "kunena neno la kumfaraiji yule ategemezwaye"**
**JPSOA "kuyanena maneno kwa yule ayegemezwaye"**
**REB "kumtuliza yule ategemezwaye"**

Kwa namna iliyo dhahiri toleo la MT ni la kiutata kwa sababu neno"kumtegemeza" (BDB 736, KB 804) linajitokeza hapa tu.

**50:4c, d** Kuna*Hiphil*ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 734, KB 802), "huniamsha" iliyorudiwarudiwa" Katika *Hiphil* neno hili linatumika kuzindua au kuchochea tendo fulani.

1. 13:17 –Wamedi (Yer. 51:11)
2. 41:2,25 – Koreshi II
3. 45:13 – Koreshi II
4. hapa – Mtumishi
5. Dan. 11:2 –mtwala wa kipindi cha uwazi wa Agano la Kale na Agano Jipya

YHWH analilinda neno la historia na ukombozi wa ulimwengu!

**50:6**Tiba maalum ya Mtumishi mwaminifu ni utabiri wa tiba ya Yesu. Kifungu hiki kinautambulisha wimbo wa nne wa Mtumishi katika 52:13-53:13, hasa mist. ya 3,4-5,7-9. Mtumishi huyo atalipa gharama kubwa kwa ajili ya unyenyekevu wake, tumaini, na utii wake katika YHWH (kama vile Zab. 2, 22). Kuna makusudi katika kuteseka kwake(kama vile Marko 10:45; II Kor. 5:21; kitabu cha Waebrania).

**50:7-9** Mstari wa kwanza wa ubeti huu unarudiwa katika ubeti huu katika mst. wa 9a, "Bwana MUNGU (*Adon*) (YHWH) atanisaidia."

Kwa kuwa Mtumishi huyu

1. hataibishwa
2. ataukaza uso wake kama gumegume (kama vile Luka 9:51)
3. atafedheheshwa

Kwa nini, kwa sababu YHWH anatenda badala ya, anayetambulishwa kwa mfululizo wa maswali mengine (mist. ya 8-9). Muundo wa kisarufi (yaani, "Nani. . .?") unafupishwa kupitia mst. wa 10.

**50:8**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"anipatiaye"** |
| **NKJV, LXX** | **"aithibitishaye"** |
| **TEV** | **"aniakikishiaye kutokuwana hatia"** |
| **NJB** | **"aitunzaye haki"** |
| **JPSOA** | **"mthibitishaji wangu"** |
| **REB** | **"atalisafisha jina langu"** |

Kama mist. ya 6-7 inafafanua juu ya mashtaka yasiyo ya haki, hivyo mst. wa 8 unafafanua maamuzi. Hiki KITENZI (BDB 842, KB 1003) ni *Hiphil* ya KAULI YA ENDELEVU ambacho kinamaanisha "sitamhesabia haki " (kama vile Kut. 23:7; Kumb. 25:1; I Fal. 8:32; Mit.17:15). Kitenzi hiki kinatumika katika kataiak muktadha hasi katika Isa. 5:23. Hiki kinambainisha

1. Mungu katika muktdha huu
2. Mtumishi katika 53:11

◙**"Na tusimame pamoja"** Hii ni *Qal* ya KAULI ISIOTIMILIFU katika maana ya KAULI AMRISHI. Hiki KITENZI (BDB 620, KB 670) kinatumika kuyakaribia mashtaka ya hukumu. Tambua hapa kuwa Mtumishi ndiye Hakimu.

**50:10-11** AB inaichukulia mistarai hii kama mwitikio wa Mtumishi (uk. 116), kwa uwazi kabisa ni pamoja na YHWH (Leupold, uk. 196). Kuna tofauti kati ya aina mbili za "mienge."

1. amchaye Bwana aitiiye sauti ya mtumishi wake? (mst. wa 10)
   a. naye alitumainia jina la Bwana – *Qal ya* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 105, KB 120) kifungu hiki kinatumika katika maana ya KAULI AMRISHI
   b. kumtegemea Mungu wake – *Qal* yaKAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU (BDB 1043, KB 1612) kitenzi hiki kinatumika katika maana ya KAULI AMRISHI
2. mjifungiao hiyo mienge (yaani, moto, angalia Mada Maalum katika 47:14)endeni ninyi katika mwali wa moto wenu (*Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ambao mwishowe utawateketeza (yaani, wataangukia katika huzuni, mst. wa11)

# ISAYA 51

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Israeli inaonywa | BWANA anafariji Sayuni | wokovu kwa uzao wa Ibrahimu | maneno ya faraja kwa Sayuni | Baraka za hazina kwa ajili ya wateule |
| 51:1-3 | 51:1-2 | 51:1-3 | 51:1-2 | 51:1-3 |
| (1-3) | (1-2) | (1-3) | (1-2) | (1-3) |
| | 51:3 | | 51:3 | |
| | (3) | | (3) | |
| 51:4-8 | 51:4-6 | 51:4-8 | 51:4-6 | 51:4-8 |
| (4-8) | (4-6) | (4-8) | (4-6) | (4-8) |
| | 51:7-8 | | 51:7-8 | |
| | (7-8) | | (7-8) | |
| | | | | Uamsho wa Yahweh |
| 51:9-11 | 51:9 | 51:9-11 | 51:9-11 | 51:9-11 |
| (9-11) | (9) | (9-11) | (9-11) | (9-11) |
| | 51:10-11 | | | Yahweh Mshauri |
| | (10-11) | | | |
| 51:12-16 | 51:12-16 | 51:12-16 | 51:12-16 | 51:12-16 |
| (12-16) | (12-16) | (12-16) | (12-16) | (12-16) |
| | Hasira ya Mungu Inaondolewa | Ufalme wa Mungu 51:17-52:12 | Mwisho wa mateso ya Yerusalemu | uamsho wa Yerusalemu |
| 51:17-20 | 51:17-20 | 51:17-20 | 51:17-20 | 51:17-23 |
| (17-20) | (17-20) | (17-20) | (17-20) | (17-23) |
| 51:21-23 | 51:21-23 | 51:21-23 | 51:21-23 | |
| (21-23) | (21-23) | (21-23) | (21-23) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi na kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kuna mfululizo wa KAULI SHURUTISHI ambazo zinawahitaji watu wa kiagano wa Mungu kuamka kiroho na kuwa na mwitikio kiusahihi.
   1. sikia, zingatia, 51:1,4,7,21
   2. amka, 51:19 [mara tatu], 17 [mara mbili]
   3. tazama, inua macho yako, 51:1-2,6

   Msisitizo huu unaendelezwa katika sura ya 52.

B. Maudhui ya muktadha huu unapelekwa sambamba na mfululizo wa maswali yasiyo hitaji majibu: 51:9-10,12-14; 52:5

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 51:1-3**
**[1] Nisikilizeni, ninyi mnaoifuatia haki;**
**ninyi mnaomtafuta Bwana;**
**uangalieni mwamba ule ambao mlitolewa kwa kuchongwa,**
**na tundu la shimo ambalo mlitolewa kwa kuchimbuliwa.**
**[2]Mwangalieni Ibrahimu, baba yenu, na Sara, aliyewazaa;**
**kwa maana alipokuwa mmoja tu nalimwita,**
**nikambariki, nikamfanya kuwa wengi.**
**[3]Maana Bwana ameufariji Sayuni;**
**amepafariji mahali pake palipokuwa ukiwa;**
**amefanya jangwa lake kuwa kama bustani ya Edeni,**
**na nyika yake kama bustani ya Bwana;**
**furaha na kicheko zitaonekana ndani yake,**
**kushukuru, na sauti ya kuimba.**

**51:1 "sikia"** Hili ni neno la Kiebrania *Shema* (BDB 1033, KB 1570). Lenye maana "sikia ili uweze kufanya." KAULI SHURUTISHI inajirudia katika Isaya! Neno hilohilo linaanza na maombi maarufu ya uungu mmoja ya Kumbu kumbu la Torati 6:4-6.

◙**"enyi ambao…."** Hii inazungumzia watu waaminifu wa kiagano (kama vile 50:10). Kuna tungo tatu zenye maelezo.
1. wale waitafutao haki, mstari wa 1
2. wale wamtaftao Bwana, mstari wa 1
3. wale waishikao sheria katika mioyo yao, mstari wa 7

Inawezekana kwamba "ukombozi" (BDB 841, "haki") inakuwa sambamba na YHWH katika mstari wa 2, hivyo inaweza kuwa cheo, "Mwenye haki." Ile "enyi ambao. . ." ingezungumzia wale waaminifu ambao
1. wanamtafta Mungu, mstari wa 1
2. wanamtaka Mungu, mstari wa 2

◙**"Mwamba. . . kuchimbuliwa"** Hii inamrejerea Ibrahimu na Sara (kama vile mstari wa 2) Mahali pa kijiografia pa wito wa Ibrahimu (yaani Uru ya Wakaldayo) ilikuwa ni mahali palepale pa mateka wa kibabeli (Channel Chebar). YHWH alikuwa amehaidi kumbariki Ibrahimu na uzao wake (kama vile Mwanzo 12:1-3; 15:1-11; 18:18; 22:16-18).

**51:2 "aliyewazaa kwa maumivu"** Hii inarejerea kuzaa kwa kawaida (kama vile Mwanzo. 3:16).

◙**"nikambariki, nikamfanya kuwa wengi"** YHWH alihaidi vitu viwili:
1. kumbariki Ibrahimu – BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU

2. kumzidisha – BDB 915, KB 1176, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
   Mungu alimuahaidia Ibrahimu nchi na uzao. Aliambiwa namna uzao wake ambavyo ungekuwa
   1. vumbi la nchi (Mwanzo 13:16; 28:14; Hes. 23:10)
   2. nyota za mbinguni (Mwanzo 15:5; 22:17; 26:4)
   3. mchanga wa baharini (Mwanzo 22:17; 32:12

Kutoka Isaya na Mika tunajifunza kwamba Familia ya Ibrahimu ingekuwa hata kubwa zaidi kuliko namna mtu yoyote angeweza kuwaza “Mataifa na Wayahudi” (kama vile Rum. 2:28-29; 3:21-31; 4:1-25; Gal. 3:1-29; 6:16).

**51:3 “Maana Bwana ameufariji Sayuni”** KITENZI “kufariji” (BDB 636, KB 688, *Piel* kauli ya wakati timilifu) inatokea mara mbili katika mstari wa 1 na mstari wa 2. Hii ni maudhui inayojitokeza tokeza katika kipengele hiki cha Isaya (kama vile 40:1[mara mbili]; 49:13; 51:3 [mara mbili],12,19; 52:9; 54:11; 61:2; 66:13 [mara mbili]). Maana yake ya kimsingi katika *Piel* ni “kufariji,” mpaka “kutia moyo.” Hii inamaana kumaliza utumwa na kuwarejesha katika ardhi yenye rutuba ya Ahadi (kama vile 40:1). Huku ni kufanya upya tena taasisi kwa Mungu kwa agano la Kumbu kumbu la Torati 27-28.

◙**“mahali pake palipokuwa ukiwa; amefanya jangwa.........kama bustani ya Edeni, na nyika yake kama bustani ya Bwana”** Uzuri wa nje na kuzaa matunda ni ishara ya baraka za Mungu (kama vile Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 27-29). Kutajwa kwa Edeni kunamaanisha utele tu lakini ushirika na Mungu wa sasa! Edeni ilikuwa madhabahu ya Mungu (kama vile John H. Walton, *ANE Thought and the OT*, p. 124).

## MADA MAALUM: EDENI (BDB 727)

Edeni ni eneo la kijiografia (yaani., huko Sumeri, "eneo tambarare" au "nchi tambarare"; huko Ugariti, "sehemu tambarare") katika Mwanzo 2-3, ambayo inajumuisha bustani maalum iliyopandwa mimea na kuandaliwa na Mungu (kama vile Mwa. 2:8) kwa ajili ya uumbaji wake uliotukuka, yaani mwanadamu (yaani., akimuumba kwa sura na mfanano wake, kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 9:6). Bustani maalum imedokezwa katika Isa. 51:3; Ezek. 28:13; 31:9,16,18 (mara mbili); 36:35; na Yoel 2:3.

Inavyoonekana neno linamaanisha "utele" kutokana na asili ya Kiarama. Katika Kiebrania (BDB 727 III, KB 792 II) asili ya neno linamaanisha "kufurahia" au "starehe" (kifasihi). Baadaye katika kitabu cha Mwanzo neno likajakuwa stiari kwa ajili ya sehemu iliyonyeshewa vizuri, yenye kustawi. Bustani ya Edeni ilikuwa inawakilisha kipindi mwafaka cha ushirika kati ya Mungu na mwanadamu. Hatimaye, likajakuwa ni taswira iliyotumika kuhusu mbingu (kama vile Ufunuo 21-22).

Kwangu mimi, nimekuja kuuamini uumbaji wa mwanadamu hivi karibuni (yaani., 40,000-15,000 K.K.), na sio mwanzoni. Hii inaitwa "dhana ya uumbaji endelevu." Kwa maana hiyo katika maisha yangu, ni namna ya kuruhusu Biblia kutetea neno "Nani" na kwa Nini" kuhusu uumbaji na kuwaruhusu wanasayansi wa leo kunijulisha juu ya neno "kwa vipi" na "lini." Sikasirishwi kwa ajili ya "mabadiliko," bali kwa ajili ya "uasilia"!

◙**“furaha na kicheko.....kushukuru, na sauti ya kuimba”** Hii inaaksi maisha ya kijamii yenye furaha ambayo pia ni ishara ya Baraka za Mungu.

**51:4-8** Tambua mara katika Kiingereza ambazo VIWAKILISHI VYA NAFSI vinatokea
1. YHWH
   e. Yeye, mstari wa 4c,d, 8a
   f. YHWH, 4a, 5a, 7a
2. mtumishi/Masihi
   a) Mimi, mistari 4a,c; 6a; 7a; 8a,b,d,e

b) Mimi, mistari ya 4b; 5b,c; 6a,c; 7b,c,d
c) Yangu, mistari ya 4d; 5a; 6a,b,c; 7c

Lahaula! Ni uwepo binafsi na kujizatiti kwa nmna gani ambako YHWH kwa Mtumishi!

**51:4** Tambua usambamba wa mstari wa 1 na wa 2. KAULI SHURUTISHI:
1. kuzingatia – BDB 904, KB 1151, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI
2. kusikiliza – BDB 24, KB 27, *Hiphil* KAULI SHURUTISHI

Mistari ya 3 na 4 pia ina mrandano. Tambua tena mafundisho ya YHWH (Torah, BDB 435) yamekusudiwa kubariki:
1. Israeli
2. ulimwengu (kama vile 42:6; 49:6; 60:1,3); tazama WINGI "watu" katika 51:5b na "pwani" katika 51:5c; walisubiri kwa mategemeo kwa ajili ya Mtumwa wa YHWH

◙**"sheria . .haki"** NOMINO hizo mbili pia zina mrandano. Zinazungumzia ukweli wa YHWH na mapenzi kwa wanadamu ambayo sasa inapatikana kwa wote (yaani Maandiko, ufunuo).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 51:4-8**
**4 Nisikilizeni mimi, enyi watu wangu;**
**nisikieni, taifa langu; maana sheria itatoka kwangu,**
**nami nitaistarehesha hukumu yangu iwe nuru ya mataifa.**
**5 Haki yangu i karibu, wokovu wangu umekuwa wazi,**
**na mikono yangu itawahukumu kabila za watu;**
**visiwa vitaningoja, navyo vitautumainia mkono wangu.**
**6 Inueni macho yenu mbinguni,**
**mkaitazame nchi chini;**
**maana mbingu zitatoweka kama moshi,**
**na nchi itachakaa kama vazi,**
**nao wakaao ndani yake watakufa kadhalika;**
**bali wokovu wangu utakuwa wa milele,**
**na haki yangu haitatanguka.**
**7 Nisikilizeni, ninyi mjuao haki,**
**watu ambao mioyoni mwenu mna sheria yangu;**
**msiogope matukano ya watu,**
**wala msifadhaike kwa sababu ya dhihaka zao.**
**8 Maana nondo itawala kama vazi,**
**na funza atawala kama sufu; bali haki yangu itakuwa ya milele,**
**na wokovu wangu hata vizazi vyote.**

**51:5 "Haki yangu i karibu, wokovu wangu umekuwa wazi"** KITENZI (BDB 422, KB 425) ni *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU. Mstari huu wa ushairi unamrandano katika 46:13. YHWH yuko tayari kutenda kazi na kupitia Mtumishi wake. Mstari wa 5 inazungumzia njaa ya kiroho ya mataifa ya Wapagani. Israeli lazima ionywe juu. Wa-Yudea wengi walirudi Palestina wakimtumainia Mungu lakini wengi wao zaidi hawakuamini!. Wale wasiofanya hivyo watakutana Naye kama Hakimu!

◙**"mikono yangu"** Hii ni lugha ya wanadamu kama mstari wa 9; 52:10. Mungu hana mwili. Hii ni sitiari ya shughuli za Mungu katika Historia. Angalia Mada Maalum 41:2.

**51:6 "maana mbingu zitatoweka kama moshi"** Mbingu na nchi walikuwa mashahidi wa kale lakini hata watapita (kama vile 65:17; 66:22; II Pet. 3:10).

◙
**NASB (tanbihi)**
**NKJV, NRSV** **"funza"**
**TEV, REB** **"sufu"**
**NJB** **"funza"**
**JPSOA** **"sawasawa"**

Hii ni tungo ngumu sana. Neno hili katika WINGI mara kwa mara linafasiriwa kama "mbu" (BDB 485 I).

◙**"Wokovu wangu utakuwa wa milele"** Mistari miwili ya mwisho ina mrandano. Umilele wa Mungu unalinganishwa na mtazamo wa ukomo wa ubinadamu (kama vile Mstari 12; 40:6-8; Ayubu 14:1-2; Zab. 90:5-6; 103:15-18; Mt. 24:35; Ebr. 1:10-12; I Pet. 1:24-25).

**51:7 "sikia"** Huu ni wito mwingine wa usikivu (kama vile mstari wa 1).

◙**"yeye ambaye. . ."** Tazama namna gani watu wa Mungu wanapewa sifa.

1. enyi mjuao haki, mstari wa 7a
2. watu ambao ndani ya mioyo yao kuna sheria yangu, mstari 7b (kama vile Yer. 31:31-34)

katika ufahamu

1. msiogope – mstari wa 7c, BDB 431, KB 432, *Qal* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU ikitumika katika hali za HALI YA KUSIHI
2. usiogope – mstari wa 7d, BDB 369, KB 365, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU katika HALI YA KUSIHI

◙**"watu ambao mioyo yao kuna sheria yangu"** Katika maandiko ya Musa nahau hii ya uhusiano wa karibu na kupatikana kwa kudumu kwa kweli kunatumika (kama vile Kutoka. 28:29; Kumb. 6:6). Inatokea katika Fasihi za Hekima (kama vile Mithali 3:3;7:3; Zab. 37:31; 40:8), kama vile Fasihi za Kinabii (kama vile Isa. 51:7; Yer. 17:1).

**51:8 "funza.....sufu"** Wanyama kadhaa wanatajwa katika muktadha huu (kama vile mstari wa 6 [Tanbihi ya NASB], "mbu"). Katika 14:11 na 66:24 "mnyoo" kinatumika kama kiwakilishi kwa mauti na uharibifu. Asili inaondoa badala ya kutoa!

◙**"Haki Yangu . .wokovu Wangu"** Hizi zilikuwa mrandano wa mstari wa 5 pia. Pale walienda mbele lakini hapa wanabaki milele. Angalia Mada Maalum katika 45:17. Mlinganisho wa namna gani kati ya wasioamini na waaminio!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 51:9-11**
**9 Amka, amka, jivike nguvu, Ee mkono wa Bwana;**
**Amka kama katika siku zile za kale,**
**Katika vizazi vile vya zamani.**
**10 Si wewe uliyemkata-kata Rahabu?**
**Uliyemchoma yule joka?**
**Si wewe uliyeikausha bahari,**
**Na maji ya vilindi vikuu;**
**Uliyevifanya vilindi kuwa njia,**
**Ili wapite watu waliokombolewa?**
**11 Nao waliokombolewa na Bwana watarejea,**
**Watafika Sayuni, wakiimba;**
**Furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao;**
**Watapata shangwe na furaha;**

**Huzuni na kuugua zitakimbia.**

**51:9 "Amka, amka"** Hii KAULI SHURUTISHI kwa mara tatu (BDB 734, KB 802, *Qal* KAULI SHURUTISHI) inahitaji matendo: (1) matendo katika upande wa Mungu, mstari wa 9 na (2) matendo katika upande wa Israeli, mstari wa 17 (kama vile 52:1,11).

◙**"Amka kama katika siku zile za kale"** Haya ni maelezo juu ya shughuli za YHWH katika Kutoka (kama vile Kutoka 6:6; Kumb. 4:34; 5:15; 26:8).

◙**"Rahab. . .joka"** Neno hili (KB 1193) lina matumizi matatu.

1. jitu la baharini la kimiujiza – Isa. 51:9; Ayubu 9:13; 26:12; Zab. 74:13; 89:10; 148:7
2. Sitiari kwa Misri ikijikita katika ugeuzaji wa Mto Nile – Isa. 30:7; Zab. 87:4; Ezek. 29:3
3. "wenye kiburi" (NASB, BDB 923) au maadui wa YHWH – Zab. 40:5

Ya 1 pia inaelezewa na neno "nyoka" (BDB 49) katika Ayubu 7:12.

**51:10 "vina"** Hii pia lilikuwa neno la kimiujiza linalotumika katika masimulizi ya uumbaji ya Kisumeri na Kibabeli. Katika Biblia si mungu (kama vile Mwanzo 1:2) lakini kina cha maji – *tiamat* (BDB 1062, 63:13).

◙**"Uliyevifanya vilindi kuwa njia ili wapite watu waliokombolewa"** Hii kidhahiri ni maelezo kwa mgawanyiko wa Bahari ya Shamu wakati wa safari ya kutoka Misri (kama vile Kutoka 14,15).

**51:11** Kama Mungu alivyowaokoa watu wake kutoka katika utumwa wa Misri, ndivyo pia atakavyowaokoa watu wake kutoka kwa Waashuru na uhamisho wa Wababeli! Wazao wa Ibrahimu watarudi kwenye nchi ya ahadi.

◙**"furaha isiyokuwa na mwisho"** Neno "isiyokuwa na mwisho" ni *'olam* (BDB 761). Angalia Mada Maalum katika 45:17. Isaya analitumia mara kwa mara kuelezea zama mpya.

1. agano lisilokuwa na mwisho, 24:5; 55:3; 61:8
2. YHWH kama Mwamba usiokuwa na mwisho, 26:4
3. furaha isiyokuwa na mwisho, 35:10; 51:11; 61:2
4. Mungu asiyekuwa na mwisho, 40:28
5. wokovu usiokuwa na mwisho, 45:17
6. wema usiokuwa na mwisho (*Hesed*), 54:8
7. utawala usiokuwa na mwisho, 55:13
8. jina lisilokuwa na mwisho, 56:5; 63:12,16
9. nuru isiyokuwa na mwisho, 60:19,20

Matumizi yaliyojikita katika hasi yanahusiana na adhabu ya milele kwa wabaya inapatikana katika 33:14, "kuchomwa kwa milele." Isaya mara kwa mara anatumia "moto" kuelezea ghadhabu ya Mungu (kama vile 9:18,19; 10:16; 47:14), "isiyokuwa na mwisho" lakini hapa tu (kama vile Dan. 12:2).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 51:12-13**
***12*Mimi, naam, mimi, ndimi niwafarijiye;**
**wewe u nani hata ukamwogopa mtu atakayekufa,**
**na mwanadamu atakayefanywa kuwa kama majani?**
***13*Ukamsahau Bwana, Muumba wako, yeye aliyezitanda mbingu,**
**na kuiweka misingi ya dunia;**
**nawe unaogopa daima mchana kutwa kwa sababu ya ghadhabu yake yeye aoneaye**
**hapo afanyapo tayari kuharibu;**
**nayo i wapi ghadhabu yake aoneaye?**

**51:12 “mtu. . .mwana wa mtu”** Hii ni njia ya Kiebrania ya kurejerea mwanadamu (kama vile Zab. 8:4; Ezek. 2:1). Ilikuja baadaye kuwa cheo kwa Yesu kwasababu ilithibitisha ubinadamu Wake na kwasababu ya Dan. 7:13, Uungu Wake.

## MADA MAALUM: MWANA WA ADAMU (kutoka Danieli 7:13)

Kifungu cha lugha ya Kiaramu ("*ben enosh*," BDB 1085 MUUNDO WA MANENO na 1081) "mwana wa Adamu" ni tofauti kutokana na kifungu kinachofanana na cha Kiebrania ("*ben adam*") kinachopatikana katika Zaburi na Ezekieli. Vifungu vyote vinatumika katika ufanano kwenye Ayubu 25:6; Zab. 8:4; 90:3; 144:3; Isa. 13:12. Hili ni dhahili linarejerea kwa Masihi na kuhusiana na ubinadamu wake (kama vile Dan. 8:17; Ayubu 25:6; Zab. 8:4; Ezek. 2:1 [na vingine vingi] katika Ezekieli), lenye maana ya fungu la maneno ya Kiarama na Kiebrania, "mwana wa Adamu," akiwa na Uungu wake kwa sababu mawingu husafirisha Uuungu (kama vile Dan. 7:13; Mt. 24:30; 26:64; Marko 13:26; 14:62; Ufu. 1:7; 14:14).

Yesu anatumia kifungu kujirejerea Mwenyewe katika Agano Jipya. Hakikutumika kumhusu Masihi kwenye sheria za Kiyahudi. Hakina vidokezo vya utenganisho, vidokezo vya utaifa, vidokezo vya kijeshi, kipekee kabisa kinamwelezea Masihi kama mwanadamu kamili na Mungu kamili (kama vile 1 Yohana 4:1-3). Matumizi ya Danieli ni ya kwanza ambayo yanatizamisha juu ya dhana ya Uungu!

Yesu alikitumia kifungu kwa ajili yake katika maana tatu.
1. mateso yake na kifo (mf., Marko 8:31; 10:45; 14:21; Luka 9:22,44)
2. ujio wake kama mwamuzi (mf., Mt. 16:27; 25:31; Yn 5:27)
3. kuja kwake katika utukufu kutengeneza ufalme wake (mf., Mt. 16:28; 19:28; Marko 13:26-27; 14:62)

Kutoka katika The Jewish Study Bible, uk . 1657 (pia angalia George E. Ladd, *A Theology of the New Testament,* kur. 136-139), tamaduni za baadaye za Kiyahudi kuhusiana na andiko hili zimeorodheshwa.
1. Huu muktadha ni wa Kimasihi (kama vile I Enoch 46:1; 48:10; 4 Ezra [2 Esdras] sura 13; b. Sanh. 98a)
2. utabiri wote katika muktadha umekwisha kutimia (kama vile b. Sanh. 97b)
3. Muktadha haurejerei siku za mwisho (kama vile Gen. Rab. 98:2)
4. Muktadha huwakilisha Israeli (kama vile Ibn Ezra and Rashi)

◙**“atakayekufa. . .kama nyasi”** Mrandano unasisitiza udhaifu na ukomo wa maisha ya mwanadamu (kama vile 40:6,7; Ayubu 14:1-2; Zab. 90:5-6; 103:15; I Pet. 1:24). Muktadha huu kama I Pet. 1:24-25, unaweka ulinganifu wa nguvu na umilele wa Mungu na ule wa Uuumbaji wake (yaani YHWH kama muumbaji katika mstari wa 13).

**51:13** Hii inaweza kuwa maelezo yaliyofunikwa kuelezea ibada za sanamu za watu wa Mungu katika kuabudu *Ba’al* kama muumbaji na mtoaji wa uhai na ustawi badala ya YHWH. Ibada zao za miungu ndizo zilizosababbisha uhamisho wao na matendo ya watesaji ambao Mungu aliruhusu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 51:14-16**
**[14]Yeye aliyehamishwa na kufungwa atafunguliwa kwa haraka; wala hatakufa na kushuka shimoni, wala chakula chake hakitapunguka. [15]Maana mimi ni Bwana, Mungu wako, niichafuaye bahari, mawimbi yake yakavuma. [16]Bwana wa majeshi ndilo jina lake. Nami nimetia maneno yangu kinywani mwako, nami nimekusitiri katika kivuli cha mkono wangu, ili nizipande mbingu, na kuiweka misingi ya dunia, na kuuambia Sayuni, Ninyi ni watu wangu.**

**51:14** Haya ni maelezo ya matu katika gereza ambao watafunguliwa, ingawa neno “shimo” (BDB 1001, KB 1472) linaweza kurejerea
1. kabuli au *Sheol* – Ayubu 33:22,24,28; Zab. 16:10; 49:9
2. Hapa mrandano unapendekeza “gereza”

**51:15** Kama mistari ya 9-11 mstari huu ni maelezo ya YHWH kuwafungua watu wake kutoka Misri. Pia kama mistari ya 9,10, kuna rejea ya Mwanzo 1, ambapo YHWH anayagawa maji na kuyadhibiti. Angalia kidokezo kamili katika mstari wa 10.

◙**"(BWANA wa majeshi ndilo jina Lake)"** Neno "majeshi" linaweza kutumika katika namna mbili:

1. YHWH kama muumbaji na mdhibiti wa nyota na sayari
2. YHWH kama amiri jeshi Mkuu wa malaika

Katika namna zote mbili uwezekano upo katika mwitikio wa ibada za nyota za Wababeli ambazo ziligeuza vitu zilieleavyo angani kuwa miungu. Angalia Mada Maalum : Majina ya Miungu katika 40:3.

**51:16** Kuna VITENZI JINA vitatu *Qal* katika mstari huu.

1. kupanda (BDB 642, KB 694)
2. kukuta au kuanzisha (BDB 413, KB 417)
3. kusema (BDB 55, KB 65)

Kwa muktadha wa mstari huu unatakiwa uwe na uhusiano wa kukombolewa kwa kurudi kwa Israeli. Hatahivyo VITENZI JINA vina nguvu sana kwa wanadamu kuweza kuvitimiliza. Hatahivyo lazima irejeree "Mtumishi," Waisraeli maaum wa Mungu ambao watatimiliza kile ambacho Israeli hawakutimiliza. Uhamisho katika sura za 40-53 za jina "Mtumishi" kutoka taifa la Israeli, 41:8-9; 42:1,19; 43:10, kuelekea "umoja," 49:1-7 na 52:13-53:12.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 51:17-20**
**17 Amka, amka, simama, Ee Yerusalemu,**
**Wewe uliyenywea, mkononi mwa Bwana, Kikombe cha hasira yake;**
**Bakuli la kikombe cha kulevya-levya Umelinywea na kulimaliza.**
**18 Hapana hata mmoja wa kumwongoza Miongoni mwa wana wote aliowazaa,**
**Wala hapana hata mmoja wa kumshika mkono Miongoni mwa wana wote aliowalea.**
**19 Mambo haya mawili yamekupata;**
**Ni nani awezaye kukusikitikia?**
**Ukiwa na uharibifu, na njaa na upanga; Niwezeje kukutuliza?**
**20 Wana wako wamezimia,**
**Wamelala penye pembe za njia kuu zote Kama kulungu wavuni;**
**Wamejaa hasira ya Bwana,**
**Lawama ya Mungu wako.**

**51:17-20** YHWH anatia moyo watu Wake kupuuzia Hukumu Yake ilokwisha kuwekwa tayari na kuandaa kurudi Yerusalemu!

**51:17 "Amka, amka, simama, Ee Yerusalemu"** Hizi ni KAULI SHURUTISHI tatu katika ubeti kwa ajili ya msisitizo.

1. amka – *Hithpolel* au *Hithpael* (BDB 734, KB 802)
2. ikirudiwa
3. inuka – *Qal* (BDB 877, KB 1086)

◙**"Kikombe....hasira yake"** Hizi mbili zina marandano na zina maanisha nahau ya hukumu kama kikombe cha kinywaji kikali kumfanya mtu alewe na kuanguka (kama vile 29:9; 63:6; Ayubu 21:20; Zab. 60:3; 75:8; Yer. 25:15-16; 51:17; Omb.4:21; Ezek. 23:32-34). Pia tazama matumizi yake katika Agano Jipya.

1. ya Yesu kama mbebe dhambi– Mt. 20:22; 26:38-42; Marko 14:36; Luka 22:42; Yohana 18:11
2. waabuduo mnyama – Ufunuo 14:10; 16:19; 19:15

**51:19** Tazama kile kilichotokea kwa watu wa agano na namna inavyotokea kwa Babeli.

1. kukengeuka (BDB 994)
2. uharibifu(BDB 991)
3. njaa (BDB 944)
4. upanga (BDB 352)

Hakuna hata mtu mmoja wa kuifaliji Babeli; Yupo wa kufariji uzao wa Ibrahimu (kama vile mistari ya 3,12; 40:1).

**51:20** Wakati Ashuru na Babeli alipouvamia mji waliuwa wazee, vijana na wenye nguvu katika eneo lililokuwa likijulikana na bayana (yaani "katika kituo cha kila mtaa"). Hivyo, tendo hili ovu bado linafanywa kwao.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 51:21-23**
**21 Basi, kwa sababu ya hayo, ulisikilize neno hili, ewe uliyeteswa,**
**na kulewa, lakini si kwa mvinyo;**
**22 Bwana, Bwana wako na Mungu wako, awateteaye watu wake,**
**asema hivi, Tazama, nimeondoa mkononi mwako kikombe cha kulevya-levya,**
**hilo bakuli la kikombe cha hasira yangu; hutakinywea tena;**
**23 nami nitakitia mikononi mwao wakutesao;**
**waliokuambia nafsi yako, Inama, tupate kupita;**
**nawe uliufanya mgongo wako kuwa kama nchi,**
**na kama njia, kwa hao wapitao juu yake.**

**51:21-23** Mungu alihaidi kuchukua hukumu ya kikombe Chake, ambacho kiliwachanganya Israeli na Yuda na hata kukitoa kwa watesi wao. Ashuru na Babeli watavuna sawasawa na kile walichopanda (kama vile 17:10; 32:19; Gal. 6:7-10)! Mungu anashughulikia muda na historia!

**51:23 "wapitao juu yake"** Huku kukanyaga juu ya waliokufa kwa kushindwa kunachukuliwa katika sanaa za ukutani za Kimisri (kama vile IVP Bible Background Commentary, ukurasa wa 633).

1. "lala chini" – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 1005, KB 1457)
2. "tembea juu yako" *Qal* HALI YA KUSIHI (BDB 716, KB 778)

# ISAYA 52:1-12

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Aliyeteuliwa kwa ajili ya kuisujudia Sayuni | Mungu Aikomboa Yerusalemu | Ufalme wa Mungu (51:17-52:12) | Mungu ataikomboa Yerusalemu | Ukombozi wa Yerusalemu |
| 52:1-2 (1-2) | 52:1-2 (1-2) | 52:1-2 (1-2) | 52:1-2 (1-2) | 52:1-2 (1-2) |
| 52:3-6 (3-6) | 52:3 | 52:3-6 | 52:3-6 | 52:3-6 |
| 52:4-6 (4-6) | | | | |
| 52:7-10 (7-10) | 52:7-10 (7-10) | 52 :7-10 (7-10) | 52:7-8 (7-8) | 52:7-12 (7-12) |
| 52:9-12 (9-12) | 52:11-12 (11-12) | 52:11-12 (11-12) | 52:11-12 (11-12) | |
| Mtumishi Aliyetukuzwa Wimbo wa Mtumishi | Wimbo wa Mtumishi kuhusu Mwenendo wa dhambi (52:13-53:12) | Wimbo wa nne wa Mtumishi (52:13-53:12) | Mtumishi Ateswaye (52:13-53:12) | Wimbo wa nne wa Mtumishi (52:13-53:12) |
| 52:13-15 (13-15) | 52:13-15 (13-15) | 52:13-15 (13-15) | 52:13-15 (13-15) | 52:13-15 (13-15 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Muktadha wa sura ya 51 unaendelea kupitia 52:12.
B. Watambue watu tofautitofauti ambao wana wanatolewa ufafanuzi wa hizi KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU (52:1-52:12).

1. Watu wangu. . .Enyi mataifa yangu (51:4-8)
    a. Nisikilizeni – *Hiphil* (BDB 904, KB 1151
    b. nisikieni – *Hiphil* (BDB 24, KB 27)
    c. Inueni macho yenu – *Qal* (BDB 669, KB 724)
    d. mkaitazame – *Hiphi l*(BDB 613, KB 661)
    e. nisikieni – *Qal* (BDB 1033, KB 1570)
2. Ee mkono wa Bwana (51:9-11)
    a. amka – *Qal* (BDB 734, KB 802)
    b. amka – ni sawa na kifungu cha "jivike – *Qal* (BDB 527, KB 519)
    c. amka – ni sawa na "a"
3. Yerusalemu (51:17-23)
    a. amka – *Hithpolel* au *Hithpael* (BDB 734, KB 802)
    b. amka – ni sawa na "a"
    c. amka – *Qal* (BDB 872, KB 1086)
4. Sayuni , Ee Yerusalemu (52:1)
    a. amka – *Qal* (BDB 734, KB 802)
    b. jivike – ni sawa na "a"
    c. jivike – *Qal* (BDB 527, KB 519)
    d. jivike – sawa na "c"
5. wamechukuliwa (52:5)
    a. ikung'ute – *Hithpael* (BDB 654, KB 707)
    b. uondoke – *Qal* (BDB 877, KB 1086)
    c. Jifungulie – *Hithpael* (BDB 605, KB 647 [toleo la MT lina JINSI YA KIUME bali *qere* ni JINSI YA KIKE)
6. iyobainishwa (52:9-10, inaendana na #1,3,4, au 5)
    a. imbeni pamoja – *Qal* (BDB 822, KB 953)
    b. Pigeni kelele za furaha – *Piel* (BDB 943, KB 1247)
7. isiyobainishwa (52:11-12, inayobainishwa #1,3,4, au 5)
    a. nendeni zenu – *Qal* (BDB 693, KB 747)
    b. nendeni zenu – sawa na "a"
    c. tokeni huko – *Qal* (BDB 422, KB 425)
    d. msiguse kitu kichafu – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI (BDB 619, KB 668)
    e. tokeni kati yake – ni sawa na "c"
    f. iweni safi ninyi – *Niphal* (BDB 140, KB 162)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 52:1-2**
[1]**Amka, amka,**
**jivike nguvu zako, Ee Sayuni;**
**Jivike mavazi yako mazuri,**
**Ee Yerusalemu, mji mtakatifu;**
**Kwa maana tokea sasa hataingia ndani yako Asiyetahiriwa, wala aliye najisi.**
[2]**Jikung'ute mavumbi; uondoke,**
**Uketi, Ee Yerusalemu; Jifungulie vifungo vya shingo yako,**
**Ee binti Sayuni uliyefungwa**.

**52:1-2 "amka. . . jivike. . . ikung'ute . . . uondoke"** Huu ni mfululizo wa KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU (angalia Tambuzi za Kimuktadha, B), kama 51:9,17. Walio wengi wanakilinganisha kifungu hiki na hali chanya ya mji wa Babeli katika 47:1na kuendelea.

**52:1e "Asiyetahiriwa, wala aliye najisi**
**Kwa maana tokea sasa hataingia ndani yako "** Kipengele hiki hakiweze kulilejelea tendo la kutengwa kwa Mataifa kutoka katika ukombozi, bali ni kwamba hakuna mpagani ambaye angeivamia tena Nchi ya Ahadi . Hili linaweza kuwa chimbuko la taswira ya Yohana katika Ufu. 21:27.

**52:2**
**NASB, NRSV,**
**NJB, NET "mliochukuliwa"**
**NKJV "kaa chini"**
**LXX, Vulgate,**
**TEV, JPSOA "mliokaa [juu ya kiti chako cha enzi]"**

Toleo la MT lina kifungu "kaa" (BDB 442, KB 444, *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, שבי,lakini baadaye katika mstari שביה(BDB 985), kinatafsiriwa kama "mliochukuliwa"). Toleo la UBS Text Project linalipa neno "mliokaa" daraja B (kuna mashaka fulani). Yampasa Israeli kuamka na kaka juu ya kiti chake cha enzi.

◙**"uondoke"** Hili ni eneo ambalo toleo la MT lina muundo wa JINSI YA KIUME WINGI ya *Hithpael* KAULI SHURUTISHI, lakini wasomi wa Kiamsoteriki walipendekeza (*qere*) muundo wa JINSI YA KIKE UMOJA.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 52:3-6**
**[3]Maana Bwana asema hivi, Mliuzwa bure; nanyi mtakombolewa bila fedha. [4] Maana Bwana MUNGU asema hivi, Watu wangu hapo kwanza walishuka Misri ili wakae huko hali ya ugeni; na Mwashuri akawaonea bila sababu. [5] Basi sasa, nafanya nini hapa, asema Bwana, ikiwa watu wangu wamechukuliwa bure? Hao wanaowatawala wanapiga yowe, asema Bwana, na jina langu linatukanwa daima mchana kutwa. [6] Kwa hiyo watu wangu watalijua jina langu kwa hiyo watajua siku ile ya kuwa mimi ndimi ninenaye; tazama ni mimi.**

**52:3 "mtakombolewa bila fedha"** Mstari huu lazima uonekane katika mwelekeo 45:13. Koreshi atawaachilia Wayahudi kurudi makwao kwa uhuru. Koreshi aliirejeleasera ya maboresho ya makazi ya nchi zote za Waashuru na Wababeli. Huyu aliwaruhusu watu wote waliokuwa wakitawaliwa kurudi katika makazi yao nan a kujeyajenga mahekalu ya taifa mataifa yao. Hii ilikuwa njia yake ya kuurejesha mpangilio wake kwa himaya yake na pia alikuwa mshirikina na aliyataka makundi yote ya watu waliorejea kuiomba miungu yao kwa ajili yake na warithi wake.

**52:4-5** Mstari wa5 unaurejelea uhamisho wa Babeli ingawa Babeli haitajwi kwa jina lake. Mistarai hii inayaangalia mateso ya wakati uliopita (yaani, Misri na Ashuru). Kithiolojia Israeli na Yuda walikuwa uhamishoni kwa sababu ya dhambi zao dhidi ya YHWH(kama vile 43:22-24; 50:1).

**52:4"Misri. . .Ashuru**" Hawa walikuwa maadui wawili wa awali wa Wayahudi kabla yaBabeli (kama vile 10:5 na kuendelea).

**52:5** Kuna namna kadhaa za kulitazamia andiko la Kiebrania.

1. Watawala ("wale watawalao," BDB 605, KB 647, *Qal* ya KAULI ENDELEVU)
    a. watawala wa Yerusalemu watakao "omboleza" (BDB 410, KB 413, *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) juu ya kuanguka kwa Yerusalemu
    watawala wa Babeli "huiga" kama Yerusalemu ilivyoanguka

◙**"jina langu linatukanwa daima"** Hiki KITENZI (BDB 610, KB 658) ni muundo wa *Hithpolel* ulio adimu. Jina la Mungu lilihusianishwa na hali ya Israeli. Mungu atatenda, si kwa sababu ya uzuri wa Israeli bali ni kwa sababu ya jina lake (kama vile 48:11; Eze. 20:9,14,22,44;36:19-20,22-23; Dan. 9:17-19; Rum. 2:24).

**52:6** Kwa ukombozi waYHWH watu wake watatambua kwamba imaliimarisha agano upya. Jina lake litakuwa na maana tena!

## MADA MAALUM: JINA LA YHWH (AGANO LA KALE)

Utumiaji wa "jina" kama mbadala kwa ajili ya YHWH Mwenyewe unafanana na ule wa Kut. 23:20-33 wa utumiaji wa neno "malaika," ambaye anasemekana kuwa na kifungu cha maneno "Jina Langu li ndani yake." Mbadala wa aina ile ile waweza kuonekana katika utumiaji wa maneno "utukufu Wake" (yaani., Yohana 1:14; 17:22; angalia Mada Maalum: Mungu Anaelezewa kama Mwanadamu). Haya yote ni kujaribu namna ya lugha ya binadamu kuelezea uwepo binafsi wa YHWH (kama vile Kut. 3:13-16; 6:3). Hakika YHWH ameongelewa katika maneno ya kibinadamu,lakini pia ilikuja kujulikana kuwa kiroho alikuwepo wakati wa uumbaji wote (kama vile 1 Fal. 8:27; Zab. 139:7-16; Yer. 23:24; Mdo. 7:49 inairejea Isa. 66:1).

Kuna mifano mbalimbali ya "jina" lenye kuwakilisha maana ya Uungu wa YHWH na uwepo wake binafsi.

1. Kumb. 12:5; 2 Sam. 7:13; 1 Fal. 9:3; 11:36
2. Kumb. 28:58
3. Zab. 5:11; 7:17; 9:10; 33:21; 68:4; 91:14; 103:1; 105:3; 145:21
4. Isa. 48:9; 56:6
5. Ezek. 20:44; 36:21; 39:7
6. Amosi 2:7
7. Yn 17:6,11,26

Dhana ya "wito" (yaani., kuabudu) jina la YHWH linaonekana mwanzoni mwa kitabu cha Mwanzo.

1. Mwa. 4:26, uzao wa Sethi
2. Mwa. 12:8, Ibrahamu
3. Mwa. 13:4, Ibrahamu
4. Mwa. 16:13, Hagai
5. Mwa. 21:33, Ibrahamu
6. Mwa. 26:25, Isaka

Na katika kitabu cha Kutoka:

1. Kut. 5:22-23, kusema naye kwa jina lako
2. Kut. 9:16, kutangaza jina Langu katika dunia yote (kama vile Rum. 9:17)
3. Kut.20:7, usilitaje jina la Bwana Mungu wako bure (kama vile Law. 19:12; Kumb. 5:11; 6:13; 10:20) Kut. 20:24, nitakapotia ukumbusho wa jina langu (kama vile Kumb. 12:5; 26:2)
4. Kut. 23:20-21,malaika ("kwa kuwa jina langu liko ndani yake")
5. Kut. 34:5-7, Musa analiita (au "kuliitia") jina la Bwana. Haya ni moja ya maandiko machache yenye kuielezea tabia ya YHWH (kama vile Neh. 9:17; Zab. 103:8; Yoel 2:13)

Kumjua mtu kwa jina lake ni kumaanisha ule ukaribu uliopo (kama vile Kut. 33:12); Musa alilijua jina la YHWH na katika 33:17, YHWH alilijua jina la Musa. Huu ni ule muktadha ambao Musa alihitaji kuuona utukufu wa Mungu (kama vile mst. 18), lakini Mungu aliruhusu kuuona "wema wake" (mst. 19), ambao ni wenye kufanana na "jina" (mst. 19).

Waisraeli walitakiwa kuangamiza "jina " la miungu wa Kanaani (kama vile Kumb. 12:3) na kuliitia jina lake (kama vile Kumb. 6:13; 10:20; 26:2) mahali litakapotia ukumbusho wa jina lake (kama vile Kut. 20:24; Kumb. 12:5,11,21; 14:23,24; 16:2,6,11; 26:2).

YHWH ana kusudi la wote likihusisha jina lake.

1. Mwa. 12:3

2. Kut. 9:16
3. Kut. 19:5-6
4. Kumb. 28:10,58
5. Mika 4:1-5

◙**"siku ile"** Angalia Mada Maalum kutokana na maoni yangu juu ya Manabii wa Karne ya Nane , hapa chini.

## MADA MAALUM: SIKU HIYO

Kifungu, "siku hiyo" au "kwenye siku hiyo," ni namna ya manabii wa karne ya nane kuzungumzia juu ya ujirio wa Mungu (uwepo), kwa ajili ya hukumu na urejesho.

| **Hosea** | | **Amosi** | | **Mika** | |
|---|---|---|---|---|---|
| chanya | hasi | chanya | hasi | chanya | hasi |
| 1:11 | 1:5 | | 1:14(2) | | 2:4 |
| | 2:3 | | 2:16 | | 3:6 |
| 2:15 | | | 3:14 | 4:6 | |
| 2:16 | 4:5 | | 5:18 (2) | | 5:10 |
| 2:18 | 5:9 | | 5:20 | | 7:4 |
| 2:21 | 6:2 | | 6:3 | 7:11(2) | |
| | 7:5 | | 8:3 | 7:12 | |
| | 9:5 | 9:11 | 8:9 (2) | | |
| | 10:14 | | 8:10 | | |
| | | | 8:13 | | |

Kipengele hiki kiuhalisia kinazungumzia juu ya manabii. Mungu anakwenda kutenda dhidi ya dhambi kwa wakati, lakini pia hutoa siku toba na msamaha kwa wale wanaopenda kubadili mioyo na matendo yao (yaani., kupokea roho mpya, mawazo mapya, na roho mpya, kama vile Ezek. 36:22-27)! Kusudi la Mungu la ukombozi na urejesho utatimilizwa! Atakuwa na watu watakaoaksi tabia Zake. Kusudi la uumbaji (ushirika kati ya Mungu na mwanadamu) utatimilizwa!

◙
**NASB, NJB,**
**REB** **"ni mimi"**
**NKJV** **"Tazama, ni mimi"**
**NRSV** **"ni mimi"**
**JPSOA** **"sasa niko mkononi"**
**LXX** **"niko hapa"**
**Peshitta** **"ni mimi"**

Mara nyingi hiki ni kifungu cha mwitikio wa imani kutoka kwa mwanadamu ambaye ameusiwa na Mungu (yaani, Mwa. 22:1,11; Kut.. 3:4; Isa. 6:8). Hiki kinaweza kudokeza juu ya kuwepo kwa mapenzi ya Mungu.

Ni katika Isaya pekee ambapo kifungu hiki kinatumika kwa Mungu na kkudokeza juu ya uwepo wake, uweza, na uwezo wa kulitenda lilie aliloliahidi (kama vile 58:9; 65:1).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 52:7-10**
7 **Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima Miguu yake aletaye habari njema,**
**Yeye aitangazaye amani,**
**Aletaye habari njema ya mambo mema,**
**Yeye autangazaye wokovu,**
**Auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki!**
8 **Sauti ya walinzi wako! Wanapaza sauti zao, wanaimba pamoja;**
**Maana wataona jicho kwa jicho, Jinsi Bwana arejeavyo Sayuni.**
9 **Pigeni kelele za furaha, imbeni pamoja,**
**Enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa;**
**Kwa kuwa Bwana amewafariji watu wake, Ameukomboa Yerusalemu.**
10 **Bwana ameweka wazi mkono wake mtakatifu Machoni pa mataifa yote;**
**Na ncha zote za dunia Zitauona wokovu wa Mungu wetu**.

**52:7-9** Mistari hii inatumia mistiri ya(1) mjumbe wa serikali aletaye habari njema (kama vile mst. wa 7) na (2) mlinzi (kama vile mst. wa 9) katika lango la kuutangazia mji wote. Mji ni Sayuni; habari njema ni kwamba YHWH anatawala tena kama Mfalme wa watu wake waliorejeshwa.

**52:7** KITENZI cha Kiebrania "Aletaye habari njema" (BDB 142, KB 163, *Piel* ya KAULI YA WAKATI ENDELEVU, mara mbili) kinadokezwa katika Rum. 10:15 kwa kifungu "habari njema" za injiliya Yesu Kristo (kama vile Isa. 52:13-53:12).

◙Utambue ufanano kati ya habari njema iliyotangazwa.
1. amani (BDB 1022)
2. furaha/nzuri (BDB 373 I)
3. wokovu (BDB 447)

## MADA MAALUM: AMANI *(SHALOM)*

Neno la Kiebrania *shalom* (BDB 1022, KB 1532) ni la kawaida katika asili ya Kisemiti.

A. Lugha ya Akkadia
   1. Kutokudhurika
   2. Kuishi vizuri
   3. Kuwa katika hali nzuri
B. Ugariti (Wakaanani)
   1. Kutodhurika
   2. Kuwa mzima
C. Kiarabu
   1. Kuwa mwenye afya
   2. Kuwa katika hali ya amani
D. Kiarama
   1. Kuwa mkamilifu
   2. Kufikia mwisho/kuhitimisha
   3. Kuhitmisha amani
   4. Kubaki pasipo kudhuriwa
E. Vidokezo vya Kiebrania
   1. Kuwa mtimilifu
   2. Mwenye kusikika
   3. Kustawi
   4. amani

siku hizi neno *shalom* ni neno la salamu na maelezo ya kutakiana heri. Bado linamaanisha kukosekana kwa uovu na uwepo wa mema(yaani., kutosheka na maisha). Inamaanisha hali ya akili ya usalama na utosherevu. Tambua namna Agano la Kale linavyozungumzia juu ya "agano la amani" (kama vile Hes. 25:12; Ezek. 34:25; 37:26; pia kumbuka Mwa. 26:29,31; Yos. 9:15). Lazima litendeke (kama vile Zab. 34:14; Rum. 14:19). AB, juzuu. 5, uk. 206, inasema, "amani," "ukweli," na "haki" zinafanana na dhana ya Kiebrania (kama vile Zak. 8:16-19). YHWH anaitwa "Bwana wa amani" (kama vile Amu. 6:24; Rum. 16:20; 2 Kor. 13:11; Fil. 4:9; 1 The. 5:23). Masihi ataitwa "Mfalme wa Amani" (kama vile Isa. 9:5). Siku mpya wakati amani, ukweli, na haki itakuwa wazi kwa uzoefu wa mwanadamu (kama vile Isa. 60:17; 66:12,22). "uzuri" wa Mwanzo 1:31 tena ni uwezekana, ahadi (yaani., "mbingu mpya na nchi mpya").

◙ "**Mungu wako anamiliki**" Hiki kifungu cha (BDB 573, KB 590, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ni utimilifu wa 24:23. Hiki kinaweza kuuakisi taratibu wa liturgia inayojulikana (kama vile Zab. 93:1; 96:10; 97:1; 99:1).

**52:8**
**NASB, TEV,**
**NJB "wataona jicho kwa jicho "**
**NKJV "wataona jicho kwa jicho"**
**NRSV "katika taswira ya macho yao"**
**JPSOA "kila jicho litatazama"**
**NET Bible "wataona kwa macho yao"**

Toleo la MT lina kifungu "jicho kwa jicho." Leupold, katika maoni yake kuhusiana na Isaya, anatengeneza hija nzuri."Hiki kifungu 'jicho kwa jicho' kina maana kamili iliyo tafauti katika lugha ya Kiingereza kuliko lugha ya Kiebrania. Katika lugha ya Kiingereza kifungu hiki kinamaanisha jambo fulani kama kukubali moja kwa moja katika mtazamo wa mtu na maoni yake pamoja na mtu mwingine. Katika Kiebrania maana yake ni 'kuukaribia mkono,' kitu kama kuwa karibu ya kwamba unaweza kuuona ule weupe wa macho ya mtu aliyekaribu" (uk. wa 219).

**52:10** Israeli ilihimarishwa na YHWH kuwa ufalme wa makuhani ulimwenguni (kama vile Mwa. 12:3; Kut.19:4-6). Hata hivyo, uvunjifu wa agano uliihitaji hukumu ya Mungu, hivyo, ulimwengu kamwe haukuiona sifa ya Mungu. Kwa Mungu kuikomboa Israeli kutoka matekanai, Misri ya Kwanza, kisha Ashuru, na sasa Babeli, watu wote wa dunia hii wataiona nguvu , pendoe, na Baraka za Mungu.

◙ **"ameweka wazi mkono wake"** Hiki KITENZI (BDB 362, KB 359, *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU) ni stiarai ya lugaha ya kibinadamu (angalia Mada Maalum katika 41:2) kwa utayari wa YHWH kutenda/kukomboa (kama vile Eze. 4:7).

Mara nyingi kifungu "ameweka wazi mkono wake" linadokeza matendo ya ki-Ungu (kama vile Kut. 6:6; Kumb. 4:34; 5:15; 26:8). Angalia maelezo katika 51:9.

◙**"Machoni pa mataifa yote"** Kifungu hiki kinafanana na kifungu kinachofuatia, "miisho yote ya dunia iyaona." Pia kifungu hiki kinafanana na kifungu "kila chenye mwili kitaona" (40:5; pia tambua Yoeli 2:28 kwa taswira yote ya kiulimwengu).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 11:12**
[11]**Nendeni zenu, nendeni zenu, tokeni huko,**
**msiguse kitu kichafu; tokeni kati yake;**
**iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana.**
[12]**Maana hamtatoka kwa haraka,**
**wala hamtakwenda kwa kukimbia,**
**kwa sababu Bwana atawatangulia;**
**na Mungu wa Israeli atawafuata nyuma; awalinde**

**52:11-12** Misari hii inatumia mingozo ya Mungu kwa makuhani (kama vile mst. wa 11d) kama njia ya kuhakikisha kwamba Mungu yu pamoja na watu wote wa agano nay u pamija nao (kama vile mst. wa 12). Hili ni angalizo lililofichwa la kuziacha ibada za miungu ya Mesopotamia nyuma yao!

Watu hawa waliorejea watachukua vyombo kutoka katika hekalu la YHWH lililo miongoni mwao (kama vile Ezra 1:5-11; 5:14; 6:8; pia tambua II Nyakati 4 ambapo watu hawa wanatolewa ufafanuzi). Hawa waliicha Babeli kama walivyoiacha Misri (kama vile Kut.11:2; 12:35-36) kama mateka wan chi pamoja nao (yaani, ishara ya kuliondosha taifa na miungu yake).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri. Hii inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Isaya anautumia wito wa Ibrahimu kama kuwatia moyo Wayahudi katika hali yao ya kuwa mateka?
2. Ni kwa namna gani uumbaji na kitabu cha Kutoka vinasababisha kuwatia moyo Israeli na Yuda?
3. Je! Sura ya 51:16 inamrejelea nani?
4. Je! Ni kwa namna gani Mungu alilitumia taifa la Israeli kuyafikia Mataifa?

# ISAYA 53 (52:13-53:12)

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mtumishi mwenye Mateso | Mtumishi mwenye kuibeba dhambi (52:13-53:12) | Wimbo wa nne wa mtumishi (52:13-53:12) | Mtumishi mwenye mateso (52:13-53:12) | Wimbo wa nne wa mtumishi (52:13-53:12) |
| 53:1-3 (1-3) | 53:1-3 (1-3) | 53:1-3 (1-3) | 53:1-3 (1-3) | 53:1-7 (1-7) |
| 53:4-6 (4-6) | 53:4-6 (4-6) | 53:4-6 (4-6) | 53:4-6 (4-6) | |
| 53:7-9 (7-9) | 53:7-9 (7-9) | 53:7-9 (7-9) | 53:7-9 (7-9) | |
| | | | | 53:8-9 (8-9) |
| 53:10-12 (10-12) | 53:10-12 (10-12) | 53:10-12 (10-12) | 53:10-12 (10-12) | 53:10 (10) |
| | | | | 53:11 (11) |
| | | | | 53:12 (12) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI(angalia uk.wa xxiv kipengere cha utangulizi)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya ya tatu
12. Nk

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Hili ni andiko muhimu kwa ajiri ya kulielewa Agano jipya juu ya huduma na utambulisho wa Yesu kama mtumishiwa YHWH mwenye kuteseka. Tambua mahali pale palipo rejewa au dokezwa katika agano Jipya.
    1. 52:15 – Rum. 15:21
    2. 53:1 – Rum. 10:16; Yn 12:38
    3. 53:3 – Luka 18:31-33 (dokezo); Marko 10:33-34 (dokezo); Yn 1:10-11 (dokezo)

4. 53:4 – Mt. 8:17; I Pet. 2:24 (dokezo)
5. 53:5 – Rum. 4:25 (dokezo); I Kor. 15:3 (dokezo); Ebr. 9:28 (dokezo); I Pet. 2:24-25 (dokezo)
6. 53:6 – I Pet 2:25 (dokezo)
7. 53:7-8 – Mt. 26:63 (dokezo); Mt. 27:12-14 (dokezo); Marko 14:61 (dokezo); Marko 15:5 (dokezo); Luka 23:9 (dokezo); Yn 19:9 (dokezo); Mdo 8:22-23 (dondoo); I Pet. 2:23 (dokezo)
8. 53:9 – Mt. 27:57-60 (dokezo); I Pet. 2:22
9. 53:10 – Yn 1:29 (dokezo); Marko 10:45 (dokezo)
10. 53:11 – Yn 10:14-18 (dokezo); Rum. 5:18,19 (dokezo); I Pet. 2:24 (dokezo)
11. 53:12 – Luka 22:37; 2 Kor. 5:21 (dokezo); Fil. 2:6,7 (dokezo)

B. Ninashangazwa kwamba andiko hili la mbadala halirejelewimoja kwa moja katika Agano jipya. Upendeleo wangu kama Mkristo wa kiinjilisti unaonekana dhahili juu ya muktadha huu.kwangu mimi Agano la kale ni lazima lijitafsiri kwenye nuru ya siku zake (yaani ., kusudi la kiuandishi),lakini pia kwa kutumia maandiko yote (2 Tim. 3:16), ni lazima tusome Agano la kale kupitia ufunuo wa Yesu na mitume.

C. Nafikilia njia ya kusaidia kuukabili wimbo/shairi la agano la kale hili la nguvu, na kwa maana ya kipekee, ingalikuwa
1. Kutambua beti zilizopo
2. Kumtambua mnenaji
3. Kuuelezea ujumbe

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 52:13-15**
**[13]Tazama, mtumishi wangu atatenda kwa busara,**
**atatukuzwa, na kuinuliwa juu, naye atakuwa juu sana.**
**[14] Kama vile wengi walivyokustaajabia,**
**(uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu ye yote,**
**na umbo lake zaidi ya wanadamu),**
**[15]ndivyo atakavyowasitusha mataifa mengi;**
**wafalme watamfumbia vinywa vyao;**
**maana mambo wasiyoambiwa watayaona;**
**na mambo wasiyoyasikia watayafahamu.**

**52:13 "atatenda"** KITENZIhiki (BDB 968, KB 1328, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kina madokezo mawili.
1. Ili waone, na kujua, na kufikiri – Isa. 41:20; 44:18; Kumb. 32:29; Zab. 64:9
2. kutukuzwa, "kuinuliwa juu" – I Sam. 18:15; Isa. 52:13; Yer. 20:11; 23:5

Swali ni kuwa ni upi mfanano mzuri kati ya hivi VITENZI vyenye kufuatana "atatukuzwa" "kuinuliwa juu", na "atakuwa juu sana". Je mtumishi atakuwa
1. anasikilizwa
2. Kuinuliwa juu

Yote haya yanafaa kwenye muktadha wa Sura ya 44-55.

◙**"atatukuzwa, na kuinuliwa juu, naye atakuwa juu sana."** Swali lenye kuwa na VITENZI vitatu vikiwa na maana yenye kufanana vinapanua wazo.
1. atatukuzwa – BDB 926, KB 1202, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile. 6:1; 57:15
2. kuinuliwa juu – BDB 669, KB 724, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (na *waw*), kama vile. 6:1; 33:10; 57:15

3. Atakuwa juu sana – BDB 146, KB 170, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (ikiwa na*waw*), kama vile. 5:16

**52:14**
**NASB, NKJV,**
**LXX "itakushangaza wewe"**
**NRSV "itamshangaza yeye"**
**NJB "atashikwa na hofu"**
**JPSOA "yeye ataogopeshwa"**
**REB "atarudi nyuma mbele zake"**
**Peshitta "yeye atastaajabu"**

Toleo la MT lina neno "wewe"עליד(pia toleo LXX), lakini neno "yeye"עליו linasomeka kwenye toleo la Targums na baadhi ya matoleo ya Kishamu. Toleo la UBS linatoa alama B kwenye neno "wewe".

Kuna sintofahamu kati ya mtazamo wa jamii nzima juu ya neno ("wewe") na mtu mmoja mmoja juu ya neno ("yeye") katika nyimbo za mtumishi. Mwisraeli mmoja mmoja alilipa gharama kamilifu kwa ajili ya kundi la Isareli (kama vile. 53:8) na jamii ya watu!

◙**"mtu wangu"** Hili haliko kwenye maandiko ya Kiebrania cha Kimasoreti. Mtumishi hatambuliwi na jamii ya Israeli bali kwa mtu mmoja mmoja, Mwisraeli kamili.

◙**"uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu ye yote,**
**na umbo lake zaidi ya wanadamu "** Yesu alipigwa vibaya sana, kiasi cha kutotambulika , kwanza na baraza kuu la Sinagogi na baadae kwa askari wa kirumi. Waalimu wa dini ya kiyahudi wanautumia mstari huu kusema kwamba Masihi atakuwa na ukoma.

◙
**NASB, NKJV "atakavyowashitusha"**
**NRSV, JPSOA,**
**NET "shitua"**
**NJB, LXX "shangaza"**
**Peshitta "safisha"**

Hili ni neno la kidhabihu (BDB 633 I, KB 683, *Hiphil* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile. Kut. 29:21: Law. 4:6; 8:11; 14:7). Tafsiri nyingi za kisasa zina neno"shitusha" (BDB 633 II, "sababisha kuruka"), ambalo linatokana na asili ya Kiarabu. Hii linafuatiwa na toleo la LXX na Vulgate.

Swali ni " je ni kwa namna gani wafalme wanasikia na kuona?"

1. Mtu aliyeharibiwa (mstr. 14; 53;5)
2. Mtu ambaye atatukuzwa, kuinuliwa juu, na atakuwa juu sana (mst. 13)

Je? KITENZI cha mst. 15a kinamaanisha:

1. kushituka kwa furaha
2. kushituka kwa mshangao
3. Atakavyowashtusha kama dhabihu (kama vile. 53:4-5,10)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 53:1-3**
**1 Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta?**
**Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani?**
**2 Maana alikua mbele zake kama mche mwororo,**
**Na kama mzizi katika nchi kavu;**
**Yeye hana umbo wala uzuri;**
**Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.**
**3 Alidharauliwa na kukataliwa na watu;**
**Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko;**
**Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao,**
**Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.**

**53:1 "Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta "** Mnenaji (WINGI) hajulikani , lakini huenda ni (1)mabaki ya wayahudi waaminifu au (2) manabii. Ni wazi kwamba ni wachache sana wanaelewa dhana ya Masihi aliyeteseka (kama vile. Yn 12:38; Rum. 10:16)! Hata hivyo, siku moja wafalme wa ulimwengu wataelewa (kama vile. 52:15 na Fil. 2:6-11)!

Kwa ajiri ya "waamini" (BDB 52, KB 63, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) tazama mada maalum katika 42:3.

◙**"mkono wa BWANA"** Hiki ni kifungu chenye lugha ya mwanadamu kumwelezea Mungu (kama vile. 51:9; 52:9,10; Kumb. 5:15, tazama mada maalum katika 41:2) kwa ajiri ya matendo ya YHWH,hapa inahusiana na huduma ya mtumishi.

**53:2 "kama mche mwororo"** Hii (BDB 413) inarejelea mwanzo wake usioonekana kwa urahisi. Ina maana sawa na uhusiano na neno la Kimasihi "tawi" (BDB 666, kama vile. Isa. 4:2; 11:1,10). Yote yametumika pamoja katika Isa. 11:1.

## MADA MAALUM:YESU MNAZARETI

Kuna maneno mbalimbali ya Kiyunani ambayo Agano Jipya hutumia kumzungumzia Yesu.

A. Haya ni maneno ya Agano Jipya
   1. Nazareti – mji katika Galilaya (kama vile Luka 1:26; 2:4,39,51; 4:16; Matendo 10:38). Mji huu hautajwi katika vyanzo vya wakati huu, bali umekutwa katika kumbukumbu ya maandishi ya baadaye. Kwa upande wa Yesu kuwa alitoka Nazarethi haikujitosheleza (kama vile Yohana 1:46). Alama ya msalaba wa Yesu ambayo imeliweka jina la eneo hili ilikuwa alama ya aibu kwa Wayahudi.
   2. Nazarēnos – pia inataja maeneo ya kijiografia (kama vile Luka 4:34; 24:19).
   3. Nazōraios – inaweza kuurejea juu ya mji, lakini pia ingeweza kuwa mwaminifu na mtenda haki Masihi wa Kiebrania "Utanzu" (netzer, BDB 666, KB 718 II, kama vile Isa. 11:1; maana zinazokaribiana, BDB 855, Yer. 23:5; 33:15; Zek. 3:8; 6:12; iliyodokezwa katika Ufu. 22:16). Luka akilitumia hili kumhusu Yesu katika 18:37 na Matendo 2:22; 3:6; 4:10; 6:14; 22:8; 24:5; 26:9.
   4. Iliyohusiana na #3 nāzir (BDB 634, KB 684), ambalo linamaanisha "aliyewakifishwa kwa maana ya nadhiri."

B. matumizi ya Kihistoria ya neno nje ya Agano Jipya.
   1. Lilimaanisha kundi la ausi la Kiyahudi (Mkristo wa awali) (nāsōrayyā ya Kiaramu).
   2. Lilitumika katika mzunguko wa Kiyahudi kuwatambulisha waamini katika Kristo (kama vile Matendo 24:5,14; 28:22, nosri).
   3. Lilikuja kuwa neno la kawaida katika kumaanisha waamini katika makanisa ya Kisiria (Kiaramu). "Mkisto" lilitumika katika makanisa ya Kiyunani kumaanisha waamini.
   4. Wakati mwingine baada ya kuanguka kwa Yerusalemu, Wafarisayo walikusanyika huko Yamnia na walichochea utengano rasmi kati ya sinagogi na kanisa. Mfano wa aina ya maapizo ya mazungumzo dhidi ya Wakristo unapatikana katika "*the Eighteen Benedictions" from Berakoth 28b-29a*, ambayo "Wanazarethi."
      "Wanazarethi na waasi waliweza kutoweka kwa muda mfupi; walifutwa kutoka katika kitabu cha uzima na kutoandikwa kuwa walikuwa na imani."
   5. Ilitumiwa na Justin Martyr, Dial. 126:1, ambaye alitumia netzer ya (Isa. 11:1) kumhusu Yesu.

C. Maoni ya Mwandishi
   Nashangazwa sana na herufi za maneno, Ingawa nafahamu kwamba hili ni jambo geni kusikika katika Agano la Kale "Yoshua" ina herufi mbalimbali katika Kiebrania. Maelezo yafuatayo yananisababisha kubaki na mashaka kama maana yake dhahiri :

   1. kama vile maana yake ya karibu na neno la Kimasihi "tawi" (netzer) au neno lililo sawa nāzir (aliyepakwa mafuta kwa maana ya nadhiri)

2. vidokezo hasi vya eneo la Galilaya kuyahusu mataifa
3. uchache au kutokuwepo kwa uthibitisho wa fasili za sasa kuhusu mji wa Nazarethi katika Galilaya
4. inatoka katika kinywa cha pepo katika maana ya hukumu (yaani, "Umekuja kutuangamiza?").

Kwa wasifu kamili wa masomo ya kundi la neno hili, tazama Colin Brown (ed.), *New International Dictionary of New Testament Theology,* juzuu. 2, uk. 346 au Raymond E. Brown, Birth of the Messiah, kur. 209-213, 223-225.

◙**"Yeye hana umbo wala uzuri;**
**Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani "** Yesu hakuwa na umbo la kawaida au la kuvutia. Hakujitokeza mbele za umati wa watu kwa namna yoyote (yaani., angeweza kutowekakatikati ya umati wa watu pasipo wao kujua, kama vile. Yn. 8:59;12:36).

**53:3 "Alidharauliwa "** KITENZI hiki (BDB 102, KB 117, *Niphal* KAULI ENDELEVU) kimetumika kama jina , "aliyedharauliwa" katika 49:7. The *Qal* KAULI TENDWA ENDELEVU imetumika katika Zab. 22;6, ambayo wakristo wanaamini kuwa inaelezea kusurubiwa kwa Yesu (kama vile. Mt. 27:35,39,43,46; Marko 15:29,34; Luka 23:34; Yn 19:24; 20:25).

Hivyo maandiko mengi katika sehemu hii ya Isaya yametumika kwenye Agano jipya. Isaya anafunua kwa uwazi mpango wa ukombozi wa Mungu kwa ajiri ya wanadamu wote (tazama mada maalum katika 40:15).

◙ mistari miwili ya mwisho ya mst. 3 imetafsiriwa kwa njia kadhaa.

1. Baadhi ya walimu wa sheria ya Kiyahudi wanasema Yesu alikuwa na makosa (kama vile. mst. 11)
2. Wengine wanahusianisha na 52:14 na kuliona hili linarejerea na kupigwa kwa Yesu alikopokea toka katika mikono ya walinzi wa Herode na Pilato
3. Wengine wanasimulia maneno ya Yesu katika Mt. 26:31; Marko 14:27 ( kutoka Zak. 13:7) au Yn. 16:32

◙**"huzuni"** neno hili (BDB 456) linaweza kumaanisha

1. Maumivu ya kimwili – Kut. 3:7
2. Maumivu ya hisia kubwa – Zab. 38:17-18; Yer. 45:3

Limetumika katika muktadha huu (mist. 13 na 14) juu ya maumivu ya mtumishi kwa niaba ya Israeli (kama vile. mst. 8) na wanadamu wote (kama vile. mst. 6).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 53:4-6**
**4Hakika ameyachukua masikitiko yetu,**
**Amejitwika huzuni zetu;**
**Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa,**
**Amepigwa na Mungu, na kuteswa.**
**5Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu,**
**Alichubuliwa kwa maovu yetu;**
**Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake,**
**Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.**
**6Sisi sote kama kondoo tumepotea;**
**Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe;**
**Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote.**

**53:4 "masikitiko"** Neno hili dhahili linamaanisha "magonjwa" (BDB 318, kama vile. Kumb. 28:59,61), lakini limetumika kwa maana iliyo pana zaidi katika Kiebrania (Zab. 107:3; Isa. 1:6; 6:10). Hii inaongelea kazi mbadala ya Yesu (kama vile. Marko10:45; 2 Kor. 5: 21).

Wengi wanajaribu kuutafsiri ubeti huu na mst. 5d kama mafundisho ya kwamba kifo cha Yesu kilishughulika na dhambi na magonjwa ya waaminio, lakini hii ni kupotosha dhana ya ufanano (kama vile. Zab. 103:3).

“magonjwa” ni Nahau ya Kiebrania kwa ajiri ya dhambi (kama vile . Isa. 1:5-6). Mwandishi mwenye kipaji nimpendaye , Gordon Fee, ameandika chapisho lenye nguvu juu ya habari hii yenye kichwa cha habari: *The Disease of the Health and Wealth Gospels*.

## MADA MAALUM: UPONYAJI NI MPANGO WA MUNGU WA KILA KIZAZI?

Inanishangaza kuona kuwa si wote walioponywa katika Agano Jipya “waliokolewa”(yaani., walimwamini Kristo na kuwa na uzima wa milele). Uponyaji wa mwili ni mbadala duni kwa ajili ya wokovu wa kiroho. Miujiza inaonekana kuwa ya msaada zaidi pale tu inapoturejeza mbele za Mungu. Wanadamu wote tunaishi katika ulimwengu ulioanguka. Mambo mabaya hutokea. Mara nyingi Mungu huchagua kutoingilia kati, lakini hili halisemi kitu chochote juu ya pendo na uhusika wake. Uwe mwangalifu pale unapotaka Mungu aingilie kati kutenda kimiujiza kwa kila hitaji unalolitaka katika kizazi hiki cha uovu. Yeye ni Mungu Mkuu na hatujui maana yake kamili kwenye hali fulani inayotolewa.

Kwa maana hiyo ningalipenda kuongeza kumbukumbu za fasiri yangu toka kwa 2 Tim. 4:20 kuhusu Paulo na uponyaji wa kimwili (angalia [www.freebiblecommentary.org](http://www.freebiblecommentary.org) ):

> "kuna maswali mengi ambayo tungepaswa kuwauliza waandishi wa Agano Jipya. Somo moja ambalo waaminio wote wanalifikiria ni kuhusu uponyaji wa kimwili. Katika kitabu cha Matendo (kama vile 19:12; 28:7-9) Paulo anaweza kuponya, lakini hapa na katika 2 Kor. 12:7-10 na Fil. 2:25-30, anaonekana kutoweza. Kwa nini baadhi waponywe na sio wote, na kuna muda ambapo dirisha linalohusiana na mambo ya uponyaji huwa linafungwa?

Hakika ninaamini kwenye nguvu ya ajabu, Baba mwenye rehema ambaye Yeye huponya kimwili vile vile kiroho, lakini ni kwa nini hii dhana ya uponyaji inaonekana kuwepo na baadaye tena haionekani? Sifikirii kuwa inahusiana na imani ya mwanadamu, kwa hakika Paulo alikuwa na imani (kama vile 2 Wakorintho 12). Nahisi kuwa uponyaji na kuiamini miujiza huthibitisha ukweli na mamlaka ya injili, ambayo bado inatenda katika maeneo ya ulimwengu ambayo mwanzoni ilitangazwa. Hata hivyo, nahisi kuwa Mungu anatuhitaji tutembee katika imani na sio kwa mtazamo. Pia, uponyaji wa kimwili mara nyingi huruhusiwa katika maisha ya watu:

1. kama adhabu ya muda mfupi kwa ajili ya dhambi
2. kama matokeo ya maisha kwenye ulimwengu ulioanguka
3. kuwasaidia waaminio kukuwa kiroho

Tatizo langu ni kuwa sikuwahi kujua ni yupi anahusika! Ombi langu kwa ajili ya mapenzi ya Mungu yaweze tendeka katika kila jambo sio kuwa na uhaba wa imani bali ni jaribio la uaminifu ili kuruhusu Mungu mwenye rehema na mwingi wa fadhila kutenda mapenzi yake katika kila maisha."

Hapa kuna hitimisho langu:

1. uponyaji ulikuwa ni dhana ya huduma ya Yesu na Mitume.
2. ulikusudia kimsingi kuthibitisha moja kwa moja ujumbe mpya kuhusu Mungu na ufalme Wake.
3. kuonyesha moyo wa Mungu kwa ajili ya watu wanaoumia.
4. Mungu hajawahi kubadilika (Mal. 3:6) na atatenda kwa upendo, katika uponyaji (karama zote za kiroho bado zinaendelea, kama vile 1 Kor. 12:9,28,30).
5. Kuna mifano mingi ambapo uponyaji kwa wale wenye imani kubwa haukutenda kazi ( kijitabu kilichonisaidia mimi katika eneo hili ni kile cha Gordon Fee, *The Disease of the Health, Wealth Gospel*).
   a. Paulo, 2 Kor. 12:7-10
   b. Trofimo, 2 Tim. 4:20
6. dhambi na magonjwa yalihusianishwa kwenye fikra za walimu wa dini ya Kiyahudi (kama vile Yohana. 9:2; Yakobo 5:13-18).
7. Uponyaji sio ahadi ya Agano Jipya. Sio sehemu ya upatanisho wa Mungu ulioelezewa katika Isa. 53:4-5 na Zab. 103:3, ambapo uponyaji ni taswira kwa ajili ya msamaha (angalia Isa. 1:5-6, ambapo magonjwa ni stiari kwa ajili ya dhambi).
8. kuna fumbo la kweli kuhusu ni kwa nini baadhi wanapona na baadhi hawaponi.
9. yawezekana kuwa ingawa uponyaji upo katika kila kizazi, kulikuwepo na ongezeko lenye umuhimu kipindi cha maisha ya Yesu; hili ongezeko litatokea tena kabla ya kurudi kwake.

Mwandishi wa kisasa ambaye amenisaidia mimi kutambua kuwa tamaduni zangu za kimadhehebu zimeshusha

utendaji wa Roho, hasa ile ya kimiujiza, iliyoandikwa na Gordon Fee. Ana vitabu mbalimbali, lakini viwili nivipendavyo ni vile vinavyoshughulika na eneo hili ni

1. *Paul, the Spirit, and the People of God*
2. *God's Empowering Presence: The Holy Spirit and the Letters of Paul*

Kama yalivyo masuala mengi ya Kibiblia, kuna mawili makubwa. Lazima tutembee katika nuru tulio nayo katika upendo, lakini siku zote tukijifungua katika nuru zaidi toka kwenye Biblia na Roho wa Mungu.

◙**"ameyachukua . . .amejitwika"** VITENZI hivi viwili ni vyenye kufanana.

1. ameyachukua – BDB 669, KB 724, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kimetumika kwa aliyetiwa hatiani kwa ajili ya mtu mwingine, Mwa. 4: 13, Law. 5:1,17; 7:18; Hes. 5:31; 14:34; Ezek. 14:10; 44:12, lakini pia vimetumika kwa mtu au kwa baadhi ya wanyama kuchukua hatia ya mwingine, kama vile. Law. 10:17; 16:22; Hes. 14:33; Ezek. 4:4,5,6 na huduma ya ukombozi wa mateso ya mtumishi Isa. 53:4
2. amejitwika – BDB 687, KB 741, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU; kwa maaana iliyo wazi ni "kujitwika mzigo mzito," imetumika kwa ajili ya mtumishi katika mst. 4 na mst. 11 (*Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU)

Tambua mfuatano wa VITENZI katika mist. 4-6 kwa YHWH alichofanya kwa mtumishi kwa ajiri ya manufaa ya mwanadamu.

1. Amepigwa na Mungu, mst. 4 – BDB 645, KB 697, *Hophal* KAULI ENDELEVU
2. Kuteswa ( na Mungu),mst. 4 – BDB 776, KB 853, *Pual* KAULI ENDELEVU
3. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, mst. 5 – BDB 319, KB 320, *Poal* KAULI ENDELEVU
4. Alichubuliwa kwa maovu yetu, mst. 5 – BDB 193, KB 221, *Pual* KAULI ENDELEVU
5. Adhabu ya amani yetu ilikuwa (hakuna KITENZI) juu yake, mst. 5
6. Kwa kupigwa kwake sisi tumepona, mst. 5

Msingi wa andiko hili ni kwa ajiri ya mafundisho ya kuwakilishwa, upatanisho mbadala.

◙**"amepigwa na Mungu"** ni mapenzi ya Mungu kwamba Yesu afe (kama vile. mst. 10; Yn. 3:16; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21). Majaribu ya Yesu na kifo havikuwa ni bahati mbaya au makosa , lakini ni mpango wa Mungu (kama vile. Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; I Pet. 1:20).

**53:5 "alijeruhiwa . . .alichubuliwa"** kama "ameyachukua" na "amejitwika" kwenye mst. 4 yako sambamba, hivyo pia , VITENZI hivi.

1. alijeruhiwa – BDB 319, KB 320, *Poal* KAULI ENDELEVU hasa kwa upanga kwenye vita,lakini sio hapa. Asili ile ile inamaanisha "chafua" kwa ajiri ya utakaso na msamaha wa mwanadamu.
2. alichubuliwa – BDB 193, KB 221, *Pual* KAULI ENDELEVU; KITENZI hiki kimetumika mara kadhaa katika Isaya
   a. 57:15 – *Niphal* KAULI ENDELEVU, "moyo wenye toba"
   b. 3:15 – *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, "kugandamiza watu wangu"
   c. 19:10; 53:5 – *Pual* KAULI ENDELEVU, "kugandamizwa"
   d. 53:10 – *Piel* TUNGO YA KITENZI JINA HALISI, "kugandamiza"

Inamwonyesha mtu aliye mnyenyekevu. Kwa muktadha huu ni YHWH peke yake kwa ajiri mema mazuri kwa wanadamu wote.

**53:6** Hiki ni kifanani cha Agano la kale kwa Rumi. 3:9-18,23; 5:12,15,18; 11:32; Gal. 3:22. Hii inaonyesha ukuaji wa kutisha wa anguko la Mwanzo 3 (kama vile . Mwa. 6:5,11-12; Zab. 14:3; 143:2).

◙**"Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake "** Yesu alikufa kwa ajiri ya ulimwengu mzima. Kila mmoja anaweza kuokolewa na Kristo (kama vile. Yn. 1:29; 3:16-17; Rum. 5:18; Tito 2:11; I Yn. 2:2; 4:14). Hili litatimizwa kwa wasio amini kuwa mbali na Mungu. Baadhi ya wafasiri wanajaribu kuonyesha utofauti kati ya neno "sote" [mara mbili] kwenye mst. 6 na "wengi" kwenye mist. 11d na 12e. Hata hivyo, mfanano wa Rum. 5:18, "sote" na "wengi" wa

5:19, ni wazi unaonyesha kwamba unarejelea kundi moja (yaani., kuanguka kwa mwanadamu aliyeumbwa kwa sura na mfano wa YHWH, Mwa. 1:26-27). Mungu anatamani wanadamu wote waokolewe – Yn. 4:42; I Tim. 2:4; 4:10; 2 Pet. 3:9).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 53:7-9**
**7 Alionewa, lakini alinyenyekea,**
**Wala hakufunua kinywa chake;**
**Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni,**
**Na kama vile kondoo anyamazavyo Mbele yao wakatao manyoya yake;**
**Naam, hakufunua kinywa chake.**
**8 Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa;**
**Na maisha yake ni nani atakayeisimulia?**
**Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai;**
**Alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu.**
**9 Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya;**
**Na pamoja na matajiri katika kufa kwake;**
**Ingawa hakutenda jeuri,**
**Wala hapakuwa na hila kinywani mwake**.

**53:7 “kama mwana-kondoo”** Dokezo la dhabihu ni la muhimu sana (kama vile. Yn. 1:29 na 2 Kor. 5:21).

◙**“wala hakufunua kinywa chake”** Hii inamaanisha kwamba mtumishi hakujaribu kujitetea. Kuna vidokezo vingi kwenye majaribu haya ya Yesu.

1. Jaribu la Yesu usiku ule mbele za Kayafa – Mt. 26:63; Marko 14:61
2. Jaribu la Yesu mbele za Pilato – Mt. 27:12-14; Marko 15:5; Yn. 19:9
3. Yesu mbele ya Herode – Luka 23:9

**53:8 “kwa sababu ya makosa ya watu wangu”** tungo hii inaonyesha kwamba neno “mtumishi”kwenye muktadha huu haliwezi kuwa taifa la Israeli. Mtumishi alikufa (kama vile. 8c) kwa ajili ya Israeli.

Huu wimbo/shairi una MATAMSHI adimu na yasiyo ya kawaida.

1. 52:15, “mambo wasiyoambiwa” – *Pual* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (BDB 707, KB 765)
2. 52:15, “watayafahamu” – *Hithpolel* KAULI YA WAKATI TIMILIFU (BDB 106, KB 122)
3. 53:4, “amepigwa” – *Hophal* KAULI ENDELEVU (BDB 645, KB 697)
4. 53:4, “kuteswa” – *Pual* KAULI ENDELEVU (BDB 776, KB 853)
5. 53:5, “alijeruhiwa” – *Poal* KAULI ENDELEVU (BDB 319, KB 320)
6. 53:5, “alichubuliwa” – *Pual* KAULI ENDELEVU (BDB 193, KB 221)
7. 53:7, “apelekwaye” – *Hophal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 384, KB 383)
8. 53:8, “atayeisimulia” – *Polel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 967, KB 1319)

**53:9** Mistari hii inaelezea kwa dhahili kusulubiwa na kuzikwa kwa Yesu (kama vile. Mat. 27:38,59), kama ilivyofanyika kwenye Zab. 22.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 53:10-12**
**10 Lakini Bwana aliridhika**
**kumchubua; Amemhuzunisha;**
**Utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi,**
**Ataona uzao wake,**
**ataishi siku nyingi,**
**Na mapenzi ya Bwana yatafanikiwa mkononi mwake;**

**[11] Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake,**
**na kuridhika.**
**Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki**
**Atawafanya wengi kuwa wenye haki;**
**Naye atayachukua maovu yao.**
**[12]Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu,**
**Naye atagawanya nyara pamoja nao walio hodari;**
**Kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa,**
**Akahesabiwa pamoja na hao wakosao.**
**Walakini alichukua dhambi za watu wengi,**
**Na kuwaombea wakosaji**.

**53:10 "Lakini Bwana aliridhika kumchubua; Amemhuzunisha**"

Tambua mpatanishi na kusudi la hivi VITENZI.

1. YHWH aliridhika (Kifasihi. "ni mapenzi ya" – BDB 342, KB 339, *Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU).KITENZI hiki kinamaanisha "kufurahia" (kama vile. 58:2; 62:4) au "kutamani" (55:11). Hata Kimetumika pia kwa YHWH kupendezwa kumweka mtu fulani katika kifo katika Amu. 13:25; I Sam. 2:25. Inashangaza kutumia KITENZI kama hiki kinahusiana na utendeaji usio sawa, wa mateso kwa mtumishi mwenye haki. YHWH alikuwa na mpango wa ukombozi (tazama mada maalum:katika 40:15)!
2. Mapenzi ya YHWH na makusudi ni "kumuumiza" (*Piel* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, kama vile. mst. 5) na "kumhuzunisha" (*Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 317, KB 311). KITENZI hiki kinamaanisha "kumfanya mgonjwa" (toleo la JPSOA) au "kumuumiza kwa kumpiga." Palikuwepo na gharama kubwa na ya kugharimia kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu! YHWH na mtumishi wake wamelipa yote na bure!

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihgu kwa dhambi"** |
| **NKJV, NRSV** | **"utakapofanya roho yake kuwa dhabihu kwa dhambi"** |
| **TEV** | **"kifo chake ni sadaka ya kuleta msamaha"** |
| **NJB** | **"kama akitoa maisha yake kama dhabihu ya dhambi"** |
| **JPSOA** | **"kama alijitoa yeye kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi"** |
| **Peshitta** | **"aliweka maisha yake kama dhabihu kwa ajili ya dhambi"** |

Tungo hii bado ni ya maana sana na ya kina. inahusisha

1. Mapenzi ya YHWH
2. Mapenzi ya mtumishi
3. Yeye aliye mdhambi alichagua kupokea dhabihu hii ya dhambi (imedokezwa)

Hii ni dhana ya kitheolojia ya Kiebrania "kuhusu mwili." Imeelezwa kwa mifano na

1. Utaratibu wa kidhabihu (Law 1-7), lakini hasa Siku ya upatanisho (kama vile. Law 16)
2. Dhambi ya Akani iliathiri jeshi la Israeli (Joshua 7)
3. Maelezo sahihi kwenye Rumi 5:12-21
4. Mfano mwingine mkubwa katika 2 Kor. 5:21

mwenye haki mmoja analipa gharama moja ya kuwaweka huru wote wenye dhambi!

◙**" ataishi siku nyingi "** Ni dhahili kwamba mtumishi alikufa (kama vile. mist. 8,9,12). Hivyo basi, mstari huu lazima urejelee maisha baada ya kufa!

Tambua mambo yote ambayo YHWH atafanya kwa ajiri yake.

1. Ataona uzao wake (Kifasihi. "uzao"), mstr. 10
2. Atazidisha siku zake (hii lazima inarejelea baada ya kufa kwake), mst. 10
3. Mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake (yaani., mipango ya YHWH ya kurejesha ushirika na mwanadamu), mst. 10

4. Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake na kuridhika, mst. 11 (inarejelea mafanikio ya YHWH [mapenzi]), mst. 10b
5. Atawafanya wengi kuwa wenye haki, mstr. 11
6. Atamgawia sehemu pamoja na wakuu, mstr. 12
7. Atagawa nyara pamoja nao walio hodari, mst. 12

Mara zote Shairi huwa ni vigumu kulitafsiri. Baadhi ya hivi vipengele havijulikani!

**53:11 "nafsi"** Toleo la LXX na Gombo la Bahari ya Chumvi lina neno "nuru" (NRSV, NJB).Toleo la MT halina neno "nafsi" (tazama toleo NKJV). Toleo la UBS linafikilia neno "nuru" lingaliweza kuondolewa kwenye andiko.

◙**"kwa maarifa yake"** Toleoe la NRSV lina kifungu "atapata amani kupitia maarifa yake." Swali juu ya "maarifa yapi" linaonekana kuhusiana na

1. Kuona uzao wake (mst. 10c)
2. Kuzidisha siku zake (mst. 10d)
3. Mafanikio ya mapenzi ya YHWH (mst. 10e)
4. Ataona mazao yake (mst. 11a)

◙**"mwenye haki. . .haki"** haya maneno yote yanatoka kwenye muundo wa asili moja (BDB 842, 843). YHWH ni mchukua maovu (kama vile mist. 11e) mtumishi atakamilisha haki kwa wale wote watakao amini na kupokea (kama vile. Yoh. 1:12; 3;16; Rum. 10:9-13).

◙**"wote"** tazama muhtasari katikaneno "sote" kwenye mst. 6.

◙**"naye atayachukua maovu yao"** KITENZI sawa (BDB 687, KB 741, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kimetumika pia kwenye mst. 4. Tazama muhtasari wake.

**53:12a,b "Naye atagawanya nyara pamoja nao walio hodari "** hii ni sitiari ya ushindi. Haipaswi kuchukuliwa kikawaida, lakini kitamathari ni ushindi wa kiroho (kama vile. 52:13)!

◙**" alimwaga nafsi yake hata kufa"** KITENZI hiki(BDB 788, KB 881, *Hiphil* KAULI YA WAKATI TIMILIFU) Ni dhahili kinamaanisha "kuwa uchi" au "kuwa wazi" au "kuwa tupu." Kimetumika katika Isaya kwa maana mbalimbali.

1. Kuifunua silaha, Isa. 22:6
2. Kwa ajiri ya Roho tuliyepewa (yaani.,kumimina ), Isa. 32:15
3. Toleo la BDB inaita ni sitiari katika andiko hili linaloakisi matumizi ya neno *Piel* katika #3 (kama vile. Zab. 141:8)
4. Toleo la KB linaita "kumwaga," sitiari ya "kuyatupilia mbali maisha ya mtu hata kifo"

◙**"Akahesabiwa pamoja na hao wakosao "** Luka 22:37 inadokeza mstari huu kama ulivyozungumzwa na Yesu katika bustani ya Gethsemane walipokuja askari na walinzi kumkamata . Tambua neno sawa (BDB 833) limetumika kwenye uovu wa Israeli katika mst. 8 na uovu wa mwanadamu mst. 5.

◙**"alichukua dhambi za watu wengi"** Hii inamaanisha upatanisho mbadala, wa kushangaza (kama vile. Mt. 20:28; Marko 10:45; 14:24; 2 Kor. 5:21; Gal. 1:4; I Tim. 2:6; Tito 2:14). Toleo la UBS linafikilia neno "uovu" laweza kuwa WINGI(alama B kwa tathimini).

◙**"Na kuwaombea wakosaji**." Na bado anaendelea kuomba (kama vile. Rum. 8:27,34; Ebr. 7:25; 9:24; I Yn. 2:1)!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwatafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Je jina la "mtumishi wangu" linarejelea Wayahudi au Masihi?
2. Kwanini matoleo mengi juu ya mataifa yana maana sana kwenye kifungu hiki?
3. Kwanini Mungu aliwachagua Wayahudi?
4. Kwanini mtumishi aliteswa?
5. Kwanini Mungu alipendezwa kwa kumchubua?
6. Ni nini katika Isa. 53:6 inasema juu ya uovu?
7. Kwa nini kifungu hiki kina ushawishi katika kanisa?

# ISAYA 54

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ustawi wa Sayuni | Mwendelezo wa agano la amani | Wimbo wa amani kwa Israeli | Upendo wa Mungu kwa Israeli | Yerusalemu inarejeshwa kwa upendeleo wa YHWH |
| 54:1-3 (1-3) | 54:1-3 (1-3) | 54:1-3 (1-3) | 54:1-3 (1-3) | 54:1-10 (1-10) |
| 54:4-8 (4-8) | 54:4-8 (4-8) | 54:4-8 (4-8) | 54:4-5 (4-5) | |
| | | | 54:6-10 (6-10) | |
| 54:9-10 (9-10) | 54:9-10 (9-10) | 54:9-10 (9-10) | Yerusalemu ijayo | Yerusalemu mpya |
| 54:11-17 (11-17) | 54:11-15 (11-15) | 54:11-17 (11-17) | 54:11-12 (11-12) | 54:11-17 (11-17) |
| | | | 54:13-15 (13-15) | |
| | 54:16-17 (16-17) | | 54:16-17 (16-17) | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. Xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozokwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Ayaya kwanza
10. Ayayapili
11. Ayatatu
12. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kuna madokezo mbalimbali kwenye kipindi cha wazee wa imani (mwanzo 12-50) katika aya hii.
   1. Akina mama wasio na watoto
   2. kuishi kwenye mahema

3. utumiaji wa neno "kizazi" kwa ajili ya uzao

B. Pia kuna dokezo kwenye gharika ya Nuhu (mwanzo 6-9) katika mst. 9.

C. YHWH anafanya upya ukombozi wa ahadi la agano.
1. Toka Misri
2. toka Mesopotamia
3. Toka maadui wa siku za mwisho

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 54:1-3**
**[1] Imba, wewe uliye tasa, wewe usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele, wewe usiyekuwa na utungu; maana watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wake yeye aliyeolewa, asema Bwana. [2]Panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako; usiwakataze; ongeza urefu wa kamba zako; vikaze vigingi vya hema yako. [3]Kwa maana utaenea upande wa kuume na upande wa kushoto; na wazao wako watawamiliki mataifa; wataifanya miji iliyokuwa ukiwa kukaliwa na watu.**

**54:1-3** Ubeti wa kwanza una KAULI SHURUTISHI mbalimbali ambazo zinahusiana na kuijenga Yuda/Yerusalemu iliyorejeshwa (kama vile49:20).

1. Imba kwa furaha – *Qal* KAULI SHURUTISHI, BDB 943, KB 1247
2. Pazeni sauti zenu – *Qal* KAULI SHURUTISHI, BDB 822, KB 953
3. pigeni kelele – *Qal* KAULI SHURUTISHI, BDB 843, KB 1007
4. panua mahali pa hema yako – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, BDB 931, KB 1210
5. na wayatandaze mapazia – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, BDB 639, KB 692, ikitumika kwa maana AMRISHI
6. usiwakateze – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 362, KB 359, ikitumika kwa maana AMRISHI
7. ongezeni urefu wa kamba yako – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, BDB 72, KB 88
8. Vikaze vigingi vya hema yako – *Piel* KAULI SHURUTISHI, BDB 304, KB 302

Paulo anatumia rejea hii kwenye uainishi wake kuhusu wana wa Ibrahimu na maagano mawili katika Gal. 4:21-31. Mara nyingi ilinishangaza namna waamini ya leo wanavyoichukulia aya kama hii moja kwa moja nje ya muktadha na kuitumia kwa ajili ya hotuba juu ya ujenzi wa jengo jipya la kanisa! Ukikubali kutochukua uzingativu juu ya muundo wa kwanza na kusudi la mwandishi wa awali, unaweza kuunga mkono kitendo chochote. Inaonekana kuwa Wakristo wa kiinjili wa leo kisaikolojia wanahitaji andiko la Biblia ili kuyawezesha matukio na mipango yao yote! Angalia hotuba ya utafasiri wa Kibiblia kwenye mtandao *www.freebiblecommentary.org*

**54:3 "wazo wako watamiliki mataifa"** Kwa mtazamo wa haraka kifungu hiki kinaonekana kama kile cha maandiko ya Isaya kwa watu wote, lakini kumbuka dhana ya ufanano kwenye mstari unaofuata. Huu ni urejereaji wa kuvutia juu ya maeneo ya kikabila ya Yuda na Benjamini. Inarejerea kwa tamko la Koreshi II kuhusu uzao wa Ibrahimu kurejea Palestina baada ya kukimbilia Ashuru na Babeli **(**kama vile 14:1-2)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 54:4-8**
**[4] Usiogope; maana hutatahayarika; wala usifadhaike;**
**maana hutaaibishwa;**
**kwa kuwa utaisahau aibu ya ujana wako,**
**pia mashutumu ya ujane wako hutayakumbuka tena.**
**[5]Kwa sababu Muumba wako ni mume wako;**
**Bwana wa majeshi ndilo jina lake;**
**na Mtakatifu wa Israeli ndiye Mkombozi wako;**
**Yeye ataitwa Mungu wa dunia yote.**
**[6]Maana Bwana amekuita kama mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni,**
**kama mke wakati wa ujana,**

**atupwapo, asema Mungu wako.**
**[7]Kwa kitambo kidogo nimekuacha;**
**lakini kwa rehema nyingi nitakukusanya.**
**[8]Kwa ghadhabu ifurikayo nalikuficha uso wangu dakika moja;**
**lakini kwa fadhili za milele nitakurehemu,**
**asema Bwana, Mkombozi wako.**

**54:4 "usiogope" Hii ni** *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 431, KB 432) ikitumika kwa maana ya AMRISHI. Hili ni somo lenye kujirudia katika Isaya (kama vile 7:4; 8:12; 35:4; 41:10,13,14; 43:15; 44:2; 51:7; 54:4,14; 57:11). Uzao wa Ibrahimu wapaswa kukumbuka kuwa wao ni wapokeaji wa

1. Uwepo wa YHWH
2. Ahadi za YHWH
3. Kusudi la YHWH

◙**"maana hutatahayarika;**
**wala usifadhaike; maana hutaaibishwa"**
Tambua ahadi tatu kwa uzao wa Abrahamu uliorejea.

1. hutatahayari – kanushwa *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 101, KB 116 (kinyume cha 1:29; 20:5)
2. usifadhaike – kanushwa *Niphal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 482, KB 480, kama vile 45:17; 50:7
3. hutaabishwa – kanushwa *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 344, KB 340

◙**"utaisahau. . .hutayakumbuka tena"** Tambua ufanano uliopo. Haya marudio yanatiwa hamasa na utumiaji wa maneno mawili yaliyozoeleka**.**

1. Ujana wako
2. Ujane wako

Israeli ilikuwa yenye dhambi katika siku zake za mwanzo (na ikaendelea), kwa hiyo, ilifukuzwa na YHWH (yaani., ujane wako), lakini sasa wote watasahauliwa na kwa tumaini kubwa siku mpya ya imani na uaminifu inaanza!

**54:5 Tena**, kama ulivyo mst. 4, stiari za kifamilia zimetumika. Tambua majina tofauti kwa ajili ya mume wa Israeli (mistari ya.6-8; Hosea 1-3).

1. Muumba wako, – YHWH kama mume na muumbaji, kama vile 43:1,7; 44:2,21,24; Kumb. 32:18
2. Bwana wa majeshi – Angalia Mada Maalum hapo chini
3. Mwokozi wako – majina yanayojirudia katika Isaya (kama vile 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:41; 48:17; 49:7,26;54:5,8; 59:20; 63:16)
4. Yeye aliye Mtakatifu wa Israeli – jina linalojirudia katika Isaya (kama 1:4; 5:19,24; 10:20; 12:6; 17:7; 29:19,23;30:11,12,15; 31:1; 37:23; 41:14,16,20; 43:3,14,15; 45:11; 48:17; 49:7; 54:5; 55:5; 60:9,14 (katika vipengere vyote vya Isaya, 1-39 na 40-66)
5. Mungu wa dunia yote – huu ujumuishaji ni tabia ya Isaya, yaani., 6:3; 11:9; 45:6;52:10

Majina haya ni ya namna ya Kiebrania ya kusisitiza tabia ya Mungu wa Israeli! Kwa ajili ya maandiko mengine juu ya tabia ya Mungu angalia Kut. 34:6; Hes. 14:;18; Neh. 9:17; Zab. 86:15; 103:8; 145:8-9. Angalia Mada Maalum katika 49:7.

## MADA MAALUM: BWANA WA MAJESHI

Hili jina la ki-Uungu, "Bwana wa Majeshi" (kama vile 1 Sam. 1:3,11 kama matumizi ya kwanza ya kuwepo kwa mamia kadhaa) linaundwa na

A. Jina la Mungu la agano, YHWH. Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu
B. Neno la kijeshi "majeshi" (BDB 838, KB 994) linaweza kudokeza
   1. malaika kwa ujumla (kama vile Neh. 9:6)
   2. jeshi la malaika wa mbinguni (kama vile 1 Sam. 17:45; Dan. 8:10; Luka 2:13)

3. kusanyiko la kimalaika (kama vile 1 Fal. 22:19; Dan. 7:10)
4. watu wa YHWH (kama vile Kut. 12:41, ambayo inaakisi Kut. 3:8,10 kama inavyorejelea juu ya Israeli, kama vile 2 Sam. 7:27)
5. jeshi la mwanadamu (yaani, Mwa. 21:22,32; Hes. 2:4,6; Amu. 8:6; 9:29)
6. nuru ya mbinguni wakati wa usiku (yaani, "majeshi," Mwa. 2:1; Isa. 45:12), inafikiriwa kuwa nguvu za kiroho (yaani, Babeli kuabudu jua mwezi na vitu vyote katika jeshi la mbinguni, kama vile Kumb. 4:19; 17:3; 2 Fal. 17:16; 21:3,5; 23:4-5; 2 Nya. 33:3,5; Yer. 8:2; 19:13)
7. Hili linakuwa jina la YHWH katika Amosi 4:13; 5:27 (likiwa na KIBAINISHI katika Amosi 3:13; 6:14; 9:5 na pasipo KIBAINISHI katika Amosi 5:14,15,16; 6:8; 1 Fal. 19:10,14). Hili lilidokeza mapigano ya YHWH kwa niaba ya Israeli.

Kuna matumizi mahususi katika Yos. 5:14-15 ambayo yanaweza kurejelea kwa Mikaeli, malaika wa kiulinzi kwa Israeli. Jina hili kwa namna fulani lina ufanano na Malaika wa Bwana kama uwakilishi wa Mungu Mwenyewe (huenda kabla ya Kristo kufanyika katika umbo la kibinadamu).

**54:6** Israeli inaelezewa kama mwanamke asiye na imani ambaye ametalikiwa (kama vile 49:14-21; 50:1,2; 62:4).

**54:7** YHWH alimtalikisha mkewe asiye na imani lakini sasa anamtafuta tena (kama vile Hosea 1-3). Hili katika ufahamu wa maandiko ya Musa kuhusu kutokuoa mwanamke yule yule.

◙**"kwa kitambo kidogo nimekuacha"** Angalia Isa. 26:20. Mungu hatashika hasira yake milele (kama vile Zab. 103:9-14).

◙**"nitawakusanya"** Hii ni (*Piel* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 867, KB 1062) namna ya kurejerea tatizo la ukimbizi, safari mpya ya kutoka Mesopotamia (kama vile 11:12; 43:5; 49:18; 56:8; 60:4).

**54:8** Katika Agano la Kale tabia ya YHWH kama mwenye upendo na huruma inakinzana na Yeye kama Mungu wa haki na asiye na upendeleo. Israeli ni chombo cha YHWH kwa namna zote za upendo na ghadhabu (kifasihi "kujawa na ghadhabu," BDB 1009, KB 1637, linapatikana hapa tu). Kithiolojia hapa ni pale kazi ya Masihi (52:12-3:13) inapohitajika. Upendo na haki vilikutana kalvari!

◙**"lakini kwa fadhiri za milele nitakurehemu"** Haya ni maneno yenye nguvu ya upendo na ahadi za Mungu.

1. "milele" – angalia Mada Maalum katika 45:17
2. "wema" – angalia Mada Maalum katika 40:6
3. "rehema" – *Piel* KAULI ILIYOTIMILIFU, BDB 933, KB 1216; hili linatumika kwa YHWH katika 14:1; 30:18;49:10,13,15; 54:7,8,10; 55:7; 60:10; Mika 7:19 (kwa namna iliyo kinyume katika 9:17; 27:11)

◙**"Bwana"** Hii kwa maana iliyo wazi ni "YHWH"; angalia Mada Maalum katika 40:3.

◙**"Mwokozi"** Angalia Mada Maalum katika 41:14

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 54:9-10**
**[9]Kwa maana jambo hili limekuwa kama maji ya Nuhu kwangu; maana kama nilivyoapa ya kwamba maji ya Nuhu hayatapita juu ya dunia tena, kadhalika nimeapa ya kwamba sitakuonea hasira, wala kukukemea. [10]Maana milima itaondoka, na vilima vitaondolewa; bali wema wangu hautaondoka kwako, wala agano langu la amani halitaondolewa; asema Bwana akurehemuye.**

**54:9-10 Aya hizi mbili lazima zitakuwa zikielezea** "agano jipya" la Yer. 31:31-34 (kama vile Ezek. 36:22-38)kwa sababu Waisraeli waliorudi waliendelea kutenda dhambi (kama vile Malaki).

**54:9 Aya hii moja kwa moja ni dokezo la gharika ya Mwanzo** 6-9 (hasa 8:21; 9:11).Kwa Kiebrania kifungu "maji ya kwenye gharika ya Nuhu" yanaweza kuwa "kama zile siku za Nuhu" (NASB) na DSS na matoleo mengine ya kale, lakini sio lile toleo la LXX ambalo lina kifungu "kutokana na maji ya kipindi cha Nuhu."

**54:10 "agano langu la amani" Yumkini hii ni njia nyingine ya kurejerea kwenye** "agano la milele" (kama vile 55:2; 59:21; 61:8; Mwa. 17:7; Zab. 105:10; Yer. 32:40; 50:5). Kipindi hiki kinaelezewa mara nyingi katika Ezekieli (kama vile 16:60; 20:37; 34:25; 37:26; kwa ajili ya kujifunza zaidi angalia fasiri yangu katika mtandao *www.freebiblecommentary.org*).

Tatizo ni kuwa YHWH alilivunja agano lake za uzao wa Ibrahimu kwa maangamizi na kukimbilia uhamishoni kwa Yerusalemu na kulikataa hekalu (Ezekieli 8-10). Sehemu ya tatizo letu ni kwa ajili ya neno la Kiingereza "daima" au "milele" angalia Mada Maalum katika 45:17). Sehemu nyingine ya tatizo letu katika kuyatafasiri maandiko kama haya ni kuhusu maagano mawili! Kuna kitu muhimu ambacho kimetokea kwa Kristo. Yeye ni utimilifu wa ahadi zote za Agano la Kale. Agano Jipya ni kumhusu Yeye na wote wanaoamini katika Yeye, sio kuhusu taifa la Israeli. Hili ni gumu kwetu kuweza kuamini kwa sababu upendo wetu na imani ya Biblia na asili ya nguvu ya haya maandiko. Hata hivyo, sio Yesu wala mwandishi yeyote wa Agano Jipya amewahi kuthibitisha tena ahadi kwa taifa la Israeli (angalia Mada Maalum katika 40:9).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 54: 11-17**
**11 Ewe uliyeteswa, uliyerushwa na tufani, usiyetulizwa, tazama, nitaweka mawe yako kwa rangi nzuri, nitaweka misingi yako kwa yakuti samawi. 12 Nami nitaifanya minara yako ya akiki nyekundu, na malango yako ya almasi, na mipaka yako yote ya mawe yapendezayo. 13 Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako itakuwa nyingi. 14 Utathibitika katika haki; utakuwa mbali na kuonewa, kwa maana hutaogopa; na mbali na hofu, kwa maana haitakukaribia. 15 Tazama, yamkini watakusanyana; lakini si kwa shauri langu. Watu wo wote watakaokusanyana juu yako wataanguka kwa ajili yako. 16 Tazama, nimemwumba mhunzi avukutaye moto wa makaa, akatoa silaha kwa kazi yake; nami nimemwumba mharibu ili aharibu. 17 Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa. Huu ndio urithi wa watumishi wa Bwana, na haki yao inayotoka kwangu mimi, asema Bwana.**

**54:11-13** Tambua idadi ya vito vya thamani vilivyotumika kama njia ya kuonyesha upendeleo wa Mungu (kama vile Ezek. 28:13).

1. Mawe yenye rangi nzuri (BDB 806, KB 918) – huenda ni mawe meusi, kama vile I Nya. 29:2, au udongo mweusi, kama vile Isa54:11
2. Yakuti samawi (BDB 705, KB 764) – yumkini kito cha nili na zari
3. Akiki nyekundu (BDB 461, KB 460)
4. Almasi (BDB 869, KB 82) – yumkini kito cha ahdhari
5. Mawe ya thamani, lakini hayakuelezewa ni yapi kati ya hayo

Moja ya hivi vito vya thamni (#2) kilitumika kama deraya ya kifua cha kuhani mkuu (kama vile Kut. 28:17-19; 39:10-11).Sura ya kuta zilizopambwa kwa vito vya thamani imechukuliwa na Yohana katika Ufu. 21:18-21.

**54:11 "Ewe uliyeteswa" Hili kiushairi linafanana na** "Ewe uliyetasa" ya mst. 1. Yote yanarejerea kwenye wale wote waliorudi toka uhamishoni.

**54:13 "Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana"** Hili linasikika vizuri kama lililoko Yer. 31:34 (yaani., "agano jipya"). Yesu anarejea aya hii katika Yohana 6:45 ikihusiana na Baba akiwavuta waumini/wanafunzi kuja kwake kupitia Yesu.Toleo la NEB linalitangua toleo la MT na kubadili kifungu "na wana wenu wote" kwenda "waashi wenu," lakini toleo la UBS lenyewe linatoa alama A kwenye kifungu "na wana wenu wote" (uwezekano mkubwa).

**54:14** Aya hii inataja mambo manne ambayo wale wote watakaorudi yatawatokea juu ya ulinzi na uangalizi wa Mungu**.**

1. Wataimalishwa katika haki – *Hithpolel* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 465, KB 464)
2. Ukandamizwaji utakuwa mbali nanyi – *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 934, KB 1221)

3. Hautaogopa – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 431, KB 432)
4. Hofu haitawaijilia karibu yenu – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU (BDB 897, KB 1132)

**54:15-17** Hakika hii ni aya juu ya ukuu wa YHWH. Mtu atashangaa ni namna gani huu ukweli unahusiana na mateso ya waamini siku ya mwisho.

**54:15** Hii aya ina maana yenye kufanana na ile ya Mwa. 12:3b. Wale warudio wanaweza kupitia matatizo lakini hayatokani na Mungu na wataadhibiwa (kama vile 41:11-16). Kuna *Qal* KITENZIJINA HALISI, *Qal*KAULI ISIO TIMILIFU, na *Qal* KAULI TIMILIFU za asili ile ile ya Kiebrania (BDB 158, KB 184). Muundo wa kisarufi unasisitiza uwezekano wa tatizo lao lakini Mungu anawahakikishia kutenda kwa niaba yao.

**54:16-17** Aya, kama ile ya Yohana 6:45, inasisitiza ukuu wa YHWH kulitimiza kusudi lake kupitia uzao wa Ibrahimu (yaani., Israeli na Masihi).

**54:17 "watumishi wa Bwana"** Toleo la NASB Study Bible lina kumbukumbu nzuru juu ya ya kifungu hiki (uk. 1033)."Baada ya sura ya 53 neno 'mtumishi' halitokei tena katika Isaya. Neno 'mtumishi' (angalia 63:17;65:8-9,13-15; 66:14) ni waamini wa kweli — kwa wote Wayahudi na watu wa mataifa (angalia 56:6-8) — ambao ni waaminifu kwa Bwana. Wako katika maana ya 'mtoto"wa mtumishi (53:10)."

◙**"na haki yao inayotoka kwangu Mimi"** Hakuna KITENZI katika toleo la MT. YHWH atawaokoa watu wake.

# ISAYA 55

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Rehema ya bure | Mwaliko wa Maisha Tele | Wimbo wa Furaha na ushindi | Ahadi ya Mungu ya ya rehema | Mwaliko wa Mwisho |
| 55:1-5 (1-5) | 55:1-5 (1-5) | 55:1-5 (1-5) | 55:1-2 (1-2) | 55:1-3a (1-3a) |
| 55:3-555:3b-5 (3-5) | (3b-5) | | | |
| 55:6-13 (6-13) | 55:6-7 (6-7) | 55:6-7 (6-9) | 55:6-9 (6-9) | 55:6-11 (6-11) |
| 55: 8-9 (8-9) | | | | |
| 55:10-11 | 55:10-11 (10:-11) | 55:10-11 (10-11) | Hitimisho (10-11) | |
| | 55:12-13 (12-13) | 55:12-13 (12-13) | 55:12-13 | 55:12-13 (12-13) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni<u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu.
Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

13. Aya ya kwanza
14. Aya ya pili
15. Aya ya tatu
16. N.k

## MASWALI YA UTANGULIZI

1. Je! Sura hii inamzungumzia nani? (Wayahudi waliokuwa uhamishoni au wanadamu wote)
2. Nini majitoleo kwao: (urejesho kwa Nchi ya Ahadi au wokovu wa kiroho [yaani, Ibn Ezra])
3. Hapa ndipo kanuni za ufasiriwa wa kibiblia zinapokinzana!
    a. Kila ukurasa lazima ufasiriwe katika mwangaza wa uhalisia, katika kusudi asilia la mwandishi. Njia bora ya kutoa maamuzi ya fasiri ni, "Nini ambacho wasikilizaji asilia (yaani, hadhira iliyokusudiwa) wangekielewa?" Kila andiko lina maana moja tu.

   b. Kitabu cha Agano Jipya ni utimilifu kamili na mfasiri wa kitabu cha Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-48). Yesu ni kusudi na sababu ya ahadi za Agano la Kale. Katika yeye na katika yeye pekee lazima kitabu cha Agano la Kale kifasiriwe. Agano Jipya linamuhusu Yesu na ukombozi wa ulimwengu, halilihusu taifa la Israeli.
4. Tambua kwamba safari ya kurudi toka uhamishoni haitajwi bayana (isipokuwa mst. wa 12a,b) au kudokezwa. Ombi ni la moja kwa moja, lina mapana zaidi

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kwa vyo vyote vile mazingira haya ni ya
   1. karamu ta ki-Masihi, Mt. 25:6-8; Luka 14:15-24; 22:16,18; Ufu. 19:9
   2. sehemu ya soko la Yerusalemu
B. Manabii wa Agano la Kale mara nyingi waliyatumia matukio ya kihistoria ya siku zao wenyewe kutabiri matukio ya siku za mwisho (tazama Kiambata cha pili).
C. Kama Mkristo waAmri Kuu (yaani, Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Matendo 1:8) ambaye anaamini katika upendeleo wa injili na uanafunzi, sura hii inashikilia nafasi pendwa ndani ya moyo na huduma yangu. YHWH, kupiti kwa nabii wake, anawasihi wanadamu walioanguka kurudi kwake ili aweze kuwapa msamaha kamili na ulio huru (kama vile mst. ya 1-5). Hili ndiyo shabaha ya Mwa. 3:15!

   Hata hivyo, mamlaka ya mwitikio wa agano (kama vile mist. ya 6-7). Wanadamu wanapaswa kutubu, kuamini, kutii, na kustahimili. YHWH anao mpango wa ukombozi wa milele (kama vile mist. ya 8-11). Tazama Mada Maalum katika 40:15! Ufunuo wa Mungu kupitia uzao wa Ibrahimu ulikuwa ujumbe kwa ulimwengu wote. Sasa uzao wa Ibrahimu ni waamini wote katika Kristo (kama vile Rum. 2:28-29)!

D. Tambua mzungumzaji katika ushairi niYHWH Mwenyewe (au Hekima Iliyoainishwa ya Mit. 9:1-6). Mwaliko pekee wa mist. ya6-7 ndio unaozungumzwa na nabii ambaye amekirimiwa huruma za YHWH.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 55:1-5**
**1 Haya, kila aonaye kiu, njoni majini,**
**Naye asiye na fedha; njoni, nunueni mle;**
**Naam, njoni, nunueni divai na maziwa, Bila fedha na bila thamani.**
**2 Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula?**
**Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha?**
**Nisikilizeni kwa bidii, mle kilicho chema,**
**Na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono.**
**3 Tegeni masikio yenu, na kunijia; Sikieni,**
**na nafsi zenu zitaishi;**
**Nami nitafanya nanyi agano la milele, Naam, rehema za Daudi zilizo imara.**
**4 Angalieni, nimemweka kuwa shahidi kwa kabila za watu;**
**kuwa kiongozi na jemadari kwa kabila za watu.**
**5 Tazama, utaita taifa usilolijua,**
**na taifa lisilokujua wewe litakukimbilia,**
**kwa sababu ya Bwana, Mungu wako, na kwa ajili yake Mtakatifu wa Israeli;**
**maana amekutukuza.**

**55:1-3** Mwaliko waYHWH kwa mwanadamu (yaani, "kila aonaye kiu," kama vile mst. wa 1a) una masharti mengi ambayo hasa ni msisitizo wa mialiko ya ki-Uungu.

1. njoni majini – *Qal* ya KAULI SHURUTISHI (BDB 229, KB 246)
2. njoni – ni sawa na #1
3. kwa – *Qal*yaKAULI SHURUTISHI(BDB 991, KB 1404)
4. mle– *Qal* ya KAULI SHURUTISHI (BDB 37, KB 46)
5. njoni – ni sawa na #1 na 2
6. nunueni – ni sawa na #3
7. Nisikilizeni kwa bidii – *Qal* ya KAULI SHURUTISHIna KITENZI JINA HALISI cha asili ile ile (BDB 1033, KB 1570) kwa ajili ya msistizo
8. mle – ni sawa na #4
9. kujifurahisha nafsi zenu– *Qal*ya KAULI ISIYO TIMILIFU (BDB 772, KB 851) inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI
10. Tegeni masikio yenu – *Hiphil*ya KAULI SHURUTISHI (BDB 639, KB 692)
11. kunijia – I sawa na #1,2,5; yatambue mambo binafsi
12. Sikieni – *Qal*ya KAULI SHURUTISHI (BDB 1033, KB 1570)
13. nafsi zenu zitaishi – *Qal* ya KAULI AMRISHI (BDB 310, KB 309)
14. nitafanya nanyi agano la milele – *Qal* ya KAULI YA KUSIHI (BDB 503, KB 560, tazama Mada Maalum: Agano katika 40:1)

**55:1 "kila aonaye"** Kifungu hiki kinazungunzia mwaliko wa Mungu wa kiulimweengu (kama vile mist. ya 4-5; Mwa. 3:15; 12:3;Kut. 19:5-6; Yohana 1:12; 3:16; 4:42; I Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; II Pet. 3:9; I Yohana 2:1; 4:14)

◙**" kiu"** Kipengele hiki kinaonekana kuwa na maana ya hitaji la kiroho. Mara nyingi hii ni hatua ya kwanza ambapo yampasa kila mwanadamu aliyeanguka kuichukua (kama vile Mt. 5:6; Ufu. 22:17).

◙**"majini"** Kanisa la mwanzo lilikifasiri kifungu hiki kama ubataizo. Huu ni mfano mzuri wa maelezo ya umakinifu (fasiri ya andiko linalorudia kile tunachokiamini). Kwa watu wa jangwani, hii ilikuwa ishara ya uhai na mafanikio (kama vile 41:17; 44:3).

◙**"kwa ajili ya kitu ambacho si chakula"** Kifungu hiki kinarejelea hali ya rasilimali binafsi. Neema, si faida, ndiyo ya mwanadamu, hata Israeli, tumaini tu (kama vile Eze. 36:22-38).

◙**"mle"** Mlo lilikuwa tendo la muhimu sana katika Mashariki ya Kati. Maagano na urafiki vilifungamanishwa kwa chakula.

◙**"nunueni. . . bila thamani"** Kwa namna iliyo dhahiri huu ni usemi wa kimafumbowenye kudadavua hitaji la amani ya mwanadamu pamoja na Mungu.
1. haiwezi kununuliwa pasopo gharama kulipwa
2. kwa namna ya kukata tamaa mara nyingi wanadamu hujaribu kuitafuta amani na furaha, lakini hawafaidiki (kama vile Mhubiri 1-2)
3. Mungu ametoa njia kupitia "Daudi" mpya kwa ajili ya kumjia yeye
4. Bado kuna gharama, lakini sasa ni toba na kukipokea kile Mungualichokitoa bure katika Masihi wa uzao wa Daudi.

**55:2 "Kwani kutoa fedha. . .kwa kitu kisichoshibisha"** Kifungu hiki kinaakisi hitaji endelevu la mwanadamu kwa ajili ya kuhitaji furaha katika mambo, shauku, au uweza (kama vile kitabu cha Mhubiri).

◙**"kujifurahisha nafsi zenu kwa unono"** Mungu anatutaka tuwe na furaha na kuwa na shauku ya kuwa na ushirika katika yeye (kama vile Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 27-28; Yohana 5:11). Dunia pamoja na uzuri wake na unono ni kwa ajili ya furaha ya mwanadamu!

**55:3 "kunijia"** Uhusiano binafsi ndiyo msingi wa imani ya kibiblia! YHWH mwenyewe ndiyo shabaha, si ukweli unaomhusu yeye! Tazama Mada Maalum katika 45:5.

◙**"Sikieni"** Hiki ni kifungu kinachotokana na neno*Shema* (kama vile Kumb. 6:4-5). Hiki kinaweza kumaanisha "kusikiliza na kutenda."

◙**"agano la milele"** Angalia maeleo katika40:28.Neno Milele (BDB 761, tazama Mada Maalum katika 45:17) linatumika kutoa ufafanuzi wa vitu vingi katika Isaya 40-66.

◙**"rehema za Daudi zilizo imara"** Kifungu hiki kinatokana na neno*hesed* (BDB 338). Hiki kinamaanisha "uaminifu wa agano.Tazama Mada Maalum katika 40:6.

◙**"Daudi"**Huu ni mfano wa upendo wa Mungu na kujali kwake hata kwa wale wasio waaminifu (kama vile Zab. 32,51). Pia rejea hii ina maana za ki- Masihi (kama vile II Sam. 7:1 na kuendelea), ambazo zina sifa ya ndani.

**55:4 ". . . kiongozi na jemadari kwa kabila za watu"** Kifungu hiki kinaenda mbali zaidi ya Daudina kumwelekea Masihi (kama vile f. II Samweli 7) kwa sababu kivuli ni Mataifa (kama vile mist. ya 4-5).

Toleo la MTna LXX linaneno "yeye" lenye kurejelea uzao wa Daudi (yaani, Masihi), kwa sababu zingine, matoleo ya Shamu yana neno "wewe." Hili ni suala lile lile la kithiolojia laandiko la "Mtumishi Ateswaye" la 52:12- 53:13.

◙**"watu. . . taifa"** Mataifa yanajumuishwa (tambua WINGI).

**55:5** Mataifa yatamjia Mungu waIsraeli na kuwaheshimu watu wake (kama vile 45:14,22-25; 49:6,12,23; Zek. 8:20-23). Swali linabaki: Je! Hili ni swali kwa Israeli iliyoamini, iliyorejeshwa (si utawala wa Israeli ya sasa) au hili ni rejea ya matukio ya siku za mwisho kwa Amri Kuu?

◙ Yatambue majina ya Uungu waIsraeli(tazama Mada Maalum katika 40:3).

1. YHWH
2. Wewe ni*Elohim*
3. Aliye Mtakatifu wa Israeli (tazama maelezo katika Isa. 1:4 mtandaoni katika*www.freebiblecommentary.org)*

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 55:6-13**
**6 Mtafuteni Bwana, maadamu anapatikana,**
**Mwiteni, maadamu yu karibu;**
**7 Mtu mbaya na aache njia yake,**
**Na mtu asiye haki aache mawazo yake;**
**Na amrudie Bwana,**
**Naye atamrehemu;**
**Na arejee kwa Mungu wetu,**
**Naye atamsamehe kabisa.**
**8 Maana mawazo yangu si mawazo yenu,**
**wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana.**
**9 Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi,**
**kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu,**
**na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.**
**10 Maana kama vile mvua ishukavyo, na theluji, kutoka mbinguni,**
**wala hairudi huko;**
**bali huinywesha ardhi, na kuizalisha na kuichipuza,**
**ikampa mtu apandaye mbegu, na mtu alaye chakula;**
**11 ndivyo litakavyokuwa neno langu,**

**litokalo katika kinywa changu;**
**halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu,**
**nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma.**
**12 Maana mtatoka kwa furaha, Mtaongozwa kwa amani;**
**Mbele yenu milima na vilima vitatoa nyimbo;**
**Na miti yote ya kondeni itapiga makofi.**
**13 Badala ya michongoma utamea msunobari, Na badala ya mibigili, mhadesi;**
**Jambo hili litakuwa la kumpatia Bwana jina,**
**Litakuwa ishara ya milele isiyokatiliwa mbali.**

**55:6 "Mtafuteni Bwana,"** Hiki kifungu"Mtafuteni"ni*Qal ya* KAULI SHURUTISHI (BDB 205, KB 233). Hiki KITENZI mara nyingi kinatumika katika kumhitaji Mungu katika maana binafsi (kama vile Kumb. 4:29; Isa. 58:2; 65:10). Huku kumhitaji kutafafanuliwa vema katika Kumb. 30:1-3,10na Yer. 29:13-14; Amosi 5:14-15.

◙**"maadamu anapatikana"** Hakuna awezaye kuja kwa Mungu pasipo kuwa na mvutano (kama vile 45:22; Yohana 6:44.65), bali anapowavuta, yawapasa wanadamukuwa na mwitikio. Kamwe Mungu hawezi kuubatilisha uumbaji wake (kama vile Zab. 103:8-14), bali kuna wakati wa kuchagua. Ikiwa nyakati zitapita, ugumu wa moyo wa mwanadamu utaendelea katika ukosefu wa uwezo wa kumsikiliza Mungu na kumwitika yeye.

◙**"Mwiteni, maadamu yu karibu"** Hiki kifungu"Mwiteni" pia ni*Qal* ya KAULI SHURUTISHI(BDB 894, KB 1128). Huu mstari wa ushairi unafanana na mstari wa hapo juu. Hii lugha inadokeza mazingira ya ibada, kama ilivyo Rum. 10:9-13 auYohana 1:12. Yawapasa wanadamu kuitikia katika toba na imani (kama vile Yer. 3:12-13; 4:1-4; Yoell 2:12-13; Amosi5:4-7,14-15; Marko 1:15; Yohana 3:16; Matendo 20:21). Hili agano lililo sahihi ni la kweli kwa Agano la Kale pamoja na Agano Jipya. YHWH hukusudia ushirika, kwa watu wote!

**55:7 "Mtu mbaya na aache njia yake"** Maisha ya toba ni muhimu. Tazama Mada Maalum katika 44:22.

◙Angalia ufanano uliopo katika ya mistari miwili ya mwanzo.Uovu unaelezwa katika namna mbili.
1. matendo ya mtindo wa maisha
2. mawazo ya maisha

Walimu wa sheria za Kiyahudi wanayo mawazo ya msaada huhusu hili. Hawa wanafafanua mawazo ya maisha kama bustani ambayo iko tayari kusiiwa mbegu. Kile tunachokiona kupitia macho yetu na masikio yetu huangukia katika udongo ulio tayari. Ikiwa tutachagua kuishi katika hicho ndivyo tutakavyokuwa.Dhambi huanza katika maisha ya mawazo, lakini muda hutimia na kuwa katika mkono/mguu/mdomo! Hebu yalinde mawazo yako ya maisha!

VITENZI vitatu vya mwanzo vya mst. wa7 ni KAULI AMRISHI.
1. aache – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 736, KB 806) inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI
2. amrudie – *Qal* ya KAULI AMRISHI (BDB 996, KB 1427, kama vile 31:6; 44:22
3. atamrehemu – *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 933, KB 1216) inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI, 49:10,13; 54:8

◙**"Naye atamsamehe kabisa"** Naipenda sura hii! Huu ni mwaliko wa kushangaza kwa watu wenye njaa ya kiroho ambao wamehitajika kwa shari baada ya kupendwa, kusamehewa, na Mungu muumbaji!

Vitambue VITENZI vyenye nguvu.
1. "kabisa" – *Hiphil*ya KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU
2. atawasamehe – *Qal*ya KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO

Wale waliokwisha kulipokea pendo na msamaha wa Mungu wana nguvu, huu ni ujumbe wa kustaajabisha wenye kushirikishwa katika ulimwengu ulioogopeshwa, uliokanganywa, wenye majeraha, uliokatishwa tamaa, ulimwengu wenye dhambi!

◙**"Naye atamrehemu. . . atamsamehe kabisa"** Mungu anaposamehe, husahau (kama vile Zab. 103:12; Isa. 1:18; 38:17; 43:25; 44:22; Mika 7:19). Ni ukweli ulioje unaostaajabisha wa pendo na msamaha wa Mungu(kama vile Heb. 9:14; I Yohana 1:7). YHWH anayo hiari, yu tayari, na anaweza kukubali, kusamehe, na kuurejesha uumbajiwake ulioanguka katika sura yake!

**55:8-11** Mistari hii ina dhima zinazofanana, Makusudi ya ukombozi wa YHWH! Beti za mst. wa 8 zinazofanana zinazungumzia upekee wa sifa ya utukufu wake. Wanadamu huofia kifo lakini yeye huwapa uzima, amani, na uwepo wake binafsi! Kwa ujumla yeye ni tofauti na wanadamu, lakini anawapenda wanadamu. Yeye aliwaumba kama yeye mwenyewe (kama vile Mwa. 1:26-27) kwa ushirika (kama vile Mwa. 3:8; Law. 26:12). Hatatuacha twende tu! Yeye anatutunza katika huruma na katika Kristo!

**55:11 "neno langu. . .  halitanirudia bure"** Mungu ni mkuu (kama vile 40:8). Neno la Mungu lililonenwa lina nguvu kubwa katika Agano la Kale (kama vile Mwanzo 1). Katika sura hii uweza wake, makusudi ya neno ni kwa ajili ya huruma, msamaha, na ushirika (kama vile 14:24; 25:1; 45:23; 46:10; 59:21; Mt. 24:35)!

## MADA MAALUM: DHAMANA YA MKRISTO

Dhamana ni(1) kweli ya kibiblia, (2) uzoefuwa imani ya mwamini, na (3) uthibitisho wa mtindo wa maisha.

A. Misingi ya kibiblia ya dhamana ni
    1. Tabia za Mungu Baba na kusudi
        a. Kutoka 34:6-7 (tazama Mada Maalum: Tabia za Mungu wa Israeli)
        b. Nehemia 9:17
        c. Yohana 3:16; 10:28-29 (tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi wa Milele)
        d. Warumi 8:38-39
        e. Waefeso 1:3-14; 2:5,8-9
        f. Wafilipi 1:6
        g. 2 Timotheo 1:12
        h. 1 Petro 1:3-5
    2. Kazi ya Mungu Mwana
        a. Maombi yake ya kikuhani, Yohana 17:9-24, hasa mst. wa12; Waebrania 7-9
        b. Kujitoa kwake kama dhabihu(kama vile. Isa. 52:13-53:12)
            1) Marko 10:45
            2) 2 Wakorintho 5:21
            3) 1 Yohana 2:2; 4:9-10
        c. Kusihi kwake katika hali endelevu
            1) Warumi 8:34
            2) Waebrenia 7:25
            3) 1 Yohana 2:1
    3. Uwezesho wa Mungu Roho Mtakatifu
        a. Wito wake, Yohana 6:44,65
        b. Hatima yake
            1) 2 Wakorintho 1:22; 5:5
            2) Waefeso 1:13-14; 4:30
        c. Dhamana yake binafsi
            1) Warumi 8:16-17
            2) 1 Yohana 5:7-13

B. Umuhimu wa mwitikio wa kimaagano wa mwaminini (angalia Mada Maalum: Agano)
   1. Toba na imani ya mwanzo na endelevu (tazama Mada Maalum: Je! "Pokea," "Amini," "Kiri/Ungama," na "Kusihi"kuna maanisha nini?)
      a. Marko 1:15
      b. Yohana 1:12
      c. Matendo 3:16; 20:21
      d. Warumi 10:9-13
      e.
   2. Kumbuka kwamba lengo la wakovu ni kumfanana Kristo
      a. Warumi 8:28-29
      b. 2 Wakorintho 3:18
      c. Wagalatia 4:19
      d. Waefeso 1:4; 2:10; 4:13
      e. 1 Wathesalonike
      f. 2 Wathesalonike 3:13; 4:3; 5:23
      g. Tito 2:14
      h. 1 Petro 1:15
   3. Kumbuka kwamba dhamana inakamilishwa na mtindo wa maisha
      a. Yokobo
      b. 1 Yohana
   4. Kumbuka kwamba dhamana inakamilishwa kwa imani thabiti na stahimilivu (tazama Mada Maalum: Ustahimilivu)
      a. Marko 13:13
      b. 1 Wakorintho 15:2
      c. Waebrania 3:14; 4:14
      d. 2 Petro 1:10
      e. Yuda 1:20-21

**55:12-13** Katika muktadha wa Agano la Kale ishara ya uwepo wa Mungu na baraka ilikuwa kuwepo kwa mavuno tele (yaani, mist. ya 1-2). Mara nyingi uumbaji unabainishwa kama kufurahi katika uwepo wa Mungu. Uhusiano mzuri wa Bustani ya Edeni unarejeshwa! Lazima mfasiri aulize, Je! Hili lilikamilishwa kwa kurudi kwake chini ya Zerubabeli, Yoshua, Ezra, Nehemia?
Jibu dhahiri ni, hapana! Hivyo, suala hili lazima litazamiwe kama mazingira ya matukio ya siku za mwisho.

# ISAYA 56

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Thawabu kwa ajili ya Utii kwa Mungu | Wokovu kwa Mataifa | Baraka kwa wale wote wanaitunza Sabato | Watu wa Mugu Watayajumuisha Mataifa yote | Ahadi kwa Wageni |
| 56:1-5<br>(1-5) | 56:1-25<br>(1-2) | 6:1<br>(1) | 56:1-2 | 56:1-7<br>(1-7) |
| | | 56:2<br>(2) | | |
| | | | 56:3a | |
| | 56:3-5<br>(3-5) | 56:3-5<br>(3-5) | 56:3b-5 | |
| 56:6-8<br>(6-8) | 56:6-8<br>(6-8) | 56:6-8<br>(6 -8) | 56:6-7 | |
| | | | 56:8 | 56:8-9<br>(8-9) |
| | Watawala wa Israeli Wasiowajibika | Ddhidi ya Watawala Waliopotoka | Watawala wa Israeli wanalalamikiwa | |
| 56:9-12<br>(9-12) | 56:9-12<br>(9-12) | 56:9-12<br>(9-12) | 56:9-12 | Kutostahili kwa Watawala wa Taifa la Israeli |
| | | | 56:10-57:2 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xvi katika kipengele cha utangulizi)

*KUFUATATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

13. Aya ya kwanza
14. Aya ya pili
15. Aya tatu
16. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA.

Kuna badiliko kutoka katika ujumbe wa Isaya kwa wale waliorejea kutoka uhamishoni Mesopotamia (sura ya 40-55) hadi kwa wale wasio na imani, watu wa agano katika Palestine (sura ya 56-66).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 56:1-3 (5)**
**[1]Bwana asema hivi,**
**Shikeni hukumu, mkatende haki;**
**kwa maana wokovu wangu u karibu kuja,**
**na haki yangu kufunuliwa.**
**[2]Heri afanyaye haya,**
**na mwanadamu ayashikaye sana;**
**azishikaye sabato asizivunje,**
**auzuiaye mkono wake usifanye uovu wo wote.**
**[3] Wala mgeni, aambatanaye na Bwana,**
**asiseme hivi, Hakika yake Bwana atanitenga na watu wake;**
**wala towashi asiseme, Mimi ni mti mkavu.**
**[4] Kwa maana Bwana awaambia hivi matowashi,**
**wanaozishika sabato zangu, na kuyachagua mambo yanipendezayo, na kulishika sana agano langu;**
**[5]Nitawapa hawa nyumbani mwangu, na ndani ya kuta zangu,**
**kumbukumbu na jina, lililo jema kuliko kuwa na wana na binti;**
**nitawapa jina lidumulo milele, lisilokatiliwa mbali.**

**56:1** Sura hiiinaanzanamaagizo mawili yaliyohusiana na maisha ya imani inayofaa (kama vile 55:7).
1. Shikeni hukumu – *Qal* ya SHURUTISHI (BDB 1036, KB 1581, kama vile 1:17); neno “mema,” angalia Mada Maalum katika 42:1
2. mkatende haki – *Qal* ya KAULI SHURUTISHI(BDB 793, KB 889); neno “haki,”angalia Mada Maalum katika 48:1

◙ Sababu ya kuishi maisha ya imani ni
1. wokovu wangu u karibu kuja – *Qal ya*KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO (BDB 97, KB 112, kama vile 46:13;51:5; Zab. 85:9)
2. haki yangu kufunuliwa , – *Niphal* ya KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO

(BDB 162, KB 191, angalia marejeleo ya mistari miwili ya kwanza ya aina hiyo hiyo kama #1)
Yawapasa waamini kuishi maisha ya imani kila siku kama vile Bwana anakuja leo! Mtazamo na maisha haya hutuweka karibu na Mungu (kama vile Zab. 85:9).

**56:2** Tambua kuwa mistarai miwili ya kwanza inafanana. Pia kifungu cha “Heri mtu yule ” kama vile Zab. 112:1; 119:1-2,22,168;128:1) ni yule apendezwaye/aishikaye sheria ya Mungu.

◙ Mistari miwili ya pili inayabainisha mambo maalum ambayo “mtu mwenye heri” hatayafanya.
1. kuikufuru sabato (kama vile Kut. 20:8-11)
2. kufanya uovu wa aina yo yote (muhutasari wa kifungu)

Hiki KITENZI “azishikaye” (BDB 1036, KB 1581) kinajitokeza mara nne katika sura hii (mist. 2 [mara mbili],4,6). Mtindo wa maisha ya imani na utii ndiyo vipengele vikuu na muhimu vya uhusiano binafsi na YHWH.

**56:3** Mstari huu unawahakikishia wale ambao walikuwa wakitengwa na Mungu waIsraeli mara kwa mara ya kwamba nao watajumuishwa.
1. yule anayeabudu lakini si Mwisraeli (kama vile mist. 4-5)
2. mtu aliyeathiriwa kimwili (kama vile mist. ya 6-8, Kumb. 23:1-8)

Neno “linasema,” kifungu abacho kimarudiwa mara mbili (mgeni, aambatanaye na Bwana) ni *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU(BDB 55, KB 65) inayotumika katika maan ya KAULI AMRISHI.

◙**“aambatanaye na Bwana”** Kifungu hiki kinamrejelea mtu
1. mwenye kuwa na tatizo kwenye kende zake
2. mtu aliyehasiwa

Habari za yule towashi wa Kikushi katika Matendo 8 yaliyokubaliwa ndani ya watu wa Mungu kupita imani katika Yesu Kristo, Mtumishi Ateswaye, ndiyo mfano mkuu wa aina hii ya kuambatanishwa kwa watu!

◙**“Hakika yake Bwana atanitenga”** Hiki ni kifungu cha *Hiphil* ya KITENZIJINA HALISI na *Hiphil* ya KAULI ISIYO TIMILIFU kutokana na asili ile ile (BDB 95, KB 110) kifungu kinachotumika kusistiza. Hata hivyo, msistizo mkubwa kwamba usemi huu si wa kweli!

**56:5** Matowashi wasingeweza kuwa na watoto wa asili hivyo YHWH atawapa kumbukumbu matowashi waaminifu ndani ya nyumba yake. Yeye atawapa “jina la milele” (yaani, nahau ya Kiebrania inayomaanisha vizazi).

◙

**NASB, REB** **“ kumbukumbu”**
**NRSV, LXX, Peshitta** **“mahali”**
**NJB, JPSOA** **“ukumbusho”**

Hili neno la Kiebrania kiuhaliasia ni “mkono” (BDB 388, #4) lakini linatumika kinahau kumaanisha kumbukumbu (kama vile I Sam.15:12; II Sam. 18:18)

**ANDIKO LA NASB 9LILILOBORESHWA) 56: 6-8**
**6 Na wageni, walioandamana na Bwana**
**ili wamhudumu, na kulipenda jina la Bwana,**
**kuwa watumishi wake;**
**kila aishikaye sabato asiivunje, na kulishika sana agano langu;**
**7 Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu,**
**na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala;**
**makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu;**
**kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote.**
**8 Bwana MUNGU, akusanyaye waliofukuzwa katika Israeli asema,**
**Pamoja na hayo nitamkusanyia na wengine, zaidi ya hao walio wake waliokusanywa.**

**56:6** Tambua kuwa wageni waaminifu wanaainishwa.
1. wameandamana na Bwana – *Niphal* ya KAULI YA ENDELEVU (BDB 530, KB 522)
2. wanahudumu kwa ajili yake – *Piel* ya TUNGO YA KITENZI JINA (BDB 1058, KB 1661)
3. wanalipenda jina la Bwana – *Qal* ya TUNGO YA KITENZI JINA (BDB 12, KB 17)
4. wanakuwa watumishi wake – *Qal* ya KAULI YA KITENZI JINA (BDB 224, KB 243)
5. wanaishika sabato – *Qal* ya KAULI ENDELEVU (BDB 1036, KB 1581, kama vile mist. ya 2,4) na *Piel* ya TUNGO YA KITENZI JINA (BDB 320, KB 319)
6. Wanalishika sana agano lake – *Hiphil* ya KAULI ENDELEVU (BDB 304, KB 302)

wafuasi wa YHWH walio wa kweli wanajulikana kwa mtindo wa maisha yao ya imani (kama vile Mathayo 5-7, hasa 7:15-23,24-27).

**56:7-8** Kama mst. wa6 ulivyofafanua kuhusu matendo ya wagaeni, ndivyo mist. ya 7-8 inavyofafanu yale ambayo Mungu mwaminifu atayatenda kwao.
1. Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu (yaani, hekalu)
2. kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala
3. makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu

4. nitamkusanyia na wengine, zaidi ya hao walio wake waliokusanywa

**56:7 "nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote"** Haya ni maelezo ya sababu ya kujengwa kwa hekalu la Suleimani (kama vile Fal. 8:41-43). Yesu anaunukuu mstari huu katika Mt. 21:13; Marko 11:17; Luka 19:46 kama alilisafisha hekalu lilikuwa mahali pa kuuzia wanyama na kubadilishia fedha.

**56:8**
**NASB "nitamkusanyia na wengine"**
**NKJV "nitamkusanyia wengine kando kando"**
**NRSV, Peshitta "nitawakusanyia wengine"**
**TEV "amehaidi kuwa bado atawaleta watu wengine kwa ajili ya kuungana nao**
**NJB "kuna wengine nitakao kusanya"**

Kuna uwezekano wa namna mbili.

1. YHWH atavikusanya hata vizazi vua Abrahamu vilivyokuwa uhamishoni (JPSOA)
2. YHWH atawakusanya wale waliotengwa (yaani, wageni, matowashi)

Matumizi ya Yesu ya andiko hili (kama vile Marko 11:17 linalofuatiatilia LXX) yanaonyesha mtazamo mpana uliokusudiwa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 56:9-12**
**9 Enyi hayawani wote wa nyikani,**
**njoni, Mle, enyi hayawani wote wa mwituni.**
**10 Walinzi wake ni vipofu,**
**wote pia hawana maarifa;**
**wote ni mbwa walio bubu,**
**hawawezi kulia; huota ndoto, hulala, hupenda usingizi.**
**11 Naam, mbwa hao wana choyo sana, hawashibi kamwe;**
**na hao ni wachungaji wasioweza kufahamu neno;**
**wote pia wamegeuka upande, wazifuate njia zao wenyewe,**
**kila mmoja kwa faida yake, toka pande zote.**
**12 Husema, Njoni, nitaleta divai, Na tunywe sana kileo;**
**Na kesho itakuwa kama leo, Sikukuu kupita kiasi.**

**56:9** Huu ni mwigo wa mwaliko wa karamu ya ki-Uungu (kama vile mst. wa 12; 55:1-2), lakini hapa katika muktadha wa hukumu (mist. ya 10-12) ni amri ("njoni" – *Qal*ya KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO). Hii ni meza ya hukumu!

Kuna maswali yenye kutafsirika ambayo yanahusiana na mist. ya 9-12, ambapo yanabainisha lini jambo hili litatokea.

1. Kabla ya uhamisho
2. Kwenye uhamisho
3. Baada ya uhamisho

Suala ni kwamba ni kipindi gani cha historia ya Israeli ambacho kinarejelewa na mistari hii? Huenda kipindi hiki kinahusiana na baadhi yao katika kila kipindi. Mara kwa mara kulikuwa na watawala na watu wasio waaminifu.

**56:10-12** Mistari hii iko katika tofauti kali ya waaminifu waliotengwa wa mist. ya mist. ya 1-8. Hawa wanaibainisha hali ya kiroho ya Israeli (hasa viongozi wake).

1. walinzi wake ni vipofu
2. wote pia hawana maarifa
3. wote ni mbwa walio bubu
4. ndoto /kichaa (kutokana na asili ya Kiarabu au "pumzi" [KB 243], lenye kuwarejea "mbwa" ya mist. ya 10c)
5. hupenda usingizi
6. wana choyo

7. hawashibi kamwe
8. wachungaji wasioweza kufahamu neno
9. wazifuate njia zao wenyewe
10. kila mmoja kwa faida yake, toka pande zote

Lahaula! Ni maelezo yenye kuogofya kwa namna iliyoje kwa watu wa agano. Wala wao ni wala rushwa na mithali ni ya kweli, kama vile mtawala, kama watu! Ufunuo wa Mungu, hekalu, na wacha Mungu hawana tofauti. Matunda yao ni dhahiri (yaani, yao wenyewe)!

**56:10 "walinzi wake ni vipofu"** Wasomi wa toleo la MT waligundua tatizo katika andiko la Kiebrania. Hili linasomwa *Qal* ya KAULI YA TIMILIFU (BDB 859, KB 1044), lakini linapendekeza *Qal* ya KAULI ENDLEVU. Kwa vyo vyote hili halibadilishi maana ya andiko hili.

**56:12"Njoni"** Hii KAULI SHURUTISHI (*Qal*, BDB 87, KB 102) inaendana na mst. wa 9c! Wanadamu wamegeukia ulevi na kumkana Mungu (mst. wa 12b), hivyo wanyama wanaalikwa na Mungu kuwararua watu wake wa agano (kama vile. 18:6; Yer. 7:33; 12:9; 15:3; 34:20)

# ISAYA 57

| MIGAWANYO YAAYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Watawala Waovu Wanakaripiwa | Israeli na ibada ya sanamu | Dhidi ya Ibada za Samamu | Israeli inashutumiwa kwa ajili ya Ibada za Sanamu | kutokuwepo uaminifu kwa viongozi wa Maifa ya Israeli (56:10-57:2) |
| 57:1-10 (1-10) | 57:1-2 (1-2) | 57:1-12 (1-12) | 57:1-2 | (56:10-57:2) |
| | | | | Dhidi ya ibada za Sanamu |
| | 57:3-6 (3-6) | | 57:3-10 | 57:3-13 (3-13) |
| | 57:7-10 (7-10) | | | |
| 57:11-13 (11-13) | 57:11-13 (11-13) | | 57:11-13 | |
| | Uponyaji kwa Walioanguka | | Ahadi za msaada wa Mungu na Uponyaji | Wokovu kwa wanyonge |
| 57:14-21 (14-21) | 57:14 (14) | | 57:14 | 57:1 4-16 (14-16) |
| | 57:15-18 (15-18) | | 57:15-17 | |
| | | | | 57:17 (17) |
| | | | 57:18-21 | 57:18-21 (18-21) |
| | 57:19-20 (19-20) | | | |
| | 57:21 (21) | | | |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xxiv kipengere cha utangulizi)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

17. Aya ya kwanza
18. Aya ya pili
19. Aya ya tatu
20. Nk

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

A. Kimuktadha ni wazi dhambi ya Israeli inaendelea kutoka Sura ya 56.
B. Hii inaelezea Agano la kale kama chaguo la "njia mbili" moja ya uzima na amani nyingine yenyewe , ya dhambi, na uharibifu (kama vile. Kumb. 30:15,19).
C. Leupold ametoa maelezo yenye shauku (uk. 271) kwamba kama Sura ya 56 ilivyohitimishwa juu ya viongozi wasio na imani, Sura ya 57 inahusika na watu wasio na imani.
D. Mpangilio wa kuabudu sanamu haukuwa Mesopotamia bali ibada za ustawi wa Kanaani (yaani., *Ba'al*, *Asherah*, *Molech*). Hii ilifikia kilele chake chini ya mfalme Manase.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 57:1-10**
**1 Mwenye haki hupotea, wala hakuna atiaye hayo moyoni;**
**na watu watauwa huondolewa, wala hakuna afikiriye**
**ya kuwa mwenye haki ameondolewa asipatikane na mabaya.**
**2 Yeye huingia katika amani;**
**wao hustarehe katika vitanda vyao,**
**kila mtu aendaye katika unyofu wake.**
**3 Lakini ninyi karibuni hapa, enyi wana wa mwanamke mchawi,**
**uzao wa mzinzi na kahaba.**
**4 Mnafanya dhihaka yenu juu ya nani?**
**Mmepanua vinywa vyenu,**
**na kutoa ndimi zenu?**
**Je, ninyi si wana wa uasi,**
**uzao wa uongo;**
**5 ninyi mnaowasha tamaa zenu kati ya mialoni,**
**chini ya kila mti wenye majani mabichi;**
**ninyi mnaoua watoto mabondeni,**
**chini ya mianya ya majabali?**
**6 Sehemu yako i katika makokoto ya bonde;**
**hayo ndiyo kura yako;**
**umeyamwagia hayo sadaka ya kinywaji,**
**umeyatolea sadaka ya unga;**
**je! Niwe radhi na mambo hayo?**
**7 Umeweka kitanda chako**
**juu ya mlima mrefu ulioinuka sana;**
**ukaenda huko ili kutoa dhabihu.**

**[8]Na nyuma ya milango na miimo**
**umeweka kumbukumbu lako;**
**kwa maana umejifunua nafsi yako kwa ajili ya mwingine, si kwa ajili yangu,**
**ukakwea juu; umekipanua kitanda chako,**
**nawe umefanya maagano na hao;**
**ulikipenda kitanda chao hapo ulipokiona.**
**[9]Ulimwendea mfalme na mafuta ya marhamu,**
**ukaongeza manukato yako,**
**ukawatuma wajumbe wako waende mbali,**
**ukajidhili sana hata kuzimu.**
**[10]Ulikuwa umechoka kwa ajili ya urefu wa njia yako;**
**lakini hukusema, Hapana matumaini;**
**ulipata kuhuishwa nguvu zako;**
**kwa sababu hiyo hukuugua.**

**57:1** mwovu husherehekea pale ambapo wenye haki huteswa na kuuwawa, na hakuna anaeonekana kujali hali hiyo!

1. Hakuna atiaye hayo moyoni
2. Hakuna afikiliye

◙**"ameondolewa asipatikane na mabaya"** kamawaouvu wanavyoangalia ubinafsi na dhambi, wenye haki wanaokolewa kutoka kwenye ushawishi mkubwa wa kuangamizwa (kama vile. Mwa 3; 6:5,11-12).

**57:2** Mstari huu unaelezea hali ya kiroho ya mtu mwenye haki.

1. Huingia katika amani (kwa sababu ya mst. 1 hii lazima ni ukomavu wa akili)
2. Hustarehe katika vitanda vyao (BDB 1012). Kuna mchezo wa maneno umetumika hapa katika neno hili juu ya wenye haki, lakini katika Mistari ya 7, 8, ya waovu.
   a. Kitanda kwa ajiri ya kulalia
   b. Kitanda kwa ajiri kujamiana
   c. kaburi
3. Aendaye katika unyofu wake (yaani , mtindo wa maisha ya uaminifu)

**57:3-4** Mistari hii inaelezea Uovu unaotajwa kwenye mst. 1. Wanaainishwa kama

1. Wana wa mwanamke mchawi (BDB 778 II)
2. Uzao wa uzinzi (BDB 610)
3. Uzao wa kahaba (BDB 275)

   YHWH anawaita wajitokeze (*Qal* KAULI SHURUTISHI, BDB 897, KB 1132) kwa ajili ya hukumu.
4. Uzao wa uongo (BDB 833)
   a. mnafanya dhihaka juu ya nani
   b. mmepanua vinywa vyenu juu ya nani
   c. mmemtolea nani ndimi zenu nje (hii inaelezea shutuma zao dhidi ya wenye haki)
5. Wana wa uasi (BDB 1055)

**57:5-6** kuabudu sanamu kunaelezewa kama

1. mnawasha tamaa zenu kati ya Mialoni (*Niphal* KAULI ENDELEVU, BDB 328, KB 328, hii inarejelea kuabudu miungu inayohusika na uzao ya *Ba'al* na*Ashera*,yaani., Yer. 2:23-27)
2. mnaouwa watoto (*Qal ya KAULI ENDELEVU*, BDB 1006, KB 1458, usemi huu unarejelea kumwabudu *Molech*)
3. chini ya mianya ya majabali (*Qal ya* KAULI YA WAKATI IMILIFU, BB 1049, KB 1629)
4. umeyatolea sadaka ya unga (*Hiphil ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU*, BDB 748)

## MADA MAALUMU: IBADA YA USTAWI WA MASHARIKI YA KARIBU YA KALE

I. Sababu ya

A. Wanadamu wa kale walianza kama wawindaji walioishi sehemu moja, lakini maisha ya kuhamahama yaliimarika, hitaji kwa ajili ya mazao na mifugo.
B. Wakazi wa Mashariki ya Karibu ya kale walikuwa hatarini kukabiliana na nguvu ya asili. Kadiri ustaarabu ulivyokua kuzunguka maeneo ya vyanzo vikubwa vya maji safi, walikuwa wategemezi kwa utaratibu wa kila siku wa majira.
C. Nguvu za asili ikawa miungu iliyotakiwa kujazwa na kuongozwa/kuendeshwa.

II. Wapi na kwanini
- A. Dini za kuabudu kuzaa ilikua katika
  1. Misri (Nile)
  2. Mesopotamia (Hedekeli na Frati)
  3. Kanaani (Yordani)
- B. Kuna ufanano wa msingi kati ya dini za uzao za Mashariki ya Karibu ya kale.
- C. Majira yanayobadilika na yasiyofikirika na hali ya hewa ilisababisha ukuaji wa hadithi za kishujaa kwa kutumia analojia ya kibinadamu /kiungu kama msingi wa maisha katika ulimwengu war oho na duniani.

III. Nani na namna gani
- A. Nani (miungu ya kiume na kike)
  1. Misri
     a. Isis (wa kike)
     b. Osiris (wa kiume)
  2. Mesopotamia
     a. Ishtar/Inanna (wa kike)
     b. Tammuz/Dumuzi (wa kiume)
  3. Kanaani
     a. Ba'al (wa kiume)
     b. Ashera, Astarte, Anathi (wa kike)
- B. Kila moja ya jozi hizi zilikuwa hadithi za kimiujiza katika namna inayofanana
  1. Mmoja anafariki
  2. mwingine anarejesha
  3. Utaratibu wa kufa na kuinuka kwa miungu kunaiga mzunguko wa kila mwaka wa asili
- C. Uigaji wa kimiujiza uliona muunganiko wa ujamiiana wa kibinadamu (yaani ndoa za miungu) kama njia ya kuhakikisha ustawi wa mazao, mifugo na watu.

IV. Waisraeli
- A. Watu wa YHWH walionywa (yaani Mambo ya Walawi na Kumbukumbu la Torati) kukwepa ibada za ustawi (haswa za Kanaani).
- B. Dini/ibada hizi zilikuwa maarufu kwasababu ya uchawi wa wanadamu na chagizo la nyongeza la tendo la ndoa
- C. Ibada ya sanamu ilishirikisha Baraka ya uzima kutafutwa katika njia za shetani badala ya imani binafsi na tumaini kwa YHWH.

V. Masomo yanayopendekezwa
- A. W. F. Albright, *Archaeology and the Religion of Israel*
- B. J. H. Breasted, *Development of Religion and Thought in Ancient Egypt*
- C. James G. Frazer
  1. *Adonis, Attis, Osiris*
  2. *Folklore in the Old Testament*
  3. *The Worship of Nature*

D. C. H. Gordon, *Before the Bible*
S. N. Kramer, *Mythologies of the Ancient World*

**MADA MAALUM: *MOLECH***

Hili neno (BDB 574, KB 592) halina uyakinifu. Kumekuwa na nadharia kadhaa.

1. zinazohusianana miungu iliyo ulimwenguni
   a. "*Malik*" kutokana na bamba za Ebla (± 2,300 B.C. kutoa Shamu ya kaskazini)
   b. "*Maliku*" au "*Muluk*" kutokana bamba za huko Mari (± 1800-1750 K.K. kutoka mji wa Sumeria ulio kandokando ya Mto Frati)

2. zinazohusiana na aina ya dhabihu kutokana na matumizi ya neno lenye kuhofisha "*molk*" kutokana na nguzo ya mawe ya afrika Kaskazini kuanzia karne ya 4 hadi karne ya 1 K.K.). Hili linaweza kuwa limemuhusisha kondoo mbadala aliyeteketezwa kwa niaba ya mtoto (Eissfeldt). Toleo la N. H. Snaith theorizes lilimaanisha kwamba watoto walitokana na mapenzi ya kikahaba, yaliyojikita juu ya
   a. Law. 18:19-23 yenye kuhusika na dhambi za uzinzi, hivyo mstari wa 18 pia unaweza kuwa hivyo
   b. Hivi ndivyo Kitabu cha Sheria za Kiyunani kinavyolichukulia neno hili pia

3. huenda mkanganyiko uliopo katika neno *Milcom* (kama vile *Molech* katika 1 Fal. 11:7, lakini tambua kuwa neno *Milcom* linatajwa kama 1 Fal. 11:5,33. Hata hivyo, hawa miungu wote wanarejelewa katika Zab. 106:35-39).

4. Hili neno ni uchezeaji wa neno la Kiebrania unaotokana na konsolnanti za neno "Mfalme" (MLK, BDB 591) zilizounganishwa pamoja na irabu zinazotokana na neno "aibu" (BDB 101 or 102). Hata kama suala hili ni kweli, hili halimwelezi mungu au dhehebu.

Dhehebu la *Molech* linaelezwa kama dhabihu ya mwanadamu kuwatoa watoto kama dhabihu, kwa moto (kwa vyovyote vile waliteketezwa wakiwa hai au walitolewa sadaka baada ya kuuawa kwa namna nyingine, haijulikani). ikiwa hili ni la kweli hii ilikuwa

1. aina ya dhehebu la ustawi
2. dhehebu ambalo lilimwabudu mungu wa ulimwenguni

Huyu mungu alikuwa akiabudiwa humo Yerusalemu katika bonde la wana wa Hinomu, bonde ambalo lilikuja kujulikana kama "Tofethi" (kama vile Isa. 30:33; 57:5; Yer. 7:31; 32:35). Ibada ilikuwa ikibainishwa kwa kutumia wana na mabinti zao kuwateketeza motoni (kama vile Kumb. 12:31; 18:10; 2 Fal. 16:3; 17:17,31; 21:6; Zab. 106:37; Yer. 7:31; 19:5; Eze. 16:20-21). Neno lenyewe linajitokeza katika Law. 18:21; 20:2,3,4,5; 1 Fal. 11:7; 2 Fal. 23:10; Yer. 32:35; huenda Amosi 5:26; Matendo 7:43. Hili dhehebu lilihusiana zaidi na Wafalme wa Yuda, Ahabu na Manase, ingawa linaonekana katika uhusiano wa kale wa Kiyahudi na ibada za ustawi za wapagani walioizunguka.

**57:6e**
**NASB “ Niwe radhi na mambo hayo”**
**NKJV “Yanipasa kupokea faraja katika haya”**
**NRSV “Niridhike kwa ajili ya mambo haya”**
**TEV “Mnafikiri nafurahishwa na hili”**

Ibada za Ustawi za Waisraeli, hata kama zilifanyika kwa jina la YHWH, hazikukubalika!

**57:7** Kifungu hiki kinazirejelea madhabahu za *Ba'al naAsherah* ambazo zilikuwa zimejengwa juu ya vilima (kama vile Kumb. 12:2; II Fal. 17:10; Yer. 3:6; 17:2; Hos. 4:13). Hiki kifungu "Umeweka kitanda chako" kinarejelea juu ya zile taratibu za matendo ya uzinzi yaliyofanyika kwa ajili ya usawi wa nchi, mifugo, na ongezeko la mwanadamu (kama vile mst. wa 8b-d).

**57:8** Mistari miwili ya kwanza ni yenye utata. Kipengele hiki kingaliweza kurejelea taswira ya ibada ya sanamu iliyokuwa

1. katika nyumba zao
2. katika kuta za vijiji vyao
3. ndani ya hekalu lenyewe (kama vile Ezekieli 8-10)

Mtu anastaajabu ikiwa kifungu hiki kilihusiana na umoja wa kisiasa/kijeshi pamoja na mataifa ya kipagani ambayo yalidai kuiabudu miungu ya kigeni (kama vile mist. ya 8d-e, 9).

◙

**NASB "ulikipenda kitanda chao hapo ulipokiona"**
**NKJV "ulipouona mkono wao"**
**TEV "ndipo ulipoitoshereza tamaa zako"**
**NJB "kwa macho yako juu ya alama iliyowakifishwa"**
**JPSOA "imeichagua hamu yako"**
**NRSV, NIV,**
**Peshitta "ulipouona utupu wao"**
**NET Bible "ulipoutazama uchi wao"**

Tatizo ni neno la Kiebrania יד (BDB 388, KB 386) ambalo kiuhalisia ni "mkono." Katika lugha ya Ugariti neno ידדlinamaanisha "upendo"; katika Kiarabuודי inamaanisha "kiungo cha uzazi cha mwaname" (kama vile NIDOTTE, juzuu 2, uk. 56). Hii pia ingeweza kurejelea "uweza" hapa katika maana ya ibada ya usawi. Kuna tafisda kadhaa zilizotumiwa na waandishi wa Kiebrania kuvirejelea viungo vya uzazi (mfano mwingine ni "miguu," BDB 919, kama vile Kut. 4:25; Kumb. 28:57; Amu. 3:24; Ruthu 3:8; I Sam. 24:3; Eze. 16:25).

**57:9-10** Kipengele hiki kinaonekana kurejelea juu ya taratibu za kisiasa ili kuhakikisha juu ya usalama wao dhidi ya uvamizi wa wageni.

**57:9 "mfalme"** Kifungu hiki kinaweza kueleweka kama chenye kumrejelea *Molech* mungu w**a**ustawi, ambaye jina lake lina konsonanti zinazofanana na zile za kifungu cha "mfalme" katika Kiebrania. Toleo la UBS linakipa kifungu "mfalme" daraja B (kuna mashaka fulani).

◙**"marhamu"** Angalia Mada Maalum: Wafu Wako Wapi? katika 44:23.

**ANDIKO A NASB (LILILOBORESHWA) 57:11-13**
**[11] Tena ni nani uliyemwogopa na kumhofu,**
**hata ukasema uongo,**
**wala hukunikumbuka mimi,**
**wala kuweka hayo moyoni?**
**e! Mimi sikunyamaza tangu zamani,**
**hata huniogopi?**
**[12] Mimi nitatangaza haki yako,**
**na matendo yako hayatakufaa.**
**[13]Utakapolia, na wakuponye hao uliowakusanya;**
**akini upepo utawachukua;**
**uvuvio tu utawachukulia mbali;**
**lakini yeye anayenitumaini ataimiliki nchi,**
**na kuurithi mlima wangu mtakatifu.**

**57:11-13** Ubetihuu unaanza na mfululizo wa maswali kutoka kwa YHWH kuwaelekea watu wake wa agano wasio waaminifu.
Huzuni ilikuwa kwamba hawa walikuwa "watu wa kidini" (kama vile mist ya 12,13a) lakini

1. wala hukunikumbuka mimi (*Qal* ya KAULI TIMILIFU, BDB 269, KB 269, iliyokanushwa)
2. hata mkasema uongo (kif. "wala kuweka hayo moyoni ," *Qal* ya KAULI YA WAKATAI TIMIIFU, BDB 962, KB 1321, iliyokanushwa)

Sababau zilizowafanya kumkataa YHWH zilikuwa ni kwa ajili ya ukimya wake (mst. wa 11d). Kifungu hikli kinaweza kuwarejelea manabii wa kweli ambao hawakutumwa au ambao hata hawakusikia.
sanamu ni "majivuno" na "utupu." Upepo uliwaondosha na kuwapeleka mbali, wale walioitumaini miungu hii.

**57:11**
**NASB, NJB "tangu zamani "**
**NKJV "tokea zamani"**
**TEV "kwa muda mrefu"**
**JPSOA "kwa mudamrefu sana"**
**REB "tazama "**
**NAB "kutoona"**

Toleo la JPSOA linayataja marekebisho ambayo yalizaa matunda ya kifungu "na kuayafumba macho yangu" (uk. 898), ambacho kinafuatiwa na toleo la REB na NAB. Konsonanti zile zile za Kiebrania ומעלם zinaweza kutafsiriwa "na toka umilele" au "na aliyefichika."

**57:13d-e** Lakini wale wachache walio waaminifu wanao mtumaini YHWH na "kuchukuwa hifadhi" (*Qal ya KAULI ENDELEVU*, BDB 340, KB 337) katika yeye watatunzwa na kuvikwa taji kwa kupewa

1. Nchi Iliyoahidiwa
2. Uwepo wa YHWH (yaani, hekalu)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 57:14-21**
**14 Naye atasema,**
**Tutieni, tutieni, Itengenezeni njia,**
**Kiondoeni kila kikwazacho Katika njia ya watu wangu.**
**15 Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele;**
**ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi;**
**Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu;**
**tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea,**
**ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu.**
**16 Kwa kuwa sitashindana na watu siku zote,**
**wala sitakuwa na hasira siku zote;**
**maana roho ingezimia mbele zangu, na hizo nafsi nilizozifanya.**
**17 Kwa sababu ya uovu wa kutamani kwake naliona hasira, nikampiga;**
**nalificha uso wangu, nikaona ghadhabu;**
**naye akaendelea kwa ukaidi, kuifuata njia ya moyo wake mwenyewe.**
**18 Nimeziona njia zake; nami nitamponya;**
**nitamwongoza pia, nitamrudishia faraja zake, yeye na hao wanaomlilia.**
**19 Mimi nayaumba matunda ya midomo;**
**Amani, amani, kwake yeye aliye mbali, na kwake yeye aliye karibu;**
**asema Bwana; nami nitamponya.**
**20 Bali wabaya wanafanana na bahari iliyochafuka;**
**maana haiwezi kutulia, na maji yake hutoa tope na takataka.**
**21 Hapana amani kwa wabaya; asema Mungu wangu.**

**57:14** Kuna mfululizo wa KAULI SHURUTISHI ambapoYHWH anaagiza kwamba maandalizi yote yaliyo ya muhimu yafanywe kwa ajili ya wale waaminifu wake waweze kurudi toka uhamishoni (kama vile 40:3-4; 62:10)

1. kujenga (mara mbili) – *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, BDB 699, KB 757
2. kuandaaa njia – *Piel* ya KAULI SHURUTISHI, BDB 815, KB 937
3. kuondoa kila kizuizi – *Hiphil* ya KAULI YA WAKATI SHURUTISHI, BDB 926, KB 1202

**57:15** Tambua majina na sifa bainishi za Mungu.

1. aliye juu**,** – *Qal* yaKAULI ENDELEVU, BDB 926, KB 1202 (KITENZI kile kile kinachotumika katika mst. wa 14 chenye kutafsiriwa "ondoa ," yaani, inua)
2. aliyetukuka – *Niphal ya KAULI ENDELEVU*, BDB 669, KB 724 (KITENZI kile kile kinachotumika katika mist. ya . 7,13, katika maana tofauti)
3. akaaye milele; – *Qa* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 1014, KB 1496, (kif. "ambaye makao yake ni ya milele"; Biblia ya NET [uk. 1275] inatoa dhahaniol kwamba katika muktadha huu kifungu hiki chapaswa kuelewekaka kama "yeye atawalaye milele")
4. ambaye jina lake ni Mtakatifu
5. Nakaa mimi mahali palipoinuk**a** – *Qal* ya KAULI ISIYO TIMILIFU, BDB 1014, KB 1496 (katika utofauti na miungu wa ustawi)
6. pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu (BDB 194 I) na kunyenyekea (BDB 1050) (BDB 924)
7. kuzifufua roho za wanyenyekevu – *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, BDB 310, KB 309, kilichotumiwamara mbili
   a. juu ya YHWH, #6
   b. juu ya uaminifu wake

**57:16a-b** Kifungu hiki kinaendele kutoa sifa bainifu zaYHWH kupitia YHWH.

1. "sitashindana na watu siku zote" – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 936, KB 1224, kama vile Mwa. 6:3
2. "wala sitakuwa na hasira siku zote" – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 893, KB 1124, kama vile Zab. 79:5; 85:5; 103:9; Mika 7:18-19

Kifungu hiki hakipaswi kutafasiriwa kama kipindi cha wakati kilichowekwa na Mungu baada ya neema yake kusitishwa, lakini ukweli ni kwamba wanadamu wanapolikataana kuenenda kinyume na neno lake na mapenzi yake, kuna matokeo ya kutisha yalijili kwa ajili ya kushupaza shingo zao.
Moyo wa mwanadamu hukosa uwezo wa kusikia na kuitikia!

Inatia shauku kwamba kitabu cha Agano la Kale kinazitofautisha hisia za upendo wa mwanadamu na ghadhabu pale kinapotaoa ufafanuzi wa sifa bainifu za Mungu.

1. upendo ni wa milele ni hakika –Kumb. 5:10; 7:9; Zab. 30:5; Isa. 54:7-8; Yer. 31:3
2. gadhabu huwa ni ya muda mfupi – Kumb. 5:9; Zab. 30:5; Isa. 26:20; 54:7-8; 57:16-19

**57:16c-d** YHWH anazifunua sababu zinazomfanya asikae na gadhabu (angalia Mada Maalum: Mungu Anaelezwa kama Mwanadamu katika 41:2). Kifungu hiki kinafanana sana na Zab. 103:8-14.

1. kwa maana roho (angalia Mada Maalum katika 40:7) ingezimia mbele zangu
2. na hizo nafsi nilizozifanyazingalizimia

Tambua ufanano wa neno "roho" (BDB 924) na neno "nafsi" (BDB 675) kama ilivyo katika 42:5. Udhaifu wa kimwili ambao sasa ni hali yakisaikolojia ya mwanadanu aliyeanguka hauwezi kuendeleza ukimya (mist ya 11,17) na gadhabu (mist.ya 16,17) ya Muumbaji na Mkombozi wao!

**57:17** Hukumu yaYHWH inafanana na adhabu ya mzazi (kama vile Hosea 11). Yeye hulifanya tendo hili ili watoto wake waweze kujifunza na kugeuka toka dhambini, bali kwa huzuni wengine hawataweza (mst. wa 17c; 1:3,4).

**57:18-21** Kuna tofauti iliyo dhahiri kati ya namna ambayo YHWH hutumia kwa wale waliotubu na waliokuwa wakaidi.

1. waliotubu – mist. ya 15-16,18-19

2. ukaidi –mst. wa 17,20-21

**57:18-19** Tambua kile atakachokifanyaYHWH kwa wale waliotubu na wenye unyenyekevu wa moyo (mst. wa 15), wale wote walio karibu na wenye hofu (mst. wa 19).

1. kuzifufua, mst. wa 15 – *Hiphil* ya TUNGO YA KITENZI JINA HALISI (BDB 310, KB 309)
2. sitashindana, mst. wa 16 – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 936, KB 1224)
3. sitakuwa na hasira siku zote, mst. wa 16 – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIF*U* (BDB 893, KB 1124)
4. nitamponya, mst. wa 18 – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 950, KB 1272)
5. nitamwongoza , mst. wa 18 – *Hiph*il ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 634, KB 685)
6. nitamrudishia faraja, mist. ya 18 – *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU (BDB 1022, KB 1532)
7. nayaumba matunda ya midomo;Amani, mst. wa 19 *Qal* ya KAULI ENDELELEVU(BDB 135, KB 153)
8. nitamponya , mst. wa 19 *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU (BDB 950, KB 1272)

**57:20-21** Hawa wakaidi, watu wa agano wasio waaminifu wanabainishwa kama

1. bahari iliyochafuka
2. bahari ambayo haiwezi kutulia
3. bahari ambayo maji yake hutoa taka taka
4. bahari ambayo maji yake hutoa tope
5. Hapana amani

# ISAYA 58

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kuutunza mfungo | Kufunga kunako Mpendeza Mungu | Bwana hahitaji mfungo lakini ni wema na haki | Mfungo wa kweli | Kufunga kunako mpendeza Mungu |
| 58:1-12<br>(1-12) | 58:1-3a<br>(1-3a) | 58:1-5<br>(1-5) | 58:1-2 | 58:1-12<br>(1-12) |
| | | | 58:3a | |
| | 58:3b-5<br>(3b-5) | | 58:3b-5 | |
| | 58:6-9a<br>(6-9a) | 58:6-9a<br>(6-9a) | 58:6-7 | |
| | | | 58:8-9a | |
| | 58:9b-12<br>(9b-12) | 58:9b-12<br>(9b-12) | 58:9b-12 | |
| Kuitunza Sabato | | | Thawabu ya kuitunza Sabato | Sabato |
| 58:13-14<br>(13-14) | 58:13-14<br>(13-14) | 58:13-14<br>(13-14) | 58:13-14 | 58:13-14<br>(13-14) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. Xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozokwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

17. Ayaya kwanza
18. Ayayapili
19. Ayatatu
20. N.k

## HISTORIA YA NYUMA

A. Hii ni sura inayolaani ibada za kidini pasipo imani binafsi (kama vile Isa 29:13; Jeremia 7).
B. Hili ni tatizo la kiroho lililosababisha watu kukimbilia uhamishoni.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 58:1-12**
**[1] Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao. [2]Walakini wanitafuta kila siku; hupenda kujua njia zangu; kama vile taifa waliotenda haki, wasioacha sheria ya Mungu wao, hutaka kwangu amri za haki; hufurahi kumkaribia Mungu. [3]Husema, Mbona tumefunga, lakini huoni? Mbona tumejitaabisha nafsi zetu, lakini huangalii? Fahamuni, siku ya kufunga kwenu mnatafuta anasa zenu wenyewe, na kuwalemea wote watendao kazi kwenu. [4] Tazama, ninyi mwafunga mpate kushindana na kugombana, na kupiga kwa ngumi ya uovu. Hamfungi siku hii ya leo hata kuisikizisha sauti yenu juu. [5] Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua mimi? Je! Ni siku ya mtu kujitaabisha nafsi yake? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga, na ya kukubaliwa na Bwana? [6]Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? [7]Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? [8]Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde. [9]Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu; [10]na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri. [11]Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui. [12]Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia.**

**58:1** Sura hii, kama zilivyo sura zingine za Isaya (yaani., alama halisi ya kifasihi kwa ajili ya shairi jipya), ikianza na mfuatano wa KAULI SHURUTISHI. Maswali ya kiutafasiri ni:

1. Nani mnenaji?
2. Nani mpokeaji?

Hapa pana orodha ya kile kichoamriwa (kumbuka dhana ya ufanano):

1. Piga kelele – *Qal* KAULI SHURUTISHI, BDB 894, KB 1128
2. usiache – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 362, KB 359, ikitumika kwa maana ya KUAMRISHA
3. Paza sauti – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, BDB 926. KB 1202
4. tangaza – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI, BDB 616, KB 665

Mnenaji ni YHWH kwa kinywa cha nabii wake na mpokeaji ni:

1. wakimbizi wa mwanzo wa Israeli
2. wakimbizi wa Israeli
3. Waisraeli waliorudi
4. watu wa Mungu wa siku za mwisho

◙**"tarumbeta"** Hii ni kutoka BDB 1051. Angalia Mada Maalum hapa chini.

### MADA MAALUM: PEMBE ZITUMIKAZO NA ISRAELI

Kuna maneno manne katika Kiebrania yahusianayo na pembe/tarumbeta.

1. "pembe ya mwana kondoo" (BDB 901) – ikigeuzwa kuwa chombo cha sauti, kama vile Yosh. 6:5. Neno hilihili linatumika kwa ajili ya mwanakondoo aliyenaswa na pembe zake ambaye Ibrahimu alimfanya mbadala wa Isaka katika Mwanzo 22:13.
2. "tarumbeta" (BDB 1051) – kutoka katika neno la kiashuru ikimaanisha kondoo wa porini (ibex). Hii ni pembe ambayo ilitumika katika Kutoka 19:16,19 katika Mlima Sinai/Horeb; #1 na #2 zina usambamba na Yos. 6:5. Ilitumika kuwasiliana wakati wa ibada na wakati wa kupigana (yaani Yeriko ilikuwa vyote, kama

vile Yosh. 6:4).

3. "pembe ya mwana kondoo" (BDB 385) – kutoka neno la kifoinike kwa ajili ya mwana kondoo (kama vile Yosh. 6:4,6,8,13). Ilisimama pia kwa ajili ya Mwaka wa Jubilei (kama vile Mambo ya Walawi 25:13,28,40,50,52,54; 27:17,18,23,24).
   (Zote za hizi tatu za kwanza zinaonekana kubadilishana bila kutenganishwa. Toleo Mishnah [RH 3.2] iliruhusu mnyama yoyote—kondoo, mbuzi au paa.)
4. "matarumbeta" (BDB 348) – yawezekana kutoka katika KITENZI VERB "kujinyoosha," ikimaanisha mfupa ulionyooka (sio pembe ya mnyama iliyojikunja). Hizi zilikuwa zimefanywa kwa shaba (baada ya uumbo na muundo wa Misri).
   Hizi zinatumika
   a. zikiwa na ibada za kuabudu (kama vile Hesabu. 10:2,8,10; Ezra 3:10; Neh. 12:35,41)
   b. kwa makusudi ya kijeshi (kama vile Hesabu. 10:9; 31:6; Hosea 5:8)
   c. kwa makusudi ya kifalme (kama vile II Wafalme. 11:14)

Moja ya hizi pembe za chuma zinachukuliwa na msaidizi wa Tito katika Rumi; pia Josephus akiwaelezea katika *Antiq*. 3.12.6.

◙**"kosa lao. . .dhambi zao"** Ibada rasmi zimekuwa mbadala wa haki binafsi. Zilikuwa za kidini lakini mbali na YHWH (kama vile II Tim. 3:5). Dini yawezakuwa kikwazo kwa imani binafsi ya kweli!

**58:2** Tambua namna imani ya uongo inavyoainishwa.

1. wanitafuta kila siku.
2. hupenda kujua njia zangu.
3. kama lilivyo taifa. . .wasivyoacha sheria za Mungu wao.
4. hutaka kwangu amri za haki.
5. hufurahi kumkaribia Mungu.

Haya yote yanaeleweka vizuri lakini lilikuwa ni onyesho, kichekesho, mchezo wa kidini; maneno, na sio matendo (kama vile. 29:13).

◙**"kama vile taifa waliotenda haki"** Hii ni kejeli.

◙**"hutaka kwangu amri za haki"** Hili linarejerea kwa

1. Urim and Thummin (yaani., kuhani mkuu, kama vile Kut. 28:30; Hes. 27:23; Kumb. 33:8; Neh. 7:65
2. manabii
3. Walawi wa mahali

**58:3 "tumefunga. . .tumejitaabisha nafsi zetu"** Neno "tumefunga" (*Qal* KAULI TIMILIFU, BDB 847, KB 1012) linafanana na neno "kujitaabisha" (*Piel* KAULI TIMILIFU, BDB 776, KB 853, kama vile Law. 6:29,31). Wanafikiri Mungu lazima ayabariki matendo yao ya dini. Agano la Kale lilikuwa na mfungo mmoja tu kwa mwaka (Mambo ya Walawi 16), siku ya kujutia makosa yao (kama vile mst. 6a). kipindi cha kukimbilia uhamishoni Wayahudi wakalizidisha hili kwa siku nne za mifungo ili kukumbukia matukio ya kuhuzunisha kipindi wakiwa katika taifa lao (yaani., kuanguka kwa Yerusalemu, kuharibiwa kwa hekalu, n.k., kama vile Zak. 7:3,5; 8:19).

◙**"siku ya kufunga kwenu mnatafuta anasa zenu wenyewe,**
**na kuwalemea wote watendao kazi kwenu"** Hufunga kwa ajili ya sababu za "kidini" na hawawezi kuwaruhusu wajakazi wao kupumzika ili nao washiriki! Madhara ya anguko yanaendelea!

**58:4** siku ya kwanza ya mfungo huleta maumivu na sio imani.

◙

**NASB "kupiga kwa ngumi ya uovu"**
**AB "kumpiga maskini kwa ngumi"**
**LXX "kumpiga mtu mnyenyekevu kwa ngumi yako"**

Toleo la MT lina kifungu "kumpiga kwa ngumi ya uovu," lakini tambua namna toleo la LXX linachukua dokezo toka mst wa 3c-d.

◙**"kuisikizisha sauti yenu juu"** Kusudi moja la kufunga lilikuwa ni kusaidiwa kwa maombi, lakini yalileta majibu tofauti (kama vile 1:15; 59:2).

**58:5** Hii ni orodha za alama za nje za kuomboleza, kama kuvaa nguo za magunia na kujipaka majivu, lakini katika uhalisia haya yalikuwa kwa ajili ya kujionesha tu (kama vile Mt. 6:5,16-18). Angalia Mada Maalum katika 47:1.

**58:6-7 "je? Saumu niliyoichagua sio ya namna hii"** Mungu anaorodhesha kile anachokihitaji toka kwa watu wake (yaani., haki ya kijamii ya kila siku, kama vile Kut. 21:2; Law. 25:39-41; Kumb. 15:12; na Yer. 34:8-11, ambayo hurejerea kwenye mwaka wa Yubilei; Tito 1:16).

1. kufungua vifungo vya uovu – *Piel* KITENZIJINA HALISI, BDB 834, KB 986
2. kulegeza kamba za nira – *Hiphil* KITENZIJINA HALISI, BDB 684, KB 736
3. kuwaacha huru walioonewa – *Piel* KITENZIJINA HALISI, BDB 1018, KB 1511
4. kuvunja kila nira – *Piel* KAULI TENDWA YA HALI YA KUENDELEA, BDB 954, KB 1285
5. kuwagawia wenye njaa chakula chako – *Qal* KITENZIJINA HALISI, BDB 828, KB 969
6. kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako – *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 97, KB 112, kama vile Mt. 25:35; Rum. 12:13; I Tim. 3:2; Tito 1:8; Ebr. 13:2; I Pet. 4:9
7. kuwavika nguo walio uchi – *Piel* KAULI TIMILIFU, BDB 491, KB 487, kama vile Yakobo 2:14-18
8. wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe – *Hithpael* KAULI TIMILIFU, BDB 761, KB 834, kama vile I Tim. 5:8

Hiki ni moja ya kigezo cha Masihi aliyetukuka kwa ajili ya kuwatenga kondoo (waamini waminifu) kutoka kwenye mbuzi (wasioamini watendao kiubinafsi) katika Mt. 25:31-46. Hii sio kazi ya kutenda haki, bali ni ushuhuda wa stadi ya maisha kuwa matokeo ya anguko (yaani., mtu mwenyewe) yamekwisha kugeuzwa (yaani., wengine).

**58:8-9b** Hii ni ahadi ya urejesho kama wakitubu na kuonyesha maisha ya imani. Tambua kile uaminifu wa kweli huleta.

1. nuru itapambazuka kama asubuhi
2. afya yako itatokea mara
3. haki yako itakutangulia
4. utukufu wa Bwana utakufuata na ukulinde
5. utaita na Bwana ataitika
6. utalia naye atasema "Mimi hapa" (kama vile 65:1)

Hiki ndicho Mungu alitaka kukifanya kwa watu wake, lakini dhambi zao na uasi wao ukasababisha hukumu na matengano!

◙**"na Bwana atakuongoza daima"** Hii inarejerea kwenye wingu la utukufu la*Shekinah* likiwa kama ulinzi wao kama ilivyokuwa wakati wa kuondoka kwao Misri (kama vile Kut. 14:19 na Isa. 52:12).

**58:9c-10 "kama"** Hii (kama vile mistari ya 9 na 10) inaonyesha kipengere chenye masharti cha uhusiano sawa wa kimaagano wa Mungu pamoja na watu wake. Tambua masharti.

1. ondoeni nira
2. wala kuonyosha kidole, kama vile Mit. 6:13
3. jizuie kunena maovu
4. mkunjulieni mtu mwenye njaa nafsi yako (*Hiphil* KAULI AMRISHI, BDB 807, KB 920)
5. ishibishe nafsi iliyoteswa

**58:9 "kunyoosha kidole"** Hii inarejerea kwenye maneno na ishara za uovu (kama vile Mith. 6:13).

**58:10c-12** Baraka za "baadaye" ni sehemu ya agano lenye masharti (kama vile Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 28-29) linavyodokeza.

1. nuru yako itapambazuka gizani
2. kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri
3. Bwana atakuongoza daima
4. ataishibisha nafsi yako
5. ataitia nguvu mifupa yako
6. utakuwa kama bustani iliyotiwa maji
7. kama chemichemi ambayo maji yake hayapungui
8. watu wako watapajenga mahali palipo na ukiwa
9. utaiinua misingi ya vizazi vingi
10. utaitwa mwenye kutengeneza mahali palipobomoka
11. mwenye kurejeza njia za kukalia

Manabii hutumia vyanzo mbalimbali vya taswira kuelezea uwepo wa YHWH na baraka.

1. nuru dhidi giza
2. sura ya mchungaji
3. Baraka za mashambani
4. taswira ya ujenzi

**58:11** Kuna masuala mawili ya kimaandiko katika mstari

1. mst. 11b

   **NASB "ataishibisha nafsi yako"**
   **NKJV "ataishibisha nafsi yako pasipokuwapo na maji**
   **TEV "ataishibisha nafsi yako na mambo mazuri"**
   **NJB "atayashibisha mahitaji yako mahali pakame"**
   **JPSOA "atakata kiu yako mahali pasipokuwepo maji"**
   **Peshitta "ataishibisha nafsi yako kwa chakula"**
   **LXX "utashibishwa kwa kadri ya nafsi yako"**

   Neno "shauku" ni *nephesh* (BDB 659) lina vidokezo vingi. "maeneo pasipopatikana maji" linapatikana hapa tu (BDB 850, KB 1019) na maana yake haijulikani.
2. mst. 11e

   Toleo la NASB, NKJV "sehemu ambapo maji yake hayakauki" KITENZI cha andiko la Kimasoreti (BDB 469, KB 467, *Piel* KAULI ISIO TIMILIFU) kinamaanisha "kutanda" au "." Maana yake inaonekana kuwa maji atoayo Mungu kamwe 'hayakomi' (yaani., mara zote hutiririka [NJB])

**58:12**
**NASB "mwenye kutengeneza mahali palipobomoka"**
**JPSOA "hutengeneza mahali pa makazi"**
**LXX "husababisha njia kati yao wapate pa kupumzika"**
**Peshitta "mwenye kutengeneza njia zilizobomoka"**
**REB "mwenye kutengeneza magofu yaliyo na ukiwa"**
Toleo la MT lina neno "njia" (BDB 677), yumkini liweze eleweka kama "Mahali pa kujengeka" kwa sababu ya KITENZI "kuishi" (*Qal* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, BDB 442, KB 444).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 58:13-14**
**[13] Kama ukigeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; [14] ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo.**

**58:13-14** Ubeti unatumia neno utii kwa hitaji la sabato kama njia ya kufahamu mwenendo wa mtu na uaminifu wake.

1. kugeuza miguu yako toka kwenye anasa zako, kuielekea sabato ya YHWH (kama vile mst. 13)
2. ukiita sabato kuwa “siku ya furaha” (KITENZI כבד,, BDB 457, KB 455, kimetumika mara mbili katika mst. 13) Tambua tena agano lenye masharti (“kama. . .hatimaye”). faida zake zimeorodheshwa katika mst. 14b,c.

**58:13 “Sabato”** Angalia Kutoka 20:8-11 na Isaya 56. Angalia Mada Maalum hapo chini.

## MADA MAALUM: SABATO

Hili linatokana na maana ya kiebrania "pumziko" au "kuacha kwa muda" (BDB 992). Linahusiana na siku ya saba ya uumbaji ambapo Mungu aliacha kazi zake baada ya kumaliza uumbaji wake wa mwanzo (kama vile Mwa. 2:1-3). Mungu hakupumzika kwa sababu alikuwa amechoka, lakini ni kwa sababu (1) uumbaji ulikuwa umekamilika na kuonekana unapendeza machoni pake (kama vile Mwa. 1:31) na (2) kumpa mwanadamu mwongozo kwa ajili ya ibada na pumziko. Utaratibu kama ilivyo siku ya kuabudu ulianzia Mwa. 2:2-3, ambapo YHWH alitumia pumziko lake kama utaratibu kwa ajili ya wanyama (kama vile Kut. 23:12) na mwanadamu (binadamu huhitaji utaratibu wa kila mara wa kazi, pumziko, na ibada). Sabato ilianza kama ilivyo siku zote za mwanzo 1, jioni; kwa hiyo, Ijumaa jioni mpaka Jumamosi jioni ulikuwa ni muda rasmi kwa ajili ya sabato. Maelezo yote juu ya kuishika sabato yametolewa katika kitabu cha Kutoka (hasa katika sura 16; 20; 31; na 35) na Mambo ya Walawi (hasa sura ya 23-26). Hasa utumiaji wa kwanza wa siku hii kwa Waisraeli ilikuwa ni katika Kut. 16:25-26 kwenye kusanyiko la manna. Baadaye ikajakuwa sehemu ya "amri kumi" (kama vile Kut. 20:8-11; Kumb. 5:12-15). Huu ni mfano mojawapo ambapo Amri Kumi katika Kutoka 20 kwa kiasi kidogo zimetofautiana na zile zilizoko katika Kumbukumbu la Torati 5. Zile za Kumbukumbu la Torati lilimwandaa Mwisraeli kwa ajili ya makazi, maisha ya kilimo huko Kanaani.

Mafarisayo walizichukua hizi taratibu na, kwa majadiliano yao ya kusimuliana, wakazitafasiri kwa namna ya kuzitumia kwenye sheria nyingi. Yesu mara nyingi alitenda miujiza, akijua wazi anakwenda kinyume na sheria zao ili kwamba waweze kuingia kwenye mjadala. Ilikuwa sio sabato aliyoikataa Yesu, bali kujihesabia kwao haki na kukosekana kwa upendo.

**58:14 “kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo”** Hili linaelezea uaminifu na nguvu ya ahadi za Mungu (kama vile Isa. 55:11)!

## MASWALA YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana

1. Nini tofauti kati ya imani ya kibiblia na ile ya kidini?
2. ni kwa namna gani maadili yanahusiana na thiolojia?
3. Nini kusudi la kufunga?
4. Nini kusudi la sabato? Je bado ina umuhimu katika siku za leo?

# ISAYA 59

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI YA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| kujitenga na Mungu za watu | Kujitenga na Mungu | Wito wa mataifa kutubu | Nabii alaani dhambi | Wimbo wa majuto |
| 59:1-8 | 59:1-3 | 59:1-8 | 59:1-3 | 59:1-4 |
| (1-8) | (1-3) | (1-8) | | (1-4) |
| | 59:4-5 | | 59:4-8 | |
| | (4-5) | | | |
| | | | | 59:5-8 |
| | | | | (5-8) |
| | 59:6-8 | | | |
| | (6-8) | | | |
| Kukiri makosa | Dhambi zinatubiwa | | Watu wanakiri dhambi zao | |
| 59:9-15a | 59:9-15a | 59:9-15a | 59:9-11 | 59:9-11 |
| (9-15a) | (9-15a) | (9-15a) | | (9-11) |
| | | | 59:12-15a | 59:12-15a |
| | Mwokozi wa Sayuni | | Bwana anajiandaa Kuokoa watu wake | |
| 59:15b-20 | 59:15b-19 | 59:15b-19 | 59:15b-21 | 59:15b-20 |
| (15b-20) | (15b-19) | (15b-19) | | |
| | 59:20 | 59:20 | | Unabii |
| | (20) | (20) | | |
| 59:21 | 59:21 | 59:21 | | 59:21 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

21. Aya ya kwanza
22. Aya ya pili
23. Aya ya tatu
24. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Ni kuona namna gani mashairi tofauti (yaani., sura) yanavyohusiana katika kipengere hiki cha Isaya. Nakubaliana na R. K. Harrison kuwa Isaya ni mkusanyiko wa mafundisho ya Isaya / mahubiri/ maandiko yaliyowekwa pamoja baada ya yeye kufa. Yameunganishwa kwa namna ya Kimashariki (kiinsha, namna ya kuyachezea maneno) na sio namna ya kimagharibi wa mpangilio wa matukio.

B. mtu hushangaa kuhusu hizi nabii.
   1. Ni utimilisho wa pamoja (yaani., 7:14; na Dan. 11:31; 12:11)?
   2. Je zinaelezea moyo wa Mungu na shauku kwa ajili ya Israeli, tukitambua kuwa hata pamoja na faida zote za agano (kama vile Rum. 9:4-5) zisingaliweza kutendeka?
   3. Je shairi/nabii zinatoka kwenye kipindi kingine cha huduma ya Isaya, zikielezea nyakati tofauti za historia ya Israeli, lakini sasa zikipangwa katika mpangilio ambao watu wa leo wasingaliuweza?

C. watafasiri wa kisasa lazima wakumbuke kuwa
   1. Huu ni ushairi, na sio simulizi za kihistoria
   2. Mashairi haya yanawasilishwa pasipo muundo maalum wa kihistoria
   3. Mengi ya maneno yake yanatumika mara moja tu katika Biblia au fasihi ya Kisemiti inayojulikana.
   4. Uwe mwangalifu na madai ya mafundisho ya kung'ang'aniza kutoka kwenye ushairi usiokamilika. Jaribu kuangalia
      a. Ufanano
      b. vifungu vinavyofanana hasa katika Isaya na Mika
      c. utumiaji wa Agano Jipya wa andiko/wazo (kama vile F. F. Bruce, *Answers To Questions*, kur. 87-88)

D. Toleo la Jewish Study Bible (uk. 901) linaiangalia sura hii katika sehemu tatu.
   1. Nabii akihubiri dhambi za watu (yaani., kwa pamoja)
   2. wale walio waaminifu katika taifa wakikiri dhambi zao (kibinafsi)
   3. Nabii akitangaza
      a. rehema za YHWH kwa wale waaminifu waliotubu (kama vile mistari. 20,21)
      b. hukumu kwa wenye kushupaza shingo zao
         1) Wayahudi
         2) Kwenye visiwa (yaani., watu wa mataifa)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA):59:1-8**
**1 Tazama, mkono wa Bwana haukupunguka, hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia;**
**2lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone,**
**hata hataki kusikia. 3Kwa maana mikono yenu imetiwa unajisi kwa damu, na vidole vyenu vimetiwa unajisi kwa**
**uovu; midomo yenu imenena uongo, ndimi zenu zimenong'ona ubaya. 4 Hapana adaiye kwa haki, wala hapana**
**atetaye kwa kweli; hutumainia ubatili, hunena uongo; hupata mimba ya madhara, na kuzaa uovu. 5Huangua**
**mayai ya fira, na kusuka wavu wa buibui; yeye alaye mayai yao hufa, na hilo livunjwalo hutoka nyoka. 6Nyavu**
**zao hazitakuwa mavazi, wala hawatajifunika kwa kazi zao; kazi zao ni kazi za uovu, na vitendo vya udhalimu**
**vimo mikononi mwao. 7Miguu yao hukimbilia mabaya, nao hufanya haraka kumwaga damu isiyo na hatia;**
**mawazo yao ni mawazo ya uovu; ukiwa na uharibifu zaonekana katika njia kuu zao. 8Njia ya amani hawaijui;**
**wala hapana hukumu ya haki katika miendo yao; wamejifanyizia njia zilizopotoka; kila apitaye katika njia hizo hajui amani.**

**59:1-2** Vifungu hivi vya ufunguzi kwa wazi vinaonyesha tatizo lililopo kwenye ahadi za Mungu kwa Israeli; hayakuwa maneno yake, tabia, au nguvu bali ni dhambi zao zenye kujirudia na zilizoendelea. mstari wa kwanza unaaksi jibu la nabii kwenye swali alilollisikia toka kwa Waisraeli wa siku zake (yaani., ziko wapi ahadi za Bwana?). Isaya anashuhudia malalamiko ya watu mara kadhaa (yaani., 40:27; 49:4,14).

**59:1 "mkono"** Mara nyingi hii ni nahau ya Kiebrania kwa ajili ya shughuli (kama vile 51:9). Angalia Mada Maalum katika 40:2.
tambua idadi ya sehemu za miili ya watu iliyotumika kuelezea Uungu (angalia Mada Maalum katika 41:2).
1. Mkono
2. Sikio

3. Uso

pia tambua ni kiasi gani sehemu za mwili wa mtu zilivyoelezea uovu wa mwanadamu.

1. mikono , mst 3
2. vidole , mst. 3
3. Midomo , mst 3
4. ulimi, mst. 3
5. Miguu iliyodokezwa katika mst. 8

**59:2 "lisiweze kusikia"** Neno hili (BDB 457, KB 455, *Qal* KAULI TIMILIFU) linamaanisha"kuwa mzito," "kuelemewa na mzigo," au"kuheshimiwa." Katika muktadha huu linarejelea kutokuweza sikia. Linatumika kwa namna ile ile kama yalivyo "macho" katika Mwa. 48:10 na "moyo" wa Farao katika Kut. 9:7.

◙**"maovu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu"** KITENZI (BDB 95, KB 110, *Hiphil* KAULI ENDELEVU) kimetumika katika maana mbalimbali.

1. Mungu akitenga nuru na giza katika Mwa. 1:4
2. Mungu akiwatenga Israeli mbali na watu wengine
3. Kufanya utofauti kati ya kilicho safi na kisich safi
4. Kugawanya kimafungu (yaani., kutoa dhabihu)
5. YHWH na Musawakiwatenga Walawi (hasa Haruni, I Nya. 23:13)
6. Kumwondoa mtu toka Israeli (kama vile Kumb. 29:30)
7. Kuwajumuisha wageni (kama vile Neh. 13:3)
8. Kuwaweka akiba wanamuziki
9. Mtu kujitenga toka kwa wageni na wapagani kwenye jamii moja (kama vile Ezra 6:21; 9:1; 10:11; Neh. 9:2)
10. kujitenga toka kwa kiongozi (yaani., Daudi, I Nya. 12:8) katika muktadha huu linatumika kwa maana ya kipekee. Dhambi za Israeli kihisia na kiroho ziliwatenga watu wa agano toka kwenye agano la Mungu na uwepo Wake, ahadi, na ulinzi!njia moja kuielezea hali hii mbaya ya kiroho ni ule mstari sambamba unaofuata wa ushairi. Mungu akauficha uso wake kwao (yaani., ili asisikie maombi yao)!

**59:3-8** Mistari hii inaorodhesha (katika mistari yenye kufanana) dhambi za Israeli zilizosababisha matengano.

1. Mikono yenu imetiwa unajisi kwa damu, mst. 3
2. Midomo yenu imenena uongo, mst. 3
3. Hakuna adaiye kwa haki, v. 4 (tambua VITENZIJINZ HALISI vinne)
4. Hupanga uovu na kumwaga damu, mistari ya 5-7 (kama vile Ayubu 8:14-15; 15:35; Mith. 1:16; kwa ajili ya mst. 7 angalia Rum. 3:15-17)
5. Hawaijui njia ya amani (kama vile 26:3,12; 57:20-21; Luka 1:79) au haki, mst. 8 (tambua VITENZI TIMILIFU)

**59:4** Mstari wa 4, kama ulivyo mst. 13, hutumia VITENZIJINA HALISI kuelezea tabia za uovu wa mwanadamu.

1. Hutumaini ubatili, *Qal*. BDB 105, KB 120
2. Hunena uongo, *Piel*, BDB 180, KB 210
3. Hupata mimba ya madhara, *Qal*, BDB 247, KB 255 (kama vile Ayubu 15:35)
4. Huzaa uovu, *Hiphil* BDB 408, KB 411

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):59:9-20**
**9 Kwa sababu hiyo hukumu ya haki i mbali nasi,**
**wala haki haitufikilii; twatazamia nuru,**
**na kumbe! Latokea giza; twatazamia mwanga,**
**lakini twaenda katika giza kuu.**
**10 Twapapasa-papasa kutafuta ukuta kama kipofu,**
**naam, twapapasa kama watu wasio na macho;**
**twajikwaa wakati wa adhuhuri,**

**kana kwamba ni wakati wa ukungu wa alfajiri;**
**kati yao waliowanda tumekuwa kama wafu.**
**11Sisi sote twanguruma kama dubu;**
**twaomboleza kama hua;**
**twatazamia hukumu ya haki,**
**lakini hapana; na wokovu, lakini u mbali nasi.**
**12Maana makosa yetu yamezidi kuwa mengi mbele zako,**
**na dhambi zetu zashuhudia juu yetu;**
**maana makosa yetu tunayo pamoja nasi,**
**na maovu yetu tumeyajua;**
**13katika kukosa na kumkana Bwana,**
**na katika kugeuka tusimfuate Mungu wetu,**
**tukinena jeuri na uasi,**
**na kukusudia maneno ya uongo na kuyatoa moyoni.**
**14Na hukumu imegeuka ikaenda nyuma,**
**na haki inasimama mbali sana;**
**maana kweli imeanguka katika njia kuu,**
**na unyofu hauwezi kuingia.**
**15Naam, kweli imepunguka kabisa,**
**na yeye auachaye uovu ajifanya kuwa mateka;**
**naye Bwana akaona hayo,**
**akachukizwa kwa kuwa hapana hukumu ya haki.**
**16Akaona ya kuwa hapana mtu,**
**akastaajabu kwa kuwa hapana mwombezi;**
**basi, mkono wake mwenyewe ndio uliomletea wokovu;**
**na haki yake ndiyo iliyomsaidia.**
**17 Akajivika haki kama deraya kifuani,**
**na chapeo cha wokovu kichwani pake,**
**akajivika mavazi ya kisasi yawe mavazi yake, naye alivikwa wivu kama joho.**
**18Kadiri ya matendo yao, kwa kadiri iyo hiyo atawalipa,**
**ukali kwao wampingao, malipo kwa adui zake;**
**naye atavirudishia visiwa malipo.**
**19 Basi, wataliogopa jina la Bwana toka magharibi,**
**na utukufu wake toka maawio ya jua;**
**maana yeye atakuja kama mkondo wa mto ufurikao,**
**uendeshwao kwa pumzi ya Bwana.**
**20Na Mkombozi atakuja Sayuni,**
**kwao waachao maasi yao katika Yakobo, asema Bwana.**

**59:9-11** Mistari hii inaelezea matokeo ya dhambi za Israeli (kur. 3-8).

1. hukumu ya haki I mbali nasi
2. Wala haki haitufikilii
3. Twatazamia nuru, kumbe, kwatokea giza
4. twatazamia mwanga, lakini twatembea katika giza kuu
5. twapapasa-papasa kutafuta ukuta kama vipofu (BDB 178, KB 206, *Piel* KAULI YENYE KUSIHI, mara mbili, kama vile Kumb.28:29; Yer. 13:16; Amos 5:18,20)
6. Twaunguruma kama dubu
7. Twaomboleza kama hua
8. Twatarajia hukumu ya haki, lakini hapana
9. Twatarajia wokovu, lakini u mbali nasi

Mstari wa 6 ni stiari, na unapatikana hapa tu katika Agano la Kale. Toleo laTEV huutafasiri (ufafanuzi) na mstari unaofuata kama "tumetishwa na kuogopeshwa." Tanbihi ya toleo la NASB Study Bible linauainisha kama "asiye mvumilivu na kukatisha tamaa."Stiari ya mstari wa 7 inapatikana katika 38:14; Ezek. 7:16; na Nahum 2:7.

**59:12** Mstari wa 12 unaelezea hali ya kiroho ya sasa.

1. Makosa ya Israeli yanaongezeka mbele ya YHWH
2. Dhambi za Israeli zinawashuhudia juu yao
3. Makosa ya Israeli wanayo pamoja nayo
4. Israeli wanazijua dhambi zao

Tambua kuwa Isaya, kama alivyo Ezra, anakiri dhambi ya jamii nzima ya watu wa Agano (kama vile Ezra 9:6-7). hiki ndicho kuhani mkuu hufanya siku ya upatanisho (kama vile Mambo ya Walawi 16). Makosa ya pamoja hugharimu, kama ilivyo dhambi binafsi na na madhara yake!

**59:13** Mstari wa 13 unaelezea dhambi.

1. kumkosa – BDB 833, KB 981, *Qal* KITENZIJINA HALISI
2. Kumkana Bwana – BDB 471, KB 469, *Piel* KITENZIJINA HALISI
3. Wakigeukia mbali na Mungu – BDB 690, KB 744, *Niphal* KITENZIJINA HALISI
4. Wakinena jeuri na uasi – BDB 180, KB 210, *Piel* KITENZIJINA HALISI
5. wakikusudia maneno ya uongo mioyoni mwao – BDB 247, KB 255, *Poel* KITENZIJINA HALISI
6. Wakinena maneno ya uongo toka mioyoni mwao – BDB 211, KB 237, *Poel* KITENZIJINA HALISI

Tambua ni namna gani mwandishi kisanii anatumia KITENZIJINA HALISI katika mistari ya 4 na 13! Kizazi cha Ibrahimu kisicho na imani kinaonyesha mwelekeo wao wa kweli (yaani., wao wenyewe) kwa stadi yao ya maisha (kama vile Tito 1:16). Wanazungumza kuhusu YHWH lakini wanaishi kwa ajili yao wenyewe (kama vile 6:9-10; 29:13).

**59:14-15a** Matokeo ni yapi kwa huu uasi wa kiroho wa kimakusudi?

1. Haki imegeuka ikaenda nyuma
2. Haki inasimama mbali sana
3. kweli imeanguka katika njia kuu
4. Unyoofu hauwezi kuingia
5. ukweli unakosekana

zingatia uwasilishaji! Yule anayejaribu kuwa haki ndiyo mlengwa na mhanga kwa ajili ya dhambi!

**59:15b-16b** Israeli, watu wa agano, ilikuwa ni namna ya YHWH ya kujidhihirisha Mwenyewe ulimwenguni. Kwa masikitiko makubwa wameshindwa.

1. matendo na mienendo yao haifurahishi
2. Hapana hukumu ya haki
3. hakuna mwenye haki hata mmoja
4. Hapana mwombezi (kama vile Ezek. 22:30). kwa hiyo, YHWH lazima atende Mwenyewe. Hili kithiolojia linafanana na Ezek. 36:22-38, lenye kuelezea "agano jipya" la Yer. 31:31-34.

Zingatia kuwa nabii huzungumza kuhusu YHWH katika mistari ya 15b-20. YHWH huzungumza kwa ajili yake Mwenyewe katika mst. 21.

**59:16d** katika mtizamo wa uweza wa mwanadamu aliyeanguka (hata agano la mwanadamu) YHWH huchagua kutenda.

1. Mkono wake Mwenyewe humletea wokovu, kama vile 52:10; 63:5
2. Na haki yake ndiyo iliyomsaidia

Ni nani azungumzwaye "Yeye"? katika muktadha angewezakuwa Mtumishi Ateswaye (yaani., Masihi) au nabii wa YHWH (yaani.,Isaya).

**59:17** YHWH anaelezewa kama "mpiganaji" mwenye kujiandaa kwa ajili ya vita. Andiko hili ni historia ya nyuma ya agano la kale kwa ajili utumiaji wa Paulo wa taswira za kivita katika Efe. 6:10-17.

1. Akajivika haki kama deraya kifuani
2. Akajivika chepeo cha wokovu
3. Akajivika mavazi ya kisasi
4. Akavikwa wivu kama joho

**59:18 "kadiri ya matendo yao, kwa kadiri iyo hiyo atawalipa"** Hii ni kweli inayojirudia katika maandiko.

1. Ayubu 34:11
2. Zaburi 28:4; 62:12
3. Mithali 24:12
4. Mhubiri 12:14
5. Yeremia 17:10; 32:19
6. Mathayo 16:27; 25:31-46
7. Warumi 2:6; 14:12
8. I Wakorintho 3:8; II Wakorintho 5:10
9. Wagalatia 6:7-10
10. II Timotheo 4:14
11. I Petro 1:17
12. Ufunuo 2:23; 20:12; 22:12

Wanadamu wote huvuna kile wanachopanda! Kuna gharama ya kuchagua na matendo yanayotufuata muda wote. Ashukuliwe Mungu kwa msamaha wa Kiungu na kuyasahau yote!

◙**"visiwa"** Neno hili (BDB 15 I) linatumika mara nyingi katika sehemu hii ya Isaya (kama vile 40:15; 41:1,5; 42:4,10,12,15; 49:1; 51:5; 59:18; 60:9; 66:19. Linatumika mara nyingi katika maana ya mataifa mengine au mataifa yasiyo ya Wayahudi.

**59:19-20** Kusudi la Mungu kufanya malipizo (BDB 168) ni kwa ajili ya ukombozi (yaani., litiini jina la Bwana). Mwokozi (kama vile 41:14; 43:1; 44:22) atatoka Israeli (yaani., Masihi). anakuja kwa wale wote wanaotaka "kurudi" (BDB 996, KB1427, *Qal* KAULI ENDELEVU, angalia mada maalum katika 44:22). katika Agano Jipya muktadha unaoshughulika na kutokuamini kwa Wayahudi na uasi ni Warumi 9-11. Paulo hutumia mst. 20 katika 11:26-27. Nafikiri kuwa Rum. 3:21-31; 9-10; Wagalatia 3; na kitabu cha Waebrania ni vyenye maandiko mazuri katika Agano Jipya kuelewa namna gani Agano la Kale na Agano Jipya yametofautiana na kuungana tena!

**59:19 "jina la Bwana"** Angalia Mada Maalum katika 52:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):59:21**

**21 Tena katika habari zangu, hili ndilo agano langu nao, asema Bwana; roho yangu iliyo juu yako, na maneno yangu niliyoyatia kinywani mwako, hayataondoka kinywani mwako, wala kinywani mwa wana wako, wala kinywani mwa wajukuu wako, asema Bwana, tangu leo na hata milele.**

**59:21** YHWH anawaambia ("kwa ajili Yangu") Israeli (au kizazi cha imani ya kiroho ya Ibrahimu, kama vile Rum. 2:28-29;9:6; Gal. 6:16). Aliahidi

1. Roho wake
2. Ufunuo wake
3. Mamlaka yake kwa vizazi

◙**"toka sasa na hata milele"** Angalia Mada Maalum katika 45:17. Moja ya kitabu nikipendacho juu ya kuutafasiri unabii ni cha D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*. Amekuwa na mjadala mzuri wa matumizi ya kiistiari ya neno "milele," angalia kur. 99-101. Anaelezea kuwa mara nyingi "linasaidia kuimalisha kitenzi kinachobadilishwa.

# ISAYA 60

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Sayuni iliyotukuzwa | Watu wa mataifa Waibariki Sayuni | Kuurejesha utukufu wa Yerusalemu | Utukufu ujao wa Yerusalemu | Uzuri wa Yerusalemu |
| 60:1-3 (1-3) | 60:1-3 (1-3) | 60:1-3 | 60:1-3 (1-3) | 60:1-11 (1-11) |
| 60:4-9 (4-9) | 60:4-7 (4-7) | 60:4-16 (4-16) | 60:4-5 (4-5) | |
| | | | 60:6-7 (6-7) | |
| | 60:8-9 (8-9) | | 60:8-9 (8-9) | |
| 60:10-14 (10-14) | 60:10-12 (10-12) | | 60:10-12 (10-12) | |
| | | | | 60:12 (12) |
| | 60:13-14 (13-14) | | 60:13-14 (13-14) | 60:13-18 (13-18) |
| 60:15-22 (15-22) | 60:15-16 (15-16) | | 60:15-16 (15-16) | |
| | 60:17-18 (17-18) | 60:17-22 (17-22) | 60:17-18 (17-18) | |
| | Mungu Mtukufu Kwa watu wake | | | |
| | 60:19-22 (19-22) | | 60:19-22 (19-22) | 60:19-22 (19-22) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. Xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozokwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Ayaya kwanza
2. Ayayapili
3. Ayatatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kuna mabadiliko makubwa kwenye mazingira ya sura ya 59 na sura ya 60-62.
B. Sura ya 60-62 inaunda kipengere kinachoshughulika na utukufu ujao wa watu wa Mungu kama ulivyoonekana kwenye urejesho wa Yerusalemu.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 60:1-3**
**1 Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja, Na utukufu wa Bwana umekuzukia. 2Maana, tazama, giza litaifunika dunia, Na giza kuu litazifunika kabila za watu; Bali Bwana atakuzukia wewe, Na utukufu wake utaonekana juu yako. 3Na mataifa wataijilia nuru yako, Na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako.**

**60:1 "Ondoka, na uangaze"** Kauli mbili*Qal* SHURUTISHI zinawasihi watu wa agano la Mungu kuwa kama walivyoitwa kuwa kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya ulimwengu. Nuru ni stiari yenye kujirudia katika sura hii kuelezea:
1. Uwepo wa Mungu, 60:1,2,9-20; Ufu. 21:23; 22:5
2. Utakatifu wa kiroho, 60:1,3,5,21; 62:1
3. Stiari yenye kujirudia ya nuru katika Isaya (kama vile 9:2; 58:8; 59:9)

◙**"kwa kuwa nuru yako imekuja"** Mada ya mistari ya 1-22 ni kuhusu "Sayuni" (kama vile mst. 14), ikimaanisha watu wa Mungu. KITENZI kilichozoeleka cha neno "imekuja" (BDB 97, KB 112) kinatumika mara nyingi katika sura hii.
1. imekuja – *Qal* KAULI TIMILIFU, mst. 1
2. inakuja – *Qal* KAULI TIMILIFU, mst. 4
3. itakuja – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, mst. 4
4. itakuja – *Qal* KAULI ISIO TIMLIFU, mst. 5
5. itakuja – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, mst. 6
6. itakuja – *Hiphil* KITENZIJINA CHA MUUNDO WA MANENO, mst. 9
7. imeleta – kama ile ya #6, mst. 11
8. itakuja – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, mst. 13

9-10. italeta – *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU, mara mbili, mst. 17
11. ataweka – *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, mst. 20

Kumbuka kipengere cha muda hakiko katika KITENZI cha Kiebrania lakini kimetumika katika muktadha huu.

◙**"utukufu wa Bwana"** Hili linafanana na lile la "nuru" katika mstari wa 1. Limetumika katika sehemu zingine katika Isaya likihusianishwa na nuru (kama vile 24:23; 58:8) na utele wa kustawi mazao ya kilimo (kama vile 35:2). Neno la Kiebrania kwa ajili ya "utukufu" (BDB 458), kwa sababu ya uhusiano wake na wingu la utukufu *Shekinah* (kama vile Kut. 13:21-22; 14:19,20,24; 19:16-18; 20:21), linamaanisha uwepo binafsi wa YHWH ukiwa na Waisraeli kipindi cha kutoka Misri. Moto na mianga ya radi zilihusianishwa na ujio wa YHWH katika Mlima Sinai (kama vile Kutoka 19-20), kwa hiyo mwanga ukajakuwa ni dhana ya "utukufu."

**60:2** Hili lina baadhi ya dokezo la lile giza halisi la Mwa. 1:1-2 au Kut. 10:21-23 au hata 9:1, na giza la kiroho linalosababishwa na dhambi. YHWH hataruhusu lile giza la anguko (kama vile Mwanzo 3), ambalo huwafunika wanadamu, wabakiao. Nuru yake ya ufunuo na wokovu itawaangazia (*Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 280, KB 281).

**60:3 "Mataifa wataijilia nuru yako"** Ni dhahili kuwa kusudi la mwanzo la Mungu kwa ajili ya Israeli lilikuwa ni kuuvuta ulimwengu wote kwake (kama vile 61:6,11b; 62:2,11; Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6). Angalia Mada Maalum katika 40:15. Katika manabii wote, isipokuwa Mika na Yona, ni Isaya tu aliyeona madokezo ya ulimwengu juu ya

1. Imani ya Mungu mmoja
2. ahadi za agano la Kale juu ya wazee wa imani
3. kusudi la Israeli juu ya uinjilisti

Kumbuka 2:3; 45:14,22-25; 49:23. Hakika huyu ni mjumbe wa Yohana 3:16; I Tim. 2:4; II Pet 3:9. Agano Jipya, likifuatiwa na mafundisho ya Yesu, linajumuisha ahadi za Agano la Kale kwa Israeli, kwa ulimwengu mzima (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 60:4-9**
**[4]Inua macho yako, utazame pande zote; Wote wanakusanyana; wanakujia wewe; Wana wako watakuja kutoka mbali. Na binti zako watabebwa nyongani. [5]Ndipo utakapoona na kutiwa nuru, Na moyo wako utatetemeka na kukunjuka; Kwa kuwa wingi wa bahari utageuzwa kukujia, Utajiri wa mataifa utakuwasilia. [6]Wingi wa ngamia utakufunika, Ngamia vijana wa Midiani na Efa; Wote watakuja kutoka Sheba; Wataleta dhahabu na uvumba; Na kuzitangaza sifa za Bwana. [7]Makundi yote ya Kedari yatakusanyika kwako, Kondoo waume wa Nebayothi watakutumikia; Watapanda juu ya madhabahu yangu kwa kibali, Nami nitaitukuza nyumba ya utukufu wangu. [8]Ni nani hawa warukao kama wingu, Na kama njiwa waendao madirishani kwao? [9]Hakika yake visiwa vitaningojea, Na merikebu za Tarshishi kwanza, Ili kuleta wana wako kutoka mbali, Na fedha yao na dhahabu yao pamoja nao, Kwa ajili ya jina la Bwana, Mungu wako, Kwa ajili yake Mtakatifu wa Israeli, Kwa kuwa amekutukuza wewe.**

**60:4 "inua macho yako. . .utazame"** Hizi ni kauli mbili*Qal* SHURUTISHI (kama vile 49:18; Yohana 4:35). KAULI SHURUTISHI mara nyingi huanza na ubeti mpya.

◙**"wana wako watakuja toka mbali"** Katika sura ya 60-62, kuna alama mbili kubwa juu ya matukio ya siku ya mwisho yanayoshughulika na kusafiri.

1. watu wa Mungu watarudi kwenye makazi yao ya zamani ya baba zao, ikimaanisha mji wa Yerusalemu
2. mataifa, badala ya kuwachukua Wayahudi waliokuwa mateka na kuwafukuza, watawaajilia watu wa Mungu kwa zawadi na nyimbo za sifa

**60:5** Kwa maaana hiyo ya watu wa Mungu waliokwishatubu "wataona" (*Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 906, KB 1157), tambua matokeo yaliyokwisha kuelezewa ya kuona nuru ya Mungu (kama vile mistari ya 1,4,19,20).

1. kutiwa nuru – *Qal* KAULI TIMILIFU, BDB 626, KB 676
2. sisimka (kifasihi kutetemeka) – *Qal* KAULI TIMILIFU, BDB 808, KB 922
3. kufurahia – *Qal* KAULI TIMILIFU, BDB 931, KB 1210

Sababu kwa ajili ya hili tumaini na furaha ni matendo yenye utukufu ya Mungu.

1. kwa wingi wa bahari utageuka kuwa wako (yaani., utajiri wa watu wanao safari baharini)
2. utajiri wa mataifa utakujilia (kama vile mistari 6-7,11; 61:6)

Mistari inayofanana ya ushairi unaelezea shukrani ya mataifa kwa ajili Israeli

1. kumdhihirisha YHWH
2. kuleta uhalisia wa uwepo wa YHWH duniani
3. kufungua njia kwa ajili ya kuwajumuisha watu wa Mungu wa agano (kama vile 56:7)

**60:6 "wataleta dhahabu na uvumba na kuzitangaza sifa za Bwana"** KITENZI (*Piel* KAULI ISO TIMILIFU, BDB 142, KB 163) kinarejerea kwenye rehema ya Mungu kwa Israeli na kwa mataifa yote (kama vile 40:9-10; 41:27; 42:10-13; 52:7). Je, haishangazi kusikia mataifa ya kipagani yakimsifu Mungu wa Israeli? Huu ni mpango wa wazi wa kithiolojia wa imani ya Mungu mmoja (angalia Mada Maalum katika 40:14). Kuna Mungu mmoja na watu wote wameumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwa. 1:26-27) kwa ajili ya kuwa na ushirika naye (maana ya Mwa. 3:8; Law. 26:12). Ahadi ya Mwa. 3:15 kwa wanadamu wote na tumaini la Baraka za agano kwa watu wa dunia hii katika

Mwa. 12:3 limekwisha timizwa.

**60:7 "Nabayothi"** Hili linarejerea makabila ya Uarabuni, kama kisemavyo kifungu, "makundi yote ya Kedari," yatakusanyika kwako. Kabila hili limetajwea katika Mwa. 25:13. wanaitwa Nabateans kwa lugha ya Kiyunani na Kirumi.

**60:8 "Ni nani hawa warukao kama wingu,**
**Na kama njiwa waendao madirishani kwao"** Hii inarejerea kwenye safari za merikebu ziendazo zaidi ya upeo wa macho kuelekea Yerusalemu mpya iliyorejeshwa (kama vile mst. 9).

**60:9 "Hkika yake visiwa vitaningojea"** Neno "uwanda wa pwani" (au "visiwa") linatumika katika kipengere hiki cha Isaya kama stiari kwa ajili ya watu wa mataifa. KITENZI "watangojea" (*Piel* KAULI ISIO TIMILIFU, BDB 875, KB 1082) mara nyingi kinatumika kwa ajili ya kuamini katika YHWH (kama vile 8:17; 25:9; 26:8; 33:2). Tambua namna kinavyotumika kwa ajili ya YHWH katika 30:18!

◙**"merikebu za Tarshishi"** Tarshishi yaweza kurejerea
1. sehemu ya kusini mwa Hispania
2. Sardinia
3. matumizi ya kimethali kuonyesha miisho ya dunia

◙ Tambua majina ya agano ya Uungu (pia angalia mistari ya 14,16).
1. YHWH (Mungu kama mwokozi na mkombozi)
2. *Elohim* (Mungu kama muumbaji na mtoaji)
3. Yeye aliye Mtakatifu wa Israeli (Mungu wa agano) angalia Mada Maalum katika 40:3.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):60:10-14**
**[10]Na wageni watajenga kuta zako, Na wafalme wao watakuhudumu; Maana katika ghadhabu yangu nalikupiga, Lakini katika upendeleo wangu nimekurehemu. [11]Malango yako nayo yatakuwa wazi daima; Hayatafungwa mchana wala usiku; Ili watu wapate kukuletea utajiri wa mataifa, Na wafalme wao wakiongozwa pamoja nao. [12]Kwa maana kila taifa na ufalme wa watu Wasiotaka kukutumikia wataangamia; Naam, mataifa hayo wataharibiwa kabisa. [13]Utukufu wa Lebanoni utakujia wewe, Mberoshi na mtidhari na mteashuri pamoja; Ili kupapamba mahali pangu patakatifu, Nami nitapatukuza mahali pa miguu yangu. [14]Na wana wa watu wale waliokutesa Watakuja kwako na kukuinamia; Nao wote waliokudharau Watajiinamisha hata nyayo za miguu yako; Nao watakuita, Mji wa Bwana, Sayuni wa Mtakatifu wa Israeli.**

**60:10 "katika ghadhabu yangu nalikupiga,**
**lakini katika upendeleo wangu nalikurehemu"** Hapa tunaona vipengere viwili muhimu juu ya YHWH katika Biblia: Rehema yake (kipindi kirefu, kama vile Zab. 103:10-14) na ghadhabu yake (kipindi kifupi, kama vile 57:16; Zab. 103:9). Hukumu yake ni ya kiasili ni ya kimalezi na humaanisha kuusababisha uumbaji wake kumrejea kuja kwake (kama vile Warumi 1-3; Ebr. 12:1-13).

**60:11 "Na malango yako nayo yatakuwa wazi daima"** Hiki kifungu kinatumika kuonyesha (1) uhakika wa ulinzi (2) upatikanaji wa wa uhakika (kama vile Ufu. 21:25).

**60:12 "kila taifa na ufalme usiotaka kukutumikia utaangamia"** Onyo hili linafanana na agano la Mungu kwa Ibrahimu katika Mwa. 12:3 (kama vile 27:29).

**60:13** Aya hii inazungumuzia juu ya ujenzi wa mahali patakatifu papya (yaani hekalu.,) pakiwa na miti mizuri kama ya Lebanoni.

◙**"mahali pangu patakatifu;**
**name nitapatukuza mahali pa miguu yangu"** Sanduku la Agano na mahali patakatifu pa patakatifu panamaanisha uwepo wa Mungu juu ya dunia. Wayahudi wanalifikiria eneo hilo ni kati ya mbawa za makerubi kama mahali pa kuweka miguu ya Mungu (kama vile Zab. 99:5; 132:7); kiti chake cha Enzi kiko mbinguni.

**60:14 "Sayuni"** Neno "Sayuni" (BDB 851) ni kisawe cha mji wa Yerusalemu. Hekalu lilijengwa juu ya Mlima Moria, lakini mji mara chache ulirejerewa kwa neno hili (kama vile 62:1).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):60:15-22**
**[15]Na kwa kuwa umeachwa na kuchukiwa, Hata ikawa hapana mtu aliyepita ndani yako, Nitakufanya kuwa fahari ya milele, Furaha ya vizazi vingi. [16]Utanyonya maziwa ya mataifa, Utanyonya matiti ya wafalme; Nawe utajua ya kuwa mimi, Bwana, ni mwokozi wako, Na mkombozi wako, Mwenye enzi wa Yakobo. [17]Badala ya shaba nitaleta dhahabu, Na badala; ya chuma nitaleta fedha, Na badala ya mti, shaba, Na badala ya mawe, chuma; Tena nitawafanya wasimamizi wako wawe amani, Na hao wakutozao fedha kuwa haki. [18]Jeuri haitasikiwa tena katika nchi yako, Ukiwa na uharibifu hazitakuwa mipakani mwako; Bali utaziita kuta zako, Wokovu, Na malango yako, Sifa. [19]Jua halitakuwa nuru yako tena wakati wa mchana, Wala mwezi hautakupa nuru kwa mwangaza wake; Bali Bwana atakuwa nuru ya milele kwako, Na Mungu wako atakuwa utukufu wako. [20]Jua lako halitashuka tena, Wala mwezi wako hautajitenga; Kwa kuwa Bwana mwenyewe atakuwa nuru yako ya milele; Na siku za kuomboleza kwako zitakoma. [21]Watu wako nao watakuwa wenye haki wote, Nao watairithi nchi milele; [22]Mdogo atakuwa elfu, Na mnyonge atakuwa taifa hodari; Mimi, Bwana, nitayahimiza hayo wakati wake**.

**60:15-22** Sura hii inafanana na na ile ya Ufu. 21:1-27, ambayo inaelezea "Yerusalemu mpya." Pamekuwepo na maoni mawili makuu juu ya uhusiano wa ahadi za agano la Kale kuelekea agano Jipya:

1. Yanamaanisha kuchukuliwa kifasihi na Yerusalemu itajengwa upya ikiwa na hekalu la kutolea dhabihu katikati, yaani., mgawanyo baada ya miaka elfu moja.
2. Sura hizi ni alama za kanisa na umuhimu wake unaonekana katika agano jipya kama watu wapya wa Mungu, yaani., miaka elfu moja. Utata wa aina ile ile waweza kuonekana katika 61:6, ambapo Israeli inarejerewa kama "ufalme wa makuhani" (kama vile Kutoka. 19:6). Lakini maneno yale yale yanatumika katika I Pet. 2:5,9 na Ufu. 1:6 kuelezea kanisa. Kusudi la Israeli siku zote limekuwepo kuuleta ulimwengu kwa Mungu (kama vile 62:2,11; angalia Mada Maalum katika 40:15). Hata hivyo, walishindwa na Mungu

kuamua kulichagua kanisa kutimiliza kazi hii. Angalia Mada Maalum katika 40:9!

**60:15 "kwa kuwa umeachwa na kuchukiwa"** Kifungu hiki ni lahaja ya Kiebrania inayohusiana na mambo ya ndoa. Tunaweza kuliona hili katika maneno yanayoelezea "Lea" katika Mwa. 29:21 na kuendelea. Nahau ile ile kuhusu mambo ya ndoa inaendelea katika 62:4-5 na katika Agano Jipya kama ilivyo kanisa katika Efe. 5:21-31. "chuki" ni lahaja ya Kiebrania kwa ajili ya kulinganisha.

**60:17** Yumkini hili ni dokezo kwa I Fal. 14:26-27 likihusiana na uwekaji pamoja wa madini ya chuma toka hekaluni kwa ajili ya kulipia kodi kwa nchi ya Misri.

◙**"Nitakufanya fahari ya milele,**
**na furaha ya vizazi vingi"** Hili linaweza kuaksi serikali ya Kimasihi iliyotajwa katika sura ya 7-14.

**60:18** Unabii huu hakika hautumiki kwenye historia ya Israeli iliyofanikiwa! Hii inaonekana kuonyesha kutokuwepo kwa magomvi ya kijamii na matatizo katika Enzi ya Kimasihi.

**60:19-20** Yohana anaitumia hii taswira katika Ufu. 21:23; 22:5. Uwepo wa YHWH ni nuru halisi!

**60:20 "na siku za kuomboleza kwako zitakoma"** Siku mpya/itachomoza, kama vile Isa. 35:10; 65:19; Ufu. 21:4.

**60:21 “watu wako nao watakuwa wenye haki”** Baraka za Mungu zitawaijilia pale tu watu watakapotubu (angalia Mada Maalum katika 44:22). Yeye, Mwenyewe, atawapa moyo mpya na fikra mpya (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38). Aina hii ya ahadi ndio chanzo cha mjadala wa kithiolojia juu ya ukuu na mapenzi huru. Je mwanadamu aliyeanguka aweza kufanya chochote dhidi ya wokovu wao au kila kitu (yaani., imani, toba) zawadi toka kwa Mungu (kama vile Mdo. 5:31; 11:18; II Tim. 2:25). Maandiko mengine yanaelekeza kwenye mahubiri yanayovuta watu kwenye toba (yaani., wajibu wa mapenzi huru kwenye zawadi ya Kiungu,kama vile Mt. 3:8; Luka 3:8; Yohana 1:12; Mdo. 2:38;). Kwa kiasi Fulani yote ni ya Kibiblia! Hili ndilo tatizo la Kimagharibi dhidi ya mkanganyiko wa Kimashariki!

◙**“Nao watairithi nchi milele”** Hili laweza kuwa dokezo kwa Mwa. 17:8. Neno “milele” ni tatizo la kiutafasiri. Angalia Mada Maalum katika 45:17.

◙**“Tawi la mapando yangu”** Hii stiari ya aina ile ile imetumika katika 61:3. Inaonekana kuaksi Zaburi 1, lakini pia inaonekana katika Isa. 11:1. Agano la Kale linatumia stiari nyingi za kilimo.

**60:22 “taifa”** Hili neno laweza kumaanisha “maelfu.” Angalia Mada Maalum hapo chini.

## MADA MAALUM: ELFU (*ELEPH)*

Neno la Kiebrania *eleph* linamaanisha "elfu" (BDB 48, KB 59 II). Linatumika kwa maana mbali mbali katika agano la Kale.

1. 1.sehemu ya familia, Yos. 22:14; Amu. 6:15; 1 Sam. 23:23; Zak. 9:7; 12:6
2. sehemu ya jeshi, Kut. 18:21,25; Kumb. 1:15
3. uhalisia wa tarakimu elfu, Mwa. 20:16; Kut. 32:28
4. ishara ya namba, Mwa. 24:60; Kut. 20:6; 34:7; Kumb. 7:9; Yer. 32:18
5. lenye kufanana na neno la lugha ya Ugaritiki *alluph* linalomaanisha "mtemi," Mwa. 36:15

Haya madokezo tofauti yanasababisha watafasiri wa leo kuuliza uhalisia wa hesabu

1. za wana wa Israeli waliotoka Misri
2. jamii ya kikabila ya jeshi la Israeli

◙**“Mimi, Bwana, nitayahimiza hayo wakati wake”** Historia ipo mikononi mwa Mungu (kama vile 45:23; 61:11).

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozowa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini sura hii imejazwa na stiari zenye kuelezea “mwanga” au “nuru”?
2. Patakuwepo na urejeshwaji wa wazi wa Wayahudi au hili linarejerea kwa Enzi ya Kimasihi?
3. Kwa nini watu wa mataifa watakimbilia Yerusalemu?
4. Ni uhusiano gani uliopo kati ya Mistari ya 15-22 na kitabu cha Ufunuo?

# ISAYA 6I

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Furaha kwa Wanyenyekevu | Habarai njema ya wokovu | Ujumbe kwa Sayuni | Habari Njema ya Ukombozi (61:1-62:12) | Ujumbe wa Nabii |
| 61:1-3 (1-3) | 61:1-3 (1-3) | 61:1-4 (1-4) | 61: 1-4 (1-4) | 61:1-9 (1-9) |
| 61:4-9 (4-9) | 61:4-7 (4-7) | | | |
| | | 61:5-7 (5-7) | 61:5-7 (5-7) | |
| | 61: 8-9 (8-9) | 61:8-11 (8-11) | 61:8-9 (8-9) | Shukrani |
| 61:10-11 (10-11) | 61:10-11 (10-11) | | 61: 10-11 (10-11) | 61:10-11 (10-11) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu nimwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KMUKTADHA

A. Sura ya 60 inaeleza kinachotokea mwishoni, ambapo sura ya 61 inaeleza maana ya Baraka za Mungu.
B. Yesu anakitumia kifungu hiki kujizungumzia mwenyewe katika Luka 4:16-21; 7:18-23. Kwa sababu ya hili, lazima kifungu hiki kiwe cha ki-Masihi (yaani, Mtumishi).
C. Kwa namna iliyo dhahiri hapa Roho wa Bwana ni (yaani, anayetabiri) yule Roho wa Agano Jipya Maana ya Utatu.
    1. tazama Mada Maalum: “Roho” katika Biblia katika 40:7
    2. tazama Mada Maalum: Utatu katika 40:13
**D.** Ni dhahiri kwamba huu ni mfano wa hali ya historia ya mahali katika maisha ya Israeli kutumika katika kutabiri matukio ya nyakati za Masihi (yaani, uainishaji).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 61:1-3)**
**[1]Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu;**
**kwa sababu Bwana amenitia mafuta**
**niwahubiri wanyenyekevu habari njema;**
**amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo,**
**kuwatangazia mateka uhuru wao,**
**na hao waliofungwa habari zakufunguliwa kwao.**
**[2]Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa,**
**na siku ya kisasi cha Mungu wetu;**
**kuwafariji wote waliao;**
**[3]kuwaagizia hao waliao katika Sayuni,**
**wapewe taji ya maua badala ya majivu,**
**mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito;**
**wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili atukuzwe.**

**61:1 "Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu"** Jambo hili lilionekana wazi katika maisha ya Yesu wakati wa ubatizo wake(kama vile 11:1-2; 42:1; Mt. 3:13-17; Marko 1:9-11; Luka 3:21,22; Yohana 1:31-34), lakini roho alikuwa pamoja na Yesu mara zote. Tazama Mada Maalum :Utu wa Roho katika 42:1.

◙**"amenitia mafuta" Hili ni sawa na maana ya neno** "Masihi" (BDB 602, tazama Mada Maalum katika 40:10) au Aliyetiwa Mafuta. Hii ilikuwa ishara ya baraka za Mungu za kipekee na kumuwakifisha kwa ajili ya kazi maalum (kama vile Zab. 23:5). Katika Agano la Kale manabii, makuhani, na wafalme, walikuwa wakitiwa mafuta kama ishara ya tendo la uwepo maalum wa Mungu na wito wa maisha yao. Kutokana na John Calvin anavidadavua vipengele vitatu fungamano vya kuibainisha huduma ya Kristo kama nabii, kuhani, na mfalme (kama vile Ebr. 1:2-3)

### MADA MAALUM : KUPAKWA MAFUTA KATIKA BIBLIA

(kitenzi cha Kiebrania, BDB 602, KB 643 I; nomino, BDB 603)

A. Yaliyumikakwaajiliyaurembeshaji (BDB 691 I. kama vile Kumb. 28:40; Ruthu 3:3; 2 Sam. 12:20; 14:2; 2 Nya. 28:15; Dan. 10:3; Mik. 6:15)
B. Yalitumikakwaajiliyawageni (BDB 206, kama vile Zab. 23:5; Luka 7:38,46; Yohana 11:2)
C. Yalitumikakwaajiliyauponyaji (BDB 602, kama vile Isa. 61:1; Marko 6:13; Luka 10:34; Yakobo 5:14) [yalitumikakwamaanayatibanakingakatikaEze. 16:9]
D. Yalitumikakatikamaandaliziyamazishi (kama vile Marko 16:1;Yohana 12:3,7; 19:39-40; 2 Nya. 16:14, lakinilikiwabilakitenzi "kutiwamafuta")
E. Yalitumikakatikamaanayakidini (yajambo, BDB 602, kama vile Mwa. 28:18; 31:13 [nguzo]; Kut. 29:36 [madhabahu]; Kut. 30:26; 40:9-16; Law. 8:10-13; Hes. 7:1 [hema])
F. Yalitumikakuwasimikaviongozi
   1. Makuhani
      a. Haruni (Kut. 28:41; 29:7; 30:30)
      b. WanawaHaruni (Kut. 40:15; Law. 7:36)
      c. Waliowekwawakfu (Hes. 3:3; Law. 16:32
   2. Wafalme
      a. Na Mungu (kama vile 1 Sam. 2:10; 2 Sam. 12:7; 2 Fal. 9:3,6,12; Zab. 45:7; 89:20)
      b. Na manabii (kama vile 1 Sam. 9:16; 10:1; 15:1,17; 16:3,12-13; 1 Fal. 1:45; 19:15-16)
      c. Na makuhani (kama vile 1 Fal. 1:34,39; 2 Fal. 11:12)

d. Nawazee (kama vile Amu. 9:8,15; 2 Sam. 2:7; 5:3; 2 Fal. 23:30)
e. JuuyaYesukamamfalmewaKimasihi
(kama vile Zab. 2:2; Luka 4:18 [Isa. 61:1]; Matendo 4:27; 10:38; Heb. 1:9 [Zab. 45:7])
f. WafuaswaYesu (kama vile 2 Kor. 1:21; 1 Yohana 2:20,27 [mafuta)
3. Juuyamanabiikadriiliyowezekana (kama vile 1 Fal. 19:16; Isa. 61:1)
4. Kuvikomboavyombovisivyoaminikavyaki-Uungu
a. Koreshi (kama vile Isa. 45:1)
b. MfalmewaTiro (kama vile Eze. 28:14, ambapoalitumia stiraizaBustaniyaEdeni)
5. Neno au cheo "Masihi" maanayakeni "Mtiwamafuta " (BDB 603), kama vile Zab. 2:2; 89:38; 132:10
Matendo 10:38 nimsitari ambapo nafsitatuzaUunguzinazwekwapamojakatikakutiwamafuta.Yesualipakwamafuta (kama vile Luka 4:18; Matendo 4:27; 10:38). Dhanainapanuliwailikuwajumuishawaaminiwote (kama vile 1Yohana2:27). Mpakwamafutaanakuwawapakwamafuta! HiiinawezakuwasambambanaMpingaKristonawapinga kristo (kama vile 1Yohana 2:18). Tendo la isharayaAgano la Kale la kumiminiwamafutamwilini (kama vile Kut. 29:7; 30:25; 37:29) linahusianana wale walioitwanakuandaliwanaMungukwakazimaalumu (yaani, manabii, makuhani, nawafalme). Neno“Kristo”nitafsiriyaneno la Kiebrania“mpakwamafuta ” au Masihi.

◙**“niwahubiri wanyenyekevu habari njema”**Ujumbe waMasihi (tazama Mada Maalum : Masihi katika 40:10) utakuwa tumaini na msamaha kwa wale waliotengwa, waliokataliwa, na wanaonyanyaswa kijamii (kama vile 35:5-6).

Tambua mtiririko wa VITENZIJINA HALISI katika mist. ya1-3 ambavyo vinatoa ufafanuzi wa kazi ya Masihi.
1. niwahubiri wanyenyekevu habari njema – *Piel*, BDB 142, KB 163
2. kuwatangazia mateka uhuru wao – *Qal*, BDB 894, KB 1128
3. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa – sawa na #2
4. kuwafariji wote waliao – *Piel* BDB 636, KB 688
5. kuwaagizia hao waliao katika Sayuniwapewe taji ya maua badala ya majivu
   a. kuwaagizia – *Qal*, BDB 962, KB 1321
   b. wapewe– *Qal* BDB 678, KB 733
6. Hii ni TUNGO nyingine ya KITENZI JINA lakini moja kwa moja inamwelekea Masihi, Mwenyewe – “ili atukuzwe” – *Hithpael,* BDB 802, KB 908

**61:2 “mwaka wa Bwana uliokubaliwa”** Hili ni dokezo la mwaka waJubilei (kama vile Law. 25:10). Huu ulikuwa mwaka wa kuachiliwa kutokakatika madeni na kurudisha ardhi kwa wamiliki wake halisi kila baada ya miaka mitano.
Hauna mfano mmoja katika Agano la Kale ya kwamba kihistoria hili lilidumishwa.

◙**“siku ya kisasi cha Mungu wetu”** Ni muhimu kutambua kuwa mwaka uliokubaliwa na siku ya kisasi vyote vilitukia kwa wakati ule ule. Kwa wale wanaomjua Mungu katika Masihi, ni siku ya kupewa taji. Kwa wale wasio mjua Kristo wetu, hiini siku ya hukumu na huzuni kubwa. Lazima iwe habari mbaya kabla ya habari njema! (kama vile Warumi 1-3).

**61:3** Zitambue tofauti(yaani, “badala”).
1. taji ya maua badala ya majivu
2. furaha badala ya maombolezo
3. vazi la sifa badala ya roho nzito

Pia zitambue tofauti zinazofanana katika mst. wa7.
1. Badala ya aibu yenu mtapata maradufu
2. badala ya fedheha wataifurahia sehemu yao

◙**"taji. . majivu"** Hii ni mifano ya aina ya vitu vinavyovaliwa kichwani (kama vile Eze. 24:17).

◙**"Mafuta ya furaha"** Watu wa kale walikuwa na uhaba wa vipodozi, hivyo, ilikujiandaa kwa ajili ya nyakati za furaha na tamasha, walijipaka mafauta ya mizeituni (kama vile Zab. 45:7).

◙**"Vazi la sifa"** Hapa kuna mfano wa mavazi ya kipindi cha Agano la Kale yaliyotumika kama stiari ya mtazamo na nafasi ya kiroho.

◙**"miti ya haki. . . iliyopandwa na Bwana"** Katika Zaburi 1 kifungu hiki kinaurejelea upendo wa awali wa Mungu na uendelevu wa kujali kwake na utoaji wake (kama vile Yer. 17:7-8). Hapa kifungu hiki kinamrejelea Masihi (kama vile 60:12).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 61:4-9**
**4 Nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa,**
**watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani,**
**watatengeneza miji iliyoharibiwa,**
**mahali palipoachwa kizazi baada ya kizazi.**
**5 Na wageni watasimama na kulisha makundi yenu,**
**na watu wa kabila nyingine watakuwa wakulima wenu,**
**na watunzaji wa mizabibu yenu.**
**6 Bali ninyi mtaitwa makuhani wa Bwana;**
**watu watawaiteni wahudumu wa Mungu wetu;**
**mtakula utajiri wa mataifa, na kujisifia utukufu wao.**
**7 Badala ya aibu yenu mtapata maradufu,**
**na badala ya fedheha wataifurahia sehemu yao;**
**basi katika nchi yao watamiliki maradufu; furaha yao itakuwa ya milele.**
**8 Maana mimi, Bwana, naipenda hukumu ya haki,**
**nauchukia wivi na uovu;**
**nami nitawalipa malipo katika kweli, nitaagana nao agano la milele.**
**9 Na kizazi chao kitajulikana katika mataifa,**
**na uzao wao katika kabila za watu;**
**wote wawaonao watakiri ya kuwa wao ni kizazi kilichobarikiwa na Bwana.**

**61:4 "watajenga mahali pa kale palipoharibiwa"** Ni vigumu kwa wale wasio Wayahudi kufikiri juu ya nguvu ya hisia ambazo zinahusianishwa na Nchi ya Ahad**i** (kama vile 49:8; 58:12; 60:10).
Mstari huu unaorodhesha mambo kadhaa ambayo atayafanya yule aliyewekwa huru.

1. watajenga mahali pa kale palipoharibiwa
2. watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani
3. watatengeneza miji iliyoharibiwa

Ubeti wa mwisho wa mst. wa 4 unaonyesha kwamba mwandishi anawaasa wale waliotoka uhamishoni Mesopotamia.

**61:5 Mstari wa** 5 unaendeleza ujumbe wa wageni watokao Yerusalemu wakiwa na zawadi na huduma, kwa ajili ya kumwabudu Mungu wa Israeli.Kutokana na ufunuo wa Agano Jipya tunafahamu kwamba kipengele hiki kinalirejelea agano jipya katika Kristo linalopatikana kwa wote kupitia toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21)! Nazifasiri ahadi za Agano la Kale juu ya taifa la Israeli kama utimilifu wa nabii za makutano. Hizi hazikuweza kutimizwa kamwe katika historia ya Israeli kwa sababu ya dhambi na uasi wake. Zimekamilishwa katika Kristo pekee.Tazama Mada Maalum katika 40:9 na 40:15!

◙**" ninyi mtaitwa makuhani wa Bwana"** Israeli ilimaanishwa kuwa taifa la makuhani, na sasa itakuwa! Petro anakitumia kifungu hiki sana kulifafanua kanisa katika I Pet. 2:5,9 (kama vile Kut. 19:56-6; piatazama matumizi yake katika Ufu. 1:6).

**61:7 "mtapata maradufu"** Kifungu hiki kinaonekana kuurejelea urithi wa mzaliwa wa kwanza katika muundo waIsraeli ya kale (kama vile Kumb. 21:17). Kama Israeli ilivyokumbwa na ghadhabu ya YHWH maradufu (kama vile 40:2),na sasa ni thawabu maradufu.

◙**"Furaha yao itakuwa ya milele"** Hii ahadi ya kustaajabisha yenye kufanana inapatikana katika Zab. 16:11. Swali ni kwamba hili litatukia lini.

1. hilli halitatukia kwa wale waliorudi toka uhamishoni Mesopotamia
2. hili halikutukia kwa Wayahudi waliokuwa chini ya Uyunani au Rumi
3. kisha baadaye
    a. Israeli baada ya kuja kwa Masihi
    b. kanisa
    c. miaka elfu
    d. Bustani ya Edeni iliyorejeshwa

Hili ni la kale, ushairi uliovuviwa! Hili halielezi maswali yote ya sasa. Ni vizuri sana kuichukua maana ya msingi ya ubeti huu na kuitolea maoni kupitia ufunuo wa Agano Jipya!

**61:8 "Maana mimi, Bwana, naipenda hukumu ya haki"**YHWH ni wa mwenendo mwema, ni wa maadili. Yeye anadai mwenendo mwema, matendo mema kutoka kwa watu wake!
Zitambue sifa bainishi zake zilizoorodheshwa.

1. Naipenda hukumu ya haki
2. nauchukia wivi na uovu

Andiko lingine la kushangaza ambalo linaeleza sifa za YHWH ni Kut. 34:6; Hes. 14:18; Neh. 9:17; Zab. 86:15; 103:8-14; 145:8-9! Tazama Mada Maalum katika 49:7.

◙**"nauchukia wivi na uovu"** Toleo la Agano la Kale la Kiebrania na huenda baadhi ya tofauti za toleo la Masoretic Text lina kifungu "na uharibifu" (sawa na konsonanti). Toleo la UBS Text Project linakipa hiki kifungu uovu daraja B.

◙**"nita. . . agano la milele"** Kwa uendelevu Wayahudi walilivunja agano la kwanza**,** kadri nilivyosoma I Wafalme na II Wafalme I Nya. na II Nya zitaonyesha. Kwa sababu ya hili, Hatimaye Mungu aliliruhusu Agano likamilishwe (Roho wake analiacha hekalu; Anguko la Yerusalemu). Sababu ya kukamilishwa huku ulikuwa mwanzo wa agano jipya lenye umuhimu mkubwa wa kiroho (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38).

**61:9** Hapa kuna rejea nyingine juu ya Israeli kama ishara na ujumbe (yaani, nuru, kama vile 42:6; 49:6; 51:4; Matendo13:47) unaohusu asili ya Mungu kwa mataifa mengine.

**ANDIKO LA NASB ( LILILOBORESHWA) 61: 10-11**
**10 Nitafurahi sana katika Bwana,**
**nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu;**
**maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki,**
**kama bwana arusi ajipambavyo kwa kilemba cha maua,**
**na kama bibi arusi ajipambavyo kwa vyombo vya dhahabu.**
**11 Maana kama nchi itoavyo machipuko yake,**
**na kama bustani ioteshavyo vitu vilivyopandwa ndani yake;**
**ndivyo Bwana MUNGU atakavyootesha haki na sifa mbele ya mataifa yote.**

**61:10 "Nitafurahi sana katika Bwana,**
**Nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu"** Mstari huu ungeweza kumrejeleaMasihi au taifa (kama vile 12:1-2;25:9; 41:16) lenye kufurahi katika utoaji wa YHWH. AB inapendekeza kwamba sura hii inawazungumzaji watatu.

1. nabii, mist. ya 1-7 (huenda ni Mtumishi)
2. YHWH, mist. ya 8-9
3. Sayuni iliyohuishwa, mist. ya 10-11 (uk. 181)

Kipengele hiki kinaonyesha utata wa haya mashairi kama ilivyo kwa wazungumzaji na wapokeaji (yaani, kipindi cha wakati). Watoa maoni wengi wanafikiri 61:1-3 ni Wimbo wa tatu wa Mtumishi. Nafikiri mist.ya10-11 ni ubinadamu uliorejeshwa na kukombolewa (kama vile Mwa. 3:15), ambao unaelezwa katika Efe. 2:11-3:13; Warumi 9-11. Hiki KITENZI CHA WAKATI USIOTIMILIFU, "Nitafurahi sana,"ni*Qal* ya KITENZI JINA HALISI na*Qal*ya KAULI ISIYO TIMILIFU.KITENZI chenye asili ile ile (BDB 965, KB 1314).Hii ilikuwa namna ya Sarufi ya Kiebrania ya kuonyesha uweza. Mstari unaofuata unafanana na KITENZI "inuka" ni *Qal*ya KAULI AMRISHI (BDB 162, KB 189).

◙**"amenivika mavazi ya wokovu"**Huu ni mfano wa furaha ya siku ya harusi iliyotumika kama stiari ya furaha ya kiroho ya kumjua Mungu. Stiari hii inapanuliwahadi katika Agano Jipya ili kuwarejelea waamini kama wenye kuvaa mavazi ya haki ya Kristo (kama vile II Kor. 5:21).

**61:11** TazamaIsa. 40:8 na 55:10-11.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ikiwa hili linamrejelea Masihi, kwa nini limewekwa katika kifungu cha namna ya maneno ya kitaifa?
2. Toa ufafanuzi wa neno Masihi.
3. Ni katika maana na kusudi gani Wayahudi kuwa ufalme wa makuhani?
4. Kwa nini Mungu alilivunja agano lake la milele la awali kati yake na taifa la Kiyahudi?
5. Kwa nini matumizi ya mst.wa10 ya stiari ya vazi ni muhimu sana? Ni kwa namna gani stiari inatumika katika muumini wa Agano Jipya kabla ya Mungu?

# ISAYA 62

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Utukufu wa Sayuni Na jina jipya | Uhakika wa wokovu Sayuni | Utukufu wa watu wa Mungu | Habari njema ya ukombozi (61:1-62:12) | Fahari ya Yerusalem |
| 62:1-5 (1-5) | 62:1-5 (1-5) | 62:1-9 (1-9) | 62:1-5 (1-5) | 62:1-5 (1-5) |
| 62:6-9 (6-9) | 62:6-7 (6-7) | | 62:6-7 (6-7) | 62:6-9 (6-9) |
| | 62:8-9 (8-9) | | 62:8-9 (8-9) | Hitimisho |
| 62:10-12 (10-12) | 62:10-12 (10-12) | 62:10-12 (10-12) | 62:10-12 (10-12) | 62:10-11 (10-11) |
| | | | | 62:12 (12) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xxiv kipengere cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozokwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

21. Aya ya kwanza
22. Aya ya pili
23. Aya ya tatu
24. Nk

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 62:1-5**
**1 Kwa ajili ya Sayuni sitanyamaza,**
**na kwa ajili ya Yerusalemu sitatulia,**
**hata haki yake itakapotokea kama mwangaza,**
**na wokovu wake kama taa iwakayo.**
**2 Na mataifa wataiona haki yako,**
**na wafalme wote watauona utukufu wako;**

**nawe utaitwa jina jipya,**
**litakalotajwa na kinywa cha Bwana.**
**3Nawe utakuwa taji ya uzuri katika mkono wa Bwana,**
**na kilemba cha kifalme mkononi mwa Mungu wako.**
**4Hutaitwa tena Aliyeachwa,**
**wala nchi yako haitaitwa tena, Ukiwa;**
**bali utaitwa Hefsiba;**
**na nchi yako Beula;**
**kwa kuwa Bwana anakufurahia ,**
**na nchi yako itaolewa.**
**5 Maana kama vile kijana amwoavyo mwanamwali,**
**ndivyo wana wako watakavyokuoa wewe;**
**na kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi,**
**ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe.**

**62:1 "Sayuni. . .Yerusalemu"** Haya yana uhusiano mfanano wa Kiebrania. Yerusalemu imejengwa juu ya vilima saba. Mlima Sayuni sio eneo la Hekalu, lakini ni eneo la jumba la kifalme la MfalmeDaudi na linarejelea eneo lote la mji wa Yerusalemu.

◙ KITENZI hiki "sitanyamaza" (*Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 364, KB 361) na "sitatulia" (*Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 1052, KB 1641), chenye kukanusha, kinahusiana na maelezo chanya ya 61:1. Neno "mimi" linaweza kurejelea nabii au mtumishi/Masihi (Uungu unavunja ukimya uliotajwa kwenye 42:14; 57:11; 64:12; 65:6). Ni wazi katika Sura za 60-62 ni sehemu ya fasihi.

◙**"haki . . .wokovu"** maneno haya mawili pia yana uhusiano unaofanana. haki (angalia Mada Maalumu katika 48:1) inaongelea hali na mtindo wa maisha ya watu wa Mungu ambao matokeo yake ni kukombolewa kimwili kutoka kwa maadui zao. Katika Agano la kale neno "wokovu" kimsingi linarejelea ukombozi wa kimwili, ambapo katika Agano jipya neno hili kimsingi linarejelea msamaha wa kiroho na kusimama mbele za Mungu. Siku mpya za Sayuni (kama vile. 61:10-11) zimekwisha kuwadia na zitaathiri ulimwengu mzima (kama vile. mst. 2; 60:3)!

## MADA MAALUM: WOKOVU (Kipindi Cha AGANO LA KALE)

Neno hili (BDB 447, KB 446, zote NOMINO JINSI YA KIKE NA KIUME), ambazo kimsingi humaanisha "pana na yenye nafasi kubwa" au "kuwa huru," lina vidokezo mbalimbali.

1. usalama, 2 Sam. 22:3; Ayubu 5:11; Zab. 12:5
2. ustawi, mafanikio, Ayubu 30:15
3. wokovu wa Kiungu wenye kujumuisha wokovu wa kimwili na kiroho
    a. Mwa. 49:18
    b. Kumb. 32:15
    c. 2 Sam. 23:5
    d. Zab. 3:2,8; 22:1; 35:3; 62:2; 69:29; 70:5; 78:22; 80:3; 89:26; 91:16; 106:4; 140:7
    e. Isa. 12:2; 33:2; 51:6,8; 52:7,10; 56:1; 59:11; 60:18; 62:1,11
4. wazo la ukombozi wa kiroho na kimwili kwa wazi unaonekana katika Yona 2:9-10
5. ushindi, Kut. 14:30; 15:2; 1 Sam. 14:45; Zab. 20:6; 21:5; 44:4-5; 68:19-20; 118:14,15,21; Isa. 12:2; Hab. 3:8
6. mara nyingi neno "furahini" linahusiana na wokovu wa YHWH, 1 Sam. 2:1; Isa. 25:9; 26:1; Zab. 9:14; 13:5; 21:1; 35:9; 118:15,21

Wokovu unahusisha uanzishaji wa ushirika wa mwanzo wa YHWH uliokusudiwa na jamii ya wanadamu. Inajumuisha ujumla wa kibinafsi na kijamii!

◙**"mwangaza. . .iwakayo"** uwepo wa YHWH tena unaunganishwa na Nuru, kama ulivyokuwa katika Mlima Sinai (kama vile. Kut 19-20). Angalia kumbukumbu katika 60:1.

Israeli inamaanisha kuwa "Nuru" ya YHWH kwenye giza la upagani na ibada zao za upagani.
hata hivyo,alitekwa na wao. Agano jipya linatupatia mpango wa aina ile ile ya ufunuo (kama vile . Yesu ni Nuru kuu ya Mungu, kama vile. Yn 1:4; 8:12; 12:35) na injili kwa waaminio (kama vile. Mt. 5:14-16).

**62:2 "mataifa wataiona haki yako"** Israeli amechaguliwa na Mungu ili kuwa shahidi kwa ulimwengu mzima ili kuwaleta watu kwa YHWH (kama vile. mst. 11; 52:10; 60:3; 61:6,11; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Hii ni maana ya kweli ya kifungu "ukuhani wa kifalme" (kama vile. Kut. 19:5-6).

◙**"nawe utaitwa jina jipya "** kutaarifu jina jipya kunadokeza enzi mpya ya kiroho. Maagano mapya yamepatikana.

Neno "jipya" (BDB 294 I) limetumika kwa upana zaidi katika sehemu ya pili ya Isaya kuelezea enzi mpya ya haki.

1. Vitu vipya, 42:9; 48:6
2. Wimbo mpya, 42:10 (kama vile. Ufu. 5:9; 14:3)
3. Jambo jipya, 43:19 (kama vile. Ufu. 3:12)
4. Jina jipya, 62:2 (kama vile. 56:5)
5. Mbingu mpya na nchi mpya, 65:17; 66:22 (kama vile. 2 Pet 3:13)

Siku "mpya" (kama vile. Ufu. 21:5) iko katika uhalisia, siku ambayo kwamba Mungu anaitaka kwa ajili ya wanadamu, lakini anguko katika kitabu cha Mwa.3 lilisababisha utenganisho wa kutisha! Ni ukweli unaowezekana kwamba taswira ya kibiblia ya mbinguni imerejeshwa katika bustani ya Edeni (kama vile. Ufu. 21:2).

**62:3** *The Jerome Bible Commentary*, juzuu. 1, uk. 383, linataja kwamba watu wa kale wa mashariki waliamini miungu yao iliyovishwa taji lenye sura ya mji waliouabudu. Kama ni hivyo, basi hili lawezakuwa ni dokezo la kitamaduni kwenye wazo hili. Maono haya yanategemea

1. YHWH kuwa ndiye mnenaji wa Sura ya 62
2. Kwa namna gani dhana hii ya upagani imeenea na kufahamika

Biblia inatumia taswira ya upagani kuelezea na kumtukuza YHWH. Mifano minne kati ya mingi:

1. "Mungu wa mbinguni" katika Nehemia
2. Dokezo kwa uungu wa Uajemi, Mal. 4:2
3. Dokezo kwa ishara kumi na mbili za unajimu katika Ufu. 12:1
4. Dokezo kwa Ibilisi kama Joka

Katika Isa. 28:5 YHWH pekee ni taji ya watu wa maagano.Yeye ni utukufu wao, Nuru, awapaye chakula, ulinzi, na ushindi!

katika Zek. 9:16 watu wa maagano ni vito vya thamani kwenye taji ya YHWH.

**62:4 "aliyeachwa. . .ukiwa"** Hii inaelezea ufafanuzi wa uhamisho wa Israeli (yaani.,hili lilikuwa jina kwa ajili yao wenyewe). Walijihisi kwamba wameachwa (kama vile. 54:6-7)na Mungu na wakaingiwa hofu kama atawapenda tena.

◙**"amekufulahia"** Neno "furahia" labda jina la "Hefsiba" (BDB 343, kama vile. 2 Fal. 21:1). Huu ni mwanzo wa sitiari ya kustahimili kuhusu Mungu kama mwanandoa mwenza (kama vile mistr. 4-5). Ni vigumu kumwelezea Mungu Mtakatifu Muumbaji asiye na mwisho, hivyo basi, tunatumia analojia ya mwadamu (tazama Mada Maalumu katika 41:2). Ni kawaida kwenye Biblia kumwelezea Mungu kama Baba, kama Mme,kama ndugu wa

karibu.

◙**"itaolewa"** hili pia linaweza kutafsiriwa kama "Beula" (BDB 127). Mistari ya 4 na 5 labda ni "jina jpya"la mst wa 2.

KITENZI hiki (BDB 127, KB 42) kimetumika mara nne kwenye mistari ya 4-5.

1. *Qal* KAULI TENDWA ENDELEVU, mst. 4
2. *Niphal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, mst. 4
3. *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, mst. 5
4. Ni sawa kama # 3

**62:5**
**NASB, NKJV "hivyo wana wako watakuoa wewe"**
**NRSV "hivyo mjenzi wako watakuoa wewe"**
**TEV "aliyekuumba atakuoa wewe"**
**NJB "aliyekujenga atakuoa wewe"**
**REB "hivyo utaolewa na mjenzi wako"**
**LXX "hivyo wana wako watakaa kwako"**

kwa Urudiaji tena wa konsonanti (בניד)wa neno "wana " linakujakuwa neno "wajenzi" (yaani YHWH, kama vile. Zab. 51:18;102:16; 147:2), ambapo ubeti huu unafaa kwa taswira ya ndoa. *The Expositor's Bible Commentary*, juzuu. 1, uk. 336, inasema juu ya mistari hii "Mstari wa 5 unawakilisha analojia ngeni kama kwamba iliyoko katika 60:16. Kwa hali zote panaonekana kuwepo na uvunjaji sheria wa kimakusudi katika matumizi ya kawaida ya analojia, labda katika umuhimu wa wazo la wazi. Kama analojia ni fumbo kwetu, lakini hatuwezi kuwasahau wao!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 62:6-9**
**6 Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalemu;**
**hawatanyamaza mchana wala usiku;**
**ninyi wenye kumkumbusha Bwana, msiwe na kimya;**
**7 wala msimwache akae kimya,**
**mpaka atakapoufanya imara Yerusalemu, na kuufanya kuwa sifa duniani.**
**8 Bwana ameapa kwa mkono wake wa kuume, na kwa mkono wa nguvu zake,**
**Hakika sitawapa adui zako nafaka yako tena kuwa chakula chao;**
**wala wageni hawatakunywa divai yako, uliyoifanyia kazi.**
**9 Lakini walioivuna, ndio watakaoila, na kumhimidi Bwana;**
**na walioichuma, ndio watakaoinywa, ndani ya nyua za patakatifu pangu.**

**62:6** Hii inarejelea kwa manabii (kama vile. 52:8; 56:10 [kukanusha]; Yer. 6:17; Ezek. 3:17; 33:7), ingawa waalimu wa sheria ya kiyahudi wanaona hii inarejelea kwa malaika (kama vile. Zek. 1:12-17).

◙**"ninyi wenye kumkumbusha BWANA. . .wala msimwache akae kimya mpaka atakapoufanya imara . . .Yerusalemu"** Hili labda linarejelea ukweli wa thiolojia kwamba Mungu mwenyewe ameweka mipaka katika maombi ya watoto wake (kama vile. Yak 4:2). Sio kutotaka kushinda hali ya kutomjali Mungu, bali ni kutetea huduma ya watu wa Mungu wanaotangaza ahadi za Mungu (tazama Mada Maalumu katika juzuu. 11A, katika 37:21-24).
VITENZI hivi "nimeweka " na "kumkumbusha" vyote ni *Hiphils*.

**62:8 "BWANA ameapa kwa mkono wake wa kuume, na kwa mkono wa nguvu zake "** Hii ni tungo ya elimu ya binadamu ya asili (tazama Mada Maalumu katika 41:2).Mungu hana mwili. Yeye ni Roho (kama vile. Yoh 4:24),na bado anaapa kwa uwezo wake wa kutenda! YHWH ni Mungu ambaye, anatamani, na kutenda kwa kila mmoja mmoja anayeishi, kama vile kwa mataifa.

kiapo cha Mungu ni ahadi ya muhimu sana (kama vile. 54:9; Ebr. 6:13-20; 7:20-28). Kinatukumbusha sisi kama

1. Nguvu ya neno la Mungu, 55:11; 66:2d
2. Tabia ya uaminifu wa Mungu, 45:22-23

Mungu ana mpango wa ukombozi wa milele kwa ajili ya wanadamu wote aliowaumba kwa mfano na sura yake (kama vile. Mdo 2:23; 3:18; 4:28; I Pet. 1:20, tazama Mada Maalumu katika 40:15). Wimbo wa Mtumishi atesekaye katika 52:13-53:12 ni suluhisho kwa ajili ya ukombozi wa ulimwengu (kama vile. Rum. 5:12-21). Ushirika wa Edeni utarejeshwa kwa ajiri ya wale watakao tubu na kumwamini Masihi wa Mungu.

◙**"maadui. . .wageni"** Hii inarejelea wageni walioivamia Palestina. Ni rejeo la moja kwa moja la baraka dhidi ya matendo ya laana Law. 26:16 na Kumb. 28:30-33. Israeli walivunja maagano. Israeli waliteseka na matokeo hayo. YHWH aliahidi siku zijazo ambapo Baraka zitakuwa dhahili.

**62:9 "watakaoinywa, ndani ya nyua za patakatifu pangu."** Hii inarejelea karamu ya ushirika kati ya Mungu na mshirika Wake wa maagano (kama vile. Kumb. 12:18). Watu hawa wamerudi katika nchi yao na hekalu limerejeshwa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 62:10-12**
**[10] Piteni, piteni, katika malango;**
**Itengenezeni njia ya watu;**
**Tutieni, tutieni barabara;**
**toeni mawe yake; Twekeni bendera kwa ajili ya kabila za watu.**
**[11] Tazama, Bwana ametangaza habari mpaka mwisho wa dunia,**
**Mwambieni binti Sayuni, Tazama, wokovu wako unakuja;**
**Tazama, thawabu yake i pamoja naye, Na malipo yake yako mbele zake.**
**[12] Nao watawaita, Watu watakatifu,**
**Waliokombolewa na Bwana;**
**Nawe utaitwa, Aliyetafutwa, Mji usioachwa.**

**62:10-11** Huu ni ujumbe kwa ajili ya watu waliopewa na nabii kwa niaba ya YHWH. Kuna mfuatano wa KAULI SHURUTISHI nane.
1. piteni – *Qal*, BDB 716, KB 778
2. piteni – sawasawa na ule #1
3. itengenezeni njia– *Piel*, BDB 815, KB 937
4. tutieni – *Qal*, BDB 699, KB 757
5. tutieni –sawasawa na ule # 4
6. toeni mawe – *Piel*, BDB 709, KB 768
7. twekeni bendera – *Hiphil*, BDB 926, KB 1202
8. mwambieni – *Qal*, BDB 55, KB 65

**62:10 "piteni katika malango"** Hili linaweza kurejelea
1. malango ya miji ya Mesopotamia ambapo Waisraeli na Wayuda walipelekwa uhamishoni (hasa. Babeli)
2. yumkini ni nje ya utaratibu wa kimatukio na inarejelea malango yaliyojengwa tena
   a. Yerusalemu (Ezra, Nehemia)
   b. hekalu

◙**"twekeni bendera"** Hii inarejelea bendera ya kabila au kikosi cha kijeshi. Tambua hapa bendera inakuwa juu ya "watu" na mst. 11a "mpaka mwisho wa dunia." Alama ya Israeli ni bendera kwa wale wote ambao wanamwamini,kumpokea, na kumfahamu YHWH.

◙**"itengenezeni njia ya watu;**
**tutieni,tutieni barabara"**

Hii ni sitiari kwa ajili ya kuandaa njia ya ujio wa kifalme (kama vile. Isa. 35:6-10; 40:3-4; 57:14). Hii imetumika kwa namna mara kadhaa ndani ya Biblia.

1. Imetumika kurudi kutoka uhamishoni
2. Imetumika kwa Yohana mbatizaji kama utambulisho wake wa huduma yake

**62:11 "mpaka mwisho wa Dunia"** hii ni sura ya ahadi za YHWH kwa ulimwengu kwamba ni ishara ya upendo na wokovu wake kwa ajili ya wanadamu wote, sasa sio kwa Israeli pekee. Tazama Mada Maalumu katika 40:15.

◙**"mwambieni. . ."** kuna kweli tatu zimezungumzwa hapa (*Qal* KAULI SHURUTISHI).

1. Wokovu wako unakuja (kama vile. 49:6)
2. Thawabu yake i pamoja naye
3. Malipo yake yako mbele zake (kama vile. 40:10)

**62:12 "nao watawaita"** Hili ni dokezo la "jina jipya" la mst. 2. Wasiokuwa Waisraeli sasa wataitwa, "wasioachwa" au "kuwa ukiwa" (mst. 4),lakini

1. Watu watakatifu
2. Waliokombolewa na BWANA
3. waliotafutwa

◙**"waliokombolewa na BWANA"** Neno "kukombolewa" (BDB 145 I, angalia Mada Maalumu katika 41:14) inahusiana na dhana ya *Go'el*. Huyu ni mkombozi wa ndugu yake aliyemrejesha kutoka kwenye umasikini au mateka.

YHWH kama *go'el* ni mfano mwingine wa Uungu unaoelezewa kwa undani sana kwenye hali ya kifamilia.

◙**"aliyetafutwa, mji usioachwa"** jina hili lina maana sana kwa sababu linasema ukweli kwamba Mungu hakuwakataa Wayahudi bali aliwaelekea Wayahudi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wafasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwatafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Je Isaya 62 pekee inarejelea uhamishoni au ni uainishi unaorejelea utawala wa Masihi?
2. Elezea maneno "haki" na "wokovu" kwenye Agano la kale
3. Kwa nini Mungu anakumbushwa kwenye mst. 6 juu ya ahadi zake?
4. Je Mungu ana upendo wa kipekee kwa ajili ya Israeli na kwamba hana upendo huo kwa ajili ya mataifa mengine?

# ISAYA 63

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kisasi cha Mungu Juu ya Mataifa | Bwana katika hukumu na Wokovu | Shairi la Kisasi cha Uungu | Ushindi wa Bwana juu ya Mataifa | Hukumu juu ya Mataifa |
| 63:1-6 (1-6) | 63:1a (1a) | 63:1a (1a) | 63:1a | 63:1-6 (1-6) |
| | 63:1b (1b) | 63:1b (1b) | 63:1b | |
| | 63:2 (2) | 63:2 (2) | 63:2 | |
| | 63:3-6 (3-6) | 63:3-6 (3-6) | 63:3-6 | |
| Rehema za awali zinaombwa tena (63:7-64:11) | Rehema za Mungu zinakumbukwa | Zaburi ya Kusihi (63:7-64:12) | Wema wa Mungu juu ya Isreli | Upatanisho wa historia ya Israeli |
| 64:7-14 (7-14) | 63:7-10 (7-10) | 63:7-9 (7-9) | 63:7 (7) | 63:7 (7) |
| | | | 63:8-10 | 63:8-10 (8-10) |
| | | 63:10-14 (10-14) | | |
| | 63:11-14 (11-14) | | 63:11-13a | 63:11-14 (11-14) |
| | | | 63:13b-14 | |
| "Wewe ndiwe Baba Yetu" (63:15-64:12) | Ombi la toba | | Ombi la Rehema na Msaada | |
| 63:15-19 (15-19) | 63:15-19 (15-19) | 63:15-19 (15-19) | 63: 15-17 | 63:15-19b (15-19b) |
| | | | 63:18-64:7 | |
| | | | | 63:19c-64:11 (19c-64:11) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

25. Aya ya kwanza
26. Aya ya pili
27. Aya ya tatu
28. N.k

## USOMAJI WA NENO A KIFUGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 63:1-6**
**1 Ni nani huyu atokaye Edomu,**
**Mwenye mavazi ya kutiwa damu kutoka Bosra?**
**Huyu aliye na nguo za fahari,**
**Anayekwenda katika ukuu wa uweza wake?**
**2 Kwani mavazi yako kuwa mekundu,**
**Na nguo zako kama za mtu akanyagaye zabibu?**
**3 Nalikanyaga shinikizoni peke yangu;**
**Wala katika watu hakuwapo mtu pamoja nami;**
**Naam, naliwakanyaga kwa hasira yangu,**
**Naliwaponda kwa ghadhabu yangu; Na mavazi yangu yametiwa madoa kwa damu yao,**
**Nami nimezichafua nguo zangu zote.**
**4 Maana siku ya kisasi ilikuwamo moyoni mwangu,**
**Na mwaka wao niliowakomboa umewadia.**
**5 Nikatazama, wala hakuna wa kusaidia;**
**Nikashangaa kwa kuwa hakuna mwenye kutegemeza;**
**Basi, mkono wangu mwenyewe uliniletea wokovu,**
**Ghadhabu yangu ndiyo iliyonitegemeza.**
**6 Nikazikanyaga kabila za watu kwa hasira yangu,**
**Nikawalevya kwa ghadhabu yangu,**
**Nami nikaimwaga damu yao chini.**

**63:1-6 Haya ni majibizano ama shutuma** (swali -jibu) kati ya nabii/ Mtumishi na YHWH.

1. Nabii anauliza swali la kwanza, mst. wa 1 – YHWH anaelezwa kama atokaye Edomu katika namna ya mwonekano wa utukufu, mist. ya 1a-d,2
2. YHWH anazungumza, mst. wa 1e
   a. anazungumza katika haki
   b. Mkuu Mwenye kuokoa
3. Nabii anauliza swali la pili, mst. wa 2
4. YHWH anajibu, mist. ya 3-6
   a. Nalikanyaga shinikizoni peke yangu(yaani, hukumu)
   b. hakuna hata mmoja miongoni mwa watu aliye pamoja na naye (kama vilemst. wa 5; 59:16)

**63:1 "Edomu" Hili taifa lililojirani, mara nyingi ni ishara kwa mataifa yote ya Wapagani** (kama vile 34:5-15) ambayo yanahukumiwa na YHWH.

## MADA MAALUM: EDOMU NA ISRAELI

A. Edomu ni taifa mashariki mwa bahari ya Chumvi, linalotokana na kaka yake na Yakobo (kama vile Mwanzo 25-28; 32-33). Edomu inamaania "wekundu" wakati Esau linamaanisha "mwenye nywele" (kama vile Mwanzo 25:25, 30).
B. Israeli aliamuriwa kuheshimu Edomu kwasababu walikuwa ni ndugu (kama vile Kumb. 23:7)
C. Israeli na Edomu walikuwa na matatizo yanayoendelea.
   1. Hes. 20:14-21
   2. Amu. 11:16-17
   3. 1 Sam. 14:47-48
   4. 2 Sam. 8:14
   5. 1 Fal. 11:14-22
   6. 2 Fal. 14:22; 16:5-6
   7. 2 Kor. 20:10-30; 21:8 na kuendelea
   8. Amosi 1:6, 9
D. Unabii dhidi ya Edomu.
   1. Isa. 34:5 na kuendelea; 63:1 na kuendelea
   2. Yer. 49:7-22
   3. Maombolezo 4:21-22
   4. Ezek. 25:12-14; 35:1-15; 36:2-6
   5. Amosi 1:11-12
E. Katika Obadia, Edomu alishutumiwa
   a. Majivuno yake, mistari ya 3-4
   b. katika ulinzi wa kijiografia
   c. katika ushirika wa kisiasa na nguvu za kijeshi
   d. katika mali za biashara
   e. katika hekima za kidesturi
2. Kuvunja kwake sheria huko Yuda, ndugu zake, Obadia mistari ya 10-14
   a. alifurahi juu ya kuanguka kwa Yerusalemu (Maombolezo 2:15-17; 4:21)
   b. walikataa kusaidia (Obadia mstari wa 11)
   c. kushiriki vyema kwa adui (Obadia mstari wa 14)
   d. walichukua mali za Yuda (Yer. 13:19)
3. kukataa kwake na kumpuuzia YHWH (Obadia mistari ya 16)
F. inaweza kuwa kiwakilishi (aina) kwa mataifa yote ambayo wanamwasi Mungu na watu wake, Obadia mistari ya 15-21 (kama vile Zaburi 2).
G. Uwezekano wa utimilizwaji wa unabii huu
   1. kuharibiwa kwa Edomu na Babeli ya kisasa takribani miaka 5 baada ya anguko la Yerusalemu mwaka 580 k.k.
   2. kuondolewa na kuhamishwa kwa Edomu kutoka Petra kulikofanywa na Waarabu wa Nabatean takribani miaka ya 550-449 k.k (kama vile Mal. 1:2-5). Edomu hatajwi katika orodha ya Nehemia ya maadui waliomzunguka, lakini anawekewa mbadala na makabila ya kiarabu. Edomu anahamia Negebu.
   3. kushindwa kwa Edomu kulikofanywa na makamanda wa kijeshi wa Alexander Antigonus mwaka 312 k.k (inaandikwa katika Diodorus Seculus)
   4. kushindwa kwa Edomu katika Negebu kulikofanywa na Judah Makabayo takribani 175 k.k (kama vile I Makabayo 5.3,15; II Makabayo 10.15; Maandiko ya kale ya Josephus ya wayahudi 12.8.1; 13.9.1
   5. Edomu analazimishwa akubali dini ya Kiyahudi kulikofanywa na John Hyrcanus mwaka 125 k.k. Sasa

wanaitwa wa-Idumeans.
6. Kamanda wa Kirumi, Titus, kwa asilimia zote za ushawishi wa wa-Idumean mwaka wa 70 b.k.

◙**"Bosra"** Huu ulikuwa mji mkuu huko Edomu, mara nyingi haya ndio yalikuwa makao yake makuu. Mara nyingi huu unatajwa katika maono ya hukumu ya "Ole" (kama vile Isa. 34:6; 63:1; Yer. 49:13,22; Amosi 1:12).

◙
**NASB, NRSV,**
**TEV, NJB"watembeao"**
**NKJV "waenendao"**
**JPSOA "waendao kwa haraka"**
**REB "wapigao hataua"**
Katika 51:14 hili neno( צעה, BDB 858, KB 1040) linaeleweka kama "kuinama," lakini ni kwamba hapa, maana nyingine haiendani. Wengine wanapendekeza mabadiliko kwenye mzizi wa neno, צעד(KB 1040), ambalo linamaanisha "kutembea" au "kupiga hatua." Toleo la UBS Text Project linalipa neno "kuinama " daraja B, lakini neno hili haliendani na ufanano uliopo.

**63:3 "shinikizoni"** Hii taswira ya hukumu pia inapatikana katika Omb. 1:15; Yoeli 3:13; Ufu. 14:19,20; 19:15. Huyu ni Mungu/Masihi kama Mpiganaji wa Kiungu.

**63:4** Tambua namna siku ya kisasi (kama vile 34:8; 35:4,8; 61:2) ilivyo ya muhimu kwa mjumbe wa siku hiyo (mwaka) ya ukombozi!

Siku ya Bwana na siku ya wokovu ni pande mbili za yule ajaye! Kwa ujio wa Mungu mwaminifu ni umoja wa ushirikamwingine mkuu; kwa wale ambao sio waaminifu, ujio wake ni tendo la mwisho la utengeufu na ukataliwaji (kama vile Mt. 25:31-46; Ufu. 20:11-15)!

**63:5 "mkono wangu mwenyewe uliniletea wokovu,**
**Ghadhabu yangu ndiyo iliyonitegemeza"** Kipengele hiki kinahusiana na mistari ya1-2. YHWH hawezi kuutegemea msaada wa mwanadamu katika kuuleta wokovu. Yeye pekee ndiye awezaye kulifanya hili (kama vile Eze. 36:22-38). Ndiko hili linaweza kuwa taswira ya Mtume Yohana aliyoitumia katika kitabu cha Ufunuo 5, yeye pekee ndiye astahiliye kukifunua kitabu, yeye pekee, aliyesulibiwa, Mwana-Kondoo wa Mungu aliyefufuka/Masihi/Mtumishi!

**63:6** Hukumu yaYHWH inafafanuliwa kwa matumizi ya stiari tatu (yaani, YHWH kamaMpiganaji wa Kiungu, kama vile 59:17; Kut. 15:3).
1. Nikazikanyaga – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 100, KB 115 (kifungu hiki kinafananishwa na neno "anayekwenda," lililotumika mara tatu katika mist. ya 2-3)
2. Nikawalevya – *Piel*ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 1016, KB 1500 (hukumu kama ulevi, kama vile 51:22-23; Zab. 75:8)
3. nikaimwaga (kif. "nikaimwaga mvinyo yao chini") – *Hiphil*ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 432, KB434 (watu waliokufa wasio waaminifu)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 63:7-14**
[7] **Nitautaja wema wa Bwana,**

**sifa za Bwana kwa yote aliyotukirimia Bwana;**
**na wingi wa wema wake kwa nyumba ya Israeli,**
**aliowakirimia kwa rehema zake, na kwa wingi wa wema wake.**
**8 Maana alisema, Hakika ndio watu wangu hawa, wana wasio na hila;**
**akawa Mwokozi wao.**
**9 Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa;**
**kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe;**
**akawainua, akawachukua siku zote za kale.**
**10 Lakini wakaasi, wakamhuzunisha Roho yake Mtakatifu;**
**kwa hiyo akawageukia, akawa adui, akapigana nao.**
**11 Ndipo alipozikumbuka siku za kale, za Musa,**
**na watu wake, akisema,**
**Yuko wapi yeye aliyewapandisha toka baharini pamoja na wachungaji wakundi lake?**
**Yuko wapi yeye aliyetia kati yao Roho yake Mtakatifu?**
**12 Aliyewaongoza kwa mkono wake mtukufu, kwa mkono wa kuume wa Musa?**
**Aliyeyatenga maji mbele yao, ili ajifanyie jina la milele?**
**13 Aliyewaongoza vilindini, kama farasi jangwani, wasijikwae?**
**14 Kama ng'ombe washukao bondeni, Roho ya Bwana akawastarehesha;**
**ndivyo ulivyowaongoza watu wako, ili ujifanyie jina lenye utukufu.**

**63:7 "wema wa Bwana"** Hili ni agano maalum la NOMINO,*hesed*. Tazama Mada Maalum katika 40:6.

◙**" na" Tambua namna toleo la** NASB linavyolitumia neno hili mara tatu kwa kutoa sifa pambanuzi za YHWH.

1. wingi wa wema wake
2. kwa rehema zake
3. kwa wingi wa wema wake

**63:8 "watu wangu hawa" Hii ni lugha ya kimaagano** (kama vile Kut. 6:7; Isa. 51:4).

◙**"wana wasio na hila"** Huu ni ukinzani halisi wa**1**:2-3 (kama vile Yer. 3:22).

◙**"akawa Mwokozi wao"** Elewa tofauti iliyopo kati ya mist. ya5 na 8b. Ijapokuwa Ukuu wa Mungu unasistizwa, hapo bado ni nafasi ya uaminifu wa Israeli!

**63:9 "Katika mateso yao yote yeye aliteswa"** Katika lugha ya Kiingereza huu ni usemi wenye nguvu wa umoja kati ya YHWH na watu wake wa agano (kama vile 57:15), lakini toleo la MT ni gumu kulifuatia.

1. Hiki kifungu kinaweza kuhusiana na ibara ya mwisho ya mst. wa 8 (NRSV, TEV).
2. Hiki kifungu kinaweza kuhusiana na ibara ya pili ya mst. wa 9 (NJB).

Toleo la MT lina neno "si" לא lakini wanazuoni wa Kimasoreti wanapendekeza לו, neno "yeye" (*qere*, JPSOA).

◙**" malaika wa uso wake"** Hili ni dokezo la moja kwa moja la Kut. 23:20-23; 33:14,15. Hili linadokeza juu ya matukio yaliyotukia katika Kipindi cha Kutangatanga Jangwani. Dhambi ya Israeli ilimsababisha YHWH kujiondoa katika mwonekano binafsi (yaani,malaika wa Bwana).
YHWH aliuthibitisha uwepo wake wa kipekee (kama vile Kumb. 32:9-14).

1. aliwakomboa – *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 145, KB 169

2. akawainua – *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU*,* BDB 642, KB 694
3. akawachukua– *Piel* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 669, KB 724 (kama vile 46:3; Kumb. 1:31)

Pia zitambue Nafsi tatu za Uungu za Agano Jipya katika mist. ya 9-10.

1. Baba, mst. wa 9a
2. Masihi alitangulia kulivaa umbo-mwli, mist. 9b
3. Roho Mtakatifu, mst. wa 10b

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

F. Injili
  3. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
  4. Yohana 14:26

G. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39

H. Paulo
  9. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
  10. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
  11. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
  12. Gal. 4:4-6
  13. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
  14. 1 The. 1:2-5
  15. 2 The. 2:13
  16. Tit. 3:4-6

I. Petro – 1 Pet. 1:2

J. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

B. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
  3. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
  4. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7

F. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
  5. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
  6. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
  7. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
  8. Zakaria 3:1-2

G. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14

H. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12

I. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10

J. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

5. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
6. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
7. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
8. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na

Roho
Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

4. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
5. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
6. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho

**63:10** Vitambue VITENZI viwili vinavyoifafanua dhambi yaIsraeli na VITENZI viwili vinavyoupambanua mwitikio wa YHWH (ufanano wa kivisawe).

1. wakaasi– *Qal* ya KAULI TIMILIFU, BDB 598, KB 632
2. wakamhuzunisha Roho wake Mtakatifu – *Piel* ya KAULI YA WAKATI ULIOPO, BDB 780, KB 864 (kama vile Matendo 7:51; angalia Mada Maalum: Utu wa Roho katika 42:1; kwa kiambata kizuri kilichoambatanishwa "Roho Mtakataifu wa Agano la Kale ni Nani?" tazama *Hard Sayings of the Bible*, kr. 273-274, pia kr. 306-207)
3. akawageukia, akawa adui– *Niphal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 245, KB 253, kama vile Kut. 23:22; Omb. 2:4-5
4. akapigana nao – *Niphal ya* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 535, KB 526

**63:11-14** Sehemu hii inaorodhesha mambo aliyoyatendaYHWH kwa ajili ya Israeli wakati wa kipindi cha uhamisho.

1. Aliyewapandisha toka baharini (kama vile Kutoka 14-15)
2. Aliyetia kati yao Roho wake Mtakatifu(kama vile Hes. 11:17,25,29; Hagai 2:5)
3. Aliyewaongoza kwa mkono wake mtukufu, kwa mkono wa kuume wa Musa(kama vile Kut. 6:6; 15:16)
4. Aliyeyatenga maji mbele yao
   a. Bahari ya Damu – Kutoka 14-15 (Isa. 11:15; 51:10)
   b. Mto Yordani – Yoshua 3
5. Aliyewaongoza vilindini(sawa na #4)
6. Akawastarehesha (yaani, Roho Mtakatifu, kama vile Yos. 21:44; 23:1)
7. Ulivyowaongoza watu wako

YHWH aliyatenda haya yote kwa ajili ya Israeli "ili ujifanyie jina lenye utukufu." YHWH alitaka kujifunua kwa wanadamu wote kupitia Israeli. Matendo yake kwao yalikuwa ni kwa ajili ya wingi wa wema wake (yaani, mpango wa ukombozi wa milele, tazama Mada Maalum katika 40:15).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 63:15-19**
**15 Tazama toka mbinguni, ukaone toka makao ya utukufu wako na fahari yako;**
**uko wapi wivu wako, na uweza wako?**
**Shauku ya moyo wako, na huruma zako zimezuiliwa kwangu.**
**16 Maana wewe ndiwe Baba yetu, ijapokuwa Ibrahimu hatujui,**
**wala Israeli hatukiri;**
**wewe, Bwana, ndiwe Baba yetu, mkombozi wetu tangu milele ndilo jina lako.**
**17 Ee Bwana, mbona umetukosesha njia zako,**

**ukatufanyiza kuwa na mioyo migumu hata tusikuogope?**
**Urudi kwa ajili ya watumishi wako, kabila za urithi wako.**
**18Watu wako watakatifu waliumiliki kwa kitambo tu;**
**adui zetu wamepakanyaga patakatifu pako.**
**19Tumekuwa kama watu usiowamiliki kamwe;**
**kama watu wasioitwa kwa Jina lako.**

**63:15 "Tazama. . . ukaone**" Hizi ni KAULI mbili SHURUTISHIzenye kuhitaji umakini kwa YHWH.

1. tazama – *Hiphil ya* KAULI SHURUTISHI, BDB 613, KB 661, kama vile Kumb. 26:15
2. ukaone – *Qal ya* KAULI YA WAKATI SHURUTISHI, BDB 906, KB 1157, kama vile Zab. 80:14

◙**"makao ya utukufu wako na fahari yako"** Hii ni namna ya kuzungumzia hekalu**.** Kwa Waisraeli wa kale, Sanduku la Agano lilikuwa miguu ya YHWH, ambapo waliamini kuwa aliishi mbinguni (kama vile I Nya. 28:2; Zab.99:5; 132:7; Isa. 66:1; Omb. 2:1; Mt. 5:35; Matendo 7:49).
Kitabu kipya kilichoandikwa na John Walton, *The Lost World of Genesis One*, kinadai kwamba Mwanzo. 1:1-2:3 YHWH analijenga hekalu lake.

◙**"Shauku ya moyo wako, na huruma zako zimezuiliwa kwangu"** Huu ushairi wenye nguvu unaibainisha Yerusalemu yenye kumshawishi YHWH ili kwamba aitambue na kuigeukia mara nyingine.

**63:16 "wewe ndiwe Baba yetu"** Hili ni hitimisho la kimantiki kutokana naIsraeli kuitwa "wana" (yaani, 1:2). Hiki kifungu kinarudiwa katika 64:8.

## MADA MAALUM : UBABA WA MUNGU

I. Agano la Kale
   A. kuna maana kuwa Mungu ni Baba kwa maana ya uumbaji.
      1. Mwa. 1:26-27
      2. Mal. 2:10
      3. Mdo. 17:28
   B. Baba ni ushabihiano uliotumika katika maana mbalimbali.
      1. baba wa Israeli (kwa kuchaguliwa)
         a. "Mwana" – Kut. 4:22; Kumb. 14:1; Isa. 1:2; 63:16; 64:8; Yer. 3:19; 31:9,20; Hosea 1:10; 11:1; Mal. 1:6
         b. "mzaliwa wa kwanza" – Yer. 31:9
      2. baba wa mfalme wa Israeli (kwa maana ya Kimasihi)
         a. 2 Sam. 7:11-16
         b. Zab. 2:7; Mdo. 13:33; Ebr. 1:5; 5:5
         c. Hosea 11:1; Mt. 2:15
      3. mshabihiano wa kuwapenda wazazi
         a. baba (stiari)
            1) abebavyo mwanae – Kumb. 1:31
            2) kumwadibisha – Kumb. 8:5; Mith. 3:12
            3) mtoaji (yaani., Kutoka) – Kumb. 32:6
            4) hatawasahau – Zab. 27:10
            5) huwapenda – Zab. 103:13
            6) rafiki/mlinzi – Yer. 3:4

7) mponyaji/mwenye kusamehe – Yer. 3:22
8) hukupa rehema – Yer. 31:20
9) mfundishaji – Hosea 11:1-4
10) mwana wa pekee – Mal. 3:17

b. mama (stiari)
1) hatawasahau – Zab. 27:10
2) upendo wa mama aleaye – Isa. 49:15; 66:9-13 na Hosea 11:4 (pakiwepo na mpango wa marekebisho ya kimuktadha wa neno "nira" kwenda "mtoto mchanga")

II. Agano Jipya
A. Utatu (maandiko yote matatu yametaja)
1. Injili
a. Mt. 3:16-17; 28:19
b. Yohana 14:26
2. Paulo
a. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
b. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
c. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
d. Gal. 4:4-6
e. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4
f. 1 The. 1:2-5
g. 2 The. 2:13
h. Tito 3:4-6
3. Petro – 1 Pet. 1:2
4. Yuda – Mistari ya 20-21

B. Yesu
1. Yesu kama "mwana apendezwaye nae" – Yohana 1:18; 3:16,18; 1 Yohana 4:9
2. Yesu kama "Mwana wa Mungu" – Mt. 4:3; 14:33; 16:16; Luka 1:32,35; Yohana 1:34,49; 6:69; 11:27
3. Yesu kama mpendwa – Mt. 3:17; 17:5
4. Matumizi ya Yesu ya neno *abba* kwa ajili ya Mungu – Marko 14:36
5. matumizi ya Yesu ya VIHISISHI kuonyesha vyote kuhusu Yeye na uhusiano wetu na Mungu
a. "Baba Yangu," mf., Yohana 5:18; 10:30,33; 19:7; 20:17
b. "Baba yako," mf., Mt. 5:16,45,48; 6:1,4,6,8,9,14,15,18,26,32; 7:11; 10:20,29; 18:14
c. "Baba yetu," mf., Mt. 6:9,14,26

C. moja ya stiari nyingi za kifamilia kuelezea ushirika wa ndani kati ya Mungu na mwanadamu:
1. Mungu kama Baba
2. waamini kama
a. wana wa Mungu
b. watoto
c. wamezaliwa na Mungu
d. wamezaliwa mara ya pili
e. wameasiliwa
f. wamezaliwa
g. familia ya Mungu

**◙". . . ijapokuwa Ibrahimu hatujui**
**wala Israeli hatukiri"**

Mababa wa imani wasingeweza kuwajua/kuwatambua hawa Wayudea kwa sababu ya

1. kipindi kati ya vizazi vyao

2. dhambi za vizazi hivi

◙**"mkombozi"** Tazama maelezo katika41:14. Kwa dhana ya neno "mkombozi" tazama Mada Maalum katika 41:14.

**63:17** Hii mistari miwili ya mwanzo ya ubeti huu inaonyesha namna dhana ya ukuu wa Mungu inavyoweza kutumikakupunguza mamlaka binafsi. Tazama Mada Maalum: Uchaguzi/Maamuzi ya Kabla na Hitaji kwa Ajili ya Ulinganifu wa Kithiolojiakatika 44:18 naMaamuzi ya Kabla Dhidi ya Mapenzi Huru ya Mwanadamuhapa chini.

## MADA MAALUMU: MAAMUZI YA KABLA (CALVINISM) DHIDI YA MAPENZI HURU YA KIBINADAMU (ARMINIANISM)

Tito 2:11 Ni mlinganyo wa vifungu vingine vya Agano Jipya kwenye uchaguzi. Nilifikiri inaweza kuwa ya msaada wa kitheolojia kusaidia kutoa maelezo yangu ya kiufafanuzi kutoka kwa Warumi 8:29 na sura ya 9, pamoja na Waefeso 1.

I. Warumi 8:29 – Paulo anatumia "naliwajua kabla" (*proginōskō*, "kujua kabla") maradufu, hapa na 11:2. Katika 11:2 inamaanisha upendo wa Agano la Mungu kwa Israeli kabla ya wakati kuanza. Kumbuka kwamba neno "kujua" kwa kiebrani linahusiana na uhusiano binafsi,wa ndani, sio kumwambia ukweli kuhusu mtu fulanii (kama vile Mwa. 4:1; Yer. 1:5). Hapa ilikuwa imejumuisha katika mlolongo wa matukio ya milele (kama vile. Waru. 8:29-30). Neno hili lilihusishwa na kuamuliwa kabla. Hata hiyo, ni lazima ieleweke kwamba maarifa ya Mungu ya mambo yajayo sio msingi wa uchaguzi kwa sababu ikiwa ni hivyo, basi uchaguzi utakua umeegemea katika mwitikio wa baadaye wa binadamu uliyeanguka, ambao utakua utendaji wa kibinadamu. Neno hili pia linapatikana katika Matendo 26:5; Pet 1. 1:2,20 na Pet 1. 3:17.

   A. "aliowajua tagu asili" (*proginōskō*, "kujua kabla")

      Maneno "aliowajua tangu asili" na "aliwachagua tangu asili"yote ni maneno ambatani pamoja na kihusishi "kabla" na, kwa hiyo inapaswa kutafsiriwa, "kujua kabla ," "kuweka mipaka kabla," au "alama kabla." Vifungu ya uhakika juu ya kuamuliwa kabla katika Agano Jipya ni Warumi. 8:28-30; Waef. 1:13-14; na Warumi 9. Maandiko haya ni dhahiri kusisitiza kwamba Mungu ni Mfalme.Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu yote. Kuna mpango wa ki-Uungu uliowekwa tayari ili kufanywa kwa wakati. Hata hivyo, mpango huu sio wa kiholela wala kuchagua. Inategemea sio tu juu ya Ufalme wa Mungu na ujuzi wa asili, lakini kwa tabia yake isiyobadilika ya upendo, huruma, na neema isiyostahili. Tazama Mada Maalumu: YHWH's Mpango wa Ukombozi wa Milele.

      Tunapaswa kua makini na ubinafsi wetu wa magharibi (Amerika) au moyo wetu wa uinjilisti wa kuulemba ukweli huu wa ajabu. Tunapaswa pia kulindwa dhidi ya kukingamizwa ndani ya historia, kitheolojia kati ya Augustine dhidi ya Pelegius au Calvinism dhidi ya Arminianism.

   B. "imeamriwa kabla" (*proorizō*, "kuweka mipaka kabla")

      Kuamriliwa kabla sio mafundisho yenye maana ya kupunguza upendo wa Mungu, neema, na huruma wala kuwatenga wengine kutoka kwenye injili. Ilikuwa na maana ya kuimalisha wanaoamini kwa kuunda maoni yao ya ulimwengu. Mungu ni kwa ajili ya binadamu wote (kama vile. Yohana 1:12; 3:16; Tim 1. 2:4; Petro 2. 3:9; Yohana 1. 2:2; 4:14).Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu vyote. Nani au nini kinachoweza kututenganisha na yeye (kama vile Warumi. 8:31-39)? Mungu anaona historia yote mambo yaliyopita kama yapo sasa; binadamu ni kiumbealiyefungwa na muda. Mtazamo wetu na uwezo wa akili ni wenye mipaka/kikomo. Hakuna kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, Ni muundo wa Agano. Huu ni mfano mwingine uliotolewa katika mvutano wa lahaja. Mafundisho ya kibiblia yanatolewa kwa mtazamo tofauti. Mara nyingi huonekana fumbo la maneno. Ukweli ni mlinganyo kati ya jozi zilizo kinyume. Hatupaswi kuondoa mvutano kwa kuchukua moja ya ukweli. Hatupaswi kutenganisha ukweli wowote wa Kibiblia ndani ya chumba.

      Ni muhimu kuongeza kwamba lengo la uchaguzi sio mbinguni tu wakati tunapokufa,lakini mapenzi

ya Kristo sasa. (kama vile Warumi. 8:29-30; Wakorintho 2. 3:18; Gal. 4:19; Waefeso. 1:4; 2:10; 4:13; The. 1. 3:13; 4:3; 5:23; The 2. 2:13; Tito 2:14; Pet 1. 1:15). Tumechaguliwa kuwa "watakatifu wasio na lawama." Mungu huchagua kutubadili ili wengine waweze kuona badiliko na kuitikia kwa imani kwa Mungu katika Kristo. Majaaliwa sio pendeleo la kibinafsi, bali ni wajibu wa Agano. Huu ni ukweli mkuu wa kifungu hiki. Hili ni lengo la Ukristo. Utakatifu ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini. Uchaguzi wa Mungu ni mapenzi ya Kristo (kama vile. Waefeso 1:4),sio msimamo maalumu. Mfano wa Mungu ulotolewa kwa binadamu katika uumbaji (kama vile. Mwanzo. 1:26; 5:1,3; 9:6), ni kurejeshwa.

C. "kubali kugeuzwa kwa mfano wa mwanawe"—Lengo kuu la Mungu ni kurejesha picha iliyopotea kwenye anguko. Waamini wamewekwa mbele kwa mapenzi ya Kristo kama vile. Waefeso. 1:4).

II. Warumi 9

A. Warumi 9 ni mojawapo ya kifungu cha Agano Jipya juu ya Ufalme wa Mungu (mwingine kuwa Waef. 1:3-14), wakati sura ya 10 inasema kuwa uhuru wa binadamu ni dhahiri na hujirudia mara kwa mara (kama vile. "kila mtu" War. 9:4; "kila mtu" 9:11,13; "wote" 9:12 [maradufu]). Paulo kamwe hakujaribu kupatanisha mvutano huu wa kitheolojia. Wote ni wa ukweli! Mafundisho mengi ya Biblia yanawasilishwa kwa fumbo la maneno au jozi za lahaja. Mifumo mingi ya theolojia ni yenye mantiki na nusu ya ukweli . Augustinianism na Calvinism dhidi ya nusu-Pelegianism na Arminianism zina misingi ya ukweli na yenye makosa. Mvutano wa kibiblia kati ya mafundisho ni bora kwa maandishi ya ushahidi, yenye kutangazwa kama imani ya kanisa, ya kimantiki, ya mfumo wa kitheolojia ambayo inasisitiza Biblia kwenye mstari wa ramani iliyoelezea kabla.

B. Ukweli huo huo (unapatikana katika Warumi. 9:23) umeelezwa katika Warumi. 8:29-30 na Waefeso. 1:4,11. Sura hii ni maelezo yenye nguvu zaidi ya uweza wa Mungu katika Agano Jipya. Haiwezi kuwapo na migogoro kwa vile Mungu ndiye muhusika wa jumla wa uumbaji na Ukommbozi. Ukweli huu mkubwa haupaswi kamwe kufutwa au kupunguzwa. Hata hiyo, ni lazima pawepo na mlinganyo na uchaguzi wa Mungu wa agano kama njia ya kuhusianisha na uumbaji wa mwanadamu, uliofanywa kwa mfano wake. Kama vile Mwanzo 15 isiyokuwa na masharti na haihusiani kabisa na majibu ya mwanadamu, lakini maagano mengine yenye masharti juu ya majibu ya binadamu (mf., Edeni, Nuhu, Musa, Daudi).Mungu ana mpango wa ukombozi kwa uumbaji wake;hakuna mwanadamu anayeweza kuathiri mpango huu. Mungu amechagua kuruhusu watu binafsi kushiriki katika mpango wake. Nafasi hii ya ushiriki ni mvutano wa kitheolojia kati ya Ufalme( Warumi 9) na mapenzi ya Kibinadamu (Warumi 10).

Sio sahii kuchagua msisitizo mmoja wa Biblia na kupuuza mwingine. Kuna mvutano kati ya mafundisho kwa sababu watu wa mashariki wanawasilisha kweli katika lahaja na jozi kujaza mvutano. Mafundisho lazima yafanyike katika mahusiano na mafundisho mengine. Ukweli ni kweli za Musa.

III. Waefeso 1

A. Uchaguzi ni mafundisho ya ajabu. Hata hivyo si wito kwa upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa ajili ya huduma; katika agano jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia haipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa Kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile 10:11,13).

Umuhimu wa mvutano huu wa kitheolojiaunaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni "ndiyo" ya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo).Mara nyingi

sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!

Mafundisho huja huja kutokana na kweli zingine, sio kama moja, lisilohusiana na ukweli. Mfuatano mzuri ungalikuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika namna ya kimashariki na sio kimagharibi. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho ( Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu aliye dhahili: usalama dhidi ya uvumilivu;Yesu aliye sawa na Mungu baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu; Uhuru wa kikristo dhidi ya wajibu wa kikristo kwa mwenzi wa agano, nakadharika).

Dhana ya kitheolojia ya "agano" inaunganisha Uweza wa Mungu (ambaye daima huchukua hatua kwa kuweka mswada) wenye mwanzo muhimu na mwendelezo wa mwitikio wa imani ya toba kutoka kwa mtu. Kuwa mwangalifu na uhakiki wa maandiko wa upande mmoja na kupuuza mwingine! Kuwa mwangalifu wa kuthibitisha mafundisho yako pendwa au mfumo wa theolojia.

B. "alivyotuchagua" katika Efe. 1:4 ni KAULI YA KATI ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFUambayo inasisitiza somo. Hii inalenga katika uchaguzi wa Mungu kabla ya wakati. Chaguo la Mungu halipaswi kueleweka kwa maana ya kiislamu ya falsafa za maamuzi.Mungu aliahidi kuwakomboa wanadamu walioanguka (kama vile. Mwanzo 3:15). Mungu alimwita na kumchagua Ibrahimu kuchagua wanadamu wote (kama vile. Mwanzo 12:3; Kutoka. 19:5-6).

Mungu mwenyewe alichagua wanadamu wote ambao wangetenda imani katika kristo. Mungu daima huchukua maamuzi mwenyewe katika wokovu (kama vile. Yohana 6:44,65). Nakala hii na Warumi 9 ni msingi wa Kibiblia kwa mafundisho ya majaaliwa yaliyosisitizwa na Augustine na Calvin.Mungu alichagua wanaoamini si tu kwa wokovu (kuhesabiwa haki), lakini pia kwa utakaso (kama vile. Wakolosai 1: 10-12).

Hii inaweza kuhusiana na (1) nafasi yetu katika Kristo (kama vile. Wakorintho 2. 5:21) au (2) Nia ya Mungu kuzalisha tabia yake katika wana wake (kama vile. Waef. 2:10; Warumi. 8:28-29; Wagalatia. 4:19). Mapenzi ya Mungu kwa wana wake ni kuwaona wote mbinguni siku moja na kufanana na Kristo sasa!

"katika yeye" ni dhana muhimu ya Efe . 1:4. Baraka za Mungu, neema, na wokovu hupitia kwanjia ya kristo (kama vile. Yohana 14:6). Angalia kurudia rudia kwa umbo hili la kisarufi (ENEO LA MAHALI) katika Waefeso. 1:3, "katika kristo"; 1:4, "katika yeye"; 1:7, "katika yeye"; 1:9, "katika yeye"; 1:10, "katika kristo," "katika yeye"; 1:12, "katika kristo" na 1:13, "katika yeye" (maradufu).Yesu ndiye mwanadamu aliyechaguliwa na wote wanawezekana kuchaguliwa ndani yake. Wote wa Mungu Baraka za Baba zinapatikana katika Kristo.

Maneno "kabla ya msingi wa Dunia" pia hutumiwa katika Mt. 25:34; Yohana 17:24; Pet 1. 1:19-20 na Ufu. 13:8. Inaonyesha nafsi tatu kwa moja ya shughuli ya ukombozi wa Mungu hata kabla ya Mwanzo. 1:1. Binadamu anakikomo kwa maana za wakati; kila kitu kwetu ni cha muda uliopita, wa sasa,na wa baadaye, lakini si kwa Mungu.

Lengo la kuamua kabla ni utakatifu sio pendeleo. Wito wa Mungu sio wa wachache waliochaguliwa wa wana wa adamu, bali kwa wote! Wito ulikuwa ni kile Mungu alichotaka mwanadamu kuwa kama yeye mwenyewe (kama vile1 Wathesalonike 5:23; 2 Wathesalonike 2:13);katika sura yake (kama vile. Mwanzo 1:26-27). Ili kugeuza majaaliwa kuwa katika kanuni ya theolojia badala ya maisha takatifu kuwa janga. Mara nyingi theolojia yetu huzungumza kwa sauti zaidi kuliko maandiko ya Kibiblia.

Neno "wasio na lawama" (*amōmos*) au "bila lawama" linatumika

1. Yesu (kama vile. Waebrania 9:14; Pet 1. 1:19)
2. Zekaria na Elisabeti (kama vile Luka 1:6)
3. Paulo (kama vile. Wafilipi 3:6)
4. wakristo wote wa kweli (kama vile. Wafilipi. 2:15; Wathesalonike 1. 3:13; 5:23)

Mapenzi ya Mungu yasiyowezekana kubadilika kwa kila Mkristo sio baadaye mbinguni tu, lakini ni mapenzi ya kristo sasa (kama vileWarumi 8:29-30; Wagalatia 4:19; Pet 1. 1:2). Wanaoamini wanapaswa kuitazamisha tabia ya Mungu kwa ulimwengu uliopotea kwa dhumuni la Uinjilisti.

Kisarufi maneno “katika upendo” katika Tito 2:2 yanaweza kwenda pamoja na Tito 2:4 au 5. Hata hivyo wakati maneno haya yanatumika katika maeneo mengine katika Waefeso daima yanahusu upendo wa Kibinadamu kwa Mungu (kama vile Waefeso 3:17; 4:2,15,16).

C. Katika Waefeso 1:5 neno "alitangulia kutuchagua" ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Neno hili la Kiyunani ni neno ambatani kwa “kabla” na “alama kabla.” Inahusu mpango wa ukombozi wa Mungu uliotanguliwa kabla (kama vile Luka 22:22; Matendo 2:23; 4:28; 17:31; Warumi 8:29-30). Majaaliwa ni moja ya ukweli kadhaa kuhusiana na wokovu wa mwanadamu. Ni sehemu ya kikolezo cha kitheolojia au mfululizo wa ukweli unaohusiana. Haikuwa na maana ya kusisitizwa katika kutengwa! Kweli ya Kibiblia imetolewa katika mfululizo wa mvutano wa anguko, jozi za fumbo la maneno. Ufuasi wa kimadhehebu umejaribu kuondoa mvutano wa kiibiblia kwa kusistiza kweli moja tu ya ukweli wa lahaja (majaaliwa dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu ; usalama wa mwamini dhidi ya uvumilivu wa watakatifu; dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari; kutokuwa na dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo; utakaso wa mara moja dhidi ya utakaso wa kuendelea;imani dhidi ya kazi; Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo; Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu wa asili).

Uchaguzi wa Mungu haukutegemea ujuzi wa mbele wa utendaji wa mwandamu, lakini kwa tabia yake ya neema (kama vileEfe. 1:7,9,11). Alitamani kwamba wote (hapana mmoja kama mwenye mafunuo) angeokolewa (kama vile Ezek. 18:21-23,32; Yohana 3:16-17; Tim 1. 2:4; 4:10; Tito 2:11; Pet 2. 3:9; Yohana 1. 2:2; 4:14). Neema ya Mungu (tabia ya Mungu) ni muhimu kitheolojia kwa kifungu hiki (kama vileEfe. 1:6a, 7c, 9b), kama huruma ya Mungu ni muhimu kwa kifungu kingine juu ya kuamuliwa kabla kwa mambo, Warumi 9-11.

Tumaini pekee la wanadamu walioanguka ni neema na huruma ya Mungu (kama vile. Isay. 53:6 na nyingine kadhaa za Agano la Kale zilizotajwa katika Warumi. 3:9-18). Ni muhimu sana kwa kutafsiri sura hizi za kwanza za kitheolojia ili kutambua kwamba Paulo anasisitiza mambo hayo ambayo hayahusiani kabisa na utendaji wa mwanadamu: kuamuliwa kabla kwa mambo (Waefeso 1), neema (Waefeso 2), na mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu (Ajabu, Waefeso 2:11- 3:13). Hii ilikuwa ni kusawazisha mkazo wa walimu wa uongo juu ya sifa ya binadamu na kiburi.

◙**“Urudi kwa ajili ya watumishi wako”** Hii ni*Qal*ya KAULI SHURUTISHI(BDB 996, KB 1427) inayotumika kama maombi.

**63:18-19** Hii mistari inaonyesha namna Wayudea walivyojitambua.

1. waliumiliki kwa kitambo tu
2. adui zetu wamepakanyaga patakatifu pako
3. Tumekuwa kama watu usiowamiliki kamwe
4. kama watu wasioitwa kwa Jina lako

# ISAYA 64

| MIGAWANYO YAAYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maombi kwa ajiri ya Rehema na msaada | Maombi ya toba<br>(63:15-64:12) | Zaburi ya kusihi<br>(63:7-64:12) | Maombi kwa ajiri ya rehema na msaada<br>(63:15-64:12) | Tafakuri ya Israeli katika historia<br>(63:7-64:12) |
| | | | | (63:19b-64:12) |
| | | | 63:18-64:7 | |
| 64:1-7<br>(1-7) | 64:1-5<br>(1-5) | 64:1-12 | | |
| | 64:6-7<br>(6-7) | | | |
| 64:8-12<br>(8-12) | 64:8-12<br>(8-12) | | 64:8-12 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk.wa xxiv kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

25. Aya ya kwanza
26. Aya ya pili
27. Aya ya tatu
28. Nk

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 64:1-7**
**1Laiti ungepasua mbingu, na kushuka,**
**ili milima iteteme mbele zako;**
**2kama vile moto uchomapo vichaka, na moto uchemshapo maji;**
**ili kuwajulisha adui zako jina lako,**
**mataifa wakatetemeke mbele zako!**
**3Ulipofanya mambo ya kutisha tusiyoyatazamia,**
**ulishuka, milima ikatetema mbele zako.**
**4Maana tangu zamani za kale watu hawakusikia, wala kufahamu kwa masikio,**
**wala jicho halikuona Mungu, ila wewe,**
**atendaye mambo kwa ajili yake amngojaye.**
**5Wewe wamlaki yeye afurahiaye yaliyo haki na kuyatenda,**
**watu wale wakukumbukao katika njia zako;**
**tazama, ulikuwa na hasira, nasi tulitenda dhambi;**

**tumekuwa katika mambo haya muda mwingi;**
**nasi, je! Tutaokolewa?**
**6Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu,**
**na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi;**
**sisi sote twanyauka kama jani,**
**na maovu yetu yatuondoa, kama upepo uondoavyo.**
**7Tena hapana aliitiaye jina lako,**
**ajitahidiye akushike;**
**kwa kuwa umetuficha uso wako,**
**nawe umetukomesha kwa njia ya maovu yetu.**

**64:1** Mistari miwili ya mwanzo ina utambulisho kama ule wa 63:19 katika toleo la MT. kuna mfuatano wa VITENZI TIMILIFU kutoka mst. 18 kupitia mstr. 19.

YHWH, aketiye juu, "hulipenya" (*Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 902, KB 1146, kama vile. 34:4; Ufu. 6:14) anga la Dunia (yaani.,mbinguni, kama vile Mwa. 1:1).

Kama Muumbaji ajitokezapo uumbaji hutetemeka (*Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 272, KB 272 [muundo huu unajitokeza hapa pekee na Rum. 5:5,ambazo ni sifa / Zaburi za Debora aliposhindwa Hazori na jeshi lake], kama vile. mst. 2; Zab. 18:7-15; 68:8; 77:18; 144:5)

kwa aijiri ya" mbingu " tazama Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM:MBINGU (AGANO LA KALE)

Neno la Kiebrania (BDB 1029, KB 1559, linalotafasiriwa kama "mbingu," "anga," "mbingu," "hewa") laweza kurejerea kwenye vitu mbalimbali (yaani., mfuatano wa kuba au tufe la uumbaji wa mwanzo):

1. katika Mwa. 1:8-20 laweza kurejerea kwenye anga-hewa juu ya nchi mahali pale mawingu hutembea na ndege kuruka.
2. huu mhimili (kama vile Mwa. 1:6,20; Isa. 40:22; 42:5) juu ya ardhi ndipo Mungu huitoa mvua (yaani., "madirisha ya mbinguni," kama vile Zab. 78:23-29; Mal. 3:10 au "mabirika ya mbinguni," kama vile Ayubu 38:37).
3. huu mhimili ndipo nyota hukaa na sayari huzunguka. Laweza kurejea ulimwengu mzima (lenye kujumuisha makundi ya nyota na sayari).
4. juu ya huu mhimili ndipo makazi ya Mungu (yaani., mbingu ya tatu au ya saba; angalia Mada Maalum: Mbingu na Mbingu ya Tatu). Ni mbingu iliyoko juu sana (mf., Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27,30,32; Zab. 2:4; 148:4; Isa. 66:1).
5. misisitizo ya kithiolojia
   a. Mungu ni muumbaji wa vitu vyote.
   b. huudhibiti uumbaji (yaani., nuru na giza, mvua na ukame).
   c. aliumba na kuweka mianga ya usiku (jua, mwezi, nyota, sayari, vimondo).
   d. kuna maeneo na falme za kweli:
      1) Nchi
      2) juu ya nchi
      3) vitu visivyoonekana/vya kimalaika (kama vile Kol. 1:16)
      4) uwepo wa Mungu na makazi
   e. vyote vinahusika na kutawaliwa na mapenzi yake

**64:2 "Moto"** tazama Mada Maalum katika 47:14.

◙ tambua  kusudi la  YHWH  ni kwamba jina lake lifahamike na mataifa watetemeke (matumaini katika toba, kama vile. Zab. 99:1-5; Yer. 33:9).

**64:3**
**NASB, NKJV,**
**NRSV, REB "mambo ya kushangaza "**
**TEV "mambo ya kutisha"**
**NJB "miujiza isiyotarajiwa"**
**JPSOA "maajabu"**

Neno laKiebrania (BDB 431, KB 432, *Niphal* KAULI ENDELEVU) ni dhahili lina maanisha ya "hofu," lakini katika muundo huu linadokeza Ukuu, miujiza ya kushangaza ya  YHWH mbele ya  Israeli (kama vile. Kumb. 10:21; 2 Sam. 7:23; 1 Kor. 17:21; Zab. 66:3,5-6; 106:22; 145:6).

Katika Zab. 139:14  maneno kadhaa ya Kiebrania yametumika sambamba.

1. BDB 431 – kutisha
2. BDB 811  na  810 – ajabu kuu

Tazama mada maalumu hapa chini.

## MADA MAALUM: MAMBO YA AJABU (פלא)

Neno (BDB 810, KB 927) linaonyesha kitendo ambacho wanadamu hawawezi kukitimiliza wao wenyewe au hata kukielezea, vitendo vyenye kusababisha maajabu na mshangao (kama vile Mwa. 18:14; Yer. 32:17,27; Zak. 8:6).

KITENZI

1. Waisraeli kuondoka Misri, Kut. 3:20; 34:10; Mika. 7:15
2. mapigo, Kumb. 28:59
3. kuvuka Mto Yordani, Yos. 3:5
4. mambo ya Mungu yaliyopita, Amu. 6:13; 1 Nya. 16:9,12,24; Neh. 9:17
5. kuzaliwa kwa Samson, Amu. 13:19
6. upendo wa Daudi kwa Yonathani, 2 Sam. 1:26
7. mara nyingi kwa Ayubu, 5:9; 9:10; 10:16; 37:5,14; 42:3
8. mara therathini na mbili katika Zaburi
9. baraza la YHWH, Isa. 28:29
10. matendo ya YHWH, Isa. 29:14 (mara mbili); Yoeli 2:26

NOMINO

1. kupewa ruhusa kwa Waisraeli ,Kut. 15:11; Zab. 77:11,14; 78:12
2. 2.kuhusiana na wafu, Zab. 88:10,12
3. mbingu zinasifu matendo ya YHWH, Zab. 89:5
4. sheria za YHWH, Zab. 119:129
5. Masihi wa YHWH, Isa. 9:6
6. matendo ya YHWH, Isa. 25:1; 29:14
7. matukio ya siku ya mwisho, Dan. 12:6

Mungu anatenda kwa namna ya ukombozi wenye nguvu kujidhihirisha Yeye Mwenyewe kwenye uumbaji wake (mwanadamu).  Anawahitaji waje kwake na kumwamini.  Matendo yake ni ufunuo, uwekaji kumbukumbu wa matendo hayo ni uvuvio, na kuyaelewa matendo hayo ni nuru.  YHWH anahitaji ulimwengu umujue Yeye! Angalia Mada Maalum zifuatazo.

1. Mada Maalum: Akamjua
2. Mada Maalum: Uvuvio
3. Mada Maalum: Nuru

**64:4** Swali la kufafanua ni nani ambao KIWAKILISHI NOMINO "wao" kinarejelea.

1. Taifa la Israeli
2. Waaminifu waliorejea
3. mataifa (kama vile. mst. 2)
4. namba 2 na namba 3 kwa pamoja

◙**"Mungu akiwa upande wako"** Angalia Mada Maalum: Imani ya Mungu Mmoja 40:14.

◙**"atendaye. . ."** Neno hili ni "afanyae" (*Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 793, KB 889). Huku ni kuonyesha utofauti wa thiolojia kati ya YHWH na sanamu. Sanamu haiwezi kuona, kusikia, kutenda, kuongea, lakini YHWH anaweza na kutenda!

◙**"kwa ajiri yake amngojaye"** Hii inamwelezea mtu wa imani. Yeye anaengojea (*Piel* KAULI ENDELEVU, BDB 314, KB 313). Neno hili lina kidokezo cha " matumaini, kuamini, kungojea" Mungu (kama vile. 8:17; 30:18; Hab. 2:3). Asili nyingine (BDB 875 I) pia imetafsiriwa "ngojea," lakini mara nyingi sio kama maana ya thiolojia (kama vile Isa. 25:9; 26:8; 33:2; 40:31; Zab. 25:3; 27:14; 37:34; 40:1; 130:5; Mit. 20:22).

**64:5 "wewe wamlaki yeye. . ."** KITENZI hiki (*Qal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU, BDB 803, KB 910) katika muktadha huu kinadokeza kukabiliwa na/kwa ajiri ya ushirika na / au huruma.

tambua aina ya watu YHWH "aliokutana " nao.

1. Yeye afurahiaye kwa kutenda haki
2. Watu wale wakukumbukao katika njia zako

Huu ni ufanano (tazama kiambatisho cha kwanza: shairi la Kiebrania).

◙ Mistari ya 3-5 inauliza swali la kufaa. Israeli ni watu waliovunja maagano. Watu watenda maovu wanaweza "kuokolewa" (yaani , "kukombolewa," BDB 446, KB 448)

1. Kutoka kwenye mwili wenye matokeo ya dhambi
2. Kutoka kwenye roho yenye matokeo ya dhambi

Nataka kuamini, "ndiyo,ndiyo,ndiyo" (kama vile Mist. 8-9)! Lakini Neema na Rehema za kiroho pekee (Sura hii ni maombi kwa ajiri ya YHWH kuingilia kati) zinaweza kutenda hivyo (andiko lenye kupendelewa ni la tafasiri ya UBS , uk. 164). Matokeo ya kitabu cha Mwa. 3 yanashangaza na yasiyotulia.

Hata hivyo, katika muktadha huu (yaani.,mist. 4-7)mistari hii si ya ukombozi lakini ya kuhukumu (mist. 8-12 ni kilio kwa ajili ya Rehema). Israeli wamefanya dhambi sasa na wakati uliopita. Kama hili litakubaliwa kwa maana hiyo KITENZI "kukombolewa" (ובושע, BDB 446, KB 448) lazima kibadilike kuwa "nasi tulitenda dhambi" (ונרשע, UBS Text Project, uk. 163; NET Bible, #16, uk. 1283).

◙

**NASB** **"tumekuwa katika mambo haya muda mwingi;**

**"nasi, je! Tutaokolewa"**

**NKJV** **"katika siku hizi tumeendelea'**

**"na tunahitaji kuokolewa"**

**NRSV** **"tuna hatia ndio sababu umeficha uso wako"**

**NJB** **"na sasa tumeendelea kuwepo kwenye njia yako tutaokolewa"**

**JPSOA** **" tumeinuka na kuanguka toka zamani**

**"na tunaweza kuokolewa?"**

**LXX** **"hivyo basi tumeenda mbali"**

Toleo la MT halijulikani .Toleo la AB linapendekeza marekebisho ya konsonanti mbili zenye kuzaa kifungu , "muda mwingi tumekuwa waasi" (uk. 190)

**64:6-7**Tambua matokeo ya dhambi.

1. Sisi sote – nafasi ya tatizo (kama vile Rum. 3:9-18,23; 11:32; Gal. 3:22)
2. Aliye mchafu (BDB 379)
3. matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi (nguo ya hedhi, BDB 723, kama vile. Law. 15:19-24)
4. twanyauka (BDB 614, KB 663, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile 1:30; 34:4) kama jani
5. upepo watuondolea mbali
6. hapana aliitiaye jina la Bwana (yaani .,kuabudu)

YHWH anawajibu watu hawa waovu wa maagano,inamaanisha anatangaza na kubainisha tabia yake.

1. Ameuficha uso Wake (kama vile. 1:15; 54:8; Kumb. 31:18)
2. Ametuleta sisi (toleo la MT neno "kuyeyuka," BDB 556, KB 555) chini ya utawala (yaani .,matokeo) ya uovu wetu (hili kithiolojia linafanana na Rum. 1:24,26,28!)

Mistari hii imetumika kama ombi la kukiri kosa. Hakuna sababu kwanini YHWH atasamehe / kusahau, lakini alifanya hivyo (kama vile. 55:6-7)! Maagano mapya yanaonekana hapa (kama vile. Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38). YHWH atahusika nao (yaani ., Israeli) na watu wote katika msingi mpya wa tabia yake, matendo yake,makusudi yake, kupitia kwa Roho na Mwana Wake!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 64:8-12**
**8 Lakini sasa, Ee Bwana, wewe u baba yetu;**
**sisi tu udongo, nawe u mfinyanzi wetu;**
**sisi sote tu kazi ya mikono yako.**
**9 Ee Bwana, usione hasira nyingi,**
**wala usiukumbuke uovu siku zote;**
**tazama, angalia, twakusihi, sisi sote tu watu wako.**
**10 Miji yako mitakatifu imekuwa jangwa,**
**Sayuni umekuwa jangwa,**
**Yerusalemu umekuwa ukiwa.**
**11 Nyumba yetu takatifu, nzuri,**
**walimokusifu baba zetu,**
**imeteketea moto;**
**vitu vyetu vyote vyenye kupendeza vimeharibika.**
**12 Utajizuia usiyaangalie mambo haya, Ee Bwana?**
**Utanyamaza, na kututesa sana?**

**64:8-12** Haya ni maombi yenye tumaini kwa ajiri ya YHWH ili kulikumbuka Agano na sio dhambi za watoto wake.

1. Wewe u baba yetu (tazama Mada Maalum katika 63:16)
2. Nawe u mfinyanzi
3. Sisi sote tu kazi ya mikono yako (kama vile 29:16; 45:9)

**64:8** kuna mfuatano wa maagizo katika maana ya hitaji la maombi.

1. Usiwe na hasira nyingi – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU(BDB 893, KB 1124) imetumika katika maana ya KITENZI AMRISHI, kama vile54:7-8
2. Usiukumbuke uovu siku zote – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU(BDB 269, KB 269) imetumika katika maana ya KITENZI AMRISHI, kama vile 43:25
3. Angalia, sisi sote tu watu wako – *Hiphil* KAULI SHURUTISHI(BDB 613, KB 661)

Hizi zote zinafanana na 57:16-17; Zab. 103:8-14.

**64:10-11** VITENZI hivi vyote ni KAULI ZA WAKATI TIMILIFU("umekuwa "likitumika mara nne). Inaelezea kumalizika kwa hasira ya YHWH juu ya kuharibiwa kwa miji.

1. Miji ya Palestina imekuwa jangwa
2. Yerusalemu umekuwa ukiwa
3. Hekalu limeteketea kwa moto (yaani , Babeli mwaka wa 586 K.K. na Tito mwaka wa 70 B.K.)
4. Vitu vyetu vyote vyenye kupendeza vimeharibika

**64:12** watu wa Mungu wanalia kwa ajiri kujitawala wenyewe na kuonewa huruma.Tafadhali,tafadhali,mateso haya yasizidi,walilia tafadhali rudi utugeukie tena!

# ISAYA 65

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFASIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Watu walioasi | Hukumu ya Mungu ya Haki | Majibu ya Mungu | Adhabu ya Mungu kwa walioasi | Hukumu ijayo |
| 65:1-7<br>(1-7) | 65:1-7<br>(1-7) | 65:1-16<br>(1-16) | 65:1-5 | 65:1-7<br>(1-7) |
| | | | 65:6-7 | |
| 65:8-12<br>(8-12) | 65:8-12<br>(8-12) | | 65:8-10 | 65:8-25<br>(8-25) |
| | | | 65:11-16 | |
| 65:13-16<br>(13-16) | 65:13-16<br>(13-16) | | | |
| Mbingu mpya na Nchi mpya | Uumbaji mpya wa utukufu | | Uumbaji mpya | |
| 65:17-25<br>(17-25) | 65:17-19<br>(17-19) | 65:17-25<br>(17-25) | 65:17-25 | |
| | 65:20-23<br>(20-23)<br>65:24-25<br>(24-25) | | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia uk. Xvi kipengele cha utangulizi)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

29. Ayaya kwanza
30. Ayayapili
31. Ayatatu
32. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura mbili za mwisho zinajumuishwa katika sehemu ya fasihi ambayo inaanzia sura ya 56 hadi sura ya 66. Yaweza kuainishwa kama “Siku Mpya” au “Enzi Mpya.”
B. Manabii wa Agano la Kale walitumia matukio yaliyopo kutabiri matukio yajayo. Kurudi kwa wale waliokimbilia uhamishoni kunaonekana kutabiri kurudi kwa hali ya kiroho ya wanadamu wote walioumbwa na Mungu kwenye ushirika wa Adamu wa kwanza kule bustani ya Edeni (kama vile Mada Maalum katika 40:15).

C. Sura ya 65 yumkini inawajibika kwa maombi ya pamoja ya Isaya kwa ajili ya msaada na huruma ambayo imeandikwa katika 63:7-64:12. Jibu la msingi la Mungu ni kuwa amekwisha kuwa tayari (kama vile 55:6-7), lakini watu wake wamekwenda mbali naye (mst. 5).

D. Kwa kiasi Fulani inafurahisha kuwa Paulo anatumia Isa. 65:1-2 katika Rum. 10:20-21. Paul anautafasiri mst. 1 kama wenye kurejerea kwa watu wa mataifa na mst.2 kama wenye kurejerea Wayahudi. Katika muktadha huu mistari yote inaonekana kuhusiana na kurudi kwa Wayuda wa siku za Ezra na Nahemia. Hata hivyo, mst. 1d, wenye kifungu, "kwa lile taifa ambalo halikuliitia Jina Langu,"laweza kurejerea taifa la Kiyahudi isipokuwa likitumika kwa namna Fulani ya kejeri, au ibada ya sanamu.

E. Sura ya 65 pia nayo ni ya kipekee katika unabii kwa sababu inachukua dhana ya kimwili ndani ya eneo la uwajibikaji binafsi. Makundi yote mawili kwa uwazi yanaweza kuonekana vizuri katika 65:10c na 11a. Mungu atatofautisha ndani ya taifa kati ya wale waliomkubali na wale waliomkataa (kama vile Ezek. 18:1-21; 33:10-20; na Yer. 31:29-30.

F. Isaya 65 inahitimisha msisitizo pekee wa Isaya juu ya upendo wa Mungu kwa ulimwengu wote ukijumuisha na watu wa mataifa (yaani., 2:2-4; 42:6; 49:6; 51:4-5; 56:7; 60:1,3). Anakwenda mbali zaidi kwa kusema kuwa hata Mungu atathubutu kuwafanya baadhi ya watu wa mataifa kuwa makuhani na Walawi (kama vile mst. 21). Hili ni la muhimu kwa uwazi wa hitimisho la wazi la Wayahudi wa imani ya Mungu mmoja na wito wa Ibrahimu katika Mwa. 12:1-3, ambalo pia linajumuisha ulimwengu wote (angalia Mada Maalum katika 40:15).

G. Inashangaza kuwa hii zama mpya inaelezewa pasipokuwa na dokezo lolote kwa Masihi katika sura za 9 na 11.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):65:1-7**
**1 Watu wasionitaka wanauliza habari zangu; nimeonekana na hao wasionitafuta; naliliambia taifa lisiloitwa kwa jina langu, 2 Nitazameni, nitazameni. Mchana kutwa nimewanyoshea mikono yangu watu walioasi, watu waendao katika njia isiyo njema, wakifuata mawazo yao wenyewe; 3 watu wanikasirishao mbele za uso wangu daima, wakitoa dhabihu katika bustani zao, na kufukiza uvumba juu ya matofali; 4 waketio kati ya makaburi, na kulala katika mahali pao pa siri; walao nyama ya nguruwe, na mchuzi wa vitu vinichukizavyo u katika vyombo vyao; 5 watu wasemao, Simama peke yako, usinikaribie mimi, kwa maana mimi ni mtakatifu kuliko wewe; watu hao ni moshi puani mwangu, moto uwakao mchana kutwa. 6 Tazama, neno hili limeandikwa mbele zangu. Sitanyamaza, lakini nitalipa, naam, mimi nitawalipa ujira wao vifuani mwao; 7 maovu yenu na maovu ya baba zenu pamoja, asema Bwana, ninyi mliofukiza uvumba juu ya milima, na kunitukana juu ya vilima; basi, kwa ajili ya hayo nitawapimia kwanza kazi yao vifuani mwao.**

**65:1 "Wanaouliza habari zangu....wanaonitafuta"** Siku zote Mungu huchukua nafasi katika masuala ya kiroho (yaani., Yn 6:44,65).Hata katika muktadha huu anaruhusu mwenyewe kupatikana, anajiwasilisha mwenyewe kwa Wayahudi na watu wa mataifa. Hii mistari ya ufunguzi inanikumbusha mimi juu ya Warumi 11.

◙**"Nitazameni, nitazameni"** Utamkaji mara mbili ni kwa ajili ya msisitizo! Haya ni maneno ya lahaja za Kiebrania kwa ajili ya upatikanaji (yaani., 6:8). Mungu siku zote yupo bali watu wake ndio hawaitikii ("ombeni," "tafuteni").

◙**"naliliambia taifa lisiloitwa kwa jina langu"** Katika muktadha hili linarejerea huenda kwa (1) Taifa la Kiyahudi ambalo husihi sanamu, hasa miungu ya ustawi au (2) watu wa mataifa (kama vile Rum. 10:20-21). Dhana ya kulitumia jina la mtu Fulani ni wazo la kuajibika kwao. Paulo anatumia dhana ile ile ya kuliitia jina la Bwana katika Rum. 10:9-13 (kama vile Mdo. 7:59; 9:14,21; 22:16; I Kor. 1:2; II Tim. 2:22). Hili lilifikiriwa kama ni tendo la imani na kuabudu.

## MADA MAALUM: JINA LA BWANA

Hiki kilikuwa ni kifungu cha kawaida kwenye Agano la Kale kwa ajili ya uwepo wa Mungu na nguvu za utendaji za Mungu wa Utatu katika kanisa. Ilikuwa sio kanuni ya kimiujiza, lakini ni ombi la tabia ya Mungu kama ilivyoonekana kwa Yesu.

Mara nyingi hiki kifungu kinarejerea kwa Yesu kama Bwana (kama vile Fil. 2:11)

1. Kwenye kipawa cha imani ya mtu ndani ya Yesu (kama vile Rum. 10:9-13; Mdo. 2:21,38; 8:12,16; 10:48; 19:5; 22:16; 1 Kor. 1:13,15; Yakobo 2:7)
2. kwenye upungaji pepo (kama vile Mt. 7:22; Marko 9:38; Luka 9:49; 10:17; Mdo. 19:13)
3. kwenye uponyaji (kama vile Mdo. 3:6,16; 4:10; 9:34; Yakobo 5:14)
4. kwenye tendo la huduma (kama vile Mt. 10:42; 18:5; Luka 9:48)
5. kwenye kipindi cha kulionya kanisa (kama vile Mt. 18:15-20)
6. kipindi cha kuwahubiri watu wa mataifa (kama vile Luka 24:47; Mdo. 9:15; 15:17; Rum. 1:5)
7. katika maombi (kama vile Yn. 14:13-14; 15:7,16; 16:23; 1 Kor. 1:2)
8. njia ya kurejerea Ukristo (kama vile Mdo. 26:9; 1 Kor. 1:10; 2 Tim. 2:19; Yakobo 2:7; 1 Pet. 4:14)

Chochote tukifanyacho kama wapiga mbiu, wahudumu, wasaidizi, waponyaji wenye kutoa pepo, n.k., tunatenda katika tabia yake, nguvu zake, —katika Jina Lake (yaani., Fil. 2:9-10)!

**65:2 "Mchana kutwa nimewanyoshea mikono yangu watu walioasi"** Hii ni stiari ya lugha ya mwanadamu kumwelezea Mungu (angalia Mada Maalum katika 41:2) ambayo inaonyesha uzito na uwazi wa pendo la Mungu (kama vile Rum. 10:21). Mara nyingi huwa ni ishara za maombi lakini hapa ni ukaribishaji.

◙**"Waendao katika njia isio njema, wafuatao mawazo yao wenyewe"** Mistari ifuatayo inaorodhesha dhana ya ibada ya sanamu inayowaainisha Wayahudi. Ni vigumu katika kipindi hiki cha historia moja kwa moja kuweza kuelewa kila moja ya dhana hizi kwa undani (kama vile mistari ya 3-7). Baadhi wanasema wote walikwisha kamatika katika ibada ya kule bustanini iliyotajwa katika mst. 3, wakati wengine wanatofautisha kati ya haya makundi. Jambo la wazi ni kuwa watu wa Mungu wameigeukia miungu mingine. Baadhi ya maelezo yenye kuwezekana kwa hizi tabia za ibada ya sanamu ni

1. kutoa dhabihu bustanini kwao
2. kufukiza uvumba juu ya matofali
3. waketio kati ya makaburi
4. hulala katika mahali pa siri
5. walao nyama ya nguruwe
6. mchuzi wa vitu vinichukuzavyo vi katika vyombo vyao
7. wafukizao uvumba juu ya milima
8. kunitukana juu ya vilima
9. kuandaa meza kwa ajili ya bahati, mst. 11
10. kuijazia ajali vyombo vya divai iliyochanganyika

◙**65:3 "Watu wanikasirishao mbele za uso wangu daima"** Hii ni stiari ya Kiebrania ya kujirudia, ukaidi wa wazi mbele za Mungu. Ibada ya sanamu imekwisha kuwa ya kawaida na kukubalika kiasi kwamba hata haikuwa ya kujificha.

◙**"Hutoa dhabihu katika bustani zao"** Hatuna uhakika kama hii ni ibada ya kale ya kuiabudu miti kama ilivyokwisha onekana katika Isa. 1:29 au ni ibada ya kipekee iliyoandaliwa bustanini (kama vile 66:17).

◙**"wakifukiza uvumba juu ya tofari"** Imekwisha shauriwa kuwa neno "matofari" yanaweza kurejerea kwa

1. Madhabahu ya mawe ya kuchonga (kama vile Law. 20:24-25)
2. Kuiabudu sanamu ya *Ba'al* (kama vile Law. 26:1)

3. Vigae venye kuhusiana na ibada ya miungu nyota ya Wababeli
4. Kufukiza uvumba madhabahuni (angalia*IVP Bible Background Commentary: OT*, uk. 640)

Uwezekano mwingi unatuonyesha kuwa kiwastani hatujui hili lina maana gani.

**65:4 "Waketio kati ya makaburi"** Hii inaonekana kuwa aina Fulani ya ibada au mawasiliano na wafu, yumkini utaalamu wa kuwasiliana na mizimu au ibada za mizimu (kama vile Kumb. 18:10-12).

◙**"wakilala mahali pao pa siri"** Neno la Kiebrania lililotafasiriwa "mahali pa siri" (BDB 665) kwa maana iliyo wazi inamaanisha "angalia," "linda," au "tunza" lakini hapa inaonekana kudokeza siri.

1. Vitu vya siri, Isa. 48:6
2. Sehemu za siri, Isa. 65:4
3. Mawazo ya siri, Mit. 7:10

Hakika hatuna wazo lolote kujua hili rejea inamhusu nani lakini inaonekana kuhusiana na sanaa za kimadhehebu kwa namna fulani.

◙**"walao nyama ya nguruwe,**
**na mchuzi wa vitu vinichukizavyo u katika vyombo vyao"** Mara nyingi matendo haya mawili yanahusiana na watoa maoni ingawa hili halijulikani. Ni uvunjaji wa sheria ya vyakula ya Walawi (kama vile 11:7). Nguruwe walikuwa ni kawaida kutolewa kama dhabihu katika mataifa jirani yaliyowazunguka (yaani., maandiko ya lugha ya Ugariti).

Toleo la MT lina neno (*kethiv*) "kipengele" ( פרק,895, BDB 830) lakini BDB linashauri neno (*qere*) מרק, BDB 600 II, "mchuzi wa nyama ulionona," pamoja na toleo la DSS, LXX, na Aramaic Targum.

**65:5 "watu wasemao, Simama peke yako, usinikaribie mimi,**
**kwa maana mimi ni mtakatifu kuliko wewe!'"** VITENZI viwili vya mwanzo ni vyenye kuamuru.

1. Simama peke yako – *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 897, KB 1132
2. usinikaribie – *Qal*KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 620, KB 670 kikitumika kwa maana ya KUAMRISHA

Tambua kuwa hizi amri mbili ni kutoka kwa waabudu sanamu (kama vile mistari ya 2-4,7,11-12), yumkini "makuhani" wao. Walihusiana na

1. Kuuondoa "utakatifu" (kama vile Ezek. 44:19, yaani., kwa namna Fulani upunguzaji wa nguvu zao au heshima)
2. Uondoaji ukiwa na athari hasi kwa waumini wa kipagani

◙

**NASB, NKJV "Mimi ni Mtakatifu kuliko wewe"**
**NRSV "Mimi ni Mtakatifu zaidi yako"**
**TEV "Sisi ni Watakatifu zaidi ya kuweza kuguswa"**
**NJB "kiasi cha Utakatifu kuweza kukujilia"**
**JPSOA "nitauachilia kwako utakatifu"**
**REB "utakatifu wangu utakuambukiza"**
**Peshitta "nimetakaswa"**

Toleo la UBS linaleta utofauti wa utumiaji wa irabu, "imekutakasa," lakini sio toleo la MT, "nimetakatifuzwa kwa ajili yako" lina alama "B" katika kulipima.

◙**"watu hao ni moshi puani mwangu,**
**moto uwakao mchana kutwa"** Hii nahau inaonyesha maumivu ya Mungu na hasira katika aina hii ya mtizamo na shughuli za za ibada ya sanamu.

**65:6 “Tazama, neno hili limeandikwa mbele Yangu,**
**Sintanyamaza, nitalipa”** Wazo la kitu fulani “lililoandikwa” ni stiari ya kale ambayo inarejerea kwenye kumbukumbu za Mungu (kama vile Kitabu cha Matendo na Kitabu cha Uzima, Dan. 7:10; Ufu. 20:12- 15). Ukweli ni kwamba siku moja hukumu itakuja. Hili ni neno ambalo wanadamu wote wanahitaji kulisikia. Tambua kile YHWH atakifanya.

1. sintanyamaza
2. nitalipa ujira
3. Nitawalipa ujira vifuani mwao

## MADA MAALUM: VITABU VIWILI VYA MUNGU

A. Mungu amejifunua katika namna mbili.
   1. asili (yaani, uumbaji, kama vile Zab.19:1-6; iitwayo "mapinduzi asilia")
   2. Maandiko (kama vile Zab. 19:7-14; yaitwayo "mapinduzi maalumu/kipekee")

Ndiyo maana sifikiti yakwamba daima lazima kuwepo mvutano kati ya sayansi na imani, kweli yote ni kweli ya Mungu. Tafadhali angalia maoni yangu kuhusu Mwanzo 1-11 mtandaoni katika *www.freebiblecommentary.org*

B. Kuna vitabu viwili vilivyotajwa katika Dan. 7:10 na Ufu. 20:12.
   1. Kile"kitabu cha matendo" kilicho na sababu zote na matendo ya wanadamu, yote yaliyo mema na mabaya. Katika maana hii, hii ni stiari ya kumbukumbu ya Mungu na y a kwamba siku moja wanadamu wote watatoa hesabu ya utumishi wa vipawa vya maisha yao kwa Muumba wao.
      a. Zab 56:8; 139:16
      b. Isaya 65:6
      c. Malaki 3:16
      d. Ufunuo 20:12-13
   2. Kile"kitabu cha uzima" chenye kilicho orodhesha wale walio na imani/waliotubu/walio utii uhusiano na YHWH/ Yesu. Hii ni stiari ya kumbukumbu ya Mungu ya wale waliokombolewa na kuunganishwa na mbingu.
      a. Kutoka 32:32-33
      b. Zab. 69:28
      c. Isaya 4:3
      d. Danieli 12:1
      e. Wafilipi 4:3
      f. Waebrania 12:23
      g. Ufunuo 3:5; 13:8; 17:8; 20:12,15; 21:27
      h. Pia kilichotajwa katika Enoko 47:3; 81:1-2; 103:2; 108:3

Hivi vitabu vinawakilisha uaminifu wa Mungu kwa Neno lake. Kwa wale walioasi na kukataa,anazikumbuka dhambi zao; kwa wale waliotubu, kuamini, kutii, kutumika, na kustahimili, Yeye husahau dhambi zao (kama vile Zab. 103:11-13; Isa. 1:18; 38:17; 43:25; 44:22; Mika7:19). Jambo hili hutupa uhakika mwingi na ujasiri wa kutobadilika kwa Mungu, sifa ya huruma, ahadi, na utoaji. Mungu ni mwaminifu! Jambo alilolifunua kumhusu ni la kweli!

◙**“nitawalipa ujira vifuani mwao”** Sitiari kwa ajili ya “vifuani” inamaanisha “nitarejea kwenye dhambi zao” (kama vile Ayubu 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mit. 24:12; Wimb. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; I Kor. 3:8; II Kor. 5:10; Gal. 6:7-10; II Tim. 4:14; I Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12).

**65:7 “Maovu yenu na maoni ya baba zenu”** Huu ni muunganiko wa dhambi ya pamoja na binafsi, dhambi ya hiari. Tumeathiriwa sio tu na ushirika wetu wa nyuma, na ushirika wetu wa sasa, lakini pia na chaguzi zetu za sasa. Tunajifunza toka kwenye amri kumi za Mungu katika kitabu cha Kutoka 20:5, Kumb. 5:9, kuwa tunaathiriwa na dhambi za wazazi wetu wa kizazi cha tatu na cha nne. Tunajifunza pia toka Ezekieli 18 ukweli ulio kinyume kuwa tunawajibika kwa dhambi zetu wenyewe.

◙**“ninyi mliofukiza uvumba juu ya milima,**

**na kunitukana juu ya vilima"** Hili, kutokana na nabii Hosea, ni dhana ya ibada ya mungu wa ustawi*Ba'al* (kama vile Hos. 4:13-14).

◙

**NASB, NKJV "kazi zao za mwanzo"**
**NRSV "nitawalipa"**
**TEV "matendo yao ya mwanzo"**
**NJB, JPSOA "nitawalipa"**

Toleo la NASB linafuatisha toleo la MT. Toleo la NRSV, NJB, na JPSOA linashauri marekebisho ya neno ראשנה (BDB 911) likimaanisha "mwanzo," kwenda בראשו (BDB 1168) likimaanisha "kuwalipa" (Law. 5:24) au "mwanzo" (Yer. 16:18)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):65:8-12**
**8 Bwana asema hivi, Kama vile divai mpya ipatikanavyo katika kichala, na mtu mmoja husema, Usikiharibu kwa maana mna baraka ndani yake; ndivyo nitakavyotenda kwa ajili ya watumishi wangu, ili nisiwaharibu wote.**
**9 Nami nitaleta uzao toka Yakobo, na mrithi wa milima yangu toka Yuda, na mteule wangu atairithi, na watumishi wangu watakaa huko. 10 Na Sharoni itakuwa zizi la makundi ya kondoo, na bonde la Akori mahali pa kulala makundi ya ng'ombe, kwa ajili ya watu wangu walionitafuta. 11 Bali ninyi mmwachao Bwana, na kuusahau mlima wangu mtakatifu, na kuandika meza kwa ajili ya Bahati, na kuijazia Ajali vyombo vya divai iliyochanganyika; 12 mimi nitawaandikia kuuawa kwa upanga, na ninyi nyote mtainama ili kuchinjwa; kwa sababu nilipoita hamkuitika; niliponena, hamkusikia; bali mlitenda yaliyomabaya machoni pangu, mlichagua mambo nisiyoyafurahia.**

**65:8 "kama divai mpya ipatikanayo katika kichala"** Hii ni stiari inayosema kuwa hata katika kichala cha mzabibu kilicho na baadhi ya matunda mabovu mara nyingi pia huwa na matunda mazuri. Huu ni mwanzo mzuri wa mazungumzo yanayoanzia toka mst.8 hadi mst. 10 ambayo inaelezea kuwa mabaki ya Wayahudi (angalia Mada Maalum katika 46:3) watakuwa waaminifu kwa YHWH. Hata hivyo, mistari ya 11-13 inaonyesha kukataliwa moja kwa moja na hukumu ya wale watu wa Yuda wanaoendelea kumkataa Mungu. Huu ndio mwanzo wa maumivu lakini msisitizo wa kweli ni kuwa hukumu itaanza na watu wa nyumbani mwa Mungu. Kuna muundo wa dini zetu ambapo Mungu hatiliwi maanani sana. Mungu anaangalia moyo (kama vile Isa. 29:13).

Kwa ajili ya "mvinyo mpya" angalia Mada Maalum hapo chini.

## MADA MAALUM: MTAZAMO WA BIBLIA DHIDI YA ULEVI NA KILEO

Maneno ya Kibiblia

A. Agano la Kale
   1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hiii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
   2. *Tirosh* – Hiii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
   3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya" BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
   4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mzizi wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi hiki huongezwa ndani yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).

B. Agano Jipya
   1. *Oinos* – neno lililo sawa kimaana na *yayin*

2. *Neos oinos* (divai mpya) – ni neno linalofanana la Kiyunani sawa na tirosh (kama vile Marko 2:22).
3. *Gleuchos vinos* (divai mpya, asis) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

I. Matumizi ya Kibiblia

A. Agano la Kale

1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
2. Divai ni sehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
3. Mvinyo ilitumika katika sherehe za Israeli (kama vile Kumb. 14:26)
4. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2;Mit. 31:6-7).
5. Divai inaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu –Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria– 2 Sam. 11:13; Amnoni– 2 Sam. 13:28; Ela– 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i– 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amosi 4).
6. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
7. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
8. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).

B. Kipindi cha utulivu kati ya Agano la Kale na Agano Jipya

1. Divai katika upatanisho ina msaada (Mhubiri 31:27-33).
2. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai ni kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa ya kulevya yanahitajika." (BB 58b).

C. Agano Jipya

1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11).
2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima moja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1na kuendelea; Ufu. 19:9).
7. Ulevi huleta majuto (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

II. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

A. Mkazo wa Kiupembuzi

1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
2. Ulevi ni tatizo kubwa.
3. Waamini katika baadhi ya tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1- 23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).

B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka iliyokusudiwa

1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote mazuri.
   a. chakula – Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
   b. vitu vyote visivyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
   c. Vitu vyote vilivyo vya kisheria– 1 Kor. 6:12; 10:23
   d. Vitu vyote vilivyo safi – Tito 1:15
2. Mwanadamu aliyeanguka amezitumia vibaya karama za Mungu kwa kuzifanyia kazi nje ya mipaka ya Mungu aliyoikusudia.

C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uumbaji wa vitu vinanyoonekana (kama vile Rum. 14:14,20).

III. maelezo ya kufungia

A. kuwe na uhakika na uzoefu wako, thiolojia, na utafasiri wa kibilia havimshushi thamani Yesu na tamaduni

za Kikristo/ Kiyahudi za karne ya kwanza! Kiuhakika hawakuwa wenye kujizuiya kunywa mvinyo.

B. Mimi sitetei jamiii ya watumia pombe. Hata hivyo, wengi wamekwenda mbali juu ya nafasi ya Biblia kuhusu somo hili na sasa kudai kuwa wenye haki sana wakisimamia juu ya upendeleo wa kimadhehebu/ kitamaduni.

C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 vimetoa mwanga na mwongozo uliosimamia juu ya upendo na heshima kwa wapendwa wengine na uenezaji wa injili katika tamaduni zetu, na sio uhuru binafsi au ukosoaji wa kimaamuzi. Kama Biblia ndio chanzo pekee cha imani na utendaji, kwa hiyo yawezekana wote tulifikirie jambo hili.

Tukijizuiya kabisa kunywa mvinyo kama yalivyo mapenzi ya Mungu, tunadokeza nini kuhusu Yesu, pia tamaduni za sasa za wale wanaotumia kileo mara kwa mara (mf. Ulaya, Israeli, Argentina)

**65:10-11 "kwa ajili ya watu wangu walionitafuta.**
**bali ninyi mmuachao Bwana"** Hii inaonyesha dhana mpya katika Agano la Kale. Mungu amekwisha kushughulika katika dhana ya ushirika na taifa. Taifa lote lilibarikiwa au taifa lote lililaaniwa (yaani., Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 28-29). Sasa tunakuja kwenye mtazamo wa ubinafsi wa Ezek. 18:32; 30:10-20; na Yer. 31:29-30, ambapo pana tofauti ndani ya watu wa Mung kama wale waaminio na wale wasioamini (kama vile Kumb. 29:24-28). Baadaye katika sura ya 66 patakuwepo na tofauti kati ya wanadamu wote, kati ya wale waliomkataa na wale waliomkubali YHWH.

**65:11 "ninyi mmuachao Bwana"** KITENZI (*Qal* CHA HALI YA KUENDELEA, BDB 736 I, KB 806) kinamaanisha "kutelekeza" au "kuacha." Mara nyingi hutumika kwa maana ya kumuacha Mungu (kama vile Kumb. 28:20; 31:16; Amu. 10:10; Yer. 1:16; Yona 2:9). Wakamwacha YHWH kwa ajili ya sanamu (kama vile II Fal. 9-22; II Nya. 36:13-21). Mungu naye atawaacha (kama vile Kumb. 31:17; Isa. 41:17; 49:14; 54:7).

◙**" kuandika meza kwa ajili ya Bahati,**
**na kuijazia Ajali vyombo vya divai iliyochanganyika"** Neno "bahati" (BDB 151 II, KB 176 II) na neno la Kiebrania "kudra" (BDB 584, KB 602) ni majina ya miungu wa kipagani (kama vile Yos. 11:17), yumkini inaelezea miungu ya dunia hii (kama vile Yer. 7:18; 44:17), ambayo ilikuwa ni ibada ya "malkia wa anga." Inafahamika kuwa maneno haya yanarejea kwenye ibada za sanamu kwa namna fulani!

**65:12**
**NASB "nitawauweni kwa upanga"**
**NKJV "nitawahesabu kuwauwa kwa upanga"**
**NRSV, NJB "nitawaandikia kuwauwa kwa upanga"**
Tambua mchezo wa maneno kwenye KITENZI(*Qal* HALI ILIYO TIMILIFU, BDB 584, KB 599), unaotumika kama jina kwa ajili ya mungu wa uongo katika mst.11, "bahati" (BDB 584).

◙**"kwa sababu nalikuita, lakini hukutaka kuitika"** Huu ni muhtasari wa mistari ya 1-7. Mungu anaendelea kuwapenda na kuwaita lakini wao walikataa na kuukataa wito wake (kama vile 41:28; 50:2; 66:4; Hos. 11:2). Mistari ya mwisho ya aya ya 12 imejirudia katika 66:4.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 65:13-16**
**[13] Kwa hiyo Bwana MUNGU asema hivi, Tazama, watumishi wangu watakula, bali ninyi mtaona njaa; tazama, watumishi wangu watakunywa, bali ninyi mtaona kiu; tazama, watumishi wangu watafurahi, bali ninyi mtatahayarika; [14] tazama, watumishi wangu wataimba kwa furaha ya moyo, bali ninyi mtalia kwa huzuni ya moyo; mtapiga kelele kwa sababu ya uchungu wa roho zenu. [15] Nanyi mtaliacha jina lenu kuwa laana kwa wateule wangu. Na Bwana MUNGU atakuua; naye atawaita watumishi wake kwa jina lingine. [16] Hata itakuwa yeye atakayejibariki duniani, atajibariki kwa Mungu wa kweli; naye atakayeapa duniani, ataapa kwa Mungu wa kweli. Kwa kuwa taabu za kwanza zimesahauliwa, na kwa kuwa zimefichwa machoni pangu.**

**65:13-16** Huu ni mwendelezo juu ya utofauti kati ya aina mbili za uzao (yaani., vizazi) wa Ibrahimu—wanao amini na wasi amini. Katika Agano Jipya hili linawageukia wanadamu wote (kama vile Rum. 2:28-29).

**65:14** Tambua utofauti uliopo kati ya

1. Walio waaminifu – wataimba kwa furaha ya moyo
2. Wasio waaminifu – watalia kwa huzuni ya moyo.

Kuna mgawanyiko kati ya wanadamu (kama vile Mt. 7:13-14,15-23,24-27; Luka. 13:22-30), hata wale wanaoonekana "kuwa wa kidini"!

**65:15 "Nanyi mtaliacha jina lenu kuwa laana kwa wateule wangu"** Kuna mchezo mwingine kwenye neno "jina" (BDB 1027). Hapa ni dhana kuwa jina la wasio amini litakuja hukumiwa, wakati wale wanaoamini watapewa jina jipya. Kutokana na mtazamo wa haraka hatufahamu jina jipya watakalo itiwa. Jina jipya la Mungu limetolewa katika mstari wa 16—"Mungu wa Amina," "Mungu wa Ukweli," au "Mungu wa Uaminifu" (kama vile Ufu. 3:14). Jina jipya la wale wanao amini yumkini linahusiana na hilo. Katika kitabu cha Mwanzo ahadi za YHWH kwa Ibrahimu zilikuwa na tahadhari na Baraka zenye kuhusiana na tabia za Ibrahimu akitumia "jina" kumwasilisha Yeye kama mtu (kama vile Mwa. 12:2; 18:18; 22:18).

**65:16 "Kwa kuwa taabu za kwanza zimesahauliwa,**
**na kwa kuwa zimefichwa machoni pangu"** Katika Biblia kifungu "Mungu atasahau" ni stiari kwa ajili ya msamaha. Tambua mwendelezo wa stiari ile isemayo dhambi zimefichika machoni pake. Hii ni mada yenye kujirudia ya Agano la Kale. Mungu akisamehe, husahau (kama vile Zab. 103:11-13; Isa. 1:18; 38:17; 43:25; 44:22; na Mika 7:19)!

◙

**NASB, NKJV,**
**NJB "Mungu wa ukweli"**
**NRSV "Mungu wa uaminifu"**
**TEV "Mungu mwaminifu"**
**LXX, JPSOA "Mungu wa kweli"**
**REB "kwa Mungu ambaye jina lake ni Amini"**

Jina la Uungu , "Mungu," אלה(BDB 43), mara nyingi hutumika katika mashairi ya kale (kama vile Kumb. 32:15,17; Ayubu 3:4; Zab. 18:32; 50:22; 114:7; 139:19; Mit. 30:5; Isa. 44:8; Hab. 3:3). Sehemu ya pili ya jina ni "Amina." Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM:AMINA

I. AGANO LA KALE
   A. Neno "Amina" linatoka kwenye neno la Kiebrania lenye maana ya
      1. "ukweli" (emun, emunah, BDB53)
      2. "Uaminifu" (emun, emunah, BDB 53)
      3. "imani" au "uaminifu"
      4. "amini" (dmn, BDB 52)
   B. Asili yake ya neno inadokeza mkao wa mwili wa mtu ulivyo imara. Kinyume cha hili kinaonyesha mwili wa mtu Yule asio imara, unaotereza (kama vile. Zab. 35:6; 40:2; 73:18; Yeremia 23:12) au kizuizi (kama vile. Zab. 73:2). Kutokana na utumiaji huu wa fasihi unatengeneza upanuzi wa kiisitiari wa imani, uaminifu, utiifu na wa kutegemewa (kama vile. Hab. 2:4)
   C. Utumiaji maalumu (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika agano la kale)
      1. Nguzo, 2 Fal. 18:16 (1 Tim. 3:15)
      2. Kuthibitika, Kut. 17:12
      3. Uimalifu, Kut. 17:12

4. Uthabiti, Isa. 33:6
5. Ukweli, 1 Fal. 10:6; 17:24; 22:16; Mit. 12:22
6. Thabiti, 2 Nya. 20:20; Isa. 7:9
7. Stahili (sheria alizopewa Musa), Zab. 119:43,142,151,160

D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yanatumika kwa ajili ya imani thabiti
   1. Bathach(BDB 105), imani
   2. Yra(BDB 431), hofu, heshima, abudu (kama vile. Mwa. 22:12)
E. Kwa maana ya kuamini au uaminifu ulioanzishwa kwa matumizi ya liturujia ambao ulitumika kuthibitisha maelezo ya kweli ya mtu mwingine (kama vile. Hes. 5:22; Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Neh. 5:13; 8:6; Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48; Yer. 11:5; 28:6).
F. Kiongozi cha kithiolojia kwenye neno hili sio uaminifu wa mwanadamu, bali ni wa Mungu mwenyewe (kama vile Kut. 34:6; Kumb. 32:4; Zab.108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni neema, uaminifu, kutii Agano la Mungu na ahadi zake. Wale wanaomfahamu Mungu wanahitajika kufanana naye (kama vile. Hab. 2:4). Biblia ni historian na kumbu kumbu ya Mungu kurejesha taswira yake (kama vile Mwa. 1:26-27) kwa mwanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu. Hii ndio sababu ya kuumbwa kwetu.

II. AGANO JIPYA

A. Utumiaji wa neno "amina" kama hitimisho la kiliturujia kwa minajili ya kuthibitisha ukweli wa maelezo/taarifa ni la kawaida katika Agano Jipya (kama vile. 1 Kor. 14:16; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12).
B. Utumiaji wa neno kama kifungio cha maombi ni wa kawaida kwenye Agano Jipya (kama vile. Rum. 1:25; 9:5; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 6:18; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 2 The. 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2 Tim. 4:18).
C. Yesu ndiye yeye aliyelitumia hili neno (limezidishwa mara 25 katika Yohana, yaani., Yohana 1:51; 3:3,5,11; n.k.) kuyatambulisha maelezo muhimu (kama vile. Luka 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43).
D. Linatumika kama cheo kwa Yesu katika Ufu. 3:14 ( pia angalia 2 Kor. 1:20, yamkini jina la heshima la Mungu kutoka Isa. 65:16)
E. Dhana ya kusadiki au sadiki, au kuamini au amini inaelezewa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis*, ambalo linatafasiliwa katika Kiingereza kama "imani","sadiki","kuamini"(angalia mada maalumu: Sadiki, Kuamini au Imani).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA):65:17-25**

**17 Maana, tazama, mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya, na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala
hayataingia moyoni. 18 Lakini furahini, mkashangilie daima, kwa ajili ya hivi niviumbavyo; maana, tazama,
naumba Yerusalemu uwe shangwe, na watu wake wawe furaha. 19 Nami nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea
shangwe watu wangu; sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena, wala sauti ya kuomboleza. 20 Hatakuwapo
tena mtoto wa siku chache, wala mzee asiyetimia siku zake; kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka
mia; bali mtenda dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa. 21 Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani
yake; watapanda mizabibu, na kula matunda yake. 22 Hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake;
hawatapanda, akala mtu mwingine; maana kama siku za mti ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu, na
wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi. 23 Hawatajitaabisha kwa kazi bure, wala
hawatazaa kwa taabu; kwa sababu wao ni wazao wa hao waliobarikiwa na Bwana, na watoto wao pamoja
nao. 24 Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa katika kunena, nitasikia. 25 Mbwa-
mwitu na mwana-kondoo watalisha pamoja, na simba atakula majani kama ng'ombe; na mavumbi yatakuwa
chakula cha nyoka. Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu mtakatifu wote, asema Bwana.**

**65:17 "Tazama, Mimi, naumba mbingu mpya na nchi mpya"** Muktadha wa mistari ya 17-25 ni muhimu zaidi kwa sababu ni yenye maelezo muhimu, sio tu kwa ajili ya zile sura mbili za mwisho—kuwa Mungu atakwenda kufanya mambo yote kuwa mapya (kama vile 42:9; 48:6; 66:22; II Pet. 3:13), bali ni majadiliano ya zama mpya za Masihi (kama vile Rum. 8:18-25). Pia zinadokeza kuwa utaratibu wa sasa utaondolewa (kama vile Isa. 51:6 na II Pet. 3:10). Pia kuna uhusiano kati ya mistari ya 16 na 17 kuwa utaratibu mpya hautajumuisha dhambi kwa sababu watakuwa wamesamehewa, kama ilivyokwisha tajwa kwenye sehemu ya mst.16. Istilahi ya kifungu "mbingu mpya na nchi mpya" ni cha kawaida katika fasihi ya Kiyahudi ya matukio ya siku ya mwisho (kama vile II Esdras 6:11-24; I Enoch 91:16). Hili likajakuwa ni taswira kwa ajili ya Ufunuo 21-22! Nchi itarudi kwenye kusudi na utukufu wake wa Mwanzo 3.

**65:18** Mstari wa kwanza wa ushairi una KAULI SHURUTISHI zenye kufanana.

1. furahini – *Qal* KAULI SHURUTISHI, BDB 965, KB 1314, kama vile 61:10 (mara mbili); 62:5; 64:5; 65:18,19; 66:10,14
2. furahini – *Qal* KAULI SHURUTISHI, BDB 162, KB 189, kama vile 61:10; 65:18,19; 66:10 AB, uk. 198, angalia haya kama majina mapya kwa ajili ya Yerusalemu na wale wanaorudi.

◙**"milele"** Hili neno (BDB 723 I) linaonyesha mwendelezo wa ushirika na Muumba na vyombo vyake alivyoviumba yaani binadamu (kama vile I Nya. 28:9; Mika 7:18).

**65:19 "Sauti ya kulia haitasikika ndani yake tena,**
**wala sauti ya kuomboleza"** Hili ni somo linaloendelea la Isaya kuwa zama mpya haitakuwa na maumivu ya ile dhambi ya awali –nchi iliyo laaniwa (kama vile Isa. 25:8; 30:1; 35:10; 55:11). Hili linaonekana kuwa dokezo la Ufu. 21:4.

**65:20 "Hatakuwepo motto wa siku chache,**
**wale mzee asiyetimiza siku zake**" Haya maelezo yenye kukosoa mno yanaweza kuwa na vyanzo viwili au kimoja.

1. Dokezo kwa maisha marefu ya Mwanzo 1-5, hivyo kumaanisha ule muda wa kurudi bustanini Edeni
2. Njia ya Agano la Kale kuelezea "zama mpya," ambayo tunaifahamu toka katika Agano Jipya haihusiani na mwendelezo wa maisha ya kimwili bali maisha mapya ya milele (*zoa*)

Kwa ajili ya mjadala mzuri juu ya mazungumzo ya Isaya ya mwendelezo wa maisha na mjadala wa Agano Jipya juu ya maisha ya milele, angalia *Hard Sayings of the Bible*, kr. 307-309.

**65:22** Hizi ni stiari zenye kuelezea ukweli kuwa watu wataishi katika nchi na kufurahia matunda. Ni dokezo la moja kwa moja kwenye safari ya kukimbilia uhamishoni kwa wana wa Israeli na ahadi ya kurudi Palestina. Angalia Mada Maalum katika 40:9. Tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yanaliangalia neno "mti" (BDB 781) kama lenye kurejerea "mti wa uazima" katika bustani ya Edeni, kama ilivyofanyika katika toleo la Aramaic Targums.

**65:24** Hii ni ahadi nzuri ya majibu ya maombi yaliyojibiwa papo kwa papo na hata zaidi kuliko Mt. 6:8.

**65:25 "Mbwa-Mwitu na Mwana kondoo watalisha pamoja"** Hapa tena ni taswira tulivu ya Mungu na mwanadamu kuwa pamoja katika bustani ya Edeni wakikaa na wanyama (kama vile Isa. 11:6-9; Mwanzo 1,2; Ufu. 21:22). Hii inaenda sambamba hasa na thiolojia yangu kuwa hatuendi mbinguni, bali mbingu inarejea kujiumba na na kuitakasa nchi. Itakuwa kama ilivyokuwa!

◙**"na mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka"** Hii inaonekana kuwa nahau isio ya kawaida kwa sababu mavumbi yalikuwa ni chakula cha kawaida cha nyoka katika siku hizo. Hata hivyo, yawezakuwa rejeo kwa

1. Mwa.3:14, inavyoonyesha kuwa majaribu ya shetani yatakwisha moja kwa moja kwa kadri ya madhara yake juu ya kuamini kwao na kufanyika upya kwa mwanadamu
2. Isa. 11:8, ubeti ambao pia unaelezea zama mpya

# ISAYA 66

| MIGAWANYO YA AYA KATAIKA TAFSRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mbingu ni Kiti cha Enzi cha Mungu | Ibada ya kweli na ya Uongo | Hitimisho la Maono | Bwana Anayahukumu Mataifa | Unabii juu ya Hekalu |
| 66:1-2 (1-2) | 66:1-2 (1-2) | 66:1-2 (1-2) | 66:1-2 (1-2) | 66:1-2 (1-2) |
| Wanafiki Wanakaripiwa | | | | |
| 66:3-6 (3-6) | 66:3-4 (3-4) | 66:3-5 (3-5) | 66:3-4 (3-4) | 66:3-4 (3-4) |
| | Bwana anailinda Sayuni | | | Hukumu juu ya Yerusalemu |
| | 66: 5 (5) | | 66:5-6 (5-6) | 66:5 (5) |
| | 66:6 (6) | 66:6 (6) | | 66:6 (6) |
| 66:7-9 (7-9) | 66: 7-9 (7-9) | 66:7-9 (7-9) | 66:7-9 (7-9) | 66:7-9 (7-9) |
| Furaha Ijayo katika Yerusalemu | | | | |
| 66:10-17 (10-17) | 66:10-11 (10-11) | 66:10-11 (10-11) | 66:10-11 (10-11) | 66:10 (10) |
| | | | | 66:11 (11) |
| | 66:12-13 (12-13) | 66: 12-16 (12-16) | 66:12-14 | 66:12a (12a) |
| | Utawala na Sononeko la Mungu | | | 66:12b-13 (12b-13) |
| | 66:14-16 (14-16) | | | 66:14 (14) |
| | | | 66:15-16 | 66:15 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | (15) |
| | | | | 66:16-17 (16-17) |
| | 66:17 (17) | 66:17 | 66:17-19a | Hotuba ya Matukio ya Siku za Mwisho |
| 66:18-24 (22-24) | 66:18-21 | 66:18-21 | | 66:18-22 |
| | | | 66:19b-21 | |
| | 66:22-23 (22-23) | 66:22-23 (22-23) | 66:22-24 | |
| | | | | 66:23-24 (23-24) |
| | 66:24 (24) | 66:24 | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia uk. wa xvi kipengele cha utangulizi)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

33. Aya ya kwanza
34. Aya ya pili
35. Aya ya tatu
36. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB 9LILILOBORESHWA) 66:1-2**
[1]**Bwana asema hivi,**
**Mbingu ni kiti changu cha enzi,**
**na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu; mtanijengea nyumba ya namna gani?**
**Na mahali pangu pa kupumzikia ni mahali gani?**
[2]**Maana mkono wangu ndio uliofanya hivi vyote,**
**vitu hivi vyote vikapata kutokea, asema Bwana;**
**lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia,**
**mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo** neno langu.

**66:1 "Mbingu ni kiti changu cha enzi**
**mtanijengea nyumba ya namna gani?**

**Na mahali pangu pa kupumzikia ni mahali gani"** Hili ni dokezo lililo dhahirila maombi ya kuwekwa wakfu ya Suleimani katika I Fal. 8:27 na tena yanadokezwa katika Matendo 8:47-48.

Kilicho kigumu kukielewa ndicho kinachohusiana na kipindi hiki cha kihistoria. Wengine wanaliona hili kuwa linahusiana na kurudi toka uhamishoni na kujenga upya Hekalu, jambo ambalo linawezekana kutokana na andiko. Hata hivyo, wengine wanasema kwamba Mungu haishi ndani ya majengo aliyoyatengeneza mwanadamu na suala hili linarejelea juu ya

1. hekalu la mwili wa mwanadamu ambalo Mungu ameuumba
2. familia ya Mungu, imani ya uzao wa Ibrahimu (Wayahudi na Mataifa ya imani, kama vile Rum. 2:28-29)
3. hekalu ya kiulimwengu la Mwanzo 1, tazama John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*

**66:2 "Maana mkono wangu ndio uliofanya hivi vyote"** Kwa ajili ya neno "mkono" tazama Mada Maalum katika 40:2. Tunajifunza kutokana na Agano Jipya kwamba yeye ndiye yule mwanzilishi katika uumbaji hakuwepo mwingine zaidi ya Kristo aliyeuvaa mwili (kama vile Yohana 1:3; I Nya . 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2).

**◙"lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia,**
**mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu"** Mungu huiangalia shauku na tabia ya mwanadamu. YHWH anayafahamu mawazo na makusudi ya moyo (kama vile mst. wa 18).

1. I Sam. 2:3; 16:7
2. I Fal. 8:39
3. I Nya. 28:9
4. II Nya. 6:30
5. Zabs. 7:9; 17:3; 26:2; 44:21; 139:1,23
6. Mit. 15:11; 16:2; 21:2; 24:12
7. Yer. 11:20; 17:9-10; 20:12
8. Luka 16:15
9. Matendo 1:24; 15:8
10. Rum. 8:2

Pia Yesu anayajua mawazo ya ndani na shauku za wanadamu, tazama Yohana 2:24-25; 6:61,64; 13:11!

Huu ufafanuzi unaofanana unatumika kueleza ungamo la Daudi juu ya dhambi ya Bathsheba (kama vile Zab. 51:17); tambua 57:15; Zab. 34:18; Mt. 5:3-4; Luka 18:13-14.

Huu pia unamajina mawili ya watu wa Mungu ambayo ni mazuri sana na yenye kuelezeka.

1. Watu walio wanyenyekevu na wenye kutubu
2. Wale wanaolitetemekea neno lake (kama vile mist. ya 5)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 66:3-6**
**3 Yeye achinjaye ng'ombe ni kama yeye amwuaye mtu;**
**na yeye atoaye dhabihu ya mwana-kondoo ni kama yeye avunjaye shingo ya mbwa;**
**na yeye atoaye matoleo ni kama yeye atoaye damu ya nguruwe;**
**na yeye afukizaye uvumba ni kama yeye abarikiye sanamu;**
**naam, wamezichagua njia zao wenyewe, na nafsi zao zafurahia machukizo yao.**
**4 Mimi nami nitachagua mapigo yao, nitaleta hofu zao juu yao;**
**kwa sababu nilipoita, hawakuitika; na niliponena, hawakusikia; bali walifanya yaliyo maovu machoni pangu, na kuyachagua nisiyoyafurahia.**
**5 Lisikilizeni neno la Bwana, ninyi mtetemekao kwa sababu ya neno lake;**
**Ndugu zenu wawachukiao ninyi, waliowatupa kwa ajili ya jina langu, wamesema, Na atukuzwe Bwana, tupate kuiona furaha yenu;**
**lakini watatahayarika.**

**[6] Sauti ya fujo itokayo mjini!**
**Sauti itokayo hekaluni! Sauti ya Bwana awalipaye adui zake adhabu!**

**66:3-4** Hapa inaonnyesha kuwa taratibu pekee hazitoshelez**i** (kama vile 29:13; Yeremia 7), Bali wale waliochanganya mienendo na taratibu hizo yawapasa kuwa wanyenyekevu na wenye moyo wa toba. Kile tukifanyacho mara kwa mara hubadilika na kuwa kawaida, bali katika eneo la imani, shauku yetu ndiyo ya msingi (kama vile mst. wa 2).

**66:3 "na nafsi zao zafurahia machukizo yao"** Kifungu hiki kinazirejelea desturi mbalimbali za ibada za wapagani (kama vile 65:4,7,11). Hawa walizipenda na kuzichagua (BDB 103, KB 119, kifungu hiki kimetumika mara tatu katika mist. ya 3-4) dhambi (kama vile 1:4; 57:17;65:2; 66:18; Zab. 81:11-12)!

**66:4**
**NASB "mapigo yao"**
**NKJV "maafa "**
**NRSV, JPSOA "mock"**
**TEV "majanga"**
**NJB "kuwafanya wapumbavu"**
**REB "mwendezo uliokusudiwa"**

Hili neno (BDB 760, KB 1768) linapatikana hapa tu na katika 3:4. Toleo la KB linapendekeza

1. matendo ya utukutu (yaliyofanywa na mtoto toka asili ya neno, עולל(BDB 760) kwa 3:4
2. tiba ya magonjwa

   Toleo la NET Bible linapata maana inayotokana na neno עלל (BDB 760), "kuwashughulikia ipasavyo."

◙ **"nitaleta hofu zao juu yao" Aaa**! Ni laana ya namna gani itokayo kwa Mungu (kama vile Mit. 1:27; 10:24)!

◙**"kwa sababu nilipoita, hawakuitika"** Kwa mara nyingine tena hapa kuna marudio yenye dhamira (kama vile 41:28; 50:2; 65:12).

**66:5 Kuna huzuni na mvutano miongoni mwa watu waMungu** (kama vile Rum. 9:6-8). Mateso ya manabiii waliyopewa na Wayahudi wenzao ni mfano mzuri wa suala hili (kama vile Mt. 5:10-12; 10:22). Mambo mengi ya kutisha yamefanywa na watu wa "kidini" kwa kutumia jina la Mungu! Tambua namna watu wa Mungu walio wa kweli wanavyopaswa kuyaitikia mateso —furaha (BDB 970, kama vile 51:11; 55:12; 61:7; tambua 66:10 ambayo ina maneno mengine yenye visawe vya neno furaha.

1. changamkeni – BDB 162
2. furahini – BDB 965 (mara mbili)
3. pia *Qal* ya KAULI SHURUTISHI ya neno "furaha" (BDB 970)

   Kuna amri tano katika mst. wa 5.

   1. Lisikilizeni neno la Bwana – *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, BDB 1033, KB 1570
   2. Na atukuzwe Bwana – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, BDB 457, KB 455, inayotumika katika maana KAULI AMRISHI (Toleo la LXX linakitafsiri kifungu hiki kama KAULI TENDWA)
   3. tupate kuiona furaha yenu – *Qal ya* KAULI YA WAKATAI USIO TIMILIFU, BDB 906, KB 157, inayotumika katika maana ya KAULI AMRISHI

**66:6** Kumekuwa na mjadala mwingi miongoni mwa watoa maoni kuhusu namna mstari huu unavyohusiana na muktadha huu. Wengine wanasema hili ni tukio la kistoria lisilojulikana, ambapo wengine wanasema kuwa mstari huu unahusiana moja kwa moja na mst. wa 5, ambao unaonyesha hukumu ya kiburi, na Wayahaudi wasio amini.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 66:7-9)**
**7 Kabla hajaona utungu alizaa;**
**Kabla maumivu yake hayajampata, Alizaa mtoto mwanamume.**
**8 Ni nani aliyesikia neno kama hili?**
**Ni nani aliyeona mambo kama haya?**
**Je! Nchi yaweza kuzaliwa siku moja?**
**Taifa laweza kuzaliwa mara?**
**Maana Sayuni, mara alipoona utungu, Alizaa watoto wake.**
**9 Je! Mimi nilete wana karibu na kuzaliwa, nisizalishe? Asema Bwana;**
**mimi nizalishaye, je! Nilifunge tumbo? Asema Mungu wako.**

**66:7-13** Muktadha huu unairejelea Sayuniyenye kuzaa taifa kwa siku moja ambalo linamaanisha Mataifa. Wengine wanaliona hili kama tendo la kurudi kutoka uhamishoni, lakini tukio hili halikuyahusisha Mataifa. Hivyo, lazima lizungumzie matukio ya siku za mwisho (yaani, Agano Jipya).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 66:10-17**
**10 Furahini pamoja na Yerusalemu, shangilieni kwa ajili yake,**
**ninyi nyote mmpendao; furahini pamoja naye kwa furaha, ninyi nyote mliao kwa ajili yake;**
**11 mpate kunyonya, na kushibishwa kwa maziwa ya faraja zake,**
**mpate kukama, na kufurahiwa kwa wingi wa utukufu wake.**
**12 Maana Bwana asema hivi, Tazama, nitamwelekezea amani kama mto,**
**na utukufu wa mataifa kama kijito kifurikacho, nanyi mtapata kunyonya;**
**mtabebwa; na juu ya magoti mtabembelezwa.**
**13 Mfano wa mtu ambaye mama yake amfariji, ndivyo nitakavyowafariji ninyi;**
**nanyi mtafarijiwa katika Yerusalemu.**
**14 Nanyi mtaona, na mioyo yenu itafurahi,**
**na mifupa yenu itasitawi kama majani mabichi;**
**na mkono wa Bwana utajulikana, uwaelekeao watumishi wake,**
**naye atawaonea adui zake ghadhabu.**
**15 Maana Bwana atakuja na moto,**
**na magari yake ya vita kama upepo wa kisulisuli;**
**ili atoe malipo ya ghadhabu yake kwa moto uwakao, na maonyo yake kwa miali ya moto.**
**16 Kwa maana Bwana atateta na wote wenye mwili,**
**kwa moto na kwa upanga wake;**
**nao watakaouawa na Bwana watakuwa wengi.**
**17 Watu wale wajitakasao, na kujisafisha katika bustani,**
**nyuma yake aliye katikati; wakila nyama ya nguruwe, na machukizo, na panya;**
**watakoma pamoja, asema Bwana.**

**66:10** Kama yalivyo matokeo ya kile alichokifanya YHWH katika kuwarejesha watu wake katika Nchi ya Ahadi (yaani, Mwa. 12:1; 15:16), masharati ni

1. Furahini – *Qal* ya KAULI SHURUTISHI, BDB 970, KB 1333
2. shangilieni – *Qal* ya KAULI YA KAULI TIMILIFU, BDB 162, KB 189
3. furahini pamoja naye kwa furaha – *Qal* ya KAULI YA SHURUTISHI naNOMINO, BDB 965, KB 965

**66:12** Hii taswira ya ya upendo wa Mungu kudumu kwa watu wake ina nguvu sana katika mstari huu. YHWH anaelezwa katika stiari ya za jinsi ya kike (kama vile 49:15; 66:9-13; tazama Mada Maalum katika 41:2). Hii ni dhana kwamba Mungu angetumia kifungu "mwanamke aleaye" kujitolea ufafanuzi, inazungumzia uwezo.

## MADA MAALUM : WANAWAKE KATIKA BIBLIA

I. Agano la Kale
   A. Katika mila na desturi wanawake walichukuliwa kama ni mali kwa aliyenaye
      1. Walijumuishwa katika orodha ya mali (Kutoka 20:17)
      2. Walivyotendewa wanawake watumwa (Kutoka 21:7-11)
      3. Nadhiri za wanawake kufutwa na waume wenye madaraka (Hesabu 30)
      4. Wanawake kama mateka wa vita (kumbukumbu 20:10-14; 21:10-14)
   B. Kiutendaji palikuwa na ushirikiano
      1. Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27)
      2. Heshima kwa baba na mama (Kutoka 20:12 [Kumb. 5:16])
      3. heshima kuu kwa baba na mama (Mambo ya Walawi 19:3; 20:9)
      4. mwanaume na mwanamke wangeweza kuwa Wanazareti (Hesabu6:1-2)
      5. mabinti wana haki ya urithi (Hesabu 27:1-11)
      6. ni sehemu ya watu wa agano (Kumbu kumbu. 29:10-12)
      7. wanapata mafundisho ya baba na mama (Mithali 1:8; 6:20)
      8. wana wa kiume na mabinti wa Hemani (nyumba ya Kilawi) waliongoza muziki ndani ya Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 25:5-6).
      9. Wana wa kiume na wa kike watatoa unabii katika enzi mpaya (Yoeli 2:28-29)
   C. Wanawake katika dhima ya uongozi
      1. Dada yake Musa, Miriamu, aliitwa nabii wa kike (Kutoka 15:20-21 vile vile nukuu Mika 6:4)
      2. Wanawake walikirimiwa toka kwa Mungu kusokota nguo za aina mbalimbali kwa ajili ya Vibanda(Kutoka 35:25-26)
      3. Mwanamke aliyeolewa, Debora, pia nabii (kama vileWaamuzi. 4:4), aliyaongoza makabila yote (Amu. 4:4-5; 5:7)
      4. Hulda alikuwa nabii ambaye mfalme Yosia alimsihi kusoma na kutafsiri kitabu kipya kilichotolewa "*Book of the Law*" (2 Falme 22:14; 2 Nya. 34:22-27)
      5. Malkia Esta, mwanamke aliyemcha Mungu, aliwaokoa Wayahudi katika Uajemi

II. Agano Jipya
   A. Kwa utamaduni wa dini za Kiyahudi na ulmwengu wa kale wa Kiyunani na Rumi, wanawake walikuwa raia wa daraja la pili wenye haki na vipaumbele vichache (isipokuwa Makedonia).
   B. Wanawake katika dhima ya uongozi
      1. Elizabeti na Mariamu, wanawake waliomcha Mungu kwa kujihudhurisha mbele za Mungu (Luka 1-2)
      2. Ana, nabii mwanamke akihudumu katika Hekalu (Luka 2:36)
      3. Lidia, mwamini na kiongozi wa kanisa la nyumbani (Matendo 16:14,40)
      4. Mabinti Filipo wanne waliokuwa mabikra na manabii (Matendo 21:8-9)
      5. Fibii, shemasi wa kike wa kanisa katika Kenkrea (Rum. 16:1)
      6. Priska (Prisila), mtendakazi pamoja na Paulo na mwalimu wa Apolo (Matendo 18:26; Rum. 16:3)
      7. Maria, Trifaina, Trifosa, Persisi, Yulia, dada wa Nerea, wanawakae kadhaa watenda kazi amoja na Paulo (Rum. 16:6-16)
      8. Yunia (KJV), bila shaka mwanamke mtume (Rum. 16:7)
      9. Euodia na Sintike, watenda kazi pamoja na Paulo (Flp. 4:2-3)

III. Ni kwa namna gani mwamini wa sasa atailinganisha mifano hii tofauti ya kibiblia?

A. Ni kwa namna gani mtu ataupambanua kweli wa kihistoria na kiutamaduni, anaoutumia katika mazingire asilia pekee, kutoka katika ukweli wa milele ulio halali kwa makanisa yote, waamini wa rika zote?

1. Kwa umakini yatupasa kuchukuliana na kusudio la mwandishi asilia aliyevuviwa. Biblia ni neno la Mungu na njia na chanzo pekee cha imani na matendo.
2. Yatupasa kushughulika dhahiri na maandiko yenye masharti nay a kihistoria yaliyovuviwa.
    a. Utaratibu wa ibada (yaani, utaratibi na liturujia) wa Israeli (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3)
    b. dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza
    c. semi dhahiri za Paulo zenye masharti kihistoria na katika 1 Wakorintho
        1) mfumo wa kisheria wa wapagani katika Rumi (1 Wakorintho 6)
        2) kubaki katika hali ya utumwa (1 Kor. 7:20-24)
        3) ujane/useja (1 Kor. 7:1-35)
        4) mabikra (1 Kor. 7:36-38)
        5) chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor. 8; 10:23-33)
        6) matendo yasiyofaa katika Karamu ya Bwana (1 Wakorintho 11)
3. Kwa uwazi na kwa ukamilifu Mungu alijifunuaa kwa utamaduni maalumu, siku maalumu. Yatupasa kuuchukua ufunuo kwa umakini mkubwa, sio kufanya marekebisho kwa kila kipengele. Neno la Mungu liliandikwa katika maneno ya mwanadamu, likaelezwa katika utamaduni maalumu kwa wakati maalumu .

B. Tafsiri za kibiblia inapaswa kutafuta kusudi la asilia la mwandishi, nini alichokuwa akikizungumzia katika sihu zake zile? Hili ndilo jambo la kimsingi na la muhimu sana la tafsiri sahihi. Lakini basi yatupasa tulitumie hili kwa wakati wetu huu tulio nao. Tatizo kubwa la kiutafsiri linanaweza kuelezea maana ya neno. Je! Ni wapi palikuwa na huduma nyingi kuliko wachungaji ambao walionekana kama viongozi? Je! Ni wapi wahudumu au mashemasi wa kike na manabii wa kike walionekana kama viongozi? Ni dhahiri sana kuwa Paulo, katika 1 Kor. 14:34-35 na 1 Tim. 2:9-15, anadai kuwa wanawake wasishike nafasi katika ibada ya hadharani! Lakini alitumie kwa namna gani katika siku kama hizi? Nisingetaka utamaduni wa Paulo au utamaduni wangu kunyamazisha neno la Mungu na mapenzi yake. Bila shaka katika siku zile za Paulo palikuwa na mipaka sana, lakini pia katika siku zangu hizi inaweza kuwa wazi mno. Najisikia kukosa amani sana kusema kwamba kuwa maneno na na mafundisho Paulo ni ya kimasharti, karne ya kwanza, ukweli unaoendana na mazingira ya wenyeji hao. Mimi ni nani hata niweze kusababisha akili yangu au utamaduni wangu kumpinga mwandishi aliyevuviwa?!

Hata hivyo, nitafanya nini ikiwa kuna mifano ya kibiblia ya wanawake waliokuwa viongozi (hata katika maandiko ya Paulo, kama vile Warumi 16)? Mfano mzuri wa hili ni mjadala wa Paulo kuhusu ibada ya hadharani katika 1 Wakorintho 11-14. Katika 1 Kor. 11:5 anaonekana kuyaruhusu mahubiri na maombi ya wanawake katika ibada za hadharani huku vichwa vyao vikiwa vimefunikwa, lakini bado katika 14:34-35 anawahitaji wawe kimya! Kulikuwa na watoa huduma wanawake (kama vile Rum. 16:1) na manabii wa kike (kama vile Matendo 21:9). Ni utofauti huu unaonipa uhuru wa kutambua maoni ya Paulo (kama inavyohusiana na maagizo kwa mwanamke) kama ilivyozuiliwa huko Korintho na Efeso katika karne ya kwanza. Katika makanisa yote mawili palikuwa na matatizo kwa wanawake katika kutumia uhuru wao mpya uliopatikana (kama vile. Bruce Winter, *After Paul Left Corinth*), ambapo ingeweza kusababisha ugumu kwa kanisa kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo. Uhuru wao ulibidi kupunguzwa ili kwamba injili iweze kuleta matokeo mazuri.

Siku zangu ziko kinyume na siku za Paulo. Katika siku zangu injili inaweza kuwekewa mipaka ama ikiwa wanawake wenye uwezo wa kusema, waliofunzwa hawaruhusiwi kuchangia katika injili, hawaruhusiwi kuongoza! Ni nini hatima ya lengo la ibada ya hadharani? Si uinjilisti na nidhamu? Je! Mungu anaweza kuheshimiwa na kufurahishwa na viongozi wa kike? Biblia kwa ujumla wake inaonekana kusema "ndiyo"!

Nataka kukubaliana na Paulo; theolojia yangu kimsingi ni ya Kipauline. Sitaki kuathiriwa kwa kiwango kikubwa au kugeuzwa kifikra na sera za kisasa za kupigania haki za wanawake. Hata hivyo, nahisi kwamba kanisa limeenda pole pole katika kuitikia ukweli ulio wazi wa kibiblia, kama matendo yasiyo stahili kuhusu utumwa, ubaguzi, itikadi kali, na ubaguzi wa kijinsia. Hili pia limechelewa kwa kutoitikia vyema masuala ya uzalilishaji wa wanawake katika ulimwengu wa kisasa. Mungu katika Kristo amemweka huru mtumwa na mwanamke. Si thubutu kuruhusu maandiko yenye utamaduni unaopingana na haya.

Hoja moja zaidi: kama mtafsiri ninafahamu kuwa Korintho lilikuwa ni kanisa lililoharibiwa sana. Vipawa vilivyotolewa vilikuwa vya majivuno. Wanawake wangeweza kuwa wameshikwa katika hili. Pia ningeweza kuamini kuwa Efeso ilikuwa imeaathiliwa na walimu wa uongo waliofanikiwa kutumia wanawake kama wasemaji mbadala ndani ya makanisa ya Efeso.

C. Mapendekezo kwa usomaji zaidi
   1. *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart (kur. 61-77)
   2. *Gospel and Spirit: Issues in New Testament Hermeneutics* by Gordon Fee
   3. *Hard Sayings of the Bible by* Walter C. Kaiser, Peter H. Davids, F. F. Bruce, na Manfred T. Branch (kur. 613-616; 665-667*)*

**66:13** Hili neno "nitakavyowafariji" (BDB 636, KB 688) linatumika mara tatu katika mstari huu.
1-2. *Piel* ya KAULI SHURUTISHI (mara tatu)
3. *Pual* ya KAULI ISIO TIMILIFU

Hili linakumbushia moja ya kifungu 40:1 (*Piel* ya KAULI SHURUTISHI, mara mbili); pia tambua 12:1; 53:3 (mara mbili,12,19; 52:9; 61:2 (57:18, BDB 637). Hii ni dhima ya Isaya40-66. YHWH ameyatenda haya kwa ajili ya kusamehe, kusahau, na kuwarejesha wale wanaomtumainia na kulitetemekea neno lake (mist. ya 2,5)!

**66:15-16** Zitambue stiari tofautitofauti zilizotumika kutoa ufafanuzi wa hukumu ya YHWH.
1. moto (BDB 77; tazama Mada Maalum katika 47:14)
2. upepo wa kisulisuli (BDB 693 I, kama vile 5:28; Yer. 4:13)
3. ghadhabu yake (BDB 60 I**)** kwa miali (BDB 404, kama vile 42:25; 51:20; 63:3,6)
4. maonyo yake kwa miali ya moto, kama vile 29:6; 30:30
5. atahukumu kwa moto
6. upanga wake kwa wote wenye mwili, kama vile 65:12

**66:16 "nao watakaouawa na Bwana watakuwa wengi "** Kifungu hiki kinaeleza kwamba hukumu itaanza na wale walio nyumbani mwa Mungu. Tunahitaji kukumbuka kwamba kuna wengi miongoni mwa jamii ya Kiyahudi na, Mungu atusaidie, katika Kanisa, ambao hawamjui YesuKristo kwa uhalisia

**66:17 "katika bustani"** Hii inaonekana kurejelea aina ya ibada ya wapagani (kama vile 65:3).

◙**"nyuma yake aliye katikati"** Neno lililotafasiriwa kama"katikati" (BDB 1063) pia linataumika kumaanisha "mti wa uzima wa milele " katika Mwa. 3:3. Toleo la Agano la Kale la Kiebrania pia linaiona 65:22 kama yenye kurejelea mti wa uzima. Hapa kifungu hiki kinaweza kuirejelea mipaka au ncha za miamba ya *Asherah* zaIbada za ustawi wa Kanaani. Tazama Mada Maalum kataika 57:5-6.

◙ **"walao. ."**
1. nyama ya nguruwe, kama vile 69:4
2. machukizo (BDB 1054, kama vile Law. 11:10,11,12,13,20,23,41,42)
3. panya (BDB 747, kama vile Law. 11:29)

Nafiki ri kuwa miiko ya vyakula kwenye Mambo ya Walawi 11 si ya kiafya bali ni ya kishirikina. Hii ilimaanisha kuepusha Israeli dhidi ya uhusiano wa Wakanaani.

**ANDIKO LA NAB (LILILOBORESHWA) 66: 18-24**

**18 Nami nayajua matendo yao na mawazo yao; wakati unakuja nitakapokusanya mataifa yote na lugha zote; nao watakuja, nao watauona utukufu wangu.**
**19 Nami nitaweka ishara kati yao, nami nitawatuma hao waliookoka kwa mataifa, Tarshishi, na Puli, na Ludi, wavutao upinde, kwa Tubali na Yavani, visiwa vilivyo mbali; watu wasioisikia habari yangu, wala kuuona utukufu wangu; nao watahubiri utukufu wangu katika mataifa.**
**20 Nao watawaleta ndugu zenu wote kutoka mataifa yote, kuwa sadaka kwa Bwana, juu ya farasi, na katika magari, na katika machela, na juu ya nyumbu, na juu ya wanyama wepesi, mpaka mlima wangu mtakatifu Yerusalemu, asema Bwana; kama vile wana wa Israeli waletavyo sadaka yao nyumbani kwa Bwana katika**
**chombo safi.**
**21 Na baadhi ya hao nitawatwaa kuwa makuhani na Walawi, asema Bwana.**
**22 Kama vile mbingu mpya na nchi mpya,**
**nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu, asema Bwana,**
**ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa.**
**23 Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya,**
**na sabato hata sabato,**
**wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema Bwana.**
**24 Nao watatoka nje na kuitazama mizoga ya watu walioniasi;**
**maana funza wao hatakufa, wala moto wao hautazimika**
**nao watakuwa chukizo machoni pa wote wenye mwili.**

**66:18-21 "wakati unakuja nitakapokusanya mataifa yote na lugha zote"** Hili neno "wakati" limetolewa na Eben Ezra katika tafsiri yake ya Masoretic Text.Kuna baadhi ya mkanganyiko kutokana na mazingira halisi ya mstari huu. Hiki KITENZI "inajua" hakimo katika andiko la Kiebrania.
Kwa namna fulani hii ni rejea ya kuyakusanya mataifa. Haya yanaonekana kuja kwa shari dhidi ya watu wa Mungu (yaani, "wenye kuokoka"). Bali, katika tendo la Mungu kuwashindia (kama vile mst. wa 24b) baadhi wanabadilika na kumwamini. Kisha Mungu anawatuma kama ishara, mst. wa 19 (kama vile 11:10,12), kwa mataifa yao wenyewe kama wainjilisti. Tena, maajabu yastaajabishayo – watu wa kidunia waliuitikia ujumbe na kumurudia Mungu huko Yerusalemu kwa ajili ya kumwabudu na kuwafanya baadhi yao kuwa makuhani na Walawi (kama vile mst. wa 21).
Kipengele hiki, mist. ya 19-24, hakika kinashangaza katika nguvu yake ya kiulimwengu. Jambo hili limesababaisha hofu kubwa na kutokuwa na uyakinifu miongoni mwa walimu wa sheria za Kiyahudi, katika muktadha huu, kwa namna iliyo dhahiri huu ni ukamilifu wa ahadi ya uzao wa Ibrahimu waMwa. 3:15; 12:1-3.
Tazama Mada Maalum katika40:15.

**66:18 "Nami nayajua matendo yao na mawazo yao"** Mungu anaijua mioyo ya wanadamu wote. Tazama maelezo kamili katika 1:2.

**66:20** Hii ni moja ya maandiko kadhaa ambayo yanazungumzia Mataifa yasiyo ya Wayahudi yaletayo zawadi na vitu huko Yerusalemu/hekaluni (kama vile 2:2-3; 56:7; Zab. 22:27; 86:9; Yer. 3:17; Mika 4:1-2).

**66:22** Tazama maelezo kamili katika 65:17. Hiki KITENZI "zitakavyokaa" (BDB 763, KB 840) kimetumika mara mbili.
1. vile mbingu mpya na nchi mpya zikavyokaa – *Qal* ya KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU
2. uzao wa waaminifu utakaa – *Qal* ya KAULI YA WAKATI TIMILIFU

Hili neno, ingawa linatumika mara kwa mara katika kipengele cha Isaya (kama vile 44:11; 46:7; 47:12,13; 48:13; 50:8; 59:14; 61:5), linatafsiriwa kama "zitavyokaa" katika 66:22 pekee.

**66:23 “wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu,” asema Bwana”** Hiki KITENZI (BDB 1005, KB 295) ni adimu *Hishtapael* (kinapatikana hapa pekee). Hii ni maana iliyo dhairi ya Imani ya Mungu Mmoja (tazama Mada Maalum katika 40:14).

**66:24** Huu ni ufafanuzi wa wote wasio waaminifu Wayahudi na watu wa Mataifa. Sifikiri kama mtu anaweza kuitengeneza thiolojia ya adhabu ya nyakati za mwisho iliyojikita katika mstari huu. Hiki ndicho chanzo kamili cha matumizi ya Yesu ya neno*Gehenna*, ambalo linamaanisha “bonde la wana wa Hinoni,” ambalo lilikuwa jalala la uchafu huko Yerusalemu. Yesu alilitumia neno hili kueleza kutengana milele na Mungu (tazama Mada Maalum katika 57:9). Tatambue mambo ya majuto ambayo hayawezi kubadilka na jalada ambalo haliwezi kufutwa. Hizi ni stiari zilizochaguliwa na Yesu mwenyewe kwa ajili ya kueleza hatima ya wale waliokataa kumwamini (kama vile Mt. 25:46)

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini dhama kuu ya Isaya 65-66?
2. Orodhesha ibada za kipagani za sura ya 65.
3. Je! 65:1 na 2 inamrejelea nani na kwa nini?
4. Nini kitu cha pekee cha Isaya 65 ambacho hasa kinaonekana katika mist. ya 10 na 11?
5. Kwa nini Mungu aliumba mbingu mpya nan chi mpya?
6. Nini umuhimu wa 66:19-23?

# KIAMBATISHO CHA KWANZA
# UTANGULIZI WA USHAIRI WA KIEBRANIA

## I. UTANGULIZI

A. Aina hii ya fasihi imechukua 1/3 ya agano la Kale. Hasa ni ya kawaida kwa “manabii”(wote lakini Hagai na Malaki wanao ushairi) na “vipengere vya “maandiko”ya sheria za Kiebrania.

B. Ni tofauti na ushairi wa Kiingereza. Mashairi ya Kiingereza yametokana na ushairi wa Kiyunani na Kilatini, ambao kimsingi unaeleweka vizuri. Ushairi wa Kiebrania unaendana na ushairi wa Kikanaani. Hauna mistari yenye lafudhi ya mashairi ya Mashariki ya Karibu(lakini kuna kipimo cha shairi).

C. Uvumbuzi wa mabaki ya kale Kaskazini mwa Israeli katika maeneo ya Ugariti (Ras Shamra) umewasaidia wanazuoni kuuelewa ushairi wa Agano la Kale. Ushairi wa tokea karne ya 15 K.K dhahiri una uhusiano wa kifasihi na ule ushairi wa Kibiblia.

## II. TABIA ZA USHAIRI KWA UJUMLA

A. Ni wenye kushikamana .

B. Unajaribu kuelezea ukweli, mawazo au taswira ya uelewa.

C. Kimsingi umeandikwa sio kwa kusimuliwa. Kwa kiasi kikubwa umeumbika. Huu muundo unaelezewa katika:

1. Mistari iliyolingana (dhana ya ufanano)
2. Kuyachezea maneno
3. Ufasaha wa sauti

## III. MUUNDO WENYEWE (R. K. Harrison, Introduction To The Old Testament, kur.965-975)

A. Askofu Robert Lowth katika kitabu chake, Lectures on the Sacred Poetry of the Hebrews (1753) alikuwa wa kwanza kuanisha ushairi wa Kibiblia kama mawazo ya mistari yenye kulingana. Wengi wa watafasiri wa leo wamepanga kuonyesha mistari ya ushairi.

1. Visawe –mistari inaelezea mawazo yale yale kwa maneno tofauti:
   a. Zaburi 3:1; 49:1; 83:14; 103:13
   b. Mithari 19:5; 20:1
   c. Isaya 1:3,10
   d. Amosi 5:24; 8:10
2. Namna ya utabainishaji – mistari inajaribu kuelezea mawazo tofauti kwa namna ya kutofautiana au akianza na mawazo chanya na baadaye hasi:
   a. Zaburi 1:6; 90:6
   b. Mithari 1:29; 10:1,12; 15:1; 19:4
3. Uunganishaji wa maneno – mistari miwili au mitatu inayofuata huanzisha mawazo - Zab. 1:1-2; 19:7-9; 29:1-2
4. Tamathari za usemi – sehemu ya ushairi unaoelezea ujumbe katika hali ya mtiririko. Hoja kuu hupatikana katikati ya maelezo.

B. A. Briggs katika kitabu chake, General Introduction to the Study of Holy Scripture (1899) kimeanzisha hatua mpya ya uchunguzi juu ya ushairi wa Kiebrania:

1. Kama ishara ya – kishazi kimoja chenyewe na cha pili kiistiari, Zab. 42:1; 103:3.

2. Upeo au ngazi ya juu – vishazi vinadhihirisha ukweli katika namna ya mtiririko, Zab. 19:7-14; 29:1-2; 103:20-22.
3. kugeuzwa –mlolongo wa vishazi, mara nyingi kwa kawaida vinne huhusiana na muundo wa ndani wa mstari wa 1 hadi 4 na 2 hadi 3 - Zab. 30:8-10a

C. G. B. Gray katika kitabu chake, The Forms of Hebrew Poetry (1915) anaanzisha wazo la vishazi linganifu zaidi kwa:
   1. Ulinganifu kamili – ambapo kila neno katika mstari wa kwanza unarudiwa au kulinganisha na neno la mstari wa pili - Zab 83:14 na Isaya 1:3
   2. Ulinganifu usio kamili ambapo vishazi havina urefu unaolingana - Zab. 59:16; 75:6

D. Siku hizi kuna ukuaji wa kuvitambua vipengere vya kimuundo wa fasihi katika Kiebrania kiitwacho tamathari za semi, zinazoonyesha namba witiri za mistari zenye kufanana zinazounda umbo la shisha ambapo mstari wa kati ndio unaosisitizwa.

E. Aina ya vipengere vya sauti vinavyopatikana katika ushairi kwa ujumla, lakini sio mara nyingi katika ushairi wa kimashariki
   1. vinashirikiana kwenye alfabeti (aina ya chemshabongo. Kama vile. Zab. 9,34,37,119; Mith. 31:10 na kuendelea; Lm. 1-4)
   2. vinashirikiana kwenye konsonanti (marudio ya silabu za mwanzo, kama vile Zab. 6:8; 27:7; 122:6; Isa. 1:18-26)
   3. vinashirikiana kwenye irabu (ushairi, kama vile Mwa. 49:17; Kut. 14:14; Ezek. 27:27)
   4. vinashirikiana kwenye urudiaji wa vina vya maneno yenye kufanana vikiwa na maana tofauti
   5. vinashirikiana kwenye maneno ambayo, yakitajwa, yanasikika kama kitu kilichotajwa (mlio wa kitu)
   6. Ufunguzi na ufungaji maalum (jumuishi)

F. Kuna aina mbalimbali za ushairi katika agano la kale. Baadhi unahusiana na mada na mwingine unahusiana na muundo.
   1. Nyimbo za kuwakifisha - Hes. 21:17-18
   2. Nyinbo za kazini - (zimedokezwa lakini hazikuandikwa katika Amu. 9:27); Isa. 16:10; Yer. 25:30; 48:33
   3. Tumbuizo - Hes. 21:27-30; Isa. 23:16
   4. Nyimbo wakati wa kunywa – zilizo kinyume, Isa. 5:11-13; Amos 6:4-7 na zilizo chanya, Isa. 22:13
   5. Mashairi ya mapenzi – Wimbo ulio Bora, mafumbo ya kwenye harusi - Amu. 14:10-18, nyimbo za harusini - Zab. 45
   6. maombolezo -(dokezo lakini halikuandikwa katika II Sam. 1:17 na II Nya. 35:25) II Sam. 3:33; Zab. 27, 28; Yer. 9:17-22; Lm.; Ezek. 19:1-14; 26:17-18; Nah. 3:15-19
   7. Nyimbo za vitani - Mwa. 4:23-24; Kut. 15:1-18,20; Hes. 10:35-36; 21:14-15; Yosh. 10:13; Amu.5:1-31; 11:34; I Sam. 18:6; II Sam. 1:18; Isa. 47:1-15; 37:21
   8. Dua maalum au Baraka za wazee - Mwa. 49; Hes. 6:24-26; Kumb. 32; II Sam. 23:1-7
   9. Maandiko ya kimiujiza - Balaamu, Hes. 24:3-9
   10. Mashairi matakatifu – Zaburi
   11. Mashairi ya kuchemshabongo - Zab. 9,34,37,119; Mith. 31:10 na kuendelea na Maombolezo 1-4
   12. Laana - Hes. 21:22-30
   13. Mashairi ya kudhihaki - Isa. 14:1-22; 47:1-15; Ezek. 28:1-23

14. Kitabu cha mashairi ya vita (Jashar) - Hes. 21:14-15; Yosh. 10:12-13; II Sam. 1:18

IV. MWONGOZO WA KUUTAFASIRI USHAIRI WA KIEBRANIA

A. Tazama kiini cha sehemu ya wimbo au ubeti (hii ni kama aya katika lugha ya mjazo.) toleo la RSV lilikuwa ni tafasiri ya kwanza ya kisasa kuutambua ushairi kwa kutumia ubeti. Linganisha tafasiri za kisasa kwa ajili ya tambuzi zenye kusaidia.

B. Tambua lugha ya kitamathari na uielezee katika lugha ya mjazo. Kumbuka aina hii ya fasihi ni ya mjazo, mengi yamebaki kwa ajili ya msomaji kuyajaza.

C. Uwe na uhakika kulinganisha hoja ndefu ilibobea kwenye mashairi na fasihi zake za kimuktadha (mara nyingi kitabu kizima) na muundo wa kihistoria.

D. Waamuzi 4 na 5 ni ya kimsaada juu ya namna ushairi ulivyoelezea historia nzima. Waamuzi 4 ni lugha ya mjazo na Waamuzi 5 ni ushairi wa tukio la aina ile ile (pia linganisha Kutoka 14 na 15).

E. Jaribu kutambua aina ya ufanano uliohusika, ikiwa ni visawe, namna ya utabainishaji, au uunganishaji wa maneno. Hii ni muhimu.

# KIAMBATISHO CHA PILI

# MADA MAALUMU: UNABII WA AGANO LA KALE

## I. UTANGULIZI

A. Maelezo ya Ufunguzi

1. Jamii ya waaminio haiamini namna ya ya kutafsiri unabii. Kweli zingine zimekwisha weka wekwa bayana kama ilivyo kwa nafasi ya Waorthodox katika karne nyingi, lakini si katika karne hii.
2. Zipo hatua kadhaa za unabii wa Agano la Kale
   a. Premornarchial (Kabla ya utawala wa Kifalme)
      (1) Watu binafsi walioitwa manabii
         (a) Ibrahimu – Mwanzo 20:7
         (b) Musa – Hesabu 12:6-8; Kumbukumbu la Torati 18:15; 34:10
         (c) Haruni – Kutoka 7:1 (Msemaji wa Musa)
         (d) Miriam – Kutoka 15:20
         (e) Medad na Eldad – Hesabu 11:24-30
         (f) Debora – Waamuzi 4:4
         (g) Wasiokuwa na majina – Waamuzi 6:7-10
         (h) Samweli - 1 Samweli 3:20
      (2) Rejea ya manabii kama kundi – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
      (3) Kundi la Kinabii au ushirika – 1 Samweli 10:5-13; 19:20; 1 Wafalme 20:35, 41; 22:6, 10-13; 2 Wafalme 2:3,7; 4:1, 38; 5:22; 6:1, nakadhalika.
      (4) Masihi aitwaye nabii – Kumbukumbu la Torati 13:1-5; 18:20-22
         a. utawala wa kifalme usioandikwa (wakimlenga mfalme);
            (1) Gadi – 1 Samweli 22:5; 2 Samweli 24:11; 1 Mambo ya Nyakati 29:29
            (2) Nathan – 2 Samweli 7:2; 1 Wafalme 1:22
            (3) Ahijah – 1 Wafalme 11:29
            (4) Yehu – 1 Wafalme 16:1, 7, 12
            (5) Wasiotajwa – 1 Wafalme 18:4, 13, 22
            (6) Eliya – 1 Wafalme 18- 2 Wafalme 2
            (7) Mikaya – 1 Wafalme 22
            (8) Elisha 2 Wafalme 2:9, 12-13
         b. Maandiko ya kale ya manabii (yanayo lenga taifa pamoja na mfalme); Isaya – Malaki (isipokuwa Danieli)

## B. ISTILAHI ZA KIBIBLIA

1. *Ro'eh* = "muonaji" (BDB 906, KB 1157), 1 Samweli 9:9. Rejea hii yenyewe inatuonesha mpito kutoka katika neno nabi. Ro'eh inatokana na istilahi ya jumla "kuona." Mtu huyu alizielewa njia za Mungu na mipango yake na aliulizwa kutambua mapenzi ya Mungu katika jambo lolote.
2. *Hozeh* = "muonaji"(BDB 302, KB 3011), 2 Samweli 24:11. Ni jamii ya neno lenye maana sawa na Ro'eh. Inatokana na neno "kuona." Njeo ya wakati uliopita ya neno hili ni"tazama" ambalo limetumika mara nyingi ikimaanisha manabii.
3. Nabi' = "nabii" (BDB 611, KB 661), inayohusiana na lugha ya Akkadiaya kitenzi *Nabu* = "kuita" na kiarabu *Naba'a* = "kutangaza". Hili ni neon limetajwa mara nyingi katika Agano la kale kumaanisha nabii. Limetumika zaidi ya mara 300. Asili kabisa haijulikana kwa hakika japo "kuita"kwa wakati huu inaonekana kama mbadala mzuri zaidi. Yawezekana uelewa mzuri zaidi unatoka YHWH's yanayoeleza mahusiano ya Musa kwa Farao kupitia Haruni. (rejea kutoka 4:10-16; 7:1; Kumbukumbu la torati 5:5). Nabii ni mtu anayezungumza kwa niaba ya Mungu kwa watu wake. (Amosi 3:8; Yeremia 1:7,17; Ezekieli 3:4).

4. Istilahi zote tatu zinatumika katika huduma ya Nabii katika 1 Mambo ya Nyakati 29:29; Samueli – *Ro'eh*; Nathan – *Nabi*' and Gadi – *Hozeh.*
5. Kifungu cha maneno, '*ish ha* – '*elohim*, "Mtu wa Mungu" pia ni namna pana ya kumaanisha msemaji wa Mungu. Inatumika mara 76 katika Agano la Kale kwa kumaanisha "nabii"
6. Neno "Nabii" kwa asili ni la Kigiriki. Inatokana na neno (1) *pro* = "kabla" au "kwa niaba ya" na (2) *phemi* = "kuzungumza."

## II. MAANA YA UNABII

A. Neno unabii lilikuwa pana kimaana katika lugha ya kiebrania kuliko Kingereza. Vitabu vya historia vya Yoshua, Wafalme (isipokuwa Ruth) vinatajwa na Wayahudi kama "Manabii waliopita". Wote Ibrahimu (Mwanzo 20:7; Zaburi. 105:15) and Moses (Kumbukumbu la Torati 18:18) wanatajwa kama Manabii (pia Miriam, Kutoka 15:20). Kwahiyo kuwa makini unapokuwa unatazama maana kutoka katika lugha ya Kingereza!

B. "Unabii kisheria kabisa waweza kusema ni ule uelewa wa historia unaokubali maana zile tu zinazohusiana na uungu, kusudi la kiungu, ushirika wa kiungu," *Interpreter's Dictionary of the Bible*, toleo la. 3, ukurasa wa. 896.

C. "Nabii si mwanafalsafa au mwana taaluma ya Theolojia, bali msaidizi wa agano aletaye neno la Mungu kwa watu wake ili kutengeneza hatima zao kwa kufanya mageuzi ya siku zao za sasa," <u>Prophets and Prophecy</u>, *Encyclopedia Judaica* toleo la. 13 ukurasa wa. 1152.

## III. KUSUDI LA UNABII

A. Unabii ni njia ya Mungu kuzungumza na watu wake, kuwapa miongozo katika mazingira yao ya sasa na tumaini katika kuyaendesha maisha yao na matukio ya duniani. Ujumbe wao ulikuwa wa jumla. Ilikusudiwa kuonya, kutia moyo, kuhamasisha imani na toba, na kuwafahamisha watu wa Mungu kuhusu Mungu mwenyewe na mipango yake. Iliwashikilia watu wa Mungu katika maagano na Mungu. Katika hili inatakiwa iongezwe kuwa mara nyingi imekuwa ikitumika kufunua uchaguzi wa Mungu wa wasemaji (Kumbukumbu la Torati 13:1-3; 18:20-22). Hii ukiipa umaanani kabisa utagundua ilimaanisha Mesiya

B. Mara nyingi nabii aliichukua historia na migongano ya kithiolojia ya siku zake na kuangazia hayo katika mazingira ya matukio ya siku za mwisho. Namna ya muono huu wa siku za mwisho kihistoria katika Israel ni wa kipekee na katika hali yakeya uchaguzi wa kiungu na ahadi za kiagano.

C. Ofisi ya nabii inaonekana kutengeneza usawa (Yeremia 18:18) na kuchukua ofisi ya Kuhani Mkuu kama njia ya kufahamu mapenzi ya Mungu. Urimm na Thummim inabadilika katika ujumbe wa mdomo kutoka kwa msemaji wa Mungu. Ofisi ya nabii inaonekana pia kupita mbali katika Israeli baada ya Malaki. Haitokei mpaka baada ya miaka 400 baadae kwa Yohana Mbatizaji. Haieleweki namna ambavyo kipawa cha "unabii" kwa Agano Jipya kinavyoshabihiana na Agano la Kale. Manabii wa Agano Jipya (Matendo ya Mitume 11:27-28; 13:1; 15:32; 1 Wakorintho. 12:10,28-29; 14:29,32,37; Waefeso. 4:11) sio vifunuo vya ufunuo mpya au maandiko, bali wasimulizi wa yajayo na wazungumzaji wa mambo ya mbele ya mapenzi ya Mungu katika hali za agano.

D. Unabii hauna msingi sana au hausisitizi katika utabiri kwa asili. Utabiri ni njia mojawapo ya kutthibitisha ofisi yake na ujumbe wake, ila lazima izingatiwe "chini ya asilimia 2% ya unabii wa Agano la Kale ni kuhusu wa kimasiya". Chini ya asilimia 5% kiuhalisia inafunua nyakati za Agano Jipya. Chini ya asilimia 1% inahusu matukio yajayo. "fee na Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa wa 166).

E. Manabii wanamwakilisha Mungu kwa watu, wakati Makuhani wanawawakilisha watu kwa Mungu. Haya ni maelezo ya jumla. Kuna utofauti kwa kama Habakkuki, ambaye anauliza maswali kwa Mungu.

F. Sababu moja inayoleta ugumu kuwaelewa manabii ni kwasababu hatujui muundo wa vitabu vyao. Havina mfuatano unaoeleweka. Vinaonekana ni vyenye hoja na mada kweli lakini si kama vile mtu angetegemea. Mara nyingi hakuna mazingira ya wazi ya kihistoria wala muda maalumu, au mgawanyiko wa wazi wa mambo ya kiungu. Vitabu hivi ni vigumu

1. Kuvisoma kwa mara moja
2. Kufafanua kwa mada
3. Kug'amua kweli kuu au kusudio la mwandishi katika kila uungu.

## IV. TABIA ZA UNABII

A. Katika Agano la Kale inaonekana kukua kwa dhana ya "nabii" na "unabii". Hapo mwanzo katika Israeli kulitokea ushirika wa manabii, ukiongozwa na viongozi shupavu wenye uvuvio wa Mungu kama Eliya na Elisha. Kuna wakati neno "wana wa manabii," ilitumika kuzungumzia kundi hili (II Wafalme 2). Manabii walikuwa na tabia ya kujawa na furaha ya kupiliza (1 Samweli 10:10-13; 19:18-24)
B. Hata hivyo kipindi hiki kilipita mara kwa manabii mmmoja mmoja. Kulikuwa manabii (wa kweli na waongo) waliojitambulisha pamoja na mfalme, na waliishi katika Kasri la Kifalme (Gad, Nathan). Pia, kulikuwa na wale waliojitegemea, wakati mwingine wasiokuwa na hadhi kabisa za jamii ya ki-Israeli (Amos) walijumuisha wote wanawake na wanaume (2 Wafalme 22:14)
C. Nabii mara nyingi alikuwa mfunuaji ya hatima, anayefanya katika mazingira ya mwanadamu yanavyoenda. Mara nyingi jukumu la nabii ilikuwa ni kufunua mpango wa Mungu kwa uumbaji wake ambao hauathiriwi na mwitikio wa kibinadamu. Huu mpango wa wa ulimwengu wa matukio ya mwisho wa nchi ni wa kipekee katika manabii wa Mashariki ya Karibu ya kale. Utabiri na Agano ni mapacha waendao pamoja katika ujumbe wa kinabii (rejea Fee na Stuart, ukurasa wa 150). Hii inamaanisha manabii husisitiza ujumuishwaji katika lengo. Siku zote, japo si kila eneo, hujielekeza katika kuambia taifa.
D. Mambo mengi ya kinabii yakitolewa kwa njia ya kinywa. Baadae iliunganishwa kwa njia ya mada, mfululizo, au namna nyingine ya uandishi wa Mashariki ya Karibu ambao imepotea huku kwetu. Kwakuwa ilikuwa kwa njia ya kinywa, haikuwa na muundo kama unaokuwa katika kazi iliyo andikwa. Hii inafanya vitabu kuwa vigumu kusoma na ngumu kuelewa bila kuwa na historia ya mazingira halisi.
E. Manabii walitumia namna kadhaa kuwasilisha jumbe zao
    1. Matukio ya kimahakama – Mungu anawapeleka watu wake mahakamani, mara nyingi ni kesi ya kutalikiana ambapo YHWH anamkataa mke wake (Israeli) kwasababu ya kukosa uaminifu wake (Hosea 4; Micah 6).
    2. Mazingira ya msiba – mzani haswa kwa jaili ya ujumbe wa namna hii na tabia zake "ole" inajitenga kama aina yake kivyake vyake (Isaiah 5; Habbakkuk 2)
    3. Matamko ya Agano la Baraka - asili ya masharti ya Baraka imesisitizwa na madhara yake, yote ya wema na ubaya, yanatajwa kwa ajili ya baadae (Kumbukumbu la Torati 27-28).

## V. MIONGOZO YA KUKUSAIDIA KATIKA KUTAFSIRI UNABII

A. Tafta kujua lengo la kwanza la nabii (mwandishi) kwa kuzingatia mazingira ya kihistoria na muktadha wa maandishi ya kiungu.
B. Soma na tafsiri mambo yote, sio sehemu tu; fafanua na yaliyomo. Angalia inavyoshabihiana na mazingira ya unabii. Jaribu kufafanua kitabu kizima.
C. Endelea na kufanya makisio ya utafsiri wa kawaida wa hadithi mpaka vitu katika habari vikuelekeze katika matumizi yaliyofichwa kimaana; hivyo badili lugha iliyofichwa katika maandishi.
D. Fafanua matendo ya kiishara katika ufahamu wa mazingira ya kihistoria na usambamba wa hadithi. Kuwa na uhakika wa kukumbuka maanadishi ya kale ya Mashariki ya Karibu si kama yale ya kisasa ya kimagharibi.
E. kuwa mwangalifu wa utabiri
    1. Je unahusisha siku za mwandishi?
    2. Je uliwahi kutimia katika historia ya Israeli?
    3. Je ni kweli yamekwisha kuwa matukio yajayo?
    4. Je yana kutimizwa kwa sasa nab ado yanasubiri kutimizwa siku zijazo?
    5. Waruhusu waandishi wa Biblia wakuongoze katika majibu na sio waandishi wa kisasa.

F. Vitu vya kuzingatia
   1. Je utabiri umekidhi kigezo cha sharti la mwitikio
   2. Kuna uhakika kwa Yule ambaye unabii umemlenga? (Na kwa nini)?
   3. Je kuna uwezekano, wa kibiblia na/au kihistoria, wa kutimia mara mbili?
   4. Waandishi wa Agano Jipya, chini ya uvuvio waliweza kumuona mesiya katika sehemu nyingi katika Agano la Kale kiasi ambacho hakipo kwetu. Wanaonekana kutumia aina hii ya mchezo. Kwakuwa hatujavuviwa basi ni bora tukawaachia utaratibu huu wao.

## VI. VITABU VYA KIMSAADA

A. *A Guide to Biblical Prophecy* by Carl E. Amending and W. Ward Basque
B. *How to Read the Bible for All Its Worth* by Gordon Fee and Douglas Stuart
C. *My Servants the Prophets* by Edward J. Young
D. *Plowshares and Pruning Hooks: Rethinking the Language of Biblical Prophecy and Apocalyptic* by D. Brent Sandy
E. *New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, vol. 4, pp. 1067-1078
F. *The Language and Imagery of the Bible* by G. B. Caird

# KIAMBATISHO CHA TATU

## MAPITIO MAFUPI YA KIHISTORIA

Mapitio ya historia fupi ya mamlaka za Mesopotamia (tukitumia tarehe zenye kusimamia kimsingi juu ya John Bright'sA History of Israel, uk. 462 na kundelea):

A. Himaya ya Waashuru (Mwa. 10:11):
   1. dini na tamaduni kwa kiasi kikubwa zilishawishiwa na himaya ya Wasumeri/Wababeli
   2. Orodha ya mfano ya watawala na makisio ya tarehe:
      a. 1354-1318 Asshur-Uballit I:
         (1) akaupiga mji wa Wahiti wa Karkemishi.
         (2) wakaanza kuondoa ushawishi wa Wahiti na kuruhusu Ashuru kukua.
      b. 1297-1266 Adad Nirari I (mtawala mwenye nguvu).
      c. 1265-1235 Shalmaneser I (mtawala mwenye nguvu).
      d. 1234-1197 Tukulti-Ninurta I– ushindi wa kwanza wa himaya ya Babeli kuelekea Kusini.
      e. 1118-1078 Tiglath-Pileser I– Ashuru inakuwa tawala yenye nguvu huko Mesopotamia.
      f. 1012- 972 Ashur-Rabi II
      g. 972- 967 Ashur-Resh-Isui II.
      h. 966- 934 Tiglath-Pileser II.
      i. 934- 912 Ashur-Dan II.
      j. 912- 890 Adad-Nirari II.
      k. 890- 884 Tukulti-Ninurta II.
      l. 890- 859 Asshur-Nasir-Apal II.
      m. 859- 824 Shalmaneser III.
         – vita ya Qarqar katika mwaka wa 853
      n. 824- 811 Shamashi-Adad V.
      o. 811- 783 Adad-Nirari III.
      p. 781- 772 Shalmaneser IV.
      q. 772- 754 Ashur-Dan III.
      r. 754- 745 Ashur-Nirari V.
      s. 745- 727 Tiglath-Pileser III:
         (1) wakaitwa kwa jina la kiti chao cha enzi cha Babeli, Pul, katika II Fal. 15:19
         (2) mtawala mwenye nguvu sana
         (3) wakaanzisha utaratibu wa kuwaondoa watu walioshindwa
         (4) katika mwaka wa 735 K.K. palikuwepo na uanzishaji wa ligi ya "Syro-Ephramatic," ambayo ilikuwa ikijaribu kuunganisha rasilimali zote zilizopo za kijeshi za mataifa ya ng'ambo ya Yordani tokea kwenye vyanzo vya Mto Frati huko Misri kwa ajili ya kusudi la kubatilisha kuinuka kwa mamlaka ya jeshi la Ashuru. Mfalme Ahazi wa Yuda akakataa kuungana nao na kuvamiwa na Israeli na Shamu. Akamwandikia Tiglath-Pileser III kwa ajili ya msaada dhidi ya ushauri wa Isaya (kama vile Isa. 7-12).
         (5) katika mwaka wa 732 Tiglath-Pileser III akavamia na kuzishinda Shamu na Israeli na kuweka mfalme kibaraka juu ya kiti cha enzi cha Israeli, Hoshea (732-722 k.k.). maelfu ya Wayahudi wakakimbilia huko Umedi (kama vile II Fal. 15-16).
      t. 727- 722 Shalmaneser V– Hoshea akatengeneza ushirikiano na Misri na kuvamiwa na Ashuru (kama vile II Fal. 17)

u. 722- 705 Sargon II:

(1) baada ya kuuzingira mji kwa muda wa miaka mitatu, kulikoanzishwa na Shalmanesa V, jemedari wake na mrithi Sargon II, akaupiga mji mkuu wa Israeli, Samaria. Zaidi ya watu 27,000 wakakimbilia Umedi.

(2) Himaya ya Wahiti pia ikapigwa.

(3) katika mwaka wa 714-711 ushirika mwingine wa mataifa yaliyoko ng'ambo ya Yordani na Misri yakaasi dhidi ya Ashuru. Ushirika huu ulijulikana kama "uasi wa Ashdodi." Hata Hezekia wa Yuda mwanzoni alishiriki. Ashuru ikavamia na kuiangamiza miji mbalimbali ya Wafilisti.

v. 705- 681 Sennacherib:

(1) katika mwaka wa 705 ushirika mwingine wa mataifa yaliyoko ng'ambo ya Yordani na Misri yakaasi baada ya kifo cha babaye, Sargon II. Hezekia aliunga mkono kikamilifu huu uasi. Senakeribu akavamiwa katika mwaka wa 701. Uasi ulishindwa lakini Yerusalemu ikahurumiwa kwa tendo la Mungu (kama vile Isa. 36-39 na II Fal. 18-19.)

(2) Senakeribu pia akauweka chini uasi huko Elam na Babeli.

w. 681- 669 Esarhaddon:

(1) mtawala wa kwanza wa Ashuru kuivamia na kuipiga Misri.

(2) alikuwa na huruma kubwa kwa ajili ya Babeli na kuujenga upya mji wake mkuu.

x. 669- 663 Asshurbanipal:

(1) pia uliitwa Osnappar katika Ezra 4:10

(2) kakaye Shamash-shum-ukin alitawazwa kuwa mfalme wa Babeli. Pakaja kuwepo na miaka mingi ya amani kati ya Ashuru na Babeli lakini palikuwepo na mipango ya chini kwa chini ya kudai uhuru iliyoripuka katika mwaka wa 652, ikiongozwa na kakaye.

(3) kuanguka kwa Tebesi, 663

(4) kushindwa kwa Elamu, 653, 645

y. 633- 629 Asshur-Etil-Ilani.

z. 629- 612 Sin-Shar-Ishkun.

aa. a,a. 612- 609 Asshur-Uballit II:– mfalme aliyetawazwa akiwa uhamishoni huko Harani baada ya kuanguka kwa Asshur katika mwaka wa 614 na Nineva katika mwaka wa 612.

B. Himaya ya Babeli mpya:

1. 703- ? Merodach-Baladan: akaanzisha uasi mbalimbali dhidi ya utawala wa Ashuru.
2. 652 Shamash-Shum-Ukin:

(a) mwana wa Esarhadoni na nduguye Ashurbanipal.

(b) akaanzisha uasi mpya dhidi ya Ashuru lakini alishindwa.

3. 626- 605 Nabopolasar:

a. alikuwa ni mtawala wa kwanza wa himaya ya Babeli mpya.

b. aliivamia Ashuru tokea kusini wakati Kaizari wa Umedi akavamia tokea Kaskazini.

c. mji mkuu wa kale wa Ashuru, Ashurr uliangushwa mwaka wa 614 na mji mkuu maarufu wa Nineva ukaangushwa mwaka wa 612

d. mabaki ya jeshi la Ashuru yakakimbilia Harani. Hata wakaamua kumsimamisha mfalme

e. katika mwaka wa 608 Farao Necho II ( kama vile II Fal. 23:29) akaelekea Kaskazini kusaidia mabaki ya jeshi la Ashuru kwa ajili ya kusudi la kuunda kinga ya ulinzi dhidi ya mamlaka inayoinukia ya Babeli. Yosia, mfalme wa Yuda mwenye maadili ya Kiungu (kama vile II Fal. 23), akakipinga kikundi cha jeshi la Misri kilichopitia Palestina. Kulikuwepo na vita ndogo huko Megido.Yosia alijeruhiwa

na kufariki (II Fal. 23:29-30). mwanae, Yehoahazi, akawa mfalme.
Farao Necho II akachelewa kuuzuia uharibifu wa majeshi ya Waashuru huko Harani. Alishambuliwa na majeshi ya Babeli yaliyoamriwa na mwana wa mfalme Nebukadneza II na alishindwa vibaya katika mwaka wa 605 huko Karkemishi juu ya mito ya Frati. akiwa njia kuelekea Misri akasimama Yerusalemu na kuuteka nyara mji. Alimbadilisha na kumwondoa Yehoahazi baada tu ya miezi mitatu. Akamweka mwanae mwingine wa Yosia kwenye kiti cha ufalme, Yehoiakimu (kama vile II Fal. 23:31-35).

f. Nebukadneza II akalifukuza jeshi la Wamisri kuelekea kusini kupitia Palestina lakini alipokea ujumbe wa kifo cha babaye na akaamua kurudi Babeli.
Baaadaye mwaka huo huo akarudi Palestina. Akamwacha Yehoiakini akiwa kwenye kiti cha ufalme wa Yuda lakini akawachukua mateka wakazi wengi na jamii ya familia ya kifalme. Danieli na rafikize walikuwa ni moja ya watu walifukuzwa.

4. 605-562 Nebukadneza II:
   a. tokea mwaka wa 597-538 Babeli rasmi ikaitawala Palestina.
   b. katika mwaka wa 597 safari nyingine toka Yerusalemu ikatokea kwa sababu ya Yehoiakimu kushirikiana na Misri (II Fal. 24). Akafa kabla ya kuja kwa Nebukadneza II. Mwanae Yehoiakini alitawala kwa muda wa miezi mitatu tu mpaka pale alipokimbilia Babeli. Watu elfu kumi, akiwemo Ezekieli, wakaweka makazi karibu na mji wa Babeli kwenye mfereji wa Kebari.
   c. katika mwaka wa 586, baada ya kuendelea kucheza na Wamisri, mji wa Yerusalemu moja kwa moja ukaangamizwa (II Fal. 25) na kundi kubwa la watu kukimbia likatokea. Zedekia, aliyewekwa mbadala wa Yehoiakini, alikimbia na Gedalia akachaguliwa kuwa gavana.
   d. Gedalia aliuwawa na majeshi yaliyoasi. Na majeshi haya yalikimbilia Misri na kumrazimisha Yeremia kwenda nao. Nebukadneza akavamia mara ya nne (605, 596, 586, 582) na kuwafukuza Wayahudi wote walioonekana kubaki.
5. 562-560 yule mwovu-Merodaki, pia alijulikana kama Amel-Marduk
   – akamwachia Yehoiakimu toka gerezani lakini alitakiwa kubaki huko Babeli (kama vile II Fal.25:27-30; Yer. 52:31).
6. 560-556 Neriglissar.– alikuwa generali mkuu wa Nebukadneza aliyeuangamiza mji wa Yerusalemu
7. 556- Labaski-Marduk
   – alikuwa mwana wa Neriglisa lakini aliuwawa baada ya miezi minane tu
8. 556-539 Nabonidasi:
   (a) Nabonidasi hakuwa akihusiana na nyumba ya kifalme kwa hiyo akamwoa binti wa Nebukadneza II
   (b) aliutumia muda wake mwingi kulijenga hekalu la mungu wa mwezi Sin huko Tema. Alikuwa mwana wa kuhani wa kike wa mungu wa kike. Hii ilimsababishia uadui na makuhani wa Marduk, mungu mkuu wa Babeli.
   (c) alitumia muda wake mwingi akijaribu kuutuliza uasi na kuimalisha ufalme
   (d) alielekea Tema na kuachia mambo yote ya kiserikali kwa mwanae, Belshaza, ndani ya mji mkuu huko Babeli (kama vile Dan. 5)
9. ? -539 Belshaza (mtawala mwenza)– mji wa Babeli ulianguka haraka mikononi mwa jeshi la Wamedi na Waajemi chini ya Gobryas wa huko Gutiumu kwa kuchepusha maji ya Mto Frati na kuingia ndani ya mji pasipo kuzuiliwa.Makuhani na watu wa mji waliwaona Waajemi kama wakombozi na warejeshaji wa Marduku. Gobryasi alifanywa kuwa gavana wa Babeli na Koreshi II. Huenda Koreshi II au Gobryasi ni“Dario Mmedi” wa Dan. 5:31 na 6:1. Jina Dario linamaanisha “mtu wa familia ya kifalme.”

A. Himaya ya Umedi na Uajemi: Utafiti juu ya kuinuka kwa Koreshi II (Isa. 44:28; 45:1-7):

1. 625-585 Kaizari was the king of Media who helped Babylon defeat Assyria.
2. 585-550 Astyages alikuwa mfalme wa Umedi. Koreshi alikuwa mwanae mkubwa kwa Mandane.
3. 550-530 Koreshi II wa Anshamu alikuwa mfalme kibaraka aliyeasi.

   (a) Nabonida, mfalme wa Babeli, alimuunga mkono Koreshi.
   (b) Koreshi II akamwondoa kwenye kiti cha utawala Astyages.
   (c) Nabonida, ili kurejesha usawa kwenye madaraka, alishirikiana na:

(1) Misri.
(2) Kroesa, mfalme wa Lidia (Asia Ndogo).

4. 547- Koreshi II akaukabili mji wa Sardi (mji mkuu wa Lidia).
5. November 2, 539, Gobryas wa Gutiumu, akiwa na jeshi la Koreshi, akaichukua Babeli pasipo upinzani. Gobryas akawa gavana wa Babeli.
6. 539- kwenye mwezi wa kumi, Koreshi II "mkuu" binafsi akaingia kama mkombozi. Sera zake za wema kwenye makundi ya kitaifa yakaigeuza sera ya kitaifa ya miaka ya kuikimbia nchi.
7. 538- Wayahudi na wengineo wakaruhusiawa kurudi nyumbani na kuyajenga makazi yao.
8. 530- Mwana wa Koreshi, Kambiase II, akamurithi babaye.
9. 530-522 kutawala kwa Cambiase II.– aliiongeza himaya ya Misri katika mwaka wa 525 kuwa moja ya himaya ya Umedi na Uajemi.
   – yawezekana alijiua.
10. 522-486 Dario I akaingia kwenye kutawala.
    (a) alikuwa sio mmoja wa ukoo wa kifalme lakini alikuwa generali wa jeshi
    (b) (b)aliimiliki himaya ya Uajemi akitumia mipango ya Koreshi kwa ajili ya maliwali wa Kiajemi (kama vile Ezra 1-6; Haggai;Zekaria)
    (c) Akaweka sarafu kama Lidia.
11. 486-465 kutawala kwa Ahusuaero I:
    (a) aliuangusha uasi wa Wamisri.
    (b) akakusudia kuivamia Ugiriki na kutimiza ndoto ya Uajemi lakini akapigwa kwenye vita vya Thermopoly katika mwaka wa 480 na Salamisi katika mwaka wa 479.
    (c) Mume wa Esta aliyeitwa Ahasuero katika Biblia aliuawa katika mwaka wa 465.
12. 465-424 Artashasta I akatawala (kama vile Ezra 7-10; Nehemia; Malaki):
    (a) Ugiriki ikaendelea kusonga mbele mpaka walipokabiliana na vita ya ndani ya Pelopanisia.
    (b) Ugiriki ikagawanyika (Atheni - Pelopanisian).
    (c) Vita ya ndani ya Uturuki ilidumu kwa muda wa mika 20.
    (d) wakati wa kipindi hiki jamii ya Wayahudi iliendelea kuimalika.
13. 423-404 Dario II akatawala.
14. 404-358 Artashasta II akatawala.
15. 358-338 Artashasta III akatawala.
16. 338-336 Arsa akatawala.
17. 336-331 Dario III akatawala.

D. mapitio juu ya Misri:

1. Hyksos (mfalme wa wachungaji – mtawala wa Kisemiti)-1720/10-1550 K.K.
2. Utawala wa karne ya 18th (1570-1310 K.K.)
   a. 1570-1546 Amosi

b. 1546-1525 Amenophi I (Amenhotep I).
c. 1525-1494 Thutmosi I
d. ? Thutmosi II
e. ? Hatshepsuti
f. 1490-1435 Thutmosi III
g. 1435-1414 Amenophi II.
h. 1414-1406 Thutmosi IV
i. 1406-1370 Amenophi III
j. 1370-1353 Amenophi IV (Akhenaten)
k. ? Smenkhare
l. ? Tutankhamun
m. ? Ay
n. 1340-1310 Haremhab

3. Utawala wa karne ya 19 (1310-1200 K.K.):
   a. ? Ramesesi I
   b. 1309-1290 Seti I
   c. 1290-1224 Ramesesi (Ramesesi II)
   d. 1224-1216 Marniptah (Merenptah)
   e. ? Amenmesesi
   f. ? Seti II
   g. ? Siptah
   h. ? Tewosret
4. Utawala wa karne ya 20 (1180-1065 K.K.):
   a. 1175-1144 Ramesesi III
   b. 1144-1065 Ramesesi IV – XI
5. Utawala wa karne ya 21 (1065-935 K.K.):
   a. ? Smenda
   b. ? Heriho
6. Utawala wa karne ya 22 (935-725 K.K - Libya):
   a. 935-914 Shishaki (Shosenki I au Sheshong I)
   b. 914-874 Osorkoni I
   c. ? Osorkoni II
   d. ? Shoshneki II
7. Utawala wa karne ya 23 (759-715 K.K. - Libya)
8. Utawala wa karne ya 24 (725-709 K.K.)
9. Utawala wa karne ya 25 (716/15-663 K.K. - Kushi/Nubi):
   a. 710/09-696/95 Shabako (Shabaku)
   b. 696/95-685/84 Shebteko (Shebitku)
   c. 690/89, 685/84-
      664 Tirhakah (Taharqa)
   d. ? Tantamun
10. Utawala wa karne ya 26 (663-525 K.K. - Saitic):
   a. 663-609 Psammetichus I (Psamtik)
   b. 609-593 Neco II (Necho)
   c. 593-588 Psammetichus II (Psamtik)

d. 588-569 Apries (Hophra)
e. 569-525 Amasis
f. ? Psammetichus III (Psamtik)

11. Utawala wa karne ya 27 (525-401 K.K. - Uajemi):
    a. 530-522 Cambyses II (mwana wa Korshi II)
    b. 522-486 Dario I
    c. 486-465 Ahusuaero I
    d. 465-424 Artashasta I
    e. 423-404 Dario II

*kwa ajili ya kuutofautisha mfuatano wa matukio angalia Zondervan's Pictorial Bible Encyclopedia, juzuu ya 2 uk. 231.

E. Utafiti juu ya Ugiriki:
1. 359-336 Filipo II wa Makedonia:
    a. akaijenga Ugiriki.
    b. aliuawa mwaka wa 336.
2. 336-323 Iskanda II “mkuu” (mwana wa Filipo):
    a. akamkimbia Dario II, mfalme wa Uajemi, kwenye vita ya Isus.
    b. akafa mwaka wa 323 huko Babeli kwa homa akiwa na umri wa miaka 33/32.
    c. magenerali wa Iskanda wakaigawa himaya wakati wa kifo chake:
        (1) Cassender - Makedonia na Ugirik
        (2) Lysimicus – Thrace
        (3) Seleucus I - Shamu na Babeli
        (4) Ptolemy – Misri na Palestina
        (5) Antigonus - Asia Ndogo (hakudumu muda merfu)
3. Wajumbe wa utawala wa Uyunani waliokuwa wakitawala Shamu (Seleucids) dhidi ya majina ya watawala wote wa Makedonia walioko Misri (Ptolemies) kwa ajili ya kuidhibiti Palestina
    a. Shamu (wajumbe wa utawala wa Uyunani):
        (1) 312-280 Seleucus I
        (2) 280-261 Antiochus I Soster
        (3) 261-246 Antiochus II Theus
        (4) 246-226 Seleucus II Callinicus
        (5) 226-223 Seleucus III Ceraunus
        (6) 223-187 Antiochus III the Great
        (7) 187-175 Seleucus IV Philopator
        (8) 175-163 Antiochus IV Epiphanes
        (9) 163-162 Antiochus V
        (10) 162-150 Demetrius I
    b. Watawala wa Misri (Ptolemaic):
        (1) 327-285 Ptolemy I Soter
        (2) 285-246 Ptolemy II Philadelphus
        (3) 246-221 Ptolemy III Evegetes
        (4) 221-203 Ptolemy IV Philopator
        (5) 203-181 Ptolemy V Epiphanes
        (6) 181-146 Ptolemy VI Philometor

c. mapitio kwa ufupi:

(1) 301- Palestina chini ya mtawala Ptolemy kwa miaka mingi

(2) 175-163 Antiokia IV Epiphanes, mtawala Seleucid wa karne ya 8, akataka kuwabadili Wayahudi kuwa Wayunani kwa nguvu:


(a) akajenga nyumba ya kufanyia mazoezi ya viungo.

(b) akajenga madhabahu ya wapagani ya Zeus Olympius ndaniya hekalu

# KIAMBATISHO CHA NNE

# (MICHORO)

## KIPINDI MUHIMU CHA MATUKIO YA AGANO LA KALE


MALAKI
ARTAXERXES I (P)
XERXES I – AHASUERO (P)
EZRA 7-10
NEH.
ESTA
10
UKUTA WA YERUSALEMU – NEHEMIA
KURUDI MARA YA TATU – EZRA
9
UAJEMI
DARIO I (P)
CAMBECE II (P)
KORESHI II (P)
OBADIA
YOELI
HAGAI
ZAKARIA
EZRA 1-6
8
KURUDI MARA YA PILI – ZERUBABELI
KURUDI MARA YA KWANZA – SHESHBAZA
BELSHAZA (B)
KURIMBILIA
NABONIDA (B)
UHAMISHONI
BABELI
NEBUKADREZA (B)
NABOPOLASA (B)
YEREMIA
EZEKIELI
DANIELI
NAHUMU
HABAKUKI
SEFANIA
h i j k l m n o
1 & 2 WAFALME
2 MAMBO YA NYAKATI
P – GEDALIA (P)
O – ZEDEKIA (J)
n – YEHOAKINI (J)
m – YEHOAKIMU (J)
l – YEHOAHAZI (J)
k – YOSIA (P)
j – MANASE (J)
i – HEZEKIA (J)
h – UZIA (J)
g – YEROBOAMU II (I)
ASHURU
ASUR-BANI-PALI (A)
ESAR-HADONI (A)
SENAKERIBU (A)
SAGONI II (A) YONA
SHALMANESA V (A)
TIGRATH-PILESERI III (A)
AMOSI
HOSEA
g
6
ISAYA
MIKA
ELIYA
ELISHA
e f
ISRAELI
YUDA
d
5
4
Yeshua (Sebe) (SDS)
3
1 & 2 SAMWELI
1 MAMBO YA NYAKATI
f – AHABU (I)
e – YEROBOAMU I (I)
d – REHOBOAMU (J)
c – SULEIMANI (UM)
b – DAUDI (UM)
a – SAULI (UM)
SHAMU
FILISTIA
KAANANI
MISRI
Law; Kut.
Kumb. Hel.
2
Mwa. 12-50
1
AYUBU
MWANZO 1-11
MNARA WA BABELI (4)
GHARIKA YA NUHU (3)
ANGUKO LA MWANADAMU (2)
UUMBAJI (1)
DR. BOB UTLEY
BIBLE LESSONS INT'L 96

## WAFALME NA MATUKIO YA WABABELI, WAAJEMI, NA WATAWALA WA KIYUNANI

612 K.K. Nineva ikaangukia mikononi mwa jeshi la Babeli Mpya (Nebukaadneza)
608 Pharao Necho II akamwendea Karkemeshi kuzuia kupanuka kwa mamlaka Babeli Mpya, Yosia mfalme wa Yuda, akajaribu kumuzuia
Mauti ya Yosia na jaribio la mwanae, Yehoahazi kukikalia kiti cha ufalme
Yehoiakimu, mwana mwingine wa Yosia, akafanyika mbadala wa Yehoahazi juu ya mamlaka ya Farao
Necho II ndani ya miezi 3
Palestina na Shamu chini ya utawala wa Misri
Mageuzi ya Yosia yakagonga mwamba
605. Nabopolasa akatuma vikosi kupigana na jeshi la Waashuru waliobaki na Wamisri huko Karkemeshi
Nebukadneza akawafukuza kote mpaka kwenye nyanda za Palestina
Nebukadneza akapata habari ya kifo cha baba yake (Nabopolasa) kwa hiyo akarudi Babeli kwenda kuvishwa taji ya kifalme
Akiwa njiani kuelekea huko akawachukua Danieli na wafuasi wengine wa familia ya kifalme kuwapeleka uhamishoni

605 - 538 Babeli ikaikalia mamlaka ya Palestina, 597; 10,000 wakakimbilia uhamishoni huko Babeli
586 Yerusalemu na hekalu vikaangamizwa na wengi wao wakakimbilia uhamishoni
582 kwa sababu wapiganaji wengi wa msituni wakamuua Gedaliana kutokana na kundi kubwa kukimbilia uhamishoni

## WARITHI WA NEBUKADNEZA

562 - 560 Mwenye hila-Merodaki akamfungua Yehoiakimu (ukoo wa kimasihi) toka kifungoni
560 - 556 Neriglisa
556 Labaski-Marduk akatawala
556 - 539 Nabonida:

Akatumia muda mwingi kumjengea hekalu mungu wa hasira, *Sin*. Hili likasababisha uadui na kuhani wa Marduk.
Akatumia muda wake uliobaki kuweka chini maasi yote na kuimalisha ufalme.
akaelekea Tema na kukabidhi mambo yote ya nchi kwa mwanaye, Belshaza
Belshaza:
Alitumia muda wake mwingi kujaribu kuimarisha utaratibu mzuri.
Tishio kubwa la Babeli lilikuwa ni Umedi

## KUINUKA KWA KORESHI

585 - 550 Astyages alikuwa mfalme wa Umedi (Koreshi wa II alikuwa mjukuu wake kwa Mandane)
550 Koreshi II, kibaraka wa mfalme, akamuasi
Nabonida, ili kurejesha usawa wa madaraka, akashirikiana na:

1. Misri
2. Crecus, mfalme wa Lidia
547 Koreshi akaukabili Sardi (mji mkuu wa Lidia) na kuiteka Asia Ndogo yote
539 Gobiyasi akaichukua Babeli pasipo upinzani wowote (Dan. 5; Belshaza kaimu mwenza wa Nabonida;
Pia Gobiyasi yumkini Dario Mmedi, Dan. 5:31).
Oct. 11, 539 Koreshi akaingia kama mkombozi baada ya mungu wa kike wa Nabonidusi, *Zin*

## WARITHI WA KORESHI

530 Koreshi akamrithi (Kambiasi II)
530 - 522 Utawala wa Cambyses (magombo ya kisiwa cha Elefantino)
Akaiongeza Misri katika mwaka wa 525 kwenye himaya ya Umedi na Uajemi
522 - 486 Dario akaingia madarakani
Akaiongoza Himaya ya Uajemi pamoja na mpango wa Koreshi wa Gavana wa majimbo
Akaweka mpango wa kutengeneza sarafu kama wa huko Lidia
486 - 465 Ahusuero I (Esta)
Kuuangusha uasi wa Wamisri
Alikusudia kuivamia Ugiriki, lakini akashindwa katika vita na Thermopoly mwaka 480
Ahusuero I aliuawa katika mwaka wa 465
480 Vita ya Thermopoly
465 - 424 Artishasta I Longimanus (Ezra 7-10, Nehemia, na Malaki)
Uyunani ikaendelea kusonga mbele mpaka walipokabiliana na vita ya Pelopanisia
Vita ikadumu kwa muda wa miaka 20
Wakati wa kipindi hiki jamii za Kiyahudi zikatengenezwa upya
423 – 404 Dario II
Akaruhusu karamu ya mikate isiyochacha katika hekalu la Elephantino
404 - 358 Artishasta II
358 – 338 Artishasta III
338 – 336 Arses
336 - 331 Dario III

## UGIRIKI

359 – 336 Filipo II wa Makadonia akaijenga Ugiriki
aliuawa mwaka wa 336
336 - 323 Iskanda Mkuu (mwana wa Filipo)
Akamfukuza Dario II kwenye vita ya ISUS
Alikufa mnamo mwaka 323 huko Babeli kwa homa baada ya kuzitwaa Mashariki ya Mediterania na Mshariki ya Karibu
Makamanda wa Iskanda wakaigawa himaya yake wakati wa kufa kwake:
1. Cassander - Makedonia na Ugiriki
2. Lysimicus - Thrace
3. Selects I - Shamu na Babeli
4. Ptolemy – Misri na Palestina

5. Antigonus – sehemu ndogo ya Asia Ndogo

## Tatawa za Shamu dhidi ya Makedonia

301 Palestina ilikuwa chini ya utawala wa Ptolemy kwa muda wa miaka 100
175 - 163 Antiochus Epiphanes
Akataka kuwageuza Wayahudi kuwa Wayunani, akajenga ukumbi wa michezo ya viungo
Akajenga madhabahu ya kipagani; makuhani wao wakatendwa visivyo
Dec. 13, 168 Hog akauawa juu ya madhabahu na baadhi wakalifikiria hili kama chukizo lenye kuhuzunisha.

# WATAWALA

**BABELI** **UMEDI**

626 – 605 Nabopolasa akafa ("Nabu, akasimama")
625 - 585
Kaizari
605 - 562 Nebukadneza II
("Nebo, akaulinda mpaka")
585 - 550
Astyages
562 - 560 Merodack muasi 550
Koreshi II
556 Labaski Marduk
556 – 539 Nabonida
Belshaza
539 - Gobiyas

# UMEDI NA UAJEMI

| | |
|---|---|
| 550 - 530 | Koreshi II (mwaka wa 538 Umedi na Uajemi ukamiliki madaraka ya Himaya ya Akaemenia |
| 530 - 522 | Kambiasi II (akajiongezea Misri na Cyprus) |
| 522 | Gaumata, Smerdis (akatawala miezi 6) |
| 522 - 486 | Dario I (Hystaspes) |
| 486 - 465 | Ahusuero I (mme wa Esta) |
| 465 - 424 | Artashasta I (Ezra na Nehemia wakiwa huko Palestina) |
| 423 - | Ahusuero II |
| 424 - 404 | Dario II Nothus |

| | |
|---|---|
| 404 - 359 | Artashasta II Mnemon |
| 359 - 338 | Artashasta III Ochus |
| 338 - 336 | Arses |
| 336 - 331 | Dario III Codomannus |

## UYUNANI

| | |
|---|---|
| 359 – 336 | Filipo II wa Makedonia |
| 336 – 323 | Iskanda Mkuu |
| 323 - | Majenerali waliigawa Himaya |

1. Kasanda - Makedonia
2. Lysimicus - Shamu
3. Seleucus I - Shamu na Babeli
4. Ptolemy - Misri
5. Antigonus - Asia Ndogo (aliuawa mnamo mwaka wa 301 K.K.)

Watawala wa Makedonia wakaitawala Palestina, lakini katika mwaka wa 175 - 163 utawala ukawa mikononi mwa watawala wa Shamu
175 - 163 Antiochus IV Epiphanes, mtawala wa nane wa Shamu

*Tarehe na majina kwa kiasi kikubwa yamechukuliwa toka kwenye kitabu cha *A History of Israel* cha John Bright, kurusa za 461-471.

# WAFALME WA UFALME ULIOGAWANYIKA

| WAFALME WA YUDA(I NYA. 3:1-16; MT. 1:6-11) | | | | | WAFALME WA ISARELI | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAJINA NA TAREHE | BRIGHT T | YOUNG | HARRISON | MAANDIKO YA BIBLIA | MAJINA NA TAREHE | BRIGHT T | YOUNG | HARRISO N | MAANDIKO YA BIBLIA |
| Rehoboamu | 922-915 | 933-917 | 931/30-913 | 1 Fal. 11:43-12:27; 14:21-31 2 Nya. 9:31-12:16 | Yerohoboam I | 922-901 | 933-912 | 931/30-910/09 | 1 Fal.11:26-40; 12:12-14:20 |
| Abiya (Abiyamu) | 915-914 | 916-914 | 913-911/10 | 1 Fal.14:31-15:8 2 Nya.11:20,22 | | | | | |
| | | | | | | 901-900 | 912-911 | 910/09-909/08 | 1 Fal.14:20; 15:25-31 |
| Asa | 913-873 | 913-873 | 911/10-870/69 | 1 Fal.15:8-30; 16:8,10,23,29; 22:41,43,46 Yer.41:9 | Nadabu | | | | |
| | | | | | Baasha | 900-877 | 888-887 | 886/85-885/84 | 1 Fal.15:16-16:17; 2 Fal. 9:9 2 Nya. 16:1-6 Yer. 41:9 |
| Yehoshefati | 873-849 | 873-849 | 870/69-848 | | | 877-876 | 888-887 | 886/85-885/84 | 1 Fal.16:8-14 |
| | | | | 1 Fal.15:24; 22:1-51 2 Fal.3:1-12; 8:16-19 1 Nya.3:10 2 Nya. 17:1-12:1 | Ela | | | | |
| (Yehoramu kaimu mwenza) | ----------- | ----------- | 853-848 | | | 876 | 887 | 885/84 | 1 Fal.16:9-20 2 Fal.9:31 |
| | | | | 1 Fal.22:50 2 Fal. 1:17; 8:16; 12:18 | Zimri (kamanda wa jeshi) | 876-869 | 887-877 | 885/84-874/73 | 1 Fal.16:15-28 2 Fal.8:26 Mika 6:16 |
| Yehoramu | 849-842 | 849-842 | 848-841 | | Omri (kamanda wa jeshi) | | | | |
| Ahazia | 842 | 842 | ------------- | | 1 Nya.21:1-20 Mathayo 1:8 | 869-850 | 876-854 | 874/73-853 | 1 Fal.16:29-22:40 |
| | | | | | | | | 853-852 | |
| | | | | 2 Fal.8:24-9:29 2 Nya. 22:1-9 | Ahabu | 850-849 | 854-853 | | 1 Fal.22:40,41, 49,51-53 2 Nya.18:1-3,19 |
| | | | | | Ahazia | | | 852-841 | 2 Fal.1:17;3:1-27;8:16-9:29 |
| Atalia (malkia) | 842-837 | 842-836 | 841-835 | | | 849-842 | 853-842 | | |
| Yoashi | 837-800 | 836-797 | 835-796 | 2 Fal.8:26; 11:1-20 2 Nya.22:2-23:21 | Yehorumu | 842-815 | 842-815 | 841-814/13 | 1 Fal.19:16-17 2 Fal.9:1-10:36 15:12 2 Nya.22:7-9 Hosea 1:4 |
| Amazia | 800-783 | 797-779 | 796-767 | 2 Fal.11:2-3; 12:1-21 2 Nya.22:11-12; 24:1-27 | Yehu (kamanda wa jeshi) | | | | |
| | | | | | | | | 798-782/81 | |
| (kaimu | ---------- | ----------- | 791/90-767 | | | 801-786 | 798-783 | | 2 Fal.13:9-13,25 2 Nya.25:17-25 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| mweza wa Uzia) | | | | | | | | | Hosea 1:1<br>Amosi 1:1 |
| | | | | 2 Fal.12:21;<br>14:1-22<br>2 Nya. 25:1-28 | | | | | |
| | | | | | | | | 793/92-<br>782/81 | 2 Fal.13:13;<br>14:16,23-29<br>Hosea 1:1 |
| (kaimu mwenza wa Yothamu) | 750-742 | ----------- | 750-740/39 | 2 Nya.26:1-23<br>Hosea 1:1<br>Amosi 1:1<br>Zakaria 14:5 | Yehosa | ----------- | ---------- | 782/81-753 | Amosi 1:1;<br>7:9-11 |
| | | | | | | | | 753-752 | |
| Yothamu | 742-735 | 740-736 | 740/39-<br>732/31 | | | 786-746 | 783-743 | | 2 Fal.15:8-12 |
| | | | | | | | | 752 | |
| | | | | 2 Fal.15:7,<br>32-38 | (kaimu mwenza wa Yer. II) | 746-745 | 743 | | 2 Fal.15:10,<br>13-15 |
| (kaimu mwenza wa Ahazi) | ----------- | ----------- | 744/43-<br>732/31 | | | 745 | 743 | 752-742/41 | 2 Fal.15:14,<br>16-22 |
| | | | | 1 Nya. 5:17<br>2 Nya.26:23-<br>27:9<br>Isa.1:1;7:1<br>Hosea 1:1<br>Mika1:1 | Yeroboamu II | | | 742/41-<br>740/39 | |
| Ahazi | 735-715 | 736-728 | 732/31-<br>716/15 | | Zakaria | 745-738 | 743-737 | | 2 Fal.15:23-26 |
| (kaimu Hezekia) | ---------- | ----------- | 729-716/15 | 2 Fal. 15:30-<br>16:20<br>2 Nya.27:9-<br>28:27 | Shalumu | 738-737 | 737-736 | 740/39-<br>732/31 | |
| | | | | | | | | | 2 Fal.15:27-31<br>16:5<br>2 Nya.28:6<br>Isa.7:1 |
| Hezekia | 715-687 | 727-699 | 716/15-<br>687/86 | Isa.1:1; 7:1ff;<br>14:28;38:8<br>Hosea1:1<br>Mika1:1 | Menahemu | 737-732 | 736-730 | 732/31-<br>723/22 | |
| | | | | | | | | | 2 Fal.17:1-18 |
| | | | | 2Fal.16:20;<br>18:1-20,21<br>2 Nya. 28:27-<br>32:33<br>Mith.25:1 | Pekahia | | | 722 K.K | |
| (Kaimu mwenza wa Manase) | ----------- | ----------- | 696/95-<br>687/86 | | | 732-724 | 730-722 | | |
| Manase | 687/86-<br>642 | 698-643 | 687/86-<br>642/41 | Isa.1:136:1-39:8<br>Hosea 1:1<br>Mika 1:1<br>Mt.1:9-10 | Peka | 724 K.K | 722 K.K | | |
| Amoni | 642-640 | 643-641 | 642/41-<br>640/39 | | | | | | |
| | | | | 2 FAL. 20:21-<br>21:18;<br>23:12,26;24:2 | Hosea | | | | |
| Yosia | 610-609 | 640-609 | 640/39-609 | | | | | | |
| | | | | 2 Nya.32:33-<br>33:20<br>Yer.15:4ff<br>2 Fal.21:18-26 | Samaria kuangukia mikononi mwa Shamu | | | | |
| Yehoahazi | | | | | | | | | |
| | 609<br>(miezi 3) | 609 | 609 | 2 Nya. 33:20-25<br>Yer.1:2<br>Zef.1:1<br>1 Fal.13:2-3 | | | | | |
| Yehoiakimu | 609-598 | | | | | | | | |
| | | 609-598 | 609-597 | | | | | | |
| | | | | 2 Fal.21:24;<br>22:1-23:30<br>2 Nya.33:25-<br>35-27 | | | | | |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Yehoiakini<br><br>Zedekia<br><br><br><br>Kuanguka kwa Yerusalemu mikononi mwa Babeli | 598/97 (miezi 3)<br><br>597-586<br><br><br><br>586 K.K | 598<br><br>598-587<br><br><br><br>587 K.K | 597<br><br>597-587<br><br><br><br>587 K.K | Yer.1:2<br>Zef.1:1<br>Mat.1:10-11<br><br>2 Fal.23:30-34<br>2 Nya.36:1-4<br><br>2 Fal.23:34-24:6,19<br>2 Nya.36:4-8<br>Yer.1:3;<br>22:18-23<br>25:1ff<br>26:1ff;27:1ff<br>35:1ff; 36:1ff<br>Dan.1:1-2<br><br>2 Fal.24:17-25:7<br>25:27-30<br>2 Nya.36:8-9<br>Yer.52:31<br>Ezek.1:2<br><br>2 Fal.24:17-25:7<br>2 Nya. 36:10-11<br>Yer.1:3; 21:1-7;<br>24:8-10<br>27:1ff; 32:4-5;<br>34:1-22;<br>37:1-39:7;<br>52:1-11<br><br>Kitabu cha Maombolezo | | | | | | |

**Kwa ajili ya mjadala mzuri juu ya matatizo uwekaji tarehe angalia E. R. Thiele, *The Mysterious Numbers of the Hebrew Kings.***

# KIAMBATISHO CHA TANO
## KAULI YA KIMAFUNDISHO

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milelekwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine". Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.

9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

"Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo."